Ni matumaini yangu kwamba Baraza la Wawakilishi litaona taarifa zilizomo katika ripoti hii ni za muhimu katika kuisimamia Serikali na kuongeza uwajibikaji katika matumizi ya fedha na usimamizi wa rasilimali za umma ili kuhakikisha kunakuwa na utoaji bora wa huduma kwa umma wa wazanzibari ambao inawahudumia. Katika suala hili nitashukuru kama nitapokea maoni kutoka kwa watumiaji wa ripoti hii juu ya jinsi ya kuiboresha zaidi katika siku zijazo.

Nichukue fursa hii kwa dhati kumshukuru na kumpongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dk. Hussein A. Mwinyi kwa jitihada zake anazoendelea kuzichukuwa katika kufuatilia Ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa lengo la kusimamia na kuimarisha uwajibikaji katika matumizi ya rasilimali za Umma hali inayopelekea kuimarika kwa utawala bora.

.....................................

**DKT. OTHMAN ABBAS ALI**

**MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI**

**ZANZIBAR**

## MUHTASARI

Ripoti ya jumla inatoa matokeo ya ukaguzi wa hesabu za Serikali Kuu kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ambao unahusu Wizara kumi na sita (16) na Taasisi za Umma hamsini na saba (57) zilizowasilisha taarifa za hesabu na kukaguliwa. Hata hivyo sikuweza kushiriki kwa baadhi ya ukaguzi shirikishi ninaoufanya na Taasisi ya Taifa ya Ukaguzi kutokana na kutokuwa na bajeti toshelevu.

### Hati za Ukaguzi

Kwa ujumla, nimebaini taasisi zilizokaguliwa zimeonesha utendaji mzuri kutokana na kuongezeka kwa taasisi zilizopewa hati zinazoridhisha kutoka hati 53 kwa mwaka wa fedha 2019/2020 hadi kufikia hati 62 kwa mwaka wa fedha 2020/2021 kukiwa na ongezeko la hati 9 sawa na asilimia 17 ya ongezeko.

Aidha, hati zenye kasoro (modified opinion) zimepungua kutoka hati 10 kwa mwaka wa fedha 2019/2020 hadi kufikia hati zero (0) kwa mwaka wa fedha 2020/2021 sawa na asilimia 100 ya mafanikio yatokanayo na muamko mkubwa wa Maafisa Masuuli katika kusimamia matumizi ya fedha na rasilimali za Umma. Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali inapongeza kwa dhati jitihada zilizochukuliwa na Serikali za kuwajengea uwezo maafisa masuuli katika kusimamia majukumu yao pamoja na kuhakikisha kunakuwa na matumizi mazuri ya fedha na rasilimali za umma.

Ni imani yangu ya kwamba jitihada hizo zitaendelea katika kusimamia matumizi ya fedha na rasilimali za umma ikiwa ni pamoja na kuendelea kufuata sheria, kanuni pamoja na miongozo mbali mbali inayoelekeza utaratibu mzima unaopaswa kufuatwa ili kuweza kufikia katika viwango vinavyokubalika vya utayarishaji na uwasilishaji wa hesabu za mwisho wa mwaka vya kitaifa na kimataifa.

### Ufuatiliaji na utekelezaji wa Mapendekezo ya miaka iliyopita

Hali ya utekelezaji wa mpango kazi ulioandaliwa na Serikali kupitia Maafisa Masuuli juu ya mapendekezo ya ukaguzi yaliyotolewa kwa Wizara pamoja na Taasisi mbali mbali kwa kuzingatia majibu ya Serikali yaliyowasilishwa kwa Kamati ya kudumu ya Baraza la Wawakilishi kwa lengo la kuboresha na kuimarisha usimamizi na udhibiti wa fedha za Umma.

Kwa mwaka wa fedha 2019/2020, jumla ya mapendekezo 2,820 yakijumuishwa na maagizo ya Kamati ya PAC yaliyotolewa kwenda kwa maafisa masuuli wakati wa kamati hiyo ikifuatilia utekelezaji wa hoja zilizoibuliwa kwenye kitabu cha Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Katika kufanya ukaguzi kuhusu mapendekezo yaliyotolewa imebainika kwamba jumla ya mapendekezo 2,100 yalitolewa kwa Maafisa Masuuli kupitia barua za mapungufu "Letter of Weakness" yaliweza kufanyiwa kazi hali iliyopelekea kupatikana kwa maboresho kutokana na kuongezeka kwa umakini katika usimamizi wa majukumu ambapo kutokana na hali hiyo dosari hizo hazikuweza kujirejea katika ukaguzi wa mwaka wa fedha 2020/2021.

Hata hivyo jumla ya mapendekezo 320 yalipitwa na muda, vile vile imebainika mapendekeo 400 bado hayajatekelezeka na kupelekea baadhi ya dosari kujitokeza kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ambapo baadhi yake yamepelekea kupatikana kwa hati zisiozoridhisha kwa baadhi ya Taasisi.

Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali inatambua na kuthamini juhudi za Serikali kupitia Maafisa masuuli pamoja na Ofisi ya Rais Fedha na Mipango kuendelea kuchukuwa jitihada za kufanya maboresho makubwa ya utekelezaji wa hoja za ukaguzi ikiwemo utayarishaji wa hesabu za mwisho wa mwaka zenye kukidhi viwango vya uhasibu vilivyowekwa ambapo kwa namna ya pekee imepelekea kupungua kwa dosari za uandaaji wa hesabu hizo hali ambayo imesaidia kuboresha

mifumo ya udhibiti wa ndani itakayosaidia kujiepusha kujirudia kwa hoja za ukaguzi pamoja na kuzingatia umuhimu wa uwajibikaji na Utawala Bora.

**Usimamizi na Ukusanyaji wa Mapato**

Kwa mwaka wa fedha 2020/2021 imebainika hali ya usimamizi na ukusanyaji wa mapato imeimarika kwa baadhi ya taasisi kwa kuweza kufikia malengo waliyojipangia pamoja na uwepo wa janga la maradhi ya UVIKO 19 lililoikumba Dunia ambapo imepelekea uchumi wa nchi mbali mbali kuyumba jambo ambalo limeathiri utekelezaji wa bajeti kwa nchi zenye uchumi wa kati ikiwemo Tanzania. Hata hivyo kwa upande wa makusanyo kwa baadhi ya Taasisi ikiwemo Mabaraza ya Miji na Halmashauri imebainika kuwepo kwa ukiukwaji wa sheria na miongozo inayohusiana na usimamizi wa makusanyo kwa kujitokea vitendo vya ukusanyaji wa mapato nje ya mifumo iliyowekwa ambapo kumejitokeza kwa viashiria vya upotevu wa fedha za umma na kupelekea baadhi ya miradi ya maendeleo kutokutekelezeka ipasavyo au kutekelezwa kwa kiwango kisichoridhisha. Aidha imebainika uwepo wa dosari za kukosekana kwa makadirio ya vyanzo vya mapato kwa baadhi ya Taasisi na kupelekea kutokujulikana kwa fedha halisi iliyokusanywa pamoja na iliyowasilishwa Mfuko Mkuu wa Hazina kwa ajili ya kuingia katika matumizi ya Serikali.

Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali inaishauri Serikali kufanya utafiti wa vyanzo vipya vya mapato na kuhamasisha ulipaji kodi kwa hiari ili kuhakikisha makusanyo yanaendana na matumizi yaliyokusudiwa. Aidha, taarifa za makusanyo ya fedha na matumizi zinapaswa kufanyiwa usuluhisho kwa wakati, kuhesabiwa na kutotumika kabla ya kuwasilisha taarifa hizo katika Mfuko Mkuu wa Serikali. Hata hivyo jitihada za makusudi zinatakiwa zichukuliwe ikiwemo kusimamia na kufuta Sheria na kanuni zinazoruhusu baadhi ya taasisi kukusanya mapato na kuyatumia wenyewe kabla ya kuwasilishwa Mfuko Mkuu wa Serikali kwa Lengo la kuweza kudhibiti matumizi ya makusanyo yanayofanywa na Taasisi hizo.

**Usimamizi wa Matumizi**

Usimamizi wa matumizi ni eneo muhimu kwenye utendaji wa kila siku wa Serikali, hivyo ni jambo nililolipa umuhimu mkubwa katika ukaguzi huu. Katika mwaka wa fedha 2020/2021 hakuna tofauti kubwa iliyojitokeza ya ukiukwaji wa sheria ambapo imepelekea kujitokeza kwa matumizi mabaya ya fedha ikilinganishwa na Ripoti ya awali ya mwaka 2019/2020 ambapo imebainisha dosari mbali mbali zinazopaswa kufanyiwa kazi na maafisa masuuli ili kuboresha usimamizi wa rasilimali za umma kwa kuweka nidhamu ya matumizi ya fedha za walipa kodi.

Mapungufu ya matumizi mabaya ya fedha za umma yamebainishwa kwa kina kutokana na dosari mbali mbali zilizobainishwa katika ripoti hii ikiwemo kujitokeza kwa upotevu mkubwa wa fedha za umma zinazotokana na kulipa na kufanya matumizi ya fedha kusikozingatia sheria ya tozo za kodi ambapo kumepelekea Serikali kukosa mapato yatokanayo na kutokulipwa kodi za zuio au ongezeko la thamani. Hata hivyo kumejitokeza kwa kasoro za matumizi yanayotokana na kutokuzingatiwa usimamizi wa mikataba jambo ambalo limepelekea kufanyika kwa malipo bila ya kuzingatia matakwa ya makubaliano ya mikataba hiyo na kupelekea kuitia hasara Serikali.

Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali inashauri maafisa masuuli kuendelea kuimarisha mifumo ya udhibiti kwenye usimamizi wa matumizi ili kupunguza hatari ya matumizi mabaya ya fedha. Katika utekelezaji wa lengo hili Ofisi ya Rais Fedha na Mipango ni vyema kuweka Mfumo madhubuti utakao wezesha usimamizi wa matumizi ya fedha zinazotumwa kwa Mabaraza ya Miji, Halmashauri pamoja na kuhakikisha fedha ambazo hazijatumika zinarejeshwa Mfuko Mkuu wa Hazina ili kuweza kupangiwa matumizi kwa mwaka unaofuatwa, vile vile kuhakikisha nyaraka za malipo zinapatikana zinapohitajika kwa ajili ya ukaguzi zikiwa halisi (original) na toshelezi. Aidha kuhakikisha kuwa Sheria za Kodi na ununuzi zinazingatiwa kwa kudai stakabadhi za kielektroniki pamoja na kukata kodi ya zuio na ongezeko la thamani na kuziwasilisha kwenye mamlaka husika.

**Usimamizi wa Deni la Taifa**

Deni la taifa linajumuisha madeni yote inayodaiwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ndani na nje ya nchi kupitia Serikali Kuu na Wakala wake wakiwemo Wizara, Mamlaka za Serikali za Mitaa pamoja na Mashirika ya Umma.

Deni la ndani linajumuisha mikopo ya muda mrefu na muda mfupi, mikopo ya muda mrefu ni hati fungani,hisa za Serikali na Hati fungani Maalum. Mikopo ya muda mfupi ni dhamana za Serikali za muda mfupi na nakisi ya Serikali kwenye akaunti za Benki Kuu (Government Overdraft). Mikopo ya muda mfupi hutumika kulipia dhamana za Serikali zilizoiva na mikopo ya muda mrefu hutumika kugharamia utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa lengo la kusogeza huduma bora kwa wananchi.

Deni la nje linajumuisha ukopaji kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo kutoka Taasisi za kimataifa, Nchi marafiki, benki za kibiashara, pamoja na wakopeshaji wa kibiashara.

Katika ukaguzi wa mwaka wa fedha 2020/2021 imebainika kuongezeka kwa Deni la Taifa kwa asilimia 3.80, kwa upande wa deni la nje ukaguzi umebaini kwamba deni la Taifa bado ni himilivu kwa kuzingatia vigezo vilivyowekwa kitaifa na kimataifa kama ifuatavyo:-

- Thamani ya Deni la Ndani linalodhaminiwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imebainika kufikia jumla ya shilingi Bilioni 194.098 wakati uchumi wa Zanzibar hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 una thamani ya shilingi Bilioni 4,513.9. Hivyo uwiano wa deni la taifa dhidi ya GDP ni asilimia 4.3 wakati ukomo wa kigezo cha nchi za Uchumi wa Kati ni asilimia 70 kwa kiwango cha chini.
- Deni la Ujumla la shilingi Bilioni 886.965 na ukuwaji wa uchumi wa Zanzibar wa shilingi Bilioni 4,513.9 sawa na asilimia 19.65 ya kiwango cha asilimia 70 ya Nchi za Uchumi wa Kati kwa kiwango cha chini.
- Mapato halisi ya ndani yaliyokusanywa ya shilingi Bilioni 723.6 kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ambapo asilimia 27 ya mapato hayo ingelitosha kulipa deni lote linalodhaniwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Kutokana na mchanganuo nilioubainisha hapo juu inaonesha kuwa deni la Serikali ya Mapunduzi ya Zanzibar bado ni himilivu hivyo Ofisi ya mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali inaishauri Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuendelea kukopa zaidi ili kuendeleza utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa lengo la kuwaletea maendeleo wananchi wa Zanzibar.

**Tathmini ya Mifumo ya Udhibiti wa Ndani na Utawala Bora**

Kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ukaguzi ulifanya tathmini ya Mifumo ya udhibiti wa ndani na utawala bora pamoja na mfumo wa ukaguzi wa ndani, kamati ya ukaguzi, tathmini ya ubadhirifu, TEHAMA na usimamizi wa vihatarishi. Katika tathmini iliyofanyika ya mifumo ya udhibiti wa ndani ilibainika kuwa kuna taasisi kumi na nane (18) zenye mapaungufu ambayo yalitokea katika mfumo wa ukaguzi wa ndani. Katika tathmini ya Kazi ya Kamati za Ukaguzi, ilibainika jumla ya Taasisi 21 zenye mapungufu ambapo baadhi ya Taasisi hizo hazina vitengo vya Kamati ya ukaguzi au kutokufanya kazi kwa Kamati hizo kwa mujibu wa matakwa ya Kisheria. Aidha tathmini ya Usimamizi wa Vihatarishi ilibainika taasisi 3 zina mapungufu makubwa.

Tathmini ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) inaonesha kuwa kuna Taasisi 12 zenye mapungufu katika mfumo jambo ambalo limepelekea kujitokeza kwa viashiria vya ubadhirifu wa fedha za umma ikiwemo udanganyifu wa manunuzi. Matokeo ya kina yameonyeshwa katika matokeo na mapendekezo ya ukaguzi katika kila ripoti za taasisi husika kwenye kitabu cha ukaguzi cha Serikali Kuu cha mwaka wa fedha 2020/2021.

Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali inashauri ili kusimamia vyema rasilimali za umma inapendekeza kuimairishwa kwa udhibiti wa ndani kwa kuhakikisha Sheria na taratibu zilizowekwa zinafuatwa. Aidha ni vyema kuhakikisha usimamizi wa vihatarishi na mifumo ya utawala inafanya kazi ipaswavyo ili kuondoa mianya ya upotevu wa fedha za umma.

# RIPOTI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI KUHUSU UKAGUZI WA TAARIFA ZA FEDHA ZA SERIKALI KUU KWA KIPINDI CHA MWAKA WA FEDHA UNAOISHIA TAREHE 30 JUNI , 2021

## SURA YA KWANZA

### 1.0 UTANGULIZI

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anawajibu wa kukagua hesabu zote za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Ukaguzi huo unafanyika kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 kifungu nambari 112 . Ukaguzi wa Hesabu za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar unajumuisha hesabu zote za Serikali kuu, Mashirika ya Umma na Taasisi zinazojitegemea, Serikali za Mitaa, Mamlaka na Taasisi mbali mbali pamoja na Miradi mbali mbali ya maendeleo na baadae kutoa taarifa ya ukaguzi wa hesabu hizo kwa mujibu wa masharti ya Katiba ya Zanzibar.

Kutokana na mamlaka ya kikatiba Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anawajibu wa kuhakikisha kwamba fedha zote zinazokusudiwa kutolewa kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar matumizi yake yameidhinishwa kisheria ambapo Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anawajibu wa kuidhinisha matumizi kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na kufanya Ukaguzi wa hesabu hizo.

### 1.1 MAJUKUMU YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI

Kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 kifungu nambari 112 Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anawajibika kukagua hesabu za Taasisi za Serikali na baadae kutoa taarifa zake za ukaguzi huo kila mwaka. Taarifa hizo zitaelezea hali halisi za mapato na matumizi ya fedha kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar pamoja na utekelezaji wa sheria mbali mbali zikiwemo Sheria za fedha, Sheria za manunuzi na sheria nyenginezo.

Kwa mujibu wa kifungu nambari 112 (3) cha Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu anawajibika kufanya yafuatayo:-

"a) Kuhakikisha kwamba fedha zote zinazokusudiwa kutolewa kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, matumizi yake yameidhinishwa kisheria na iwapo atatosheka kwamba masharti hayo yatatekelezwa ipasavyo basi ataidhinisha fedha hizo zitolewe.

b) Kuhakikisha kwamba fedha zote ambazo matumizi yake yameidhinishwa yanatokana na fedha zilizomo katika Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar au fedha ambazo matumizi yake yameidhinishwa na sheria iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi, na ambazo zimetumika kwa ajili ya shughuli zilizohusika na matumizi ya fedha hizo na kwamba matumzi hayo yamefanywa kwa kufuata idhini iliyotolewa kuhusu matumizi hayo; na

c) Angalau mara moja kwa kila mwaka kufanya ukaguzi na kutoa taarifa juu ya ukaguzi wa hesabu za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, hesabu zinazosimamiwa na watumishi wote wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, hesabu za Mahkama zote za Zanzibar, hesabu za Tume au vyombo vyengine vilivyoanzishwa na Katiba hii na hesabu zozote zinazohusika na Baraza la Wawakilishi. "

Ukaguzi wa hesabu umefanywa kwa kuzingatia miongozo na vigezo mbali mbali vya ukaguzi ili kukidhi matarajio ya wadau wetu na wananchi kwa ujumla. Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali inaendelea kufanya uchambuzi wa njia bora zaidi kwa kufanya ukaguzi utakaoleta tija na kuongeza wigo na maeneo yanayokaguliwa kwa lengo la kuimarisha utendaji na uwajibikaji katika sekta za Umma.

## 1.2 UPEO NA MADHUMUNI YA RIPOTI YA UKAGUZI

Ripoti hii imekusanya taarifa za ukaguzi wa hesabu za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar yakiwemo Mawizara na Taasisi mbali mbali za Serikali kwa kuzingatia taarifa za mapato na matumizi ya kawaida, matumizi ya maendeleo pamoja na michango mbali mbali kutoka kwa Washirika wa Maendeleo, kwa kipindi cha mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2021.

Ukaguzi ulifanyika kwa mujibu wa viwango vya kitaifa na kimataifa vya ukaguzi na kujiridhisha kwamba taarifa zitakazotolewa zitaonyesha sura halisi ili kutoa uhakika kwamba taarifa za mapato na matumizi zimefuata Sheria, Kanuni na taratibu zilizopo. Taarifa za hesabu zilizokaguliwa zilijumuisha hesabu za mwisho wa mwaka pamoja na taarifa mbalimbali zinazohusiana na hesabu hizo.

Miongoni mwa taarifa hizo ni kama zifuatazo:-

I. Mizania ya Hesabu

II. Taarifa ya Mapato na Matumizi

III. Taarifa kuhusu mabadiliko ya mtaji

IV. Taarifa ya mtiririko wa fedha

V. Taarifa ya uwiano na bajeti na kiasi halisi cha matumizi

VI. Sera za uhasibu na maelezo ya taarifa za fedha

Mabadiliko ya mifumo ya ukaguzi na uhasibu yanayotokea kwa mujibu wa viwango vya kitaifa na kimataifa yamepelekea kuwepo na mafanikio makubwa katika utendaji na uwajibikaji kwenye sekta za Umma katika ukusanyaji wa mapato na matumizi ya rasilimali za umma. Mafanikio hayo yametokana na kuimarika kwa mfumo wa fedha pamoja na utekelezaji wa sheria mbalimbali zikiwemo Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma, Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma, pamoja na Sheria nyenginezo na kupelekea kuimarika kwa uwazi na uwajibikaji katika taasisi za Umma pamoja na utekelezaji wa miradi mbali mbali ya maendeleo na kuleta tija kwa wananchi na kufanikisha lengo la Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kuimarisha dhana nzima ya utawala bora.

## 1.3 NJIA ZILIZOTUMIKA KATIKA UKAGUZI

Katika kufanya ukaguzi wa hesabu za Serikali mbinu na njia mbali mbali za ukaguzi zilitumika ikiwemo taratibu za ukaguzi zifuatazo: -

1. Kutoa barua za awali za maandalizi ya ukaguzi (Engagement Letter) kwa Taasisi inayokaguliwa.

2. Kuangalia viashiria vya maeneo hatarishi katika taasisi zinazokaguliwa kwa lengo la kupata uelewa wa mazingira ya taasisi hiyo ikiwemo mfumo wa udhibiti wa ndani na kubaini viashiria vitakavyoathiri udhibiti wa ndani pamoja na utendaji wa taasisi.

3. Kuandaa mikakati ya ukaguzi kuanzia mpango wa awali hadi mpango mkuu wa ukaguzi (Pre Planning, Strategic Planing and detailed Planning) itakayozingatia muelekeo na upeo wa ukaguzi ambapo utaonyesha dira na dhamira nzima ya ukaguzi huo.
4. Kufanya kikao cha kuanza kazi za ukaguzi (Entrance Meeting) pamoja na uongozi wa Taasisi zinazokaguliwa.
5. Kupitia na kuhakiki nyaraka mbalimbali pamoja na kupata taarifa kutoka kwa wahusika ili kupata uelewa wa kazi za Taasisi zinazokaguliwa.
6. Kutumia njia na mbinu mbalimbali za ukaguzi kama ilivyoainishwa kwenye muongozo wa ukaguzi (Regularity Audit Manual).
7. Kufanya kikao cha kumaliza ukaguzi (Exit Meeting) na uongozi wa Taasisi inayokaguliwa baada ya kumaliza ukaguzi ambapo katika kikao hicho wakaguzi na uongozi wa taasisi hupitia kwa pamoja hoja zilizojitokeza wakati wa ukaguzi.
8. Kutoa ripoti ya ukaguzi ya awali (Management letter) kwa uongozi wa taasisi inayokaguliwa itakayoainisha hoja za ukaguzi pamoja na mambo mbalimbali yaliyobainika wakati wa ukaguzi na kutoa nafasi kwa uongozi kutoa majibu na vielelezo kuhusiana na ripoti hiyo kwa muda unaotakiwa kwa mujibu wa sheria.
9. Kufuatilia majibu ya hoja za ukaguzi yaliyotolewa katika ripoti ya ukaguzi ya awali ili kuweza kujiridhisha na majibu ya hoja hizo.
10. Kutoa ripoti ya ukaguzi ya mwisho kwa taasisi zinazokaguliwa inayoonesha hoja za ukaguzi zilizotolewa katika ripoti ya ukaguzi ya awali ambazo hazikupata majibu yenye kuridhisha kutokana na hoja zilizotolewa.
11. Kutoa ripoti kuu ya mwaka kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984.

## 1.4 UMUHIMU WA UKAGUZI KATIKA KUIMARISHA UTAWALA BORA

Lengo kuu la kufanya ukaguzi ni kuhakikisha kwamba fedha inayoidhinishwa na Baraza la Wawakilishi kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali kwa mujibu wa sheria inatumika ipasavyo na kwa malengo yaliyokusudiwa kwa kuleta ufanisi na tija kwa maslahi ya wananchi na taifa kwa ujumla. Aidha ukaguzi wa hesabu unalenga kuimarisha uwajibikaji wa matumizi ya rasilimali za umma na kupelekea kuimarika kwa dhana nzima ya Utawala Bora.

Kuimarika kwa utendaji wa kazi za ukaguzi kunapelekea kuongezeka na kuimarika kwa uwazi na uwajibikaji katika ukusanyaji wa mapato na matumizi ya fedha na rasilimali za umma na kuleta tija na ufanisi na kufanikisha kutekeleza malengo yaliyopangwa na Serikali kwa wakati uliopangwa. Aidha kuimarika kwa utendaji wa kazi za ukaguzi kunapelekea kuimarika kwa hali ya uchumi wa nchi na kufanikiwa kuimarika kwa hali za wananchi kwa jumla.

Katika kufanikisha malengo ya Serikali ya kuimarisha utawala bora nchini, Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali imejipanga kutekeleza majukumu yake ya kikatiba kwa kuongeza ufanisi wa kazi pamoja na kuendelea na jitihada zake za kuwajengea uwezo wafanyakazi kwa kuwapatia mafunzo na mbinu mbali mbali za ukaguzi ili kwenda sambamba na mabadiliko ya mifumo ya uhasibu na ukaguzi pamoja na mabadiliko ya kasi ya teknolojia duniani katika masuala ya udhibiti na ukaguzi wa hesabu za Serikali.

## 1.5 KAMATI ZA BARAZA LA WAWAKILISHI

Katika kuleta ufanisi na kufikia malengo ya Serikali iliyojipangia, Baraza la Wawakilishi ni nguzo imara katika kuimarisha uwajibikaji na kusimamia rasilimali za umma kuweza kutumika kwa malengo yaliyokusudiwa na kuleta tija kwa jamii. Aidha Kamati za Baraza la Wawakilishi zinatoa mchango mkubwa katika kujenga na kusimamia misingi ya utawala bora na uwajibikaji wa matumizi ya rasilimali za Umma.

Kwa kuzingatia majukumu na umuhimu wa Kamati za Baraza la Wawakilishi Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali imekuwa ikishirikiana na Kamati hizo katika kufuatilia utekelezaji wa bajeti ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar pamoja na kuhakikisha kwamba taasisi za Serikali zinatekeleza malengo waliyojipangia kama yalivyoainishwa katika Bajeti zilizoidhinishwa na Baraza la Wawakilishi.

Hata hivyo upeo wa mahusiano wa Taasisi za ukaguzi duniani (SAIs) na Mabunge (Baraza la Wawakilishi) unatofautiana baina ya nchi na nchi duniani ambapo kuna baadhi ya nchi taasisi za ukaguzi huwa ni sehemu ya Bunge (Legislative) na baadhi huwa chini ya utawala (Executive) na baadhi ya nchi nyengine Taaisisi za ukaguzi huwa haziko kokote yaani (si lagislative wala Executive). Kwa hivyo taasisi za ukaguzi zina jukumu ya kuzijengea uwezo kamati za ukaguzi za Bunge (Baraza la Wawakilishi) kwa lengo la kuzisimamia ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na kutoa ushauri na mapendekezo yao kwa taasisi za umma pamoja na Serikali.

Kutokana na utendaji kazi wa Kamati za Baraza la Wawakilishi (LAAC na PAC) matokeo ya ukaguzi yanayotolewa pamoja na suala zima la kuidhinishwa bajeti ya taasisi za ukaguzi yamewekwa chini ya mamlaka ya Kamati hizo kwa mujibu wa kifungu cha 35(1)(2) cha Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016 kwa lengo la kuimarisha ufanisi, uwazi na uwajibikaji.

Aidha kwa mujibu wa chapisho la mwaka 2006 lililotolewa na Taasisi za ukaguzi za Juu duniani (INTOSAI) linaeleza mahusiano ya Mabunge na Taasisi za ukaguzi lazima yaoneshwe katika Katiba kufuatana na matakwa ya nchi husika kama ilivyobainishwa na kifungu 112 cha Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 ambapo matoleo hayo yameeleza Taasisi za ukaguzi zinafanya kazi za ukaguzi kama mawakala wa mabunge kwa mujibu wa muongozo wa "Supreme Audit Institution".

# SURA YA PILI

## HATI ZA UKAGUZI

## 2.0 UTANGULIZI

Kwa mujibu wa Viwango vya Kimataifa vya Ukaguzi Na. 1200 (ISSAI 1200), lengo la kufanya ukaguzi wa hesabu ni kumuwezesha mkaguzi kutoa hati ya ukaguzi iliyo huru na inayoeleza iwapo hesabu zinaonesha hali halisi ya kifedha ya Shirika na Taasisi zinazojitegemea iwapo hesabu zao zimeandaliwa kwa kufuata viwango na mfumo unaokubalika.

Ukaguzi wa hesabu unafanyika ili kumpa uhakika mtumiaji wa hesabu husika kwamba hesabu hizo zimeandaliwa kwa kuzingatia viwango vinavyokubalika. Hili linafikiwa kwa kupanga na kutekeleza ukaguzi utakaomuwezesha mkaguzi kupata uhakika kwamba hesabu kwa ujumla wake hazina dosari kubwa zinazotokana na makosa ya kiutendaji au kughushi.

Hati ya ukaguzi ni maoni ya ukaguzi kuhusu hesabu zilizokaguliwa ili kumuwezesha mtumiaji kujua kama hesabu hizo zimeandaliwa kwa kufuata viwango vinavyokubalika vya uhasibu na vile vilivyotolewa na Bodi za Taaluma za uhasibu na ukaguzi za kimataifa zinazokubalika kwenye Mashirika ya Umma na Taasisi zinazojitegemea.

## 2.1 AINA ZA HATI ZA UKAGUZI ZILIZOTOLEWA

Kuna aina nne za Hati ya Ukaguzi na kila moja hutolewa kulingana na ushahidi uliokusanywa wakati wa ukaguzi. Hati hizo ni kama zifuatazo:-

### 2.1.1 Hati Inayoridhisha

Hati hii inatolewa na Mkaguzi pale anaporidhika kuwa taarifa za fedha alizokagua zimetayarishwa kwa usahihi na kwa kuzingatia viwango kubalifu vya kimataifa vinavyohusu uandaaji wa taarifa za fedha.

### 2.1.2 Hati Zisizoridhisha

Hati za Ukaguzi zilizopo kwenye kundi hili zinatolewa pale ambapo mkaguzi ameshidwa kutoa Hati inayoridhisha. Hati zilizopo kwenye kundi hili zimegawanywa katika aina tatu kama ilivyoonyeshwa hapa chini:-

### 2.1.3 Hati Yenye Shaka

Hati Yenye Shaka hutolewa pale ambapo Mkaguzi wa Hesabu za Serikali ameshindwa kupata vielelezo au ushahidi wa kuthibitisha usahihi wa taarifa za fedha zilizoandaliwa na amejiridhisha kuwa madhara yanayoweza kutokana na kukosekana kwa vielelezo au ushahidi huo yanaweza kuathiri usahihi wa taarifa hizo za fedha zilizoandaliwa.

#### 2.1.4 Hati Mbaya (Adverse Opinion)

Hati hii hutolewa pale ambapo mkaguzi amepata ushahidi na vielelezo vya kutosha kuwa dosari zilizobainika wakati wa ukaguzi kwa ujumla wake zina mapungufu makubwa na ya msingi katika usahihi wa taarifa za fedha husika.

#### 2.1.5 Kushindwa Kutoa Maoni (Disclaimer of Opinion)

Hati hii hutolewa pale ambapo mkaguzi anaposhindwa kupata ushahidi na vielelezo vinavyo jitosheleza vinavyohusiana na taarifa za fedha zilizoandaliwa kwa ajili ya ukaguzi. Hati ya aina hii inapotolewa inamaanisha kuwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ameshindwa kutoa maoni yake kutokana na dosari hizo.

### 2.2 MASUALA YENYE MSISITIZO (EMPHASIS OF MATTER) NA MAMBO MENGINEYO (OTHER MATTER)

Pale inapofaa, ripoti ya mkaguzi juu ya taarifa za kifedha inaweza kujumuisha aya yenye maswala yenye msisitizo. Aya hizo, hazibadilishi hati za ukaguzi (Hati Zisizoridhisha) na hazibadilishi maoni zaidi (kwa maoni yaliyobadilishwa) aidha pia Aya hiyo haibadilishi maoni yaliyotolewa juu ya Taarifa za fedha zilizoandaliwa.

#### 2.2.1 Aya ya Masuala yenye Msisitizo (Emphasis of Matter)

Aya hii inajumuishwa katika ripoti ya ukaguzi ikirejea maswala yaliyowasilishwa ipasavyo au kufichuliwa katika taarifa za kifedha kwamba, kwa maoni ya kitaalam ukaguzi umeona umuhimu wa kuwaeleza watumiaji wa taarifa za kifedha. Aya hii imejumuishwa katika ripoti ya ukaguzi kwa kichwa cha Habari kijulikanacho kama **'Masuala Yenye Msisitizo'.**

#### 2.2.2 Mambo Mengineyo (Other Matter)

Aya hii inajumuishwa katika ripoti ya ukaguzi ili kuweka mkazo kwenye masuala mengine nje ya yale yaliyofafanuliwa katika taarifa za Fedha ikiwemo maoni ya kitaalamu pale ambapo ukaguzi uliofanyika umeona kuna umuhimu wa kuwafahamisha watumiaji wa Taarifa za fedha. Aya hii imejumuishwa katika ripoti ya ukaguzi ikiwa na kichwa cha Habari **'Mambo Mengineyo'.**

### 2.3 MSINGI WA HATI ZA UKAGUZI

Ili kufikia kwenye hati zilizotolewa, ukaguzi ulizingatia hali halisi ya matokeo ya ukaguzi kwa kila tasisi iliyokaguliwa. Ukaguzi huo ulifanyika kulingana na matakwa ya Viwango vya Kimataifa vya Taasisi Kuu za Ukaguizi (ISSAIs). Viwango hivyo vinanitaka kuandaa mpango wa ukaguzi, kufanya ukaguzi, na kutoa ripoti ya matokeo ya ukaguzi huo. Pia, vinanitaka kufuata maadili ya ukaguzi ili kuhakikisha kuwa ukaguzi uliofanyika una ubora unaokubalika kwa hali ya juu. Ukaguzi ulijumuisha uchunguzi wa nyaraka mbalimbali zinazohusiana na kiasi cha fedha kilichoripotiwa kwenye taarifa za fedha. Pia, ulijumuisha tathmini ya makadirio na maamuzi yaliyofanywa na menejimenti ya Mawizara, Idara na Taasisi wakati wa uandaaji wa taarifa za fedha, utoshelezi wa mambo yaliyoripotiwa kwenye taarifa za fedha, iwapo sera za uhasibu zinazotumika zinaendana na mazingira halisi ya utekelezaji wa majukumu ya taasisi inayokaguliwa na kwa mujibu wa Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu katika Sekta za Umma, na kama sera hizo zinajitosheleza na zimekuwa zikitumika mwaka hadi mwaka.

Kaguzi zilizofanyika zilipangwa na kutekelezwa kwa namna ambayo iliwezesha ukusanyaji wa taarifa zote muhimu na maelezo ya menejimenti yaliyokuwa yanahitajika ili kuhakikisha upatikanaji wa kutosha wa nyaraka kwa ajili ya kutoa uhakika iwapo taarifa za fedha zilizokaguliwa hazina mapungufu makubwa yaliyosababishwa na ubadhirifu au kwa bahati mbaya.

Nilifanya ukaguzi wangu kwa uhuru na sikuwa na mgongano wa maslahi na taasisi yoyote niliyoikaguwa kwa mujibu wa kanuni za maadili zilizotolewa na Bodi ya Kimataifa ya Viwango vya Maadili kwa Wahasibu pamoja na Kanuni za Maadili zilizotolewa na Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu Tanzania na nilitekeleza wajibu wangu wa kimaadili kwa mujibu wa matakwa hayo.

Ni imani yangu kuwa ushahidi nilioupata ulikuwa sahihi na ulijitosheleza katika kutoa hati za ukaguzi na pale ambapo nilishindwa kupata ushahidi wa kutosha sikutoa hati za ukaguzi.

## 2.4 HATI ZA UKAGUZI ZILIZOTOLEWA KWA WIZARA NA TAASISI ZA SERIKALI KUU KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021

Katika mwaka wa fedha 2020/2021 jumla ya hati za ukaguzi sabini na tatu (73) zimetolewa kwa Mawizara na taasisi mbali mbali za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ambapo hati hizo zimetolewa kutokana na ukaguzi uliofanyika kupitia vitabu na kumbukumbu za hesabu kwa mujibu wa sheria na kanuni za ukaguzi. Kati ya hati 73 zilizotolewa jumla ya taasisi sitini na mbili (62) zimepata Hati zinazoridhisha, na jumla ya taasisi kumi na moja (11) zimepata Hati zisizoridhisha na hakuna taasisi iliyopata hati yenye shaka au kushindwa kutoa maoni ya ukaguzi kwa mwaka wa fedha unaoishia 30 Juni, 2021.

Orodha ya taasisi zilizokaguliwa na kupatiwa hati za ukaguzi ni kama inavyoonekana katika jadweli lifuatalo:-

**Jadweli Nambari 1: Orodha ya Wizara na Taasisi zilizopata Hati za Ukaguzi kwa mwaka wa fedha 2020/2021**

| Namba | Fungu | Wizara/Taasisi | Aina ya Hati iliyotolewa |
|---|---|---|---|
| 1. | A01 | Ofisi ya Rais na Menyekiti wa Baraza la Mapinduzi | Hati Inayoridhisha |
| 2. | A02 | Ofisi ya Rais Baraza la Mapinduzi | Hati Inayoridhisha |
| 3. | B01 | Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais | Hati Inayoridhisha |
| 4. | C01 | Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na BLW | Hati Inayoridhisha |
| 5. | C02 | Baraza la Wawakilishi | Hati Inayoridhisha |
| 6. | C03 | Tume ya Uchaguzi Zanzibar | Hati Inayoridhisha |
| 7. | C05 | Tume ya Ukimwi Zanzibar | Hati Inayoridhisha |
| 8. | Ruzuku | Kamisheni ya Kukabiliana na Maafa | **Hati Isiyoridhisha** |
| 9. | D01 | Wizara ya Nchi (OR) Tawala za Mikoa,Serikali za Mitaa na Idara Maalum | Hati Inayoridhisha |
| 10. | D02 | Jeshi la Kujenga Uchumi | **Hati Isiyoridhisha** |
| 11. | Ruzuku | Wakala wa Ulinzi JKU - (SGA) | Hati Inayoridhisha |
| 12. | D03 | Chuo cha Mafunzo | Hati Inayoridhisha |
| 13. | D04 | Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo | **Hati Isiyoridhisha** |
| 14. | D05 | Kikosi cha Zimamoto na Uokozi | Hati Inayoridhisha |
| 15. | D06 | Kikosi cha Valantia | Hati Inayoridhisha |

| Namba | Fungu | Wizara/Taasisi | Aina ya Hati iliyotolewa |
|---|---|---|---|
| 16. | D07 | Mkoa wa Mjini Magharibi | Hati Inayoridhisha |
| 17. | D08 | Mkoa wa Kusini Unguja | Hati Inayoridhisha |
| 18. | D09 | Mkoa wa Kaskazini Unguja | Hati Inayoridhisha |
| 19. | D10 | Mkoa wa Kusini Pemba | Hati Inayoridhisha |
| 20. | D11 | Mkoa wa Kaskazini Pemba | Hati Inayoridhisha |
| 21. | D12 | Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii | **Hati Isiyoridhisha** |
| 22. | E05 | Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi | Hati Inayoridhisha |
| 23. | E07 | Kamisheni ya Utumishi wa Umma | Hati Inayoridhisha |
| 24. | E08 | Tume ya Utumishi Serikalini | Hati Inayoridhisha |
| 25. | Ruzuku | Tume ya Maadili ya Viongozi | Hati Inayoridhisha |
| 26. | Ruzuku | Wakala wa Miundombinu ya TEHAMA | Hati Inayoridhisha |
| 27. | -- | Hesabu Jumuishi ya Mfuko Mkuu wa Serikali | **Hati Isiyoridhisha** |
| 28. | F01 | Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais Fedha na Mipango | Hati Inayoridhisha |
| 29. | F02 | Mfuko Mkuu wa Serikali | Hati Inayoridhisha |
| 30. | F03 | Tume ya Mipango | Hati Inayoridhisha |
| 31. | Ruzuku | Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali | Hati Inayoridhisha |
| 32. | G01 | Wizara Nchi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora | Hati Inayoridhisha |
| 33. | G02 | Mahkama Kuu Zanzibar | Hati Inayoridhisha |
| 34. | G03 | Ofisi ya Mwanasheria Mkuu | Hati Inayoridhisha |
| 35. | G04 | Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka | Hati Inayoridhisha |
| 36. | G05 | Tume ya Kurekebisha Sheria | Hati Inayoridhisha |
| 37. | H01 | Wizara ya Afya,Ustawi wa Jamii Wazee Jinsia na Watoto | **Hati Isiyoridhisha** |
| 38. | H02 | Hospitali ya Mnazi Mmoja | Hati Inayoridhisha |
| 39. | Ruzuku | Wakala wa Chakula, Dawa na Vipodozi (ZFDA) | **Hati Isiyoridhisha** |
| 40. | Ruzuku | Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu | Hati Inayoridhisha |
| 41. | J01 | Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale | Hati Inayoridhisha |
| 42. | J02 | Kamisheni ya Utalii | Hati Inayoridhisha |
| 43. | J03 | Wizara ya Habari, Vijana Utamaduni na Michezo | Hati Inayoridhisha |
| 44. | K01 | Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali | Hati Inayoridhisha |
| 45. | Ruzuku | Baraza la Mitihani Zanzibar | Hati Inayoridhisha |
| 46. | Ruzuku | Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Elimu | Hati Inayoridhisha |
| 47. | Ruzuku | Mrajis wa Baraza la Elimu | Hati Inayoridhisha |
| 48. | Ruzuku | Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu Zanzibar | Hati Inayoridhisha |
| 49. | Ruzuku | Taasisi ya Elimu Zanzibar | Hati Inayoridhisha |
| 50. | L01 | Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji Maliasili na Mifugo | **Hati Isiyoridhisha** |
| 51. | Ruzuku | Taasisi ya Utafiti na Kilimo | Hati Inayoridhisha |
| 52. | Ruzuku | Taasisi ya Utafiti wa Mifugo | Hati Inayoridhisha |
| 53. | Ruzuku | Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo | Hati Inayoridhisha |
| 54. | L02 | Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi | Hati Inayoridhisha |
| 55. | N01 | Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi | Hati Inayoridhisha |
| 56. | Ruzuku | Bodi ya Kondominio Zanzibar | Hati Inayoridhisha |
| 57. | Ruzuku | Bodi ya Uhaulishaji Ardhi Zanzibar | Hati Inayoridhisha |
| 58. | Ruzuku | Bodi ya Kudhibiti Kodi za Nyumba Zanzibar | Hati Inayoridhisha |
| 59. | Ruzuku | Bodi ya Usajili wa Wakandarasi | Hati Inayoridhisha |
| 60. | Ruzuku | Kamati ya Udhibiti wa Ujenzi wa Idara ya Mipango Miji na Vijiji | **Hati Isiyoridhisha** |

| Namba | Fungu | Wizara/Taasisi | Aina ya Hati iliyotolewa |
|---|---|---|---|
| 61. | Ruzuku | Kamisheni ya Ardhi | Hati Inayoridhisha |
| 62. | N03 | Wizara ya Maji Nishati na Madini | Hati Inayoridhisha |
| 63. | P01 | Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi | **Hati Isiyoridhisha** |
| 64. | Ruzuku | Bodi ya Usajili Wasanifu, Wahandisi na Wakadiriaji Majengo | Hati Inayoridhisha |
| 65. | Ruzuku | Wakala wa Mjengo Zanzibar | **Hati Isiyoridhisha** |
| 66. | Ruzuku | Wakala wa Karakana Kuu | Hati Inayoridhisha |
| 67. | Q01 | Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto | Hati Inayoridhisha |
| 68. | R01 | Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda | Hati Inayoridhisha |
| 69. | Ruzuku | Taasisi ya Viwango Zanzibar ZBS | Hati Inayoridhisha |
| 70. | Ruzuku | Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali | Hati Inayoridhisha |
| 71. | Ruzuku | Wakala wa Maendeleo ya Viwanda Vidogo Vidogo, Vidogo na vya Kati (SMIDA) | Hati Inayoridhisha |
| 72. | Ruzuku | Baraza la Usimamizi wa Mfumo wa Utoaji Leseni | Hati Inayoridhisha |
| 73. | Ruzuku | Tume ya Ushindani Halali wa Biashara | Hati Inayoridhisha |

## SURA YA TATU

### 3.0 TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021

### 3.1 TAARIFA ZA MAPATO NA MATUMIZI

#### 3.1.1 Taarifa za Mapato

Kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021 mapato yaliyokadiriwa kukusanywa ni jumla ya shilingi Bilioni 1,579.2 Makadirio hayo yalitarajiwa kutoka katika vyanzo mbali mbali ikiwemo mikopo, misaada ya kibajeti na washirika wa maendeleo.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 jumla ya shilingi Bilioni 944.6 zimekusanywa ambapo ni sawa na asilimia 60 ya makadirio.

#### 3.1.2 Mapato yatokanayo na Vyanzo vya Ndani

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ilikadiria kukusanya jumla ya shilingi Bilioni 1,050.00 kwa mapato yatokanayo na vyanzo vya ndani.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 makusanyo halisi ya mapato ya ndani yalikua ni shilingi Bilioni 723.60 ambapo ni sawa na asilimia 69 ya makadirio na kupelekea kujitokeza kwa upungufu wa shilingi Bilioni 326.40 sawa na asilimia 31 ya upungufu.

#### 3.1.3 Mapato yatokanayo na Washirika wa Maendeleo

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ilikadiria kukusanya jumla ya shilingi Bilioni 423.00 kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 makusanyo halisi yalikua ni shilingi Bilioni 149.90 ambapo ni sawa na asilimia 35 ya makadirio na kupelekea kujitokeza kwa upungufu wa makusanyo ya shilingi Bilioni 273.10 sawa na asilimia 65 ya makadirio.

#### 3.14 Mapato Yatokanayo na Vyanzo Vyenginevyo

Kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021 Serikali ilikadiria kukusanya jumla ya shilingi Bilioni 106 kutoka katika vyanzo mbali mbali vya kibajeti ikiwemo Mikopo ya Ndani, Mikopo ya dharura, Marejesho ya Mikopo pamoja na Misaada ya Kibajeti.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 makusanyo halisi yalikua ni shilingi Bilioni 71 ambapo ni sawa na asilimia 67 ya makadirio na kupelekea kujitokeza kwa upungufu wa makusanyo ya shilingi Bilioni 35 sawa na asilimia 33 ya makadirio.

#### 3.1.5 Taarifa ya Matumizi ya Kazi za Kawaida

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ilikadiria kutumia jumla ya shilingi Bilioni 969.30 kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilitumia jumla ya shilingi Bilioni 740.1 sawa na asilimia 76 ya makadirio.

### 3.1.6 Taarifa ya Matumizi ya Kazi za Maendeleo

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ilikadiria kutumia jumla ya shilingi Bilioni 609.90 kwa ajili ya matumizi ya kazi za Maendeleo.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilitumia jumla ya shilingi Bilioni 213.7 sawa na asilimia 35 ya makadirio.

Mchanganuo wa taarifa za mapato na matumizi ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 2**: **Mapitio ya Bajeti kwa Mwaka wa fedha 2020/2021**

| **MAPATO** | | | |
|---|---|---|---|
| | **Tarakimu ni TZS "Bilioni"** | | |
| **MAELEZO** | **BAJETI 2020/21** | | |
| **A:Mapato** | **Bajeti** | **Halisi** | **Asilimia** |
| **Mapato ya Ndani** | **1,050.0** | **723.6** | **69%** |
| ZRB | 516.7 | 304.3 | 59% |
| TRA | 383.5 | 298.1 | 78% |
| Mapato yasiyokuwa ya Kodi | 128.7 | 100.2 | 78% |
| Mapato: Wafanyakazi wa SMT | 21.0 | 21.0 | 100% |
| **Mapato ya Washirika wa Maendeleo** | **423.2** | **149.9** | **35%** |
| Mfuko wa Pamoja wa Wafadhili (BF) | 3.8 | 2.6 | 68% |
| Ruzuku kutoka Nje | 78.9 | 20.9 | 26% |
| Mkopo kutoka Nje | 340.5 | 126.4 | 37% |
| **Mapato Mengineyo** | **106** | **71** | **67%** |
| Mkopo wa Ndani | 45.0 | 54.7 | 122% |
| Mkopo wa Dharura | - | 6.9 | |
| Marejesho ya Mkopo | 61.0 | | |
| Msaada wa Kibajeti | 100T | 9.5 | |
| **Jumla Kuu** | **1,579.2** | **944.6** | **60%** |
| | | | |
| | | | |
| **MATUMIZI** | | | |
| | **Tarakimu ni TZS "Bilioni"** | | |
| | **BAJETI 2020/21** | | |
| | **Bajeti** | **Halisi** | **Asilimia** |
| **Matumizi ya Kawaida** | **969.3** | **740.1** | **76%** |
| Mshahara Mawizara | 316.8 | 274.5 | 87% |
| Mshahara Ruzuku | 123.8 | 132.4 | 107% |
| Matumizi Mengineyo Mawizara | 182.6 | 79.4 | 43% |
| Matumizi Mengineyo Ruzuku | 108.2 | 46.0 | 43% |
| Mfuko Mkuu wa Serikali | 237.9 | 197.1 | 83% |
| Malipo ya Mkopo wa Dharura | - | 6.9 | |
| Matumizi ya Uviko 19 | - | 3.8 | |
| **Matumizi ya Maendeleo** | **609.9** | **213.7** | **35%** |
| **Fedha za Serikali** | 197.3 | 82.5 | 42% |
| **Kutoka kwa Washirika wa Maendeleo** | 412.6 | 131.2 | 32% |
| **Jumla Kuu** | **1,579.2** | **953.8** | **60%** |

### 3.1.7 TAARIFA YA GAWIO LA SERIKALI

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ilikadiria kupokea jumla ya shilingi Bilioni 24.00 ikiwa ni gawio kutoka katika Mashirika mbalimbali yanayomilikiwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 gawio halisi lililopatikana ni shilingi Bilioni 15.376 ambapo ni sawa na asilimia 64.10 ya makadirio na kupelekea kujitokeza kwa upungufu wa gawio la shilingi Bilioni 8.624 sawa na asilimia 35.90 ya upungufu.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Ofisi ya Rais Fedha na Mipango kuhakikisha kuwa wanaandaa na kuonyesha katika hesabu jumuishi makisio ya mapato yanayotokana na gawio la Serikali kwa kila shirika linalomilikiwa na Serikali yanayoakisi uhalisia wa uwezo wa Shirika husika.

Jadweli hapo chini linaonesha uchambuzi wa mapato ya gawio la Serikali yaliyopokelewa kutoka katika Mashirika mbali mbali:-

**Jadweli Nambari 3: Uchambuzi wa mapato ya Gawio la Serikali**

| Namba | Shirika | Fedha za Makisio (Tshs."000") | Fedha Halisi (Tshs."000") |
|---|---|---|---|
| **Taasisi za Kibenki** | | | |
| 1. | Benki Kuu ya Tanzania (BOT) | 13,500,000 | 6,750,000 |
| 2. | Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ) | 5,300,000 | 4,975,192 |
| **Mashirika ya Umma Zanzibar** | | | |
| 3. | Shirika la Bandari Zanzibar (ZPC) | 2,000,000 | 1,768,151 |
| 4. | Shirika la Meli Zanzibar (ZSC) | 300,000 | - |
| 5. | Shirika la Bima Zanzibar (ZIC) | 3000,000 | 500,000 |
| 6. | Shirika la Umeme Zanzibar (ZECO) | 2,000,000 | 1,382,161 |
| 7. | Shirika la Biashara la Taifa (ZSTC) | 600,000 | - |
| **Jumla** | | **24,000,000** | **15,375,513** |

## 3.2 TAARIFA YA DENI LA SERIKALI

Taarifa ya muundo wa Deni la Serikali kwa mwaka wa fedha 2020/2021 linatokana na uwepo wa deni la ndani ambalo linajumuisha dhamana zinazouzwa na Benki Kuu ya Tanzania zenye ukomo tofauti kama vile dhamana za muda mrefu na hati fungani pamoja na mikopo kutoka Taasisi za ndani.

Aidha, kwa upande mwengine deni la Serikali linatokana na muundo wa deni la nje ambalo linahusisha Mikopo kutoka Taasisi za Kimataifa pamoja na Washirika wa Maendeleo ambapo kwa mujibu wa Katiba ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania deni hilo hudhaminiwa na Serikali ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania.

### 3.2.1 Deni la Ndani

Deni la ndani la Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2020/2021 limebainika kufikia jumla ya shilingi Bilioni 194.098 ikilinganishwa na kiasi cha shilingi Bilioni 156.802 zilizofikiwa mwishoni mwa tarehe 30 Juni, 2020 ambapo imebainika deni hilo kuongezeka hadi kufikia shilingi Bilioni 37.296 sawa na asilimia 23.8 ya deni la ndani lililoripotiwa mwaka jana.

### 3.2.2 Deni la Nje

Deni la nje la Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2020/2021 limebainika kufikia jumla ya shilingi Bilioni 692.867 ikilinganishwa na kiasi cha shilingi Bilioni 667.719 zilizofikiwa mwishoni mwa tarehe 30 Juni, 2020 ambapo imebainika deni hilo kuongezeka kwa shilingi Bilioni 25.148 sawa na asilimia 3.80 ya deni la nje lililoripotiwa mwaka jana.

## 3.3 UHIMILIVU WA DENI LA TAIFA

Pamoja na kubainika kuongezeka kwa Deni la Taifa kwa asilimia 3.80 kwa upande wa deni la nje ukaguzi umebaini kwa mwaka wa fedha 2020/2021 deni la Taifa bado ni himilivu kwa kuzingatia vigezo vilivyowekwa kitaifa na kimataifa kama ifuatavyo:-

- Thamani ya Deni la Ndani linalodhaminiwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imebainika kufikia jumla ya shilingi Bilioni 194.098 wakati uchumi wa Zanzibar hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 una thamani ya shilingi Bilioni 4,513.9. Hivyo uwiano wa deni la taifa dhidi ya GDP ni asilimia 4.3 wakati ukomo wa kigezo cha nchi za Uchumi wa Kati ni asilimia 70 kwa kiwango cha chini.
- Deni la Ujumla la shilingi Bilioni 886.965 na ukuwaji wa uchumi wa Zanzibar wa shilingi Bilioni 4,513.9 sawa na asilimia 19.65 ya kiwango cha asilimia 70 ya Nchi za Uchumi wa Kati kwa kiwango cha chini.
- Mapato halisi ya ndani yaliyokusanywa ya shilingi Bilioni 723.6 kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ambapo asilimia 27 ya mapato hayo ingelitosha kulipa deni lote linalodhaniwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Kutokana na mchanganuo nilioubainisha hapo juu inaonesha kuwa deni la Serikali ya Mapunduzi ya Zanzibar bado ni himilivu hivyo ukaguzi unaishauri Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuendelea kukopa zaidi ili kuendeleza utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa lengo la kuwaletea maendeleo wananchi wa Zanzibar.

## 3.4 MAMBO YALIYOBAINIKA KATIKA UKAGUZI WA MFUKO MKUU WA SERIKALI

Kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ukaguzi ulipokea taarifa za Hesabu Jumuishi (Consolidated Financial Statement) ya Mfuko Mkuu wa Serikali katika maeneo matatu tofauti ambayo ni Hesabu Jumuishi ya Taasisi za Kibajeti inayojumuisha Wizara na Idara za Serikali, Hesabu Jumuishi za Serikali za Mitaa pamoja na Hesabu Jumuishi za Mashirika ya Umma, Mamlaka na Taasisi zinazojitegemea.

### 3.4.1 DOSARI KATIKA HESABU JUMUISHI

Ukaguzi uliofanyika katika Mfuko Mkuu wa Serikali kupitia Hesabu Jumuishi imebainika kuwepo kwa baadhi ya dosari mbali mbali katika Hesabu iliyowasilishwa kwa ajili ya ukaguzi ikiwemo mapungufu katika uandaaji na uwasilishwaji wa hesabu jumuishi kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2021. Kutokana na hali hiyo, imepelekea hesabu za Mfuko Mkuu wa Serikali kutoonyesha sura sahihi na halisi. Baadhi ya dosari zilizobainika ni kama ifuatavyo:-

#### 3.4.1.1 Kukosekana kwa uchambuzi mzuri wa taarifa za Hesabu Jumuishi

Ukaguzi ulipitia taarifa ya jumla ya mapato na matumizi ya Hesabu Jumuishi kwa kulinganisha na taarifa moja moja ya kila taasisi kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2021 na kubaini kukosekana kwa uchambuzi mzuri wa vyanzo vya mapato vya kila taasisi pamoja na uchambuzi wa matumizi wa kila Taasisi ili kuweza kulinganisha na kujiridhisha juu ya usahihi wa taarifa za fedha katika Hesabu Jumuishi.

Dosari hizo zimebainika katika taarifa za mapato na matumizi za kila taasisi katika Hesabu Jumuishi za Taasisi za Kibajeti, Mashirika, Taasisi zinazojitegemea ,Mamlaka na Mifuko ya Umma. Uchambuzi wa taarifa hizo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 4:Mapato ya kodi (Taxation) katika hesabu jumuishi ya Taasisi za kibajeti**

| Fungu | Ofisi ya Rais Fedha na Mipango | Makisio kwa mwaka 2020/2021 | Mapato halisi Kwa mwaka 2020/2021 |
|---|---|---|---|
| F01 | ZRB | 516,726,006,000 | 304,343,696,000 |
| | TRA | 383,540,769,000 | 298,157,865,000 |
| | PAYE From URT | 21,000,000,000 | 21,000,000,000 |
| | **Jumla** | **921,266,775,000** | **623,501,561,000** |

**Jadweli Nambari 5 : Mapato ya fedha (Finance Income) na Ruzuku kutoka Serikalini**

| Namba | Chanzo cha mapato | Kiasi cha fedha (Tshs) |
|---|---|---|
| **Mapato ya Fedha (Finance Income)** | | |
| 1. | Interest received on fixed Deposit | 10,217,960,438.8 |
| 2. | Interest from Tresury bill/Short call | 9,908,325,274.05 |
| 3. | Interest from Govt stock/Loan | 4,954,162,637.00 |
| 4. | Interest fromTresury bond | 8,669,784,614.79 |
| 5. | Interest from Other Institution loan | 7,740,879,120.35 |
| 6. | Interest Income | 6,502,338,461.09 |
| 7. | Interest on commercial loan and Overdraft | 8,360,149,449.98 |
| 8. | Interest on Other Investment | 9,908,325,274.05 |
| 9. | Income on Tresury Bills | 4,149,111,208.51 |
| 10. | Income on Tresury Bond | 7,555,098,021.46 |
| **Jumla** | | **77,966,134,500.08** |
| | | |
| **Mapato ya Fedha Yatokanayo na Ruzuku** | | |

| Namba | Chanzo cha mapato | Kiasi cha fedha (Tshs) |
|---|---|---|
| 11. | Mishahara Taslim | 6,126,487,631.23 |
| 12. | Matumizi ya Kawaida taslim | 2,722,883,391.66 |
| 13. | Matumizi ya Maendeleo | 2,382,522,967.70 |
| 14. | Personel Emoulment in kind | 1,361,441,695.83 |
| 15. | Other Charge in kind | 1,531,621,907.81 |
| 16. | Development in kind | 7,828,289,751.01 |
| 17. | Asset contribution- Non Current Assets | 5,971,563,578.76 |
| **Jumla** | | **27,924,810,924** |

Kukosekana kwa uchambuzi mzuri wa taarifa za fedha kumepelekea ukaguzi kushindwa kujiridhisha juu ya usahihi wa taarifa iliyowasilishwa kwa ajili ya ukaguzi katika hesabu jumuishi.

Ukaguzi unaishauri Serikali kupitia Mfuko Mkuu wa Serikali kuhakikisha inaweka utaratibu madhubuti wa uwasilishaji wa taarifa za fedha za kila taasisi zilizoripotiwa katika hesabu jumuishi na kuimarisha uwepo wa uwazi katika taarifa za fedha kwa lengo la kuboresha upatikanaji wa taarifa sahihi za fedha za Serikali zitakazotoa sura sahihi na halisi.

#### 3.4.1.2 Kutotambuliwa kwa taarifa za mapato na matumizi ya baadhi ya taasisi za Serikali katika Hesabu Jumuishi

Ukaguzi ulipitia taarifa za fedha za Taasisi zote za umma katika hesabu jumuishi zilizojigawa katika hesabu za Tasisi za kibajeti na Mashirika ya Umma , Taasisi zinazojitegemea na Mamlaka za Serikali na kubaini kwamba baadhi ya taasisi hazikujumuishwa katika hesabu zote jumuishi zilizo orodheshwa hapo juu. Baadhi ya taasisi ambazo hazikutambuliwa katika hesabu jumuishi za Mashirika ni kama zifuatazo:-

- Mamlaka ya Udhibiti wa Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia (ZPRA).
- Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA).
- Mamlaka ya kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi (ZAECA).
- Mamlaka ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma (ZPPDA).
- Shirika la Utangazaji Zanzibar (ZBC).
- Shirika la Magazeti ya Serikali (ZGP).

Kutokutambuliwa kwa taarifa za mapato na matumizi ya taasisi zilizo orodheshwa hapo juu kunatia shaka juu ya usahihi na ukamilifu wa hesabu jumuishi za Serikali.

Ukaguzi unaishauri Serikali kupitia Ofisi ya Rais Fedha na Mipango kujumuisha taarifa za fedha za Taasisi zote za Umma ili kuweza kupatikana usahihi na uhalisia wa hesabu za fedha.

#### 3.4.1.3 Kukosekana kwa uwiano wa chati ya hesabu (Chart of Accounts) katika uandaaji wa taarifa za fedha za Mashirika ya Umma

Mapitio ya hesabu za Mashirika ya Umma, Mamlaka za Serikali na Taasisi zinazojitegemea, ukaguzi umebaini kutokuwepo kwa uwiano baina ya chati ya hesabu ya Taasisi za kibajeti na chati ya hesabu inayotumika katika Mashirika ya Umma, Mamlaka na Taasisi zinazojitegemea hali inayokwaza utaratibu wa uandaaji na uwasilishaji wa hesabu jumuishi za Serikali.

Kukosekana kwa chati ya hesabu inayofanana kwa Mashirika ,Mamlaka za Serikali na Taasisi zinazojitegemea kunakwaza utaratibu wa uandaaji na uwasilishaji wa hesabu jumuishi za Serikali.

Ukaguzi unashauri Uongozi wa Ofisi ya Rais Fedha na Mipango kupitia Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali kufanyia kazi changamoto ya utofauti wa Chati za Hesabu za Mashirika,Mamlaka za Serikali na Taasis zinazojitegemea.

#### 3.4.1.4 Kukosekana kwa mfumo mzuri wa uwekaji wa taarifa za mali za Kudumu

Kifungu cha 29 cha Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016 kimeelezea moja kati ya majukumu ya Afisa muhasibu kuhusiana na usimamizi wa mali na madeni katika kutimiza majukumu ya usimamizi wa mali, Afisa mhasibu atatunza daftari la mali zote zilizopo chini ya udhibiti wa Taasisi za umma.

Ukaguzi umebaini uwepo wa changamoto kubwa katika usimamizi wa mali za umma ikiwemo kukosekana kwa daftari la kutunzia mali za kudumu (Fixed Asset) kwa baadhi ya taasisi nyingi za Serikali ikiwemo Mawizara, Mashirika ya Umma , Mamlaka za Serikali za Mitaa pamoja na Taasisi zinazojitegemea. Aidha mapitio ya hesabu za Taasisi zinazotumia mfumo wa hesabu usio taslim imebainika kwamba mfumo wa uwekaji wa taarifa za mali za kudumu unatofautiana baina ya Taasisi moja na nyengine hali inayopelekea kukwanza utaratibu wa kuandaa hesabu jumuishi za Mawizara Mashirika, Mamlaka za Serikali za Mitaa pamoja na Taasisi zazojitegemea.

Kukosekana kwa mfumo unaofanana wa uwekaji wa taarifa na kumbukumbu za mali za kudumu unakwaza utaratibu mzima wa uandaaji wa hesabu Jumuishi za Mawizara, Mashirika , Mamlaka za Serikali za Mitaa pamoja na Taasisi zinazojitegemea.

Ukaguzi unashauri Uongozi wa Ofisi ya Rais Fedha na Mipango kupitia Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali kuzifanyia kazi changamoto ya kukosekana kwa mfumo mzuri wa uwekaji wa taarifa na kumbukumbu za mali za kudumu.

#### 3.4.1.5 Kutojumuishwa kwa bakaa ya fedha za Miradi ya Maendeleo katika Hesabu Jumuishi za Serikali

Ukaguzi umebaini kwamba katika hesabu jumuishi ya hesabu za Taasisi za kibajeti , hazikujumuisha bakaa ya fedha katika miradi ya Maendeleo inayosimamiwa na taasisi hizo kwa kipindi cha mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni 2021.

Aidha, hesabu ya Wizara husika zinazosimamia miradi hiyo zilionesha kutokuwepo kwa bakaa yoyote ambapo uhalisia unaonesha kuwa miradi hiyo ina bakaa ya fedha kwa kuwa inaendelea na utekelezaji wake kwa kipindi cha zaidi ya mwaka mmoja hali iliyopelekea taarifa ya bakaa hizo kutojumuishwa katika hesabu jumuishi za taasisi za kibajeti za Serikali kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2021.

Kutojumuisha bakaa ya fedha katika miradi ya Maendeleo katika hesabu jumuishi kunapelekea hesabu jumuishi kutokutoa sura halisi na Sahihi.

Ukaguzi unashauri Uongozi wa Ofisi ya Rais Fedha na Mipango kupitia Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali kuhakikisha kwamba bakaa ya fedha za miradi ya maendeleo inajumuishwa katika hesabu za Wizara pamoja Hesabu jumuishi.

#### 3.4.1.6 Kutokufunga hesabu kwa Taasisi za Serikali zinazopokea Ruzuku Serikalini

Ukaguzi umepitia hesabu jumuishi za Taasisi za kibajeti za Serikali na kubaini kwamba baadhi ya taasisi zinazopokea ruzuku kutoka Serikali hazikufunga hesabu na kuziwasilisha kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Miongoni mwa taasisi hizo ni Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana, Tume ya Utangazaji pamoja na COSOZA.

Kutofunga hesabu kwa taasisi hizo kumepelekea kukosekana kwa uwazi wa taarifa za mapato na matumizi ya taasisi hizo.

#### 3.4.1.7 Mapungufu yaliyobainika katika taarifa za uwekaji wa kumbukumbu za madeni ya Serikali

Ukaguzi umebaini kwamba kitengo cha madeni ya Serikali hakina mfumo rasmi wa kielektroniki wa uwekaji wa kumbukumbu za taarifa za madeni ya Serikali badala yake inatumia utaratibu wa uwekaji wa kumbukumbu za madeni kwa kutumia “Excel” katika uwekaji wa taarifa za madeni.

Ukaguzi unashauri Uongozi wa Ofisi ya Rais Fedha na Mipango kupitia Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali kuhakikisha kwamba inaboresha uwekaji wa kumbukumbu za madeni ya Serikali katika mfumo unaotambulika (IFMIS).

# SURA YA NNE

## 4.0 MUHTASARI WA MAMBO YALIYOBAINIKA KATIKA UKAGUZI WA MWAKA WA FEDHA 2020/2021

Sura hii inaelezea muhtasari wa mambo yaliyobainika katika ukaguzi wa hesabu kwa mwaka wa fedha 2020/2021, ukaguzi ulibaini dosari mbali mbali ambazo hadi kukamilika kwa ukaguzi hazikupatiwa majibu au majibu yake hayakuridhisha hali iliyopelekea kujitokeza kwa hoja za ukaguzi.

## 4.1 DOSARI ZA KIUTENDAJI ZILIZOBAINIKA KATIKA UKAGUZI

Katika ukaguzi wa hesabu wa mwaka wa fedha 2020/2021 kulijitokeza dosari za kiutendaji ambazo zimepelekea kuathiri utendaji wa taasisi zilizokaguliwa pamoja na utekelezaji wa sheria mbali mbali.

Dosari hizo ni kama zifuatazo:-

1) Mfumo wa udhibiti wa ndani.
2) Utekelezaji wa Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma na Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma.
3) Usimamizi wa matumizi.
4) Mifumo ya ukusanyaji wa mapato.
5) Usimamizi wa mikataba.

### 1) Mfumo wa udhibiti wa ndani

Mfumo wa udhibiti wa ndani ni taratibu zilizowekwa kwa mujibu wa sheria za usimamizi wa fedha ambazo zinahitajika kuwa imara ili kuweza kusaidia taasisi za umma kuweza kufanya kazi zake kwa weledi na kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa sheria.

Ukaguzi ulibaini udhaifu katika mfumo wa udhibiti wa ndani kwa baadhi ya Taasisi na Mawizara kwa kutokuwa na Kamati za Ukaguzi wa Ndani au kutokufanyakazi kwa kamati hizo. Kutokufanyakazi kwa kamati za ukaguzi wa ndani (Audit Committe) kunaweza kupelekea dosari za kiutendaji kushindwa kuchukuliwa hatua za awali pale zinapojitokeza.

Aidha ukaguzi umebaini vitengo vya ukaguzi wa ndani (Internal Audit Unit) kwa baadhi ya Taasisi na Wizara zilizokaguliwa hazikuwasilisha ripoti za ukaguzi wa hesabu katika kipindi cha ukaguzi pamoja na kushindwa kukutana kwa kamati za ukaguzi wa ndani kwa lengo la kuzifanyia kazi ripoti za ukaguzi na kutoa mapendekezo kwa uongozi wa taasisi husika.

### 2) Utekelezaji wa Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016 pamoja na Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016.

Ukaguzi umebaini kutokufuatwa kikamilifu kwa Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016 pamoja na Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016 kwa baadhi ya Wizara na Taasisi jambo ambalo limepelekea kujitokeza kwa dosari za ukiukwaji wa taratibu na miongozo ya sheria hizo.

**3) Usimamizi wa matumizi**

Ukaguzi umebaini dosari katika Usimamizi wa matumizi kwa baadhi ya taasisi za Serikali. Kutokuwepo kwa mfumo mzuri wa usimamizi wa matumizi kumepelekea ukaguzi kushindwa kuthibitisha uhalali wa baadhi ya matumizi kwa Wizara na Taasisi za Umma jambo ambalo limepelekea kujitokeza kwa viashiria vya upotevu wa fedha za umma.

**4) Mifumo ya ukusanyaji wa mapato**

Ukaguzi umebaini dosari katika mifumo ya ukusanyaji wa mapato kwa baadhi ya taasisi za Serikali. Kutokuwepo kwa mfumo mzuri ya ukusanyaji wa mapato kumepelekea ukaguzi kushindwa kuthibitisha uhalali wa makusanyo yaliyokusanywa na Wizara na Taasisi za umma kwa kukosekana kwa makadirio ya mapato,mapato halisi yaliyokusanywa na kuwasilishwa pamoja na kutokujulikana chanzo kilichokusanya mapato hayo.

**5) Usimamizi wa mikataba**

Ukaguzi umebaini dosari katika usimamizi wa mikataba kwa baadhi ya Wizara na Taasisi za Serikali ikiwemo kukiuka vipengele muhimu vilivyoainishwa katika mikataba hali iliyopelekea kutokufikiwa kwa malengo yaliyopangwa katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kuwepo kwa ukiukwaji wa vipengele hivyo kumepelekea kwa baadhi ya miradi kutokamilika na kutofikia malengo yaliyokusudiwa.

Aidha, kujitokeza kwa baadhi ya Wizara na Taasisi kutelekeza miradi ya maendeleo kwa kutumia rasimu ya Mkataba jambo ambalo linaweza kupelekea kuitia hasara Serikali kwa kukosekana ushauri wa kitaalamu kuhusiana na mikataba hiyo kwa kubainika kufanya malipo bila ya kuzingatia vipegele vya malipo na kujitokeza kwa baadhi ya wazabuni kulipwa asilimia 100 ya malipo yote bila ya kukamilika kwa kazi iliyotarajiwa na hatimae kuitia hasara Serikali.

## 4.2 UWASILISHAJI WA HESABU ZA MWISHO WA MWAKA WA FEDHA 2020/2021 KWA AJILI YA UKAGUZI

Kwa mujibu wa kifungu namba 119(1) cha Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016, Wizara na Taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar zinatakiwa zitayarishe na ziwasilishe kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, hesabu za mwisho wa mwaka ndani ya miezi mitatu baada ya kumalizika mwaka wa fedha ambapo hesabu hizo zitajumuisha taarifa za mapato na matumizi ya Taasisi hizo.

Kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021 imebainika kwamba uwasilishaji wa taarifa za hesabu za Serikali umeimarika ambapo hesabu hizo zimewasilishwa kwa wakati kama ifuatavyo:-

**Jadweli Nambari 6: Orodha ya Wizara na Taasisi zilizowasilisha Hesabu kwa Ukaguzi**

| Namba | Fungu | Wizara/Taasisi | Tarehe ya kuwasilisha hesabu |
|---|---|---|---|
| 1. | A01 | Ofisi ya Rais na Menyekiti wa Baraza la Mapinduzi | 20/09/2021 |
| 2. | A02 | Ofisi ya Rais Baraza la Mapinduzi | 20/09/2021 |
| 3. | B01 | Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais | 20/09/2021 |
| 4. | C01 | Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na BLW | 03/09/2021 |
| 5. | C02 | Baraza la Wawakilishi | 21/09/2021 |
| 6. | C03 | Tume ya Uchaguzi Zanzibar | 27/09/2021 |
| 7. | C05 | Tume ya Ukimwi Zanzibar | 30/09/2021 |
| 8. | Ruzuku | Kamisheni ya Kukabiliana na Maafa | 13/09/2021 |
| 9. | D01 | Wizara ya Nchi (OR) Tawala za Mikoa,Serikali za Mitaa na Idara Maalum | 29/09/2021 |
| 10. | D02 | Jeshi la Kujenga Uchumi | 30/09/2021 |
| 11. | Ruzuku | Wakala wa Ulinzi JKU - (SGA) | 04/10/2021 |
| 12. | D03 | Chuo cha Mafunzo | 30/09/2021 |
| 13. | D04 | Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo | 30/09/2021 |
| 14. | D05 | Kikosi cha Zimamoto na Uokozi | 22/09/2021 |
| 15. | D06 | Kikosi cha Valantia | 30/09/2021 |
| 16. | D07 | Mkoa wa Mjini Magharibi | 21/09/2021 |
| 17. | D08 | Mkoa wa Kusini Unguja | 20/09/2021 |
| 18. | D09 | Mkoa wa Kaskazini Unguja | 30/09/2021 |
| 19. | D10 | Mkoa wa Kusini Pemba | 28/10/2021 |
| 20. | D11 | Mkoa wa Kaskazini Pemba | 25/10/2021 |
| 21. | D12 | Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii | 30/09/2021 |
| 22. | E05 | Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi | 29/09/2021 |
| 23. | E07 | Kamisheni ya Utumishi wa Umma | 27/09/2021 |
| 24. | E08 | Tume ya Utumishi Serikalini | 22/09/2021 |
| 25. | Ruzuku | Tume ya Maadili ya Viongozi | 29/09/2021 |
| 26. | Ruzuku | Wakala wa Miundombinu ya TEHAMA | 30/09/2021 |
| 27. | -- | Hesabu Jumuishi ya Mfuko Mkuu wa Serikali | 30/11/2021 |
| 28. | F01 | Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais Fedha na Mipango | 27/09/2021 |
| 29. | F02 | Huduma za Hesabu za Mfuko Mkuu wa Serikali | 28/09/2021 |
| 30. | F03 | Tume ya Mipango | 29/09/2021 |
| 31. | Ruzuku | Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali | 30/09/2021 |
| 32. | G01 | Wizara Nchi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora | 28/09/2021 |
| 33. | G02 | Mahkama Kuu Zanzibar | 30/09/2021 |
| 34. | G03 | Ofisi ya Mwanasheria Mkuu | 30/09/2021 |
| 35. | G04 | Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka | 30/09/2021 |
| 36. | G05 | Tume ya Kurekebisha Sheria | 30/09/2021 |
| 37. | H01 | Wizara ya Afya,Ustawi wa Jamii Wazee Jinsia na Watoto | 24/09/2021 |
| 38. | H02 | Hospitali ya Mnazi Mmoja | 30/09/2021 |
| 39. | Ruzuku | Wakala wa Chakula, Dawa na Vipodozi (ZFDA) | 29/09/2021 |
| 40. | Ruzuku | Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu | 17/09/2021 |
| 41. | J01 | Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale | 30/09/2021 |
| 42. | J02 | Kamisheni ya Utalii | 27/09/2021 |

| Namba | Fungu | Wizara/Taasisi | Tarehe ya kuwasilisha hesabu |
|---|---|---|---|
| 43. | J03 | Wizara ya Habari, Vijana Utamaduni na Michezo | 30/09/2021 |
| 44. | K01 | Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali | 30/09/2021 |
| 45. | Ruzuku | Baraza la Mitihani Zanzibar | 27/09/2021 |
| 46. | Ruzuku | Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Elimu | 24/09/2021 |
| 47. | Ruzuku | Mrajis wa Baraza la Elimu | 01/10/2021 |
| 48. | Ruzuku | Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu Zanzibar | 22/09/2021 |
| 49. | Ruzuku | Taasisi ya Elimu Zanzibar | 22/09/2021 |
| 50. | L01 | Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji Maliasili na Mifugo | 27/10/2021 |
| 51. | Ruzuku | Taasisi ya Utafiti na Kilimo | 27/09/2021 |
| 52. | Ruzuku | Taasisi ya Utafiti wa Mifugo | 30/09/2021 |
| 53. | Ruzuku | Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo | 07/09/2021 |
| 54. | L02 | Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi | 20/09/2021 |
| 55. | N01 | Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi | 29/09/2021 |
| 56. | Ruzuku | Bodi ya Kondominio Zanzibar | 30/09/2021 |
| 57. | Ruzuku | Bodi ya Uhaulishaji Ardhi Zanzibar | 28/09/2021 |
| 58. | Ruzuku | Bodi ya Kudhibiti Kodi za Nyumba Zanzibar | 30/09/2021 |
| 59. | Ruzuku | Bodi ya Usajili wa Wakandarasi | 24/09/2021 |
| 60. | Ruzuku | Kamati ya Udhibiti wa Ujenzi wa Idara ya Mipango Miji na Vijiji | 30/09/2021 |
| 61. | Ruzuku | Kamisheni ya Ardhi | 29/09/2021 |
| 62. | N03 | Wizara ya Maji Nishati na Madini | 29/09/2021 |
| 63. | P01 | Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi | 05/10/2021 |
| 64. | Ruzuku | Bodi ya Usajili Wasanifu, Wahandisi na Wakadiriaji Majengo | 24/09/2021 |
| 65. | Ruzuku | Wakala wa Mjengo Zanzibar | 08/09/2021 |
| 66. | Ruzuku | Wakala wa Karakana Kuu | 24/09/2021 |
| 67. | Q01 | Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto | 24/09/2021 |
| 68. | R01 | Wizara ya Biashara na Viwanda | 30/09/2021 |
| 69. | Ruzuku | Taasisi ya Viwango Zanzibar ZBS | 30/09/2021 |
| 70. | Ruzuku | Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali | 27/09/2021 |
| 71. | Ruzuku | Wakala wa Maendeleo ya Viwanda Vidogo Vidogo, Vidogo na vya Kati (SMIDA) | 30/09/2021 |
| 72. | Ruzuku | Baraza la Usimamizi wa Mfumo wa Utoaji Leseni | 27/09/2021 |
| 73. | Ruzuku | Tume ya Ushindani Halali wa Biashara | 29/09/2021 |

## SURA YA TANO

### 5.0 DOSARI ZA UJUMLA ZILIZOBAINIKA KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021

Katika mwaka wa fedha 2020/2021 imebainika uwepo wa dosari mbali mbali zinazotokana na makosa ya kiutendaji pamoja na ukiukwaji wa sheria mbali mbali ambapo imepelekea uwepo wa dosari hizo kujitokeza mara kwa mara kwa kila taasisi au baadhi ya taasisi zilizopo chini ya Serikali Kuu. Kuwepo kwa dosari hizo kunaweza kukapelekea kuharibu mtazamo wa hati za ukaguzi na hatimae taasisi kuweza kupata hati za ukaguzi usioridhisha au kushindwa kutoa maoni ya ukaguzi, baadhi ya dosari za ujumla zilizobainika kutoka katika Taasisi za Umma pamoja na Wizara mbali mbali ni kama inavyobainishwa hapo chini:-

#### 5.1.1.1 Mapungufu yaliyojitokeza katika ufanyaji kazi wa kamati ya ukaguzi

Kifungu 118(1) cha Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016 kinamtaka Katibu Mkuu au Mkuu wa Taasisi kuanzisha kamati ya ukaguzi kwa ajili ya kutathmini udhibiti wa ndani na pia kifungu nambari 30 cha kanuni ya fedha ya mwaka 2005 inazitaka Taasisi zote (Wizara) kuanzisha kamati hiyo ya ukaguzi.

Ukaguzi umebaini Wizara pamoja na taasisi mbali mbali bado hazina usimamizi mzuri wa udhibiti wa ndani kwa kutokuanzisha vitengo au kwa kutokufanya kazi kwa vitengo hivyo kwa mujibu wa utaratibu, au kujitokeza dosari mbali mbali za kiutendaji ambazo zinakwaza kamati hizo kufanya kazi zake kwa mujibu wa sheria jambo ambalo linapelekea kamati za ukaguzi (Audit Committee) pamoja na kitengo cha ukaguzi wa ndani (Internal Audit Unit) kutokupitia kwa ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, hesabu za mwisho wa mwaka pamoja na kushindwa kutoa maoni ya marekebisho ya dosari na kasoro mbali mbali zilizobainishwa katika ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Taasisi zilizobainika kuwa na dosari hizo ni zifuatazo:-

**Jadweli Nambari 7 : Dosari za kiutendaji zilizobainika kwa vitengo vya usimamizi na udhibiti wa ndani**

| Namba | Jina la Taasisi | Dosari zilizobainika | | |
|---|---|---|---|---|
| | | Kamati ya Ukaguzi | Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani | Bodi ya Zabuni |
| 1. | Mkoa wa Mjini Magharibi | Kutokufanya kazi vizuri kwa Kamati | Kutokuwasilisha ripoti zake kwa Kamati ya Ukaguzi | Kukosekana kwa taarifa na kumbu kumbu za vikao. |
| 2. | Kamisheni ya Utalii Pemba | - | Kutokuwepo kwa kitengo cha Ukaguzi wa ndani. | - |
| 3. | Kamisheni ya Ardhi Pemba | - | Kutokuwepo kwa kitengo cha Ukaguzi wa ndani. | - |
| 4. | Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali | - | Kutokuwepo kwa kitengo cha Ukaguzi wa ndani. | - |
| 5. | Wakala wa Serikali wa Uchapaji | - | Kutokuwepo kwa kitengo cha Ukaguzi wa ndani. | - |
| 6. | Wakala wa Karakana Kuu ya Magari Zanzibar | - | Kutokuwepo kwa kitengo cha Ukaguzi wa ndani. | - |

| Namba | Jina la Taasisi | Dosari zilizobainika | | |
|---|---|---|---|---|
| | | Kamati ya Ukaguzi | Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani | Bodi ya Zabuni |
| 7. | Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali (BPRA) | - | - | Kukosekana kwa Afisa Ununuzi |
| 8.<br>9.<br>10. | Wakala wa ulinzi JKU | - | - | Kukosekana kwa kitengo cha Ununuzi<br>Kukosekana kwa Afisa Ununuzi<br>Kukosekana kwa mpango wa Ununuzi |
| 11. | Kikosi cha Valantia | - | - | Kutofanyiwa marekebisho mpango wa Ununuzi |
| 12. | Mamlaka ya Mazingira (ZEMA) | - | Kutokufanya kazi vizuri | - |
| 13. | Wizara ya Nchi Ofisi ya Makamo wa kwanza wa Rais | - | - | Kukosekana kwa Mpango wa Ununuzi |
| 14. | Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ | Kutokuwepo kwa Kamati ya Ukaguzi | - | - |
| 15. | Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee Jinsia na Watoto | Kutokufanya kazi vizuri kwa Kamati | - | - |

Ukaguzi unashauri Taasisi za Umma pamoja na Wizara za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuhakikisha zinaweka udhibiti mzuri wa ndani ikiwemo kuvijengea uwezo vitengo vya ukaguzi wa ndani pamoja na Kamati za ukaguzi kwa kuvipatia mafunzo ya muda mfupi juu ya namna bora ya kutekeleza kazi zao ikiwemo kuzipitia na kuzitolea ufafanuzi ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa lengo la kuzishauri taasisi zao kufanya maboresho kwa dosari zote zitakazobainika kwa lengo la kuhakikisha kunakuwa na matumizi mazuri ya fedha na rasilimali za umma.

### 5.1.1.2 Ucheleweshaji wa kuwasilisha taarifa za hesabu za mwisho wa mwaka

Kwa mujibu wa kifungu nambari 119(1) cha Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016 kinawataka wakuu wa taasisi kutayarisha taarifa za mapato na matumizi na kuziwasilisha kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ndani ya kipindi cha miezi mitatu baada ya kukamilika kwa matumizi.

Ukaguzi umebaini baadhi ya Wizara na taasisi mbalimbali zimechelewa kuwasilisha hesabu za mapato na matumizi yanayosimamiwa na taasisi hizo kwa ajili ya ukaguzi kwa mujibu wa kifungu 119(1). Kuchelewa kuwasilisha taarifa za hesabu za mwisho wa mwaka kwa wakati kunapelekea kujitokeza ugumu wa kuzifanyia kazi taarifa hizo ikiwemo kuzitolea maoni ya kitaalamu kutokana na kujitokeza kwa uharaka wa kuwahi kuwasilisha taarifa zilizokaguliwa kwa Mheshimiwa Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa mujibu wa matakwa ya kifungu 122 cha Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984.

Ukaguzi unawashauri maafisa masuuli kuhakikisha wanawasilisha taarifa zao za hesabu za mwisho wa mwaka kwa wakati ili ziweze kutolewa maoni ya kitaalamu na kupelekea kuziwasilisha taarifa hizo kwa Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa mujibu wa sheria.

Baadhi ya Taasisi zilizobainika kuchelewesha kuwasilisha hesabu za mwisho wa mwaka ni kama zinavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 8 : Taasisi zilizochelewa kuwasilisha hesabu za mwisho wa mwaka**

| Namba | Fungu | Wizara/Taasisi | Tarehe ya uwasilishaji |
|---|---|---|---|
| 1. | P01 | Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi | 5/10/2021 |
| 2. | L01 | Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji Maliasili na Mifugo | 27/10/2021 |
| 3. | Ruzuku | Mrajis wa Baraza la Elimu | 1/10/2021 |
| 4. | D10 | Mkoa wa Kusini Pemba | 28/10/2021 |
| 5. | D11 | Mkoa wa Kaskazini Pemba | 25/10/2021 |
| 6. | Ruzuku | Wakala wa Ulinzi JKU - (SGA) | 04/10/2021 |

### 5.1.1.3 Kutokuwepo kwa makadirio ya Mapato

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwa baadhi ya Wizara na Taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar zinakusanya mapato kupitia vyanzo mbali mbali walivyonavyo na pia hufanya matumizi ya mapato hayo bila ya kuwepo kwa makadirio ya mapato, kutokuainishwa kwa chanzo cha mapato na fedha inayotakiwa kukusanywa kwa chanzo hicho. Aidha imebainika uwepo wa makusanyo mbali mbali yanayofanyika kupitia hesabu ya mapato kwa baadhi ya Taasisi zilizopo chini ya Ofisi za Wakuu wa Mikoa katika ngazi za Wilaya na baadae fedha hiyo huwasilishwa katika Mfuko Mkuu wa Hazina, dosari iliyobainika na ukaguzi ni kukosekana kujulikana kwa makadirio ya mapato kwa lengo la kuweza kupima ufanisi uliofikiwa kwa kila chanzo cha mapato.

Kukosekana kwa makadirio ya vianzio vya mapato na mapato halisi yaliyokusanywa na kuwasilishwa Mfuko Mkuu wa Hazina kunapelekea kujitokeza kwa viashiria vya upotevu wa mapato ambayo yanayoweza kufanyika bila ya kufuata taratibu, kanuni na sheria ya usimamizi wa fedha za umma. Taasisi zilizobainika kuwepo kwa dosari hiyo ni kama zifuatazo:-

**Jadweli Nambari 9 : Taasisi zilizokuwa hazina makadirio ya vianzio vya makusanyo ya mapato**

| Namba | Jina la Taasisi |
|---|---|
| 1. | Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi |
| 2. | Wizara ya Maji, Nishati na Madini |
| 3. | Wakala wa Miundombinu ya TEHAMA Zanzibar |

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016.

Ukaguzi unashauri Taasisi za Umma ni vyema kuweka makadirio kwa kila chanzo cha makusanyo ya mapato kwa lengo la kuweza kufanya tathmini juu ya utendaji na utekelezaji wa miradi ya maendeleo pamoja na uendeshaji wa kazi za kawaida, aidha kuwepo kwa makadirio ya vianzio vya mapato kunaweza kupelekea Taasisi za Umma kuweza kuibua vyanzo vipya vya ukusanyaji wa mapato pamoja na kuziba mianya ya upotevu wa mapato ambayo yatakusanywa na kutumika kinyume na utaratibu.

#### 5.1.1.4 Kukosekana kwa kumbu kumbu za mapato yaliopelekwa Mfuko Mkuu wa Serikali

Kwa mujibu wa kifungu namba 78(6) cha Kanuni za Fedha za mwaka 2005 kinaeleza kwamba "Maelezo ya mapato ya hazina lazima yaonekane katika daftari la fedha taslim la taasisi husika kwa kuthibitisha mapato halisi yaliokusanywa".

Ukaguzi umebaini Ofisi za Wakuu wa Mikoa zinapokea mapato yaliyokusanywa kutoka katika ngazi za Wilaya na kuziwasilishwa Mfuko Mkuu wa Serikali, dosari iliyobainika na ukaguzi ni kukosekana kwa daftari la kumbu kumbu linaloonesha kima halisi cha fedha kilichopokelewa kutoka katika ngazi za Wilaya na fedha halisi za mapato iliyowasilishwa Mfuko Mkuu wa Serikali jambo ambalo limepelekea ugumu wa kuweza kufanya tathmini ya fedha ziliyokusanywa na fedha halisi zilizopokelewa pamoja na fedha halisi zilizowasilishwa Mfuko Mkuu wa Serikali. Dosari hizo zilibainika katika Taasisi zifuatazo:-

**Jadweli Nambari 10 : Taasisi ambazo hazikuweka kumbu kumbu za mapato yaliopelekwa Mfuko Mkuu wa Serikali**

| Namba | Jina la Taasisi |
|---|---|
| 1. | Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi |
| 2. | Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Unguja |
| 3. | Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja |

#### 5.1.1.5 Kutotayarishwa kwa Taarifa za Usuluhisho wa Benki (Bank Reconciliation)

Kwa mujibu wa kifungu nambari 162(1) cha Kanuni za Fedha za mwaka 2005 kinaeleza kuwa "Bakaa ya kila hesabu ya benki kama inavyoonesha katika taarifa ya benki lazima ionekane usuluhisho wa pamoja na bakaa ya daftari la fedha taslim ukosefu kwa kila mwezi, taarifa ya usuluhisho hiyo itawekwa kwenye kumbukumbu au itarikodiwa katika daftari la fedha taslim.

Ukaguzi umekagua stakabadhi zinazotumika kwa ajili ya ukusanyaji wa mapato kwa taasisi mbali mbali ambayo yanatokana na vyanzo mbali mbali vya mapato, dosari iliyobainika katika ukaguzi ni kutokufanyika kwa usuluhisho wa kibenki kwa lengo la kujua mapato halisi yaliyokusanywa na kurikoidiwa katika kumbu kumbu ya daftari la mapato pamoja na mapato yaliyowasilishwa benki ili kuweza kujua na kuishauri taasisi juu ya fedha halisi zilizowasilishwa benki pamoja na zile zilizokuwa hazikuwasilishwa benki lakini zimerikodiwa katika daftari la mapato. Taasisi zilizobainika na dosari hizo ni kama zifuatazo:-

**Jadweli Nambari 11 : Taasisi ambazo hazikufanya usuluhisho wa kibenki**

| Namba | Jina la Taasisi |
|---|---|
| 1. | Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Unguja |
| 2. | Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja |
| 3. | Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana – Pemba |
| 4. | Wizara ya Maji Nishati na Madini – Pemba |
| 5. | Bodi ya Usajili wa Wakandarasi |
| 6. | Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali Zanzibar (BPRA) |
| 7. | Mamlaka ya Mazingira (ZEMA) |

Kutotayarishwa kwa taarifa za Usuluhisho wa Benki za kila mwezi zinazoonyesha hali halisi ya ukusanyaji wa mapato ya Taasisi za Umma kunaweza kukapelekea kutopatikana kwa taarifa sahihi za ukusanyaji wa mapato yanayotokana na vyanzo mbali mbali vya mapato vilivyopo.

### 5.1.1.6 Kuwepo kwa Usimamizi Usioridhisha wa Mapato

Kwa mujibu wa kifungu nambari 79(1) cha Kanuni za Fedha za mwaka 2005 kinamtaka Afisa Masuuli kuhakikisha kwamba kunakuwepo kwa akaunti iliyoanzishwa kwa ajili ya mapato na pia akaunti hiyo inatakiwa kuwa sahihi muda wote.

Aidha, kifungu nambari 79 (2) cha Kanuni za Fedha za mwaka 2005 kinamtaka Afisa Masuuli kumteua afisa ataeshughulika na kukagua na kuangalia usahihi wa kumbukumbu za kila siku zinazorikodiwa katika daftari la fedha, madaftari mengine ya hesabu, "counterfoils" na nakala za risiti na risiti halisi.

Aidha kifungu nambari 30(1) cha Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha ya mwaka 2016 kinaeleza kwamba afisa mhasibu atakuwa na jukumu la usimamizi wa mapato ya taasisi za umma pamoja na kifungu namba 30(2) cha Sheria ya Fedha Nambari 12 ya mwaka 2016 kinamtaka Afisa Masuuli kuchukua hatua zinazofaa kuhakikisha uanzishaji na uendeshaji wa mfumo bora na wa ufanisi wa ukusanyaji na uhifadhi wa mapato.

Ukaguzi ulikagua kumbukumbu zinazohusiana na mapato katika Ofisi mbali mbali za  na kubaini uwepo wa ukiukwaji wa kanuni na taratibu zilizoainishwa hapo juu za kutokuwepo kwa usahihi wa akaunti, usimamizi usioridhisha wa mapato na vile vile kutokuwepo kwa mfumo bora wa ukusanyaji wa mapato. Dosari hizo zilibainika katika taasisi zifuatazo:-

**Jadweli Nambari 12 : Taasisi ambazo hazina  usimamizi unaoridhisha wa  Mapato**

| Namba | Jina la Taasisi |
|---|---|
| 1. | Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja |
| 2. | Wakala wa Miundombinu ya TEHAMA Zanzibar |

Ukaguzi unawashauri wakuu wa Taasisi za Umma kuhakikisha kwamba wanasimamia na kufuatilia kwa karibu mtiririko mzima wa ukusanyaji wa mapato ili kupata fursa ya kurekebisha mapungufu yanayotokana na mapato hayo na pia kuweza kudhibiti upotevu wa mapato kwa lengo la kuongeza mapato Serikalini.

### 5.1.1.7 Kutokuwepo kwa makadirio ya mapato na matumizi

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwa taasisi mbali mbali za umma zinakusanya mapato kupitia vyanzo mbali mbali walivyonavyo, dosari iliyobainika katika ukaguzi ni kutokuandaa makadirio halisi ya kila chanzo cha makusanyo ya mapato hayo jambo ambalo linapelekea kushindwa kutathmini asilimia iliyofikiwa kwa kila chanzo cha mapato kilichokusanywa.

Aidha ukaguzi umebaini baadhi ya Taasisi za Umma hufanya matumizi mbali mbali ya shughuli za uendeshaji bila ya kuwepo kwa makadirio ya matumizi hayo pamoja na matumizi halisi yanayopaswa kupatikana kutokana na makadirio hayo jambo ambalo hupelekea kujitokeza kwa ugumu wa shughuli za uendeshaji wa taasisi hizo na kupelekea mara kwa mara kuomba matumizi katika makao makuu ya taasisi zao.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016. Dosari hizo zimebainika katika taasisi zifuatazo:-

**Jadweli Nambari 13 : Taasisi zilizokuwa hazina makadirio ya mapato na matumizi**

| Namba | Jina la Taasisi |
|---|---|
| 1. | Jeshi la Kujenga Uchumi – Pemba |
| 2. | Chuo cha Mafunzo – Pemba |
| 3. | Kikosi Maalum cha Kuzuwia Magendo – Pemba |
| 4. | Kikosi cha Valantia – Pemba |
| 5. | Kikosi cha Zimamoto na Uokozi – Pemba |
| 6. | Ofisi ya Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta – Pemba |
| 7. | Wakala wa Chakula, Dawa na Vipodozi – Pemba |

### 5.1.1.8 Kutokuwepo kwa Daftari la makadirio ya Vifungu vya Matumizi (Vote Book)

Ukaguzi umebaini kwamba baadhi ya Taasisi mbali mbali za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar hufanya matumizi mbali mbali bila kuwepo kwa daftari la makadirio ya vifungu vya matumizi (vote book).

Kutokuwepo kwa daftari la vifungu vya matumizi kunapelekea kushindwa kufanya tathmini ya uingizwaji wa fedha za matumizi kwa kila kifungu pamoja na matumizi ya kifungu hicho jambo ambalo ni kwenda kinyume na toleo lenye kumbu kumbu namba AD.5/184/01/07/80 la tarehe 9/6/2021 linalowataka wahasibu kufunga hesabu zao kwa mujibu wa daftari la makadirio ya vifungu vya matumizi. Dosari hii imebainika kwa taasisi mbali mbali kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 14: Taasisi zilizokuwa hazikufuata muongozo wa ufungaji wa hesabu**

| Namba | Jina la Taasisi |
|---|---|
| 1. | Ofisi ya Rais Katiba Sheria Utumishi na Utawala Bora – Pemba |
| 2. | Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalumu za SMZ – Pemba |
| 3. | Ofisi ya Rais Kazi, Uchumi na Uwekezaji – Pemba |
| 4. | Ofisi ya Rais Fedha na Mipango – Pemba |
| 5. | Tume ya Mipango – Pemba |
| 6. | Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais Sera Uratibu na Baraza la Wawakilishi – Pemba |
| 7. | Tume ya Uchaguzi – Pemba |
| 8. | Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale – Pemba |
| 9. | Kamisheni ya Utalii – Pemba |
| 10. | Wizara ya Ujenzi Mawasiliano na Uchukuzi – Pemba |
| 11. | Wizara ya Maji Nishati na Madini – Pemba |
| 12. | Wizara ya Habari Vijana Utamaduni na Michezo – Pemba |
| 13. | Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi – Pemba |
| 14. | Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda – Pemba |
| 15. | Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali – Pemba |
| 16. | Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma Pemba |
| 17. | Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais Makamo wa Kwanza wa Rais |
| 18. | Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa, Idara Maalum SMZ |
| 19. | Wizara ya Maji, Nishati na Madini |
| 20. | Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi |
| 21. | Kamisheni ya Ardhi |
| 22. | Bodi ya Kondominio |
| 23. | Bodi ya Uhaulishaji wa ardhi |
| 24. | Bodi ya Usajili wa Wakandarasi |
| 25. | Bodi ya Kudhibiti Kodi za Nyumba |
| 26. | Bodi ya Usajili Wasanifu, Wahandisi na Wakadiriaji Majengo |
| 27. | Hospitali ya Mnazi Mmoja |

| Namba | Jina la Taasisi |
|---|---|
| 28. | Ofisi ya Rais Kazi, uchumi , na Uwezeshaji |
| 29. | Wakala wa Ulinzi JKU |
| 30. | Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii |
| 31. | Kamisheni ya Utumishi wa Umma |
| 32. | Tume ya Maadili |
| 33. | Mamlaka ya Mazingira (ZEMA) |
| 34. | Tume ya Uchaguzi Zanzibar |
| 35. | Baraza la Wawakilishi |
| 36. | Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Zanzibar (ZARI) |
| 37. | Taasisi ya Viwango Zanzibar (ZBS) |
| 38. | Tume ya Ushindani Halali wa Biashara |
| 39. | Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo |
| 40. | Idara ya Misitu |

Ukaguzi unashauri Maafisa Masuuli kuhakikisha wanasimamia watendaji wao kikamilifu kutekeleza maagizo ya muongozo huo kwa lengo la kuhakikisha wanafuata taratibu na misingi ya ufungaji wa hesabu kwa mujibu wa viwango vilivyowekwa kitaifa na kimataifa ili kuepusha ukiukwaji wa Sheria ya Usimamizi wa fedha za Umma.

#### 5.1.1.9 Kukosekana kwa buku linaloonyesha mienendo ya safari katika vyombo vya moto (log book)

Kifungu nambari 124(2) cha kanuni ya Utumishi wa Umma ya Mwaka 2014 kinaeleza "Katibu Mkuu au Mkuu wa Taasisi atahakikisha vyombo vyote vinavyotumika katika Taasisi yake vinakuwa na buku linaloonyesha matumizi ya chombo kwa safari husika".

Ukaguzi umebaini kuwa vyombo vya moto vya Wizara na taasisi mbali mbali za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar havijawekewa buku linaloonyesha mienendo ya safari ya vyombo hivyo hali inayopelekea kushindwa kujiridhisha juu ya matumizi ya mafuta yanayonunuliwa na kutumika jambo ambalo linapelekea kujitokeza kwa ugumu wa kujua muda sahihi wa kuweza kufanyiwa matengenezo ya chombo husika.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu namba 124(2) cha kanuni ya Utumishi wa umma ya mwaka 2014. Dosari zilizobainika kwa Wizara na Taasisi za Umma ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 15: Taasisi zilizokosa buku linaloonyesha mienendo ya safari katika vyombo vya moto (log book)**

| Namba | Jina la Taasisi |
|---|---|
| 1. | Ofisi ya Rais Katiba Sheria Utumishi na Utawala Bora – Pemba |
| 2. | Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais Sera Uratibu na Baraza la Wawakilishi – Pemba |
| 3. | Tume ya Uchaguzi – Pemba |
| 4. | Wakala wa Chakula, Dawa na Vipodozi Zanzibar |
| 5. | Wakala wa Ulinzi JKU |
| 6. | Tume ya Mipango |
| 7. | Kamisheni ya Kukabiliana na Maafa |
| 8. | Mahkama Kuu - Pemba |

Ukaguzi unashauri viongozi wa Wizara na Taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuhakikisha wanaanzisha daftari maalum la kurikodia mwenendo wa gari ili kuepusha hasara inayoweza kujitokeza kutokana na kuchelewa kufanyiwa matengenezo ya gari kwa kukosekana kwa taarifa ya mwenendo wa matumizi ya gari.

### 5.1.1.10 Kukosekana kwa Mpango wa Manunuzi wa mwaka

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba baadhi ya Wizara na Taasisi za Umma hufanya matumizi mbali mbali kwa ajili ya huduma za uendeshaji wa taasisi zao dosari iliyobainika na ukaguzi ni kutokuwepo kwa mpango wa manunuzi wa mwaka ambao huonyesha tathmini au muelekeo wa vipaombele vya bajeti ya manunuzi kwa mwaka husika.

Aidha imebainika taasisi zifuatazo hazijaandaa mpango wa manunuzi jambo ambalo linaleta ugumu wa kuthibitisha uhalali wa manunuzi yanayofanyika kwa mujibu wa bajeti husika. Dosari hizo zimebainika katika taasisi zifuatazo kwa mujibu wa mchanganuo ufuatao:-

**Jadweli Nambari 16: Taasisi zilizokosa mpango wa manunuzi**

| Namba | Jina la Taasisi |
|---|---|
| 1. | Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana – Pemba. |
| 2. | Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali (BPRA) |

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 29(e) cha Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016.

Ukaguzi unashauri viongozi wa Wizara na Taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuhakikisha wanaandaa na kuutumia mpango wa manunuzi na kuacha kutegemea mpango wa manunuzi uliopo Ofisi Kuu jambo ambalo linapelekea kutokuonesha muelekeo wa matumizi kwa mujibu wa bajeti za manunuzi zilizofanywa.

#### 5.1.1.11 Kushindwa kufikia malengo ya ukusanyaji wa mapato

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika Wizara na Taasisi mbali mbali za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar zimeshindwa kufikia malengo ya makadirio ya makusanyo ya mapato kutoka katika vyanzo vyake mbali mbali vya mapato kwa mwaka wa fedha 2020/2021 jambo ambalo limepelekea kushindwa kufikia malengo yaliyojipangia. Aidha kushindwa kufikia malengo ya ukusanyaji wa mapato kunapelekea Serikali kushindwa kukamilisha malengo yaliyojipangia ikiwemo kuondosha hali duni za vipato kwa wananchi wake. Baadhi ya Taasisi na Wizara ambazo zimeshindwa kufikia malengo yao ni kama zinavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 17 : Baadhi ya taasisi zilizoshindwa kufikia malengo ya ukusanyaji wa mapato**

| Namba | Jina la Taasisi | Makadirio ya mapato (Tshs.) | Makusanyo halisi (Tshs.) | Asilimia ya makusanyo (%) |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango – Pemba | 120,798,000 | 37,697,500 | 31.21 |

Ukaguzi unashauri viongozi wa Wizara na Taasisi mbali mbali kuhakikisha wanachukuwa jitihada za makusudi za ukusanyaji wa mapato pamoja na kuibua vyanzo vipya vya mapato kwa lengo la kujiletea maendeleo endelevu katika Serikali yao.

#### 5.1.1.12 Kukosekana kwa udhibiti na utunzwaji wa mali za kudumu

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba utunzaji na udhibiti wa majengo pamoja na mali nyenginezo za kudumu za Serikali na taasisi mbali mbali haziridhishi kutokana na kutokuwa katika hali nzuri na kupelekea kupungua kwa tija na mapato yanayotarajiwa kupatikana pahala hapo.

Ukaguzi unashauri wakuu wa taasisi za Serikali waliobainika kuguswa na dosari hii kufanya utaratibu wa haraka wa kuyakarabati majengo, maeneo ya biashara, milango ya biashara, mabekari, vyombo vya moto pamoja na sehemu mbali mbali ambazo hutumika kama vianzio vya mapato kwa lengo la kuepuka kuendelea kuharibika na kuchakaa na hatimae kupelekea kutumia gharama kubwa zaidi katika matengenezo na kukosekana kwa tija na mapato yatokanayo na uzalishaji unaofanyika kupitia vyanzo hivyo vya mapato. Baadhi ya Wizara na taasisi zilizobainika kuwepo kwa dosari hiyo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 18: Taasisi zilizokosa udhibiti na utunzwaji wa mali za kudumu**

| Namba | Jina la Taasisi |
|---|---|
| 1. | Ofisi ya Rais Fedha na Mipango – Pemba. |
| 2. | Tume ya Uchaguzi – Pemba. |
| 3. | Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale – Pemba |
| 4. | Wizara ya Ujenzi Mawasiliano na Uchukuzi – Pemba |
| 5. | Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali – Pemba |
| 6. | Wakala wa Majengo – Pemba |
| 7. | Hospitali ya Mnazi Mmoja |

#### 5.1.1.13 Kukosekana Daftari la Kuhifadhia Mali za Kudumu (Fixed Assets Register)

Kwa mujibu wa kifungu nambari 29(1)(a) cha Sheria ya Usimamizi wa fedha za Umma ya mwaka 2016 kinaeleza kwamba "Afisa Mhasibu wa Taasisi za Umma atahusika na kusimamia mali za Taasisi ya Umma"

Katika ukaguzi uliofanyika katika kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021 imebainika kwamba baadhi ya Wizara na Taasisi mbali mbali za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar hazina daftari la kuhifadhia mali za kudumu jambo ambalo linaweza kupelekea kutokujua umiliki wake na hatimae kupelekea kupotea kwa mali hizo.

Kukosekana daftari la kuhifadhia mali za kudumu ni kwenda kinyume na Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma nambari 29(1)(a) ya mwaka 2016.

Kukosekana daftari la kuhifadhia mali za kudumu kunaweza kupelekea mali zilizonunuliwa,zilizochakaa,zilizouzwa pamoja na zilizohamishwa kutokutambuliwa na kusababisha upotevu wa mali hizo.

Ukaguzi unashauri viongozi wa Wizara na Taasisi mbali mbali za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuhakikisha kwamba daftari la mali za kudumu linaanzishwa kwa haraka ili kuweza kuzirikodi mali zote za kudumu za Wizara na taasisi hizo pamoja na thamani zake kwa mujibu wa sheria na kanuni husika ili kuweza kuzuia upotevu wa mali za Serikali.

**Jadweli Nambari 19: Taasisi zilizokosa daftari la kumbukumbu za mali za kudumu (Fixed Asset Register)**

| Namba | Jina la Taasisi |
|---|---|
| 1. | Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji |
| 2. | Kamisheni ya Utumishi wa Umma |
| 3. | Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali (BPRA) |
| 4. | Chuo cha Mafunzo ya Umeme wa Jua Kibokwa. |
| 5. | Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais Makamo wa Kwanza wa Rais |
| 6. | Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii |
| 7. | Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee Jinsia na Watoto |
| 8. | Ofisi ya Baraza la Mapinduzi |
| 9. | Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo |

#### 5.1.1.14 Kutokuwepo kwa Masjala ya Siri na Bayana

Kwa mujibu wa kifungu nambari 52(1) cha Kanuni ya Utumishi wa mwaka mwaka 2014 bila ya kuathiri kifungu cha 95 cha Sheria ya Utumishi wa Umma na kifungu cha 13 cha Sheria ya Kuanzishwa Uhifadhi wa Kumbukumbu na Nyaraka Zanzibar, Namba 3 ya 2008, kila Taasisi ya umma itakuwa na masjala ya siri na bayana ambazo zitahifadhi kumbukumbu zote za Taasisi husika.

Ukaguzi umebaini kwamba baadhi ya Wizara na Taasisi za Umma hazina masjala ya siri na bayana, ambapo kazi za kitengo hicho zinafanywa na Afisa Utumishi. Hali hii inaweza kupelekea upotevu wa majalada pamoja na uvujaji wa taarifa za siri za Kamisheni.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 52(1) cha kanuni ya Utumishi wa Umma ya mwaka 2014.

Ukaguzi unashauri viongozi wa Wizara na Taasisi za Umma kuhakikisha zinakuwa na Masjala ya siri na bayana kwa lengo la kuhifadhi taarifa muhimu za wafanyakazi pamoja na za Serikali ili kuepusha upotevu wa siri za Serikali pamoja na watumishi wa umma jambo ambalo litapelekea kujitokeza kwa upotevu wa haki za mtumishi kwa kukosekana taarifa za mtumishi huyo kwa kukosekana kwa taarifa katika majalada yake wakati wa ukokotoaji wa mafao ya uzeeni wakati wa kustaafu. Mchanganuo wa taasisi zenye dosari hizo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 20: Taasisi zilizokuwa hazina Masjala ya Siri na Bayana**

| Namba | Jina la Taasisi |
|---|---|
| 1. | Kamisheni ya Utalii Pemba |
| 2. | Wakala wa Ulinzi JKU |

### 5.1.1.15 Kutofuatwa Kwa Mgawanyo wa Majukumu ya Kazi

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika baadhi ya Wizara na Taasisi za Umma hutekeleza majukumu yake ya kazi mbali mbali kwa mujibu wa miongozo waliyojiekea, dosari ya ukaguzi iliyobainika ni kutokuwa na mgawanyo wa majukumu ya kazi kwa mujibu wa taaluma ya mtumishi, fani aliyosomea na kada aliyoajiriwa jambo ambalo linalotumika ni mtumishi kufanya kazi yoyote anayopangiwa pasi na kuzingatia taaluma na uzoefu wa utekelezaji wa kazi hiyo jambo ambalo linapelekea kutokuwa na ufanisi wa utekelezaji wa majukumu kwa mujibu wa miundo ya utumishi na upangaji wa madaraja ya watumishi wa umma Serikalini.

Kutokuwa na mgawanyo wa majukumu ya kazi kunasababisha taasisi kushindwa kufikia malengo waliyojipangia, kushindwa kufikia ubora wa kazi wanazozifanya na hatimae kutokuleta tija ya uwepo wa taasisi husika. Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na miongozo ya Utumishi wa Umma ya Serikalini.

Ukaguzi unashauri viongozi wa Wizara na Taasisi za Umma kuhakikisha unachukuwa jitihada za makusudi kuomba wafanyakazi wenye taaluma ambao watamsaidia kutekeleza majukumu ya taasisi kwa mujibu wa malengo ya taasisi hiyo. Mchanganuo wa taasisi zenye dosari hizo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 21: Taasisi ambazo hazina Mgawanyo wa Majukumu ya Kazi**

| Namba | Jina la Taasisi |
|---|---|
| 1. | Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali (BPRA) |
| 2. | Wakala wa Ulinzi JKU |

### 5.1.1.16 Kukosekana kwa Mpango mkakati wa muda mrefu (Strategic Plan)

Mpango mkakati (Strategic Planning) ni mfumo wa kimaandishi unaoonesha kazi zinazotakiwa kufanywa na hatua mbalimbali ili kufikia malengo yaliyowekwa kwa muda maalum.

Ukaguzi umebaini kuwa baadhi ya Wizara na Taasisi za Umma hazina mpango mkakati kwa ajili ya kuratibu kazi zote ili kufikia malengo waliyojipangia, aidha baadhi ya taasisi za umma hazifanya marekebisho ya mpango mkakati wao kwa kipindi cha muda mrefu. Kutokuepo kwa mpango mkakati wa muda mrefu ni kwenda kinyume na kifungu nambari 32(3) cha Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016.

Kufanya kazi bila ya kufuata mpango mkakati kunaisababishia Wizara na Taasisi za Umma kufanya kazi kwa mazoea na kukosekana kwa tathmini ya kazi zinazofanywa na taasisi hizo.

Ukaguzi unashauri viongozi wa Wizara na Taasisi za Umma kutengeneza na kutumia mpango mkakati kwa ajili ya ufanisi mzuri wa utekelezaji wa malengo yake.

Mchanganuo wa taasisi zenye dosari hizo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 22: Taasisi ambazo hazina mpango mkakati wa muda mfefu**

| Namba | Jina la Taasisi |
|---|---|
| 1. | Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali (BPRA) |
| 2. | Kikosi cha Valantia (KVZ) |
| 3. | Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu |

## SURA YA SITA

### 6.0 MATOKEO YA UKAGUZI KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021

Katika ukaguzi wa hesabu za mwaka wa fedha 2020/2021 imebainika kwamba mfumo wa uwekaji wa kumbukumbu na taarifa mbali mbali za hesabu ikiwemo fedha na rasilimali za umma pamoja na mfumo wa udhibiti wa ndani umekuwa ukiimarika ingawa kumejitokeza dosari za kiutendaji mbali mbali.

Katika ukaguzi huo kulijitokeza dosari za kiutendaji kwa baadhi ya Wizara na Taasisi za Serikali ambapo baadhi ya dosari ziliweza kurekebishwa na kupatiwa ufafanuzi wakati wa ukaguzi, aidha kuna baadhi ya hoja za ukaguzi ambazo hazikuweza kupatiwa ufafanuzi hadi ukaguzi unakamilika. Matokeo ya ukaguzi huo ni kama ifuatavyo:-

### 6.1 WIZARA YA NCHI OFISI YA RAIS NA MWENYEKITI WA BARAZA LA MAPINDUZI

#### 6.1.1 FUNGU A 01 - OFISI YA RAIS NA MWENYEKITI WA BARAZA LA MAPINDUZI

Ukaguzi wa hesabu za Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa mwaka wa fedha 2020/2021 umefanywa kwa kuzingatia Sheria,kanuni,taratibu na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Taarifa ya Matumizi**

Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ilikadiriwa kutumia jumla ya shilingi 8,063,500,000 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na jumla ya shilingi 1,500,000,000 kwa ajili ya kutekeleza kazi za maendeleo.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 Jumla ya shillingi 3,215,550,698 ziliingizwa na kutumika kwa kazi za kawaida sawa na asilimia 40, na jumla ya shilingi 1,500,000,000 ziliingizwa na kutumika kwa kazi za maendeleo sawa na asilimia 100.

#### 6.1.2 FUNGU A 02 – OFISI YA BARAZA LA MAPINDUZI – BLM

Ukaguzi wa hesabu za Ofisi ya Baraza la Mapinduzi kwa mwaka wa fedha 2020/2021 umefanywa kwa mujibu wa Sheria, kanuni, taratibu pamoja na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Taarifa ya Matumizi**

Ofisi ya Baraza la Mapinduzi kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ilikadiriwa kutumia jumla ya shilingi 2,237,600,000 kwa kazi za kawaida. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 jumla ya shillingi 1,794,791,800 zimeingizwa na kutumika kwa kazi za kawaida sawa na asilimia 80.21 ya makadirio.

#### 6.1.3 FUNGU B 01 – OFISI YA MAKAMO WA KWANZA WA RAIS

Ukaguzi wa hesabu za Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais Rais kwa mwaka wa fedha 2020/2021 umefanywa kwa mujibu wa Sheria, kanuni, taratibu pamoja na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Taarifa ya Mapato**

Wizara ya Nchi Ofisi ya Makamo wa kwanza wa Rais kwa mwaka wa fedha 2020/2021 imekadiriwa kukusanya jumla ya shilingi 3,929,405,513. Hadi kufikia tarehe 30, Juni 2021 Ofisi imekusanya jumla ya shilingi 1,620,471,980 sawa na asilimia 74.7 ya makadirio.

**Taarifa ya Matumizi**

Wizara ya Nchi Ofisi ya Makamo wa kwanza wa Rais kwa mwaka wa fedha 2020/2021 lilikadiriwa kutumia jumla ya shilingi 2,170,032,513 kwa ajili ya kazi za kawaida na shilingi 787,320,000 kwa ajili ya kazi za maendeleo. Hadi kufikia tarehe 30, Juni 2021 jumla ya shilingi 1,276,701,391 ziliingizwa na kutumika kwa kazi za kawaida sawa na asilimia 58.8 ya makadirio na shilingi 261,079,089 zimeingizwa na kutumika kwa kazi za maendeleo sawa na asilimia 33.2 ya makadirio.

### 6.1.4 WAKALA WA SERIKALI WA UCHAPAJI (ZAGPA) – PEMBA

### MATOKEO NA MAPENDEKEZO YA UKAGUZI

#### 6.1.4.1 Kukosekana kwa marejesho ya masurufu ya shilingi 2,000,000

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Ofisi za Wakala wa Serikali wa Uchapaji Pemba imetumia jumla ya shilingi 2,000,000 kwa ajili ya matumizi madogo madogo lakini marejesho ya matumizi hayo yamekosekana kwa ukaguzi ili kuweza kujiridhisha juu ya uhalali wa matumizi husika.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu cha 29(1) cha Sheria ya uanzishwaji wa Wakala wa Serikali wa Uchapaji Zanzibar nambari 12 ya mwaka 2018.

#### 6.1.4.2 Upokeaji wa fedha za ofisi kwa njia ya simu ya mtu binafsi shilingi 2,000,000.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Ofisi ya Wakala wa Serikali wa Uchapaji Pemba imepokea jumla ya shilingi 2,000,000 kutoka ofisi kuu Unguja kwa njia ya simu ya mtu binafsi badala ya kuingizwa katika hesabu ya taasisi husika hali ambayo inaweza kupelekea upotevu wa fedha hizo na kushindwa kupata ushahidi juu ya upokeaji na utumiaji wa fedha hizo.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wakala wa Serikali wa Uchapaji- Pemba kufanya kuhakikisha kwamba hesabu ya taasisi inafunguliwa na kuhakikisha fedha zote zinazotumwa kutoka Wizara ya Fedha au Ofisi kuu ya Wakala wa Serikali wa Uchapaji kuzingatia kanuni,sheria pamoja na miongozo mbali mbali iliyopo ili kuepusha athari inayoweza kujitokeza.

#### 6.1.4.3 Kukosekana kwa vifaa vya kiusalama katika ghala la kuhifadhia bidhaa.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Wakala wa Serikali wa Uchapaji Pemba haina vifaa vya kiusalama katika ghala la kuhifadhia bidhaa liliopo Gombani Chake Chake Pemba hali inayopelekea uwezekano wa upotevu wa mali pamoja na bidhaa zinazohifadhiwa katika ghala hilo na kusababisha hasara pindipo kutatokea majanga,uharibifu au wizi wa bidhaa zilizohifadhiwa.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu Nambari 61(5) cha Sheria Nambari 2 ya Utumishi wa Umma ya mwaka 2011.

#### 6.1.4.4 Kukosekana kwa mapato yatokanayo na mauzo ya bidhaa shilingi 77,667,000

Katika ukaguzi uliofanyia imebainika kwamba Ofisi za Wakala wa Serikali wa Uchapaji Pemba imepokea bidhaa zenye thamani ya shilingi 78,000,000 kutoka Ofisi kuu Unguja kwa ajili kufanya mauzo ya bidhaa za utoaji wa huduma za uuzaji wa machapisho, vifaa vya maofisini pamoja na vifaa vya kuandikia lakini hadi kufikia tarehe 30 Juni 2021 imebainika kwamba mauzo halisi ya bidhaa hizo ni shilingi 333,000 kukiwa na upungufu wa shilingi 77,667,000 ambazo ni sawa na asilimia 99.96 ya gharama za bidhaa zote.

Hali hii inaweza kupelekea uwezekano wa kuharibika kwa bidhaa kutokana na kupitwa na muda kwa baadhi ya bidhaa na hivyo kupelekea kupungua kwa bei halisi ya uuzwaji wa bidhaa pamoja na uwezekano wa upatikanaji wa hasara itokanayo na bidhaa hizo, ambapo ni kwenda kinyume na Sheria Nambari 12 ya uanzishaji wa Wakala wa Serikali wa Uchapaji ya mwaka 2018.

## 6.2 WIZARA YA NCHI OFISI YA MAKAMO WA PILI WA RAIS, SERA, URATIBU NA BARAZA LA WAWAKILISHI

### 6.2.1 FUNGU C 01 - OFISI YA MAKAMO WA PILI WA RAIS, SERA URATIBU NA BARAZA LA WAWAKILISHI

Ukaguzi wa hesabu za Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais, Sera Uratibu na Baraza la Wawakilishi kwa mwaka wa fedha 2020/2021 umefanywa kwa mujibu wa Sheria, kanuni, taratibu pamoja na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Taarifa ya Mapato**

Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu Baraza la Wawakilishi kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ilikadiriwa kukusanya jumla ya shilingi 45,263,608,741. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu Baraza la Wawakilishi iliweza kukusanya jumla ya shilingi 13,689,862,866 sawa na asilimia 30 ya makadirio.

**Taarifa ya Matumizi**

Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu Baraza la Wawakilishi kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ilikadiriwa kutumia jumla ya shilingi 8,034,800,306 kwa ajili ya kazi za kawaida na shilingi 50,000,000 kwa ajili ya kazi za maendeleo.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 jumla ya shilingi 6,580,382,083 ziliingizwa na kutumika kwa kazi za kawaida ambapo ni sawa na asilimia 82 ya makadirio na shilingi 50,000,000 ziliingizwa na kutumika kwa kazi za maendeleo sawa na asilimia 100 ya makadirio.

**MATOKEO NA MAPENDEKEZO YA UKAGUZI**

**MAMLAKA YA MAZINGIRA (ZEMA)**

#### 6.2.2.1 Kutokuwepo kwa uthibitisho wa utoaji wa fedha za mapato shilingi 40,098,000

Ukaguzi umebaini kuwa jumla ya shilingi 40,098,000 ni fedha ambazo zimetolewa katika daftari la ujumla la Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais , dosari iliyobainika na ukaguzi ni kukosekana kwa uthibitisho wa barua iliyoidhinisha utolewaji wa fedha hizo kwa ajili ya ukaguzi hivyo kupelekea kushindwa kujuwa uhalisia unaotokana na utolewaji wa fedha hizo ambapo ni kwenda kinyume na Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais kupitia Mamlaka ya Mazingira kuhakikisha unasimamia kikamilifu Taasisi zake ili kuhakikisha kwamba sheria, kanuni pamoja na miongozo mbali mbali ya fedha inafuatwa kikamilifu ikiwa ni pamoja na kuongeza umakini katika upatikanaji wa idhini ili kuepusha uwezekano wa kuweza kujitokeza kwa viashiria vya ubadhirifu katika matumizi ya fedha za Umma.

### 6.2.2.2 Kukosekana kwa Tozo la adhabu kwa wawekezaji wanaopatiwa huduma za kimazingira

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwa jumla wawekezaji 59 wameshindwa kukatwa tozo ya adhabu na Mamlaka ya Mazingira - ZEMA kutokana na kumaliza kwa muda wa matumizi ya vibali vya ukaguzi wa mazingira ambao ni miaka mitano ya matumizi. Kufanya hivyo kunapelekea kuikosesha Serikali mapato yatokanayo na tozo hizo ambapo ni kwenda kinyume na Sheria ya usimamamizi wa mazingira ya Zanzibar. **Kiambatisho Nambari 1 Kinahusika.**

Ukaguzi unashauri uongozi wa Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais kuhakikisha unasimamia kikamilifu Taasisi zake ili kuhakikisha kwamba sheria, kanuni pamoja na miongozo mbali mbali ya fedha inafuatwa kikamilifu ikiwa ni pamoja na kuongeza umakini katika upatikanaji wa idhini ili kuepusha uwezekano wa kuweza kujitokeza kwa viashiria vya ubadhirifu katika matumizi ya fedha za Umma.

### 6.2.2.3 Kutokuwepo kwa uwiano wa taarifa baina ya hesabu za mwisho wa mwaka pamoja na uhalisia wa matumizi ya fedha shilingi 75,148,676

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwa jumla ya shilingi 75,148,676 zinatokana na tofauti iliyobainika kupitia katika taarifa za hesabu za mwisho wa mwaka pamoja na mlinganisho wa taaarifa halisi ya matumizi ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa mafuta ya Petrol na Diesel ambapo katika hesabu za mwisho wa mwaka matumizi hayo yanaonekana ni shilingi 161,148,710 lakini katika uhalisia wa taarifa kupitia katika hati za malipo ni shilingi 86,000,034 na kupelekea tofauti iliyobainishwa hapo juu. Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais kuhakikisha unasimamia kikamilifu Taasisi zake ili kuhakikisha kwamba sheria, kanuni pamoja na miongozo mbali mbali ya fedha inafuatwa kikamilifu ikiwa ni pamoja na kuongeza umakini katika utayarishaji wa taarifa za fedha ili kuepusha uwezekano wa kuweza kujitokeza kwa utofauti wa taarifa zinazowasilishwa katika mamlaka husika pamoja na taarifa zinazotumika katika taasisi.

### 6.2.2.4 Matumizi ambayo hayakuanishwa katika mpango manunuzi shilingi 127,500,000

Jumla ya shilingi 127,500,000 zimelipwa kupitia hati namba 13/2/2021 ya tarehe 22/2/2021 ambazo amelipwa Tononoka Fireworks ltd kwa ajili ya malipo yanayohusu upigaji wa fash fash kwa mwezi wa Januari 2021 , dosari iliyobainika na ukaguzi ni kuwa matumizi hayo hayakuainishwa katika mpango wa manunuzi wa mwaka wa Ofisi wa Makamo wa Pili wa Rais ili kuepusha kufanyika kwa mtumizi ambayo hayaendani na makadirio halisi na kupelekea kutokupatikana kwa uthibitisho wa matumizi katika kipindi cha mwaka husika. Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais kuhakikisha unasimamia kikamilifu Taasisi zake ili kuhakikisha kwamba Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma inafuatwa kikamilifu ikiwa ni pamoja na kuongeza umakini katika utayarishaji wa mpango wa manunuzi wa mwaka ili kuepusha uwezekano wa kutokuingizwa kwa baadhi ya taarifa zitokanazo na ununuzi wa huduma au bidhaa.

**OFISI YA MAKAMO WA PILI WA RAIS, SERA URATIBU NA BARAZA LA WAWAKILISHI – PEMBA**

### 6.2.2.5 Kukosekana kwa uthibitisho wa matumizi ya mafuta shilingi 20,562,717

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba jumla ya lita 63,016 za mafuta ya petrol na diesel zenye thamani ya shilingi 20,562,717 zimetumika kwa Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais Pemba kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli mbali mbali bila ya kuwepo kwa uthibitisho wa matumizi ya mafuta hayo, **Kiambatisho Nambari 2 Kinahusika.**

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016 ambapo inapelekea kushindwa kujua uhalali wa utoaji na utumiaji wa mafuta hayo.

### 6.2.2.6 Mafuta ambayo hayakurikodiwa katika daftari la ghalani shilingi 5,980,752

Ukaguzi umebaini jumla ya shilingi 5,980,752 zimetumika kwa ununuzi wa mafuta lakini mafuta hayo hayakurikodiwa katika daftari la ghalani ili kuweza kuthibitisha uhalali wa mapokezi pamoja na matumizi ya mafuta hayo, **Kiambatisho Nambari 3 Kinahusika.**

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016.

### 6.2.2.7 Kukosekana kwa uthibitisho wa matumizi ya mafuta shilingi 1,656,900

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba jumla ya lita 873 za mafuta zenye thamani ya shilingi 1,656,900 zimetumika kwa Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais Pemba katika idara Zema na idara Mazingira kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli mbali mbali bila ya kuwepo kwa uthibitisho wa mapokezi na matumizi ya mafuta hayo.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016 ambapo inapelekea kushindwa kujua uhalali wa utoaji na utumiaji wa mafuta hayo. Mchanganuo wa mafuta hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 23 : Kukosekana kwa uthibitisho katika matumizi ya mafuta kwa Idara za Ofisi**

| Tarehe Yaliyopelekwa | Kutoka Ofisi Kuu | Kwenda Idarani | Idadi ya Lita | Kiasi cha fedha kilicholipwa (Tshs) |
|---|---|---|---|---|
| 11/08/2020 | Makamo wa Pili wa Rais Pemba | ZEMA | 648 | 1,247,400 |
| 30/12/2020 | Makamo wa Pili wa Rais Pemba | Idara ya Mazingira | 225 | 409,500 |
| **Jumla** | | | **873** | **1,656,900** |

### 6.2.2.8 Malipo ambayo hayakukatwa kodi ya Zuio shilingi 8,275,000

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba jumla ya shilingi 8,275,000 zimelipwa kwa watoa huduma mbali mbali lakini malipo hayo hayakukatwa kodi ya zuio.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na sheria ya Mamlaka ya Mapato Tanzania (Income Tax Act No.13) ya mwaka 2008 kifungu nambari 83. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 24 : Malipo ambayo hayakukatwa kodi ya Zuio**

| Hati Namba | Hundi Namba | Aliyelipwa | Kiasi cha fedha kilicholipwa (Tshs) | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 21/6 18/6/2021 | 21821 | Salim Environmental Care | 1,850,000 | |
| 13/4 20/4/2021 | 20485 | | 1,800,000 | |
| 10/1 8/1/2021 18939 | | | 1,850,000 | Malipo ya fedha kwa ajili ya huduma ya usafi. |
| 12/10 13/10/2020 | 17670 | | 925,000 | |
| 32/8 24/8/2020 | 17413 | | 1,850,000 | |
| **Jumla** | | | **8,275,000** | |

### 6.2.2 FUNGU C 02 - BARAZA LA WAWAKILISHI

Ukaguzi wa hesabu za Baraza la Wawakilishi kwa mwaka wa fedha 2020/2021 umefanywa kwa mujibu wa Sheria, kanuni, taratibu pamoja na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Taarifa ya Matumizi**

Baraza la Wawakilishi kwa mwaka wa fedha 2020/2021 lilikadiriwa kutumia jumla ya shilingi 21,481,600,000 kwa ajili ya kazi za kawaida. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 jumla ya shilingi 15,228,386,858 ziliingizwa na kutumika kwa kazi za kawaida ambapo ni sawa na asilimia 71 ya makadirio.

**MATOKEO NA MAPENDEKEZO YA UKAGUZI**

### 6.2.2.1 Kutokatiwa Bima kwa vyombo vya moto vya Baraza la Wawakilishi

Ukaguzi umebaini kuwa Baraza la Wawakilishi linamiliki vyombo mbalimbali vya usafiri ikiwemo gari na vespa, dosari iliyobainika na ukaguzi ni kuwa baadhi ya vyombo havijakatiwa bima. Kutokukatiwa bima kwa vyombo vya moto kunaweza kukapelekea kudumaza shughuli za taasisi pale majanga yanapotokezea na kupelekea kutumia gharama kubwa ya matengenezo jambo ambalo linaweza likapelekea kupangua mipango ya utekelezaji wa shughuli nyengine walizojipangia.

Ukaguzi unashauri ni vyema taasisi za umma kuvikatia bima vyombo vyake ili kuepkua usumbufu utakao jitokeza pindipo majanga yanapotokezea. Mchanganuo wa vyombo ambavyo havijakatika bima ni kama inavyooekana katika jadweli la hapo chini:-

**Jadweli Nambari 25 : Vyombo vya moto ambavyo havijakatiwa Bima na Baraza la Wawakilishi**

| Namba | Namba ya Chombo | Aina ya Chombo | Chassis namba | Mwaka ilonunuliwa |
|---|---|---|---|---|
| **Magari ya Baraza la Wawakilishi ambayo hayajakatiwa Bima** | | | | |
| 1. | SMZ 258 A | LAND CRUISER PRADO | JTEBH9FJ40K063074 | 2012 |
| 2. | SMZ 788 A | TOYOTA HIACE | JTFJ502P20-0029791 | 2017 |
| 3. | SMZ 789 A | TOYOTA HIACE | JTFJS02P0-00030213 | 2017 |
| 4. | SMZ 909 A | LAND CRUISER PRADO | TRJ150-0011210 | 2019 |
| 5. | SMZ 324 A | TOYOTA HIACE | LH186-1000011 | 2012 |
| 6. | SMZ 358 A | TOYOTA SURF | RZN185- 9032729 | 2013 |
| 7. | SMZ 787 A | TOYOTA HIACE | JTFJS02P70-0029642 | 2017 |
| 8. | SMZ 664 A | LAND CRUISER | FTEBH3FJ001482060 | 2016 |
| 9. | SMZ 196 A | TOYOTA SURF | RZN185- 9023147 | 2011 |
| 10. | SMZ 663 A | TOYOTA PRADO | JTEBH -3FJ10K41871 | 2016 |
| 11. | SMZ 1033 A | LAND CRUISER PRADO | GDJ150 – 0002557 | 2020 |
| 12. | SMZ 225 B | TOYOTA HILUX | PN133JV2508547458 | 2013 |
| 13. | SMZ 844 A | LAND CRUISER PRADO | JTEBH3FJ00K192989 | 2018 |
| 14. | SMZ 132 A | HYUNDAI | | |
| **Vespa za Baraza la Wawakilishi ambazo hazijakatiwa Bima** | | | | |
| 15. | SMZ 414C | STAR | MD711EAEBC3143036 | 2012 |
| 16. | SMZ 441C | STAR | MD711EAEBC3143707 | 2012 |

### 6.2.2.2 Kukosekana kwa tija ya matumizi ya shilingi 17,359,000

Ukaguzi umebaini kwamba jumla ya shilingi 17,359,000 ni malipo yaliyolipwa kwa kampuni ya Kato Ltd kwa ajili ya ukarabati wa jengo la Baraza la Wawakilishi, dosari iliyobainika katika ukaguzi ni kukosekana kwa tija ya kazi ya ukarabati wa jengo iliyofanyika ukilinganisha na fedha halisi iliyotumika kwani ukaguzi umebaini pamoja na ukarabati uliofanyika jengo hilo bado linaendelea kuvuja. Aidha, ukaguzi umepata shaka juu ya utumiwaji wa kampuni binafsi kufanya ukarabati wa jengo la Serikali jambo ambalo kazi kama hiyo ingelifanywa na Wakala wa Majengo ya Serikali kwa gharama nafuu na kwa kuzingatia ubora wa kazi yenyewe.

Kuendelea kuwatumia wakandarasi binafsi kunaweza kupelekea kuikosesha Serikali mapato yatokanayo na tozo za kodi kwa kazi wanazozifanya pamoja na kukiuka maagizo ya Serikali kwa kuacha kuwatumia wakandarasi walioteuliwa na Serikali (Wakala wa Majengo ya Serikali) kwa ajili ya kukarabati na kusimamia kazi za Serikali kwa lengo la kupatikana ubora wa kazi na tija iliyokusudiwa.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Ofisi ya Baraza la Wawakilishi kuhakikisha kwamba matumizi yote yanayofanyika yanazingatia Sheria, kanuni, taratibu na miongozo iliyopo ili kunusuru uwepo wa matumizi yasiyo na tija ambayo yataisababishia hasara Serikali.

### 6.2.3 FUNGU C 03 - TUME YA UCHAGUZI ZANZIBAR

Ukaguzi wa hesabu za Tume ya Uchaguzi Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2020/2021 umefanywa kwa mujibu wa Sheria, kanuni, taratibu pamoja na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Taarifa ya Mapato**

Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ilikadiriwa kukusanya jumla ya shilingi 57,500,000. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar iliweza kukusanya jumla ya shilingi 167,772,000 sawa na asilimia 292 ya makadirio.

**Taarifa ya Matumizi**

Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ilikadiriwa kutumia jumla ya shilingi 7,093,181,245 kwa ajili ya kazi za kawaida. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 jumla ya shilingi 6,208,523,660 ziliingizwa na kutumika kwa kazi za kawaida sawa na asilimia 87 ya makadirio.

**MATOKEO NA MAPENDEKEZO YA UKAGUZI**

#### 6.2.3.1 Kutokuingizwa kwa taarifa za mali za kudumu katika hesabu za mwisho wa mwaka

Kwa mwaka wa fedha 2020/2021 Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar iliandaa na kuwasilisha hesabu za mwisho wa mwaka katika Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Zanzibar, dosari iliyobainika na ukaguzi ni kutokuainishwa kwa baadhi ya mali za kudumu za Tume katika hesabu za mwisho wa mwaka (Financial Statements) zilizowasilishwa kwa ajili ya ukaguzi.

Kufanya Hivyo kunaweza kupelekea kutokupatikana kwa usahihi wa hesabu zilizowasilishwa kwa ajili ya ukaguzi ambapo ni kwenda kinyume na Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016. Orodha ya mali za kudumu ambazo hazikuainishwa katika hesabu ya mwisho wa mwaka ni kama zinavyoonekana hapo chini:-

- Kukosekana kwa taarifa za majengo matatu yaliopo Maisara.
- Kukosekana kwa taarifa za ghala kuu liliopo Kikwajuni.
- Kukosekana kwa taarifa za jengo liliopo Wilaya ya Magharibi A.
- Kukosekana kwa taarifa za jengo liliopo Wilaya ya Kati Unguja.
- Kukosekana kwa taarifa za jengo liliopo Wilaya ya Kusini.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar uhakikishe unafanya usahihi wa taarifa zinazotayarishwa na kuwasilishwa katika Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ikiwa ni pamoja na kujumuisha kikamilifu taarifa zote zinazohusu mali za kudumu katika kipindi cha mwaka husika.

#### 6.2.3.2 Kukosekana kwa hatimiliki za majengo

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwa Tume ya Uchaguzi Zanzibar inamiliki majengo mbali mbali, dosari iliyobainika na ukaguzi ni kukosekana kwa hati miliki za majengo hayo ili kuweza kuthibitisha uhalali wake ambapo kunaweza kupelekea upotevu wa majengo hayo pasipo na kujuwa.

Majengo hayo ni kama ifuatavyo: -

- Majengo Matatu ya Ofisi ya Tume Maisara.
- Ghala kuu la Kikwajuni.
- Jengo Wilaya ya Magharibi A.
- Jengo Wilaya ya Kati Unguja.
- Jengo la Wilaya ya Kusini.

### 6.2.3.3 Kutokatiwa Bima kwa vyombo vya moto vya Tume ya Uchaguzi

Ukaguzi umebaini kuwa Tume ya Uchaguzi Zanzibar inamiliki vyombo mbalimbali vya usafiri ikiwemo gari na vespa, dosari iliobainika ni kwa baadhi ya vyombo kutokukatiwa bima. Kutokukatiwa bima kwa vyombo vya moto kunaweza kukapelekea kudumaza shughuli za taasisi pale majanga yanapotokezea na kupelekea kutumia gharama kubwa ya matengenezo jambo ambalo linaweza likapelekea kupangua mipango ya utekelezaji wa shughuli nyengine walizojipangia.

Ukaguzi unashauri ni vyema taasisi za umma kuvikatia bima vyombo vyake ili kuepkua usumbufu utakao jitokeza pindipo majanga yanapotokezea. Mchanganuo wa vyombo ambavyo havijakatika bima ni kama inavyooekana katika jadweli la hapo chini:-

**Jadweli Nambari 26 : Vyombo vya moto ambavyo havijakatiwa Bima na Tume ya Uchaguzi**

| Namba ya Chombo | Aina ya Chombo | Chassis Namba | Engine Namba | Mwaka iliyonunuliwa |
|---|---|---|---|---|
| **Gari ambazo hazina Bima** | | | | |
| SMZ 847A | Land Cruiser Prado | JTEBH3FJ30K193019 | 1KD-FTV | 19/06/2018 |
| SMZ 841A | Landcruser | JTEBH3FJK01C193129 | 2750283 | 19/06/2018 |
| SMZ 849A | Land Cruiser Prado | JTEBH3FJ40K193112 | 1KD-FTV | 19/06/2018 |
| SMZ 390A | Nissan Motors | JNITC546120535259 | TD42166699 | 31/05/2013 |
| SMZ 393A | Nissan Motors Patrol | JNITCSY6120536737 | TD168214 | 31/05/2013 |
| SMZ 391A | Nissan Motors Patrol | JNITC346120535245 | - | 31/05/2013 |
| SMZ 386A | Nissan Motors Patrol | JNITCSY6120536779 | EI70903 | 31/05/2013 |
| SMZ 395A | Nissan Motors Patrol | JNITCSY6120536069 | TD42168995 | 31/05/2013 |
| SMZ 394A | Nissan Motors Patrol | JNITCSY6120536713 | EI700830 | 31/05/2013 |
| SMZ 387A | Nissan Motors Patrol | JNITCSY612053595 | TD042168214 | 31/05/2013 |
| SMZ 392A | Nissan Motors Patrol | JNTCSY6120536777 | EI70895 | 31/05/2013 |
| SMZ 1015A | Land Cruiser Prado | JTEBH3FJ20K193030 | IKD-FTV2982 | 26/11/2019 |
| **Vespa ambazo hazina Bima** | | | | |
| SMZ 1880C | TUK-TUK | LAACAKKCXH5000191 | 1711201248JP162FM | 06/04/2020 |
| SMZ 1880C | TUK-TUK | LAACAKKC5H5000213 | 1711201270JP162FM | 06/04/2020 |
| SMZ 1873C | TUK-TUK | LAACAKKC4H5000218 | 1711201275JP162FMJ | 06/04/2020 |
| SMZ 1874C | TUK-TUK | LAACAKKC6H5000222 | 1711201279JP162FMJ | 06/04/2020 |
| SMZ 18761C | TUK-TUK | LAACAKK1H5000225 | 1711201282JP162F | 06/04/2020 |
| SMZ 1875C | TUK-TUK | LAACAKKC8H5000223 | 1711201280JP162FM | 06/04/2020 |
| SMZ 1878C | TUK-TUK | LAACAKKCXH5000241 | 1711201298JP162FM | 06/04/2020 |
| SMZ 1877C | TUK-TUK | LAACAKKC4H5000235 | 1711201292JP162FMJ | 06/04/2020 |
| SMZ 1879C | TUK-TUK | LAACAKKCIH5000242 | 1711201299JP162FM | 06/04/2020 |
| SMZ 1871C | TUK-TUK | LAACAKKCIH5000211 | 1711201268JP162FMJ | 06/04/2020 |

### 6.2.3.4 Malipo kwa mtoa huduma ambae hakusajiliwa na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma shilingi 8,461,754

Kwa mujibu wa kifungu cha 23(1) cha Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016 kinaeleza kulingana na masharti ya sheria hii mtu, kampuni au taasisi haitawasilisha zabuni au vyenginevyo kushiriki katika manunuzi ya Umma isipokua chombo kiwe kimesajiliwa na Mamlaka ya Manunuzi.

Kwa mujibu wa kifungu cha 23(2), zabuni kutoka kwa mtu, kampuni au chombo ambacho hakijasajiliwa haifai na hakitazingatiwa na taasisi ya ununuzi.

Ukaguzi umebaini kwamba Ofisi ya Tume ya Uchaguzi Zanzibar imefanya manunuzi kwa mujibu wa hati namba 2/10 ya tarehe 16/10/20 yenye thamani ya shilingi 8,461,754 ambazo amelipwa kampuni ya **Hiffah General Trading Co Ltd** ikiwa ni Sehemu ya malipo ya Ujenzi wa Ukuta wa Ofisi ya Tume ya Uchaguzi. Dosari iliyobainika na ukaguzi ni kuwa kampuni hiyo haikusajiliwa na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya Zanzibar.

Kufanya hivyo kunapelekea kuikosesha Serikali mapato, aidha ni kwenda kinyume na Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016.

**DEPOSIT ACCOUNT - Hesabu Namba 0404346000**

### 6.2.3.5 Vifaa ambavyo havikuingizwa katika daftari la ghalani shilingi 67,533,238

Ukaguzi umebaini kuwa jumla ya shingi 67,533,238 zimetumika kwa ajili ya ununuzi wa mafuta na vifaa mbali mbali lakini mafuta na vifaa hivyo havikuingizwa katika daftari kutunzia vifaa ghalani ili kuweza kuthibitisha uhalali wa mapokezi pamoja na matumizi yake.

Kutokuingizwa mafuta na vifaa hivyo katika daftari la kutunzia vifaa vya ghalani ni kwenda kinyume na Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 27 : Mafuta na vifaa ambavyo havikurikodiwa katika daftari la ghalani**

| Hati Namba | Hundi Namba | Kiasi cha fedha kilichotumika (shs) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 60/11/20 (17/11/20) | TT | 45,779,232 | Machochoki Telecommunication & General Services | Ununuzi wa vifaa vya kuandikia |
| 59/11/20 (13/11/20) | TT | 21,754,006 | | Ununuzi wa vifaa vya kutengenezea magari. |
| **Jumla** | | **67,533,238** | | |

### 6.2.3.6 Malipo kwa Watoa huduma ambao hawajasajiliwa na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma shilingi 236,798,419

Kwa mujibu wa kifungu cha 23(1) cha Sheria ya Manunuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma kinaeleza kulingana na masharti ya sheria hii mtu, kampuni au taasisi haitawasilisha zabuni au vyenginevyo kushiriki katika manunuzi ya Umma isipokua chombo kiwe kimesajiliwa na Mamlaka ya Manunuzi.

Kwa mujibu wa kifungu cha 23(2), zabuni kutoka kwa mtu, kampuni au chombo ambacho hakijasajiliwa haifai na hakitazingatiwa na taasisi ya ununuzi.

Ukaguzi umebaini kwamba Ofisi ya Tume ya Uchaguzi Zanzibar imefanya manunuzi na watoa huduma mbali mbali ambao hawakusajiliwa na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya Zanzibar.

Kufanya hivyo kunapelekea kuikosesha Serikali mapato, aidha ni kwenda kinyume na Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 28 : Malipo yaliyofanyika kwa watoa huduma ambao hawakusajiliwa**

| Hati Namba | Kiasi cha fedha kilicholipwa (TShs) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|
| 5/7 ya 30/6/20 | 20,117,500 | Galfe Tech Engineering | Uwekaji wa mitambo ya video conference katika ofisi ya Tume Unguja & Pemba |
| 22/9 ya 9/8/20 | 2,042,500 | Planet Printing & Decoration | Fedha kwa ajili ya ufungaji wa Bannares katika hema la kuchukulia fomu za wagombea. |
| 4/8 ya 3/8/20 | 208,493,779 | GS Agents Limited | Ununuzi wa wino usiofutika pamoja na lakiri za masanduku ya vifaa vyakupigia kura. |
| 23/11/20 (3/11/20) | 4,721,640 | F.A Glass Works | Malipo kwa ajili ya ujenzi wa mnara wa tangi la maji. |
| 24/11/20 (10/11/20) | 850,000 | | Malipo kwa ajili ya matengenezo ya Ofisi ya Tume. |
| 29/12/20 (22/12/20) | 573,000 | | Malipo kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya maji. |
| **Jumla** | **236,798,419** | | |

**TUME YA UCHAGUZI – PEMBA**

### 6.2.3.7 Kukosekana kwa taarifa za usafirishaji wa Magari

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Tume ya Uchaguzi - Pemba imesafirisha gari tatu "3" zenye namba ya usajili SMZ 397A, SMZ 398A na SMZ 399A kwenda Unguja bila ya kufuatwa kwa utaratibu wa usafirishaji wa magari hayo.

Kitendo cha usafirishaji wa magari bila ya kufuata utaratibu au kuambatanisha taarifa zinazoonesha kuazimwa kwa gari hizo, kuuzwa kwa gari hizo au kwenda kutengenezwa na baadae kurudi kumetia shaka juu ya uwepo wa usafirishaji huo jambo ambalo huwenda likapelekea rasilimali za umma kupotea au kuibiwa au kuingia katika mikono isiyokuwa salama bila ya kuwepo kwa uthibitisho.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Tume ya Uchaguzi Pemba kufuata utaratibu na mwenendo wa utunzaji wa taarifa kwenye buku la kumbukumbu linaloonesha utolewaji wa mali za umma na kutumika kwa matumizi mengineyo au kuuzwa kwa lengo la uwekaji wa taarifa na kumbukumbu vizuri.

### 6.2.4 FUNGU C 05 – TUME YA UKIMWI ZANZIBAR

Ukaguzi wa hesabu za Tume ya Ukimwi kwa mwaka wa fedha 2020/2021 umefanywa kwa mujibu wa Sheria, kanuni, taratibu pamoja na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Taarifa ya Mapato**

Tume ya Ukimwi Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ilikadiriwa kupokea jumla ya shilingi 1,032,500,000 kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina na shilingi 342,337,089 kutoka washirika wa maendeleo. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 Tume ya Ukimwi Zanzibar ilipokea jumla ya shilingi 1,032,500,000 kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina kama ni ruzuku sawa na asilimia 100 ya makadirio na shilingi 440,352,569 kutoka washirika wa maendeleo sawa na asilimia 129 ya makadirio.

**Taarifa ya Matumizi**

Tume ya Ukimwi Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ilikadiriwa kutumia jumla ya shilingi 1,032,500,000 kati ya fedha hizo shilingi 1,001,650,000 kwa ajili ya kazi za kawaida, shilingi 30,850,000 kwa ajili ya kazi za maendeleo na shilingi 342,337,089 kutoka washirika wa maendeleo.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 Tume ya Ukimwi Zanzibar ilitumia jumla ya shilingi 560,620,458 kati ya fedha hizo shilingi 556,863,458 kwa ajili ya kazi za kawaida sawa na asilimia 56 ya makadirio, shilingi 3,757,000 kwa kazi za maendeleo sawa na asilimia 12 ya makadirio, na shilingi 440,352,569 kutoka kwa washirika wa maendeleo sawa na asilimia 129 ya makadirio.

**MATOKEO NA MAPENDEKEZO YA UKAGUZI**

**AKAUNTI NAMBARI: 0404438000**

#### 6.2.4.1 Malipo yaliyofanyika bila ya kufuata programu ya kazi shilingi 3,472,000

Tume ya Ukimwi Zanzibar iliandaa programu ya kazi ya ufuatiliaji ya robo mwaka kwa CTC na YFS kwa ajili ya kutathmini HIV /SRH ambapo utekelezaji ulipangiwa kuanzia tarehe 15/3 hadi 17/3/2021 kwa mujibu wa hati ya malipo nambari 3/3 ya tarehe 9/3/2021, hundi nambari 678 yenye thamani ya shilingi 3,472,000.00 kwa program hiyo.

Dosari iliyobainika katika ukaguzi ni kutokufuatwa kwa programu ya utekelezaji wa shughuli hiyo, ambapo malipo yameonyesha kulipwa tarehe 24/3/2021 kwa siku nne (4) kwa maafisa wa ZAC na siku tatu (3) kwa dereva, aidha fomu ya mahudhurio inaonyesha siku moja tu (1) yaani ya tarehe 24/3/2021. Kwa mujibu wa programu imepangwa siku tatu (3) lakini malipo yamelipwa kwa siku nne (4).

Aidha kumekuwepo kwa karatasi za mahudhurio zilizoambatanishwa na hati ya malipo zinazoonyesha mahudhurio ya tarehe 25/3/2021 na 29/3 hadi 30/3/2021, hivyo ukaguzi umeshindwa kupata vielelezo sahihi vya malipo ya utekelezaji wa programu hiyo.

Kutokana na Uwepo wa mchanganyiko wa taarifa hizo kumepelekea kujitokeza kwa viashiria vya taarifa za kuhushi kwa kupatikana idadi maalumu za siku zilizofanyika kwa program hiyo jambo ambalo linatia shaka juu ya uhalisia wa matumizi hayo ya fedha.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Tume ya Ukimwi Zanzibar kuhakikisha kwamba vielelezo sahihi vinaambatanishwa na hati za malipo kwa ukaguzi.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016.

### 6.2.4.2 Kukosekana uthibitisho wa matumizi ya uendeshaji kazi shilingi 900,000

Katika ukaguzi uliofanyika mwaka wa fedha 2020/2021 imebainika katika utekelezaji wa shughuli za kila siku za Tume ya Ukimwi Zanzibar imefanya malipo kwa hati ya tarehe 29/6/2021 yenye thamani ya shilingi 900,000 kwa ununuzi wa vifaa vya kuandikia (stationary) na mafuta lita 252 kutoka kwa Kampuni ya ambs Traders, P.O.BOX 2860, Kariakoo- Dar es Salaam kwa ajili ya uendeshaji kazi za kiofisi. Ukaguzi umebaini dosari mbali mbali katika matumizi ya fedha hizo zikiwemo:-

a. Kutokuwepo kwa ushindani wa bei (three quotations) za ununuzi wa stationary za shilingi 300,000.

b. Kutokurikodiwa kwa mafuta lita 252 ya shilingi 600,000 katika daftari la kutunzia mafuta la ghalani.

c. Kutokuwepo kwa utaratibu wa utumiaji wa mafuta hayo.

d. Kutokulipiwa kodi ya ongezeko la thamani na kodi ya tozo ya zuio.

e. Kutokuwepo barua ya dokezo ya kuhalalisha matumizi iliyosainiwa na Mkurugenzi Mkuu ambaye ndiye anayehalalisha malipo hayo.

f. Kutojuilikana Kiwango pamoja na aina ya stationary zilizonunuliwa kwa shilingi 300,000.

g. Kutokuwepo kwa karatasi ya mahitajio kutoka kwa watumiaji husika (local purchase order).

h. Kutokujuilikana aina ya vifaa (stationary) vilivyonunuliwa kutoka Kampuni ya AMBS Traders, P.O.BOX 2860 Kariakoo, Dar es saalam kwa mujibu wa risiti husika.

Kufanya malipo bila kufuata taratibu za matumizi kunapelekea uhalali wa malipo hayo kutokuthibitika na kusababisha upotevu wa fedha za serikali jambo ambalo ni kwenda kinyume na Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Tume ya Ukimwi kuhakikisha kwamba matumizi yote yanafanyika kwa mujibu wa taratibu, miongozo na sheria za fedha husika ili kuweza kuthibitisha uhalali wa matumizi hayo.

**AKAUNTI NAMBARI 0404309000**

### 6.2.4.3 Kukosekana utaratibu wa manunuzi wa kutumia ushindani wa bei shilingi 750,000

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2020/221 Tume ya Ukimwi imefanya ununuzi wa vifaa mbali mbali kwa ajili ya matumizi ya ofisi kwa mujibu wa hati namba 23/11yenye hundi namba 034892 kwa thamani ya shilingi 750,000.

Dosari iliyobainika katika ukaguzi ni kukosekana kwa taratibu za ushindani wa bei (three quotations) kwa mujibu wa sheria Nambari 11 ya ununuzi na uondoshaji wa mali za umma ya mwaka 2016. Kukosekana kwa three quatation kunaweza kupelekea taasisi ya umma kufanya mali kwa thamani kubwa zaidi ulinganisha na bei ya sokoni jambo ambalo litapelekea upotevu wa fedha za umma.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Tume ya Ukimwi Zanzibar kuhakikisha kwamba taratibu za ununuzi zinafuatwa kwa mujibu wa sheria za manunuzi husika.

#### 6.2.4.4 Malipo yaliyofanyika kwa njia ya vocha ndogo (sub-voucher) shilingi 700,000

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021 Tume ya Ukimwi Zanzibar imetoa fedha za matumizi kupitia Akaunti nambari **0404309000 ya UNICEF/UN-AIDS** kwa ajili ya matumizi mbali mbali ya Ofisi kupitia hati ya malipo ya tarehe 27/11/2020, hundi nambari 034899 yenye thamani ya shilingi 6,690,000.00 ambayo inahusika. Dosari zilizobainika katika ukaguzi ni kama zifuatazo:-

a. Jumla ya shilingi 700,000.00 zimelipwa kwa vocha ndogo (sub- voucher) kwa njia ya fedha taslim jambo ambalo ni kwenda kinyume na Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016.

b. Kukosekana kwa stakabadhi ya manunuzi hayo jambo ambalo limetia shaka juu ya uhalisia wa matumizi yaliyofanyika.

c. Kukosekana kwa saini ya mpokeaji wa fedha pamoja na saini ya mlipaji ili kuweza kuthibitisha uhalisia wa malipo hayo yalivyofanyika ili kuweza kujiridhisha uhalali wa malipo husika.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na sheria Nambari 12 ya usimamizi wa fedha za umma ya mwaka 2016.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Tume kuhakikisha kwamba fedha zote zinalipwa kwa mujibu wa muongozo wa ulipaji wa fedha husika za Serikali ili kuweza kuthibitisha matumizi hayo.

#### 6.2.4.5 Manunuzi yaliyofanyika bila ya kuambatanishwa barua ya maombi kutoka kwa mtumiaji shilingi 1,288,000

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021 Tume ya Ukimwi Zanzibar imefanya ununuzi wa mipira mine (4) ya gari SMZ 1007A kwa mujibu wa barua ya hati namba 22/6/2021 aliyelipwa Ndugu Abrahman Ismail Vuai kwa Thamani ya shilingi 1,288,000 kwa ajili Ununuzi wa mipira ya gari. Dosari iliyobainika ni Kukosekana kwa barua ya maombi ya Ununuzi huo kutoka kwa mtumiaji kwenda kwa Afisa ununuzi ili kuweza kupata uhalali wa manunuzi wa mipira hiyo.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Tume ya Ukimwi Zanzibar kuhakikisha kwamba barua ya maombi ya ununuzi wa kifaa chochote kinapatikana kwanza kutoka kwa mtumiaji kabla ya kufanya manunuzi ili kuweza kupima uawajibikaji katia vitengo vya taasisi ya umma.

**TUME YA UKIMWI – PEMBA**

#### 6.2.4.6 Kutokuripoti kazini kwa mtumishi aliyemaliza muda wa likizo bila ya malipo

Kwa mujibu wa kifungu nambari 64(1) cha kanuni za utumishi wa Umma 2014, mtumishi wa umma ambaye hajaripoti kazini baada ya likizo bila ya malipo kumalizika Katibu Mkuu au mkuu wa Taasisi atalazimika:

a) Kumkumbusha mtumishi anaehusika kuripoti kazini

b) Endapo mtumishi wa umma atashindwa kuripoti kazini hatua zote za kinidhamu zimeshachukuliwa dhidi yake.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwa **Ndugu Mohammed Said Mohammed** ambaye ni muajiriwa wa Ofisi ya Tume ya Ukimwi Pemba aliyechukua likizo bila malipo kwa vipindi viwili "2" tofauti lakini pamoja na jitihada mbali mbali zilizochukuliwa na Ofisi, bado mtumishi huyo hajaripoti kazini.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 64(1) cha Kanuni ya Utumishi wa Umma ya Zanzibar ya mwaka 2014.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Tume ya Ukimwi kuchukuwa jitihada za makusudi za kuhakikisha zinatoa haki ya kumtafuta na kumsikiliza ili kubaini mambo yaliyomkwaza kuripoti kazi kwa mujibu wa utaratibu vyenginevyo hatua za kinidhamu zichukuliwe dhidi yake ikiwemo kumfukuza kazi pale atakaposhindwa kutii maamuzi na maelekezo ya kazini.

### 6.2.4.7 Malipo kwa Watoa huduma ambao hawakusajiliwa na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma shilingi 4,085,433

Kwa mujibu wa kifungu cha 23(1) cha Sheria ya Manunuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma kinaeleza kulingana na masharti ya sheria hii mtu, kampuni au taasisi haitawasilisha zabuni au vyenginevyo kushiriki katika manunuzi ya Umma isipokua chombo kiwe kimesajiliwa na Mamlaka ya Manunuzi.

Kwa mujibu wa kifungu cha 23(2), zabuni kutoka kwa mtu, kampuni au chombo ambacho hakijasajiliwa haifai na hakitazingatiwa na taasisi ya ununuzi.

Ukaguzi umebaini kwamba Tume ya Ukimwi Pemba imefanya manunuzi na watoa huduma mbali mbali ambao hawakusajiliwa na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya Zanzibar.

Kufanya hivyo kunapelekea kuikosesha Serikali mapato ambapo ni kwenda kinyume na Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016. Mchanganuo wa watoa huduma hao ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 29 : Watoa huduma ambao Hawakusajiliwa na Mamlaka ya ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma**

| Hati Namba | Hundi Namba | Kiasi cha fedha kilicholipwa (Tshs.) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 1/8<br>10/8/2020 | 016395 | 600,000 | Fresh & Son Take Away na Misufini Colling Station | Malipo ya fedha kwa ajili ya matumizi mbali mbali ya Ofisi |
| 22/8<br>24/8/2020 | 017422 | 1,425,900 | Pemba General Supply | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa friji. |
| 23/8<br>24/8/2020 | 017423 | 249,533 | Hassan M.Cycle Spare Parts | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya magari. |
| 16/12<br>30/12/2020 | 018790 | 60,000 | Misufini Colling Station | Malipo ya fedha kwa ajili ya matumuzi mbali mbali ya ofisi |
| 4/2<br>3/2/2021 | 019303 | 300,000 | Muss Tea and Refreshment | Malipo ya fedha kwa ajili ya posho la chakula na vinywaji. |
| 2/2<br>3/2/2021 | 019303 | 350,000 | Fresh & Son Take Away | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa viburudishaji. |
| 3/5<br>5/5/2021 | 020908 | 350,000 | | |
| 6/4<br>15/4/2021 | 020394 | 350,000 | | |
| 16/5<br>5/5/2021 | 021088 | 400,000 | Hassan M.Cycle Spare Parts | Malipo ya fedha kwa ajili ya matengenezo ya pikipiki |
| **Jumla** | | **4,085,433** | | |

**ZANZIBAR AIDS COMMISSION – HESABU NAMBARI 0404316000**

### 6.2.4.8 Malipo kwa watoa huduma ambao hawajasajiliwa na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma shilingi 12,870,000

Kwa mujibu wa kifungu cha 23(1) cha Sheria ya Manunuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma kinaeleza kulingana na masharti ya sheria hii mtu, kampuni au taasisi haitawasilisha zabuni au vyenginevyo kushiriki katika manunuzi ya Umma isipokua chombo kiwe kimesajiliwa na Mamlaka ya Manunuzi.

Kwa mujibu wa kifungu cha 23(2), zabuni kutoka kwa mtu, kampuni au chombo ambacho hakijasajiliwa haifai na hakitazingatiwa na taasisi ya ununuzi.

Ukaguzi umebaini kwamba Tume ya Ukimwi Pemba imefanya manunuzi na watoa huduma mbali mbali ambao hawakusajiliwa na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya Zanzibar.

Kufanya hivyo kunapelekea kuikosesha Serikali mapato ambapo ni kwenda kinyume na Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016. Mchanganuo wa watoa huduma hao ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 30 : Watoa huduma ambao hawakusajiliwa na Mamlaka ya ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma**

| Hati Namba | Hundi Namba | Kiasi cha fedha kilicholipwa (Tshs.) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 1/9 ya 8/9/2020 | 000228 | 300,000 | Muus Tea and Refreshment | Malipo ya fedha kwa ajili ya viburudishaji |
| 1/11 ya 6/11/2020 | 000232 | 255,000 | | |
| 2/11 ya 13/11/2020 | 000230 | 405,000 | Mohammed Aboud Ali | Malipo kwa ajili ya siku ya ukimwi Duniani |
| 5/3 ya 24/3/2021 | 000238 | 300,000 | Muus Tea and Refreshment | Malipo ya fedha kwa ajili ya viburudishaji |
| 2/6 ya 3/6/2021 | 000241 | 300,000 | | |
| 3/6 ya 14/6/2021 | 000242 | 540,000 | | |
| 4/6 ya 14/6/2021 | 000243 | 600,000 | | |
| 5/6 ya 16/6/2021 | 000244 | 300,000 | | |
| 7/6 ya 18/6/2021 | 000247 | 2,970,000 | Salim Abdalla Seif | Malipo ya fedha kwa ajili ya viburudishaji |
| 8/6 ya 18/6/2021 | 000248 | 900,000 | Ahmed Issa Mohammed | |
| 10/6 ya 22/6/2021 | 000250 | 2,130,000 | Muus Tea and Refreshment | |
| 11/6 ya 23/6/2021 | 000252 | 900,000 | Ahmed Issa Mohammed | |
| 12/6 ya 23/6/2021 | 000253 | 2,970,000 | Salim Abdalla Seif | |
| **Jumla** | | **12,870,000** | | |

### 6.2.5 KAMISHENI YA KUKABILIANA NA MAAFA

Ukaguzi wa hesabu za Kamisheni ya Kukabiliana na Maafa kwa mwaka wa fedha 2020/2021 umefanywa kwa mujibu wa Sheria, kanuni, taratibu pamoja na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Taarifa ya Matumizi**

Kamisheni ya kukabiliana na Maafa kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ilikadiriwa kutumia jumla ya shilingi 682,940,429 kwa ajili ya kazi za kawaida na shilingi 192,680,810 kwa ajili ya kazi za maendeleo. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 jumla ya shilingi 682,940,429 ziliingizwa na kutumika kwa kazi za kawaida sawa na asilimia 100 ya makadirio, na shilingi 191,538,283 ziliingizwa na kutumika kwa kazi za maendeleo ambapo ni sawa na asilimia 99.4 ya makadirio.

**MATOKEO NA MAPENDEKEZO YA UKAGUZI**

#### 6.2.5.1 Fedha ambazo hazikuhaulishwa Mfuko Mkuu wa Serikali kipindi cha mwisho wa mwaka shilingi 786,830.63

Kwa mujibu wa Toleo nambari AD./184/01/07/80 la tarehe 9/6/2021 kipengele D kinaeleza kwamba Bakaa ya fedha za Wizara/Idara/Mikoa na Taasisi za SMZ (Central Government) zilizokua zimepangiwa kutumika kwa baadae (Commitment) zote ziingizwe katika hesabu Kuu ya Serikali iliyoko Benki Kuu nambari 9928161804 (C. MISCELLANEOUS DEPOSIT ACCOUNT) na bakaa ambazo hazina Commitment zirejeshwe Mfuko Mkuu wa Hazina (Mfuko Mkuu wa hazina hesabu nambari 0404381000).

Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 ukaguzi umebaini kwamba jumla ya shilingi 786,830.63 zimeonekana kubakia bila ya kufanyiwa uhaulishwaji na kupelekwa katika Mfuko Mkuu wa Serikali hesabu nambari 0404381000 ili kuendana na miongozo iliyotolewa.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na toleo nambari AD./184/01/07/80 kutoka Ofisi ya Rais Fedha na Mipango.

**MFUKO WA MAAFA (UNICEF) - HESABU NAMBARI 0404081000**

### 6.2.5.2 Kutokuingizwa kwa taarifa za fedha katika hesabu za mwisho wa mwaka shilingi 92,176,283

Kwa mwaka wa fedha 2020/2021 Kamisheni ya Kukabiliana na Maafa ilikuwa na bakaa ya jumla ya shilingi 92,176,283 iliyotokana na matumizi ya mwaka wa fedha 2019/2020. Dosari iliyobainika wakati wa ukaguzi ni kutokuainishwa bakaa hiyo katika hesabu za mwisho wa mwaka (Financial Statements) zilizowasilishwa kwa ajili ya ukaguzi katika Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Kufanya hivyo kunaweza kupelekea kutokupatikana kwa usahihi wa hesabu zilizowasilishwa kwa ajili ya ukaguzi ambapo ni kwenda kinyume na Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Kamisheni ya Kukabiliana na Maafa kuhakikisha unafanya usahihi wa taarifa zinazotayarishwa na kuwasilishwa katika Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ikiwa ni pamoja na kujumuisha kikamilifu taarifa zote zinazohusu mapato na matumizi katika kipindi cha mwaka husika.

**DISASTER FUND - HESABU NAMBARI 0404287000**

### 6.2.5.3 Fedha ambazo hazikuhaulishwa Mfuko Mkuu wa Serikali kipindi cha mwisho wa mwaka shilingi 13,959,540

Kwa mujibu wa Toleo nambari AD./184/01/07/80 la tarehe 9/6/2021 kipengele D kinaeleza kwamba Bakaa ya fedha za Wizara/Idara/Mikoa na Taasisi za SMZ (Central Government) zilizokua na Commitment zote ziingizwe katika hesabu Kuu ya Serikali iliyoko Benki Kuu nambari 9928161804 (C. Miscellaneous deposit account) na bakaa ambazo hazina Commitment zirejeshwe Mfuko Mkuu wa Hazina (Mfuko Mkuu wa hazina Hesabu Nambari 0404381000).

Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 ukaguzi umebaini kwamba jumla ya shilingi 13,959,540 zimeonekana kubakia bila ya kufanyiwa uhaulishwaji na hazikurejeshwa katika Mfuko Mkuu wa Serikali hesabu nambari 0404381000 ili kuendana na miongozo iliyotolewa.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na toleo nambari AD./184/01/07/80 kutoka Ofisi ya Rais Fedha na Mipango.

## 6.3 WIZARA YA NCHI (OR) TAWALA ZA MIKOA, SERIKALI ZA MITAA NA IDARA MAALUM ZA SMZ

### 6.3.1 FUNGU D 01 – OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA, SERIKALI ZA MITAA NA IDARA MAALUM ZA SMZ

Ukaguzi wa hesabu za Wizara ya Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum kwa mwaka wa fedha 2020/2021 umefanywa kwa mujibu wa Sheria, kanuni, taratibu pamoja na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Taarifa ya Mapato**

Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ilikadiriwa kukusanya jumla ya shilingi 30,627,192,391. Hadi kufikia tarehe 30, Juni 2021 Ofisi imekusanya jumla ya shilingi 16,028,664,447 sawa na asilimia 52.3 ya makadirio.

**Taarifa ya Matumizi**

Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ilikadiriwa kutumia jumla ya shilingi 24,675,587,266 kwa ajili ya kazi za kawaida na shilingi 5,118,805,125 kwa ajili ya kazi za maendeleo. Hadi kufikia tarehe 30, Juni 2021 jumla ya shilingi 14,478,662,373.62 ziliingizwa na kutumika kwa kazi za kawaida sawa na asilimia 58.7 ya makadirio na shilingi 1,275,002,073.38 zimeingizwa na kutumika kwa kazi za maendeleo sawa na asilimia 24.9 ya makadirio.

**MATOKEO NA MAPENDEKEZO YA UKAGUZI**

#### 6.3.1.1 Malipo nje ya Mpango wa manunuzi shilingi 1,065,448,560

Kwa kuzingatia kifungu namba 42(1) cha Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016 kinaeleza kwamba "kitengo cha ununuzi na uondoshaji wa mali za umma kitaandaa na kuwasilisha kwa mlipaji mkuu wa Serikali mpango wake wa mwaka wa ununuzi na uondoshaji kwa mwaka unaofata".

Kifungu namba 42(7) cha Sheria Nambari 11ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016 kinaeleza kwamba "ununuzi hautofanyika kinyume na mpango wa manunuzi na uondoshaji wa mali za umma isipokuwa kwa hali ya haraka na dharura.

Ukaguzi umebaini kwamba kwa mwaka wa fedha unaoishishia Juni 30, 2021 Ofisi ya Raisi, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ ilikadiria jumla ya shilingi 1,158,130,000 kupitia kasma ya "SECURITY SERVICES" yenye utambulisho wa nambari 2200112 na kufanya malipo yenye thamani ya shilingi 1,065,448,560 kwa kumlipa Umawa na Smart Secutities kwa ajili ya kupatiwa huduma ya ulinzi dosari iliyobainika ni kufanyika kwa malipo hayo nje ya mpango wa manunuzi.

Kufanya hivyo kunapelekea kuathiri matumizi yaliyopangwa kwa mujibu wa mapango wa manunuzi wa mwaka ambapo ni kwenda kinyume na vifungu vya sheria vilivyonakiliwa hapo juu. Malipo hayo kalipwa .

### 6.3.1.2 Kutorikodiwa kwa mafuta katika daftari la kutunzia mafuta ghalani shilingi 150,758,377

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum ya SMZ imetumia jumla ya shilingi 150,758,377 kwa ununuzi wa mafuta kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli mbalimbali za ofisi lakini mafuta hayo hayakurikodiwa katika daftari la kutunzia mafuta ghalani ili kuweza kuthibitisha uhalali wa mapokezi pamoja na matumizi yake.

Aidha Wizara imeshindwa kuwasilisha vitabu vilivyotumika katika mgao wa mafuta (issuer vocher) kwa ajili ya ukaguzi. Hali ambayo imepelekea wakaguzi kushindwa kujiridhisha na mtiririko mzima wa mgao wa mafuta ya ofisi hiyo. Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu namba 220(1) (2) cha kanuni za fedha za mwaka 2005.

Mchanganuo wa mafuta hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

### Jadweli Nambari 31 : Kutorikodiwa kwa mafuta katika daftari la kutunzia mafuta ghalani

| Hati Namba | Alielipwa | Thamani (Tshs) | Risiti/Ankara | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 12/8 ya 18/8/2020 | United Group Limited | 4,998,544 | Risiti namba 04971/Ankara namba 3073 | Malipo kwa ajili ya ununuzi wa mafuta ya shughuli za Ofisi |
| 39/8 ya 25/8/2020 | Zanzibar Petroleum | 1,275,925 | Risiti namba 35687/Ankara namba 5891 | |
| 18/9 ya 3/9/2020 | United Group Limited | 1,153,620 | Risiti namba 08463/Ankara namba 3215 | |
| 16/10 ya 20/10/2020 | | 2,499,154 | Risiti namba 06476/Ankara namba 3318 | |
| 18/10 ya 20/10/2020 | Gulioni Filling Station | 1,020,000 | Risiti 1336 | |
| 17/1 ya 13/1/2021 | United Group Limited | 2,999,928 | Risiti namba 327/Ankara namba 3459 | |
| 9/9 ya 3/9/2020 | | 787,500 | Risiti namba 08461/Ankara namba 3200 | |
| 10/9 ya 3/9/2020 | | 1,935,500 | Risiti namba 08462/Ankara namba 3199 | |
| 63/9 ya 22/9/2020 | Kijangwani Petrol Station | 11,200,000 | Risiti namba 0198/Ankara namba 0901 | |
| 74/9 ya 23/9/2020 | United Group Limited | 1,919,414 | Risiti namba 08473/Ankara namba 3258 | |
| 16/10 ya 20/10/2020 | | 2,499,815 | Risiti 06476 Ankara namba 3318 | |
| 4/2 ya 4/2/2021 | | 2,712,407 | Risiti namba 938/Ankara namba 3491 | |
| 27/2 ya 22/2/2021 | | 7,905,762 | Risiti namba 1268 | |
| 61/2 ya 26/2/2021 | | 16,740,000 | - | |
| 5/8 ya 4/8/2020 | Kijangwani Petrol Station | 48,791,000 | Risiti namba 3421/Ankara namba 0287 | |
| 12/8 ya 18/8/2020 | United Group Limited | 4,999,808 | Risiti namba 04971/Ankara namba 3073 | |
| 49/8 ya 26/8/2020 | Kijangwani Petrol Station | 6,120,000 | Risiti3175/ Ankara namba 0160 | |
| 80/4 ya 28/4/2021 | - | 1,200,000 | - | |
| 2/1 ya 6/1/2021 | Kijangwani Petrol Station | 30,000,000 | Risiti namba 0922/Ankara namba 0055 | |
| **Jumla** | | **150,758,377** | | |

**MRADI WA MJI SALAMA**

### 6.3.1.3 Dosari zilizojitokeza kwenye Mradi wa Mji Salama

Mradi wa Mji Salama ni moja wa mradi uliochini ya ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za mitaa na Idara Maalum za SMZ wenye dhima ya kulinda usalama wa mji wa Zanzibar. Mradi huu kwa Unguja upo Mkoa wa Mjini Magharibi na kwa Pemba unajumuisha Pemba nzima. Mradi huu upo kwenye awamu ya pili (phase 2) na unahusiana na miundo mbinu ya uwekaji wa kamera na kufanya matengenezo ya kamera hizo pale zinapokabiliwa na changamoto za aina mbalimbali.

Mradi huu wa Zanzibar Salama kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni 2021, ulikadiriwa kutumia jumla ya shilingi 8,000,000,000. Hadi kufikia tarehe 30 Juni,2021 mradi ulitumia jumla ya shilingi 7,828,326,910, aidha malipo ya mradi huu hulipwa kutoka kwenye mradi wa miundo mbinu ulioko chini ya usimamizi wa Mfuko Mkuu wa Hazina kwa kuingiza fedha moja kwa moja kwenye hesabu ya mtoa huduma aitwae "ROM Solution ltd".

Aidha ukaguzi umebaini kuwepo wa dosari mbalimbali zinazotokana na mkataba, vifaa na utekelezaji wa mradi husika. Dosari zenyewe ni kama zifuatazo;

### i) Mapungufu Yaliomo Kwenye Mkataba wa Phase II

Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ imeingia mkataba siku ya tarehe 4/12/2019 baina ya ROM Solution Ltd na ofisi hiyo kwa ajili ya uwekaji wa miundo mbinu ya kamera pamoja na kamera katika Mkoa wa Mjini Magharibi na Pemba kwa thamani ya USD 10,655,166 kwa muda wa miaka mitatu**.** Aidha ukaguzi umebaini kuwepo kwa "**addendum**" inayohuisiana na malipo iliyotiwa saini siku ya tarehe 1/7/2020 ambayo imeeleza kwamba malipo yote yatakuwa na thamani ya USD 3,701,148 sawa na asilimia 34.74.

Ukaguzi umebaini uwepo wa dosari zifuatazo zinazotokana na mkataba huo:-

- Kutofanyiwa matengenezo kwa mali za kudumu za Mradi wa Mji Salama.
- Uwepo wa pikipiki 20 zilizonunuliwa kwa ajili ya mradi huo, kati ya hizo pikipiki 14 zinaendelea kufanya kazi kama ilivyokusudiwa na zilizobaki 6 zimeharibika kwa muda mrefu bila ya kufanyiwa matengenezo.
- Uwepo wa gari 12 zilizokuwa zinatumika kwenye mradi ambazo zimeharibika bila ya kufanyiwa matengenezo na Mtoa huduma wa mradi yaani Rom Solution ltd na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 33(1) cha mkataba ulioainishwa hapo juu kinachoeleza kwamba "The supplier shall with no additional cost from the client make maintenance of the goods for the period of five years". Jadweli lifuatalo linaonyesha mchanganuo wa vyombo hivyo:-

**Jadweli Nambari 32 : Dosari katika vyombo vya Moto**

| Aina ya Chombo | Nambari ya Chombo | Nambari ya Umiliki wa Chombo | Mtumiaji wa Chombo/Mahali Kilipo Chombo | Dosari na Chombo Husika |
|---|---|---|---|---|
| Honda - KTM | SMZ 1270 C | Z-047369542 | CCTV | Battery na fuel pump) |
| Honda - KTM | SMZ 1275 C | Z-047369641 | CCTV | (Battery na fuel pump) |
| Honda – KTM | SMZ 1273 C | Z-047369608 | CCTV | (Fuel pump na valve) |
| Honda – KTM | SMZ 1280 C | Z-047369740 | CCTV | (Battery na brake liver) |
| Honda – KTM | SMZ 1282 C | Z-047369784 | CCTV | (Fuel pump) |
| Honda – KTM | SMZ 1283 C | Z-047369828 | CCTV | (Battery na fuel pump) |
| Trailer ZBV inspection vehicle | SMZ 959 A | Z-048353602 | CCTV- Bandarini | - |
| Amaroc | SMZ 632 A | Z – 047008544 | AR-TMIM za SMZ | Nosel |
| Amaruc | SMZ 636 A | Z- 047008665 | AR-TMIM za SMZ | Clutch |
| Amaruc | SMZ 583 A | Z- 046730453 | KMKM | Nosel |
| Amaruc | SMZ 577 A | Z- 046730156 | KMKM | Nosel |
| Amaruc | SMZ 581 A | Z- 046730354 | Mafunzo | Clutch, gear box na bearing |
| Amaruc | SMZ 582 A | Z-046730398 | Mafunzo | Nosel na mipira |
| Amaruc | SMZ 576 A | Z- 046730134 | Mafunzo | Nosel |
| Amaruc | SMZ 578 A | Z-0467301910 | KZU | Nosel |
| Amaruc | SMZ 579 A | Z- 046730277 | KZU | Nosel |
| Amaruc | SMZ 634 A | Z- 047008588 | KVZ Kazi Maalum | - |
| Amaruc | SMZ 572 A | Z- 046729573 | KVZ | Nosel |

Ukaguzi unashauri uongozi wa ofisi uhakikishe kwamba vyombo vyote vinavyohitaji matengenezo vifanyiwe matengenezo ili viweze kusaidia katika kutekeleza majukumu yaliowekwa na mradi.

**ii) Kutotumika na kutofanya kazi kwa baadhi ya vifaa vilivyomo kwenye mradi**

Ukaguzi ulifanya mahojiano na baadhi ya watendaji wanaohusiana na mradi wa CCTV kamera siku ya tarehe 20/10/2020 na kubaini kuwepo kwa baadhi ya vifaa ambavyo havijaanza kutumika katika mradi huo toka kupokelewa kwake. Kwa mfano ndege mbili zisizo na rubani (Drones) zinazotumika kwa ajili ya kupiga picha ambazo zimehifadhiwa kwenye maboksi badala ya kutumika kwenye shughuli mbalimbali za utekelezaji wa mradi.

Aidha ukaguzi umebaini uwepo wa gari aina ya trailer ZBV yenye namba SMZ 959 A iliyoletwa kwa ajili ya ukaguzi wa mizigo hapo bandarini ambayo toka kupokelewa kwake miaka miwili haijafanya kazi. Hii imetokana na kutofanya kazi kwa mtambo uliomo kwenye gari hilo, kwa sasa gari hii ipo Makao Makuu ya mradi hapo Maisara.

Aidha ukaguzi umebaini kutofanya kazi kwa baadhi ya kamera zilizowekwa katika maeneo tofauti yaliomo kwenye mradi.

Kutotumika na kutofanya kazi kwa baadhi ya vifaa viliomo kwenye mradi kunapelekea:

- Kutofikiwa kwa lengo kuu la Mradi wa Mji Salama.
- Kuwepo kwa matumizi mabaya ya fedha za Serikali.
- Kuharibika kwa vifaa hivyo ambavyo vimekaa kwa muda mrefu bila ya kutumika.
- Kukosekana kwa tija iliyokusudiwa na Serikali.

### 6.3.2 FUNGU D 02 - JESHI LA KUJENGA UCHUMI (JKU)

Ukaguzi wa hesabu za Jeshi la Kujenga Uchumi kwa mwaka wa fedha 2020/2021 umefanywa kwa mujibu wa Sheria, kanuni, taratibu pamoja na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Taarifa ya Mapato**

Jeshi la Kujenga Uchumi (JKU) lilikadiriwa kukusanya jumla ya shilingi 34,328,698,851 kwa mwaka wa fedha 2020/2021. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 JKU ilikusanya jumla ya shilingi 31,228,409,512 sawa na asilimia 91 ya makadirio.

**Taarifa ya Matumizi**

Jeshi la Kujenga Uchumi kwa mwaka wa fedha 2020/2021 lilikadiriwa kutumia jumla ya shilingi 34,328,098,851 kwa kazi za kawaida. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 jumla ya shilingi 31,228,409,512 zimeingizwa na kutumika kwa kazi za kawaida sawa na asilimia 91 ya makadirio.

**MATOKEO NA MAPENDEKEZO YA UKAGUZI**

#### 6.3.2.1 Hati za malipo zilizokosekana kwa ukaguzi shilingi 647,863,625

Ukaguzi umepitia taarifa ya utoaji wa fedha kwa njia ya IFMS (Exchequer releases) na kubaini jumla ya shilingi **1,329,000,000** zimetengwa kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya ujenzi wa Hanga mbili na Bwalo moja la Askari Msaani Pemba (JKU) .

Aidha, ukaguzi umepitia hati za malipo yenye jumla ya shilingi **681,136,375** na kubaini amelipwa Mzabuni SABAH STORE kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya ujenzi wa Hanga Msaani Pemba. Aidha, hati za malipo pamoja na vielelezo vinavyothibitisha uhalali wa malipo yenye thamani ya shilingi **647,863,625** hazikupatikana kwa ukaguzi.

Kutokupatikana kwa ukaguzi kwa hati za malipo pamoja na vielelezo vinavyothibitisha malipo hayo kunapelekea kujitokeza kwa viashiria vya upotevu wa fedha za umma jambo ambalo linaweza kupelekea kuisababishia hasara Serikali.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016 pamoja na kanuni na kanuni namba 95(4) ya mwaka 2005.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Jeshi la Kujenga Uchumi kuhakikisha hati za malipo zinapatikana pamoja na vielelezo vyake kwa ukaguzi ili kuthibitisha uhalali wa malipo husika. Hati za malipo zilikosekana ni kama zinavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 33: Hati za malipo zilizokosekana kwa ukaguzi**

| Hati namba | Aliyelipwa | Kiasi (Tshs) | Maelezo |
|---|---|---|---|
| Pv namba 5/5/2021 | Sabah Store | 204,814,500 | Malipo kwa ajili ya gharama za vifaa vya ujenzi Kambi ya Jku Msaani |
| Pv namba 18/6/2021 | | 299,940,375 | |
| Trh 17/6/2021 | | 96,040,000 | |
| Trh 17/6/2021 | | 49,100,000 | |
| Trh 17/6/2021 | | 31,241,500 | |
| | | **681,136,375** | |

#### 6.3.2.2 Kutofuatwa kwa taratibu za manunuzi shilingi 61,000,000

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika Jeshi la Kujenga Uchumi limefanya malipo ya shilingi 61,000,000 kwa **ndugu RASHID MOHAMMED SOUD** kwa ajili ya ununuzi wa gari mbili (2) aina ya **PRADO** kwa mujibu wa ankara namba 128 ya mwezi wa Disemba 2020. Katika ufuatiliaji wa ukaguzi wa ndugu Rashid Mohamed Soud imebainika amejisajili kutoa huduma za uuzaji wa Vipuri **(Spare Parts)** na sio uuzaji wa magari kama ilivyonunuliwa na Jeshi la Kujenga Uchumi.

Dosari iliyobainika katika ukaguzi ni kutokutangazwa kwa zabuni pamoja na kutokupatikana kwa makubaliano ya mkataba wa ununuzi wa gari hizo, kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 65 cha Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshwaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016.

Hata hivyo ukaguzi umebaini Jeshi la Kujenga Uchumi limekiuka muongozo wa Baraza la Mapinduzi wenye kumbukumbu namba BLM/97/M/C.5/VOL.V/27 wa tarehe 27 Septemba 2021 kutoka Serikalini uliotolewa na Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi kuwaagiza Wakuu wote wa Taasisi kuwasilisha maombi ya ununuzi wa gari kwa Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Fedha na Mipango na kuacha kununua magari yaliyotumika (Used Car) pamoja na kuacha kununua magari kwa wazabuni binafsi kwa lengo la kununua gari kwa thamani kubwa kuliko bei ya sokoni ambapo Jeshi la Kujenga Uchumi limenunua gari mbili zilizotumika (Used Car) bila ya kupata ridhaa ya kibali kutoka kwa Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi, hata hivyo ukaguzi haukuweza kupatiwa ripoti ya ukaguzi wa gari hizo (Inspection Report) kutoka kwa fundi mkuu wa Karakana ya Serikali kwa vile gari hizo hazikufanyiwa uchunguzi wa kina kujua umadhubuti na uzima wa gari hizo, ukaguzi haukuweza kupatiwa hatiya mapokezi ya gari hizo (Delivery Note).

Kufanya manunuzi kinyume na matoleo ya Serikali kunapelekea taasisi ya umma kutumia gharama kubwa ya ununuzi unaotokana na wazabuni kuwauzia Serikali magari kwa gharama kubwa ukilinganisha na bei ya soko ilivyo.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 65 cha Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshwaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Jeshi la Kujenga Uchumi kuhakikisha unatekeleza miongozo inayotolewa na Serikali ili kuepusha kutumia fedha za umma kinyume na utaratibu.

#### 6.3.2.3 Kukosekana kwa uhalali wa Deni la ununuzi wa Gari lenye jumla ya shilingi 31,000,000

Ukaguzi umepitia taarifa mbalimbali za Jeshi la kujenga uchumi pamoja na baadhi ya taarifa za manunuzi na kubaini kwamba Jeshi la Kujenga Uchumi limefanya manunuzi wa Gari aina ya Toyota Prado yenye chassis nambari TRT 120-5022-585 yenye usajili wa Z 128 HK iliyonunuliwa kutoka kwa Nd. Rashid Mohammed Soud, kupitia Ankara nambari 128 ya tarehe 21/12/2020 yenye thamani ya shilingi 31,000,000. Ukaguzi umebaini kuwa fedha hizo hazijalipwa hadi kumalizika kwa Ukaguzi. Ithibati za vielelezo vya kuthibitisha deni haikupatikana kwa ukaguzi miongoni mwao ni kama hizi zifuatazo:-

- Kukosekana kwa Kibali cha ruhusa ya ununuzi wa gari Used kutoka kwa Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi.
- Kukosekana kwa kumbukumbu za bodi ya manunuzi za ufunguzi wa document za Wazabuni.

- Kutotangazwa kwa zabuni ya Ununuzi wa Gari.
- Kukosekana kwa Zuio la kodi (VAT NA ZRB).
- Kukosekana kwa ripoti ya tathmini (Evaluation report).
- Kukosekana kwa fomu za viapo za wajumbe wa tathmini (Code of Ethics).
- Kukosekana kwa mkataba wa makubaliano ya mauziano ya gari 2 baina ya Rashid Mohammed Soud na Jeshi la Kujenga Uchumi Zanzibar nk.

Kufanya manunuzi kinyume na matoleo ya Serikali kunapelekea taasisi ya umma kutumia gharama kubwa ya ununuzi unaotokana na wazabuni kuwauzia Serikali magari kwa gharama kubwa ukilinganisha na bei ya soko ilivyo.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 65 cha Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshwaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Jeshi la Kujenga Uchumi kuhakikisha unatekeleza miongozo inayotolewa na Serikali ili kuepusha kutumia fedha za umma kinyume na utaratibu.

### 6.3.2.4 Tofauti ya matumizi ya fedha baina ya Exchequer na Hati za Malipo shilingi 506,551,018

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kujitokeza kwa tofauti ya malipo baina ya hati za malipo na fedha iliyoingizwa kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina. Kwa mujibu wa fedha iliyoingizwa kwa ajili ya matumizi ya Kikosi cha Jeshi la Kujenga Uchumi kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina (Exchequer Release) ilikuwa na thamani ya shilingi 2,871,550,667 ambapo JKU lilitumika jumla ya shilingi 2,364,999,649 kwa ajili ya kumlipa mzabuni Sabah Store kwa ajili ya kutoa huduma mbali mbali katika Jeshi la Kujenga Uchumi. Dosari iliyobainika katika ukaguzi ni kukosekana kwa taarifa za tofauti ya matumizi ya shilingi 506,551,018 zilizobainika pamoja na vielelezo vinavyothibitisha uhalali wa uwepo wa matumzi hayo jambo ambalo limepelelekea kuashiria upotevu wa fedha za umma.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Jeshi la Kujenga Uchumi kuhakikisha unasimamia miongozo na sheria za usimamizi wa fedha ili kuepuka kujitokeza kwa vitendo vya uhujumu wa uchumi.

### 6.3.2.5 Kukiukwa kwa taratibu za manunuzi kwa ununuzi wa chakula cha askari wanaopangiwa lindo yenye thamani ya shilingi 1,613,055,435

Ukaguzi umebaini kuwa Jeshi la Kujenga Uchumi limefanya ununuzi wa chakula kwa ajili ya huduma kwa askari wanaopangiwa kutoa huduma ya kulinda katika vituo vyao vya malindo kupitia mtoa huduma SH TRADER AND FURMIGATION na YESS BOSS SHOP. Dosari iliyobainika katika ukaguzi ni kutokutangazwa kwa zabuni pamoja na kutokupatikana kwa makubaliano ya mkataba wa utoaji wa huduma na mzabuni huyo ambapo kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 65 cha Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshwaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016.

Aidha, katika ufuatiliaji wa mapokezi ya vyakula vilivyonunuliwa ukaguzi umeshindwa kuthibitisha uhalali wa mapokezi ya vyakula hivyo kutokana na kukosekana kwa ukaguzi hati inayothibitisha mapokezi ya chakula hicho (delivery note). Hata hivyo ukaguzi umeshindwa kupatiwa taratibu walizokubaliana na mzabuni huyo katika ulipwaji wa fedha zinazotumika katika ununuzi wa chakula hicho (Mode of payment) jambo ambalo limetia shaka juu ya matumizi ya fedha za umma na kupelekea uwepo wa viashiria vya upotevu wa fedha za umma.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wakala wa Ulinzi JKU kuhakikisha unatekeleza matakwa ya kifungu nambari 65 cha Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshwaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 34 : Kutofuatwa kwa taratibu za manunuzi**

| Hati ya Malipo | Hundi Namba | Thamani (Tshs) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 45/6/2021 | T.T | 75,130,435 | YESS BOSS | Malipo ya Chakula cha watumishi wa Jeshi la Kujenga Uchumi |
| 35/3/2021 | T.T | 82,080,000 | | |
| 1/11/2020 | T.T | 74,788,750 | SH Trader and Furmigation | |
| 27/12/2020 | T.T | 74,788,750 | | |
| 24/10/2020 | T.T | 74,788,750 | | |
| 13/8/2020 | T.T | 74,788,750 | | |
| 1/7/2020 | T.T | 74,788,750 | | |
| 1/9/2020 | T.T | 74,788,750 | | |
| 17/6/2021 | TT | 120,753,300 | Yess Boss Shop | |
| 21/5/2021 | TT | 120,753,300 | | |
| 38/4/2021 | T.T | 120,753,300 | | |
| 33/3/2021 | TISS | 120,753,300 | | |
| 6/3/2021 | TISS | 120,753,300 | | |
| 27/7/2020 | TISS | 24,660,000 | Juma Mohd Pweka | |
| 26/7/2020 | TISS | 62,113,200 | Sabaha Store | |
| 26/11/2020 | TISS | 34,060,000 | Juma Mohd Pweka | |
| 25/11/2020 | TISS | 62,113,200 | Sabaha Store | |
| 24/9/2020 | TISS | 62,113,200 | | |
| 25/12/2020 | TISS | 96,173,200 | Juma mohd pweka | |
| 20/10/2020 | TISS | 62,113,200 | Sabah Store | |
| **Jumla** | | **1,613,055,435** | | |

### 6.3.2.6 Kutofuatwa kwa taratibu za manunuzi kwa ujenzi wa Mahanga shilingi 681,136,375

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika Jeshi la Kujenga Uchumi limefanya malipo kwa msambazaji **SABAH STORE** yenye thamani ya shilingi 681,136,375 kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya ujenzi wa Mahanga mawili ya Askari na Bwalo Moja - Msaani Pemba.

Dosari iliyobainika katika ukaguzi ni kutokutangazwa kwa zabuni pamoja na kutokupatikana kwa makubaliano ya mkataba wa ununuzi wa vifaa vya ujenzi, kukosekana kwa makisio ya ujenzi (B.O.Q), kukosekana kwa taarifa za vikao (minutes),kukosekana kwa ripoti ya tathmini, kukosekana kwa taratibu za malipo (TOR) zinazoonesha namna za ulipwaji wa malipo hayo (Mode of Payment).

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 65 cha Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshwaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Jeshi la Kujenga Uchumi kuhakikisha unatekeleza miongozo inayotolewa na Serikali ikiwemo kufanya malipo kwa mujibu wa mpango wa manunuzi ili kuepusha kutumia fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo (Ujenzi wa Mahanga na Bwalo – Msaani Pemba) kinyume na utaratibu. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 35 : Kutokufuatwa kwa taratibu za manunuzi**

<table>
<tr><th>Hati namba</th><th>Hundi Namba</th><th>Aliyelipwa</th><th>Kiasi (Tshs)</th><th>Maelezo</th></tr>
<tr><td>Pv namba 5/5/2021</td><td>T.T</td><td rowspan="5">Sabah Store</td><td>204,814,500</td><td rowspan="5">Malipo kwa ajili ya gharama za vifaa vya ujenzi Kambi ya Jku Msaani</td></tr>
<tr><td>Pv namba 18/6/2021</td><td>T.T</td><td>299,940,375</td></tr>
<tr><td>Trh 17/6/2021</td><td>T.T</td><td>96,040,000</td></tr>
<tr><td>Trh 17/6/2021</td><td>T.T</td><td>49,100,000</td></tr>
<tr><td>Trh 17/6/2021</td><td>T.T</td><td>31,241,500</td></tr>
<tr><td colspan="3">Jumla</td><td>681,136,375</td><td></td></tr>
</table>

### 6.3.2.7 Kutofuatwa kwa taratibu za manunuzi kwa ujenzi wa Skuli ya Ufundi JKU Mtoni shilingi 1,683,863,274

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika Jeshi la Kujenga Uchumi limefanya malipo kwa msambazaji **SABAH STORE** yenye thamani ya shilingi 1,683,863,274 kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya ujenzi wa Skuli ya Ufundi JKU Mtoni.

Dosari iliyobainika katika ukaguzi ni kutokutangazwa kwa zabuni pamoja na kutokupatikana kwa makubaliano ya mkataba wa ununuzi wa vifaa vya ujenzi, kukosekana kwa makisio ya ujenzi (B.O.Q), kukosekana kwa taarifa za vikao (minutes),kukosekana kwa ripoti ya tathmini, kukosekana kwa taratibu za malipo (TOR) zinazoonesha namna za ulipwaji wa malipo hayo (Mode of Payment), kukosekana kwa nyaraka za mzabuni (Tender Document), kukosekana kwa ripoti ya Upembuzi yakinifu (Feasibility Study Report) pamoja na kukosekana kwa cheti cha Mshauri Elekezi (Consultance Certificate) kabla ya malipo.

Aidha ukaguzi haukuweza kuthibitisha mapokezi ya vifaa hivyo kutokana na kutokupatikana kwa daftari la kupokelea mali ghalani (Site Ledger Visit) pamoja na hati ya kupokelea vifaa (Delivery Note).

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 65 cha Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshwaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Jeshi la Kujenga Uchumi kuhakikisha unatekeleza miongozo inayotolewa na Serikali ikiwemo kufanya malipo kwa mujibu wa mpango wa manunuzi ili kuepusha kutumia fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo (Ujenzi wa Skuli ya Ufundi JKU Mtoni) kinyume na utaratibu. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 36: Kutokufuatwa kwa taratibu za manunuzi**

<table>
<tr><th>Hati ya malipo</th><th>Hundi namba</th><th>Thamani (shs)</th><th>Maelezo</th></tr>
<tr><td>--ya tarehe 28/8/2020</td><td>TISS</td><td>232,791,165</td><td>Ununuzi wa vifaa vya ujenzi wa skuli ya Ufundi Jku Mtoni, pamoja na vifaa vya Funiture Rest House Gombani Pemba.</td></tr>
<tr><td>2/4/2021 ya 30/3/2021</td><td>TISS</td><td>414,829,036</td><td rowspan="3">Ununuzi wa vifaa vya ujenzi wa shule na Jku Mtoni</td></tr>
<tr><td>--ya 13/4/2021</td><td>TISS</td><td>508,907,630</td></tr>
<tr><td>5/7/2020 ya 9/7/2020</td><td>TISS</td><td>527,335,443</td></tr>
<tr><td colspan="2">Jumla</td><td>1,683,863,274</td><td></td></tr>
</table>

#### 6.3.2.8 Kutofuatwa kwa taratibu za manunuzi ya vifaa vya ujenzi shilingi 221,492,500

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika Jeshi la Kujenga Uchumi limefanya malipo yenye thamani ya shilingi 221,492,500 kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya ujenzi pamoja na samani za nyumba ya Rest House Gombani.

Katika malipo hayo jumla ya shilingi 98,730,000 zililipwa kwa msambazaji **RASHID MOHAMMED SOUD** kwa ajili ya ununuzi wa samani kwa ajili ya nyumba ya Rest House Gombani Pemba na jumla ya shilingi 122,762,500 zililipwa kwa msambazaji **SABAH STORE** kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya ujenzi.

Dosari iliyobainika katika ukaguzi ni kutokutangazwa kwa zabuni pamoja na kutokupatikana kwa makubaliano ya mkataba wa ununuzi wa samani na vifaa vya ujenzi, kukosekana kwa makisio ya ujenzi (B.O.Q), kukosekana kwa taarifa za vikao (minutes),kukosekana kwa ripoti ya tathmini, kukosekana kwa taratibu za malipo (TOR) zinazoonesha namna za ulipwaji wa malipo hayo (Mode of Payment), kukosekana kwa nyaraka za mzabuni (Tender Document), kukosekana kwa ripoti ya Upembuzi yakinifu (Feasibility Study Report) pamoja na kukosekana kwa cheti cha Mshauri Elekezi (Consultance Certificate) kabla ya malipo.

Aidha tarehe 17/01/2022 ukaguzi ulitembelea jengo hilo la Rest House Gombani Pemba kwa lengo la kufanya uhakiki juu ya uwepo wa vifaa hivyo na kubaini kwamba hakuna kumbukumbu yoyote inayoonesha mapokezi ya vifaa hivyo.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 65 cha Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshwaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Jeshi la Kujenga Uchumi kuhakikisha unatekeleza miongozo inayotolewa na Serikali ikiwemo kufanya malipo kwa mujibu wa mpango wa manunuzi ili kuepusha kutumia fedha kinyume na utaratibu. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 37: Kutokufuatwa kwa taratibu za manunuzi**

| Hati namba | Ankara namba | Aliyelipwa | Kiasi cha fedha kilicholipwa (shs) | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| –ya tarehe 28/8/2020 | 0276 ya 24/7/2020, 0285 ya tarehe 12/6/2020, 0277 ya tarehe 27/7/2020, 0278 ya 25/7/2020, 0279 ya 23/7/2020, 0286 ya tarehe 12/6/2020. | Rashid Mohammed Soud | 98,730,000 | Ununuzi wa vifaa vya Rest house Gombani Pemba |
| –-ya 28/8/2020 | 0438 ya 10/8/2020<br>0439 ya 10/8/2020 | Sabah Store | 122,762,500 | Malipo ya ununuzi wa vifaa vya ujenzi. |
| **Jumla** | | | **221,492,500** | |

### 6.3.2.9 Kutokuwasilishwa kwa baadhi ya vifaa vyenye thamani ya shilingi 62,630,000

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika Jeshi la kujenga Uchumi Zanzibar limefanya malipo yenye thamani ya shilingi 243,617,500 tarehe 28/08/2020 kwa ajili ya ununuzi wa vifaa mbali mbali vilivyokusudiwa kutumika katika jengo la Rest House Gombani kwa mwaka wa fedha 2020/2021, ukaguzi umepitia hati za malipo hayo sambamba na Ankara husika pamoja na kufanya uhakiki wa uhalisia juu ya uwepo wa vifaa hiyo, na kubaini kwamba hadi kufikia tarehe 19/01/2022 wakati wa kufanyika ukaguzi wa mwisho na kubaini baadhi ya vifaa vyenye thamani ya shilingi 62,630,000 havikuwasilishwa kabisa katika jengo hilo kwa ajili ya matumizi husika licha ya kufanyika kwa malipo ya ununuzi wa vifaa hivyo.

Aidha hakuna taarifa yeyote iliyoripotiwa na JKU kutokana na kutowasilishwa kwa vifaa hivyo. Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kanuni ya 190 na 193 ya sheria namba 12 usimamizi wa fedha za umma ya 2005.

Ukaguzi unashauri uongozi wa JKU kuhakikisha kwamba unasimamia vizuri utekelezaji wa Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016. Mchanganuo wa vifaa hivyo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 38: Gharama za Vifaa ambavyo vimenunuliwa na havikuwasilishwa kwa ujenzi**

| Nambari ya Ankara | Msambazaji | Vifaa husika | Idadi ya Ankara | Idadi iliyopo | Thamani ya vifaa visivyo wasilishwa (shs) |
|---|---|---|---|---|---|
| 0278 ya 25/7/2020 | Rashid Mohammed Soud | Fire Extinguisher | Seti 3 | 0 | 2,550,000.00 |
| | | Vitasa vya Mlango Mkubwa | 2 | 0 | 360,000.00 |
| 0279 ya 23/7/2020t | | Air Condition 1.5 tone | 12 | 0 | 19,200,000.00 |
| | | Air Condition 2 tone | 3 | 0 | 5,400,000.00 |
| | | Heater | 11 | 9 | 900,000.00 |
| | | CCTV Camera | Seti 3 | 0 | 3,600,000.00 |
| | | TV inch 32 | 13 | 0 | 6,500,000.00 |
| | | TV inch 48 | 2 | 0 | 2,600,000.00 |
| 0286 ya 12/6/2020 | | Water Pump 1.5 | 1 | 0 | 1,200,000.00 |
| 0438 of 10/8/2020 | Sabah Store General traders | Book shelf 5 door | 1 set | 0 | 4,000,000.00 |
| | | TV inch 32 | 1 | 0 | 600,000.00 |
| | | Shoes cabin | 1 | 0 | 500,000.00 |
| | | Excutive chair | 1 | 0 | 1,500,000.00 |
| | | Excutive table | 1 | 0 | 3,200,000.00 |
| 0439 of 10/8/2020 | | Conference chairs | 50 | 41 | 3,420,000.00 |
| | | Reception Table | 2 | 0 | 3,000,000.00 |
| | | TV inch 52 | 1 | 0 | 2,500,000.00 |
| | | TV inch 32 | 8 | 6 | 1,200,000.00 |
| | | TV inch 21 | 1 | 0 | 400,000.00 |
| | | **Jumla** | | | **62,630,000** |

### 6.3.2.10 Tofauti ya taarifa ya fedha zilizoripotiwa katika hesabu ya mwisho wa mwaka na matumizi halisi shilingi 733,564,213

Katika kupitia taarifa mbali mbali zikiwemo taarifa za Hesabu ya mwaka, daftari la kurikodia kumbukumbu za fedha pamoja na taarifa za matumizi (hati za malipo). Ukaguzi umebaini kwamba baadhi ya vifungu vilivyoripotiwa katika taarifa ya Hesabu ya Mwaka vinatofautiana na taarifa za hati za malipo.

Kuwepo kwa tofauti hiyo, kunapelekea ukaguzi kushindwa kuthibitisha usahihi wa taarifa zilizoripotiwa katika ripoti ya fedha ya mwaka. Hali hiyo inapelekea taarifa ya hesabu kutotoa sura (Taswira) halisi na sahihi.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Jeshi la Kujenga Uchumi kuhakikisha kwamba wanazifanyia marekebisho taarifa zenye tofauti katika ripoti ya fedha ya mwaka ili kupata ripoti yenye kuakisi uhalisia na iliyosahihi.

**Jadweli Nambari 39 : Tofauti za taarifa Fedha.**

| Kifungu | Makario (Tshs) | Taarifa ya fedha upitia hati za malipo (Tshs) | Thamani iliyoripotiwa katika taarifa za fedha (Tshs) | Tofauti (Tshs) |
|---|---|---|---|---|
| Mafuta (Petrol na Diesel) | 400,000,000 | 191,745,000 | 203,500,000 | 11,755,000. |
| Chakula cha Askari | 867,600,000 | 1,103,319,835 | 766,740,000 | 336,579,835 |
| Ujenzi wa Majengo (Msaani na Mtoni) | 4,548,203,050 | 2,522,470,813 | 2,907,700,192 | 385,229,378 |
| **Jumla** | **5,815,803,050** | **3,817,535,648** | **3,877,940,192** | **733,564,213** |

### 6.3.2.11 Kuwepo kwa tofauti baina ya taarifa za mapato zilizoainishwa katika taarifa ya fedha ya mwaka (Annual Financial Statement) na taarifa za mapato zilizorikodiwa katika daftari la fedha taslim (cash book) shilingi 96,085,000

Katika kupitia taarifa ya fedha ya mwaka 2020/2021, ukaguzi umebaini kuwa taarifa za mapato zilizoainishwa katika taarifa ya fedha ya mwaka hazilingani na makusanyo halisi ya mapato yaliyorikodiwa katika daftari la fedha taslim.

Kuwepo kwa tofauti ya mapato halisi yaliyokusanywa na taarifa za mapato zilizoripotiwa katika taarifa ya fedha ya mwaka kunapelekea kutoa taarifa zisizo sahihi.

Uongozi wa JKU unashauriwa kuhakikisha kwamba taarifa zote za hesabu zinafungwa kwa usahihi na kwa ukamilifu. Mchanganuo wa tofauti hiyo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 40 : Tofauti ya mapato baina ya taarifa ya fedha ya mwaka na taarifa zilizorikodiwa katika daftari la fedha taslim.**

| Chanzo Cha Mapato | Makadirio | Daftari la Pesa Taslim (Cash Book) (A) (shs) | Taarifa ya Fedha ya Mwaka (B) (shs) | Tofauti (B-A) (shs) |
|---|---|---|---|---|
| Rental of cloves plantation | 5,000,000.00 | 7,179,000.00 | 200,000.00 | (6,489,000) |
| Earning from sales of horticulture | 15,000,000.00 | 67,030,000.00 | 9,525,500.00 | (55,804500) |
| Earning from livestock | 2,000,000.00 | 8,193,500.00 | 2,100,000.00 | (6,093,500) |
| Earning from sale of rice | 10,000,000.00 | 21,800,000.00 | 4,000,000.00 | (17,800,000) |
| Tution fee | 36,000,000.00 | 37,500,000.00 | 38,000,000.00 | (500,000) |
| Rent of commercial cite | 2,224,000.00 | 6,000,000.00 | 1,406,500.00 | (4,593,500) |
| Small scale industries | 15,000,000.00 | 45,159,500.00 | 9,500,000.00 | (4,804,500) |
| **Jumla** | **85,224,000** | **192,862,000** | **64,732,000** | **(96,085,000)** |

**JESHI LA KUJENGA UCHUMI - PEMBA**

### 6.3.2.12 Hati za malipo zenye vielelezo pungufu shilingi 12,000,000

Ukaguzi umebaini kwamba jumla ya shilingi 12,000,000 zimetumika kwa matumizi mbalimbali ya Jeshi la Kujenga Uchumi Pemba lakini baadhi ya vielelezo havikuambatanishwa na hati za malipo ili kuweza kuthibitisha uhalali wa malipo hayo.

Kutokuambatanisha vielelezo katika hati za malipo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 34(1) cha Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 41 : Hati za malipo zenye vielelezo pungufu**

| Hati Namba | Hundi Namba | Kiasi cha fedha kilicholipwa (Tshs.) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 20/10 ya 20/10/2020 | 678053 | 3,000,000 | Kamanda wa JKU-Pemba | Malipo ya fedha kwa ajili ya huduma mbali mbali za chakula |
| 16/12 ya 16/12/2020 | 678094 | 3,000,000 | | |
| 12/12 ya 12/12/2020 | 678090 | 6,000,000 | | |
| **Jumla** | | **12,000,000** | | |

### 6.3.2.13 Bidhaa ambazo hazikurikodiwa katika daftari la ghalani shilingi 4,343,100

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwa jumla ya shilingi 4,343,100 zimetumika kwa ununuzi wa bidhaa mbali mbali dosari iliyobainika katika ukaguzi ni kutokurikodiwa kwa manunuzi hayo katika daftari la kumbu kumbu la ghalani ili kuweza kuthibitisha uhalali wa mapokezi pamoja na matumizi ya bidhaa hizo.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 42: Bidhaa ambazo hazikurikodiwa katika daftari la ghalani**

| Hati Namba | Hundi Namba | Kiasi cha fedha kilicholipwa (Tshs.) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 2/9 ya 25/9/2020 | 01101 | 193,100 | Kamanda JKU-Pemba | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa mafuta ya Diesel lita 100 |
| 01/07 ya 01/07/2020 | 077989 | 650,000 | | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa mafuta ya Petrol lita 170.9 pamoja na ununuzi wa chakula. |
| 4/12 ya 4/12/2020 | 678085 | 2,500,000 | | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa mafuta ya Diesel lita 600 |
| 9/10 ya 9/10/2020 | 678046 | 1,000,000 | | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa mafuta ya Petrol lita 300 |
| **Jumla** | | **4,343,100** | | |

### 6.3.2.14 Uhamisho wa kikazi kwa wapiganaji wa Jeshi la Kujenga Uchumi (JKU) Pemba

Kwa mujibu wa kifungu nambari 89(1)(2)(3) cha Kanuni ya Utumishi wa Umma ya mwaka 2014 kinatoa maelekezo kwa mtumishi yoyote atakaepewa uhamisho kutoka Unguja kwenda Pemba, Tanzania Bara au kinyume chake atapaswa kulipwa Posho la Usumbufu litakalokuwa sawa na posho la siku saba pamoja na usafiri wa ndani wa kufidia usumbufu atakao upata katika kutekeleza amri hiyo ya uhamisho. Aidha, kwa madhumuni ya kifungu kidogo cha kwanza na cha pili ya kanuni hii mtumishi huyo atastahiki kugharamiwa uhamishaji wa familia na mizigo yake.

Kwa mujibu wa kifungu nambari 60(g) cha Kanuni ya Tume ya Utumishi ya Idara Maalum za SMZ kinaeleza "Posho la usumbufu ambalo litafungamana na uhamisho wa kutoka Unguja kwenda Pemba au kinyume chake la asilimia 25 ya mshahara".

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Kikosi cha JKU Pemba kimefanya uhamisho wa kikazi kwenda Unguja kwa wapiganaji wake mbali mbali, dosari ya kiutumishi iliyobainika ni kutokutekelezeka kwa vifungu nilivyoviainisha hapo juu kutokana na kukosekana kwa vielelezo mbali mbali vilivyothibitisha upokeaji wa stahiki za malipo yatokanayo na shughuli ya uhamishaji wa familia na mizigo kwa mujibu wa utaratibu.

Kuwakosesha stahiki za uhamisho kwa wapiganaji hao kunaweza kupelekea kupunguza hamasa ya ufanyaji wa kazi na hatimae kujitokeza kwa malalamiko ya chini kwa chini ambayo hupelekea kuondoa imani kwa wakuu wa Vikosi vya ulinzi na Usalama.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Vikosi vya Ulinzi na Usalama kuhakikisha unatekeleza kikamilifu maagizo ya kanuni za Utumishi wa Umma pamoja na kanuni za Idara Maalum za Vikosi vya SMZ kwa lengo la kuondosha migongano na migogoro kwa wapiganaji makazini. Mchanganuo wa wapiganaji hao ni kama unavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 43 :Orodha ya wapiganaji waliohamishwa kikazi bila ya kufanyiwa malipo**

| Namba | Jina la Mpiganaji | Namba | Jina la Mpiganaji |
|---|---|---|---|
| 1 | Zainab Omar Haji | 17 | Haji Bakar Yussuf |
| 2 | Hada Diwani Juma | 18 | Jadidi Rehani Hassan |
| 3 | Mwajuma Machano Juma | 19 | Khamis Moh'd Abdalla |
| 4 | Ngwali Khamis Ngwali | 20 | Machano Shangama Khamis |
| 5 | Haji Makame Haji | 21 | Mbaraka Kombo Saleh |
| 6 | Moh'd Juma Ali | 22 | Mtumwa Saleh Amour |
| 7 | Nasra Abdu Kassim | 23 | Ngwali Machano Ngwali |
| 8 | Jaffar Khamis Juma | 24 | Moh'd Juma Mussa |
| 9 | Juma Mussa Usi | 25 | Murid Soud Khamis |
| 10 | Hasnuu Hassan Juma | 26 | Moh'd Abdulla Moh'd |
| 11 | Nassra Kassim Moh'd | 27 | Moh'd Mussa Machano |
| 12 | Husna Yakoub Khamis | 28 | Sebastin James Maziku |
| 13 | Khamis Rajab Khamis | 29 | Ibrahim Mora Ali |
| 14 | Ali Msaji Ali | 30 | Mshenga Haji Makame |
| 15 | Muhamad Juma Hussein | 31 | Omar Haji Abass |
| 16 | Ame Khamis Juma | | |

### 6.3.2.15 Malipo kwa watoa huduma ambao hawakusajiliwa na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma shilingi 15,487,640

Kwa mujibu wa kifungu cha 23(1) cha Sheria ya Manunuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma kinaeleza kulingana na masharti ya sheria hii mtu, kampuni au taasisi haitawasilisha zabuni au vyenginevyo kushiriki katika manunuzi ya Umma isipokua chombo kiwe kimesajiliwa na Mamlaka ya Manunuzi.

Kwa mujibu wa kifungu cha 23(2), zabuni kutoka kwa mtu, kampuni au chombo ambacho hakijasajiliwa haifai na hakitazingatiwa na taasisi ya ununuzi.

Ukaguzi umebaini kwamba Jeshi la Kujenga Uchumi Pemba limefanya manunuzi na watoa huduma mbali mbali ambao hawakusajiliwa na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya Zanzibar.

Kufanya hivyo kunapelekea kuikosesha Serikali mapato ambapo ni kwenda kinyume na Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 44 : Watoa huduma ambao hawakusajiliwa na Mamlaka ya ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma**

| Hati Namba | Hundi Namba | Kiasi cha fedha kilicholipwa (Tshs.) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 02/10 05/10/2020 | 001106 | 458,759 | Abdalla Anasi Ali | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa chakula. |
| 02/11 04/11/2020 | 001122 | 227,000 | Rashid Mohammed Soud | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya umeme |
| 03/11 04/11/2020 | 001123 | 455,337 | Abdalla Anasi Ali | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa chakula. |
| 11/11 27/11/2020 | 001131 | 158,000 | | |
| 01/12 08/12/2020 | 001134 | 876,453 | | |
| 04/01 05/01/2021 | 001147 | 347,919 | | |
| **Jumla** | | **2,523,468** | | |

### 6.3.2.16 Kukosekana kwa taarifa za mapato yatokanayo na uzalishaji wa mazao mbali mbali

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika Jeshi la Kujenga Uchumi Pemba linamiliki maeneo mbali mbali ya uzalishaji yenye ukubwa wa ekari zipatazo 913 ambapo maendeleo hayo hutumiwa kwa ajili ya kilimo cha mazao ikiwemo mpunga, muhogo, mahindi, minazi, mbogamboga na kunde.

Ukaguzi umebaini Jeshi la Kujenga Uchumi mara baada ya mavuno hufanya uuzaji wa mazao hayo kwa taasisi mbali mbali pamoja na watu binafsi kwa lengo la kujipatia kipato kwa ajili ya shughuli za uendeshaji wa kikosi hicho.

Dosari iliyobainika katika ukaguzi ni kukosekana kwa taarifa na kumbukumbu zinazobainisha mapato halisi yaliyopatikana yanayotokana na mauzo ya bidhaa hizo jambo ambalo linapelekea kutia shaka juu ya uhalali wa matumizi ya fedha ya mapato hayo ambapo haijulikani kima halisi cha fedha kilichopatikana pamoja na kile kilichotumika na shughuli iliyopelekea kutumika kwa mapato hayo jambo ambalo hupelekekea viashiria vya upotevu wa fedha za umma.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyime na Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 45 : Kukosekana kwa taarifa za mapato yatokanayo na uzalishaji wa mazao mbali mbali**

| Namba | Jina la Kambi | Miradi uliofanyika |
|---|---|---|
| 1 | Chokocho | Ufugaji wa kuku wa kisasa |
| | | Ufugaji wa kuku wa kienyeji |
| 2 | Mwambe | Ufugaji wa samaki |
| 3 | Chambani | Ufugaji wa ngombe |
| | | Kilimo cha mbogamboga |
| 4 | Pujini | Kilimo cha mbogamboga |
| 5 | Kwa pweza | Kilimo cha mpunga wa kutegemea mvua |
| | | Kilimo cha mbogamboga |
| | | Ufugaji wa kuku wa kisasa |
| 6 | Ngezi | Uatikaji wa miche ya minazi |
| | | Kilimo cha mbogamboga |
| | | Kilimo cha viazi vitamu |
| | | Kilimo cha njugu nyasa |
| | | Ufugaji wa kuku wa kienyeji |
| 7 | Msaani | Kilimo cha mpunga wa kutegemea mvua |
| | | Kilimo cha muhogo |
| | | Kilimo cha kunde |
| | | Kilimo cha mbogamboga |

### 6.3.2.17 Bidhaa ambazo hazikuingizwa kwenye daftari la ghalani shilingi 4,772,000

Ukaguzi umebaini kwamba jumla ya shilingi 4,772,000 zimetumika kwa ununuzi wa bidhaa mbali mbali dosari iliyobainika katika ukaguzi ni kutokuingizawa bidhaa hizo kwenye daftari la ghalani ili kuweza kuthibitisha uhalali wa mapokezi pamoja na matumizi yake.

Kutokuingizwa bidhaa katika daftari la kutunzia vifaa vya ghalani ni kwenda kinyume na kifungu cha 123(i) (ii) cha kanuni ya sheria ya utumishi wa Umma ya mwaka 2014 ya Zanzibar pamoja na Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016. Mchanganuo huo wa bidhaa hizo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 46 : Bidhaa ambazo hazikuingizwa kwenye daftari la ghalani**

| Hati Namba | Hundi Namba | Kiasi cha fedha kilicholipwa (Tshs.) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 08/10 16/10/2020 | 001113 | 2,000,000 | Mkuu wa Miradi ya JKU Pemba | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa Petrol lita 52 |
| 09/10 20/10/2020 | 001114 | 959,000 | Chake Petrol Station | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa Diesel lita 500 |
| 11/10 23/10/2020 | 001116 | 740,000 | Mkuu wa Miradi ya JKU Pemba | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya magari. |
| 05/11 18/11/2020 | 001125 | 200,000 | | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa kuku |
| 07/11 19/11/2020 | 001127 | 873,000 | | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa pembejeo. |
| **Jumla** | | **4,772,000** | | |

### 6.3.3 WAKALA WA ULINZI JKU (SGA)

Ukaguzi wa hesabu za mwaka 2020/2021 kwa Wakala wa Ulinzi JKU umefanywa kwa mujibu wa Sheria, kanuni, taratibu pamoja na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Taarifa ya Mapato**

Wakala wa Ulinzi wa JKU ilikadiriwa kukusanya jumla ya shilingi 3,157,700,000 kwa mwaka wa fedha 2020/2021. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 Wakala ilikusanya jumla ya shilingi 1,869,650,110 sawa na asilimia 59.2 ya makadirio.

**Taarifa ya Matumizi**

Wakala wa Ulinzi wa JKU kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ilikadiriwa kutumia jumla ya shilingi 2,316,050,000 kwa matumizi ya kazi za kawaida. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 jumla ya shilingi 1,876,584,907.95 zimetumika kwa kazi za kawaida sawa na asilimia 81 ya makadirio.

**MATOKEO NA MAPENDEKEZO YA UKAGUZI**

#### 6.3.3.1 Kutumika kwa stakabadhi za malipo zisizokuwa za Serikali

Katika kupitia stakabadhi za malipo zinazotolewa na wakala kwa wateja wake waliopatiwa huduma za ulinzi. Ukaguzi umebaini kuwepo kwa makusanyo yenye jumla ya shilingi 1,719,265,110.28 ambayo yamekusanywa kupitia stakabadhi zilizotengenezwa na kutolewa na Wakala wa Ulinzi kwa ajili ya huduma ya ukusanyaji wa mapato. Dosari iliyobainika na ukaguzi ni kukosekana kwa idhini ya matumizi ya stakabadhi hizo kutoka kwa mlipaji Mkuu wa Serikali. Kutumia stakabadhi ambazo hazikuthibitishwa na Serikali inapelekea kuikosesha Serikali mapato yatokanayo na uuzwaji wa stakabadhi hizo. Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 65 (1) cha Kanuni ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2021.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wakala wa Ulinzi kuhakikisha matumizi yote ya stakabadhi yanayotumika yanapata ruhusa kutoka kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali kwa lengo la kuipatia mapato Serikali.Mchanganuo wa stakabadhi na mapato hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 47 : Malipo yanayotokana na Stakabadhi za Wakala wa Ulinzi**

| Namba | Stakabadhi | Thamani (Tshs.) |
|---|---|---|
| 1. | 00817-00850 | 120,526,000.00 |
| 2. | 00851-00900 | 164,251,690.29 |
| 3. | 00901-00950 | 156,100,000.00 |
| 4. | 00951-01000 | 147,228,200.00 |
| 5. | 01001-01050 | 146,140,557.14 |
| 6. | 01051-01100 | 175,760,000.00 |
| 7. | 01101-01150 | 181,785,771.43 |
| 8. | 01151-01200 | 147,156,457.14 |
| 9. | 01201-01250 | 183,746,857.14 |
| 10. | 01251-01300 | 138,062,857.14 |
| 11. | 01301-01326 | 158,506,720.00 |
| **Jumla** | | **1,719,265,110.28** |

### 6.3.3.2 Matumizi ya ziada na makadirio shilingi 299,965,434

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika Wakala wa Ulinzi imefanya manunuzi yenye thamani ya shilingi kwa ajili ya matumizi mbali mbali ya uendeshaji wa kazi za ofisi.

Kwa mujibu wa kifungu nambari 32(2) cha Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016 Taasisi za umma zinatakiwa kupanga makadirio ya mapato na matumizi na kupata uthibitisho wa matumizi ya mapato hayo kutoka katika vikao vya Bodi au kuidhinishwa na Mlipaji Mkuu wa Serikali, dosari iliyobainika katika ukaguzi ni kwamba kutokuwepo kwa Bodi inayosimamia shughuli za wakala imepelekea kutumika kwa fedha za ziada kinyume na makadirio ya mapato hayo jambo ambalo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 32(2) cha Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wakala wa Ulinzi JKU kufanya mawasiliano ya karibu na Waziri mwenye dhamana kwa lengo la kumpendekeza Mwenyekiti wa Bodi ambae atateuliwa na Mheshimiwa Rais kwa lengo la kusimamia mapato na matumizi yatokanayo na taasisi hiyo. Mchanganuo wa matumizi hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 48 : Matumizi ya ziada na Makadirio**

| Mahitaji | Makadirio (Tshs.) | Matumizi halisi (Tshs.) | Tofauti (Tshs.) |
|---|---|---|---|
| Ununuzi wa mafuta (ulinzi) | 162,000,000 | 341,645,934 | -179,645,934 |
| Ununuzi wa chakula | 98,900,000 | 204,502,500 | -105,602,500 |
| Service za magari | 42,700,000 | 57,417,000 | -14,717,000 |
| **Jumla** | **303,600,000** | **603,565,434** | **-299,965,434** |

#### 6.3.3.3 Kukosekana kwa barua za uhaulishaji wa vifungu (Realocation)

Ukaguzi umebaini kwamba Wakala wa Ulinzi imefanya matumizi mbalimbali ambayo yamevuka kiwango halisi cha makadirio yaliyopangwa na kutumia, dosari iliyobainikka katika ukaguzi ni kufanyika kwa uhaulishaji wa fedha kutoka katika vifungu mbali mbali vya matumizi bila ya kuwepo kwa vielelezo vya ruhusa kutoka kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali jambo ambalo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 20 (1) (2) (3) cha Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wakala wa Ulinzi JKU kuhakikisha unafuata na kuzingatia misingi ya uhalishaji kwa lengo la kuweka wazi matumizi na hatimae kuleta tija iliyokusudiwa. Mchanganuo wa matumizi hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 49 : Kukosekana kwa taratibu za uhaulishaji**

| Mahitaji | Makadirio (Tshs.) | Matumizi halisi (Tshs.) | Tofauti (Tshs.) |
|---|---|---|---|
| Chakula cha walinzi | 98,900,000, | 204,502,500 | -105,602,500 |
| Ununuzi wa mafuta | 162,000,000 | 341,645,934 | -179,645,934 |
| Service za magari | 42,700,000 | 57,417,000 | -14,717,000 |
| Ujenzi wa Mahanga | - | 16,549,000 | 16,549,000 |
| **Jumla** | | | **316,514,434** |

#### 6.3.3.4 Kukosekana kwa muongozo wa ulipaji wa posho kwa wakuu wa maidara yenye jumla ya shilingi 27,330,000

Katika kupitia hati mbali mbali za malipo pamoja na daftari la fedha, ukaguzi umebaini kwamba wakala wa ulinzi amekuwa akifanya malipo kwa wakuu wa maidara na watendaji kupitia hesabu 0400001000. Ukaguzi umebaini kwamba hakuna toleo au kibali kilichoruhusu ulipwaji wa Posho hizo kwa mujibu wa miongozo ya utumishi wa umma. Kukosekana kwa miongozo ya ulipwaji wa posho kunaweza kupelekea wakala kutumia fedha za umma kinyume na utaratibu. Kufanya hivyo kunaweza kupelekea kuitia hasara Serikali.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wakala wa Ulinzi JKU kufanya ufuatiliaji wa upatikanaji wa ruhusa ya malipo au kumuandikia Waziri mwenye dhamana kuweza kuliwasilisha suala hilo katika kikao cha Baraza la Mapinduzi kwa lengo la kuomba idhini ya Matumizi hayo. Baadhi ya hati hizo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 50 : Hati za malipo zilozotumika kuwalipa wakuu wa idara na walinzi posho mbali mbali**

| Tarehe | Hati ya malipo | Jumla ya fedha kwa mujibu wa hati ya malipo (Tshs.) | Thamani ya posho inayolipwa kwa walinzi, vijana na Wakuu wa Idara (Tshs.) | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 23/06/2021 | PV. 33 | 57,390,000 | 1,500,000 | Malipo kwa ajili ya posho la walinzi, vijana pamoja na posho la wakuu wa maidara. |
| 01/12/2020 | PV. 02 | 40,000,000 | 3,450,000 | |
| 02/10/2020 | PV. 02 | 42,950,000 | 3,350,000 | |
| 29/12/2020 | PV. 29 | 41,100,000 | 3,850,000 | |
| 02/09/2020 | PV. 01 | 44,950,000 | 3,200,000 | |
| 29/04/2021 | PV. 36 | 56,750,000 | 4,090,000 | |
| 28/05/2021 | PV. 28 | 58,960,000 | 4,140,000 | |
| 24/10/2020 | PV. 21 | 10,000,000 | 3,750,000 | |
| **Jumla** | | **352,100,000** | **27,330,000** | |

### 6.3.3.5 Kukosekana kwa mikataba ya ununuzi wa mafuta wenye jumla ya shilingi 341,645,934

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika Wakala wa Ulinzi imefanya matumizi mbali mbali kwa ajili ya ununuzi wa mafuta ya uendeshaji wa shughuli za wakala kutoka kampuni ya IJITIMAI PETROL STATION na MAP OIL, dosari iliyobainika katika ukaguzi ni kutokuwepo kwa makubaliano ya mikataba midogo midogo inayotoa uhalali wa matumizi hayo.

Kutokuwepo kwa makubaliano ya mikataba midogo midogo kunaweza kukatia dosari upande wowote wa makubaliano pale ambapo itakapobainika dosari za kiutendaji na mmoja kati ya wawili atakapoamua kuvunja makubaliano hayo jambo ambalo linaweza likapelekea kupelekana katika vyombo vya Sheria na kutoa haki isiyostahiki kwa upande mmoja.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wakala wa Ulinzi JKU kuhakikisha matumizi yoyote yatakayovuka shilingi 15,000,000 ni vyema kuandikishiana mikataba ya makubaliano kwa mujibu wa matakwa ya kifungu nambari 29(m) cha Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshwaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016. Mchanganuo wa matumizi hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 51 : Kukosekana kwa mikataba ya ununuzi wa mafuta**

| Hati namba | Hundi namba | Aliyelipwa | Thamani (Tshs) | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 1/4/2021 | T.T | Ijitimai Petrol Station | 15,000,000 | Ununuzi wa mafuta kwa matumizi ya ofisi ya wakala wa ulinzi Jku |
| 4/5/2021 | T.T | | 15,000,000 | |
| 2/9/2020 | 000041 | Map Oil | 7,000,000 | |
| 1/9/2020 | 000040 | | 10,000,000 | |
| 1/8/2020 | 000037 | | 25,000,000 | |
| 4/10/2020 | 00046 | | 14,000,000 | |
| 1/10/2020 | 000042 | | 17,500,000 | |
| 1/3/2021 | T.T | Ijitimai petrol statement | 12,000,000 | |
| 1/2/2021 | T.T | | 15,000,000 | |
| 12/6/2021 | T.T | | 2,148,000 | |
| 15/6/2021 | T.T | | 15,000,000 | |
| 19/6/2021 | T.T | | 15,000,000 | |
| 39/6/2021 | T.T | | 15,000,000 | |
| 14/5/2021 | T.T | | 15,000,000 | |
| 18/4/2021 | T.T | | 15,000,000 | |
| 28/3/2021 | T.T | | 15,000,000 | |
| 20/3/2021 | T.T | | 14,000,000 | |
| 13/12/2020 | T.T | | 6,000,000 | |
| 27/1/2021 | T.T | | 13,000,000 | |
| 14/1/2021 | T.T | | 13,000,000 | |
| 27/12/2020 | 000730 | | 8,000,000 | |
| 26/12/2020 | 000731 | | 5,000,000 | |
| 14/12/2020 | 000717 | | 5,997,934 | |
| 18/11/2020 | 000694 | Map Oil | 15,000,000 | |
| 21/9/2020 | 000653 | | 10,000,000 | |
| 9/9/2020 | 000641 | | 5,000,000 | |
| 10/8/2020 | 000623 | | 12,500,000 | |
| 23/7/2020 | 000606 | | 11,500,000 | |
| **Jumla** | | | **341,645,934** | |

### 6.3.3.6 Kutofuatwa kwa taratibu za manunuzi kwa ununuzi wa chakula cha Askari shilingi 214,377,500

Ukaguzi umebaini kuwa Wakala wa ulinzi umefanya ununuzi wa chakula kwa ajili ya huduma kwa askari wanaopangiwa kutoa huduma ya kulinda katika vituo vyao vya malindo kupitia mtoa huduma YES BOSS SHOP . Dosari iliyobainika katika ukaguzi ni kutokutangazwa kwa zabuni pamoja na kutokupatikana kwa makubaliano ya mkataba wa utoaji wa huduma na mzabuni huyo ambapo kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 65 cha Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshwaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016.

Aidha, katika ufuatiliaji wa mapokezi ya vyakula vilivyonunuliwa ukaguzi umeshindwa kuthibitisha uhalali wa mapokezi ya vyakula hivyo kutokana na kukosekana kwa ukaguzi hati inayothibitisha mapokezi ya chakula hicho (delivery note). Hata hivyo ukaguzi umeshindwa kupatiwa taratibu walizokubaliana na mzabuni huyo katika ulipwaji wa fedha zinazotumika katika ununuzi wa chakula hicho (Mode of payment) jambo ambalo limetia shaka juu ya matumizi ya fedha za umma na kupelekea uwepo wa viashiria vya upotevu wa fedha za umma.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wakala wa Ulinzi JKU kuhakikisha unatekeleza matakwa ya kifungu nambari 65 cha Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshwaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 52 : Kutofuatwa kwa taratibu za manunuzi**

| Hati ya malipo | Hundi Namba | Thamani (Tshs) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 2/3/2021 | 000793 | 7,500,000 | Yess Boss Shop | Ununuzi wa chakula kwa walinzi wa wakala |
| 4/2/2021 | 000050 | 5,000,000 | | |
| 2/6/2021 | T.T | 7,700,000 | | |
| 20/6/2021 | T.T | 7,700,000 | | |
| 40/6/2021 | T.T | 11,500,000 | | |
| 24/5/2021 | 000861 | 8,000,000 | | |
| 16/4/2021 | T.T | 7,500,000 | | |
| 23/4/2021 | T.T | 1,857,500 | | |
| 34/4/2021 | T.T | 10,487,000 | | |
| 25/3/2021 | T.T | 7,500,000 | | |
| 18/3/2021 | T.T | 7,500,000 | | |
| 15/2/2021 | T.T | 7,500,000 | | |
| 8/2/2021 | 000773 | 7,500,000 | | |
| 15/1/2021 | 000753 | 7,500,000 | | |
| 2/1/2021 | 000740 | 7,500,000 | | |
| 19/12/2020 | 000721 | 7,500,000 | | |
| 19/11/2020 | 000693 | 7,000,000 | | |
| 5/11/2020 | 000680 | 5,229,000 | | |
| 4/11/2020 | 000679 | 5,000,000 | | |
| 19/10/2020 | 000675 | 6,500,000 | | |
| 10/10/2020 | 000660 | 5,500,000 | | |
| 17/9/2020 | 000648 | 7,600,000 | | |
| 4/9/2020 | 000637 | 7,600,000 | | |
| 17/8/2020 | 000651 | 5,000,000 | | |
| 5/8/2020 | 000618 | 8,000,000 | | |
| 6/7/2020 | 000587 | 7,000,000 | | |
| **Jumla Ndogo** | | **204,502,500** | | |
| 27/6/ 2021 | 000886 | 1,061,600 | Khamis Othman khamis | Ununuzi wa mikate ya walinzi |
| 6/5/2021 | 000848 | 692,200 | | |
| 6/4/2021 | 000818 | 1,000,000 | | |
| 3/3/2021 | 000796 | 915,200 | | |
| 1/2/2021 | 000769 | 984,000 | | |
| 9/12/2020 | 000710 | 940,000 | | |
| 28/12/2020 | 000733 | 831,000 | | |
| 1/10/2020 | 000656 | 928,000 | | |
| 7/9/2020 | 000640 | 853,000 | | |
| 3/8/2020 | 000619 | 835,000 | | |
| 4/7/2020 | 000588 | 835,000 | | |
| **Jumla Ndogo** | | **9,875,000** | | |
| **Jumla Kuu** | | **214,377,500** | | |

### 6.3.3.7 Matumizi yenye vielelezo pungufu shilingi 27,500,000

Ukaguzi umebaini kwamba jumla ya shilingi 27,500,000 zimetumika kwa matumizi mbalimbali ya Wakala wa ulinzi JKU , dosri iliyobainika ni kwamba baadhi ya vielelezo havikuambatanishwa na hati za malipo ili kuweza kuthibitisha uhalali wa malipo hayo.

Kutokuambatanisha vielelezo katika hati za malipo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 34(1) cha Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 53 : Matumizi yenye vielelezo pungufu**

| Hati namba | Hundi namba | Kiasi cha fedha kilicholipwa (Tshs.) | Aliyelipwa | Maelezo | Mapungufu |
|---|---|---|---|---|---|
| 1/5/2021 | 000055 | 7,500,000 | Visiwani general supplier | Ununuzi wa makoti ya mvua. | Kukosekana kwa Delivery note |
| 1/5/2021 | 000053 | 5,000,000 | | | Kukosekana kwa invoice na delivery note |
| 2/5/2021 | 000054 | 5,000,000 | | | Kukosekana kwa Delivery note |
| 26/6/2021 | 000890 | 5,000,000 | Central trading Co. | Ununuzi wa kitambaa vya uniform | |
| 25/6/2021 | 000889 | 5,000,000 | | | |
| **Jumla** | | **27,500,000** | | | |

### 6.3.4 FUNGU D 03 – CHUO CHA MAFUNZO

Ukaguzi wa hesabu za mwaka wa fedha 2020/2021 kwa Chuo cha Mafunzo umefanywa kwa mujibu wa Sheria, kanuni, taratibu pamoja na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Taarifa ya Mapato**

Katika kipindi cha mwaka 2020/2021 Chuo cha Mafunzo kilikadiriwa kukusanya jumla ya shilingi 75,720,000 kutoka katika vyanzo mbalimbali vya mapato. Hadi kufikia tarehe 30 Juni 2021 Chuo cha Mafunzo kilikusanya jumla ya shilingi 41,704,000 sawa na asilimia 55 ya makadirio.

**Taarifa ya Matumizi**

Katika kipindi cha mwaka 2020/2021 Chuo cha Mafunzo kilikadiriwa kutumia jumla ya shilingi 21,833,600,000 . Kati ya hizo shilingi 20,333,600,000 zilipangwa kutumika kwa ajili ya kazi za kawaida na shilingi 1,500,000,000 kwa kazi za maendeleo.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 Kikosi cha Mafunzo kiliingiziwa jumla ya shilingi 18,303,767,139 sawa na asilimia 83.83 ya makadirio . Kati ya fedha hizo shilingi 18,053,767,139 zilitumika kwa matumzi ya kazi za kawaida sawa na asilimia 88.79 ya makadirio na na shilingi 250,000,000 zilitumika kwa kazi za maendeleo sawa na asilimia 16.67 ya makadirio.

**MATOKEO NA MAPENDEKEZO YA UKAGUZI**

### 6.3.4.1 Matumizi ya Masurufu (imprest) ambayo hayana marejesho shilingi 10,000,000

Ukaguzi umebaini kuwa jumla ya shilingi 10,000,000 za mapato amelipwa Kamishna Chuo cha Mafunzo kupitia hati nambari 7/4/2021 ya tarehe 12/4/2021, ikiwa ni masurufu kwa ajili ya matumizi madogo madogo ya Chuo, dosari iliyobainika katika ukaguzi ni kutokupatikana kwa marejesho ya matumizi ili kuweza kuthibitisha uhalali wa malipo hayo.

Kutoambatanisha vielelezo vya malipo husika ni kwenda kinyume na kanuni ya fedha kifungu namba 95 ya 2005 na Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Chuo cha Mafunzo kuhakikisha marejesho ya matumizi yaliyokosekana pamoja na vielelezo vyake vinaambatanishwa na hati za malipo kwa ajili ya ukaguzi.

### 6.3.4.2 Malipo yasiyozingatia ushindani wa bei shilingi 32,140,500

Ukaguzi umebaini Chuo cha Mafunzo kimetumia jumla ya shilingi 32,140,500 za mapato kwa ajili ya kupata huduma pamoja na manunuzi ya vifaa mbalimbali, dosari iliyobainika ni kutokuwepo kwa ushindani wa bei jambo ambalo linaweza kupelekea kufanyika kwa malipo ya bei ya juu ukilinganisha na uhalisia wa mahitaji yanavyopatikana kwa bei ya sokoni.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Chuo cha Mafunzo kuhakikisha unafanya matumizi kwa kuzingatia matakwa ya kanuni na sheria za fedha ili kuepuka kujitokeza kwa viashiria vya upotevu wa fedha. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 54 : Malipo yasiyozingatia ushindani wa bei**

| Hati namba | Tarehe | Aliyelipwa | Thamani (Tshs) | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 1/11/2020 | 13/11/2020 | Duka chuo Cha Mafunzo | 2,558,000 | Ikiwa ni ununuzi wa vifaa vya ushoni. |
| 1/8/2020 | 3/8/2020 | | 1,750,000 | Ikiwa ni malipo ya ununuzi wa computer. |
| 2/12/2020 | 3/12/2020 | | 4,000,000 | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya vifaa vya ujenzi. |
| 6/12/2020 | 10/12/2020 | | 1,000,000 | |
| 8/12/2020 | 14/12/2020 | | 2,100,000 | |
| 9/12/2020 | 15/12/2020 | | 1,250,000 | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya uunuzi wa vifaa vya usafi. |
| 2/3/2021 | 8/3/2021 | | 1,030,000 | Ikiwa ni manunuzi ya vifaa vya kufekea majani uwanja wa ndege |
| 4/3/2021 | 8/3/2021 | | 1,150,000 | Ikiwa ni manunuzi ya mipira ya gari. |
| 5/3/2021 | 11/3/2021 | | 1,452,000 | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya ujenzi kujenga mitaro na makaro gerezani |
| 6/4/2021 | 12/4/2021 | | 6,000,000 | Ikiwa ni ununuzi wa saruji. |
| 10/4/2021 | 16/4/2021 | | 7,950,000 | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya vifaa vya matumizi ya ramadhani |
| 9/4/2021 | 14/4/2021 | | 1,900,500 | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya ununuzi wa mbao na miti. |
| **Jumla** | | | **32,140,500** | |

### 6.3.4.3 Kutokatwa kwa Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) inayotokana na ununuzi na utoaji wa huduma shilingi 373,193,601

Ukaguzi ulipitia hati mbalimbali zinazohusiana na malipo na kubaini kuwepo kwa hati za malipo zinazohusiana na manunuzi na utoaji wa huduma zenye thamani ya shilingi 373,193,601 ambazo zilistahiki kukatwa kodi ya ongezeko la thamani ya shilingi 58,918,643.

Dosari iliyobainika katika ukaguzi ni kutokukatwa kodi ya ongezeko la thamani na kuziwasilisha katika ofisi inayohusiana na mapato kwa mujibu wa sheria. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 55 : Kutokatwa kwa Kodi ya Ongezeko la Thamani**

| Hati namba | Ankara namba | Aliyelipwa | Thamani (Tshs) | VAT (15%) |
|---|---|---|---|---|
| 1/7/2020 | 0423 | Sabah Store | 48,821,450 | 7,704,150 |
| 6/8/2020 | 0435 | | 56,502,500 | 8,919,281.25 |
| 3/9/2020 | 0444 | | 53,454,960 | 8,440,260 |
| 19/10/2020 | 0604 | | 71,542,291 | 11,296,151 |
| 1/11/2020 | 0615 | | 79,049,500 | 12,481,500 |
| 21/12/2020 | 0623 | | 63,822,900 | 10,077,300 |
| **Jumla** | | | **373,193,601** | **58,918,642.25** |

Chuo cha Mafunzo kushindwa kukata kodi ya ongezeko la thamani kunapelekea kuikosesha Serikali mapato hali inayosababisha kutofikiwa kwa malengo yaliopangwa katika mpango mkakati wa Taasisi zinazosimamia kodi na Serikali ambapo kufanya hivyo ni ukiukwaji wa sheria, kanuni na miongozo ya kodi iliyowekwa.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Chuo cha Mafunzo kuhakikisha unasimamia suala zima la ukataji wa kodi ya ongezeko la thamani kwa kila manunuzi au huduma zinazotolewa ili kwenda sambamba na sheria ya kodi.

### 6.3.4.4 Malipo yaliyolipwa kinyume na utaratibu shilingi 130,844,030

Ukaguzi umebaini kwamba jumla ya shilingi 130,844,030 amelipwa Kamishna Chuo cha Mafunzo kwa ajili ya malipo ya watoa huduma mbalimbali badala ya kufanya malipo ya moja kwa moja kwa wahusika kama taratibu za fedha zinavyoelekeza. Kutokufanya malipo moja kwa moja kwa mtoa huduma kupitia hesabu yake (bank account) kunaweza kupelekea upotevu wa fedha za umma na kuikosesha Serikali mapato yatokanayo na kodi. Aidha ukaguzi umeshindwa kuthibitisha kuwa malipo hayo yamelipwa kwa njia ya hundi au fedha taslim kutokana na kutorikodiwa kumbukumbu za malipo zilizonakikiliwa katika vishina vya hundi au kuoneshwa katika hati za malipo jambo ambalo ukaguzi umetia shaka juu ya kufanyika kwa malipo hayo kwa watoa huduma hao.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Chuo cha Mafunzo uhakikishe kwamba malipo yote yanalipwa moja kwa moja kwa watoa huduma kupitia katika bank account zao kama sheria za fedha zinavyoelekeza ili kuepuka upotevu wa fedha za umma. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 56 : Malipo yaliyolipwa kinyume na utaratibu**

| Hati namba | Alielipwa | Mtoa huduma | Stakaba dhi Nam | Thamani (Tshs) | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| 5/7/2020 | Kamishna Chuo Cha Mafunzo | Duka la Chuo Cha Mafunzo | 1116 | 15,109,000 | Malipo kwa ajili ya chakula na vifaa vya usafi |
| 22/10/2020 | | | 1507<br>1508<br>1509 | 60,000,000 | Malipo ya chakula kwa ajili ya uchaguzi |
| 21/10/2020 | | | - | 14,375,000 | Magodoro na vifaa vya ujenzi |
| 7/7/2020 | | | 1115 | 15,000,000 | Malipo kwa ajili ununuzi wa dawa na mbolea |
| 21/10/2020 | | FA Glass Works | 751 | 2,259,230 | Matengenezo ya madirisha |
| 6/7/2020 | | Naima Amar Shebe | 0001 | 12,500,000 | Malipo kwa ajili vifaa mbalimbal |
| 22/10/2020 | | | 003 | 11,600,800 | Malipo ya ununuzi wa Mashine za kusagia mpunga. |

### 6.3.4.5 Kukosekana kwa Hatimiliki za vyombo vya usafiri vinavyomilikiwa na Chuo cha Mafunzo

Ukaguzi umebaini kuwa Chuo Cha Mafunzo kinamiliki vyombo mbalimbali vya usafiri zikiwemo gari 45 na pikipiki 2, ambapo gari 36 na pikipiki 2 zipo Unguja na gari 9 zipo Pemba. Ukaguzi umepitia kumbukumbu na nyaraka zinazohusika na vyombo hivyo na kubaini kuwa vyombo hivyo vinamilikiwa na Chuo, taasisi nyengine za Serikali baadhi ya vyombo umiliki wake ni watu binafsi kinyume na utaratibu, **Kiambatisho Nambari 4 Kinahusika.**

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na miongozo ya fedha taslim (IPSAS CASH) nambari 17. Aidha, ukaguzi umebaini kwamba vyombo vyote hivyo havijakatiwa Bima. Kufanya hivyo ni kinyume na Sheria namba 7 ya mwaka 2003 ya usalama barabarani pamoja na miongozo ya Serikali.

Kukosekana kwa hati miliki kunaplekea kushindwa kumiliki mali hizo kisheria, aidha kunasabisha upotevu wa mali hizo na kupelekea hasara chuo na Serikali kwa ujumla

Ukaguzi unashauri uongozi wa Chuo cha Mafunzo kuhakikisha kwamba mali zote za Chuo zina tambuliwa na kusajiliwa kisheria kwa ajili ya kupata umiliki halali, ili kuepusha upotevu wa mali hizo

### 6.3.4.6 Madeni ya Chuo cha Mafunzo wanayodaiwa kutokana na huduma walizopatiwa shilingi 847,241,905

Ukaguzi umebaini kuwa Chuo cha Mafunzo kina daiwa jumla ya shilingi 847,241,905 kutoka kwa watoa huduma mbalimbali lakini baadhi ya vielelezo vinavyohusiana na madeni hayo havikupatikana kwa ukaguzi, aidha madeni ambayo vielelezo vyake vimepatikana vinatofautiana na rikodi iliyoainishwa katika hesabu za mwisho wa mwaka. Hata hivyo ukaguzi umeshindwa kuthibitisha na kujiridhisha usahihi wa madeni hayo kutokana na Chuo kutoweka kumbukumbu na rikodi sahihi za madeni hayo. Kutokuwepo kwa kumbukumbu sahihi na usimamizi imara wa madeni kunaweza kusababisha upotevu wa fedha za Serikali na ni kwenda kinyume na sheria na miongozo ya fedha iliyopo. Aidha kutasababisha athari kwa bajeti ya mwaka unaofuata na kupelekea mipango iliyopangwa kutotekelezeka kwa wakati.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Chuo cha Mafunzo kuhakikisha unasimamia na kufuatilia kwa kina madeni yake pamoja na kuyathibitisha ili kuepuka kurejea kulipa madeni hayo jambo ambalo linapelekea upotevu wa fedha za Serikali.Mchanganuo wa madeni hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 57: Madeni ya Chuo cha Mafunzo wanayodaiwa kutokana na huduma walizopatiwa**

| Mdai | Muda wa deni | Deni katika hesabu ya mwisho wa mwaka | Vielelezo vya deni vilivyo patikana kwa ukaguzi | Tofauti |
|---|---|---|---|---|
| Visiwani General Traders | Haujulikani | 120,790,100 | 40,081,020 | 80,709,080 |
| Russan Store | | 34,160,000 | Hana vielelezo | |
| Sabah Store | | 36,142,300 | 183,621,292 | 147,478,992 |
| Issa Ali Sefu | | 8,000,000 | Hana vielelezo | |
| Abdallah Iddi Abdallah | | 7,090,000 | Hana vielelezo | |
| Afisi Ya Mapato (Farm-Earning) | | 127,012,505 | Hana vielelezo | |
| Jku | | 21,500,000 | Hana vielelezo | |
| Bi Naima Amour Shebe | | 387,267,000 | 341,734,000 | 45,533,000 |
| Amo Stationary Services | | 4,700,000 | Hana vielelezo | |
| Safiana Traders | | 65,500,000 | 65,507,000 | 7,000 |
| Juma Faki Salim | | 23,580,000 | 23,580,000 | Vimepatikana |
| M4 Hard Ware | | 11,500,000 | Hana vielelezo | |
| **Jumla** | | **847,241,905** | | |

### 6.3.4.7 Ukiukwaji wa Sheria ya Manunuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma shilingi 87,212,400

Katika ukaguzi uliofanyika kwa mwaka wa fedha 2020/2021 imebainika Chuo cha Mafunzo kimefunga mikataba minne katika kutekeleza shughuli mbalimbali za uwendeshaji wa Chuo yenye thamani ya shilingi 1,371,916,000 kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 58 : Ukiukwaji wa Sheria ya Manunuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma**

| Namba | Mtoa huduma | Namba ya Mkataba | Thamani (Tshs) | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Karibu Phamarcy | SMZ/DO3/G/ RNCB/2020/ – 2021/01 | 52,349,500 | Kupatiwa madawa ya wanafunzi kwa mwaka mmoja, Agosti 2020-2021 |
| 2. | Dundo | SMZ/DO3/G/ RNCB/2020 – 2021/02 | 154,525,000 | Kupatiwa sare za wanafunzi, mwaka Mmoja, Agosti 2020-2021 |
| 3. | Visiwani G. Supplier | SMZ/DO3/G/ RNCB/2020– 2021/03 | 603,626,500 | Kupatiwa vifaa vya ujenzi kwa kwa mradi Pemba, mwaka mmoja, Jan 2021- Feb 2021 |
| 4. | RM2 | SMZ/DO3/G/ RNCB/2020– 2021/04 | 561,415,000 | Kupatiwa chakula cha wanafunzi kwa mwaka mmoja, Agosti 2020-2021 |
| **Jumla** | | | **1,371,916,000** | |

Katika utekelezaji wa makubaliano ya mikataba hiyo ukaguzi umebaini Chuo cha Mafunzo kimefanya malipo yenye thamani ya shilingi 87,212,400 kinyume na makubaliano ya mkataba kwani imebainika kwa mujibu wa mkataba alipaswa anunue dawa kwa Karibu Pharmacy na badala yake alifanya manunuzi ya dawa kwa Magogoni Pharmacy yenye thamani ya shilingi 7,212,400 jambo ambalo halipo katika makubaliano ya mkataba wake wa awali.

Aidha, imebainika kwa mujibu wa makubaliano ya mkataba wa ununuzi wa chakula alipaswa kumlipa msambazaji RM2 Food Stuff na badala yake amelipwa Duka la Chuo cha Mafunzo malipo yenye thamani ya shilingi 20,000,000 jambo ambalo ni kinyume na makubaliano ya mkataba wa awali.

Vile vile imebainika kwa mujibu wa makubalino ya mkataba wa ununuzi wa chakula alipaswa kumlipa msambazaji RM2 Food Stuff na badala yake amelipwa Duka la Chuo cha Mafunzo malipo yenye thamani ya shilingi 60,000,000 jambo ambalo ni kinyume na makubaliano ya mkataba wa awali.

Dosari iliyobainika katika ukaguzi ni kutokutekeleza makubaliano ya mkataba aliyofunga na watoa huduma mbali mbali jambo ambalo linapelekea kujitokeza kwa viashiria vya upotevu wa fedha za umma kwa kufanya malipo kwa duka la Chuo cha Mafunzo jambo ambalo litapelekea kuikosesha Serikali mapato yatokanayo na kodi mbali mbali kwa watoa huduma. Aidha, kufanya malipo yenye thamani ya shilingi 80,000,000 kwa Chuo cha Mafunzo ni kwenda kinyume na miongozo ya Baraza la Mapinduzi inayowataka Wakuu wa Taasisi kuwacha kufanya malipo kwa njia ya fedha taslim (Cash Payment).

Kufanya malipo kinyume na makubaliano ya mikataba kunaweza kukapelekea kuingiza Serikali kwenye matatizo yasiyo ya lazima pale ambapo mtoa huduma atakapoamua kuishtaki Serikali na kupelekea Serikali kulipa fidia kubwa zaidi ya makubaliano ya kwenye mkataba.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Chuo cha Mafunzo kufuata misingi na miongozo ya fedha ili kuepuka kuitia hasara Serikali inayotokana na uzembe wa kufanya maamuzi bora.

Mchanganuo wa malipo yaliyolipwa kinyume na makubaliano ya mikataba na watoa huduma mbali mbali ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 59 : Malipo yaliyolipwa kinyume na makubaliano ya mikataba**

| Namba | Hati namba | Hundi namba | Alielipwa | Thamani (Shs) | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | 1/1/2021 | TISS | Magogoni Phamarcy | 7,212,400 | Malipo kwa ajili ununuzi wa madawa kwa mwezi wa Jan 2021.Kwa mujibu wa mkataba alipaswa kulipwa Karibu Pharmacy |
| 5 | 22/10/2020 | CASH | Duka chuo cha mafunzo | 60,000,000 | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya chakula kwa uchaguzi Oct, 2020. Kwa mujibu wa mkataba alipaswa kulipwa RM2 FOOD STUFF |
| 6 | 20/12/2020 | Cash | Duka la Chuo Cha Mafunzo | 20,000,000 | Ikiwa ni malipo ya chakula kwa maafisa na wapiganaji. kwa mujibu wa mkataba alipaswa kulipwa RM2 FOOD STUFF |
| **Jumla** | | | | **87,212,400** | |

### 6.3.4.8 Malipo yasiyozingatia ushindani wa bei shilingi 95,908,055

Ukaguzi umebaini Chuo cha Mafunzo kimetumia jumla ya shilingi 95,908,055 za mapato kwa ajili ya kupata huduma pamoja na manunuzi ya vifaa mbalimbali, dosari iliyobainika ni kutokuwepo kwa ushindani wa bei jambo ambalo linaweza kupelekea kufanyika kwa malipo ya bei ya juu ukilinganisha na uhalisia wa mahitaji yanavyopatikana kwa bei ya sokoni.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Chuo cha Mafunzo kuhakikisha unafanya matumizi kwa kuzingatia matakwa ya kanuni na sheria za fedha ili kuepuka kujitokeza kwa viashiria vya upotevu wa fedha. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 60 : Malipo yasiyozingatia ushindani wa bei**

| Namba | Hati namba | Tarehe | Alielipwa | Thamani (Tshs) | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | 5/7/2020 | 9/7/2020 | Duka la Chuo Cha Mafunzo | 15,109,000 | Malipo kwa ajili ya chakula na vifaa vya usafi |
| 2 | 6/7/2020 | 10/7/2020 | Naima Amar Shebe | 12,500,000 | Malipo kwa ajili vifaa mbalimbal |
| 3 | 7/7/2020 | 16/7/2020 | Duka la Chuo Cha Mafunzo | 15,000,000 | Malipo kwa ajili ununuzi wa dawa na mbolea |
| 4 | 7/8/2020 | 8/8/2020 | | 32,347,500 | |
| 5 | 21/10/2020 | 20/10/2020 | | 18,692,325 | Malipo kwa ajili matumizi mbalimbali |
| 6 | 22/10/2020 | 20/10/2020 | Kamishna Chuo Cha Mafunzo<br>FN GLASS WORK | 2,259,230 | Matengenezo ya madirisha |
| **Jumla** | | | | **95,908,055** | |

### 6.3.4.9 Malipo yasiyo na Mkataba pamoja na vielelezo vinavyothibitisha huduma iliyotolewa shilingi 43,000,000

Ukaguzi umebaini kwamba jumla ya shilingi 43,000,000 zimelipwa kwa ajili ya shughuli mbali mbali za utekelezaji wa mradi wa ujenzi Pemba, dosari iliyobainika katika ukaguzi ni kukosekana kwa makubaliano ya mkataba pamoja na vielelezo vinavyothibitisha gharama halisi ya kazi iliyofanyika ili kuweza kuthibitisha uhalali wa matumizi yaliyofanyika jambo ambalo limepelekea kushindwa kuthibitisha thamani halisi ya fedha na kiwango cha ujenzi kilichofanyika.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Chuo cha Mafunzo kuingia mkataba kwa ajili ya shughuli mbali mbali za utekelezaji wa mradi wa ujenzi ili kuweza kujiweka mahali salama pale zinapotokezea sintofahamu. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 61 : Malipo yaliyofanyika bila ya kuwepo kwa mkataba na vielelezo husika**

| Namba | Hati Namba | Alielipwa | Kiasi cha fedha (Tshs) | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 1. | 1/8/2020 | Mahmoud Abdallah Ramadhan | 18,000,000 | Malipo ya Posho. |
| 2. | 1/8/2020 | Said Ali Faki | 6,000,000 | Malipo ya Posho la mhandisi. |
| 3. | 1/9/2020 | Juma Faki Ali<br>(Kubwa lijalo) | 19,000,000 | Malipo kwa utengenezaji wa milango. |
| **Jumla** | | | **43,000,000** | |

### 6.3.4.10 Kutokatwa kwa Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) inayotokana na ununuzi na utoaji wa huduma shilingi 17,718,150

Ukaguzi ulipitia hati mbalimbali zinazohusiana na malipo na kubaini kuwepo kwa hati za malipo zinazohusiana na manunuzi na utoaji wa huduma zenye thamani ya shilingi 118,121,200 ambazo zilistahiki kukatwa kodi ya ongezeko la thamani ya shilingi 17,718,150.

Dosari iliyobainika katika ukaguzi ni kutokukatwa kodi ya ongezeko la thamani na kuziwasilisha katika ofisi inayohusiana na mapato kwa mujibu wa sheria. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 62: Kutokatwa kwa Kodi ya Ongezeko la Thamani**

| Hati namba | Ankara namba | Aliyelipwa | Thamani (Tshs) | VAT (15%) |
|---|---|---|---|---|
| 1/8/2020 | 3689 | Visiwani General Supplies | 6,600,000 | 990,000 |
| 1/10/2020 | 3676 | | 72,461,200 | 10,869150 |
| 1/11/2020 | 3690 na 3691 | | 39,060,000 | 5,859,000 |
| **Jumla** | | | **118,121,200** | **17,718,150** |

Chuo cha Mafunzo kushindwa kukata kodi ya ongezeko la thamani kunapelekea kuikosesha Serikali mapato hali inayosababisha kutofikiwa kwa malengo yaliopangwa katika mpango mkakati wa Taasisi zinazosimamia kodi na Serikali ambapo kufanya hivyo ni ukiukwaji wa sheria, kanuni na miongozo ya kodi iliyowekwa.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Chuo cha Mafunzo kuhakikisha unasimamia suala zima la ukataji wa kodi ya ongezeko la thamani kwa kila manunuzi au huduma zinazotolewa ili kwenda sambamba na sheria ya kodi.

**CHUO CHA MAFUNZO - PEMBA**

### 6.3.4.11 Hati za malipo zenye vielelezo pungufu shilingi 54,616,000

Ukaguzi umebaini kwamba jumla ya shilingi 54,616,000 zimetumika kwa matumizi mbalimbali ya Chuo cha Mafunzo, dosari iliyobainika na ukaguzi ni kuwepo kwa baadhi ya vielelezo pungufu vilivyoambatanishwa na hati za malipo ili kuweza kuthibitisha uhalali wa malipo hayo.

Kutokuambatanisha vielelezo katika hati za malipo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 34(1) cha Sheria Nambari 12 Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 63 : Hati za malipo zenye vielelezo pungufu**

| Hati namba | Hundi namba | Kiasi cha fedha kilicholipwa (Tshs.) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 06/07<br>20/07/2020 | 002100 ya<br>21/07/2020 | 5,868,000 | Kamanda Mkuu Chuo cha Mafunzo Pemba. | Malipo ya fedha kwa ajili ya mikato mbalimbali ya dharura wanayokatwa maofisa na wapiganaji |
| 18/08<br>21/08/2020 | 002122 ya<br>21/08/2020 | 8,360,400 | | |
| 08/09<br>21/09/2020 | 002134 ya<br>21/09/2020 | 7,013,100 | | |
| 12/10<br>19/10/2020 | 002152 ya<br>19/10/2020 | 13,615,500 | | |
| 23/11<br>25/11/2020 | | 10,717,600 | | |
| 14/12<br>23/12/2020 | 002196 ya<br>23/12/2020 | 9,041,400 | | |
| **Jumla** | | **54,616,000** | | |

### 6.3.4.12 Utumiaji wa fedha za mapato bila ya kupelekwa benki shilingi 3,602,000

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwa Chuo cha Mafunzo Pemba kinakusanya mapato kupitia vyanzo tofauti, dosari iliyobainika na ukaguzi ni kuwepo kwa baadhi ya mapato ambayo hutumika katika vituo husika bila kupelekwa benki ambapo baadhi ya kumbukumbu za makusanyo hayo zimekosekana kwa ukaguzi.

Kufanya hivyo kunapelekea kuwepo kwa upotevu wa mapato hayo, aidha ni kwenda kinyume na kifungu nambari 30 cha Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya Zanzibar ya mwaka 2016 pamoja na kifungu nambari 23 (1) na (4) cha Kanuni ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2021. Mchanganuo wa mapato hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 64 : Utumiaji wa fedha za mapato bila ya kupelekwa benki**

| Kituo | Fedha zilizokusanywa (Tshs.) | Fedha zilizopelekwa Benki | Fedha zilizotumika bila kupelekwa Benki (Tshs.) |
|---|---|---|---|
| Kituo cha Mafunzo Kengeja | 2,587,000 | 375,000 | 2,212,000 |
| Kituo cha Mafunzo Kangagani | 1,114,000 | 0 | 1,114,000 |
| Kituo cha Mafunzo Tungamaa. | 476,000 | 200,000 | 276,000 |
| **Jumla** | | | **3,602,000** |

### 6.3.5 FUNGU D 04 - KIKOSI MAALUM CHA KUZUIA MAGENDO (KMKM)

Ukaguzi wa hesabu za Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo kwa mwaka wa fedha 2020/2021 umefanywa kwa mujibu wa Sheria, kanuni, taratibu pamoja na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Taarifa ya Mapato**

Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo kilikadiriwa kukusanya jumla ya shilingi 30,384,688,766 kwa mwaka wa fedha 2020/2021. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 Kikosi kilikusanya jumla ya shilingi 30,384,688,766 sawa na asilimia 100 ya makadirio.

**Taarifa ya Matumizi**

Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo kwa mwaka wa fedha 2020/2021 kilikadiriwa kutumia jumla ya shilingi 37,462,820,260 kwa matumizi ya kazi za kawaida. Hadi kufikia tarehe 30 Juni 2021 jumla ya shilingi 30,359,568,766 zimetumika sawa na asilimia 81 ya makadirio.

**MATOKEO NA MAPENDEKEZO YA UKAGUZI**

#### 6.3.5.1 Kukosekana kwa Mshika Fedha Mkuu

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba kikosi cha Kuzuia Magendo kina wajibu wa kusimamia na kutekeleza shughuli mbali mbali zinazohusiana na usimamizi wa fedha za Serikali katika uendeshaji wa shughuli za kikosi dosari iliyobainika ni kukosekana kwa mshika fedha kuu katika kitengo cha uhasibu ambaye ndiye mwenye jukumu la kulipa na kuweka kumbu kumbu mzuri za mapato na matumizi.

Kufanya hivyo kunapelekea kupunguwa kwa ufanisi juu ya suala zima la ulipaji na uwekaji wa kumbu kumbu za fedha ambapo ni kwenda kinyume na Sheria, Kanuni na miongozo iliyopo.

Ukaguzi unashauri uongozi wa kikosi cha Kuzuia Magendo KMKM kuhakikisha unachukua hatua za kisheria ili kuweza kufanikisha upatikanaji wa Mshika fedha kwa lengo la kutekeleza mgawanyo wa majukumu pamoja na uwekaji wa kumbu kumbu mzuri za taarifa zote zinazohusiana na fedha.

#### 6.3.5.2 Kutokuainishwa kwa mapato shilingi ya 1,057,505,085.02 na matumizi ya shilingi 918,253,383 katika hesabu ya mwisho wa mwaka

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba kikosi cha Kuzuia Magendo (KMKM) kiliandaa na kuwasilisha mahesabu ya mwisho wa mwaka katika Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni 2021, dosari iliyobainika katika ukaguzi ni kutokuainishwa kwa jumla ya shilingi 1,057,505,085.02 za mapato na shilingi 918,253,383 za matumizi katika hesabu ya mwisho wa mwaka yaliyowasilishwa kwa ajili ya ukaguzi.

Kufanya hivyo kunapelekea kutokuonesha kwa sura halisi na sahihi ya hesabu za mwisho wa mwaka ya Kikosi cha Kuzuia Magendo.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Kikosi cha Kuzuia Magendo kuhakikisha unasimamia na kutekeleza uandaaji wa mahesabu ya mwisho wa mwaka kwa kuweka taarifa zote zenye uhalisia na mapato, matumizi pamoja na mali za Taasisi kwa mujibu wa Sheria pamoja na miongozo ya fedha iliyopo. Mchanganuo wa mapato na matumizi ambayo hayakuainishwa katika hesabu ya mwisho wa mwaka ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 65 : Mapato na Matumizi ambayo hayakuainishwa katika hesabu ya mwisho wa mwaka**

| Maelezo | Mapato | Matumizi |
|---|---|---|
| Ujenzi wa Afisi ya Shirika la Bandari **(mapato yatokanayo na ujenzi)** | 572,031,260.02 | - |
| Kutoka katika vyanzo vya Afya KMKM na Pharmacy KMKM | 485,473,825.00 | - |
| Ununuzi wa gari mbili (2) | - | 94,000,000 |
| Matumizi mbali mbali ya huduma za afya | - | 474,253,383.00 |
| Ununuzi wa vifaa kwa ujenzi wa Hanga 1, Hanga 2, Staff House, Mess, Hospital, Quorter guard (wete) | - | 350,000,000 |
| **Jumla** | **1,057,505,085.02** | **918,253,383** |

### 6.3.5.3 Kutokulingana kwa fedha halisi iliyotumika na iliyowasilishwa kwenye hesabu za mwisho wa mwaka shilingi 182,418,839

Katika kupitia taarifa mbali mbali zikiwemo taarifa za Hesabu ya mwaka, daftari la kurikodia kumbukumbu za fedha pamoja na taarifa za matumizi. Ukaguzi umebaini kwamba baadhi ya taarifa zilizoripotiwa katika Hesabu za Mwisho wa Mwaka zinatofautiana na taarifa za hati za malipo.

Kutokulingana kwa fedha halisi iliyotumika pamoja na iliyowasilishwa katika hesabu za mwisho wa mwaka kunapelekea kutokuonyesha kwa uhalisia wa hesabu zilizowasilishwa ambapo ni kwenda kinyume na viwango vya ufungaji wa hesabu vya kitaifa na kimataifa.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Kikosi Maalum cha Kuzuwia Magendo kuhakikisha unafuata viwango vya ufungaji wa hesabu ili kuweza kuonyesha uhalisia wa taarifa za hesabu kwa mujibu wa viwango kubalifu. Mchanganuo wa taarifa hiyo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 66 : Fedha halisi iliyotumika na iliyowasilishwa kwenye hesabu za mwisho wa mwaka**

| Kifungu | Makadirio (Tshs.) | Thamani iliyoripotiwa katika taarifa za fedha (Tshs.) (A) | Kupitia hati za malipo (Tshs.) (B) | Thamani ya mkataba (Tshs.) | Tofauti Ya shilingi (Tshs.) (A-B) |
|---|---|---|---|---|---|
| Militaring Cataring | 1,267,800,000 | 1,244,827,289 | 1,062,408,450 | 626,964,000 | 182,418,839 |

### 6.3.5.4 Kukosekana kwa taarifa za fedha zilizohaulishwa shilingi 1,667,182,238

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Kikosi cha Kuzuia Magendo KMKM kilipokea jumla ya shilingi **1,667,182,238** zilizohaulishwa kutoka (OR) Fedha na Mipango kupitia mfumo wa IFMIS kwa mwaka wa fedha 2020/2021 kwenda Canteen ya KMKM Zanzibar kwa vipindi tofauti, dosari iliyobainika ni kukosekana kwa taarifa za mapokezi na matumizi ya fedha hizo ili kuweza kuthibitisha uhalali wa upokeaji pamoja na utumiaji wa fedha zilizohaulishwa kutoka Hazina.

Kufanya hivyo kunapelekea kukosekana kwa uwekaji wa kumbu kumbu za taarifa za fedha ambapo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 34(1) cha Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Kikosi cha Kuzuia Magendo kuhakikisha kwamba unasimamia ipasavyo uwekaji wa taarifa za mapokezi na matumizi ya fedha za umma ili kuepusha kujitokeza kwa viashiria vya ubadhirifu wa fedha za umma. Mchanganuo wa uhaulishwaji wa fedha hizo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 67 : Kukosekana kwa taarifa za fedha zilizohaulishwa**

| Tarehe | Hati namba R/Db | Aliyelipwa | Kiasi cha fedha kilichohaulishwa (Tshs) |
|---|---|---|---|
| 22-Jul-2020 | D04PV2000000021 | Canteen ya KMKM Zanzibar | 281,527,300.00 |
| 20-Aug-2020 | D04PV2000000063 | | 270,058,300.00 |
| 21-Sep-2020 | D04PV2000000094 | | 281,362,833.00 |
| 22-Oct-2020 | D04PV2000000129 | | 274,778,000.00 |
| 26-Nov-2020 | D04PV2000000164 | | 279,850,150.00 |
| 21-Dec-2020 | D04PV2000000187 | | 279,605,655.00 |

### 6.3.5.5 Malipo kwa Watoa huduma ambao Hawakusajiliwa na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma shilingi 2,246,867,100

Kwa mujibu wa kifungu cha 23(1) cha Sheria ya Manunuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma kinaeleza kulingana na masharti ya sheria hii mtu, kampuni au taasisi haitawasilisha zabuni au vyenginevyo kushiriki katika manunuzi ya Umma isipokua chombo kiwe kimesajiliwa na Mamlaka ya Manunuzi.

Kwa mujibu wa kifungu cha 23(2), zabuni kutoka kwa mtu, kampuni au chombo ambacho hakijasajiliwa haifai na hakitazingatiwa na taasisi ya ununuzi.

Ukaguzi umebaini kwamba Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo kimefanya manunuzi na watoa huduma mbali mbali ambao hawakusajiliwa na Mamlaka ya Ununuzi kwa mujibu wa Sheria ambapo ukaguzi kushindwa kujiridhisha juu ya uhalali wa malipo hayo.

Kuwatumia watoa huduma ambao hawakusajiliwa kunapelekea kuikosesha Serikali mapato ambapo ni kwenda kinyume na vifungu vya Sheria vilivyonakiliwa hapo juu. Mchanganuo wa malipo kwa Watoa huduma ambao hawakusajiliwa na ZPPDA ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 68 : Watoa huduma ambao Hawakusajiliwa na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma**

| Namba | jina la mtoa huduma | Hati namba | Kiasi cha fedha kilicholipwa (Tshs) | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Kemisy | T.T | 486,539,300 | Ununuzi wa Gari |
| 2. | Haroub Ali Suleiman | 1/4/2020 yenye hundi namba 000448 | 31,000,000 | |
| 3. | Mosal Trading Enterprises | T.T | 33,977,800 | Msambazaji wa Chakula |
| 4. | Ihsan | T.T | 62,540,000 | Ununuzi wa Gari |
| 5. | Rjr Group Srl | T.T | 1,632,810,000 | Malipo kwa ajili ya ushauri elekezi. |
| **Jumla** | | | **2,246,867,100** | |

#### 6.3.5.6 Manunuzi yaliyofanyika kinyume na taratibu shilingi 33,977,800

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Kikosi cha Kuzuia Magendo kimefanya malipo yenye jumla ya shilingi 33,977,800 kwa ajili ya ujenzi wa Bekar pamoja na ununuzi wa vifaa mbali mbali vya Bekar kwa lengo la uanzishwaji wa mradi wa kutengeneza mikate kwa matumizi ya Kambi na kutoa huduma hiyo kwa wananchi watakaohitaji , dosari iliyobainika ni kutokufuatwa kwa taratibu za ujenzi na ununuzi wa vifaa kwa mujibu wa Sheria kwa kukosekana kwa taarifa muhimu kama ifuatavyo:-

- Kukosekana kwa bajeti ya ujenzi wa bekar pamoja na mchoro.
- Kukosekana kwa nukuu tatu kwa watoa huduma tofauti.
- Kukosekana kwa taarifa ya upembuzi yakinifu ya ujenzi wa bekari.
- Kukosekana kwa tathmini ndogo ya ujenzi.

Kufanya hivyo kunapelekea kukosekana kwa uwekaji taarifa zinazohitajika kwa matumizi ya baadae ambapo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 34(1) cha Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Kikosi cha Kuzuia Magendo kuhakikisha kwamba unasimamia ipaswavyo utayarishaji na uwekaji wa taarifa kwa ajili ya kumbu kumbu mbali mbali kwa mujibu wa Sheria, kanuni pamoja na miongozo ya fedha iliyopo kwa lengo la kuondoa uwezekano wa kuwepo kwa viashiria vya ubadhirifu wa fedha za Umma.

#### 6.3.5.7 Manunuzi yaliyofanyika kinyume na taratibu shilingi 699,999,500

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Kikosi cha Kuzuia Magendo kimefanya malipo kwa msambazaji Mzalendo Hardware General kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya ujenzi wa hanga namba 1, Hanga namba 2, Quorter guard, Hospital, Staff House, Messi, Msikiti, dosari iliyobainika ni kutokufuatwa kwa taratibu za ununuzi wa vifaa kwa mujibu wa Sheria kwa kukosekana kwa taarifa muhimu kama ifuatavyo:-

- Kukosekana kwa dondoo (minutes) za kikao cha Bodi ya Zabuni kilizopitisha maamuzi ya ujenzi
- Kukosekana kwa Tangazo la zabuni ya ununuzi wa vifaa vya Ujenzi katika Gazeti.
- Kukosekana kwa taratibu za utayarishaji wa B.O.Q pamoja na uwasilishaji wa michoro.
- kukosekana kwa ripoti ya tathmini.
- kukosekana kwa ushiriki wa mshauri elekezi wa fedha katika timu ya tathmini.
- kukosekana kwa ushiriki wa Enginear katika timu ya tathmini.
- kukosekana kwa Afisa Manunuzi kutoka katika Taasisi nyingine.
- Kukosekana kwa kitabu cha zabuni kwa wazabuni.
- kukosekana kwa viapo vya wajumbe wa timu ya tathmini.
- Kukosekana kwa Idhini ya Mwanasheria Mkuu ya kuendelea na taratibu za kufunga Mkataba.

- Kukosekana kwa Mkataba baina Mzabuni Mzalendo na KMKM.
- Kukosekana kwa ruhusa kutoka Mamlaka ya Manunuzi ya kuendelea na taratibu za Mkataba (Comment za Mamlaka).
- Kukosekana kwa ripoti ya Mshauri Elekezi.
- kukosekana kwa report ya technical supporting.
- Kukosekana kwa Cheti cha malipo cha Mshauri Elekezi kabla ya kufanyika kwa Malipo.
- Kukosekana kwa ripoti ya kitaalamu (technical support report) baada ya kukabidhiwa vifaa.

Kufanya hivyo kunapelekea kukosekana kwa uwekaji wa taarifa zinazohitajika kwa matumizi ya baadae ambapo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 34(1) cha Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Kikosi cha Kuzuia Magendo kuhakikisha kwamba unasimamia ipaswavyo utayarishaji na uwekaji wa taarifa kwa ajili ya kumbu kumbu mbali mbali kwa mujibu wa Sheria, kanuni pamoja na miongozo ya fedha iliyopo kwa lengo la kuondoa uwezekano wa kuwepo kwa viashiria vya ubadhirifu wa fedha za Umma. Mchanganuo wa manunuzi kinyume na taratibu ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 69 : Manunuzi yaliyofanyika kinyume na taratibu**

| Ankara namba | Hundi namba | Kiasi cha fedha kilicholipwa (Tshs) | Maelezo |
|---|---|---|---|
| 0001 na 0002 ya 8/9/2020 | T.T | 339,805,555 | Ununuzi wa vifaa vya ujenzi |
| 28/6/2021 | | 10,193,945 | Malipo ya kodi ya zuio (ZRB) |
| ... tarehe ya hati 29/4/2021 | CASH | 350,000,000 | Fedha kwa ajili ya ujenzi wa mahanga ya kulalia wapiganaji kikosi cha Kmkm Wete Pemba. |
| **Jumla** | | **699,999,500** | |

### 6.3.5.8 Manunuzi yaliyofanyika kinyume na taratibu Shilingi 575,499,205.56

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo kimefanya malipo yenye jumla ya shilingi 575,499,205.56 kwa wasambazaji KEMISY INVESTMENT CO LTD, HAROUB ALI SULEIMAN pamoja na IHSAN GENERAL TRADERS kwa ajili ya ununuzi wa gari sita (6) za zishazotumika (used car).

Dosari iliyobainika katika ukaguzi ni kutokutangazwa kwa zabuni pamoja na kutokupatikana kwa makubaliano ya mkataba wa ununuzi wa gari hizo, kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 65 cha Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshwaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016.

Hata hivyo ukaguzi umebaini KMKM imekiuka muongozo wa Baraza la Mapinduzi wenye kumbukumbu namba BLM/97/M/C.5/VOL.V/27 wa tarehe 27 Septemba 2021 kutoka Serikalini uliotolewa na Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi kuwaagiza Wakuu wote wa Taasisi kuwasilisha maombi ya ununuzi wa gari kwa Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Fedha na Mipango na kuacha kununua magari yaliyotumika (Used Car) pamoja na kuacha kununua magari kwa wazabuni binafsi kwa lengo la

kununua gari kwa thamani kubwa kuliko bei ya sokoni ambapo KMKM imenunua gari sita zilizotumika (Used Car) bila ya kupata ridhaa ya kibali kutoka kwa Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi, hata hivyo ukaguzi haukuweza kupatiwa ripoti ya ukaguzi wa gari hizo (Inspection Report) kutoka kwa fundi mkuu wa Karakana ya Serikali kwa vile gari hizo hazikufanyiwa uchunguzi wa kina kujua umadhubuti na uzima wa gari hizo, ukaguzi haukuweza kupatiwa hati ya mapokezi ya gari hizo (Delivery Note).

Kufanya manunuzi kinyume na matoleo ya Serikali kunapelekea taasisi ya umma kutumia gharama kubwa ya ununuzi unaotokana na wazabuni kuwauzia Serikali magari kwa gharama kubwa ukilinganisha na bei ya soko ilivyo.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 65 cha Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshwaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016.

Ukaguzi unashauri uongozi wa KMKM kuhakikisha unatekeleza miongozo inayotolewa na Serikali ili kuepusha kutumia fedha za umma kinyume na utaratibu. Mchanganuo wa manunuzi kinyume na taratibu ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 70 : Manunuzi yaliyofanyika kinyume na taratibu**

| Hati namba | Hundi namba | Aliyelipwa | Kiasi cha fedha kilicholipwa (Tshs) | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| PV 13/7/2020 | T.T | Ihsan General Traders | 62,540,000.00 | Ununuzi wa gari ya Fuso kwa ajili ya kikosi cha Kmkm |
| Pv 1/4/2020 ya 3/4/2020 | | HAROUB ALI SULEIMAN | 31,000,000.00 | Ununuzi wa gari ya Center Dyna kwa matumizi ya Kikosi. |
| | Dummy | Kemisy Investment Co ltd. | 289,534,775.56 | Malipo ya 60%(124,222.80). Kwa ununuzi wa gari tatu mpya USD 207,038 kwa matumizi wa kikosi. |
| | | | 192,424,430.00 | Malipo ya 40%(82,815). Kwa ununuzi wa gari tatu mpya USD 207,038 kwa matumizi wa kikosi. |
| **Jumla** | | | **575,499,205.56** | |

### 6.3.5.9 Manunuzi yaliyofanyika kinyume na taratibu shilingi 634,901,500

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Kikosi cha Kuzuia Magendo kimefanya malipo yenye jumla ya shilingi 634,901,500 kwa wasambazaji Baba Three Store (Julai hadi Disemba) na MR2 FOOD STUFF (Febuari hadi Aprili) kwa ajili ya ununuzi wa chakula kwa askari waliopo kambini, dosari iliyobainika ni kutokufuatwa kwa taratibu za ununuzi wa chakula kwa mujibu wa Sheria kwa kukosekana kwa taarifa muhimu kama ifuatavyo:-

- Kutokutangazwa kwa zabuni ya Wazi.
- kukosekana kwa barua kutoka Mamlaka ya ununuzi iliyowaruhusu kutumia njia ya (Restricted).
- Kukosekana kwa fomu za wajumbe za viapo kwa timu ya tathmini (Code of Ethic).
- kukosekana kwa barua za kuwajulisha walioshiriki mchakato wa zabuni kupitia kanuni namba 141 (1).
- Kukosekana kwa idhini ya Mwanasheria Mkuu inayoruhusu kuendelea na mkataba.

- Kukosekana kwa taarifa ya mapokezi ya bidhaa (Delivery Order).
- Kukosekana kwa hadidu rejea (TOR) inayoonyesha malipo yatalipwa kwa awamu ngapi.
- Kukosekana kwa Usajili wa Mtoa huduma kutoka Mamlaka ya Manunuzi.
- Kukosekana barua ya kuzawadiwa ushindi (Awarded latter)
- taarifa ya tathmini ya mchakato wa kumpata BABA THREE ya 22/10/2018 mpaka 31/10/2018 ripoti ya tathmini inaeleza kuwa, alipitishwa kwa shilingi 626,964,000
- Kukosekana kwa mkataba baina ya mtoa huduma MR2 na Kikosi. (mkataba ulioambatanishwa kutoka kwa mtoa huduma BABA umefungwa 5/12/2019)
- Kukosekana kwa idhini kutoka Mamlaka ya Manunuzi baada ya report ya tathmini kukamilika.
- Kukosekana kwa hati ya makubaliano ya punguzo la bei kwa ukaguzi (Negotiation report)

Kufanya hivyo kunapelekea kukosekana kwa uwekaji wa taarifa zinazohitajika kwa matumizi ya baadae ambapo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 34(1) cha Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Kikosi cha Kuzuia Magendo kuhakikisha kwamba unasimamia ipaswavyo utayarishaji na uwekaji wa taarifa kwa ajili ya kumbu kumbu mbali mbali kwa mujibu wa Sheria, kanuni pamoja na miongozo ya fedha iliyopo kwa lengo la kuondoa uwezekano wa kuwepo kwa viashiria vya ubadhirifu wa fedha za Umma.

#### 6.3.5.10 Malipo ya ujenzi yaliyofanyika kinyume na taratibu Shilingi 1,861,710,000

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Kikosi cha Kuzuia Magendo kimefanya malipo yenye jumla ya shilingi 1,861,710,000 kwa wajenzi na wasambazaji Mzalendo Hardware General Supplies, Ihsan Supplier General Traders pamoja na Mkuu wa KMKM kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa majengo tofauti tofauti, dosari iliyobainika ni kutokufuatwa kwa taratibu za ujenzi na ukarabati wa majengo tofauti tofauti kwa mujibu wa Sheria kwa kukosekana kwa taarifa muhimu kama ifuatavyo:-

- Kukosekana kwa Minutes za vikao vya Bodi ya Zabuni zilizopitisha maamuzi ya ujenzi.
- Kukosekana kwa Tangazo la zabuni ya ununuzi wa vifaa vya Ujenzi katika Gazeti.
- B.O.Q imefanyiwa marekebisho ya thamani bila ya kusainiwa na Engineer.
- Ripoti ya Enginear haikupatikana kwa ukaguzi kupitia kanuni ya manunuzi 118.
- Kukosekana kwa ushiriki wa mtaalam wa fedha katika timu ya tathmini.
- kukosekana kwa ushiriki wa Enginear katika timu ya tathmini.
- kukosekana kwa Afisa Manunuzi kutoka katika Taasisi nyingine.
- Kukosekana kwa Tender Document za wazabuni wasiopungua watatu (3).
- kukosekana kwa viapo vya wajumbe wa evaluation team.
- Kukosekana kwa Idhini ya Mwanasheria Mkuu ya kuendelea na taratibu za kufunga Mkataba.
- kukosekana kwa saini kwa upande wa anaepokea huduma (Purchaser).

- Kukosekana kwa sahihi za awali katika mkataba uliofungwa 22/6/2021.
- Kukosekana kwa ruhusa kutoka Mamlaka ya manunuzi baada ya taarifa ya tathmini. kwa ajili ya kuendelea na taratibu za Mkataba.
- Kukosekana kwa ripoti ya Mshauri Elekezi (Consultance).
- kukosekana kwa TOR inayoonyesha malipo yatalipwa kwa awamu ngapi.
- Kukosekana kwa "Certificate" ya Mshauri Elekezi kabla ya kufanyika kwa Malipo.

Kufanya hivyo kunapelekea kukosekana kwa uwekaji wa taarifa zinazohitajika kwa matumizi ya baadae ambapo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 34(1) cha Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Kikosi cha Kuzuia Magendo kuhakikisha kwamba unasimamia ipaswavyo utayarishaji na uwekaji wa taarifa kwa ajili ya kumbu kumbu mbali mbali kwa mujibu wa Sheria, kanuni pamoja na miongozo ya fedha iliyopo kwa lengo la kuondoa uwezekano wa kuwepo kwa viashiria vya ubadhirifu wa fedha za Umma. Mchanganuo wa malipo ya ujenzi kinyume na taratibu ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 71 : Malipo ya ujenzi yaliyofanyika kinyume na taratibu**

| Hati namba | Hundi namba | Kiasi cha fedha kilicholipwa (Tshs) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| Pv 4/9/2020 | **Cash** | 54,600,000 | **Mkuu wa Kmkm** | Malipo ya ufundi kwa muendelezo wa nyumba ya makamo wa pili wa Raisi Pagali |
| pv 8/10/2020 | | 10,000,000 | | |
| Pv 7/9/2020 | | 29,000,000 | | |
| Pv 13/3/2021 | | 10,000,000 | | |
| Pv 5/9/2020 | **Tiss** | 175,400,000 | **Mzalendo Hardware General Supplies** | Ununuzi wa vifaa kwa nyumba ya muendelezo wa kazi ya ujenzi wa nyumba ya makamo wa pili wa pili |
| Pv 10/10/2020 | | 57,800,000 | | Malipo ya muendelezo wa ukarabati wa nyumba za Maendeleo Michenzani |
| Pv 8/9/2020 | | 217,000,000 | | Ununuzi wa vifaa nyumba ya Makamo wa Pili Pagali |
| Pv 7/10/2020 | | 125,475,000 | | Ununuzi wa vifaa kwa ujenzi wa Shirika la Bandari |
| Pv 12/9/2020 | | 71,115,000 | | Ununuzi wa vifaa kwa ujenzi wa **Shirika la Bandari** |
| Pv .... ya tarehe 14/12/2020 | | 64,700,000 | | Ununuzi wa vifaa muendelezo wa nyumba za Michenzani block no 1 |
| Pv 12/7/2020 | | 150,000,000 | **Ihsan Supplier General Traders** | Ununuzi wa vifaa kwa ujenzi wa nyumba ya Makamo pagali |
| Pv 16/8/2020 | | 34,350,000 | | |
| Pv 15/8/2020 | | 73,800,000 | | |
| Pv 11/7/2020 | | 17,120,000 | | Ununuzi wa vifaa kwa ukarabati wa nyumba za Maendeleo Michenzani Block no 1 |
| Pv 18/7/2020 | | 20,600,000 | | |
| Pv 20/7/2020 | | 55,770,000 | | Ununuzi wa vifaa kwa muendelezo wa **Shirika la Bandari** |
| Pv3/9/2020 | | 40,250,000 | | |
| 19/7/2020 | | 50,500,000 | | Ununuzi wa vifaa muendelezo wa nyumba ya **Makamo** |
| 4/7/2020 | | 73,500,000 | | |
| 5/7/2020 | | 45,520,000 | | |

| Hati namba | Hundi namba | Kiasi cha fedha kilicholipwa (Tshs) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 14/8/2020 | Cash | 15,000,000 | Mkuu wa Kmkm | Malipo ya mafundi waliofanya **land-scaping** |
| Pv 10/9/2020 | | 12,000,000 | | Malipo ya Ufundi ukarabati wa **Baraza la Wawakilishi** |
| Pv 4/8/3020 | | 26,500,000 | | Malipo ya ufundi kwa ujenzi wa nyumba ya Makamo Pagali |
| Pv 2/7/2020 | | 10,000,000 | | Malipo ya ufundi wa **Land scaping** Nyumba ya makamo |
| Pv 11/9/2020 | | 44,550,000 | | Ununuzi wa vifaa kwa ukarabati wa **Baraza la wawakilishi la Zamani na sehemu ya Ofisi ya Makamo wa Pili Vuga** |
| Pv 5/10/2020 | | 24,500,000 | | Malipo ya ufundi kwa **Shirika la Bandari** |
| Pv 8/7/2020 | | 9,500,000 | | Malipo ya ufundi Ukarabati wa nyumba za maendeleo Michenzani block namba 1 |
| Pv 10/7/2020 | | 20,000,000 | | Malipo ya Mafundi kwa ajili ya kuandaa ujenzi wa Ofisi kuu **Shirika la Bandari** Zanzibar |
| Pv 3/7/2020 | | 27,380,000 | | Muendelezo wa ukarabati wa nyumba za Michenzani block 1 |
| Pv 17/7/2020 | | 18,500,000 | | Malipo kwa ajili ya Mafundi muendelezo wa Ofisi ya **Shirika la Bandari** |
| Pv 15/5/2021 | | 15,000,000 | | Ukarabati wa nyumba za Michenzani block namba moja ngazi ya pili |
| Pv 21/10/2020 | | 11,000,000 | | Malipo ya mafundi kwa muendelezo wa ujenzi wa Madrasa katika kijiji cha **DUNDUA** |
| Pv 9/10/2020 | | 27,800,000 | | Malipo ya ufundi kwa muendelezo wa ukarabati wa nyumba za Maendeleo Michenzani |
| Pv …. ya 10/12/2020 | | 26,300,000 | | Malipo ya mafundi kwa muendelezo wa ukarabati wa nyumba za Michenzani |
| Pv 19/8/2020 | | 97,515,000 | | Ununuzi wa vifaa kwa muendelezo wa Ofisi ya Shirika la Bandari |
| Pv 18/8/2020 | | 28,000,000 | | Malipo ya ufundi kwa Ujenzi wa Ofisi kuu Shirika la Bandari |
| Pv 5/8/2020 | | 71,665,000 | | Malipo ya muendelezo wa kazi ya ujenzi wa nyumba ya Makamo wa Pili Pagali (Chake Chake) |
| **Jumla** | | **1,861,710,000** | | |

### 6.3.5.11 Manunuzi yaliyofanyika kinyume na taratibu Shilingi 344,146,772.9

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo kimefanya malipo yenye jumla ya shilingi 344,146,772.90 kwa ajili ya ununuzi wa Dawa za binaadamu na vifaa tiba kwa wasambazaji tofauti kama wanavyoonekana katika jadweli hapo chini, dosari iliyobainika ni kutokufuatwa kwa taratibu za ununuzi wa dawa na vifaa tiba kwa mujibu wa Sheria kwa kukosekana kwa taarifa muhimu kama ifuatavyo:-

- Kutokuingizwa katika mpango wa manunuzi wa taasisi
- Kutokuwepo kwa ushindani wa zabuni
- Kutokuwepo kwa mkataba wa ununuzi wa dawa hizo
- Kukosekana kwa taarifa za upokeaji wa dawa hizi (delivery note)
- Kutokuwepo kwa utaratibu wa stock taking katika duka la Madawa hayo
- Kutokuwepo kwa bajeti ya matumizi hayo

Kufanya hivyo kunapelekea kukosekana kwa uwekaji wa taarifa zinazohitajika kwa matumizi ya baadae ambapo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 34(1) cha Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Kikosi cha Kuzuia Magendo kuhakikisha kwamba unasimamia ipaswavyo utayarishaji na uwekaji wa taarifa kwa ajili ya kumbu kumbu mbali mbali kwa mujibu wa Sheria, kanuni pamoja na miongozo ya fedha iliyopo kwa lengo la kuondoa uwezekano wa kuwepo kwa viashiria vya ubadhirifu wa fedha za Umma. Mchanganuo wa manunuzi kinyume na taratibu ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 72 : Manunuzi yaliyofanyika kinyume na taratibu**

<table>
<tr><th>Hati</th><th>Tarehe</th><th>Maelezo</th><th>Kiasi cha fedha kilicholipwa (Tshs)</th><th>Aliyelipwa</th><th>Ankara/Stakabadhi</th></tr>
<tr><td>Pv 1/11</td><td>04-Nov-20</td><td rowspan="6">Malipo kwa ajili ya Ununuzi wa dawa</td><td>3,243,000.00</td><td rowspan="6">Karibu Pharmacy</td><td>Ankara 1635 ya 2/11/2020, risiti 2692 ya 6/11/2020</td></tr>
<tr><td>Pv 1/10</td><td>20-Oct-20</td><td>12,251,000.00</td><td>Ankara 592-599 za 16/10/2020, risiti 2691 ya 22/10/2020</td></tr>
<tr><td>Pv 2/11</td><td>23-Nov-20</td><td>19,455,900.00</td><td>invoice 703 za 10/11/2020 na risiti 2727 ya 23/11/2020</td></tr>
<tr><td>-</td><td>-</td><td>9,993,000.00</td><td rowspan="3">Hati ya malipo imekosekana</td></tr>
<tr><td>-</td><td>-</td><td>9,796,200.00</td></tr>
<tr><td>-</td><td>-</td><td>9,951,000.00</td></tr>
</table>

| Hati | Tarehe | Maelezo | Kiasi cha fedha kilicholipwa (Tshs) | Aliyelipwa | Ankara/Stakabadhi |
|---|---|---|---|---|---|
| Pv 2/12 | 10-Dec-20 | Malipo kwa ajili ya kumlipa msambazaji. | 4,564,000.00 | Afya KMKM | Ankara 784 ya 5/11/2020 na Ankara 832 ya 3/12/2020. |
| Pv 22/1 | 22-Jan-21 | Malipo ya ununuzi wa reagent- Kas Medics Limited | 3,568,222.90 | | Ankara 134 ya 23 jan 2021 |
| Pv 4/1 | 27-Jan-21 | Marejesho ya Reagent za Maabara (Hemocroma plus Microcuvettes) - Hypermed Health Care | 2,210,000.00 | | Ankara HH-4070023 ya 07/01/2021 |
| Pv 5/1 | 28-Jan-21 | Malipo kwa ajili ya marejesho ya reagent za Maabara dressing na Dental za KMKM. | 3,224,000.00 | | Ankara 1001 ya 15/1/2021. risit 574 ya 28/1/2021 |
| Pv 6/1 | 28-Jan-21 | Malipo ya marejesho ya Reagent za Maabara | 5,510,000.00 | | Ankara HH-5389333 ya 3/02/2021. |
| Pv 7/1 | 27-Jan-21 | Fedha ya marejesho kwa ajili ya ununuzi wa gloves | 2,625,000.00 | Karibu Pharmacy | Ankara 4734 ya 25/01/2021. risiti 1646 |
| Pv 2/3 | 26-Feb-21 | Malipo ya marejesho ya Reagent za Maabara | 2,012,000.00 | Afya KMKM | Ankara HH-00820030 ya 29/01/2021. |
| Pv 3/3 | 26-Feb-21 | Malipo kwa ununuzi wa gloves catoon 15. | 3,000,000.00 | | Ankara 4781 ya 2/3/2021 |
| Pv 4/3 | 08-Mar-21 | Malipo kwa ajili ya marejesho ya reagent za Maabara. | 2,228,000.00 | | Ankara 1023 ya 27/01/2021. risit 260 ya 10/3/2021 |
| Pv 5/3 | 10-Mar-21 | Malipo kwa ajili ya Ununuzi wa dawa | 4,987,000.00 | Magogoni Pharmacy | Ankara MP29031ZNZ of 7/3/2021 |
| Pv 6/3 | 11-Mar-21 | Malipo kwa ajili ya marejesho ya reagent za Maabara. | 2,021,750.00 | Afya KMKM | hakuna Ankara |
| Pv 8/3 | 18-Mar-21 | Malipo kwa ajili ya marejesho ya Ununuzi wa dawa. | 10,000,000.00 | | Ankara 4655 - 4662 za 17/3/2021 na risit 20/3/2021 |
| Pv 10/3 | 30-Mar-21 | Malipo kwa ajili ya marejesho ya kumlipa KARIBU PHARMACY. | 24,000,000.00 | | Ankara 4539 za 22/2/2021. risit 1613 ya 6/4/2021 |
| Pv 5/4 | 08-Apr-21 | Ununuzi wa mashine mbili za operation. | 3,800,000.00 | | Ankara 000542 ya 5Aprl2021- NAJRAM LIMITED |
| Pv 6/4 | 08-Apr-21 | Ununuzi wa dawa wa duka la KMKM. Risiti 1476 ya 13/4/2021 | 6,500,000.00 | Karibu Pharmacy | Hakuna dokezo wala invoice |
| Pv 1/5 | 21-May-21 | Ununuzi wa dawa za hospital ya KMKM | 15,782,100.00 | Afya KMKM | Hakuna vielelezo |

| Hati | Tarehe | Maelezo | Kiasi cha fedha kilicholipwa (Tshs) | Aliyelipwa | Ankara/Stakabadhi |
|---|---|---|---|---|---|
| Pv 2/6 | 26-May-21 | Malipo ya marejesho ya Reagent za Maabara (HB) 100 | 5,535,000.00 | Hypermed Health Care | Ankara HH-6242 ya 16/4/2021 |
| Pv 4/6 | 21-Jun-21 | Malipo kwa ajili ya ununuzi wa dawa | 7,000,000.00 | KARIBU PHARMACY | Ankara 4601-06 ya 25/6/2021. risiti 1633 ya 1/7/2021 |
| Pv | 20-Jul-20 | | 1,751,000.00 | | Hakuna Ankara, dokezo ni kopi. Risiti 21/7/2020 |
| Pv 1/10 | 20-Oct-20 | | 12,251,000.00 | | Ankara 592-599 za 16/10/2020. risiti 2691 ya 22/10/2020. |
| Pv 1/11 | 09-Nov-20 | | 19,276,500.00 | | Risiti 2726 ya 9nov2020 Hakuna Ankara wala user request |
| Pv 2/11 | 23-Nov-20 | Malipo kwa ajili ya ununuzi wa dawa | 19,455,900.00 | | risit 2727 ya 23/11/2020, Ankara 703 za 10/11/2020. |
| Pv | 16-Dec-20 | | 19,819,300.00 | | risiti 2728 ya 10/12/2020 |
| Pv 1/1 | 20-Jan-21 | | 18,958,600.00 | | risiti 2739 ya 21/1/2021 Ankara 675 - 700 za 29/12/2020 |
| Pv 1/2 | 08-Feb-20 | | 13,000,000.00 | | risiti 0088 ya 13/2/2021 |
| | | | 21,301,700.00 | | risit 1457 ya 3/3/2021, Ankara 4722 za 21/1/2021 |
| Pv 1/3 | 09-Mar-21 | | 7,000,000.00 | | risit 1461. profoma Ankara ya 6/3/2021 |
| Pv 2/3 | 24-Mar-21 | | 10,075,600.00 | MAGOGONI PHARMACY | risiti MP2601ZNZ ya 30/3/2021 Ankara MP08681ZNZ ya 11/3/2021 |
| Pv 1/4 | 27-Apr-21 | Malipo kwa ajili ya ununuzi wa dawa | 10,000,000.00 | KARIBU PHARMACY | Hakuna risiti, hakuna Ankara, hakuna user request |
| Pv 2/5 | 11-May-20 | | 6,000,000.00 | | Risiti 1495 ya 20/5/2021 Ankara 2392-2395 za 11/5/2021. |
| | | | 6,000,000.00 | | Risiti 1611 ya 2/6/2021. |
| Pv 2/6 | | | 6,000,000.00 | | Risiti 1631 ya 4/7/2021, Ankara 2274 za 12/6/2021. |
| **Jumla** | | | **344,146,772.90** | | |

### 6.3.5.12 Malipo kwa mshauri elekezi wa upembuzi yakinifu wa ujenzi wa chelezo cha KMKM kinyume na taratibu shilingi 1,632,810,000

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Kikosi cha Kuzuia Magendo kimefanya malipo yenye jumla ya shilingi 1,632,810,000 kwa mshauri RJR GROUP SRL kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu wa ujenzi wa Chelezo cha KMKM, dosari iliyobainika ni kutokufuatwa kwa taratibu za kumpata mshauri elekezi huyo kwa mujibu wa Sheria kwa kukosekana kwa taarifa muhimu kama ifuatavyo:-

- Kukosekana kwa tangazo la kumtafuta Mshauri elekezi.
- Kukosekana kwa Kibali cha ruhusa kutoka Wizara ya Fedha
- Kutotangazwa kwa zabuni
- kukosekana kwa Ripoti ya tathmin (Evaluation Report)
- Kukosekana kwa mkataba
- Kukosekana kwa barua kutoka kwa Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar ya kuendelea na kufunga mkataba
- Kukosekana kwa barua kutoka Mamlaka ya Manunuzi inayotoa ruhusa ya kuendelea na taratibu za kuendelea na kufunga mkataba
- Kukosekana kwa Bid Security ya mtoa huduma (bank guarantee)
- Kukosekana kwa document za Wazabuni
- Kukosekana kwa report kabla ya kuanza kazi na baada ya kumaliza kazi
- Kukosekana kwa Cetifiketi kabla ya muendelezo wa malipo inayoruhusu kumlipa

Kufanya hivyo kunapelekea kukosekana kwa uwekaji wa taarifa zinazohitajika kwa matumizi ya baadae ambapo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 34(1) cha Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo kuhakikisha kwamba unasimamia ipaswavyo utayarishaji na uwekaji wa taarifa kwa ajili ya kumbu kumbu mbali mbali kwa mujibu wa Sheria, kanuni pamoja na miongozo ya fedha iliyopo kwa lengo la kuondoa uwezekano wa kuwepo kwa viashiria vya ubadhirifu wa fedha za Umma. Mchanganuo wa Malipo kwa Mshauri Elekezi kinyume na taratibui kinyume na taratibu ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 73 : Malipo kwa Mshauri Elekezi wa upembuzi yakinifu wa Ujenzi wa Chelezo cha KMKM kinyume na taratibu**

| Hati ya malipo | Aliyelipwa | Kiasi cha fedha kilicholipwa (Tshs) | Maelezo |
|---|---|---|---|
| (Dummy) | RJR GROUP SRL | 584,220,000 | Asilimia 30% ya mshauri Elekezi wa upembuzi yakinifu wa ujenzi wa chelezo cha Kmkm yenye thamani ya Euro 210,000 ( ex tzs 2,782 (malipo yote ni Euro 700,000) |
| | | 1,048,590,000 | Ikiwa ni asilimia 30% ya mwisho ya Mshauri elekezi wa upembuzi yakinifu wa Ujenzi wa Chelezo yenye thamani ya Euro 210,000 na Malipo ya **Chuo cha Mafunzo** ya Uzamiaji yenye jumla ya Euro 156,000 (**exchenge rate 2,865**) |
| **Jumla** | | **1,632,810,000** | |

### 6.3.5.12 Kutumika kwa fedha za Klabu ya michezo kinyume na taratibu shilingi 55,080,000

Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo kimefungua hesabu ya benki nambari **0405792000** (Michezo KMKM) kwa lengo la kuhifadhi mikato (michango) kutoka kwa wafanyakazi ambayo itatumika kwa

ajili ya kugharamikia shughuli zote za klabu ya michezo KMKM. Mkuu wa Utawala na Mhasibu mkuu wa KMKM ndio wenye dhamana ya hesabu hiyo.

Ukaguzi umebaini kwamba jumla ya shilingi 55,080,000 kutoka katika hesabu nambari 0405792000 (Michezo KMKM) zilitumika kwa ajili ya matumizi ya huduma za kiutawala na uendeshaji.

Aidha,taarifa za matumizi hayo hazikuainishwa katika ripoti za utekelezaji wa mpango wa manunuzi, ripoti za utekelezaji mpango kazi wala kuainishwa katika taarifa ya fedha ya mwaka, Matumizi hayo yapo nje ya mipaka iliyowekwa na Mlipaji Mkuu wa Serikali.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu namba 46(6) cha Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016. Mchanganuo wa matumizi hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini.

**Jadweli Nambari 74 : Fedha za Klabu zinazotumika kinyume na utaaratibu**

| Tarehe | Maelezo | Kiasi (Tshs) | Aliyelipwa |
|---|---|---|---|
| 08/09/2020 | Malipo kwa ajili ya ununuzi wa kofia za BOTSWANA kwa Afisa Wanafunzi - aliyelipwa ni (IHSANI GENERAL TRADERs) | 27,960,000 | MICHEZO KMKM |
| 23/09/2020 | Malipo kwa ajili ya ununuzi wa Fiber, machine 2 na Bettry 38. (AL-NABHANY AUTO MOBILE) | 27,120,000 | MICHEZO KMKM |
| **Jumla** | | **55,080,000** | |

### 6.3.5.13 Hati za malipo zilizokosekana kwa ukaguzi shilingi 1,170,874,800

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba jumla ya shilingi 1,170,874,800 zimetumika kwa ajili ya matumizi mbali mbali ya Kikosi cha kuzuia Magendo, dosari iliyobaini ni kukosekana kwa hati za malipo na vielelezo vinavyothibitisha matumizi ya fedha hizo.

Kufanya hivyo kunaweza kupelekea kuwepo kwa viashiria vya matumizi mabaya ya fedha za Umma ambapo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 34(1) cha Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016. Mchanganuo wa hati za malipo zilikosekana kwa ukaguzi ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 75 : Hati za malipo zilikosekana kwa ukaguzi**

| Hati namba | Hundi namba | Aliyelipwa | Kiasi cha fedha kilicholipwa (Tshs) | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 4/3/2021 ya 3/3/2021 | T.T | Gapco Zanzibar | 20,474,800 | Kwa ajili ya usambazaji wa Mkonga wa mawasiliano (Fibre Optic) |
| 20/7/2020 ya 29/7/2020 | T.T | Ihsan General Traders | 55,770,000 | Ununuzi wa vifaa kwa muendelezo wa Shirika la Bandari Zanzibar |
| 18/7/2020 ya 29/7/2020 | | | 20,600,000 | Muendelezo wa nyumba za Maendeleo Michenzani Block namba |
| 11/7/2020 ya 17/7/2020 | | | 17,120,000 | Muendelezo wa nyumba za maendeleo michenzani Block namba 1 |
| 15/8/2020 ya 12/8/2020 | | | 73,800,000 | Muendelezo wa ujenzi wa nyumba za Makamo wa Pili wa Rais Pagali Chake Chake Pemba |
| 18/8/2020 ya 12/8/2020 | | | 34,350,000 | Muendelezo wa nyumba ya Makamo wa Rais Pagali Chake |
| 12/7/2020 ya 17/7/2020 | | | 150,000,000 | Muendelezo wa ujenzi wa nyumba ya Makamo wa pili wa Rais Pagali Chake |
| 19/7/2020 ya 29/7/2020 | | | 50,500,000 | Muendelezo wa ujenzi wa nyumba ya Makamo wa pili wa Rais Pagali Chake |
| 4/7/2020 ya 8/7/2020 | | | 73,500,000 | Kufanya Lend scape kwenye nyumba ya makamo wa Pili chake |
| 5/7/2020 ya 8/7/2020 | | | 45,520,000 | Kufanya lend scaping katika nyumba ya makamo wa Pili |
| 3/9/2020 ya 4/9/2020 | | | 40,250,000 | Ununuzi wa vifaa kwa muendelezo wa Shirika la Bandari |
| 7/10/2020 | T.T | Mzalendo Hardware General Supplier | 125,475,000 | Muendelezo wa kazi za Ujenzi wa Shirika la Bandari Zanzibar |
| 8/9/2020 | | | 217,000,000 | Ujenzi wa Nyumba za Makamo wa Pili wa Pagali Chake Chake. |
| 12/9/2020 | | | 71,115,000 | Muendelezo wa ujenzi wa Shirika la Bandari Znz |
| 5/9/2020 | | | 175,400,000 | Muendelezo wa nyumba ya Makamo wa Pili wa Rais Pagali |
| **Jumla** | | | **1,170,874,800** | |

### 6.3.5.14 Hati za malipo zilizokosa idhini ya malipo ya Mkuu wa KMKM shilingi 291,710,000

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba jumla ya shilingi 291,710,000 zimelipwa kwa matumizi mbali mbali ya Kikosi cha Kuzuia Magendo KMKM kupitia hati za malipo mbali mbali, dosari iliyobainika na ukaguzi ni kutokuidhinishwa kwa malipo hayo katika hati za malipo husika na mkuu wa KMKM ambapo kunapelekea kutokuthibitika kwa malipo yaliyofanyika. Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016. Mchanganuo ya hati hizo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 76 : Hati za malipo zilizokosa idhini ya malipo ya mkuu wa KMKM**

| Hati namba | Hundi namba | Kiasi cha fedha kilicholipwa (Tshs) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| Pv 3/7/2020 | Ihsan General Traders | 27,380,000 | Mkuu wa KMKM | Muendelezo wa ukarabati wa nyumba za maendeleo Michenzani block no 1 |
| Pv 19/8/2020 | | 97,515,000 | | Ununuzi wa vifaa kwa muendelezo wa Ofisi ya Shirika la Bandari Zanzibar |
| Pv 20/8/2020 | | 50,600,000 | | Ununuzi wa vifaa kwa kufanya land scaping kwenye Nyumba za makamo wa pili wa Rais Pagali |
| Pv 5/8/2020 | | 71,665,000 | | Malipo ya muendelezo wa kazi za ujenzi wa nyumba Makamo wa pili wa Rais Chake chake |
| Pv 11/9/2020 | | 44,550,000 | | Fedha kwa ajili ya gharama za vifaa kwa ukarabati sehemu ya Baraza la Wawakilishi la zamani na sehemu ya ofisi ya makamo wa pili |
| **Jumla** | | **291,710,000** | | |

**KIKOSI MAALUM CHA KUZUIA MAGENDO (KMKM) – PEMBA**

### 6.3.5.16 Bidhaa ambazo hazikurikodiwa katika daftari la ghalani shilingi 9,722,480

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwa jumla ya shilingi 9,722,480 zimetumika kwa ununuzi wa bidhaa mbali mbali lakini bidhaa hizo hazikurikodiwa katika madaftari ya ghalani ili kuweza kuthibitisha uhalali wa mapokezi pamoja na matumizi ya bidhaa hizo.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 77: Bidhaa ambazo hazikurikodiwa katika daftari la ghalani**

| Hati namba | Hundi namba | Kiasi cha fedha kilicholipwa (Tshs.) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 04/05 30/04/2021 | 01534 | 760,480 | Malinge Enterprises | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya kuandikia. |
| 7/10 20/10/2020 | 289 | 6,022,000 | KMKM Pemba | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa Petrol lita 672.7 |
| 12/10 23/10/2020 | 291 | 1,800,000 | | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa chakula. |
| 14/10 26/10/2020 | 293 | 1,140,000 | | |
| **Jumla** | | **9,722,480** | | |

### 6.3.5.17 Malipo kwa watoa huduma ambao hawakusajiliwa na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma shilingi 15,487,640

Kwa mujibu wa kifungu cha 23(1) cha Sheria ya Manunuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma kinaeleza kulingana na masharti ya sheria hii mtu, kampuni au taasisi haitawasilisha zabuni au vyenginevyo kushiriki katika manunuzi ya Umma isipokua chombo kiwe kimesajiliwa na Mamlaka ya Manunuzi.

Kwa mujibu wa kifungu cha 23(2), zabuni kutoka kwa mtu, kampuni au chombo ambacho hakijasajiliwa haifai na hakitazingatiwa na taasisi ya ununuzi.

Ukaguzi umebaini kwamba Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo Pemba (KMKM) limefanya manunuzi na watoa huduma mbali mbali ambao hawakusajiliwa na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya Zanzibar.

Kufanya hivyo kunapelekea kuikosesha Serikali mapato ambapo ni kwenda kinyume na Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 78: Malipo kwa watoa huduma ambao hawakusajiliwa na mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma**

| Hati Namba | Hundi Namba | Kiasi cha fedha kilicholipwa (Tshs.) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 10/06 18/06/2021 | 01541 | 10,487,640 | Mbarouk Juma Ali | Malipo ya fedha kwa ajili ya chakula |
| 11/06 23/06/2021 | 0519 | 5,000,000 | Salim Ali Humoud na Khamis Hardware | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa vitendea kazi na ukarabati wa vituo vya afya. |
| **Jumla** | | **15,487,640** | | |

### 6.3.5.18 Hati za malipo zenye vielelezo pungufu shilingi 136,393,270

Ukaguzi umebaini kwamba jumla ya shilingi 136,393,270 zimetumika kwa matumizi mbalimbali ya Kikosi Maalumu cha Kuzuia Magendo lakini baadhi ya vielelezo havikuambatanishwa na hati za malipo ili kuweza kuthibitisha uhalali wa malipo hayo.

Kutokuambatanisha vielelezo katika hati za malipo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 34(1) cha Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 79 : Hati za malipo zenye vielelezo pungufu**

| Hati Namba | Hundi Namba | Kiasi cha fedha kilicholipwa (Tshs.) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 2/11 ya 3/11/2020 | 295 | 500,000 | KMKM Pemba | Malipo ya fedha kwa ajili ya matumizi mbali mbali |
| 01/05 ya 30/04/2021 | 0510 | 3,000,000 | | |
| 05/05 ya 12/05/2021 | 0513 | 11,782,000 | | Malipo ya fedha kwa ajili ya vitoweo kwa mabaharia. |
| 17/06 ya 7/6/2021 | 0518 | 11,332,000 | | |
| 05/09 ya 22/09/2020 | 0285 | 20,166,000 | | Malipo ya fedha kwa ajili ya mikato ya wapiganaji |
| 24/08 ya 24/08/2020 | 0282 | 18,706,500 | | |
| 04/07 ya 27/07/2020 | 0279 | 19,344,900 | | |
| 13/10 ya 26/10/2020 | 0294 | 17,594,870 | | |
| 23/12 ya 23/12/2020 | 01602 | 17,482,720 | | |
| 01/11 ya 30/11/2020 | 0299 | 16,484,280 | | |
| **Jumla** | | **136,393,270** | | |

### 6.3.6 FUNGU D 05 – KIKOSI CHA ZIMAMOTO NA UOKOZI

Ukaguzi wa hesabu za mwaka 2020/2021 kwa Kikosi cha Zimamoto na Uokozi umefanywa kwa mujibu wa Sheria, kanuni, taratibu pamoja na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Taarifa ya Mapato**

Kikosi cha Zimamoto na Uokozi Zanzibar kilikadiriwa kukusanya jumla ya shilingi 16,841,600,000 kwa mwaka wa fedha 2020/2021. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 Kikosi kilikusanya jumla ya shilingi 13,037,715,609 sawa na asilimia 77 ya makadirio.

**Taarifa ya Matumizi**

Kikosi cha Zimamoto na Uokozi Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2020/2021 kilikadiriwa kutumia jumla ya shilingi 16,841,600,000 kwa matumizi ya kazi za kawaida. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 jumla ya shilingi 13,037,715,609 zimeingizwa na kutumika kwa kazi za kawaida sawa na asilimia 77 ya makadirio.

**MATOKEO NA MAPENDEKEZO YA UKAGUZI**

#### 6.3.6.1 Kutofuatwa kwa taratibu za manunuzi ya Gari shilingi 232,996,000

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika Kikosi cha Zimamoto na Uokozi kimefanya muendelezo wa malipo kwa **Ndugu OMAR MOH'D OMAR** yenye thamani ya shilingi 71,996,000 kwa ajili ya ununuzi wa gari mbili (2) aina ya Mabasi zinazotumiwa kwa shughuli za Kikosi ambapo malipo ya awamu tatu yalilipwa kwa mwaka wa fedha 2019/2020 na kupelekea uwepo wa bakaa la fedha la shilingi 71,996,000 ambazo zinaendelea kulipwa kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

Aidha ukaguzi umebaini Kikosi cha Zimamoto na Uokozi kimefanya ununuzi mwengine wa magari mawili (2) ambayo ni aina ya **ISUZU** kwa ajili ya matumizi ya kubebea maji ya kuzimia moto na aina ya **CANTER** kwa ajili ya kubebea Askari kwa thamani ya shilingi 161,000,000 ambapo hadi ukaguzi unakamilika imebainika Kikosi cha Zimamoto na Uokozi kimemlipa **Ndugu OMAR MOH'D OMAR** jumla ya shilingi 16,150,000 na kubakia bakaa ya shilingi 144,850,000 anazozidai.

Dosari iliyobainika katika ukaguzi ni kutokutangazwa kwa zabuni pamoja na kutokupatikana kwa makubaliano ya mkataba wa ununuzi wa gari hizo, kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 65 cha Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshwaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016.

Hata hivyo ukaguzi umeshindwa kupatiwa taratibu walizokubaliana na mzabuni huyo katika ulipwaji wa fedha zinazotumika katika ununuzi wa gari hizo (Mode of payment) ambapo ukaguzi umebaini malipo hayo yanafanyika kwa kila mwezi kwa kutumia fedha za matumizi mengineyo (OC) jambo ambalo limetia shaka juu ya matumizi ya fedha hizo kutokana na kukiukwa matakwa ya muongozo nambari BLM/97/M/C.5/VOL.V/27 wa tarehe 27 Septemba 2021 kutoka Serikali uliotolewa na Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi kuwaagiza Wakuu wote wa Taasisi kuwasilisha maombi ya ununuzi wa gari kwa Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Fedha na Mipango na kuacha kununua magari yaliyotumika (Used Car) pamoja na kuacha kununua magari kwa wazabuni binafsi kwa lengo la kununua gari kwa thamani kubwa kuliko bei ya sokoni.

Hata hivyo alieleza kwa vile Serikali ina mpango wa kununua magari yatakayotumiwa na taasisi za umma kwa wingi ili kuepusha kutumia fedha za (OC) kutekeleza majukumu ya manunuzi ya magari na kupelekea kushindwa kutekeleza malengo waliyojipangia kwa mujibu wa makadirio ya bajeti.

Kufanya manunuzi kinyume na matoleo ya Serikali kunapelekea taasisi ya umma kutumia gharama kubwa ya ununuzi unaotokana na wazabuni kuwauzia Serikali magari kwa gharama kubwa ukilinganisha na bei ya soko ilivyo.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 65 cha Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshwaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Kikosi cha Zimamoto na Uokozi kuhakikisha unatekeleza miongozo inayotolewa na Serikali ili kuepusha kutumia fedha za umma kinyume na utaratibu. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 80: Kutofuatwa kwa taratibu za manunuzi ya gari**

| Hati Namba | Kiasi (Tshs) | Maelezo | Vielelezo vilivyothibitisha malipo kufanyika |
|---|---|---|---|
| **Malipo kwa ajili ya ununuzi wa Mabasi mawili** | | | |
| R8/8/2020 ya 08/01/2020 | 24,600,000 | Malipo ya **nne** ya ununuzi wa gari za kusafirishia maafisa na askari agost 2020. | Risiti namba 705 ya 5/8/2020 |
| R21/9/2020 ya 30/9/2020 | 19,680,000 | Malipo ya **tano** ya ununuzi wa gari za kusafirishia maafisa na askari wa kzu kwa mwezi sept 2020 | Risiti namba 707 ya 7/9/2020 |
| R23/10/2020 ya 26/10/2020 | 9,840,000 | Malipo ya **sita** ya ununuzi wa gari za kusafirishia maafisa na askari kwa mwezi oct. 2020. | Risiti namba 715 ya 29/10/2020 |
| R6/11/2020 ya 18/11/2020 | 12,300,000 | Malipo ya **saba** ya ununuzi wa gari | Risiti namba 729 ya 23/11/2020 |
| R19/12/2020 ya 19/12/2020 | 5,576,000 | Malipo ya **nane** ya ununuzi wa gari. | Risiti ya 726 ya 22/12/2020 |
| **Jumla Ndogo (A)** | **71,996,000** | | |
| **Malipo kwa ajili ya ununuzi wa ISUZU na CANTER** | | | |
| 5/1/2021 | 16,150,000 | Malipo ya awali ya ununuzi wa gari aina ya Isuzu na Canter. | - |
| **Jumla Ndogo (B)** | **16,150,000** | | |
| **Bakaa la Deni (C)** | **144,850,000** | | |
| **Jumla Kuu (A+B+C)** | **232,996,000** | | |

### 6.3.6.2 Kukosekana kwa Mkataba wa ununuzi wa mafuta (Framework Contract) wenye jumla ya shilingi 205,524,671

Katika kupitia hati za malipo pamoja na taarifa mbali mbali za utendaji wa Kikosi cha Zimamoto na Uokozi, ukaguzi umebaini ya kwamba Kikosi cha Zimamoto na Uokozi wananunua mafuta ya **Petrol** na **Diesel** kutoka kwa kampuni ya UNITED GROUP LTD kwa ajili ya kuendesha shughuli zao za kila siku za Ofisi bila ya kuwa na makubaliano ya kisheria (Mkataba), kufanya manunuzi katika taasisi za serikali bila ya kuwa na makubaliano ya kisheria ni kwenda kinyume na kifungu nambari 29(m) na kifungu nambari 42(2)(b) cha Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016.

Kukosekana kwa mkataba wa ununuzi wa mafuta kunaweza kuapelekea kuathiri shughuli za Kikosi endapo kutatokezea kutofautiana baina ya Kikosi cha Zimamoto na Uokozi na watoa huduma hizo muhimu.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Kikosi cha Zimamoto na Uokozi kuandaa mkataba kwa ajili ya kuepuka migogoro endapo ikijitokeza ili kuweka usawa pande zote mbili kati yao. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama yanavyoonekena katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 81: Malipo kwa ajili ya Ununuzi wa Mafuta**

| Hati namba | Ankara namba | Aliyelipwa | Kiasi (Tshs.) |
|---|---|---|---|
| **Ununuzi wa Mafuta ya Petroli** | | | |
| 16/07/2020 | 0281 ya 27/07/2020 | Kijangwani Petr.Station | 1,000,000 |
| 2//08/2020 | 3129 ya 30/07/2020 | United Group Ltd | 3,115,878 |
| 16/09/2020 | 3246 ya 15/09/2020 | | 2,703,000 |
| 28/10/2020 | 3338 ya 26/10 | | 1,454,400 |
| 2/11/2020 | 3366 ya 18/11 | | 1,478,400 |
| 20/12/2020 | 3411 ya 14/12 | | 2,174,400 |
| 3/01/2021 | 3468 ya 11/01/2021 | | 2,138,400 |
| 5/02/2021 | 3517 ya 3/02/2021 | | 4,455,000 |
| 3/04/2021 | 3604 ya 15/03/2021 | | 4,815,000 |
| 1/5/2021 | 3741 ya 3/05/2021 | | 5,162,500 |
| 34/6/2021 | 3865 ya 29/06/2021 | | 4,999,944 |
| **Jumla ndogo** | | | **33,496,922** |
| **Ununuzi wa Mafuta ya Diesel** | | | |
| 20/12/2020 | 3411 ya 14/12/2020 | United Group Ltd Diesel | 10,823,960 |
| 28/10/2020 | 3338 ya 26/10/2020 | | 8,543,944 |
| 2/11/2020 | 3366 ya 18/11/2020 | | 706,400 |
| 34/06/2021 | 3865 ya 29/06/2021 | | 4,998,882 |
| 2/08/2020 | 3129 ya 30/07/2020 | | 14,883,500 |
| 16/07/2020 | 0281 ya 27/07/2020 | Kijangwani Pet.Station | 3,000,000 |
| 5/02/2021 | 3517 ya 3/02/2021 | United Group Ltd Diesel | 14,696,500 |
| 28/10/2020 | 3338 ya 26/20/2021 | | 8,543,944 |
| 3/04/2021 | 3604 ya 15/03/2021 | | 15,528,000 |
| 1/5/2021 | 3741 ya 3/05/2021 | | 854,128 |
| | 3740 ya 3/05/2021 | | 16,192,000 |
| 34/6/2021 | 3865 ya 29/06/2021 | | 4,998,882 |
| 5/2/2021 | 3517 ya 3/02/2021 | | 14,696,500 |
| 3/01/2021 | 3468 ya 11/01/2021 | | 9,860,487 |
| 5/09/2020 | 3221 ya 4/09/2020 | | 13,873,860 |
| 16/09/2020 | 3246 ya 15/09/2020 | | 15,296,402 |
| 16/07/2020 | 0281 ya 27/07/2020 | | 3,000,000 |
| 02/11/2020 | 3366 ya 18/11/2020 | | 706,400 |
| 20/12/2020 | 3411 ya 14/12/2020 | | 10,823,960 |
| **Jumla Ndogo** | | | **172,027,749** |
| **Jumla Kuu** | | | **205,524,671** |

### 6.3.6.3 Kutokufuatwa kwa taratibu za manunuzi ya Compressor shilingi 236,000,000 na ujenzi wa Mahanga shilingi 700,000,000

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika Kikosi cha Zimamoto na Uokozi kimefanya malipo kwa **HIFFAH GENERAL TRADING CO.** yenye thamani ya shilingi 236,000,000 kwa ajili ya ununuzi wa Compressor kwa matumizi ya shughuli za Kikosi ambapo malipo ya awamu mbili zilizopita yalilipwa kwa mwaka wa fedha 2019/2020 na kubainika kwa mwaka wa fedha 2020/2021 Kikosi cha Zimamoto na Uokozi kimeendelea kulipa kupitia hati namba 27/10/2020 kupitia hundi namba TISS yenye thamani ya shilingi 14,250,000 ikiwa ni malipo ya awamu ya tatu kwa ajili ya ununuzi wa compressor.

Aidha ukaguzi umebaini Kikosi cha Zimamoto na Uokozi kimefanya ununuzi mwengine wa vifaa vya ujenzi kwa thamani ya shilingi 700,000,000 kwa mujibu wa makubaliano ya mkataba ambapo hadi ukaguzi unakamilika imebainika Kikosi cha Zimamoto na Uokozi kimemlipa **Ndugu JUMA FOUM MCHA** jumla ya shilingi 71,583,272.

Dosari iliyobainika katika ukaguzi ni kutokutangazwa kwa zabuni pamoja na kutokupatikana kwa makubaliano ya mkataba wa ununuzi wa vifaa vya ujenzi pamoja na compressor, kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 65 cha Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshwaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016.

Hata hivyo ukaguzi umeshindwa kupatiwa taratibu walizokubaliana na mzabuni huyo katika ulipwaji wa fedha zinazotumika katika ununuzi wa vifaa pamoja na compressor (Mode of payment) ambapo ukaguzi umebaini malipo hayo yanafanyika kwa kila awamu kwa kutumia fedha za matumizi mengineyo (OC) jambo ambalo limetia shaka juu ya matumizi ya fedha hizo kutokana mtiririko wa malipo yanayofanyika kwa awamu.

Kufanya malipo kwa awamu pasi na kujulikana makubaliano ya mikataba yanayopelekea kufanyika malipo kwa awamu na kutokujulikana malipo hayo yatalipwa kwa awamu ngapi (Mode of Payment) kunapelekea taasisi ya umma kutumia gharama kubwa ya ununuzi unaotokana na wazabuni kuwauzia Serikali vifaa kwa gharama kubwa ukilinganisha na bei ya soko ilivyo.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 65 cha Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshwaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Kikosi cha Zimamoto na Uokozi kuhakikisha unatekeleza miongozo inayotolewa na Serikali ikiwemo kufanya malipo kwa mujibu wa mpango wa manunuzi ili kuepusha kutumia fedha za matumizi mengineyo (OC) kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo (Ujenzi wa Mahanga ya Chanjaani – Pemba) kinyume na utaratibu. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 82 : Kutofuatwa kwa taratibu za manunuzi ya vifaa vya ujenzi wa Mahanga Chanjaani – Pemba na ununuzi wa Compressor**

| Hati Namba | Kiasi (Shs) | Alielipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|
| **Malipo kwa ajili ya ununuzi wa Compressor** | | | |
| 27/10/2020 | 14,250,000 | Hiffah General Trading Co. | Malipo ya awamu ya tatu ya ununuzi wa Compressor. |
| **Jumla** | **14,250,000** | | |
| **Malipo kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya Ujenzi wa Mahanga** | | | |
| Pv 13/03/2021 | 16,150,000 | Juma Foum Mcha | Malipo ya ununuzi wa vifaa vya Ujenzi wa Mahanga |
| Pv 06/04/2021 | 2,233,272 | | |
| Pv 17/12/2020 | 7,125,000 | | |
| Pv 18/10/2020 | 8,550,000 | | |
| Pv 15/09/2020 | 14,250,000 | | |
| Pv 22/08/2020 | 12,825,000 | | |
| Pv 03/07/2020 | 12,350,000 | | |
| **Jumla** | **71,583,272** | | |

### 6.3.6.4 Hati za malipo zenye vielelezo pungufu shilingi 90,302,514

Ukaguzi umebaini kwamba jumla ya shilingi 90,302,514 zimetumika kwa malipo mbali mbali ya Kikosi cha Zimamoto na Uokozi, dosari iliyobainika na ukaguzi ni kutokuambatanishwa hati za malipo na vielelezo husika ili kuweza kuthibitisha uhalali wa malipo hayo.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 34(1) cha Sheria Nambari 12 ya Ukaguzi unashauri uongozi wa Kikosi cha Zimamoto na Uokozi kuhakikisha unafanya manunuzi na kuambatanisha vielelezo vyote katika hati za malipo kwa mujibu wa taratibu na sheria za fedha. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 83 : Malipo yenye vielelezo pungufu**

| Hati Namba | Kiasi (shs) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|
| 25/03/2021 | 3,340,000 | Kamishna Zimamoto na Uokozi | Malipo ya uzalishaji posho mbali mbali. |
| 30/04/2021 | 28,048,500 | | |
| 02/07/2020 | 1,100,000 | | |
| 02/07/2020 | 2,000,000 | | Malipo ya makusanyo ya mapato |
| 14/12/2020 | 6,162,807 | | Malipo ya wanachama wa Askari wanachama wa ZSSF. |
| 31/10/2020 | 6,162,807 | | |
| 23/09/2020 | 18,488,400 | | |
| 26/08/2020 | 3,000,000 | Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Fedha za Mipango | malipo ya makusanyo ya mapato |
| 12/10/2020 | 2,000,000 | | |
| 14/09/2020 | 1,000,000 | | |
| 13/11/2020 | 1,000,000 | | |
| 14/08/2020 | 7,000,000 | Kamishna Zimamoto na Uokozi | |
| 14/08/2020 | 1,000,000 | Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Fedha za Mipango | |
| 14/12/2020 | 5,000,000 | Kamishna Zimamoto na Uokozi | Matumizi ya fedha kwa shughuli mbali mbali za Kikosi |
| 04/09/2020 | 2,500,000 | | |
| 04/09/2020 | 2,500,000 | | |
| **Jumla** | **90,302,514** | | |

**KIKOSI CHA ZIMAMOTO NA UOKOZI - PEMBA**

### 6.3.6.5 Uhamisho wa kikazi kwa Wapiganaji wa Kikosi cha Zimamoto na Uokozi

Kwa mujibu wa kifungu nambari 89(1)(2)(3) cha Kanuni ya Utumishi wa Umma ya mwaka 2014 kinatoa maelekezo kwa mtumishi yoyote atakaepewa uhamisho kutoka Unguja kwenda Pemba, Tanzania Bara au kinyume chake atapaswa kulipwa Posho la Usumbufu litakalokuwa sawa na posho la siku saba pamoja na usafiri wa ndani wa kufidia usumbufu atakao upata katika kutekeleza amri hiyo ya uhamisho. Aidha, kwa madhumuni ya kifungu kidogo cha kwanza na cha pili ya kanuni hii mtumishi huyo atastahiki kugharamiwa uhamishaji wa familia na mizigo yake.

Kwa mujibu wa kifungu nambari 60(g) cha Kanuni ya Tume ya Utumishi ya Idara Maalum za SMZ kinaeleza "Posho la usumbufu ambalo litafungamana na uhamisho wa kutoka Unguja kwenda Pemba au kinyume chake la asilimia 25 ya mshahara".

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Kikosi cha Zimamoto na Uokozi  Pemba kimefanya uhamisho wa kikazi kwenda Unguja kwa wapiganaji wake mbali mbali, dosari ya kiutumishi iliyobainika ni kutokutekelezeka kwa vifungu nilivyoviainisha hapo juu  kutokana na kukosekana kwa vielelezo mbali mbali vilivyothibitisha upokeaji wa stahiki za malipo yatokanayo na shughuli ya uhamishaji wa familia na mizigo kwa mujibu wa utaratibu.

Kuwakosesha stahiki za uhamisho kwa wapiganaji hao kunaweza kupelekea kupunguza hamasa ya ufanyaji wa kazi na hatimae kujitokeza kwa malalamiko ya chini kwa chini ambayo hupelekea kuondoa imani kwa wakuu wa Vikosi vya ulinzi na Usalama.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Vikosi vya Ulinzi na Usalama kuhakikisha unatekeleza kikamilifu maagizo ya kanuni za Utumishi wa Umma pamoja na kanuni za Idara Maalum za Vikosi vya SMZ kwa lengo la kuondosha migongano na migogoro kwa wapiganaji makazini. Mchanganuo wa wapiganaji hao ni kama unavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 84 : Orodha ya Wapiganaji waliohamishwa kikazi bila ya kufanyiwa malipo**

| Namba | Jina la mpiganaji | Namba | Jina la mpiganaji |
|---|---|---|---|
| 1 | F.997 ASP Kombo Hakim Makame | 27 | F.1945 SGT Mfaume Fakih  Haji |
| 2 | F.998 ASP Machano Silima Bakili | 28 | F. 1285 CPL Bakar Khamis Bakar |
| 3 | F.1106 ASP Moh'd Ali Haji | 29 | F.1371 CPL Haji Omar Mwadin |
| 4 | F.1113 ASP Oar Juma Ali Haji | 30 | F.1382 CPL  Zired Khalisa Juma |
| 5 | F.1287 ASP Khatb Moh'd Mussa | 31 | F.1420 CPL Ali Omar Abdisalami |
| 6 | F.1010 INSP Ali Sufiani Ali | 32 | F.1431 CPL Mariyam Juma Ali |
| 7 | F.1169 INSP Hussein Nyange Khamis | 33 | F.1450 CPL Haji Omar Silima |
| 8 | F.1181 INSP Bakar Haji  Simai | 34 | F.1469 CPL  Hassan Vuai Ame |
| 9 | F.1490 INSP Yussuf Khamis Abdalla | 35 | F.1477 CPL Salha Idrisa Mudi |
| 10 | F.1206 S/SGT Haji Makame Haji | 36 | F.1482 CPL Miza Said Machano |
| 11 | F.1297 S/SGT Badru Juma Kassim | 37 | F.1485 CPL Asha Abrahman Mbao |
| 12 | F.1218 SGT Bimkubwa Khamis Juma | 38 | F.1492 CPL Mbaraka Suleiman |
| 13 | F.1231 SGT Haji Simai Haji | 39 | F.1507 CPL Ujudi Abdalla Khamis |
| 14 | F.1235 SGT Hussein Abeid Omar | 40 | F.1513 CPL Sharif Swala Shaame |
| 15 | F.1273 SGT Miraji Sinahayo Nyendo | 41 | F.1538 CPL Issa Said Ali |
| 16 | F.1274 SGT Bahati Abdalla Faki | 42 | F.1604 CPL Angela Modest  Benecict |
| 17 | F.1406  SGT Ziada Soud Husein | 43 | F.1999 CPL Rashid Abdalla Omar |
| 18 | F.1430 SGT Kheir Ibrahim  Is –Haka | 44 | F.1795  F/M Abdul-Latif  Duchi |

| Namba | Jina la mpiganaji | Namba | Jina la mpiganaji |
|---|---|---|---|
| 19 | F.1455 SGT Kiuwa Ali Makame | 45 | F.1805 F/M Ali Ameir Ali |
| 20 | F.1474 SGT Khamis Ubwa Ali | 46 | F.1856 F/M Hamid Abdalla Hamid |
| 21 | F.1475 SGT Haji Omar Jecha | 47 | F.1878 F/M Iddi Jongo Ali |
| 22 | F. 1499 SGT Shani Rajab Maarifa | 48 | F.1888 F/M Jaku Ame Kiroja |
| 23 | F.1632 SGT Soud Hassan Ali | 49 | F.1926 F/M Kheir Haji Foum |
| 24 | F.1696 SGT Nassor Mussa Abdalla | 50 | F.1983 F/M Nassir Issa Ali |
| 25 | F.1719 SGT Omar Saleh Juma | 51 | F.2027 F/M Sini Khamis Haji |
| 26 | F.1892 SGT Jina Ali Hamid | 52 | F.1917 F/M Khamis Machano Jape |

### 6.3.6.6 Hati za malipo zenye vielelezo pungufu shilingi 102,441,300

Ukaguzi umebaini kwamba jumla ya shilingi 102,441,300 zimetumika kwa matumizi mbalimbali ya Kikosi cha Zimamoto na Uokozi Pemba lakini baadhi ya vielelezo havikuambatanishwa na hati za malipo ili kuweza kuthibitisha uhalali wa malipo hayo.

Kutokuambatanisha vielelezo katika hati za malipo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 34(1) cha Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 85: Hati za malipo zenye vielelezo pungufu**

| Hati Namba | Hundi Namba | Kiasi cha fedha kilicholipwa (Tshs.) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 6/7 ya 24/07/2020 | - | 16,671,600 | Mkuu wa KZU Pemba. | Malipo ya fedha kwa ajili ya mikato mbali mbali |
| 9/10 ya 26/10/2020 | 000756 | 17,394,700 | | |
| 07/12 ya 23/12/2020 | 000772 | 17,238,500 | | |
| 6/9 ya 24/09/2020 | 000947 | 16,339,300 | | |
| 8/8 | 000732 | 18,042,700 | | |
| 1/12 ya 01/12/2020 | 000767 | 16,754,500 | | |
| **Jumla** | | **102,441,300** | | |

### 6.3.6.7 Dosari katika Ujenzi wa Hanga la Wapiganaji

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwepo kwa ujenzi wa hanga la wapiganaji wa Kikosi cha Zimamoto - Chanjaani lakini imebainika kuwepo kwa dosari mbali mbali katika ujenzi wa hanga hilo kama ifuatavyo:-

- Kukosekana kwa uthibitisho wa vikao vya maamuzi ya kufanyika kwa ujenzi
- Kutokuwepo kwa bajeti maalumu iliyoandaliwa kwa ajili ya ujenzi huo.
- Kutokubainishwa kwa muda wa kuanza na kukamilika kwa ujenzi.
- Kukosekana kwa Bill of Quantity (B.O.Q) pamoja na mchoro wa jengo ambapo kunaweza kupelekea kukosekana kwa viwango vya ubora na thamani halisi ya ujenzi.
- Kutokujulikana kwa thamani ya fedha iliyotumika tokea kuanza kwa ujenzi hadi hatua lilipofikia.
- Kukosekana kwa kumbukumbu zinazohusiana na ujenzi huo.
- Kusita kwa ujenzi wa hanga ambapo kunawea kupelekea kuharibika kwa hanga hilo na hatimae kupelekea upotevu wa fedha za umma.

Kufanya hivyo kunaweza kupelekea matumizi yasiyoridhisha ya fedha za umma ambapo ni kwenda kinyume na Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa fedha za Umma ya mwaka 2016.

### 6.3.7 FUNGU D 06 - KIKOSI CHA VALANTIA (KVZ)

Ukaguzi wa hesabu za mwaka 2020/2021 kwa Kikosi cha Valantia umefanywa kwa mujibu wa Sheria, kanuni, taratibu pamoja na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Taarifa ya Mapato**

Kikosi cha Valantia Zanzibar kilikadiriwa kukusanya jumla ya shilingi 20,135,000,000 kwa mwaka wa fedha 2020/2021. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 Kikosi kilikusanya jumla ya shilingi 17,965,270,061 sawa na asilimia 89 ya makadirio.

**Taarifa ya Matumizi**

Kikosi cha Valantia Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2020/2021 kilikadiriwa kutumia jumla ya shilingi 21,073,690,000 kwa matumizi ya kazi za kawaida na Maendeleo. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 jumla ya shilingi 17,965,270,061 zilitumika kwa kazi za kawaida na kazi za maendeleo sawa na asilimia 85 ya makadirio.

**MATOKEO NA MAPENDEKEZO YA UKAGUZI**

#### 6.3.7.1 Malipo kwa watoa huduma ambao hawakusajiliwa na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma shilingi 538,813,156

Kwa mujibu wa kifungu cha 23(1) cha Sheria ya Manunuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma kinaeleza kulingana na masharti ya sheria hii mtu, kampuni au taasisi haitawasilisha zabuni au vyenginevyo kushiriki katika manunuzi ya Umma isipokua chombo kiwe kimesajiliwa na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma.

Kwa mujibu wa kifungu cha 23(2), zabuni kutoka kwa mtu, kampuni au chombo ambacho hakijasajiliwa haifai na hakitazingatiwa na taasisi ya ununuzi.

Ukaguzi umebaini kwamba Kikosi cha Valantia (KVZ) kimefanya manunuzi na watoa huduma mbali mbali ambao hawakusajiliwa na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya Zanzibar.

Aidha, ukaguzi umebaini Kikosi cha Valantia kimefanya manunuzi kwa Mtoa huduma aitwae **Magomeni Jitini** aliyesajiliwa kwa ajili ya usambazaji na uuzaji wa Vipuri vya vyombo vya moto (Spare Parts).

Dosari iliyobainika na kutia shaka ukaguzi ni kwamba Kikosi cha Valantia kimenunua chakula kwenye duka la uuzwaji wa vipuri jambo ambalo limetia shaka juu ya uhalali wa matumizi hayo.

Kufanya hivyo kunapelekea kuikosesha Serikali mapato ambapo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 23(1) cha Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 86 : Malipo kwa watoa huduma ambao hawakusajiliwa**

| Hati namba | Hundi namba | Aliyelipwa | Thamani (Tshs) | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| Pv 3/7/2020 | T.T | Magomeni Jitini | 43,350,168 | Ununuzi wa chakula cha Askari |
| Pv 11/10/2020 | T.T | | 12,782,608 | Ununuzi wa vifaa vya ujenzi. |
| PV 9/8/2020 | T.T | | 42,241,110 | Ununuzi wa Chakula cha Askari. |
| Pv 2/9/2020 | T.T | | 42,836,835 | |
| Pv 52/10/2020 | T.T | | 41,230,305 | |
| Pv 10/10/2020 | T.T | | 35,172,200 | |
| Pv 45/10/2020 | T.T | | 39,547,768 | |
| Pv 12/10/2020 | T.T | | 4,285,000 | Ununuzi wa vifaa vya mazoezi. |
| Pv 9/11/2020 | T.T | | 35,452,952 | Ununuzi wa chakula cha Askari. |
| Pv 3/1/2021 | T.T | | 1,563,080 | |
| Pv 11/2/2021 | T.T | | 56,213,228 | |
| Pv 3/3/2021 | T.T | | 56,213,228 | |
| Pv 8/10/2020 | CASH | | 315,000 | |
| Pv 1/4/2021 | T.T | | 63,804,837 | |
| Pv 1/5/2021 | T.T | | 63,804,837 | |
| Pv 1/6/2021 | T.T | | 64,078,273 | |
| Pv 24/4/2021 | T.T | | 6,817,391 | Ununuzi wa vifaa vya jikoni. |
| Pv 3/11/2020 | T.T | | 2,000,000 | Ununuzi wa vifaa vya michezo. |
| Pv 24/6/2021 | CASH | | 12,303,000 | Ununuzi wa vifaa vya michezo. |
| Pv 7/5/2021 | Kamanda Mkuu | | 3,191,000 | Ununuzi wa vifaa vya jikoni. |
| **Jumla** | | | **538,813,156** | |

Ukaguzi unashauri uongozi wa Kikosi cha Valantia kufuata Sheria kikamilifu katika kutekeleza majukumu yake.

**KIKOSI CHA VALANTIA - PEMBA**

**Hesabu ya Matumizi ya Kawaida**

### 6.3.7.2 Hati za malipo zenye vielelezo pungufu shilingi 34,996,000

Kwa mujibu wa kumbu kumbu ya hati za malipo namba 4/10 ya tarehe 05/10/2020 kupitia hundi namba 000489 yenye thamani ya shilingi 34,996,000 aliyolipwa Kikosi cha Valantia kwa ajili ya malipo ya fidia ya vijana waliojenga nyumba za kuishi katika eneo la Kambi Micheweni.

Ukaguzi umebaini malipo hayo yamefanyika bila ya kuambatanisha vilelezo husika kwenye hati ya malipo ili kuweza kuthibitisha uhalali wa malipo hayo. Kutokuambatanisha vielelezo katika hati za malipo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 34(1) cha Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa fedha za Umma ya mwaka 2016.

### 6.3.7.3 Malipo yaliyofanywa kwa njia ya fedha taslimu shilingi 4,000,000

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwa jumla ya shilingi 4,000,000 zimelipwa kwa ajili ya matumizi mbali mbali ya Kikosi Cha Valantia Pemba ambapo malipo hayo yamefanyika kwa mujibu wa hati namba 09/10 ya tarehe 23/10/2020 yenye thamani ya shilingi 3,000,000 iliyolipwa kwa hundi namba 000493 pamoja na hati namba 11/10 ya taehe 29/10/2020 yenye thamani ya shilingi 1,000,000 ambayo imelipwa kwa hundi namba 000495.

Dosari iliyobainika katika ukaguzi ni kufanyika kwa malipo hayo kwa fedha taslimu jambo ambalo linapelekea kuikosesha Serikali mapato.

Kufanya hivyo kwenda kinyume na Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016.

#### 6.3.7.4 Uhamisho wa kikazi kwa Wapiganaji wa Kikosi cha Valantia Pemba

Kwa mujibu wa kifungu nambari 89(1)(2)(3) cha Kanuni ya Utumishi wa Umma ya mwaka 2014 kinatoa maelekezo kwa mtumishi yoyote atakaepewa uhamisho kutoka Unguja kwenda Pemba, Tanzania Bara au kinyume chake atapaswa kulipwa Posho la Usumbufu litakalokuwa sawa na posho la siku saba pamoja na usafiri wa ndani wa kufidia usumbufu atakao upata katika kutekeleza amri hiyo ya uhamisho. Aidha, kwa madhumuni ya kifungu kidogo cha kwanza na cha pili ya kanuni hii mtumishi huyo atastahiki kugharamiwa uhamishaji wa familia na mizigo yake.

Kwa mujibu wa kifungu nambari 60(g) cha Kanuni ya Tume ya Utumishi ya Idara Maalum za SMZ kinaeleza "Posho la usumbufu ambalo litafungamana na uhamisho wa kutoka Unguja kwenda Pemba au kinyume chake la asilimia 25 ya mshahara".

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Kikosi cha Valantia Pemba kimefanya uhamisho wa kikazi kwenda Unguja kwa wapiganaji wake mbali mbali, dosari ya kiutumishi iliyobainika ni kutokutekelezeka kwa vifungu nilivyoviainisha hapo juu kutokana na kukosekana kwa vielelezo mbali mbali vilivyothibitisha upokeaji wa stahiki za malipo yatokanayo na shughuli ya uhamishaji wa familia na mizigo kwa mujibu wa utaratibu.

Kuwakosesha stahiki za uhamisho kwa wapiganaji hao kunaweza kupelekea kupunguza hamasa ya ufanyaji wa kazi na hatimae kujitokeza kwa malalamiko ya chini kwa chini ambayo hupelekea kuondoa imani kwa wakuu wa Vikosi vya ulinzi na Usalama.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Vikosi vya Ulinzi na Usalama kuhakikisha unatekeleza kikamilifu maagizo ya kanuni za Utumishi wa Umma pamoja na kanuni za Idara Maalum za Vikosi vya SMZ kwa lengo la kuondosha migongano na migogoro kwa wapiganaji makazini. Mchanganuo wa wapiganaji hao ni kama unavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 87 : Orodha ya wapiganaji waliohamishwa kikazi bila ya kufanyiwa malipo**

| Namba | Jina la Mpiganaji | Namba | Jina la Mpiganaji |
|---|---|---|---|
| 1 | AV 0016 CAPT V A Abass | 24 | MV 1466 PTE Yussuf M. Silima |
| 2 | AV 0022 CAPT J A Makwaya | 25 | MV 1501 PTE Abdul-Kadir Malik |
| 3 | AV 0026 CAPT H Kh Ali | 26 | MV 1504 PTE Abdulla Ali Haji |
| 4 | AV 0033 CAPT J Ch Masanja | 27 | MV 1511 PTE Abdul-Malik Juma |
| 5 | AV 0035 CAPT M F Hamad | 28 | MV 1515 PTE Abdul-Rahim Moh'd |
| 6 | AV 0038 CAPT H R Makame | 29 | MV 1517 PTE Juma Moh'd Juma |
| 7 | MV 0228 WOI Shoka Khatib Juma | 30 | MV 1546 PTE Ali Hamad Ali |
| 8 | MV 0162 WOI Sadi Ussi Khamiss | 31 | MV 1649 PTE Ali Hassan Pandu |
| 9 | MV 0146 S/SGT Amour Ali Amour | 32 | MV 1733 PTE Juma Maziku Ngula |
| 10 | MV 0194 SGT Khamis A. Hassan | 33 | MV 1826 PTE Maulid Husein |
| 11 | MV 0182 SGT Ibrahim Moh'd | 34 | MV 1818 PTE Makame Mussa Ali |
| 12 | MV 0537 SGT Akida Masoud Akida | 35 | MV 1879 PTE Nicolaus Peter |
| 12 | MV 0493 CPL Haji Ali Haji | 36 | MV 1899 PTE Othman Ali Amour |
| 14 | MV 1139 CPL Othman Iddi Khamis | 37 | MV 1920 PTE Rashid Juma Omar |
| 15 | MV 0584 CPL Himid Makame Vuai | 38 | MV 1937 PTE Shauri Ali Shauri |
| 16 | MV 0780 CPL Shaib Mtumwa Haji | 39 | MV 1974 PTE Talib Mbaraka |
| 17 | MV 1020 PTE Thobias Yohana | 40 | MV 2017 PTE Zubeir Juma Rashid |
| 18 | MV 1333 PTE Ali Choum Juma | 41 | MV 0203 PTE Yussuf Haji Juma |
| 19 | MV 1386 PTE Juma Said Maalim | 42 | MV 1616 PTE Fuom Haji Foum |
| 20 | MV 1389 PTE Juma Zaid Juma | 43 | MV 0308 PTE Mahmoud Gharib |
| 21 | MV 1416 PTE Makame Haji Khamis | 44 | MV 1713 PTE Juma Makame S |
| 22 | MV 0980 PTE Ibrahim Makame | 45 | MV 1605 PTE Faki Hassan Issa |
| 23 | MV 1500 PTE Abdul-Hamid Haji | | |

### 6.3.7.5 Vifaa ambavyo havikurikodiwa katika daftari la ghalani shilingi 3,500,000

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwa jumla ya shilingi 3,500,000 zimelipwa kwa bwana Salum Hamdan kupitia hati namba 01/04 ya tarehe 27/04/2021 kwa hundi namba 00076 kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya ujenzi, hata hivyo imebainika kuwa vifaa hivyo havikurikodiwa katika daftari la ghalani ili kuweza kuthibitisha uhalali wa mapokezi pamoja na matumizi ya vifaa hivyo. Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016.

### 6.3.7.6 Malipo kwa watoa huduma ambao hawakusajiliwa na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma shilingi 6,500,000

Kwa mujibu wa kifungu cha 23(1) cha Sheria ya Manunuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma kinaeleza kulingana na masharti ya sheria hii mtu, kampuni au taasisi haitawasilisha zabuni au vyenginevyo kushiriki katika manunuzi ya Umma isipokua chombo kiwe kimesajiliwa na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma.

Kwa mujibu wa kifungu cha 23(2), zabuni kutoka kwa mtu, kampuni au chombo ambacho hakijasajiliwa haifai na hakitazingatiwa na taasisi ya ununuzi.

Ukaguzi umebaini kwamba Kikosi cha Valantia kimefanya manunuzi na watoa huduma mbali mbali ambao hawakusajiliwa na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya Zanzibar.

Kufanya hivyo kunapelekea kuikosesha Serikali mapato ambapo ni kwenda kinyume na Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016.

Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 88 : Malipo kwa watoa huduma ambao hawakusajiliwa na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma**

| Hati Namba | Hundi Namba | Fedha Zilizolipwa (Tshs.) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 61/07 7/10/2020 | 00067 | 3,000,000 | Khamis Khalfan | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya ujenzi |
| 01/01 18/01/2021 | 00072 | 3,500,000 | RSM Korea Timber & Hardware | |
| **Jumla** | | **6,500,000** | | |

### 6.3.8 FUNGU D 07 – MKOA WA MJINI MAGHARIBI

Ukaguzi wa hesabu za Mkoa wa Mjini Magharibi kwa mwaka wa fedha 2020/2021 umefanywa kwa kuzingatia sheria,kanuni,taratibu na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Taarifa ya Mapato**

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021 Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi ilikadiriwa kukusanya jumla ya shilingi 125,000,000 kutoka katika vyanzo vyake vya ndani. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 jumla ya shilingi 60,309,000 zilikusanywa sawa na asilimia 48.24 ya makadirio.

**Taarifa ya Matumizi**

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021 Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi ilikadiriwa kutumia jumla ya 38,276,405,345. Kati ya hizo shilingi 38,082,003,845 kutoka Serikali kuu na jumla ya shilingi 194,401,500 zilitarajiwa kutoka kwa washirika wa maendeleo.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni,2021 jumla ya shilingi 34,941,308,520 zilitumika, kati ya hizo shilingi 34,746,907,020 kutoka Serikalini na shilingi 194,401,500 kutoka kwa washirika wa Maendeleo.

### 6.3.9 FUNGU D08 - MKOA WA KUSINI UNGUJA

Ukaguzi wa hesabu za mwaka 2020/2021 kwa Mkoa wa Kusini Unguja umefanywa kwa mujibu wa Sheria, kanuni, taratibu pamoja na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Taarifa ya Mapato**

Mkoa wa Kusini Unguja kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ulikadiriwa kukusanya jumla ya shilingi 15,748,952,435. Kati ya hizo jumla ya shilingi 50,750,000 zilikadiriwa kukusanywa kutoka vyanzo vya ndani vya Mkoa, jumla ya shilingi 15,698,202,435 zilikadiriwa kupatikana kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina ikiwa ni ruzuku.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 jumla ya shilingi 13,646,908,014 zilipokelewa ikiwa sawa na asilimia 86.65 ya makadirio, kati ya hizo jumla ya shilingi 34,458,500 zilipokelewa kutoka vyanzo vya ndani vya Mkoa sawa na asilimia 68 ya makadirio, jumla ya shilingi 13,612,449,514 zilipatikana kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina sawa na asilimia 86.7 ya makadirio.

**Taarifa ya Matumizi**

Mkoa wa Kusini Unguja kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ulikadiriwa kutumia jumla ya shilingi 15,748,952,435 kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina na mapato yao ya ndani, kati ya hizo shilingi 15,542,252,435 kwa matumizi ya kawaida na shilingi 206,700,000 kwa matumizi ya maendeleo.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 Mkoa wa Kusini Unguja uliingiziwa na kutumia jumla ya shilingi 13,646,908,014 sawa na asilimia 86.65 ya makadirio. Kati ya hizo shilingi 13,608,187,006 zilitumika kwa matumizi ya kawaida sawa na asilimia 87.56 ya makadirio na shilingi 4,262,508 zilitumika kwa matumizi ya kazi za maendeleo sawa na asilimia 2 ya makadirio.

**MATOKEO NA MAPENDEKEZO YA UKAGUZI**

### 6.3.9.1 Mapungufu yaliojitokeza kwenye Daftari la Fedha Taslim (Cashbook)

Ukaguzi ulikagua daftari la fedha taslim la kuwekea kumbukumbu zinazohusiana na mapato linalotumiwa na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja na kubaini kuwepo kwa changamoto ya kurikodiwa mapato kwa kutumia "bank statement" badala ya kutumia vitabu vya risiti. Hali hii imepelekea kutokuwepo kwa risiti namba katika kumbukumbu za mapato zilizoainishwa katika daftari hilo.

Aidha ukaguzi umebaini kutokuwepo kwa mchanganuo wa mapato halisi yaliokusanywa ya kila Wilaya yanayotokana na uhaulishaji wa ardhi na ucheleweshaji wa usajili wa vyeti vya vizazi kwenye daftari hilo.

Kuwepo kwa mapungufu yalioainishwa hapo juu kunapelekea kutopatikana kwa uhalisia wa taarifa za mapato na pia kuwepo ugumu wakati wa kuzifatilia na kuzifanyia kazi taarifa hizo.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Mkoa wa Kusini kufuata taratibu za kurikodi kumbukumbu za taarifa za fedha katika daftari la kurikodia fedha taslimu (Cash Book) kwa kutumia stakabadhi za kukusanyia mapato na kuacha kurikodi kwa kutumia taarifa za kibenki "bank statements" jambo ambalo linaweza kupelekea kupokea taarifa isiyo sahihi inayotokana na kusahauliwa kwa baadhi ya stakabadhi za malipo kurikodiwa kwa usahihi au kutokurikodiwa kwa kusahauliwa.

### 6.3.9.2 Kutofautiana kwa fedha za vifungu zilizorikodiwa kwenye Daftari Kuu na Hesabu za mwisho wa mwaka shilingi 9,207,157

Ukaguzi umefanya uwiano baina ya daftari kuu (general ledger) na hesabu za mwisho wa mwaka zinazowasilishwa kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na kubaini kutowiana kwa baadhi ya fedha za vifungu vilivyoainishwa kwenye ripoti hizo.Hali halisi ya tofauti hiyo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 89 : Tofauti ya fedha iliyobainika katika daftari kuu na Hesabu za Mwisho wa mwaka**

| Jina la Kifungu | Makadirio ya Fedha kwa Mwaka 2020/2021 (Tshs) | Fedha Halisi Zilizoripotiwa Kwenye "General Ledger" kwa Mwaka 2020/2021 (Tshs) | Fedha Halisi Zilizoripotiwa Kwenye Hesabu za Mwisho wa Mwaka 2020/2021 (Tshs) | Tofauti ya fedha Iliyojitokeza (Tshs) |
|---|---|---|---|---|
| Ada ya uhaulishaji wa ardhi | 56,760,000 | 42,185,500 | 34,458,500 | 7,727,000 |
| Usafiri wa ndani | 6,000,000 | 900,000 | 2,020,000 | (1,120,000) |
| Vifaa vya kuandikia | 30,015,000 | 20,730,745 | 13,585,745 | 7,145,000 |
| "General Social welfare" | 36,180,000 | 23,911,457 | 22,510,000 | 1,401,457 |
| **Jumla** | | | | **9,207,157** |

Kutofautiana kwa fedha za vifungu vilizorikodiwa kwenye daftari kuu na hesabu za mwisho wa mwaka kunapelekea kutopatikana kwa uhalisia na usahihi wa fedha hizo na hatimae hesabu ya mapato na matumizi kutokuonesha sura sahihi na halisi.

Ukaguzi unashauri uongozi kuhakikisha kwamba taarifa za fedha zilizorikodiwa katika daftari kuu (General Ledger) zinawiana na taarifa za hesabu za mwisho wa mwaka.

### 6.3.9.3 Malipo ya Mafuta yaliolipwa kwa fedha taslim (Cash) shilingi 2,750,000

Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja ilifanya malipo yenye thamani ya shilingi 2,750,000 kwa ajili ya ununuzi wa mafuta kwa kazi za uendeshaji , dosari iliyobainika na ukaguzi ni kufanya matumizi kwa njia ya mfumo wa fedha taslim wa malipo (cash) badala ya kulipa kwa kutumia njia ya benki (uhaulishaji yaani TISS) kwa kupitia watoa huduma mbali mbali.

Kufanya malipo kwa mfumo wa fedha taslim ni kwenda kinyume na sheria, kanuni na miongozo ya fedha na pia ni kwenda kinyume na Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa mali za umma ya mwaka 2016. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 90 : Malipo ya Mafuta yaliolipwa kwa Fedha Taslim**

| Hati Namba | Aliyelipwa | Kiasi cha fedha kilicholipwa (Tshs) | Maelezo |
|---|---|---|---|
| 2/3 ya 3/3/2021 | Zanzibar Petrolem. (Jumbi Services Station) | 500,000 | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa mafuta ya Petrol |
| 1/6 ya 1/6/2021 | | 650,000 | |
| 2/3 ya 3/3/2021 | | 1,600,000 | |
| **Jumla** | | **2,750,000** | |

### 6.3.9.4 Kutorikodiwa kwa vifaa na Mafuta katika Daftari la Kumbukumbu la Ghalani shilingi 51,091,220

Kwa mujibu wa kifungu nambari 198(1) cha Kanuni ya Fedha ya mwaka 2005 kinaeleza kuwa "Vifaa vyote vitakavyopokelewa ghalani haraka iwezekanavyo lazima viwekwe katika madaftari husika pamoja na vielelezo vya upokeaji wa vifaa hivyo kama inavyoelekeza katika kanuni hii".

Ukaguzi umebaini kwamba jumla ya shilingi 51,091,220 zimetumika kwa ajili ya ununuzi wa mafuta na vifaa mbalimbali vya Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja bila ya kurikodiwa kwenye daftari la ghalani liliopo katika ngazi ya Mkoa.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 198 (1) na kifungu nambari 203 (1) cha Kanuni ya Fedha ya mwaka 2005. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 91 : Vifaa na Mafuta ambavyo havijarikodiwa katika Daftari la Ghalani**

| Hati Namba | Aliyelipwa | Kiasi cha fedha kilicholipwa (Tshs.) | Maelezo |
|---|---|---|---|
| 4/8 ya 19/08/2020 | Zanzibar Petroleum | 1,000,000 | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa mafuta ya Petrol. |
| 28/8 ya 21/08/2020 | | 781,993 | |
| 31/8 ya 25/08/2020 | | 1,926,068 | |
| 4/10 ya 15/10/2020 | | 3,000,000 | |
| 37/10 ya 22/10/2020 | | 2,000,000 | |
| 31/10 ya 23/10/2020 | | 5,000,000 | |
| 30/8 ya 25/08/2020 | | 1,102,410 | |
| 3/11 ya 03/11/2020 | | 1,000,000 | |
| 4/11 ya 03/11/2020 | | 1,000,000 | |
| 8/2 ya 12/02/2021 | | 1,000,000 | |
| 15/2 ya 17/02/2021 | | 1,000,000 | |
| 22/2 ya 22/02/2021 | | 500,000 | |
| 11/4 ya 20/04/2021 | | 850,000 | |
| 10/5 ya 07/05/2021 | | 10,389,439 | |
| 11/5 ya 07/05/2021 | | 641,597 | |
| 12/5 ya 07/05/2021 | | 2,230,561 | |
| 36/5 ya 28/05/2021 | | 621,500 | |
| 15/6 ya 08/06/2021 | | 823,093 | |
| 9/6 ya 02/06/2021 | | 1,120,000 | |
| 9/1 ya 18/01/2021 | | 700,000 | |
| 36/5 ya 28/05/2021 | | 10,118,500 | |
| 35/1 ya 27/01/2021 | | 500,000 | |
| 36/8 ya 25/08/2020 | Mji Mpya Bureau | 513,324 | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya kuandikia |
| 2/5 ya 29/04/2021 | Amo Computer Serices | 527,583 | |
| 35/8 ya 25/08/2020 | | 475,300 | |
| 21/6 ya 09/06/2021 | One to One | 907,284 | |
| 11/1 ya 18/01/2021 | Mji Mpya Secretarial Bureuau | 662,568 | |
| 4/1 ya 07/01/2021 | RJ Refrigiration and Electric | 700,000 | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa Air Condition |
| **Jumla** | | **51,091,220** | |

Kutoingizwa vifaa katika daftari la kutunzia vifaa vya ghalani kunapelekea kukosekana kwa uthibitisho wa mapokezi pamoja na matumizi ya vifaa hivyo.

Ukaguzi unapendekeza kwamba vifaa vyote ambavyo vinanunuliwa viingizwe katika daftari la kutunzia vifaa vya ghalani pamoja na vielelezo vinavyohusika na vifaa hivyo ili kuweza kuthibitisha mapokezi na matumizi ya vifaa hivyo.

### 6.3.10 FUNGU D 09 – MKOA WA KASKAZINI UNGUJA

Ukaguzi wa hesabu za mwaka 2020/2021 kwa Mkoa wa Kaskazini Unguja umefanywa kwa mujibu wa Sheria, kanuni, taratibu pamoja na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Taarifa ya Mapato**

Mkoa wa Kaskazini Unguja kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ulikadiriwa kukusanya jumla ya shilingi 17,372,646,710. Kati ya hizo jumla ya shilingi 27,500,000 zilikadiriwa kukusanywa kutoka vyanzo vya ndani vya Mkoa, jumla ya shilingi 17,115,146,710 zilikadiriwa kupatikana kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina ikiwa ni ruzuku na jumla ya shilingi 230,000,000 zilikadiriwa kupatikana ikiwa ni msaada.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 jumla ya shilingi 15,223,044,277 zilipokelewa ikiwa sawa na asilimia 87.6 ya makadirio, kati ya hizo jumla ya shilingi 12,645,000 zilipokelewa kutoka vyanzo vya ndani vya Mkoa sawa na asilimia 45.9 ya makadirio, jumla ya shilingi 15,000,761,277 zilipatikana kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina sawa na asilimia 87.6 ya makadirio na jumla ya shilingi 206,638,000 zilipatikana ikiwa ni msaada kutoka kwa washirika wa maendeleo na wananchi sawa na asilimia 89.8 ya makadirio.

**Taarifa ya Matumizi**

Mkoa wa Kaskazini Unguja kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ulikadiriwa kutumia jumla ya shilingi 17,345,146,710 kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina na mapato yao ya ndani, kati ya hizo shilingi 17,233,766,710 kwa matumizi ya kawaida na shilingi 111,380,000 kwa matumizi ya maendeleo.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 Mkoa wa Kaskazini Unguja uliingiziwa na kutumia jumla ya shilingi 15,203,210,367.8 sawa na asilimia 87.6 ya makadirio. Kati ya hizo shilingi 15,142,149,917.8 zilitumika kwa matumizi ya kawaida sawa na asilimia 87.8 ya makadirio na shilingi 61,060,450 zilitumika kwa matumizi ya kazi za maendeleo sawa na asilimia 54.8 ya makadirio.

**MATOKEO NA MAPENDEKEZO YA UKAGUZI**

#### 6.3.10.1 Kukosekana kwa Wasimamizi wa Mapato

Kwa mujibu wa kifungu nambari 61(1) cha Kanuni ya Fedha ya mwaka 2005 kinaeleza kwamba "Afisa utumishi hatoweza kukusanya mapato ya Serikali isipokuwa awe ameruhusiwa kufanya hivyo".

Ukaguzi ulifanya mahojiano na watendaji wanaoshughulika na ukusanyaji wa mapato wa Wilaya ya Kaskazini "A" na "B" na kubaini kwamba watendaji wanakusanya mapato kinyume na nyadhifa walizokuwa nazo katika Ofisi zao. Katika Wilaya ya Kaskazini "B" afisa tarishi hutumika katika zoezi la ukusanyaji wa mapato na katika Wilaya ya Kaskazini "A" kumbukumbu za mapato hurikodiwa na mwangalizi wa Ofisi badala ya mtendaji anaehusiana na masuala ya fedha. Aidha kutokana na dosari iliyobainika hapo juu ukaguzi haukuweza kupatiwa uthibitisho na vielelezo vinavyowataka watendaji hao kufanya shughuli ya ukusanyaji wa mapato kinyume na kada wanazozifanyia kazi.

Uwepo kwa wakusanyaji wa mapato wasiokuwa na taaluma ya kazi wanazozifanya kunaweza kukapelekea kujitokeza kwa viashiria vya upotevu wa fedha za umma na hatimae kukosekana kwa taarifa na kumbukumbu za ukusanyaji wa mapato zilizoandaliwa kitaalamu.

### 6.3.10.2 Kutokuwepo kwa Ripoti za ukusanyaji wa Mapato

Katika ukaguzi uliofanyika kwa mwaka wa fedha 2020/2021 imebainika Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Unguja inakusanya mapato mbali mbali yatokanayo na vyanzo vya mapato, dosari iliyobainika na ukaguzi ni kutokuwepo kwa ripoti za ukusanyaji wa mapato jambo ambalo linapelekea ugumu wa kuweza kuthibitisha uhalali na uhalisia wa fedha zilzokusanywa na zilizowasilishwa kutoka ngazi za Wilaya kwenda ngazi za Mikoa.

Kutokuwepo kwa ripoti za ukusanyaji wa mapato kunapelekea kutokupatikana kwa kumbu kumbu halisi ya kima cha fedha kilichokusanywa kulingana na makadirio yaliyopangwa jambo ambalo litaikosesha taasisi kuweza kuitathmini juu ya kufikia lengo lililopangwa kukusanywa na hatimae kupelekea uwepo wa makadirio makubwa ambayo hayataweza kufikiwa kwa mwaka unaofuata.

Ukaguzi unashauri Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Unguja ihakikishe kwamba inawasimamia vyema watendaji wao katika suala zima la kuweka kumbukumbu za taarifa za mapato ya kila mwezi na za miezi mitatu ili kujua uhalisia wa makusanyo kwa kulinganisha na daftari la kurikodia fedha taslim.

### 6.3.10.3 Kutokuthibitishwa kazi kwa watumishi wa Umma

Kwa mujibu wa kifungu nambari 9(1) cha Kanuni ya Utumishi wa Umma ya mwaka 2014 inaeleza kwamba " Bila ya kuathiri kifungu cha 60 cha sheria ya Ajira namba 11 ya 2005, mtumishi yeyote ambae ameajiriwa kwa mara ya kwanza atalazimika kuwemo katika majaribio ya utumishi kwa muda wa miezi kumi na mbili kuanzia tarehe ya kuajiriwa".

Ukaguzi umebaini uwepo wa watendaji 11 walioajiriwa kwa mara ya kwanza ambao hawajathibitishwa kuwa wafanyakazi wa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Unguja licha ya kuwa wameshapitiliza miezi kumi na mbili toka kuajiriwa. Mchanganuo wa wafanyakazi hao ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 92 : Wafanyakazi waliokuwa hawajathibitishwa kazi**

| Jina Kamili | Kada Aliyoajiriwa | Tarehe ya Ajira | Tarehe Aliyopaswa Kuthibitishwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| Salha M. Suleiman | Afisa Utumishi | 28/07/2019 | 28/07/2020 | Hakuna hatua zozote zilizochukuliwa |
| Nasra Suleiman Mtumwa | Karani Masjala | 01/09/2019 | 01/09/2020 | |
| Khatib Khamis Ali | Afisa Tehama | 21/10/2019 | 21/10/2020 | |
| Abdulhamid Kh. Haji | Fundi Mchundo | 21/10/2019 | 21/10/2020 | |
| Hassan M. Hassan | Afisa Takwimu | 21/10/2019 | 21/10/2020 | |
| Hadia Muhidini Khamis | Muhudumu | 01/12/2019 | 01/12/2020 | |
| Munira Omar Othmani | Mtunza ghala | 07/03/2020 | 07/03/2021 | |
| Patima J. Haji | Mtunza ghala | 07/03/2020 | 07/03/2021 | |
| Tatu Khamis Moh'd | Karani Masjala | 27/03/2020 | 27/03/2021 | |
| Mwanaisha Manzil Nawaje | Karani Masjala | 27/03/2020 | 27/03/2021 | |
| Saleh Haruob Saleh | Tarishi | 21/03/2020 | 21/03/2021 | |

Kutokuwathibitisha watendaji walioajiriwa kwa wakati kunapelekea kuwakosesha haki zao za msingi ikiwemo fursa za kupata mikopo, fursa ya masomo ya muda mrefu, pamoja na kuwakosesha fursa za uingiaji wa mikataba ya kimaendeleo.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Ofisi ya Mkoa wa Kaskazini uhakikishe kwamba wanachukua hatua za haraka kuwathibitisha watendaji hao kwa wale waliotimiza masharti kwa lengo la kuwapatia fursa na stahiki zao kwa mujibu wa kanuni za utumishi wa umma.

### 6.3.10.4 Kutokuwasilishwa kwa fedha za makato ZSSF shilingi 15,636,653

Kwa mujibu wa kifungu nambari 17(1-3) cha Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii nambari 2 ya mwaka 2014 kinazitaka "Taasisi za Umma kuwasilisha makato ya mishahara ya wafanyakazi wake kwa kila mwezi kwa mujibu ya kiwango kilichowekwa kwa mujibu wa matakwa ya sheria hiyo.

Ukaguzi umebaini kwamba jumla ya shilingi 15,636,653 za makato ya mwezi wa Januari zilikatwa kwa wafanyakazi wa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Unguja, dosari iliyobainika na ukaguzi ni kwamba makato hayo hayakuwasilishwa ZSSF kwa wakati kwa mujibu wa sheria na taratibu zilizopo badala yake ziliweza kutumika kwa mambo mengineyo na kupelekea kuwasilishwa mwezi wa Februari 2021 jambo ambalo ni kwenda kinyume na kifungu kilichonakiliwa hapo juu.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Unguja kuhakikisha unawasilisha fedha za mikato ya watumishi wao kwa wakati ZSSF ili kuepuka gharama ya tozo ya adhabu kwa taasisi itakayobainika kuchelewa kuwasilisha fedha hizo na kupelelekea kuingiza hasara Serikali.

### 6.3.10.5 Kukiukwa kwa makubaliano ya mkataba

Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Unguja imeingia mkataba wenye nambari No.SMZ/D09/G/Q/2019/2020/001 uliofungwa tarehe 3/6/2020 baina ya Zenj Motors Company Ltd na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Unguja wenye thamani ya shilingi 95,000,000 kwa ajili ya ununuzi wa basi la utoaji wa huduma za usafiri kwa ajili ya wafanyakazi wa Ofisi hiyo.

Kwa mujibu wa makubaliano yaliomo kwenye mkataba "Malipo yatalazimika kulipwa kwa awamu mbili". Awamu ya mwanzo yatalipwa mara tu baada ya kusainiwa kwa mkataba kwa asilimia 70 sawa na shilingi 66,500,000 awamu ya pili italipwa kwa asilimia 30 sawa na shilingi 28,500,000 baada ya kukabidhi basi hilo kwa muajiri na muajiri kuridhika nalo.

Dosari za ukaguzi zilizobainika ni kukosekana kwa makubaliano ya kufanya malipo kinyume na asilimia zilizoainishwa katika mkataba ambapo Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Unguja imefanya malipo ya awamu ya kwanza ya asilimia 42.1 na malipo ya awamu ya pili ya asilimia 57.9. Aidha ukaguzi umebaini malipo hayo yamehaulishwa kutoka katika vifungu mbali mbali lakini hatukuweza kupatiwa vielelezo na kumbu kumbu za barua na taratibu zilizopelekea kufanyika kwa uhaulisho huo jambo ambalo linaweza kupelekea kuathiri matumizi ya bajeti ya vifungu husika.

Ukaguzi unashauri watendaji wanaohusiana na ununuzi na uondoshaji wa mali za umma kuwa makini katika kufuata sheria na kanuni pale wanapotekeleza majukumu yao ya kiutendaji ya kila siku ili kuepuka uvunjaji wa sheria.

### 6.3.10.6 Kutorikodiwa kwa Mafuta Kwenye Daftari la Ghalani shilingi 24,098,386

Kwa mujibu wa kifungu nambari 198(1) cha Kanuni ya Fedha ya mwaka 2005 kinaeleza kuwa "Vifaa vyote vitakavyopokelewa ghalani haraka iwezekanavyo lazima viwekwe katika madaftari husika pamoja na vielelezo vya upokeaji wa vifaa hivyo kama inavyoelekeza katika kanuni hii". Katika ukaguzi uliofanyika imebainika Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Unguja imefanya matumizi

mbali mbali kwa ajili ya ununuzi wa mafuta kwa kazi za uendeshaji, dosari iliyobainika na ukaguzi ni kutokurikodiwa kwa manunuzi hayo kwenye daftari la kumbu kumbu za manunuzi jambo ambalo tumeshindwa kuthibitisha uhalali wa matumizi hayo.

Kutokurikodiwa kwa taarifa za manunuzi kunaweza kukapelekea udanganyifu katika manunuzi na hatimae kujitokeza kwa upotevu wa fedha za umma.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Mkoa wa Kaskazini Unguja kuhakikisha unaimarisha udhibiti wa ndani juu ya usimamizi wa mafuta katika ngazi zote za Mkoa na Wilaya.

Mchanganuo wa manunuzi hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 93 : Matumizi ya Mafuta ambayo hayajarikodiwa kwenye Daftari la Ghalani**

| Hati Namba | Aliyelipwa | Kiasi cha fedha kilicholipwa (Tshs) | Maelezo |
|---|---|---|---|
| 6/6 ya 10/6/2021 | Gapco Zanzibar Ltd | 1,060,326 | Malipo kwa ajili ya ununuzi wa mafuta |
| 4/8 ya 19/8/2020 | | 1,800,000 | |
| 5/8 ya 19/8/2020 | Zanzibar Petroleum Ltd | 2,000,000 | |
| 10/8 ya 13/8/2020 | | 188,500 | |
| 3/8 ya 11/8/2020 | | 1,000,000 | |
| 21/6 ya 14/6/2021 | | 880,000 | |
| 8/10 ya 6/10/2020 | | 2,000,000 | |
| 10/10 ya 14/10/2020 | | 200,000 | |
| 36/10 ya 26/10/2020 | | 498,680 | |
| 28/1 ya 28/1/2021 | | 742,300 | |
| 2/3 ya 25/2/2021 | | 2,500,000 | |
| 17/4 ya 23/4/2021 | United Group Ltd | 4,000,000 | |
| 28/5 ya 24/5/2021 | | 7,228,580 | |
| **Jumla** | | **24,098,386** | |

### 6.3.11 FUNGU D10 - MKOA WA KUSINI PEMBA

Ukaguzi wa hesabu za mwaka 2020/2021 kwa Mkoa wa Kusini Pemba umefanywa kwa mujibu wa Sheria, kanuni, taratibu pamoja na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Taarifa ya Mapato**

Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kusini Pemba kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ilikadiriwa kukusanya jumla ya shilingi 25,700,000 kutoka katika vianzio vyake mbali mbali.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni 2021, jumla ya shilingi 16,248,955 zilikusanywa na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kusini Pemba sawa na asilimia 63.23 ya makadirio.

**Taarifa ya Matumizi**

Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kusini Pemba ilikadiriwa kutumia jumla ya shilingi 14,460,900,000 kwa kazi za kawaida. Hadi kufikia tarehe 30 Juni 2021, jumla ya shilingi 13,818,960,775 zimetumika kwa kazi za kawaida ambapo ni sawa na asilimia 97.82 ya makadirio.

### 6.3.12 FUNGU D 11 - MKOA WA KASKAZINI PEMBA

Ukaguzi wa hesabu za mwaka 2020/2021 kwa Mkoa wa Kusini Pemba umefanywa kwa mujibu wa Sheria, kanuni, taratibu pamoja na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Taarifa ya Mapato**

Ofisi ya Mkuu wa Mkoa Kaskazini Pemba ilikadiriwa kukusanya jumla ya shilingi 25,476,000 kutoka katika vianzio vyake mbali mbali kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni 2021, jumla ya shilingi 13,420,000 zilikusanywa na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini sawa na asilimia 52.68 ya makadirio.

**Taarifa ya Matumizi**

Ofisi ya Mkuu wa Mkoa Kaskazini Pemba ilikadiriwa kutumia jumla ya shilingi 16,876,264,986 kwa kazi za kawaida.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni 2021, kiasi cha shilingi 11,822,350,143 zimetumika kwa kazi za kawaida ambapo ni sawa na asilimia 69.97 ya makadirio.

### 6.3.13 FUNGU D12 - WAKALA WA USAJILI WA MATUKIO YA KIJAMII

Ukaguzi wa hesabu za Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii kwa mwaka wa fedha 2020/2021 umefanywa kwa mujibu wa Sheria, kanuni, taratibu pamoja na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Taarifa ya Mapato**

Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2020/2021 imekadiria kukusanya jumla ya shilingi 626,512,000 kutoka katika vyanzo vyake vya ndani. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar ilikukusanya jumla ya shilingi 636,084,634 sawa asilimia 101.5 ya makadirio.

**Taarifa ya Matumizi**

Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ilikadiriwa kutumia jumla ya shilingi 4,993,414,808 kwa matumizi ya kazi za kawaida. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 kiasi cha shilingi 2,598,752,604 kimeingizwa na kutumika kwa kazi za kawaida sawa na asilimia 52 ya makadirio.

**MATOKEO NA MAPENDEKEZO YA UKAGUZI**

#### 6.3.13.1 Kuwepo kwa tofauti ya fedha baina ya hesabu ya mwisho wa mwaka na matumizi halisi shilingi 290,425,367

Katika ukaguzi uliofanyika kupitia taarifa mbali mbali zikiwemo taarifa za Hesabu ya mwaka, daftari la kurikodia kumbukumbu za fedha pamoja na hati za malipo imebainika kwamba Jumla ya shilingi 290,425,367 ni tofauti ya fedha iliyojitokeza baina ya Hesabu za mwisho wa mwaka ikilinganishwa na matumizi halisi.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Viwango vya ufungaji wa hesabu vya kitaifa na kimataifa ambapo ni kwenda kinyume na Sheria nambari 12 ya Usimamaizi wa Fedha za Umma ya Mwaka 2016.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wakala kuhakikisha kwamba hesabu za mwisho wa mwaka zinawiana na matumizi halisi yaliofanyika katika kipindi cha mwaka husika ili kuweza kuonyesha usahihi wa hesabu hizo. Mchanganuo wa baadhi ya vifungu vilivyoonesha tofauti hiyo ni kama inavyoonekana hapo chini:-

**Jadweli Nambari 94 : Tofauti baina ya taarifa ya fedha na matumizi halisi**

| Vifungu vya matumizi | Makadirio | Kiasi cha fedha kilichoainishwa katika hesabu (Tshs) | Kiasi cha fedha kilichotumika (Tshs) | Tofauti ya fedha iliyojitikeza (Tshs) |
|---|---|---|---|---|
| Petrol | 188,870,000 | 66,898,035 | 45,048,860 | 21,849,175 |
| Sitting Alowance | 46,950,000 | 32,848,830 | 31,788,830 | 1,060,000 |
| Food and refreshment | 34,250,000 | 25,124,000 | 14,650,000 | 10,474,000 |
| Domestic Travel | 49,556,407 | 37,297,306 | 20,303,633 | 16,993,673 |
| Foreign Travel | 58,500,000 | 30,000,000 | 0 | 30,000,000 |
| Government Offices Electricity Bills | 190,000,000 | 108,666,722 | 84,799,130 | 84,799,130 |
| Stationary Supply | 49,000,000 | 49,000,000 | 37,917,000 | 11,083,000 |
| Printing Expenses | 809,700,000 | 265,180,690 | 146,146,726 | 119,033,964 |
| Cleaning Supply | 55,000,000 | 54,581,600 | 37,600,000 | 16,981,600 |
| **Jumla** | **1,292,956,407** | **602,699,148** | **373,205,319** | **290,425,367** |

**WAKALA WA USAJILI WA MATUKIO YA KIJAMII - PEMBA**

### 6.3.13.2 Kutokusajiliwa na kuhakikiwa kwa fomu za vyeti vya kuzaliwa

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba jumla ya fomu 2,378 zinazohusu maombi ya upatikanaji wa vyeti vya kuzaliwa katika Wilaya nne za Pemba hazijasajiliwa na kuhakikiwa, hivyo kupelekea uwezekano wa ucheleweshwaji wa upatikanaji wa huduma ya utoaji wa vyeti kwa wakati,hali hii inaweza kusababisha kukosekana kwa imani miongoni mwa jamii inayohitaji huduma pamoja na Wakala wa Usajili wa Matokeo ya Kijamii.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria Nambari 3 ya Uanzishwaji wa Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii ya mwaka 2018. Mchanganuo wa idadi ya fomu za vyeti ambazo hazikusajiliwa ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 95: Fomu za vyeti vya kuzaliwa ambazo hazikusajiliwa**

| Wilaya | Idadi ya Form |
|---|---|
| Wete | 720 |
| Micheweni | 492 |
| Chake | 551 |
| Mkoani | 615 |
| **Jumla** | **2,378** |

## 6.4 WIZARA YA NCHI OFISI YA RAIS FEDHA NA MIPANGO

### 6.4.1 FUNGU F 01 – OFISI YA RAIS FEDHA NA MIPANGO

Ukaguzi wa hesabu za Wizara ya Fedha na Mipango kwa mwaka wa fedha 2020/2021 umefanywa kwa mujibu wa Sheria, kanuni, taratibu pamoja na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Taarifa ya Mapato**

Ofisi ya Rais Fedha na Mipango kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ilitarajiwa kukusanya jumla ya shilingi 1,549,340,824,000 kutoka katika vyanzo vyake vya Kodi na visivyokuwa vya Kodi.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 jumla ya shilingi 891,648,458,176.28 zimekusanywa kutoka vyanzo mbalimbali vya kodi na visivyokuwa vya kodi ambavyo ni sawa na asilimia 58 ya makadirio.

**Taarifa ya Matumizi**

Ofisi ya Rais Fedha na Mipango kwa mwaka wa Fedha 2020/2021 iliidhinishiwa kutumia jumla ya shilingi 129,185,392,882 kwa matumizi ya kawaida, mishahara jumla ya shilingi8,543,512,000, matumizi mengineyo ni shilingi 15,792,788,000, shilingi 41,920,000,000 kwa kazi za maendeleo ikiwa ni mchango wa Serikali, shilingi 26,250,852,189 kwa kazi za maendeleo kupitia Washirika wa Maendeleo, na shilingi 36,678,240,693 ikiwa ni Ruzuku.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 jumla ya shilingi 48,578,035,298 zimeingizwa na kutumika kwa ajili ya matumizi ya kawaida sawa na asilimia 38 ya makadirio, ambapo shilingi 8,447,134,942 zimeingizwa na kutumika kwa Mishahara sawa na asilimia 99, matumizi mengineyo 6,132,515,064 sawa na asilimia 39, kazi za maendeleo mchango wa Serikali 8,020,847,568 sawa na asilimia 19 kwa kazi za maendeleo Washirika wa Maendeleo shilingi 3,937,000 sawa na asilimia 0.015 ya makadirio na shilingi 25,973,600,724 ikiwa ni ruzuku sawa na asilimia 71 ya makadirio.

**MATOKEO NA MAPENDEKZO YA UKAGUZI**

#### 6.4.1.1 Malipo yasiyokuwa na vielelezo shilingi 42,578,400

Katika ukaguzi uliofanyika kwa mwaka wa fedha 2020/2021 imebainika Ofisi ya Rais Fedha na Mipango imefanya matumizi kwa ajili ya ununzi wa vifaa na huduma mbali mbali za kiofisi zenye thamani ya shilingi 42,578,400. Dosari iliyobainika katika ukaguzi ni kutokuambatanishwa kwa vilelezo husika katika hati ya malipo ili kuweza kujiridhisha uhalali wa malipo hayo.

Kutokuambatanishwa kwa vielelezo husika katika hati za malipo kunapelekea kushindwa kujiridhisha kwa matumizi ya fedha yaliyofanyika na kuashiria ukiukwaji wa taratibu, miongozo, kanuni na sheria za usimamizi wa fedha jambo ambalo ni kwenda kinyume na kifungu 34(1) cha Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Ummma ya mwaka 2016. Mchanganuo wa matumizi hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli la hapo chini:-

**Jadweli Nambari 96 : Malipo yasiyokuwa na vielelezo**

| Hati Namba | Kiasi cha fedha kilicholipwa (Tshs.) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|
| R6/9ya 31/8/2020 | 2,750,000 | Common wealth Institute | Malipo kwa ajili ya ada ya mafunzo ya muda mfupi kwa wafanyakazi. |
| R9/8ya 17/8/2020 | 29,628,400 | Wizara ya Fedha | Malipo kwa ajili ya matumizi mbali mbali. |
| R1/12 ya 1/1/2020 | 10,200,000 | NBAA | Malipokwa ajili ya ada ya ushiriki wa mkutano Mkuu wa wanachama wa NBAA. |
| **Jumla** | **42,578,400** | | |

**OFISI YA RAIS FEDHA NA MIPANGO – PEMBA**

### 6.4.1.2 Kukosekana Kwa kumbu kumbu za mapato za ukodishwaji wa majengo ya Ofisi

Ofisi ya Rais Fedha na Mipango - Pemba inamiliki majengo mbali mbali katika maeneo ya Pemba kwa ajili ya ukodishwaji na kupelekea upatikanaji wa mapato ya Serikali.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kutokujulikana kwa mapato halisi yaliyopatikana yanayotokana na ukodishwaji wa majengo kutokana na kukosekana kwa kumbu kumbu za mapato za ukodishwaji wa majengo ya ofisi jambo ambalo limepelekea ukaguzi kushindwa kukamilisha kazi yao kutokana na kukosekana kwa nakala za mikataba ya Ukodishwaji, Hati za kulipia kutoka benki (Pay in slip) pamoja na taarifa za benki (bank statement) ili kuweza kujiridhisha kima halisi cha fedha kwa mujibu wa mkataba na fedha iliyokusanywa kupitia ukodishwaji huo.

Pamoja na uwepo wa dosari hiyo ukaguzi umebaini kwa baadhi ya maeneo fedha zilizolipwa haziendani na thamani halisi ya ukodishwaji wa jengo kutokana na bei ya sokoni ilivyo jambo ambalo limepelekea kujitokeza kwa mambo yafuatayo:-

**a) Jengo lililopo Kilima Tende (Miembeni Chake Chake)**

Ukaguzi umebaini jengo hili lina milango minne (4) pamoja na sehemu ya kuekea bidhaa (store) ambalo limekodishwa kwa thamani ya shilingi laki tatu (Tshs. 300,000) kwa mwezi kwa Bwana Abdalla Hemed Abdalla ambapo bei hii hailingani na bei ya soko kwa kila mlango.

**b) Jengo lililopo MTC mkabala na Hotel ya Chake Chake**

Katika jengo hili imebainika uwepo wa milango tofauti ambapo mlango wa kwanza umekodishwa kwa bwana Salum Alawy ambapo thamani ya bei aliyokodishiwa na Wizara ya Fedha haikuweza kujulikana, hata hivyo mkodishwaji huyo nae amemkodisha Bwana Said Sulum Ahmed kwa thamani ya shilingi 1,500,000 kwa mwaka kinyume na makubaliano ya mkataba wa awali.

Mlango wa pili kakodishwa Bwana Seif Mohd Khamis kwa thamani ya shilingi 10,800,000 kwa kipindi cha miaka mitatu (3).

Kukosekana kwa thamani halisi ya fedha kulingana na eneo pamoja na ukubwa wa duka kutokulingana na bei halisi ya soko kunapelekea kukosesha Serikali mapato.

#### 6.4.1.3 Ukodishaji wa majengo ya Serikali usioendana na thamani halisi ya soko.

Ofisi ya Rais Fedha na Mipango Pemba inamiliki majengo ya biashara na kuingia mikataba ya ukodishaji ili kuweza kuingizia Serikali mapato yatokanayo na kodi ya majengo hayo.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwa ukodishaji wa majengo ya serikali kwa thamani ndogo ukilinganisha na bei ya soko kwa maeneo husika.

kufanya hivyo ni kuikosesha Serikali mapato stahiki. Aidha ukaguzi umeshindwa kupatiwa bei elekezi iliyopangwa na Ofisi ya Rais Fedha na Mipango kwa ajili ya ukodishaji wa majengo ya Serikali kinyume na miongozo ya fedha.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016. Mchanganuo wa thamani halisi ya ukodishwaji wa majengo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 97 : Majengo ya Serikali yaliyokodishwa kwa thamani ndogo**

| Tarehe ya mkataba | Aina ya Jengo | Pahala | Muda wa mkataba | Aliyekodishwa | Fedha Zilizolipwa kwa mwezi (Tshs) | Fedha Zilizolipwa kwa mwaka (Tshs) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1/1/2020 - 31/12/2021 | Bekari | Chake Chake | Mwaka 1 | Mohamed Omar Khamis | 30,000 | 360,000 |
| 1/7/2020 - 30/6/2021 | Mlango wa duka | | | Khatib Omar Khatib | 15,000 | 180,000 |

#### 6.4.1.4 Gharama za huduma za usafi usiolingana na thamani halisi ya fedha shilingi 6,000,000 kwa mwezi

Ofisi ya Rais Fedha na Mipango Pemba iliingia mkataba na **AKB Cleaning Enterprises** ya Chake Chake mnamo tarehe 1/1/2021 kwa ajili ya kupatiwa huduma ya usafi wa ndani kwa muda wa miezi sita (6) ambapo malipo ya huduma hiyo kwa mwezi ni shilingi milioni sita (6,000,000) ambapo ni sawa na shilingi 72,000,000 kwa mwaka.

Ukaguzi umebaini kwamba gharama ya malipo ya huduma ya usafi zinazolipwa na Ofisi ya Rais Fedha na Mipango haziendani na uhalisia wa kazi zinazofanywa katika eneo husika ambapo gharama hiyo inajumuisha floo ya chini, ghorofa ya kwanza na ya tatu ya jengo hilo, na kuonekana gharama yake ni mara mbili zaidi ukilinganisha na eneo la jengo hilohilo la ghorofa ya pili ambalo linalipiwa huduma ya usafi kwa gharama za shilingi milioni moja kwa mwezi (1,000,000) ambapo ni sawa na shilingi 12,000,000 kwa mwaka.

Hadi ukaguzi unakamilika imebainika jumla ya shilingi 51,000,000 zimeshalipwa kwa mwaka wa fedha 2020/2021 na kupelekea uwepo wa bakaa ya shilingi 21,000,000 kwa mujibu wa makubaliano ya mkataba baina ya Ofisi ya Rais Fedha na Mipango na Kampuni hiyo.

Ukaguzi unashauri ni vyema kufanyike upembuzi yakinifu wa kuhakikisha kwamba fedha zinazolipwa zinaendana na uhalisia wa upatikanaji wa huduma ili kuepusha viashiria vya upotevu wa fedha. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama unavyooneka katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 98 : Gharama za huduma za usafi usiolingana na thamani halisi ya fedha**

| Hati Namba | Hundi Namba | Kiasi cha fedha zilizolipwa (Tshs.) | Maelezo |
|---|---|---|---|
| 5/8 | 16335 | 4,500,000 | Malipo ya fedha kwa ajili ya huduma ya usafi wa ndani kwa jengo la Ofisi ya Rais Fedha na Mipango Pemba. |
| 13/10 | 171068 | 9,000,000 | |
| 42/10 | 18065 | 4,500,000 | |
| 3/1 | 18815 | 4,500,000 | |
| 13/2 | 19350 | 10,500,000 | |
| 15/3 | 19912 | 6,000,000 | |
| 9/4 | 20402 | 6,000,000 | |
| 14/5 | 21072 | 6,000,000 | |
| **Jumla** | | **51,000,000** | |

### 6.4.1.5 Kukosekana kwa uthibitisho wa safari za kikazi shilingi 42,032,500

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika uwepo wa malipo yenye jumla ya shilingi 42,032,500 kwa ajili ya safari za kikazi lakini malipo hayo yamekosa uthibitisho wa safari kutokana na kutokuonekana kwa majina ya wasafiri hao katika kumbukumbu za kitabu cha wasafiri (manifest) kinachoonesha idadi ya wasafiri, jina la msafiri, tarehe ya safari , muda wa safari pamoja na ndege aliyosafiria.

Kutokana na uwepo wa tiketi za kusafiria tulizowasilishiwa kwa ajili ya ukaguzi tumeshindwa kujiridhisha juu ya uhalali wa uwepo wa safari hizo kutokana na kukosekana kwa taarifa za majina ya wasafiri hao katika mashirika ya usafiri wa anga kwa siku na tarehe kwa mujibu wa tiketi hizo jambo ambalo linapelekea uwepo wa viashiria vya upotevu wa fedha za umma, **Kiambatisho Nambari 5 Kinahusika.**

### 6.4.1.6 Hati za malipo yenye vielelezo pungufu shilingi 79,209,998

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika uwepo jumla ya shilingi 79,209,998 ambazo zimelipwa kwa mtumizi mbali mbali ya Ofisi ya Rais Fedha na Mipango Pemba lakini baadhi ya vielelezo vya matumizi hayo havikuambanishwa na hati za malipo ili kuweza kuthibitisha uhalali wa malipo hayo.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 34(1) cha Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli lifuatalo:-

**Jadweli Nambari 99 : Malipo yenye vielelezo pungufu**

| Hati Namba | Hundi Namba | Kiasi cha fedha kilicholipwa (Tshs.) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 06/10 ya 03/10/2020 | 017162 | 4,376,699 | Halim Enterprises | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa UPS na Betri za computer. |
| 07/10 ya 03/10/2020 | 017163 | 3,189,519 | Nassor Said Nassor | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa vitu vidogo vidogo. |
| 10/10 ya 03/10/2020 | 34600105 | 1,313,010 | Bin Amour Traders | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya Camera. |
| 11/10 ya 03/10/2020 | 01765 | 359,709 | Gombani Garage Co-oparation | Malipo ya fedha kwa ajili ya matengenezo ya Generator. |
| 12/10 ya 03/10/2020 | 017167 | 1,960,000 | Zahran Abdallah Hemed | Malipo ya fedha kwa ajili ya ya ununuzi wa Air Condition. |
| 17/10 ya 03/10/2020 | 017171 | 3,092,233 | Misufini Stationary Centre | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa wino wa Printer kwa matumizi ya Ofisi |
| 18/10 ya 03/10/2020 | 017172 | 428,155 | Seif Nassor Salim | Malipo ya fedha kwa ajili ya ya ununuzi wa maji. |
| 21/10 ya 3/10/2020 | 346106 | 9,847,573 | Quality Investment Service | Malipo ya fedha kwa ajili ya ya ununuzi wa Computer. |
| 25/12 ya 1/1/2021 | 19042 | 3,503,000 | Wizara ya fedha na Mipango Pemba | Malipo ya fedha kwa ajili ya mfuko wa maafa. |
| 36/1 ya 21/1/2021 | 22012171 | 627,000 | Idara ya hazina | Malipo ya fedha kwa ajili ya mkato wa Idara ya Hazina. |
| 37/1 ya 21/1/2021 | 22012170 | 1,350,750 | Zanzibar NHIF Collection Account | Malipo ya fedha kwa ajili ya mkato wa NHIF. |
| 42/1 ya 25/1/2021 | 19258 | 2,440,485 | Capital Technoloy Center | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa wino wa Printer. |
| 10/11 ya 5/1/2021 | 18962 | 6,580,000 | Wizara ya Fedha na Mipango Pemba | Malipo ya fedha kwa ajili ya posho mbali mbali na likizo. |
| 12/1 ya 18/1/2021 | 18973 | 2,667,408 | Halim Enterprises | Malipo ya fedha kwa ajili ya Vifaa vya kuandikia. |
| 09/3 ya 9/03/2021 | 19857 | 585,146 | Seif Moh'd Juma | Malipo ya fedha kwa ajili ya ya matengenezo ya Gari. |
| 3/7 ya 20/7/2020 | T.0 | 15,938,643 | TRA Domestic Revenue | Malipo ya fedha kwa ajili ya mkato wa Income Tax. |
| 30/8 ya 19/8/2020 | - | 883,320 | Zanzibar NHIF Collection Accounts. | Malipo ya fedha kwa ajili ya NHIF. |
| 35/8 ya 20/8/2020 | 016661 | 5,223,400 | Tahfif Auto Works | Malipo kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya gari SMZ 862A. |
| 3/9 ya 3/9/2020 | 017540 | 1,200,000 | Wizara ya Fedha na Mipango | Malipo kwa ajili ya shughuli za Idara ya IFMS na Ukaguzi. |

| Hati Namba | Hundi Namba | Kiasi cha fedha kilicholipwa (Tshs.) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 2/2 ya 5/2/2021 | 19326 | 2,865,000 | Wizara ya fedha na Mipango Mtumwa Ali Khamis Ali Abdalla Khamis Abeid Mohd Salim. | Malipo ya fedha kwa ajili ya safari ya Unguja kikazi. |
| 33/3 ya 19/3/2021 | 20002 | 3,331,000 | Mfuko wa maafa | Malipo ya fedha kwa ajili ya mfuko wa maafa. |
| 43/3 ya 19/3/2021 | 26032152 | 872,948 | TPB Bank PLC | Malipo ya fedha kwa ajili ya mkato wa TPB. |
| ¼ ya 1/4/2021 | 20327 | 735,000 | Firdaus Khatib Haji | Malipo ya fedha kwa ajili ya safari kikazi. |
| ¼ ya 1/4/2021 | 20327 | 500,000 | Haski Product And Deliver | Malipo ya fedha kwa ajili ya chakula na viburudishaji. |
| ¼ ya 1/4/2021 | 20327 | 1,940,000 | Ofisi ya Rais Fedha na Mipango | Malipo ya fedha kwa ajili ya posho la siku za mapumziko. |
| 7/4 ya 15/4/2021 | 20400 | 2,000,000 | Imprest – Masurufu | Malipo ya fedha kwa ajili ya masurufu (imprest). |
| 16/4 ya 19/4/2021 | 20473 | 1,400,000 | Halim Enterprises | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa Antivirus 14 Pc. |
| **Jumla** | | **79,209,998** | | |

### 6.4.1.7 Malipo ambayo hayakuidhinishwa shilingi 34,353,968

Jumla ya shilingi 34,353,968 zimetumika kwa ajili ya matumizi mbali mbali ya Ofisi ya Rais Fedha na Mipango lakini idhini ya kufanyika kwa malipo hayo imekosekana katika hati za malipo.

Kufanya malipo ambayo hayakuidhinishwa kunaweza kunapelekea kushindwa kuthibitika kwa uhalali wa malipo husika, aidha ni kwenda kinyume na Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya Zanzibar nambari 12 ya mwaka 2016. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama ifuatavyo:-

**Jadweli Nambari 100 : Malipo ambayo hayakuidhinishwa**

| Hati Namba | Hundi Namba | Aliyelipwa | Kiasi cha Fedha kilicholipwa (Tshs.) | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 5/1 03/1/2021 | 6012140 | Zanzibar Revenue Board | 487,849 | Malipo ya fedha ya zuio la kodi kwa Watoa huduma . |
| 6/1 03/1/2021 | 70011275 | TRA Domestic Revenue Zanzibar | 513,279 | |
| 07/1 03/1/2021 | 18818 | Wizara ya Fedha na Mipango Pemba | 2,770,000 | Malipo ya fedha ya likizo na huduma nyenginezo |
| 8/1 05/1/2021 | 18900 | Wizara ya Fedha na Mipango Pemba | 1,380,000 | Malipo ya fedha kwa ajili ya Safari kikazi. |
| 9/1 11/1/2021 | 18943 | Wizara ya Fedha na Mipango Pemba | 4,823,687 | Malipo ya fedha kwa ajili ya overtime, Viburudishaji na posho maalumu |
| 10/1 15/1/2021 | 18962 | Wizara ya Fedha na Mipango Pemba | 6,580,000 | Malipo ya fedha kwa ajili ya posho mbali mbali |
| 12/1 18/1/2021 | 18973 | Halim Enterprises | 2,667,408 | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya kuandikia. |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 15/1<br>19/1/2021 | 18984 | Wizara ya Fedha na Mipango Pemba | 1,470,000 | Malipo ya fedha kwa ajili ya safari kikazi. |
| 42/1<br>25/1/2021 | 19258 | Capital Technology Center | 2,440,485 | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa wino za Printer. |
| 41/1<br>21/1<br>22/1/2021 | 19016 | People's Bank of Zanzibar | 323,250 | Malipo ya fedha kwa ajili ya Posho la kukaimu. |
| 43/1/2021 | 19074 | Wizara ya Fedha na Mipango Pemba | 960,000 | Malipo ya fedha kwa ajili ya Safari kikazi. |
| 10/03<br>09/03/2021 | 19858 | Hahana restaurant | 547,864 | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa Chakula |
| 9/03<br>9/3/2021 | 19857 | Seif Moh'd Juma | 585,146 | Malipo ya fedha kwa ajili ya huduma za gari za Ofisi |
| 13/03<br>10/03/2021 | 19893 | Wizara ya Fedha na Mipango Pemba. | 4,410,000 | Malipo ya fedha kwa ajili ya Safari kikazi, Posho la IFMS, Overtime na Likizo. |
| 8/03<br>08/03/2021 | 19847 | Wizara ya Fedha na Mipango Pemba. | 4,395,000 | Malipo ya fedha kwa ajili ya Safari kikazi, Overtime na Likizo. |
| | | **Jumla** | **34,353,968** | |

### 6.4.1.8 Kukosekana Kwa Muongozo wa Malipo ya Posho la IFMS Shilingi 17,300,000

Jumla ya shilingi 17,300,000 zimelipwa kwa ajili ya posho la IFMS kwa baadhi ya wafanyakazi wa Ofisi ya Rais Fedha na Mipango ambapo muongozo wa malipo ya posho hilo umekosekana kwa ukaguzi.

Kukosekana kwa muongozo wa malipo ya posho la IFMS kunaweza kupelekea kutokuthibitika kwa uhalali wa malipo ya posho hilo ambapo ni kwenda kinyume na Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016. Mchangauo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 101 : Kukosekana kwa muongozo wa Malipo ya Posho la IFMS**

| Hati Namba | Hundi Namba | Aliyelipwa | Kiasi cha fedha kilicholipwa (Tshs.) | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 01/10<br>01/10/2020 | 017054 | Wizara ya Fedha na Mipango Pemba | 7,200,000 | Malipo ya fedha za posho. |
| 39/10<br>30/10/2020 | 018045 | | 3,700,000 | |
| 10/1<br>15/1/2021 | 18962 | | 3,700,000 | |
| 13/03<br>10/03/2021 | 19893 | | 2,700,000 | |
| | | **Jumla** | **17,300,000** | |

### 6.4.2 FUNGU F 02 - HESABU ZA HUDUMA ZA MFUKO MKUU WA SERIKALI

Ukaguzi wa hesabu za Huduma za Mfuko Mkuu wa Serikali kwa mwaka wa fedha 2020/2021 umefanywa kwa mujibu wa Sheria, kanuni, taratibu pamoja na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Taarifa ya Matumizi**

Katika mwaka wa Fedha 2020/2021 Hesabu za Huduma za Mfuko Mkuu wa Serikali iliidhinishwa kutumia shilingi 239,230,300,000 kwa ajili ya utoaji wa huduma mbalimbali za Mfuko Mkuu zikiwemo ulipaji wa Viinua Mgongo, Pensheni na malipo ya huduma za hati fungani.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 jumla ya shilingi 197,071,744,662.50 zimeingizwa na kutumika kwa ajili ya matumizi ya hesabu za huduma za Mfuko Mkuu wa Serikali sawa na asilimia 82.3 ya makadirio.

Aidha, hesabu za Huduma za Mfuko Mkuu wa Serikali ulikuwa na salio la shilingi 1,407,945,086.84 mwanzoni mwa mwaka wa fedha 2020/2021 katika hesabu yake ya Amana (Public Debt Deposit Account) ambazo zilitumika kwa malipo ya Viinua Mgongo na matumizi mengine maalum ya Serikali. Hadi Kufikia tarehe 30 Juni, 2021 hesabu hii ya Amana ilikuwa na bakaa ya shilingi 835,872,461.31.

**MATOKEO NA MAPENDEKEZO YA UKAGUZI**

### 6.4.2.1 Kuwepo kwa malipo yaliyofanyika kinyume na Mkataba

Ukaguzi umepitia Mkataba uliofungwa baina ya Ofisi ya Rais Fedha na Mipango na Al-Noor Motors FZCO, ambapo mkataba huo uliofungwa tarehe 2 Septemba, 2020 wenye thamani ya **USD 1,424,600.** Mkataba huo uliitaka Ofisi ya Rais Fedha na Mipango kumlipa mzabuni Al-Noor Motors FZCO asilimia 50 ya malipo yote ya Mkataba ndani ya siku kumi na nne (14) za kazi baada ya kusainiwa kwa Mkataba pamoja na kuwasilishwa kwa Ankara ya Malipo (Invoice) na asilimia 50 zilizobaki zilipwe baada ya kupokelewa kwa hati ya upokezi wa Mizigo/bidhaa (Bills of Lading) ya gari zote (19) zilizoagiziwa kwa kipindi cha miezi miwili (wiki 8).

Ukaguzi umebaini kufanyika kwa malipo ya awamu ya pili kinyume na Mkataba unavyosema kutokana na kuwepo kwa mapitio ya Mkataba (Addendum No. 2) ambayo yamesainiwa tarehe 02/11/2020 yanayofanya makubaliano baina ya Ofisi ya Rais Fedha na Mipango Zanzibar na Al-Noor Motors FZCO kuongeza muda wa kuwasilishwa kwa gari 11 ambazo hazikuweza kuwasili katika kipindi cha kwanza cha Mkataba (Miezi miwili) baada ya kupokelewa kwa gari nane (8) ambazo ziliwasili katika kipindi cha Mkataba).

Kutokuwasilishwa kwa gari 11 ambazo zilipaswa ziwasilishwe kwa mujibu wa mkataba wa awali ndani ya miezi miwili na badala yake kuamulika kufanya mkataba mdogo wa makubaliano mapya ya uwasilishwaji wa gari hizo ambapo kampuni ya Al-Noor Motors FZCO ililipwa malipo yote kabla ya mapokezi ya gari hizo kumepelekea kujitokeza kwa viashiria vya udanganyifu na ukiukwaji wa makubaliano jambo ambalo linaweza kuchelewesha kufikiwa kwa malengo yaliokusudiwa kwa wakati. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli la hapo chini:-

**Jadweli Nambari 102 : Fedha zilizolipwa kwa ajili ya ununuzi wa magari**

| Namba | Tarehe | Kiasi cha fedha kilicholipwa (USD) | Aliyelipwa |
|---|---|---|---|
| 1. | 15/09/2020 | 712,300 | AL-NOOR MOTORS FZCO |
| 2. | 24/10/2020 | 472,700 | AL-NOOR MOTORS FZCO |
| **Jumla** | | **1,185,000** | |

#### 6.4.2.2 Kutokuwasilishwa kwa kidhibiti cha Mkataba (Performance Security)

Kifungu 18.1 cha SSC ya Mkataba baina ya Wizara ya Fedha na Mipango Zanzibar na Al-Noor Motors FZCO kinamtaka Mzabuni kuwasilisha Kidhibiti cha Mkataba (Performance Security) ndani ya siku 28 baada ya kupokea kwa barua ya kumjuulisha kushinda kwa Zabuni (Clause 18.1 If require as specified in the SCC, the Supplier shall, within twenty-eight (28) days of the notification of contract award, provide a performance security for the performance of the contract in the amount specified in the SCC).

Ukaguzi umebaini kwamba Mzabuni (Al-Noor Motors FZCO) hakuwasilisha kidhibiti cha Mkataba (Performance Security) kama ilivyoelekezwa katika Mkataba.

Kutokuwasilishwa kwa kidhibiti cha mkataba na kuendelea kufanya biashara na mzabuni kwa kumlipa fedha zote za malipo aliyodai kunaweza kupelekea hasara kwa Serikali ya kutokupata marejesho ya fedha zake pale ambapo mzabuni atashidwa kuwasilisha vifaa alivyotakiwa kuwasilisha kwa mujibu wa mkataba. Aidha mzabuni atakapovunja uaminifu na kuamua kukimbia Serikali itapoteza fedha kubwa waliomlipa bila ya kuwa na kidhibiti cha kurejesha fedha hizo jambo ambalo ni kinyume na sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Mfuko Mkuu wa Serikali kuhakikisha unatekeleza vipengele vyote vya makubaliano ya mkataba ili kuepusha kujitokeza upotevu wa fedha za Serikali kunako sababishwa na kutokufuatwa na makubaliano.

#### 6.4.2.3 Kukosekana kwa Maombi ya Malipo (Payment requisition) kutoka kwa Mzabuni (Al–Noor Motors FCOZ) za madai ya malipo yake ya manunuzi ya magari.

Mkataba uliofungwa baina ya Wizara ya Fedha na Mipango na Al-Noor Motors FCOZ kupitia kifungu 16.2 kinaeleza kwamba Mzabuni atawasilisha maombi yake ya malipo kwa kuambatanisha na Ankara za malipo. (16.2 Terms of payment which states that, The Supplier request for payment shall be made to the purchasing in writing, accompanied by invoices).

Dosari iliobainika katika ukaguzi ni kutokupatikana kwa vielelezo vinavyothibitisha uwepo wa maombi hayo kwa mujibu wa kifungu 16.2 cha makubaliano ya mkataba.

#### 6.4.2.4 Kukosekana kwa Makubaliano ya mwisho yanayohusu malipo dhidi ya Kesi iliotokea baina ya Serikali na Kampuni ya Al Ghubra Marine Services LTD.

Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali imefanya malipo dhidi ya Kesi iliyotokea baina ya Kampuni ya Al-Ghubra Marine Services na Serikali ambayo ilisimamiwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Kesi hio ilitokea baada ya Wizara ya Biashara na Viwanda kutoa barua ya kuvunja Mkataba tarehe 8/4/2016. Baada ya juhudi ya kutafuta ufumbuzi wa shauri hilo nje ya Mahkama kushindikana, Kampuni ya Al-Ghubra ilifungua kesi ya madai katika Mahkama Kuu ya Zanzibar mwezi wa Julai 2016 (Kesi ya madai namba 36 ya 2016).

Ukaguzi umebaini kutokuwepo kwa makubaliano ya maandishi yatakayoonyesha jinsi ya kufanya malipo hayo (mode of payment) pamoja na muda wa kuanza na kumaliza kulipwa malipo hayo. Aidha ukaguzi haukupatiwa kumbukumbu za maamuzi ya kikao cha mwisho kinachohusiana na majadiliano ya utekelezaji ya maamuzi ya Mahkama ili kuweza kujuwa kama kuna makubaliano mapya ya malipo yatakayofanyika au ni makubaliano yale yale ya awali.

Kutokana na kumbukumbu za kikao cha pili cha majadiliano kati ya pande hizo mbili kilichofanyika tarehe 20/02/2020 kuhusu kesi hiyo, makubaliano ya malipo yalikuwa kama ifuatavyo:-

- Gharama za kodi ya jengo ni shilingi 1,548,000,000.
- Gharama za Mahkama na uwakili ni USD 41,000.

Hadi ukaguzi unakamilika haukuweza kupatiwa makubaliano ya fedha yanayotakiwa kulipwa, muda wa kuanza malipo pamoja na kumalizika kwa malipo hayo dhidi ya kesi iliyotokea baina ya Serikali na kampuni ya Al Ghubra Marine Service Ltd. Aidha kwa mujibu wa majibu tuliopatiwa kutoka Ofisi ya Rais fedha na Mipango yanayosema" Malipo ya Al Ghubra Marine Services Ltd imelipwa kwa mujibu wa maelekezo tulioyapata kutoka kwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha." Kutokana na majibu hayo ukaguzi umepata shaka ya kwamba malipo hayo yamefanyika kinyume na maamuzi ya Mahkama jambo ambalo linapelekea kujitokeza kwa viashiria vya upotevu wa fedha za Umma kwa kufanya malipo makubwa zaidi kuliko maamuzi ya Mahkama au vyenginevyo.

Ukaguzi unaushauri Uongozi wa Hesabu za Huduma za Mfuko Mkuu wa Hazina kuhakikisha malipo yoyote yanayofanyika yanakamilika kwa vielelezo vinavyothibitisha uhalali wa kufanyika malipo hayo. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli la hapo chini:-

**Jadweli Nambari 103 : Malipo yaliyofanyika kwa ajili ya kulipa madeni**

| Jina la Hesabu | Hati namba | Kiasi cha fedha (Tshs.) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| (DUMMY) | 3 of Feb | 71,000,000 | Alghurba Marine Services LTD. | Malipo ya kumalizia deni la nyuma la Tzs. 21,000,000 zilizobakia na Tzs. 50,000,000 ni malipo ya mwanzo ya deni la awamu ya pili la Tzs. 500,000,000 linalolipwa kwa amri ya Mahkama. Deni awamu ya pili 500,000,000. Kinacholipwa sasa 50,000,000, bakaa 450,000,000. |
| | PD 13/4 | 100,000,000 | Al Ghurba Marine Services Ltd | Malipo ya awamu ya 2 ya hukumu na amri ya mahkama katika kesi ya Al Ghurba. Jumla ya madai ni TZ 500,000,000. Kilicholipwa awali ni TZ 50,000,000 na awamu hii TZ 100,000,000. Kilichobaki TZ 350,000,000. Barua no. REF.LW 06/VOL.I/34 ya 10/12/20 |
| **Jumla** | | **171,000,000** | | |

#### 6.4.2.5 Kufanyika kwa malipo ya ziada ya mshahara ya shilingi 15,095,379

Katika ukaguzi uliofanyika kwa mwaka wa fedha 2020/2021 imebainika uwepo wa ziada ya malipo ya shilingi 15,095,379 yanayotokana na malipo ya mshahara ya Mamlaka ya Viwanja Vya Ndege Zanzibar yaliyolipwa na Mfuko Mkuu wa Serikali. Ukaguzi ulifanya ulinganisho wa malipo ya mishahara baina ya mwezi wa Juni 2020 wenye thamani ya shilingi 479,149,648 pamoja na mwezi wa Julai 2020 wenye thamani ya shilingi 494,245,027 kupitia taarifa za kumbukumbu za malipo (cash book report) na kubaini uwepo wa tofauti ya shilingi 15,095,379 kwa ajili ya mshahara kwa mwezi wa Julai 2020, dosari iliyobainika katika ukaguzi ni kutokupatikana sababu zilizopelekea kujitokeza kwa malipo ya ziada hayo, kutokana na kukosekana kwa mtumishi aliefanyiwa mabadiliko ya mshahara wake kwa kupata nyongeza ya mshahara au badiliko la posho jambo ambalo ukaguzi ulifanya mahojiano na watendaji wa Mfuko Mkuu kuhusiana na ziada ya fedha iliobainika ambapo wahusika walishindwa kutoa sababu ya utofauti wa uwepo wa ziada hiyo pamoja na kutokupatiwa kwa ukaguzi nyaraka ya makubaliano iliothibitishwa na uongozi kati ya Mamlaka ya Viwanja vya Ndege pamoja na Mfuko Mkuu wa Serikali inayohusu maombi ya ulipwaji wa fedha ya ziada kwa mshahara wa mwezi wa Julai 2020.

Kutokana na uhalisia huo ukaguzi unatilia shaka juu ya majibu ya Uongozi wa Mfuko Mkuu yanayoeleza kwamba Mfuko unafanya malipo kutokana na maelekezo yanayoandikwa katika barua ya maombi kutoka kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali pamoja na Mhasibu Mkuu wa Serikali jambo ambalo inabainika kufanyika kwa malipo kinyume na taratibu na kushindwa kujiridhisha kwa fedha iliyoombwa.

Kutokupata vielezo vya uthibitisho wa uhalali wa ziada ya malipo hayo kunaweza kupelekea uwepo wa matumizi mabaya ya fedha za Serikali.

#### 6.4.2.6 Malipo ya fedha yaliolipwa kwa njia ya Fedha taslim shilingi 500,000,000 na USD 43,000

Katika ukaguzi uliofanyika kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ukaguzi ulipitia hati za malipo pamoja na vielelezo mbalimbali vilivyofanyiwa malipo na kubaini jumla ya shilingi 500,000,000 na Dola za Kimarekani 43,000 zilitumika kwa ajili ya huduma mbalimbali kwa njia ya fedha taslim, dosari iliobainika katika ukaguzi ni kufanyika kwa malipo kwa njia ya fedha taslim na kukosekana kwa taarifa za kumbukumbu zilizotiwa saini ya mapokezi ya fedha hizo kama ni kielelezo kinachothibitisha uhalali wa mapokezi ya fedha hizo.

Kufanya malipo kwa njia ya fedha taslim kunaweza kukapelekea kujitokeza kwa matumizi yasio ya lazima ambayo yataambatana na upotevu wa fedha za Umma na kupelekea Serikali kupata hasara jambo ambalo litakwamisha utekelezaji wa malengo ya taasisi waliojipangia.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa hesabu za huduma za Mfuko Mkuu wa Serikali kuhakikisha unatekeleza maagizo ya Serikali ya kutokutumia malipo kwa fedha taslim ili kuepuka vishawishi vinavopelekea upotevu wa fedha za umma. Mchanganuo wa malipo ya fedha hizo ni kama inavyoonekana katika jadweli la hapo chini:-

**Jadweli Nambari 104 : Malipo yaliyofanyika kwa fedha taslim**

| Hati namba | Kiasi cha Fedha (Tshs) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|
| 8/10/20 | Tzs 500,000,000 | Ali S. Ali/ Jabir Kipenda Jabir | Malipo kwa ajili ya matumizi mbalimbali |
| 9/10/20 | USD 43,000 | Jabir Kipenda Jabir | Malipo kwa ajili ya matumizi mbalimbali DUMMY. |

### 6.4.3 FUNGU F 03 - TUME YA MIPANGO

Ukaguzi wa hesabu za Tume ya Mipango kwa mwaka wa fedha 2020/2021 umefanywa kwa mujibu wa Sheria, kanuni, taratibu pamoja na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Taarifa ya Matumizi**

Katika mwaka wa Fedha 2020/2021 Tume ya Mipango iliidhinishwa kutumia jumla ya shilingi 23,697,505,582 kwa matumizi ya kawaida, Mishahara 1,536,582,897, Matumizi Mengineyo 5,747,967,625, shilingi 11,618,700,000 kwa kazi za maendeleo ikiwa ni Mchango wa Serikali, shilingi 1,190,150,000 kwa kazi za maendeleo kwa Washirika wa Maendeleo, na shilingi 3,604,105,060 ikiwa ni ruzuku.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 jumla ya shilingi 5,110,858,910 zimeingizwa na kutumika kwa ajili ya matumizi ya kawaida sawa na asilimia 21.57 ya makadirio, shilingi 1,483,214,005 zimeingizwa na kutumika kwa mishahara sawa na asilimia 96.53,matumizi mengineyo 773,017,750 sawa na asilimia 13.45, kazi za maendeleo Mchango wa Serikali 682,000,000 sawa na asilimia 5.87, kwa kazi za maendeleo kwa Washirika wa Maendeleo, shilingi 102,320,000 sawa na asilimia 8.60 ya makadirio, na shilingi 2,070,307,155 ikiwa ni Ruzuku sawa na asilimia 57.44 ya makadirio.

**MATOKEO NA MAPENDEKEZO YA UKAGUZI**

#### 6.4.3.1 Kutokukatiwa Bima kwa vyombo vya moto vya Tume ya Mipango

Ukaguzi umebaini kuwa Tume ya Mipango inamiliki vyombo mbalimbali vya usafiri ikiwemo gari na vespa, dosari iliobainika ni kwa baadhi ya vyombo kutokukatiwa bima. Kutokukatiwa bima kwa vyombo vya moto kunaweza kukapelekea kudumaza shughuli za taasisi pale majanga yanapotokezea na kupelekea kutumia gharama kubwa ya matengenezo jambo ambalo linaweza likapelekea kupangua mipango ya utekelezaji wa shughuli nyengine walizojipangia.

Ukaguzi unashauri ni vyema taasisi za umma kuvikatia bima vyombo vyake ili kuepuka usumbufu utakao jitokeza pindipo majanga yanapotokezea. Mchanganuo wa vyombo ambavyo havijakatika bima ni kama inavyooekana katika jadweli la hapo chini:-

**Jadweli Nambari 105 : Gari ambazo hazina Bima**

| Namba | Namba ya Gari | Aina ya gari | Kabila | Namba ya Chassis | Mwaka | Muundo wa Bodi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | SMZ 342 | Mitsubishi 4m 40 | Pajero | V96WLNDDFP | 2011 | Station Wagon |

### 6.4.3.2 Malipo ya safari za kikazi na mafunzo ambayo hayakuambatanishwa na ripoti shilingi 20,945,000

Ukaguzi umebaini kwamba kuna malipo mbalimbali ya safari za kikazi na mafunzo yamefanyika lakini ripoti husika zinahusiana na safari hizo hazikuambatanishwa na hati za malipo ili kuweza kuthibitisha uhalali wa malipo hayo.

Kutoambatanisha ripoti kwa malipo husika ni kwenda kinyume na Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016 na kanuni ya 95(4) ya Kanuni ya Fedha ya Zanzibar ya mwaka 2005.

Ukaguzi unashauri Tume ya Mipango kusimamia na kuhakikisha kwamba wafanyakazi wote wanaokwenda safari za kikazi au mafunzo kuwasilisha ripoti ambazo zitaeleza tija itakayopatikana kwao na taasisi kutokana na safari, maonyesho au mafunzo hayo.

Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 106 : Malipo ya safari za kazi na mafunzo**

| Hati namba | Tarehe | Kiasi cha fedha kilicholipwa (Tshs) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 10/4 | 16/4 | 3,000,000 | Tume ya mipango | Utayarishaji wa ajenda ya utafiti |
| 5/5 | 3/5 | 2,895,000 | | Malipo kugharamia ziara ya uhakiki |
| 15/3 | 24/3 | 15,050,000 | | Malipo kwa ziara ya kimafunzo Ofisi za Mkurabita Tanzania Bara (Dodoma) |
| **Jumla** | | **20,945,000** | | |

**TUME YA MIPANGO – PEMBA**

### 6.4.3.3 Hati za Malipo zenye vielelezo pungufu shilingi 10,157,262

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba jumla ya shilingi 10,157,262 zimetumika kwa malipo mbali mbali ya Tume ya Mipango lakini baadhi ya vielelezo husika havikuambatanishwa na hati za malipo ili kuweza kuthibitisha uhalali wa malipo hayo.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 34(1) cha Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya Zanzibar ya mwaka 2016.Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 107 : Hati za Malipo zenye vielelezo pungufu**

| Hati Namba | Hundi Namba | Kiasi cha fedha kilicholipwa (Tshs.) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 1/5<br>6/5/2021 | 020939 | 3,000,000 | Tume ya Mipango Pemba | Malipo ya kwa ajili ya Mafunzo. |
| 3/5<br>6/5/2021 | 020940 | 2,116,000 | Sharif Petrol Station | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa Mafuta ya Petrol. |
| 6/4<br>15/4/2021 | 020373 | 2,500,000 | Ngoto Auto Accessories | Malipo ya Fedha kwa ajili ya kugawa partition za ofisi. |
| 2/2<br>3/2/2021 | 019294 | 968,447 | AKB Cleaning Enterprises | Malipo ya Fedha kwa ajili ya huduma ya Usafi. |
| 7/4<br>15/4/2021 | 020374 | 322,815 | AKB Cleaning Enterprises | Malipo ya Fedha kwa ajili ya huduma ya Usafi. |
| 2/8<br>7/8/2020 | 016329 | 1,250,000 | Sharif Petrol Station | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa mafuta ya Petrol. |
| **Jumla** | | **10,157,262** | | |

### 6.4.3.4 Bidhaa ambazo hazikurikodiwa katika daftari la ghalani shilingi 4,827,183

Ukaguzi umebaini jumla ya shilingi 4,827,183 zimetumika kwa ununuzi wa bidhaa mbali mbali lakini bidhaa hizo hazikurikodiwa katika daftari la ghalani ili kuweza kuthibitisha uhalali wa mapokezi pamoja na matumizi ya bidhaa hizo.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016. Mchanganuo wa bidhaa hizo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 108 : Bidhaa ambazo hazikurikodiwa katika daftari la ghalani**

| Hati Namba | Hundi Namba | Kiasi cha fedha kilicholipwa (Tshs) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 6/4 | 020373 | 2,305,825 | Ngolo Auto Accessories | Matengenezo ya Aluminium Partition. |
| 14/5 | | 713,592 | Malinge Enterprise Wete Pemba | Ununuzi wa:<br>Counter Book 4 Q 10 pcs |
| ½ | 019293 | 1,807,766 | Capital Technoloy Centre | Ununuzi wa:<br>i) HP Desk Top Core i5 (HP I TB – RAM 4 GB) 1 set<br>ii) CPU – Desk Top Core i3 |
| **Jumla** | | **4,827,183** | | |

### 6.4.4 OFISI YA MTAKWIMU MKUU WA SERIKALI

Ukaguzi wa hesabu za Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali kwa mwaka wa fedha 2020/2021 umefanywa kwa mujibu wa Sheria, kanuni, taratibu pamoja na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Taarifa ya mapato**

Ofisi ya Mtakwimu Mkuu kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ilikadiriwa kukusanya jumla ya shilingi 9,710,000,000 kutoka katika vyanzo vyake vya kodi na visivyokuwa vya kodi. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 jumla ya shilingi 4,595,269,986 zimekusanywa kutoka vyanzo mbalimbali vya kodi na visivyokuwa vya kodi sawa na asilimia 47 ya makadirio.

**Taarifa ya Matumizi**

Katika mwaka wa Fedha 2020/2021 Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali iliidhinishwa kutumia jumla ya shilingi 9,710,000,000 kwa matumizi ya kawaida,na jumla ya shilingi 3,602,300,000 kwa ajili ya matumizi mengineyo pamoja na shilingi 5,922,700,000 kwa kazi za maendeleo kutoka kwa washirika wa maendeleo.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 jumla ya shilingi 4,595,269,986 zimeingizwa na kutumika kwa ajili ya matumizi ya kawaida sawa na asilimia 47 ya makadirio, shilingi 1,654,258,070 zimeingizwa na kutumika kwa mishahara na posho sawa na asilimia 57ya makadirio,matumizi mengineyo shilingi 416,050,065 sawa na asilimia 20 ya makadirio, na shilingi 2,435,807,333 kwa kazi za maendeleo kutoka kwa washirika wa Maendeleo sawa na asilimia 41 ya makadirio.

## 6.5 WIZARA YA NCHI OFISI YA RAIS KATIBA, SHERIA, UTUMISHI NA UTAWALA BORA

### 6.5.1 FUNGU G 01 - WIZARA YA NCHI OFISI YA RAIS KATIBA, SHERIA, UTUMISHI NA UTAWALA BORA

Ukaguzi wa hesabu za Wizara Nchi Ofisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora kwa mwaka wa fedha 2020/2021 kwa umefanywa kwa mujibu wa Sheria,kanuni, taratibu na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Taarifa ya Mapato**

Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais Katiba, Sheria Utumishi na Utawala Bora kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ilikadiriwa kukusanya jumla shilingi 55,700,000. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 kiasi cha shilingi 122,885,546 kilikusanywa sawa na asilimia 221 ya makadirio.

**Taarifa ya Matumizi**

Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais Katiba Sheria Utumishi na Utawala Bora kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ilikadiriwa kutumia jumla ya shillingi 9,128,384,612. Kati ya fedha hizo shilingi 1,608,971,691 kwa ajili ya matumizi ya mshahara, shilingi 2,417,085,971 kwa matumizi ya kazi za kawaida, shilingi 3,202,326,950 ikiwa ni ruzuku na shilingi 1,900,000,000 kwa matumizi ya kazi za maendeleo.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni 2021, jumla ya shilingi 3,233,915,856 zimeingizwa na kutumika ambazo ni sawa na asilimia 35 ya makadirio. Kati ya fedha hizo shilingi 1,418,158,947 zimetumika kwa matumizi ya mishahara sawa na asilimia 88 ya makadirio, shilingi 418,401,999 zimetumika kwa kazi za kawaida sawa na asilimia 17 ya makadirio, shilingi 1,222,354,912 zimetumika kwa ruzuku sawa na asilimia 38 ya makadirio na shilingi 175,000,000 zimetumika kwa kazi za maendeleo sawa na asilimia 9 ya makadirio.

### 6.5.2 FUNGU G 02 - MAHKAMA KUU

Ukaguzi wa hesabu za Mahkama Kuu kwa mwaka wa fedha 2020/2021 umefanywa kwa mujibu wa Sheria, kanuni, taratibu pamoja na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Taarifa ya Mapato**

Mahkama Kuu ya Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ilikadiriwa kukusanya jumla ya shilingi 789,353,000. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 Mahkama Kuu ya Zanzibar imefanikiwa kukusanya jumla ya shilingi 485,218,992 sawa na asilimia 62 ya makadirio.

**Taarifa ya Matumizi**

Mahkama Kuu ya Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ilikadiriwa kutumia jumla ya shilingi 8,116,200,000 kwa matumizi ya kawaida na mishahara. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 jumla ya shillingi 6,089,238,125 ziliingizwa na kutumika kwa matumizi ya kawaida na mishahara sawa na asilimia 75 ya makadirio.

**MATOKEO NA MAPENDEKEZO YA UKAGUZI**

#### 6.5.2.1 Kutofikia lengo la ukusanyaji wa mapato

Mahkama Kuu inakusanya mapato yake mbalimbali kupitia vyanzo vyake vya ndani ambavyo ni malipo ya faini yatokanayo na kesi na malipo ya ada. Mahkama Kuu ilipangiwa kukusanya jumla ya shilingi 789,353,000 hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 ilikusanya jumla ya shilingi 485,218,972 ambazo sawa na asilimia 61 kukiwa na upungufu wa shilingi 304,134,028 sawa na asilimia 39 ya upungufu.

Aidha, ukaguzi umebaini kutokufikiwa kwa malengo yaliokusudiwa kunatokana na uwepo wa dosari zifuatazo:-

- Kukosekana kwa ripoti za mapato yaliokusanywa na Makarani wanaosimamia kesi za kila mwezi kwa kesi zote zilizotozwa faini na kulipwa faini hizo benki jambo ambalo linapelekea kujitokeza kwa vishiria vya upotevu wa mapato ya Mahkama.
- Kukosekana kwa kumbukumbu za ukusanyaji wa mapato yatokanayo na kesi zilizotozwa faini na kutakiwa mapato yake yawasilishwe benki
- Kukosekana kwa buku la kurekodia kesi "Court Case Register Book" baada ya kumalizika kesi na kutolewa maamuzi.
- Kutokujazwa kwa taarifa za kesi zote zilizotolewa hukumu kwenye buku maalum ambalo litaonesha uthibitisho wa thamani halisi ya fedha inayotakiwa kulipwa ikiwa kesi hiyo ilitozwa faini au haikutozwa faini inayoambatana na kurikodiwa nambari ya stakabadhi iliyofanyiwa malipo ya faini hiyo.

Kutokufikiwa kwa lengo la ukusanyaji wa mapato kunaweza kupelekea kushindwa kutekelezeka kwa baadhi ya malengo waliyojipangia kwa wakati na muda husika.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Mahakama Kuu kuhakikisha unaweka mfumo imara ambao utapelekea kuongezeka kwa makusanyo ya mapato yaliokusudiwa iwapo watasimamia vyema vyanzo vya mapato. Mchanganuo wa makadirio na makusanyo halisi ya vyanzo vya mapato ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 109 : Makadirio na hali halisi ya makusanyo ya mapato ya Mahkama Kuu**

| Mahkama kuu | Chanzo cha mapato | Makadirio ya mapato | Makusanyo halisi | Asilimia (%) | Tofauti |
|---|---|---|---|---|---|
| Mahkama kuu Unguja | Faini ya mahkama | 442,036,000 | 206,236,137 | 47 | 235,799,863 |
| | Ada ya mahkama | 189,446,000 | 189,329,885 | 100 | 116,115 |
| **Jumla Ndogo** | | **631,482,000** | **395,566,022** | | **235,915,978** |
| Mahkama Pemba<br>Faini ya mahkama | | 110,520,000 | 47,847,070 | 43 | 62,672,930 |
| | Ada ya mahkama | 47,351,000 | 41,805,900 | 88 | 5,545,100 |
| **Jumla Ndogo** | | **157,871,000** | **89,652,950** | **57** | **68,218,050** |
| **Jumla Kuu** | | **789,353,000** | **485,218,972** | **61** | **304,134,028** |

**MAHKAMA KUU – PEMBA**

### 6.5.2.2 Mapungufu katika daftari la kuhifadhia mali za kudumu

Kwa mujibu wa kifungu cha 29(2) cha Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016 kinaeleza kuwa "Katika kutimiza majukumu yanayohusiana na usimamizi wa mali, Afisa Mhasibu atatunza daftari la mali zote zilizopo chini ya udhibiti wa taasisi ya Umma".

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwa daftari la kuhifadhia mali za kudumu katika Ofisi ya Mahkama Kuu Pemba linamapungufu makubwa katika uwekaji wa taarifa muhimu za mali ambapo taarifa zikiwemo tarehe ya ununuzi wa mali, thamani na mali pamoja na maelezo ya mali husika zimekosekana katika daftari hilo ili kuweza kuweka udhibiti mzuri wa mali wanazomiliki yakiwemo majengo, vyombo vya moto pamoja na mali nyengine za kudumu. Aidha imebainika kutokuingizwa baadhi ya mali za kudumu katika daftari hilo zikiwemo samani za ofisi (Furniture), kompyuta na kiwanja kilichopo Changaweni Mkoani hali inaonyesha udhibiti hafifu wa Mahakama juu ya usimamizi wa mali za kudumu.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na matakwa ya kifungu cha 29(2) cha Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016.

### 6.5.2.3 Kutokupatiwa makaazi kwa wafanyakazi waliopewa uhamisho

Kanuni ya 127(3) ya Kanuni ya Utumishi wa Umma ya Zanzibar ya mwaka 2014 inaeleza kuwa "Mtumishi atakayepelekwa kufanya kazi mbali na sehemu yake anayoishi kikawaida atastahiki kupatiwa nyumba kwa njia ya kupangishwa kwa kadiri itakavyoyumkinika".

Ukaguzi umebaini kwamba jumla ya watumishi saba (7) wa Mahkama walipatiwa uhamisho wa kikazi kutoka Ofisi Kuu ya Mahkama Unguja kuja kuendelea na majukumu yao ya kazi katika Mahkama mbali mbali kisiwani Pemba. Hadi ukaguzi unakamilika Mahkama Kuu - Pemba imeshindwa kuwapatia makaazi watumishi hao ili kuweza kuepukana na usumbufu wamakaazi katika maeneo la kazi waliyopangiwa.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Kanuni ya Utumishi wa Umma ya Zanzibar ya mwaka 2014 kanuni ya 127(3). Mchanganuo wa watumishi hao ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 110 : Watumishi waliopewa uhamisho bila ya kupatiwa makaazi**

| Namba | Jina la Mtumishi | Cheo | Muda tangia kupewa uhamisho (Miezi) |
|---|---|---|---|
| 1. | Muumini Ali Juma | Hakimu wa Mkoa | 03 |
| 2. | Moh'd Amour Haji | Hakimu wa Mkoa | 14 |
| 3. | Thuweba Amour Haji | Msaidizi mtendaji | 16 |
| 4. | Ali Abrahman | Hakimu wa Mkoa | 36 |
| 5. | Yahya Ussi Yahya | Naibu Mwenyekiti Mahakama ya Ardhi Pemba | 36 |
| 6. | Ussi Khamis Mjombo | Hakimu wa Wilaya | 38 |
| 7. | Luciano Makoye Nyengo | Hakimu wa Mkoa | 39 |

### 6.5.2.4 Malipo ambayo hayakukatwa kodi ya zuio shilingi 7,138,850

Kwa mujibu wa kifungu cha 83(1)(c)(ii) na 84(1) vya Sheria ya Kodi ya Mapato ya mwaka 2004 (iliyorekebishwa mwaka 2019) vinaeleza kuwa kodi ya zuio inapaswa kukatwa kwenye ada ya huduma, malipo ya manunuzi ya bidhaa na malipo ya mikataba na kuwasilishwa Mamlaka ya Mapato Tanzania ndani ya siku saba baada ya mwisho wa mwezi.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwa Mahakama Kuu - Pemba imefanya malipo ya shilingi 7,138,850 kwa watoa huduma mbali mbali kwa ajili ya ununuzi wa bidhaa au upokeaji wa huduma bila ya kuwakata kodi ya zuio na kuiwasilisha Mamlaka ya Mapato Tanzania kinyume na Sheria ya Kodi ya Mapato.

Kushindwa kukata kodi ya zuio kutoka kwa watoa huduma kunaweza kupelekea kuikosesha serikali mapato ambapo ni kwenda kinyume na vifungu vya sheria vilivyonakiliwa hapo juu. Mchanganuo wa malipo ambayo haya kukatwa kodi ya zuio ni kama inavyoonekana hapo chini:-

**Jadweli Nambari 111 : Malipo ambayo hayakukatwa kodi ya zuio**

| Hati Namba | Hundi Namba | Kiasi cha fedha kilicholipwa (Tshs.) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 9/8<br>14/8/2020 | 16488 | 2,138,850 | Island Consultant and Supplier. | Malipo ya fedha kwa ajili ya usafi. |
| 5/1<br>4/1/2021 | 18844 | 2,500,000 | AKB Cleaning Enterprises. | Malipo ya fedha kwa ajili ya usafi |
| 12/2<br>25/2/2021 | 19609 | 2,500,000 | AKB cleaning Enterprises | Malipo kwa ajili ya usafi. |
| **Jumla** | | **7,138,850** | | |

### 6.5.2.5 Mapungufu kwenye uidhinishaji wa malipo shilingi 21,257,893

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Mahkama Kuu Pemba imefanya malipo yenye jumla ya shilingi 21,257,893 kwa ajili ya ununuzi wa bidhaa na upatikanaji wa huduma mbali mbali lakini hati za malipo hayo hazikuweza kuzikuidhinishwa na afisa mhasibu ili kuweza kuthibitisha uhalali wa malipo hayo.

Kufanya hivyo kunaweza kupelekea matumizi mabaya ya fedha za Serikali ambapo ni kwenda kinyume na Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016.

Mchanganuo wa hati za malipo ambazo hazikuidhinishwa ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 112 : Hati za malipo ambazo hazikuidhinishwa na afisa mhasibu**

| Hati Namba | Hundi Namba | Kiasi cha fedha kilicholipwa (Tshs.) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 5/8 10/8/2020 | 16376 | 1,000,000 | Zanzibar Electricity Corporaration | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa umeme. |
| 6/8 10/8/2020 | 16377 | 3,802,400 | Halim Enterprises | Malipo fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya kuandikia. |
| 9/8 14/8/2020 | 16488 | 2,138,850 | Island Consultant and Supplier. | Malipo ya fedha kwa ajili ya usafi. |
| 6/10 3/10/2020 | 017119 | 3,408,696 | Tahfif Auto Works | Malipo ya fedha kwa ajili ya utengenezaji wa magari pamoja na vipuri vyake. |
| 7/10 3/10/2020 | 17120 | 2,851,800 | Halim Enterprises | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya kuandikia. |
| 14/10 13/10/2020 | 17691 | 1,000,000 | Mahkama Kuu Pemba | Malipo ya fedha kwa ajili ya shughuli ya semina |
| 12/10 3/10/2020 | 17125 | 1,704,347 | Khamis Yussuf Hamad | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa mbali mbali |
| 7/10 3/10/2020 | 17120 | 2,851,800 | Halim Enterprises | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya kuandikia. |
| 12/2 16/2/2021 | 19609 | 2,500,000 | AKB Enterprises | Malipo fedha kwa ajili ya shughuli za usafi |
| **Jumla** | | **21,257,893** | | |

### 6.5.2.6 Kushindwa kuandaa mpango wa mafunzo kwa watumishi

Mpango wa mafunzo ni muhimu sana katika kupanga utaratibu nzuri wa kutoa mafunzo kwa watumishi na kuwaongezea ujuzi ambao utawasaidia kukuza utendaji wao wa kazi. Kanuni ya 74(1) ya Kanuni ya Utumishi wa Umma ya mwaka 2014 ya Zanzibar inaeleza "Taasisi zote za Serikali zitalazimika kuandaa Mpango Maalumu wa Mafunzo pamoja na kutenga fedha kwa ajili ya mafunzo. Mpango huo utazingatia mahitaji ya Taasisi husika kama itakavyoainishwa katika bajeti ya mwaka".

Ukaguzi umebaini kuwa Mahkama Kuu Pemba haikuandaa mpango wa mafunzo kwa watumishi wake kinyume na Kanuni ya Utumishi wa Umma inavyoelekeza. Hali hii inaweza kuwakosesha watumishi ujuzi muhimu wa kazi katika kipindi muafaka na hivyo kupelekea kupungua kwa ufanisi katika kutekeleza majukumu yao ya kazi ya kila siku.

#### 6.5.2.7 Malimbikizo ya madeni shilingi 168,517,481

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Mahkama Kuu Pemba inadaiwa madeni ya muda mrefu kwa watoa huduma yenye jumla ya shilingi 136,051,650 na wafanyakazi wa Mahkama yenye jumla ya shilingi 32,465,831 kwa ajili ya utowaji wa huduma katika Ofisi za Mahkama hali ambayo inayoweza kupelekea kujitokeza migogoro baina ya watoa huduma na wafanyakazi dhidi ya Mahkama kutokana na kutokupatiwa malipo ya stahiki zao.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu Nambari 29(3) cha Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Mahkama Kuu Pemba kuhakikisha kwamba unasimamia na kutekeleza dhima zote ambazo imeingia na watoa huduma pamoja na wafanyakazi kwa maslahi ya Mahkama ili kuweza kuimarisha uhusiano mwema katika upatikanaji wa huduma mbalimbali kutoka kwa wananchi na wafanyakazi.

#### 6.5.2.8 Kutokutenganishwa kwa Ofisi ya masjala ya siri na bayana

Katika Ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Mahkama Kuu Pemba haijatenganisha masjala ya siri na ya bayana hali ambayo inaweza kupelekea kuvuja kwa taarifa za siri za Serikali pamoja na kupelekea kuwepo kwa mchanganyiko wa majalada ya nyaraka, aidha ni kwenda kinyume na kifungu nambari 52(1) cha Kanuni ya Utumishi wa Umma ya mwaka 2014.

#### 6.5.2.9 Makadirio ya ukusanyaji wa mapato kinyume na uhalisia shilingi 157,871,000

Jumla ya shilingi 157,871,000 zilikadiriwa kukusanywa na Mahkama Kuu Pemba kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

Ukaguzi umebaini kwamba makadirio hayo ni makubwa ukilinganisha na makusanyo halisi kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ambapo hadi kufikia 30 Juni 2021, jumla ya shilingi 89,652,970 zilikusanywa sawa na asilimia 56.79 ya makadirio na kupelekea upungufu wa makusanyo yenye jumla ya shilingi 68,218,030 sawa na asilimia 43.21 ya makadirio.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 32(1)(2) cha Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016.

### 6.5.3 FUNGU G 03 – OFISI YA MWANASHERIA MKUU

Ukaguzi wa hesabu za Ofisi ya Mwanasheria Mkuu kwa mwaka wa fedha 2020/2021 umefanywa kwa mujibu wa Sheria, kanuni, taratibu pamoja na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Taarifa ya Matumizi**

Ofisi ya Mwansheria Mkuu kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ilikadiriwa kutumia jumla ya shilingi 2,273,100,000 kwa matumizi ya Ofisi. Kati ya hizo jumla ya shilingi 903,300,000 ikiwa ni mishahara na shilingi 1,369,800,000 kwa matumizi mengineyo.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 Ofisi ya Mwansheria Mkuu ilitumia jumla shillingi 1,408,189,436 kwa matumizi ya Afisi sawa na asilimia 62 ya makadirio. Kati ya fedha hizo shilingi 1,087,837,070 zilitumika kwa ajili ya mishahara sawa na asilimia 120 ya makadirio na shilingi 320,352,388 zilitumika kwa matumizi mengineyo sawa na asilimia 23 ya makadirio.

### 6.5.4 FUNGU G 04 – OFISI YA MKURUGENZI WA MASHTAKA

Ukaguzi wa hesabu za Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka kwa mwaka wa fedha 2020/2021 umefanywa kwa mujibu wa Sheria, kanuni, taratibu pamoja na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Taarifa ya Matumizi**

Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ilikadiriwa kutumia jumla ya shillingi 3,754,700,000 kwa matumizi ya kawaida, kati ya hizo shilingi 1,703,300,000 kwa ajili ya mishahara, shilingi 1,271,500,000 kwa matumizi mengineyo, shilingi 179,900,000 kwa ajili ya ruzuku, na shilingi 600,000,000 kwa ajili ya kazi za maendeleo.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka iliingiziwa na kutumia jumla ya shillingi 2,122,681,572 kwa matumizi ya kazi za kawaida sawa na asilimia 57 ya makadirio, kati ya hizo shilingi 1,640,667,325 kwa ajili ya mishahara sawa na asilimia 96 ya makadirio, na shilingi 62,446,184 ni kwa ajili ya ruzuku sawa na asilimia 35 ya makadirio, na shilingi 419,568,063 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo sawa na asilimia 33 ya makadirio.

**MATOKEO NA MAPENDEKEZO YA UKAGUZI**

#### 6.5.4.1 Dosari katika udhibiti wa matumizi ya mafuta shilingi 10,286,450

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika uwepo wa dosari ya matumizi ya mafuta yanayonunuliwa kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za Ofisi ambapo imebainika kwa mwaka wa fedha 2020/2021 Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka imetumia jumla ya lita 5,255 zenye thamani ya shilingi 10,286,450 ambapo imebainika mafuta hayo hayakutumika kwa shughuli za kiofisi badala yake yalitumika kwa shughuli binafsi za Mkurugenzi Mkuu wa Mashtaka pamoja na Naibu Mkurugenzi Mkuu wa Mashtaka hali ya kuwa viongozi hao hulipwa stahiki maalum kwa ajili ya matumizi ya mafuta ili kuhakikisha wanatekeleza majukumu yao kwa ufanisi bila ya kikwazo chochote.

Aidha, ukaguzi umebaini kati ya lita 5,255 zilizonunuliwa kwa ajilli ya matumizi ya ofisi jumla ya lita 2290 ambazo sawa na shilingi 4,387,420 zilitumiwa na Mkurugenzi Mkuu wa Mashtaka pamoja na lita 2,975 zenye thamani ya shilingi 5,899,030 zilitumiwa na Naibu Mkurugenzi wa Mashtaka jambo ambalo ni ukiukwaji wa taratibu za matumizi ya ofisi pamoja na kutokuzingatia miongozo ya utumishi wa umma inayoelekeza namna bora ya kupunguza kutumia matumizi yasio ya lazima na kuelekeza matumizi ya fedha katika maeneo yaliyokuwa na kipaumbele cha Serikali. Hata hivyo pamoja na uwepo wa dosari hio ukaguzi umebaini udhaifu uliojitokeza katika udhibiti wa mafuta kwa kukosekana mtumishi mwenye sifa wa kufanya kazi hio badala yake kazi hio imefanywa na mtu wa kalamazuu ambae hakuwa na elimu yakutosha juu ya utaratibu wa udhibiti wa mafuta.

Kutumia mafuta yaliopangiwa shughuli za uwendeshaji wa ofisi kunapelekea kuzorotesha malengo ya uwendeshaji wa shughuli za ofisi kwa mujibu yalivyopangwa na hatimae kupelekea kutokufikiwa kwa malengo yaliokusudiwa.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka kuhakikisha wanatekeleza majukumu ya kazi yao kwa mujibu wa makadirio ya matumizi ya fedha waliopangiwa ili kuepusha upotevu wa fedha za umma kwa matumizi binafsi ambayo hayana tija na taasisi ya umma. Mchanganuo wa matumizi ya mafuta hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli la hapo chini:-

**Jadweli Nambari 113 : Mafuta yaliyotumika kwa Gari ya Mkurugenzi – SMZ 834 A**

| Namba | Stakabadhi | Lita | Thamani ya fedha (Tshs.) |
|---|---|---|---|
| 1. | 202324 3/7/2020 | 60 | 95,880 |
| 2. | 202331 10/7/2020 | 60 | 105,060 |
| 3. | 202339 17/7/2020 | 60 | 105,060 |
| 4. | 202343 24/7/2020 | 60 | 105,060 |
| 5. | 202349 31/7/2020 | 60 | 105,060 |
| 6. | 207755 3/8/2020 | 50 | 87,550 |
| 7. | 207761 7/8/2020 | 60 | 105,060 |
| 8. | 207766 14/8/2020 | 60 | 113,100 |
| 9. | 227770 | 60 | 113100 |
| 10. | 227777 28/8/2020 | 60 | 113,100 |
| 11. | 227783 4/9/2020 | 60 | 113,100 |
| 12. | 227788 8/9/2020 | 40 | 96,280 |
| 13. | 227793 11/9/2020 | 60 | 114,420 |
| 14. | 227798 18/9/2020 | 60 | 114,420 |
| 15. | 230756 25/9/2020 | 60 | 114,420 |
| 16. | 230765 2/10/2020 | 60 | 114,420 |
| 17. | 230771 9/10/2020 | 60 | 114,420 |
| 18. | 230775 16/10/2020 | 60 | 115,080 |
| 19. | 230779 23/10/2020 | 60 | 115,080 |
| 20. | 230787 30/10/2020 | 60 | 115,080 |
| 21. | 230794 6/11/2020 | 60 | 115,080 |
| 22. | 230797 13/11/2020 | 60 | 116,880 |
| 23. | 243502 20/11/2020 | 60 | 116,880 |
| 24. | 243507 27/11/2020 | 60 | 116,880 |
| 25. | 243516 4/12/2020 | 60 | 116,880 |
| 26. | 243522 11/12/2020 | 60 | 114,720 |
| 27. | 243533 25/12/2020 | 60 | 114,720 |
| 28. | 243539 1/1/2021 | 60 | 114,720 |
| 29. | 243547 8/1/2021 | 60 | 114720 |
| 30. | 252104 15/1/2021 | 60 | 112,920 |
| 31. | 252109 22/1/2021 | 60 | 112,920 |
| 32. | 252116 29/1/2021 | 60 | 112920 |
| 33. | 252126 5/2/2021 | 60 | 112,920 |
| 34. | 252136 12/2/2021 | 60 | 116,040 |
| 35. | 252141 19/2/2021 | 50 | 96,700 |
| 36. | 276489 10/4/2021 | 50 | 108,250 |
| 37. | 288756 29/4/2021 | 40 | 86,600 |
| 38. | 288768 10/5/2021 | 40 | 87,800 |
| 39. | 288786 30/5/2021 | 40 | 87,800 |
| 40. | 303510 23/6/2021 | 30 | 68,160 |
| 41. | 303517 25/6/2021 | 30 | 68160 |
| **Jumla** | | **2,290** | **4,387,420** |

**Jadweli Nambari 114 : Mafuta yaliyotumika kwa Gari ya Naibu Mkurugenzi wa Mashtaka – SMZ 146 A**

| Namba | Stakabadhi | Lita | Thamani ya Fedha (Tshs.) |
|---|---|---|---|
| 1. | 202325 3/7/2020 | 50 | 79,900 |
| 2. | 202332 10/7/2020 | 50 | 87,550 |
| 3. | 202338 17/7/2020 | 50 | 87,550 |
| 4. | 202344 | 50 | 87,550 |
| 5. | 202348 31/7/2020 | 50 | 87,550 |
| 6. | 207758 7/8/2020 | 50 | 94,250 |
| 7. | 207763 10/8/2020 | 30 | 56550 |
| 8. | 207765 14/8/2020 | 50 | 94,250 |
| 9. | 207771 21/8/2020 | 50 | 94,250 |
| 10. | 207775 28/8/2020 | 50 | 94,250 |
| 11. | 207782 4/9/2020 | 50 | 94,250 |
| 12. | 207787 7/9/2020 | 40 | 75,400 |
| 13. | 207792 11/9/2020 | 50 | 95,350 |
| 14. | 207796 17/9/2020 | 20 | 38,140 |
| 15. | 230752 18/9/2020 | 50 | 95,350 |
| 16. | 230755 25/9/2020 | 50 | 95,350 |
| 17. | 230762 2/10/2020 | 50 | 95,350 |
| 18. | 230769 9/10/2020 | 50 | 95,350 |
| 19. | 230774 16/10/2020 | 50 | 95,900 |
| 20. | 230780 23/10/2020 | 50 | 95,900 |
| 21. | 230785 30/10 2020 | 50 | 95,900 |
| 22. | 230791 6/11 2020 | 50 | 95,900 |
| 23. | 230796 13/11 2020 | 50 | 97,400 |
| 24. | 243501 20/11/2020 | 50 | 97,400 |
| 25. | 243508 27/11/2020 | 50 | 97400 |
| 26. | 243514 4/12/2020 | 50 | 97,400 |
| 27. | 243520 11/12/2020 | 50 | 95,600 |
| 28. | 243526 18/12/2020 | 50 | 95,600 |
| 29. | 243532 25/12/2020 | 50 | 95,600 |
| 30. | 243538 1/1/2021 | 50 | 95,600 |
| 31. | 243546 8/1/2021 | 50 | 95,600 |
| 32. | 252103 15/1/2021 | 50 | 94,100 |
| 33. | 252108 22/1/2021 | 50 | 94,100 |
| 34. | 252115 29/1/2021 | 50 | 94,100 |
| 35. | 252125 5/2/2021 | 50 | 94,100 |
| 36. | 252132 12/2/2021 | 50 | 96,700 |
| 37. | 252139 19/2/2021 | 50 | 96,700 |
| 38. | 252148 26/2/202 | 50 | 96,700 |
| 39. | 252150 26/2/202 | 50 | 96,700 |
| 40. | 276455 5/3/2021 | 50 | 96,700 |
| 41. | 276460 12/3/2021 | 50 | 101,300 |
| 42. | 276466 19/3/2021 | 50 | 101,300 |
| 43. | 276470 24/3/2021 | 30 | 60,780 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 44. | 276472 29/3/2021 | 50 | 101,300 |
| 45. | 276479 2/4/2021 | 50 | 101,300 |
| 46. | 276485 9/4/2021 | 50 | 108,250 |
| 47. | 276492 16/4/2021 | 50 | 108,250 |
| 48. | 276497 20/4/2021 | 20 | 43,300 |
| 49. | 276500 22/4/2021 | 50 | 108,250 |
| 50. | 288757 30/4/2021 | 50 | 108250 |
| 51. | 288763 5/5/2021 | 30 | 64,950 |
| 52. | 288767 7/5/2021 | 50 | 108,250 |
| 53. | 288770 14/5/2021 | 50 | 109,750 |
| 54. | 288775 19/5/2021 | 20 | 43,900 |
| 55. | 288778 21/5/2021 | 50 | 109,750 |
| 56. | 288781 25/5/2021 | 30 | 65,850 |
| 57. | 288785 29/5/2021 | 50 | 109,750 |
| 58. | 288791 1/6/2021 | 30 | 65,850 |
| 59. | 288795 4/6/2021 | 50 | 109,750 |
| 60. | 288797 8/6/2021 | 20 | 43,900 |
| 61. | 303501 11/6/2021 | 50 | 113,600 |
| 62. | 303504 16/6/2021 | 20 | 45440 |
| 63. | 303508 18/6/2021 | 50 | 113,600 |
| 64. | 303511 24/6/2021 | 10 | 22,720 |
| 65. | 303515 25/6/2021 | 50 | 113,600 |
| 66. | 303519 30/6/2021 | 25 | 56,800 |
| **Jumla** | | **2975** | **5,899,030** |

### 6.5.4.2 Malipo yasiokuwa na tija shilingi 10,000,000

Katika ukaguzi uliofanyika kwa mwaka wa fedha 2020/2021 imebainika Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka iliingia makubaliano ya mdomo ya utengenezaji wa mfumo wa kielektroniki wa kuhifadhi kumbukumbu katika Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka na **Ndugu Shaaban H. Chum** ambaye alikuwa Mkurugenzi wa Idara ya Serikali Mtandao kwa thamani ya shilingi 29,997,500.

Aidha,ukaguzi umebaini Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka ilimlipa Bwana Shaaban H. Chumu jumla ya shilingi 10,000,000 kwa hati namba 12/3 kwa ajili ya utengenezaji wa mfumo wa kielektroniki wa kuhifadhi kumbukumbu, dosari ziliobainika katika ukaguzi ni kama zifuatazo:-

- Kutokutekelezwa kwa kazi waliokubaliana na kupelekea kutokupatikana kwa tija iliyokusudiwa.
- Kufanya malipo kwa kutumia hesabu ya mapato ya Serikali jambo ambalo ni kinyume na Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016.
- Kujitokeza kwa viashiria vya upotevu wa fedha za Umma unaotokana na kukiukwa taratibu za ufanyaji wa malipo ambapo malipo hayo yalipaswa yalipwe kupitia hesabu ya matumizi ya Wizara na sio hesabu ya mapato.
- Kufanya malipo kwa njia ya udanganyifu ambapo imebainika malipo hayo yalilipwa kwa fedha taslimu na sio kama yalivyoainishwa katika hati ya malipo kuwa yamelipwa kwa njia ya uhamisho wa muamala (TISS).

- Kutokuwepo kwa makubaliano ya mkataba wa utekelezaji wa kazi hiyo jambo ambalo limepelekea kujitokeza kwa upotevu wa fedha za Serikali ambapo kunakosekana kwa njia ya kuirejesha fedha hiyo katika mikono ya Serikali kutokana na kukosekana maandishi ya makubaliano na kulipwa fedha hizo kwa njia ya malipo taslimu.
- Kukosekana kwa tija ya matumizi ya fedha ya Serikali ambayo imepelekea kukwamisha malengo ya taasisi waliyojiwekea.
- Uwepo wa matumizi mabaya ya madaraka kwa aliekuwa Mkurugenzi wa Idara ya Serikali Mtandao kwa kuchukua maamuzi ya kutekeleza kazi hio kwa njia ya malipo ya fedha taslimu kama mfanyabiashara binafsi na sio mtumishi wa Umma jambo ambalo limepelekea ukiukwaji wa taratibu za kifedha na za kiutumishi kwa kuweka maslahi binafsi na kuisababishia hasara Serikali.
- Kuikosesha Serikali huduma iliyotarajia pamoja na kuikosesha mapato yatokanayo na kodi kama kazi hiyo ingelifanywa na kampuni au taasisi binafsi.

Kutokana na dosari zilizobainika hapo juu ukaguzi unaushauri uongozi wa Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka kuhakikisha mtoa huduma huyo anarejesha fedha yote aliyolipwa kwa ajili ya utekelezaji wa huduma iliyokosekana ili hatua nyengine ziweze kuchukuliwa kwa lengo la kuhakikisha huduma hiyo inapatikana na kuleta tija iliyokusudiwa.

**AFISI YA MKURUGENZI WA MASHTAKA - PEMBA**

### 6.5.4.3 Malipo yaliyofanywa kinyume na kifungu husika shilingi 11,890,000

Ukaguzi umebaini kuwa jumla ya shilingi 11,890,000 zimetumika kwa matumizi mbali mbali ya Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka – Pemba lakini malipo hayo yamefanyika kinyume na kifungu husika. Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 115 : Malipo yaliyofanywa kinyume na kifungu husika**

| Hati Namba | Hundi Namba | Kiasi cha fedha kilicholipwa (Tshs.) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 7/8 ya 12/4/2021 | 016433 | 5,040,000 | Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka | Malipo ya fedha kwa ajili ya safari kikazi |
| 2/4 ya 20/4/2021 | 020489 | 4,250,000 | | |
| 1/5 ya 4/5/2021 | 020886 | 2,600,000 | | Malipo ya overtime kwa walinzi |
| **Jumla** | | **11,890,000** | | |

### 6.5.4.4 Malipo kwa watoa huduma ambao hawakusajiliwa na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma shilingi 1,440,000

Kwa mujibu wa kifungu cha 23(1) cha Sheria ya Manunuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma kinaeleza kulingana na masharti ya sheria hii mtu, kampuni au taasisi haitawasilisha zabuni au vyenginevyo kushiriki katika manunuzi ya Umma isipokua chombo kiwe kimesajiliwa na Mamlaka ya Manunuzi.

Kwa mujibu wa kifungu cha 23(2), zabuni kutoka kwa mtu, kampuni au chombo ambacho hakijasajiliwa haifai na hakitazingatiwa na taasisi ya ununuzi.

Ukaguzi umebaini kwamba Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka Pemba imefanya manunuzi na watoa huduma mbali mbali ambapo watoa huduma hao hawakusajiliwa na Mamlaka ya Manunuzi kwa mujibu wa sheria ambapo kumepelekea kushindwa kujiridhisha uhalali wa malipo hayo.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na vifungu vya Sheria nilivyovinakili hapo juu vya Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka - Pemba kufanya manunuzi kwa kuzingatia kanuni,sheria pamoja na miongozo mbali mbali iliyopo. Mchanganuo wa watoa huduma ni kama inavyoonekana katika jadweli lifuatalo:-

**Jadweli Nambari 116 : Malipo kwa watoa huduma ambao hawakusajiliwa**

| Hati Namba | Hundi Namba | Kiasi cha fedha kilicholipwa (Tshs.) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 23/8 21/8/2020 | 016650 | 1,228,000 | Hilali Nassor Said | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa na matengenezo ya Ofisi. |
| ½ 4/2/2021 | 019317 | 92,000 | Classic Azam Centre | Malipo ya fedha kwa ajili ya viburudishaji |
| ½ 4/2/2021 | 019317 | 120,000 | | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa Pemba Cable |
| **Jumla** | | **1,440,000** | | |

### 6.5.4.5 Malipo ambayo hayakukatwa kodi ya zuio shilingi 5,394,292

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba jumla ya shilingi 5,394,292 zimetumika kwa ajili ya matumizi mbali mbali ya Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka - Pemba kwa watoa huduma mbali mbali bila ya kukatwa kodi ya zuio.

Kutokukata kodi ya zuio ni kwenda kinyume na kifungu namba 50(2) cha Sheria nambari 7 ya Usimamizi wa Kodi ya mapato ya mwaka 2009 pamoja na marekebisho yake ya mwaka 2020 jambo ambalo linapelekea kuikosesha mapato Serikali. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 117 : Malipo ambayo hayakukatwa kodi ya zuio**

| Hati Namba | Hundi Namba | Kiasi cha Fedha kilicholipwa (Tshs.) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 9/8 ya 21/8/2020 | 016474 | 3,631,292 | Tahfif Aluminium and glass workshop. | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya matengenezo ya Afisi. |
| 23/8 ya 21/8/2020 | 016650 | 1,228,000 | Hilali Nassor Said | |
| 11/6 ya 22/6/ 2021 | 021860 | 535,000 | Kheir Mabrouk Juma | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya kuandikia |
| **Jumla** | | **5,394,292** | | |

#### 6.5.4.6 Malipo ambayo hayakufuata utaratibu shilingi 4,450,000

Ukaguzi umebaini jumla ya shilingi 4,450,000 zimelipwa kwa maposho mbali mbali kutokana na kazi zinazofanywa na watendaji wa Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka bila ya kuwepo kwa muongozo unaoidhinisha ulipaji wa maposho hayo ili kuweza kuthibitisha uhalali wa malipo hayo.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 34(1) cha Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 118 : Malipo ambayo hayakufuata utaratibu**

| Hati Namba | Hundi Namba | Kiasi cha fedha kilicholipwa (Tshs.) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| ½ 03/02/2021 | 019317 | 700,000 | Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka Pemba. | Malipo ya fedha kwa ajili ya posho la kikao |
| | 019317 | 500,000 | | Malipo ya fedha kwa ajili ya posho la utafiti |
| | 019317 | 1,500,000 | | Malipo ya fedha kwa ajili ya posho la dhamana |
| | 019317 | 1,400,000 | | |
| | 019317 | 350,000 | | |
| **Jumla** | | **4,450,000** | | |

### 6.5.5 FUNGU G 05 – TUME YA KUREKEBISHA SHERIA

Ukaguzi wa hesabu za Tume ya Kurekebisha Sheria kwa mwaka wa fedha 2020/2021 umefanywa kwa mujibu wa Sheria, kanuni, taratibu pamoja na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Taarifa ya Matumizi**

Tume ya Kurekebisha Sheria kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ilikadiriwa kutumia jumla ya shilingi 1,173,500,000 kwa matumizi ya Taasisi. Kati ya fedha hizo jumla ya shilingi 360,500,000 kwa ajili ya mishahara ya wafanyakazi wa Tume shilingi 813,000,000 kwa ajili ya matumizi mengineo.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 Tume ya Kurekebisha Sheria ilitumia jumla shilingi 648,904,021 sawa na asilimia 55 ya makadirio. Kati ya fedha hizo shilingi 373,959,395 kwa ajili ya matumizi ya mishahara ambapo ni sawa na asilimia 104 ya makadirio na shilingi 274,944,626 kwa ajili ya matumizi ya kawaida sawa na asilimia 34 ya makadirio.

### 6.5.6 FUNGU E 07 - KAMISHENI YA UTUMISHI WA UMMA

Ukaguzi wa hesabu za Kamisheni ya Utumishi wa Umma kwa mwaka wa fedha 2020/2021 umefanywa kwa mujibu wa Sheria, kanuni, taratibu pamoja na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Taarifa ya Matumizi**

Kamisheni ya Utumishi wa Umma kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ilikadiriwa kutumia jumla ya shilingi 1,276,100,000. Kati ya fedha hizo shilingi 444,000,000 kwa ajili ya mishahara na shilingi 832,100,000 kwa matumizi mengineo.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 Kamisheni ya Utumishi ya Umma iliingiziwa na kutumia jumla ya shilingi 672,570,433 kutoka katika Mfuko wa Hazina sawa na asilimia 53 ya makadirio. Kati ya fedha hizo shilingi 511,429,600 zilitumika kwa mishahara sawa na asilimia 76 ya makadirio na shilingi 161,140,833 zilitumika kwa matumizi mengineyo sawa na asilimia 24 ya makadirio.

**MATOKEO NA MAPENDEKEZO YA UKAGUZI**

#### 6.5.6.1 Kufanyika kwa matumizi kinyume na vifungu vya matumizi shilingi 13,225,272

Ukaguzi uliofanywa umebaini jumla ya shilingi 13,225,272 zimetumika kwa ajili ya kununua huduma mbali mbali ya matumizi ya Ofisi ya Kamisheni ya utumishi wa Umma, dosari iliyobainika katika ukaguzi ni kufanya matumizi kinyume na vifungu vya matumizi husika na bila ya uwepo wa uhaulishaji wa fungu moja kwenda fungu jengine jambo ambalo huwenda likapelekea kujitokeza kwa utekelezaji mdogo kwa baadhi ya mafungu na kupelekea utekelezaji usio na tija na kutokufikiwa kwa malengo yaliyokusudiwa.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Kamisheni ya Utumishi wa Umma kuhakikisha matumizi yote yanafanywa kwa mujibu wa vifungu husika na ikitokezea matumizi mengineyo ni vyema taratibu za uhaulishaji wa fungu moja kwenda jengine zifuatwe ili kuepuka matumizi yasio na tija. Mchanganuo wa matumizi hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 119: Matumizi yaliyofanyika kinyume na vifungu vya matumizi**

| Hati namba | Hundi namba | Kiasi cha fedha kilichotumika (Tshs) | Aliyelipwa | Maelezo | |
|---|---|---|---|---|---|
| 11/5/21 | TISS | 3,601,262.14 | RJ Refrigeration and Electrical | Ununuzi wa Tv, Friji, na Cooker kwa ajili ya zawadi | Kifungu kilichotumika cha Computer 6112208 |
| 1(10)4/21 | 142 | 576,000 | Kamisheni ya Utumishi wa Umma | Malipo ya posho na viburudishaji Kikao. | 2206001 Kifungu cha Stationary |
| 6(sub 20/8) | 117 | 3,570,000 | | Posho la vikao | 2111006 Kifungu Transport allowance |
| 6(Sub19/8 | 117 | 3,900,000 | | | 2111006 Kifungu cha Transport allowance |
| 6(sub11/8 | 117 | 1,000,000 | | Malipo ya awamu ya kwanza kwa ajili ya mafunzo ya muda mfupi. | |
| 28 (sub 6/8 | 119 | 578,010 | | Malipo ya awamu ya pili kwa ajili ya ma-funzo ya muda mfupi. | 2111006 Kifungu cha Transport allowance |
| **Jumla** | | **13,225,272** | | | |

### 6.5.7 FUNGU E08 - TUME YA UTUMISHI SERIKALINI

Ukaguzi wa hesabu za Tume ya Utumishi Serikalini kwa mwaka wa fedha 2020/2021 umefanywa kwa mujibu wa Sheria, kanuni, taratibu pamoja na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Taarifa ya Matumizi**

Tume ya Utumishi Serikalini kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ilikadiriwa kutumia jumla ya shilingi 640,000,000 kwa matumizi ya Taasisi. Kati ya fedha hizo jumla ya shilingi 210,100,000 kwa ajili ya mishahara na shilingi 429,900,000 kwa matumizi mengineyo.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 Tume ya Utumishi Serikalini ilitumia jumla shilingi 340,445,120 ambapo ni sawa na asilimia 53. Kati ya fedha hizo shilingi 212,638,120 zilitumika kwa ajili ya mishahara sawa na asilimia 101 ya makadirio na shilingi 127,807,000 zilitumika kwa matumizi ya kawaida sawa na asilimia 30 ya makadirio.

### 6.5.8 TUME YA MAADILI YA VIONGOZI WA UMMA ZANZIBAR

Ukaguzi wa hesabu za Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2020/2021 umefanywa kwa mujibu wa Sheria, kanuni, taratibu pamoja na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Taarifa za Matumizi**

Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ilikadiriwa kutumia jumla ya shilingi 1,259,672,160. Kati ya fedha hizo shilingi 788,300,000 kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida , shilingi 175,000,000 kwa ajili ya matumizi ya kazi za maendeleo, na shilingi 296,372,160 kwa ajili ya mishahara ya wafanyakazi wa Tume.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 Tume ya Maadili Viongozi wa Umma Zanzibar imeingiziwa na kutumia jumla ya shilingi 654,345,208 sawa na asilimia 52 ya makadirio. Kati ya fedha hizo jumla ya shilingi 187,183,70 zilitumika kwa kazi za kawaida sawa na asilimia 24 ya makadirio, shilingi 175,000,000 zilitumika kwa kazi za maendeleo sawa na asilimia 100 ya makadirio na shilingi 292,161,502 zilitumika kwa ajili ya mishahara ya wafanyakazi wa Tume ambazo ni sawa na asilimia 99 ya makadirio.

**MATOKEO NA MAPENDEKEZO YA UKAGUZI**

#### 6.5.8.1 Kutokukamilika kwa mradi wa maendeleo wa shilingi 50,000,000

Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma Zanzibar inaendelea kuimarisha mfumo wa Tehama kwa Ofisi ya tume iliyopo Pemba ambapo mradi huo unakisiwa kuwa na thamani ya shilingi 750,000,000. Kutokana na ukubwa wa gharama za utekelezaji wa mradi wenyewe pamoja na uchache wa upatikanaji wa fedha ambazo zitawezesha mradi huo kufanikiwa, dosari mbalimbali zimebainika kujitokeza katika ukaguzi ambazo zinaweza zikapelekea matumizi mabaya ya fedha za umma na kutokupatikana kwa tija iliyokusudiwa.

Aidha, ukaguzi umebaini Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma imefanya malipo kwa awamu mbili tofauti kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya uendeshaji na ufanikishwaji wa mradi huo ambapo katika awamu ya mwanzo zililipwa jumla ya shilingi 50,000,000 kwa kampuni ya PLV Digital Investment Company ikiwa ni malipo ya ununuzi wa vifaa hivyo kwa awamu ya mwanzo. Vile vile katika awamu ya pili Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma imefanya malipo ya shilingi 175,000,000 kwa ajili ya ununuzi wa vifaa hivyo hivyo kwa awamu ya pili.

Hadi ukaguzi unakamilika jumla ya shilingi 225,000,000 zimelipwa kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya mradi huo. Kutokana na kufanyika kwa manunuzi hayo ambayo yanategemea upatikanaji wa fedha za uendeshaji wa ofisi miongoni mwa dosari zinazotegemewa kujitokeza kwa baadae ni kama zifuatazo:-

- Kutokukamilika kwa mradi huo kwa wakati kutokana na ukosefu wa upatikanaji wa fedha.
- Kutokujulikana muda wa kukamilika kwa mradi huo kutokana na kutekelezwa kwa kutegemea fedha za matumizi ya kawaida jambo ambalo linaweza kupelekea gharama za ununuzi wa vifaa kuongezeka kutokana na thamani ya shilingi kwa dola.
- Ubunifu wa mradi haukuzingatia thamani halisi ya fedha kwa wakati wa sasa na mahitaji ya vifaa vinavyohitajika kwa bei ya soko ilivyo kutokana na kupanda kwa gharama ya vifaa vya kielektroniki jambo ambalo linaweza likapelekea kutekeleza matakwa ya mradi huo kwa thamani kubwa zaidi kuliko ilivyotegemewa.
- Kujitokeza kwa uwezekano mkubwa wa vifaa vinavyonunuliwa kutokufanya kazi kama ilivyokusudiwa kutokana na vifaa hivyo kununuliwa kidogo kidogo na kuhifadhiwa ghalani kwa muda mrefu hadi vikamilike kwake vyote.
- Kujitokeza kwa gharama ya ziada ya kusafirisha vifaa hivyo pindi vitakapokamilika kwa vile vifaa hivyo vinahifadhiwa katika store ya Unguja na mategemeo ya matumizi yake kwa ajili ya Ofisi ya Pemba.
- Kujitokeza kwa marudio ya upangaji wa matumizi ya bajeti ya ununuzi wa vifaa hivyo kusikotekelezeka kutokana na ufinyu wa upatikanaji wa bajeti.

Kutokana na dosari zilizobainika hapo juu kuna uwezekano mkubwa wa kujitokeza kwa matumizi mabaya ya fedha yatakayotokana na manunuzi yanayoendelea kufanyika bila ya kuwa na tija iliokusudiwa pindi vifaa hivyo vinapo endelea kukaa kwa muda mrefu bila ya kufanya kazi na hatimae kuharibika na kuisababishia hasara Serikali.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma kuhakikisha unapeleka ombi maalum Serikalini ili kuweza kupatiwa fedha za dharura kwa ajili ya kukamilisha mradi huo kwa lengo la kuokoa uharibifu utakao jitokeza wa vifaa vilivonunuliwa na kukaa muda mrefu na hatimae kutokufanya kazi.

Aidha, ukaguzi unashauri uongozi wa Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma kuhakikisha unatafuta eneo maalum (Ofisi) ambayo itakuwa na uwezo na nafasi ya kutosha ya kuweza kufunga mitambo yao kabla ya kukamilika kwa manunuzi yanayoendelea kufanyika ili kunusuru kuendelea kuweka vifaa katika store kwa muda mrefu jambo ambalo linaweza kupelekea kuharibika au kutofanya kazi ipasavyo kwa vifaa hivyo kutokana na kukaa kwa muda mrefu katika mazingira ambayo si rafiki.

### 6.5.9 WAKALA WA MIUNDOMBINU YA TEHAMA ZANZIBAR

Ukaguzi wa hesabu za mwaka wa fedha 2020/2021 kwa Wakala wa Miundombinu ya TEHAMA Zanzibar umefanywa kwa mujibu wa Sheria, kanuni, taratibu pamoja na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Taarifa ya Mapato**

Kwa mwaka wa fedha 2020/2021 Wakala wa Miundombinu ya TEHAMA Zanzibar ilikadiriwa kupokea jumla ya shilingi 1,760,000,000 ikiwa ni ruzuku kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni 2021, Wakala wa Miundombinu ya Tehama Zanzibar ilipokea jumla ya shilingi 4,221,202,782 . Kati ya fedha hizo jumla ya shilingi 1,727,810,000 ikiwa ni ruzuku kutoka Serikali kuu, sawa na asilimia 98 ya makadirio, na shilingi 2,493,392,782 ikiwa ni makusanyo kutoka katika vyanzo vya ndani ambapo vyanzo hivyo havikuwa na makadirio.

**Taarifa ya Matumizi**

Wakala wa Miundombinu ya TEHAMA Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2020/2021 iliidhinishiwa kutumia jumla ya shilingi 1,760,000,000 kwa ajili ya matumizi ya kawaida.

Hadi kufikia tarehe Juni 30, 2021 kiasi cha shilingi 1,727,810,000 zimeingizwa na kutumika kwa kazi za kawaida sawa na asilimia 98 ya makadirio.

**MATOKEO NA MAPENDEKEZO YA UKAGUZI**

### 6.5.9.1 Kutokutekelezeka kwa Mpango wa Manunuzi

Katika ukaguzi uliofanyika kwa mwaka wa fedha 2020/2021 imebainika Wakala wa Miundombinu ya TEHAMA Zanzibar imeandaa mpango wa manunuzi kwa ajili ya utekelezaji wa manunuzi mbali mbali kwa mujibu wa makadirio ya mahitaji ya bidhaa, pamoja na huduma mbali mbali zinazohitajika kwa ajili ya shughuli mbali mbali za Wakala kama zilivyoainishwa katika mpango kazi wa mwaka.

Dosari ya ukaguzi iliyobainika ni kutokutekelezeka kikamilifu mpango wa manunuzi kwa kutokufanyika kwa manunuzi yenye thamani ya shilingi 4,000,000,000 kwa ajili ya uboreshaji wa kituo cha Kitaifa cha kuhifadhia taarifa (Data Center)jambo ambalo limetokana na ucheleweshwaji wa kuingiziwa kwa fedha za utekelezaji wa uboreshaji wa kituo hicho.

Kitendo cha kuchelewa kuingiziwa fedha kwa wakati kimepelekea kutokutekelezeka kwa mpango wa manunuzi na kurejesha nyuma jitihada za kufikia malengo yaliyopangwa na Wakala wa Miundombinu ya TEHAMA Zanzibar jambo ambalo linaweza kupelekea kutokutekelezeka kwa lengo hilo kutokana na kuwepo kwa mfumko wa bei za vifaa vya ujenzi. Aidha, utekelezaji wa jambo hilo linaweza kuathiri makadirio yaliyopangwa kutokana na kununua bidhaa kwa bei ya juu kuliko makadirio ya awali.

## 6.5.10 KAMISHENI YA WAKFU NA MALI YA AMANA - PEMBA

### 6.5.10.1 Hati za malipo zenye vielelezo pungufu shilingi 9,554,700

Ukaguzi umebaini kwamba jumla ya shilingi 9,554,700 zimetumika kwa malipo mbali mbali ya Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana Pemba lakini baadhi ya vielelezo husika havikuambatanishwa na hati za malipo ili kuweza kuthibitisha uhalali wa malipo hayo.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 34(1) cha Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 120 : Hati za malipo zenye vielelezo pungufu**

| Hati Namba | Hundi Namba | Kiasi cha fedha kilicholipwa (Tshs.) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 11/7 22/7/2020 | 001335 | 2,009,200 | Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana - Pemba | Malipo ya fedha wanazokatwa Watumishi. |
| 1/8 10/8/2020 | 001339 | 500,000 | Saleh Nassor Suleiman | Malipo ya fedha kwa ajili ya safari kikazi. |
| 6/8 17/8/2020 | 001342 | 375,000 | Juma Abdalla Kheri | Malipo ya fedha kwa ajili ya matengenezo ya Komputa pamoja na mashine ya fotokopi. |
| 12/8 18/8/2020 | 001348 | 122,500 | Masoud Ali Masoud | Malipo ya fedha kwa ajili ya kufanyakazi muda baada ya masaa ya kazi. |
| 14/12 30/12/2020 | - | 1,440,000 | Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana - Pemba | Uhaulishaji wa fedha kutoka hesabu No. 0404314000 kwenda hesabu No. 0404443000. |
| 3/10 7/10/2020 | 001373 | 2,758,000 | Ali Mbarouk Dadi | Malipo ya fedha kwa ajili ya posho la kikao. |
| 4/6 17/06/2021 | 001477 | 750,000 | Ali Haji Ali | Malipo ya fedha kwa ajili ya viburudishaji. |
| 4/5 6/5/2021 | 001466 | 1,000,000 | Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana - Pemba | Malipo ya fedha kwa ajili ya viburudishaji. |
| 6/3 | 001440 | 600,000 | Masoud Ali Masoud | Malipo ya fedha kwa ajili ya kutekeleza mpango kazi. |
| **Jumla** | | **9,554,700** | | |

### 6.5.10.2 Ukodishaji wa majengo ya Serikali kwa thamani ndogo shilingi 3,319,800

Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana Pemba inamiliki majengo ya biashara na kuingia mikataba ya ukodishaji ili kuweza kuingizia Serikali mapato yatokanayo na kadi ya majengo hayo.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika ukodishaji wa majengo ya Serikali hauendani na thamani halisi ya fedha kwa kipindi tulichonacho kwani imebainika Kamisheni kukodisha kwa wastani wa shilingi 5,000 hadi shilingi 240,000 jambo ambalo linapelekea kuikosesha mapato Serikali kutokana kwa kukosekana kwa uhalisia wa thamani ya fedha kwa mujibu wa uchumi wa kipato cha mfanya biashara.

Aidha ukaguzi umeshindwa kupatiwa bei elekezi iliyopangwa na Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana kwa ajili ya ukodishaji wa majengo ya Serikali kinyume na miongozo ya fedha. Mchanganuo wa malipo ya ukodishwaji huo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 121 : Ukodishaji wa majengo ya Serikali kwa thamani ndogo**

| Namba ya mkataba | Jina la Mkodishwaji | Mahali ilipo | Thamani ya kodi kwa mwezi (Tshs.) |
|---|---|---|---|
| WH.1/D.379 | Yakoub Ali Mohammed | Miembeni Chake Chake | 65,000 |
| WH.1/D.426 | Rashid Gharib Ali | | 91,000 |
| WH.1/D.422 | Nassor Mohammed Dadi | | 65,000 |
| WH.1/D.383 | Mzee Ali Abdalla | | 65,000 |
| WH.1/D.418 | Abdalla Ali Masoud | | 65,000 |
| WH.1/D.562 | Juma Faki Khatib | | 52,000 |
| WH.1/D.397 | Ahmed Abdalla Issa | | 65,000 |
| WH.1/D.422 | Masoud Omar Juma | | 26,000 |
| WH.2 / D.564 | Zahor Saleh Ali | | 45,000 |
| Namba 2 | Ali Muradi Dilshad | | 240,000 |
| WH.2 / D.525 | Khamis Mdungi Mwadini | | 98,700 |
| WH.1/D.379 | Khalef Kassim Hamed | Misufini Chake Chake | 65,000 |
| WH.1/D.520 | Suleiman Salum Issa | | 45,000 |
| WH.2/D.563 | Ali Said Ali | | 65,000 |
| WH.2/D.583 | Kassim Juma Mussa | | 15,000 |
| Namba 2 | Ali Muradi Dilshad | Miembeni Chake Chake | 120,000 |
| | Khalef Kassim Hamed | Misufini Chake Chake | 240,000 |
| | Jumuia Ya Ukwem | Miembeni Chake Chake | 200,000 |
| | Abdalla Issa Saleh | Miembeni Chake Chake | 240,000 |
| | Mohammed Hassan Khamis | Miembeni Chake Chake | 120,000 |
| WH.3/D.549 | Juma Mohammed Said | Misufini Chake Chake | 204,000 |
| WH.4/D.536 | Humoud Mohammed Humoud | Miembeni Chake Chake | 197,000 |
| WH.4/D.537 | Hassan Abdalla Nuhu | | 197,000 |
| WH.5/D.538 | Salha Said Ahmed | | 163,800 |
| WH.5/D.558 | Ashraf Ikbal Ibrahim | | 13,0000 |
| WH.5/D.559 | Salum Mbaraka Salum | | 144,300 |
| Namba 6 | Jumuia ya Jumaza | Mkungu Malofa | 150,000 |
| KIWANJA | Seif Mohammed Omar | Sokoni Chake Chake | 5000 |
| WH.7/D.550 | Saleh Nassor Suleiman | Kipangani Wete | 52,000 |
| AH.1/584 | Raya Khamis Hamad | Mtemani Wete | 39,000 |
| AH.2/D.594 | Mussa Alim Bajaka | | 50,000 |
| **Jumla** | | | **3,319,800** |

## 6.6 WIZARA YA NCHI (OR) KAZI, UCHUMI NA UWEKEZAJI

### 6.6.1 FUNGU Q01 – OFISI YA RAIS , KAZI, UCHUMI NA UWEKEZAJI

Ukaguzi wa hesabu za Ofisi ya Rais Kazi Uchumi na Uwekezaji kwa mwaka wa fedha 2020/2021 umefanywa kwa mujibu wa Sheria, kanuni, taratibu pamoja na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Taarifa ya Mapato**

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021 Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji ilikadiriwa kukusanya jumla ya shilingi 2,108,555,000 kutokana na vyanzo mbalimbali vya mapato vya ndani na shilingi 16,263,544,886 kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni,2021 Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji ilifanikiwa kukusanya jumla ya mapato ya shilingi 963,198,655.60 kutoka vyanzo vya ndani sawa na asilimia 46 ya makadirio, na shilingi 11,733,493,146 kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina sawa na asilimia 72 ya makadirio.

**Taarifa ya Matumizi**

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021 Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji ilikadiriwa kutumia jumla ya shilingi 16,263,544,886. Kati ya fedha hizo shilingi 15,934,151,777 zilipangwa kutumika kwa kazi za kawaida na shilingi 329,393,109 zilipangwa kutumika kwa kazi za maendeleo.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji imeingiziwa na kutumia jumla ya shilingi 11,733,493,146 sawa na asilimia 72.15 ya makadirio. Kati ya hizo shilingi 11,697,636,803 kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida sawa na asilimia 73 ya makadirio, na shilingi 35,856,343 za maendeleo sawa na asilimia 11 ya makadirio.

**MATOKEO NA MAPENDEKEZO YA UKAGUZI**

### 6.6.1.1 Kuwepo wadaiwa sugu ambao hawajarejesha mikopo kwa muda mrefu shilingi 395,374,800

Katika ukaguzi uliofanyika umebaini kuwepo kwa madeni ya wadaiwa sugu yenye thamani ya shilingi 395,374,800 ambayo haijarejeshwa kutoka mwaka 2012 hadi 2021 jambo ambalo ni kinyume na malengo ya utoaji wa mikopo hiyo.

Aidha ukaguzi umebaini waliopewa mikopo kutokulipa mikopo yao kwa kipindi kirefu jambo ambalo limesababisha fedha hiyo ya mkopo kutokuzunguka kwa wananchi wengine ambao wanahitaji mikopo hiyo.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na muongozo wa Mfuko wa Uwezeshaji wananchi kiuchumi kwa mujibu wa kifungu nambari 4.4(vi) cha mwaka 2014 kinachoeleza kwamba mteja atakayepitisha kipindi cha malipo atalazimika kulipa adhabu ya asilimia 1 ya malipo ya mwezi mara miezi iliyokiukwa kulipwa katika mwaka husika.

Aidha ukaguzi umebaini adhabu hiyo ya kuchelewa kulipa mkopo bado haijafanyiwa kazi jambo ambalo inaikosesha Serikali mapato yanayotokana na adhabu hiyo.

Wadaiwa sugu wa mkopo wa kawaida ni kama wanavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 122 : Wadaiwa sugu ambao hawajarejesha mikopo kwa muda mrefu**

| Namba | Jina la Anayedaiwa | Fedha zilizokopwa (Tshs) | Fedha ya mkopo iliyorejeshwa (Tshs.) | Fedha za mkopo ambazo hazijarejeshwa hadi sasa (Tshs) |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Mjini | 245,805,000.00 | 120,179,000 | 125,626,000.00 |
| 2 | Magharibi A | 114,400,000.00 | 48,400,700 | 65,999,300.00 |
| 3 | Magharibi B | 209,620,000.00 | 101,485,000 | 108,135,000.00 |
| 4 | Kaskazini A | 89,380,000.00 | 51,262,500 | 38,117,500.00 |
| 5 | Kasikazini B | 9,200,000.00 | 6,432,000 | 2,768,000.00 |
| 6 | Kusini | 49,200,000.00 | 31,483,000 | 17,717,000.00 |
| 7 | Wilaya ya Kati | 65,159,000 | 32,147,000 | 37,012,000 |
| **Jumla** | | **782,764,000** | **387,389,200** | **395,374,800.00** |

Kutokurejeshwa mikopo kwa wakati kunapelekea kukosekana kwa mikopo kwa vikundi vyengine na pia kusababisha mfuko wa uwezeshaji kutotimiza malengo na majukumu yake iliyojipangia kwa wakati.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Mfuko wa Uwezeshaji kuhakikisha wadaiwa wanarejesha mikopo hiyo kwa mujibu wa mikataba iliyosainiwa na pande zote mbili ili wananchi wengine wafaidike na mikopo hiyo ili kujikwamua katika maisha duni ya kila siku na waweze kupata kipato na kujitegemea.

Aidha ukaguzi unashauri uongozi wa Mfuko kukaa pamoja na wadaiwa hao ili waweze kufikia hatua mzuri juu ya urejeshaji wa mkopo huo.

**HESABU YA MKOPO WA MBOGAMBOGA (AKAUNTI NAMBARI 0451702000)**

### 6.6.1.2 Kutokurejeshwa fedha za mkopo wa mboga mboga kwa muda mrefu kutoka taasisi za Serikali shilingi 69,736,000

Katika ukaguzi uliofanyika katika kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021 kupitia Hesabu ya mbogamboga, ukaguzi umebaini Jumla ya shilingi 69,736,000 za mkopo wa mboga mboga zilikopeshwa kupitia vikundi mbali mbali vya wajasiriamali wa mboga mboga kwa muda mrefu lakini hadi ukaguzi unakamilika mikopo hiyo haijarejeshwa kwa mujibu wa mikataba husika. Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na makubaliano ya mkataba husika. Mchanganuo wa wadaiwa hao ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 123 : Fedha za mkopo wa mboga mboga ambazo hazijarejeshwa kwa muda mrefu**

| Namba | Jina la mkopaji | Fedha ya mkopo aliokopeshwa (Tshs) | Fedha zilizorejeshwa (Tshs) | Fedha za mkopo zilzokuwa hazijarejeshwa (Tshs) |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Mjini | 12,300,000.00 | 4,190,000 | 8,110,000.00 |
| 2. | Magharibi A | 12,450,000.00 | 5,145,000 | 7,305,000.00 |
| 3. | Magharibi B | 39,600,000.00 | 13,541,000 | 26,059,000.00 |
| 4. | Kaskazini A | 7,000,000.00 | 1,670,000 | 5,330,000.00 |
| 5. | Kasikazini B | 8,800,000.00 | 4,558,000 | 4,242,000.00 |
| 6. | Kusini | 21,000,000.00 | 14,015,000 | 6,985,000.00 |
| 7. | Wilaya ya Kati | 16,000,000.00 | 4,295,000 | 11,705,000.00 |
| **Jumla** | | **117,150,000.00** | **47,414,000** | **69,736,000.00** |

Kutokurejeshwa mikopo kwa wakati kunapelekea kukosekana kwa mikopo kwa vikundi vyengine vya wajasiriamali na kusababisha mfuko wa uwezeshaji kutotimiza malengo na majukumu yake iliyojipangia kwa wakati.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Mfuko wa Uwezeshaji kuhakikisha wadaiwa wanarejesha mikopo hiyo kwa mujibu wa mikataba iliyosainiwa na pande zote mbili ili fedha hizo ziweze kurejeshwa kwa wakati na wananchi wengine waweze kufaidika na mikopo hiyo kwa kuweza kujiongeza kipato kutokana na hali duni ya kimaisha ya kila siku.

### 6.6.1.3 Kutokurejeshwa fedha za mkopo kwa muda mrefu kutoka taasisi za Serikali shilingi 66,235,000

Katika ukaguzi uliofanyika katika kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021 kupitia Mfuko wa Uwezeshaji wa Wizara, ukaguzi umebaini Jumla ya shilingi 66,235,000 za mkopo zilitolewa kupitia vikundi mbali mbali vya wajasiriamali kwa muda mrefu, dosari iliyobainika na ukaguzi ni kwamba mikopo ya fedha hizo hazijarejeshwa kwa mujibu wa mikataba husika. Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na makubaliano ya mkataba husika. Mchanganuo wa wadaiwa hao ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini :-

**Jadweli Nambari 124 : Fedha za mkopo ambazo hazijarejeshwa kwa muda mrefu kutoka taasisi za Serikali**

| Walengwa wa mkopo | Jina la Mkopaji | Tarehe ya Mkopo | Fedha zilizokopeshwa (Tshs.) | Fedha ya mkopo iliyorejeshwa (Tshs.) | Tarehe ya mwisho ya kurejesha malipo ya mkopo | Fedha ya mkopo ambayo haijarejeshwa |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Kusini | Dongwe Juhudi Zetu (Bwejuu) | 08-03-16 | 20,000,000 | 16,335,000 | 02-10-20 | 3,665,000 |
| Kaskazini A | Berefoot College Of Zanzibar /Pendo/Asha Khamis (Kikobweni) | 30-07-18 | 20,060,000 | 10,000,000 | 26-09-18 | 10,000,000 |
| Mjini | Busara Njema B. Group / Khamis Islsm Suleiman (Rahaleo) | 07-11-16 | 8,000,000 | 7,600,000 | 25-08-17 | 400,000 |
| Mjini | Uwamwema (Mkunazini) | 22-01-15 | 80,000,000 | 27,830,000 | 23-07-19 | 52,170,000 |
| **Jumla** | | | **128,060,000** | **61,825,000** | | **66,235,000** |

Kutokurejeshwa mikopo kwa wakati kunapelekea kukosekana kwa mikopo kwa vikundi vyengine vya wajasiriamali kusababisha mfuko wa uwezeshaji kutotimiza malengo na majukumu yake iliyojipangia kwa wakati.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Mfuko wa Uwezeshaji kuhakikisha wadaiwa wanarejesha mikopo hiyo kwa mujibu wa mikataba iliyosainiwa na pande zote mbili ili fedha hizo ziweze kurejeshwa na wananchi wengine waweze kufaidika na mikopo hiyo kwa kuweza kujiongeza kipato kutokana na hali duni ya kimaisha ya kila siku.

### 6.6.1.4 Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi kutokuandaliwa na kutokuwasilisha taarifa za hesabu za mwisho wa mwaka kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa ukaguzi

Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi kiuchumi ni mfuko unaojitegemea ambao hutoa mikopo kwa wananchi kwa lengo la kujiajiri na kupunguza umasikini. Kifungu namba 24(1) cha "legal Suppliment (Part II) to the Zanzibar Government Gazette Vol CXXIV No. 6584" ya tarehe 9 Oktoba 2015 iliyoruhusu uanzishwaji wa Mfuko wa Kujitegemea kinaeleza kwamba mfuko lazima waweke rikodi za hesabu zao kutokana na vigezo vya uhasibu ambavyo vimekubaliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu. Hesabu hizo zilizowekwa zinatakiwa zikaguliwe na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu kwa mujibu wa kifungu namba 119(1) cha sheria ya usimamizi wa fedha za umma ya mwaka 2016.

Ukaguzi umebaini kwamba Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi unaweka kumbukumbu zake za utoaji mikopo, upokeaji na kufanya matumizi kwa mujibu wa sheria zinavyoelekeza, dosari iliyobainika na ukaguzi ni kwamba Mfuko umeshindwa kuaandaa na kuwasilisha hesabu zake za mwisho wa mwaka kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa ukaguzi.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 24(1) cha "legal Suppliment (Part II) to the Zanzibar Government Gazette Vol CXXIV No. 6584" ya tarehe 9 Oktoba 2015 na kifungu nambri 119(1) ya Usimamizi ya Fedha za Umma ya mwaka 2016..

Kutokuandaa na kutokuwasilisha taarifa za hesabu za mwisho wa mwaka za Mfuko kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kunapelekea kukiukwa kwa taratibu, miongozo na Sheria za fedha za kitaifa na kimataifa.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Mfuko kuandaa na kuwasilisha taarifa za hesabu za mwisho wa mwaka kwa Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali Zanzibar kwa mujibu wa taratibu, miongozo na Sheria za fedha husika za kitaifa na kimataifa kwa lengo la kusimamia utawala bora.

### 6.6.1.5 Uhaulishaji wa fedha kutoka hesabu nambari 404090000 kwenda hesabu nambari 021103000745 bila ya kurejeshwa shilingi 14,000,000

Jumla ya shilingi 14,000,000 zimetumika kwa ajili ya uhaulishaji wa fedha kutoka hesabu nambari 404090000 kwenda hesabu nambari 021103000745 kwa ajili ya shughuli mbalimbali za Ofisi.

Ukaguzi umebaini fedha hizo zilizohaulishwa kwa ajili ya matumizi mbali mbali ya kiofisi hazijarejeshwa hadi ukaguzi unakamilika.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma nambari 12 ya mwaka 2016. Jadweli lifuatalo linaonesha mchanganuo wa fedha zilizohaulishwa.

**Jadweli Nambari 125 : Fedha ambazo zimehaulishwa na hazikurejeshwa**

| Hati ya malipo | Uhaulishaji kutoka Hesabu nambari (Transfer A/C No.) | Kwenda hesabu nambari (To A/C) | Kiasi cha fedha kilichohaulishwa (Tshs.) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| 3/7 | 0404090000 | 021103000745 | 5,000,0000 | PBZ LTD | Ikiwa ni uhaulishaji wa fedha kutoka mfuko wa kujitegemea kwenda Barefoot college. |
| 6/7 | 0404090000 | 0404020000 | 5,000,0000 | | |
| 11/10 | 0404090000 | 0406736000 | 4,000,000 | | Ikiwa ni uhaulishaji wa fedha kwa idara ya usalama na afya kazini. |
| **Jumla** | | | **14,000,000** | | |

Kutokurejeshwa kwa fedha hizo kunapelekea shughuli zilizopangwa kutokukamilika kwa wakati .

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wizara kupitia Mfuko kuhakikisha kwamba fedha hizo zinarejeshwa kwa haraka ili kuweza fedha hizo kutumika katika shughuli zilizopangwa kwa mwaka husika.

**IDARA YA VYAMA VYA USHIRIKA**

### 6.6.1.6 Tafauti iliyojitokeza ya orodha ya vyama vya ushirika vilivyowasilishwa kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na orodha ya vyama vya ushirika kutoka Idara ya Ushirika

Ukaguzi umebaini kwamba kuna tofauti ambayo imejitokeza kati vyama vya ushirika vilivyo hai vilivyowasilishwa kutoka kwa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na kutoka Idara vyama vya Ushirika kupitia vielelezo vilivyowasilishwa kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na kubainika uwepo wa vyama 363 ambavyo taarifa zake hazikuwasilishwa na kotokujulikana sehemu vilipo na shughuli wanayofanya jambo ambalo huwenda likapelekea kujitokeza kwa tathmini isiyosahihi ya ufuatiliaji wa mienendo ya vyama hivyo. Utofauti wenyewe ni kama unavyoonekana katika jaduweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 126 : Tofauti iliyobainika ya vyama vya ushirika vilivyowasilishwa kwa ukaguzi**

| Namba | Wilaya husika | Idadi ya vyama kutoka Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali | Idadi ya vyama kutoka Idara ya Ushirika (Wakaguzi) | Tofauti ya vyama kupitia wilaya mbali mbali za Unguja |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Mjini | 116 | 120 | 4 |
| 2. | Kasikazini 'A' | 60 | 373 | 313 |
| 3. | Kasikazini 'B' | 201 | 211 | 10 |
| 4. | Magharibi 'A' | 207 | 213 | 6 |
| 5. | Magharibi 'B' | 139 | 115 | 24 |
| 6. | Kati | 180 | 184 | 4 |
| 7. | Kusini | 117 | 119 | 2 |
| **Jumla** | | **1020** | **1335** | **363** |

Kuwepo kwa utofauti kati ya orodha ya vyama vilivyowasilishwa kwa Mdhibiti na kutoka Idara ya vyama vya Ushirika kunapelekea kutokuwa na takwimu sahihi ya vyama husika kupitia Idara ya vyama vya ushirika na kusababisha kutokupatikana kwa takwimu sahihi ya vyama vilivyohai na vilivyokuwa sihai.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wizara kupitia idara ya vyama vya ushirika kuhakkikisha kwamba unachukuwa jitihada za makusudi za kuanzisha mfumo maalum ambao utasaidia upatikanaji wa takwimu sahihi ya vyama vya ushirika vilivyohai na vile vilivyokufa kwa lengo la kuisaidia Serikali kuviwezesha kiuchumi ili viweze kujiondolea umaskini na kuweza kujitegemea wenyewe. Aidha kwa vile vyama vya ushirika ambavyo vimekufa ni vyema kujuulikana sababu iliyopelekea vyama hivyo kutokuimarika ili Serikali ichukuwe jitihada za makusudi za kuhakikisha inavifufua, na kuvipatia elimu pamoja na mitaji kwa lengo la kuimarisha Sera na Mikakati ya nchi ya kuondoa umaskini na kuwawezesha wajasiria mali kuweza kufanya shughuli zao kwa ufanisi.

**IDARA YA AJIRA**

### 6.6.1.7 Mapungufu yaliojitokeza katika ukusanyaji wa mapato shilingi 6,200,000

Idara ya Ajira ina jukumu la kusimamia taarifa za ajira na kuimarisha uchumi wa Zanzibar kupitia ongezeko la ajira hasa kwa vijana kwa kuweza kujitegemea na kuwa na uwezo wa kujiajiri wao wenyewe. Aidha Idara ina jukumu la kuratibu shughuli za uwakala binafsi za ajira kwa kazi ya kusafirisha wafanyakazi mbalimbali kwenda kufanya kazi nje ya nchi.

Ukaguzi umebaini kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021 Idara ya Ajira ilisafirisha idadi ya wafanyakazi wapatao 878 kwenda kufanya kazi nje ya nchi ambapo kila mfanyakazi alistahiki kulipiwa 50,000 kutoka kwa Wakala wake. Kwa mujibu wa idadi ya wafanyakazi waliosafirishwa (878) Idara ya Ajira ilitakiwa kukusanya mapato ya shilingi 43,900,000 kutoka kwa wakala wanaosafirisha wafanyakazi nje ya nchi.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni 2021, Idara ya Ajira imekusanya jumla ya shilingi 37,700,000 kukiwa na upungufu wa mapato ya shilingi 6,200,000 ambayo hayakukusanywa kupitia idadi ya wafanyakazi 878 waliosafirishwa.

Aidha ukaguzi umeshindwa kupata maelezo na ufafanuzi juu ya upungufu wa mapato hayo ambapo kila msafiri alitakiwa kulipiwa shilingi 50,000 kupitia kwa wakala wake.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na muongozo wa ulipaji wa ada ya usafiri kwa kijana ayekwenda kufanya kazi nje kupitia sheria na kanuni ya Ajira nje ya nchi. Aidha kukusanya mapato pungufu ni kwenda kinyume na Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma nambari 12 ya mwaka 2016. Muhtasari wa mapato ni kama unavyoonekana katika jaduweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 127 : Mapungufu yaliojitokeza katika ukusanyaji wa mapato yatokanayo na vibali vya ajira.**

| Mwezi wa Makusanyo | Idadi ya vijana waliosafiri nje ya nchi | Kilichotakiwa kulipwa (Tshs.) (A) | Kilicholipwa kwa mujibu wa risiti (Tshs.) (B) | Makusanyo yaliyo kusanywa pungufu (Tshs.) (A-B) |
|---|---|---|---|---|
| Oktoba | 32 | 1,600,000 | 1,600,000 | - |
| Oktoba | 32 | 1,600,000 | 1,400,000 | 200,000 |
| Novemba | 21 | 1,050,000 | 1,050,000 | - |
| Novemba | 7 | 350,000 | 350,000 | - |
| Novemba | 3 | 150,000 | 150,000 | - |
| Novemba | 2 | 100,000 | 100,000 | - |
| Disemba | 2 | 100,000 | 50,000. | 50,000 |
| Disemba | 12 | 600,000 | 600,000. | - |
| Disemba | 62 | 3,100,000 | 3,150,000 | - |
| Disemba | 61 | 3,050,000 | 3,000,000 | 50,000 |
| Disemba | 19 | 950,000.00 | 950,000.00 | |
| Januari | 82 | 4,100,000 | 4,100,000 | |
| Januari | 22 | 1,100,000 | 2,100,000 | |
| Januari | 9 | 450,000 | 1,100,000 | |
| Januari | 44 | 2,200,000 | 450,000 | 1,750,000 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Januari | 2 | 100,000 | 2,200,000 | |
| Februari | 130 | 650000 | - | 650,000 |
| Februari | 83 | 4,150,000 | 4,700,000 | |
| Februari | 62 | 3,100,000 | - | 3,100,000 |
| Februari | 95 | 4750000 | 4,200,000 | 550,000 |
| Februari | 61 | 3,050,000 | 4,700,000 | - |
| Machi | 8 | 400,000 | 400,000 | - |
| Aprili | 17 | 850,000. | 850,000 | - |
| Mei | 2 | 100,000 | 100,000 | - |
| Juni | 8 | 400,000 | 400,000 | - |
| **Jumla** | **878** | **43,900,000** | **37,700,000.00** | **6,200,000** |

Kukusanya mapato yakiwa pungufu kunapelekea upotevu wa fedha za umma jambo ambalo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 23(1)(a) cha Kanuni ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2021.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Ofisi ya Rais Kazi, Uchumi na Uwekezaji kuhakikisha kwamba miongozo, sheria na kanuni za ukusanyaji wa mapato ya serikali zinafuatwa na kuhakikisha kwamba mapato hayo hayapungui.

### 6.6.1.8 Kutopatikana ripoti ya utekelezaji ya mpango kazi kwa ukaguzi

Mpango kazi ni moja ya nyenzo muhimu katika ustawishaji wa utekelezaji wa kazi za kila siku za Wizara kwa ajili ya kutekeleza mambo mbalimbali ya kazi.

Katika ukaguzi uliofanyika umeshidwa kupatiwa ripoti ya utekelezaji wa mpango kazi pamoja na vielelezo mbalimbali vinavyotumiwa na Wizara kwa ajili ya kutekeleza majukumu yao ya kiutendaji ya kila siku. Aidha ukaguzi umeshindwa kufanya uwiano baina ya mpango kazi na ripoti ya utekelezaji wa mpango kazi huo wa mwaka katika kipindi kinachoanzia Julai 2020 mpaka Juni 2021 kutokana na kutopatiwa kwa ripoti ya utekelezaji kwa ajili ya kazi za ukaguzi na kupelekea kushindwa kufanya tathmini ya utekelezaji wa malengo ya taasisi husika.

Kutopatikana kwa ripoti ya utekelezaji kwa ukaguzi kunapelekea:-

- Kutojulikana kwa shughuli makhususi zilizopangwa kwenye mpango kazi huo.
- Ukaguzi kushindwa kujiridhisha na mipango iliyoainishwa kwenye mpango kazi wa mwaka pamoja na utekelezaji halisi katika kilichoripotiwa kwenye ripoti ya utekelezaji ya mwaka.
- Ukaguzi umeshidwa kujua kiasi gani cha fedha kilichopatikana kupitia bajeti husika kutokana na shughuli zilizotekelezwa.
- Kushindwa kufanya tathmini ya utekelezaji wa malengo ya taasisi husika.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wizara husika kuchukuwa jitihada za makusudi kusimamia na kuandaa ripoti ya utekelezaji ya mwaka juu ya shughuli zilizotekelezwa na zisizotekelezwa kupitia bajeti husika ili kupima ufanisi wa malengo waliyojipangia kwa mujibu wa fedha ya bajeti iliyopatikana.

### 6.6.1.9 Malipo yenye vielelezo pungufu shilingi 10,604,876

Ukaguzi umebaini kwamba katika kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021 Wizara imefanya matumizi mbali mbali yenye thamani ya shilingi 23,817,876 . Katika matumizi hayo jumla ya shilingi 10,604,876 vielelezo vyake havikuambatanishwa na hati za malipo ili kuweza kuthibitisha uhalali wa matumizi hayo. Kutoambatanisha vielelezo husika vya matumizi ni kwenda kinyume na Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 128 : Malipo yenye vielelezo pungufu**

| Hati ya malipo | Hundi Namba | Thamani ya fedha (Tshs.) | Kilichoonekana Kupitia Vielelezo (Tshs.) | Fedha Ambazo Hazina Vielelezo (Tshs.) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|---|
| ¾ | 000477 | 4,400,000 | 2,925,000 | 1,475,000 | Katibu Mkuu | Ikiwa ni malipo ya ununuzi wa umeme na matumizi madogo madogo |
| 4/4 | 000478 | 3,750,000 | 1,040,000 | 2,710,000 | | Ikiwa ni malipo ya kulipa mapambo ya , comitee na kuwalipa waandishi wa habari |
| 2/1 | 57 | 8,127,876 | 2,728,000 | 5,399,876 | | Ikiwa ni marejesho ya fedha kwa ajili ya matumizi mbali mbali ya afisi ya kazi uchumi na uwekekezaji |
| 22/5 | 87 | 7,540,000 | 6,520,000 | 1,020,000 | | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya kugharamia mkutano. |
| **Jumla** | | **23,817,876** | **13,213,000** | **10,604,876** | | |

Kutoambatanisha vielelezo kamili kwenye hati za malipo kunapelekea kushindwa kujiridhisha na kuthibitisha uhalali wa malipo hayo.

Ukaguzi unashauri kwamba malipo yanayofanywa yaambatanishwe na vielelezo husika ili kuthibitisha uhalali wa malipo hayo.

### 6.6.1.10 Vifaa ambavyo havikuingizwa katika daftari la kutunza vifaa vya Ghalani shilingi 44,986,991

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba kuna malipo yamefanyika kwa ajili ya kununulia vifaa mbalimbali lakini vifaa hivyo havikuingizwa kwenye daftari la kutunza vifaa vya Ghalani ili kuweza kuthibitisha uhalali wa mapokezi pamoja na matumizi ya vifaa hivyo.

Kutoingizwa vifaa hivyo katika daftari la kutunza vifaa vya ghalani ni kwenda kinyume na sheria ya usimamizi wa fedha za umma nambari 12 ya mwaka 2016. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 129 : Vifaa ambavyo havikuingizwa katika daftari la kutunza vifaa vya Ghalani**

| Hati ya malipo Nambari | Ankara/Risiti | Thamani ya fedha (Tshs.) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 32/2 | -Risiti 58580 –Ankara 161 | 4,174,800.00 | Zanzibar Petroleum Ltd | Ikiwa ni ununuzi wa mafuta ya Wizara |
| 35/2 | -Ankara 0107 na 0541 | 3,500,000.00 | Kijangwani Petrol Station | Ikiwa ni ununuzi wa mafuta Idara ya Diaspora pamoja na Idara ya mawasiliano Ikulu |
| 25/3 | Ankara 02051 | 16,925,000.00 | Wakala Wa Smz Wa Uchapaji | Ikiwa ni ununuzi wa kalenda za ukutani na mezani kwa ajili ya Ofisi |
| 17/4 | Risiti 0239 Ankara 0102 | 8,226,291.00 | Excel Installation | Ikiwa ni ununuzi wa computer. |
| V 24/5 | Risiti 4525 Ankara 5034 | 681,150.00 | Zolla Stationary Centre | Ikiwa ni ununuzi wa vifaa vya kuandikia. |
| 49/6 | - | 800,000 | Zola Stationary Center | Ikiwa ni ununuzi wa vifaa mbali mbali |
| 17-08-20 | Risiti 509 | 7,000,000 | Barefoot Collage | Utengezaji wa mask |
| 59/6 | | 1,319,750 | Znz Petroleum Ltd | -Risiti nambari 59883<br><br>Ankara nambari 750. LTS 580.9 za petrol |
| 61/6 | - | 2,360,000 | Katibu Mkuu | Ikiwa ni ununuzi wa Meza ya Idara ya Ajira. |
| **Jumla** | | **44,986,991** | | |

Kutoingizwa vifaa katika daftari la kutunzia vifaa vya ghalani kunapelekea kukosekana kwa uthibitisho wa mapokezi pamoja na matumizi ya vifaa hivyo.

Ukaguzi unashauri kwamba vifaa vyote ambavyo vinanunuliwa viingizwe katika daftari la kutunzia vifaa vya ghalani pamoja na vielelezo vinavyohusika na vifaa hivyo ili kuweza kuthibitisha mapokezi na matumizi ya vifaa hivyo.

**CHUO CHA MAFUNZO YA UMEME WA JUA KIBOKWA – KINYASINI UNGUJA**

### 6.6.1.11 Changamoto katika Chuo cha mafunzo ya umeme wa jua

Chuo cha mafunzo ya umeme wa jua kilianzishwa Agosti mwaka 2015 na kutiliana sahihi baina ya Wizara ya Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Wanawake, Vijana na Watoto na Serikali ya Barefoot College kwa madhumuni ya kuwapa mafunzo ya umeme wa jua, mradi wa nyuki ,ushoni kwa lengo la kumtoa mwanawake kijijini na kuleta maendeleo katika kijiji chao.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 jumla ya shilingi 103,000,000 zimeshatolewa kwa ajili ya kugharamia chuo hicho.

Ukaguzi umefanya ziara na kubaini kwamba kumekuwepo na changamoto mbali mbali ambazo zinahitaji kufanyiwa marekebisho ili kuepusha kutokufikia malengo waliyopanga.

Changamoto zenyewe ni kama zifuatazo:-

- Kukosekana kwa mpango kazi na Utekelezaji wake.
- Kutokuwepo kwa mhasibu wa kitengo , kitengo cha manunuzi, kitengo cha habari na mawasiliano (ICT).
- Kukosekana kwa mkataba baina ya Wizara ya kazi uwekezaji na Uchumi na Serikali ya barefoot ambao umemaliza muda wake tangu mwaka 2018.
- Kutokufanyiwa mapitio (review) mkataba kwa muda mrefu jambo ambalo linapelekea kituo kutokufanya kazi zake kwa ufanisi.

Aidha mkataba wa awali umemaliza muda wa matumizi tarehe 3/7/2018 kwa mujibu wa mkataba (MoU) husika.

Kutokuwepo kwa mkataba husika kunapelekea mgogoro katika uendeshaji na utekelezaji wa chuo husika.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wizara kuhakikisha kwamba changamoto zote ambazo zimejitokeza zinafanyiwa kazi na mujibu wa sheria zilizopo.

Aidha ukaguzi unashauri uongozi wa Wizara kukifanyia tathmini chuo cha mafunzo ya umeme wa jua kutokana na uendeshaji wa chuo husika ili kuweza kubaini ufanisi na tija ya chuo hicho kupitia walengwa waliokusudiwa.

**HESABU YA MATUMIZI YA MAENDELEO (DEVELOPMENT ACCOUNT)**

**HESABU NAMBARI 9928190604**

### 6.6.1.12 Fedha za ujenzi wa Nyumba ya Kulelea Watoto Mazizini zilizotumika ambazo hazikuwemo katika mpango mkuu wa manunuzi wa mwaka 2020/2021

Katika ukaguzi uliofanyika umebaini kuwa Wizara imefanya malipo yenye thamani ya shilingi 350,000,000 kwa ajili ya Ujenzi wa nyumba ya Watoto Mazizini ambayo ujenzi huo haukuwepo kwenye mpango mkuu wa manunuzi.

Kwa mujibu wa kifungu nambari 32(1)(2)(3) cha Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016 kinaeleza kwamba "Afisa Mhasibu wa taasisi ya umma atawajibika na utayarishaji wa bajeti ya mwaka ya taasisi ya umma". Aidha kwa mujibu wa kifungu nambari 42(1)(2) na kifungu 43 (1)(2)(3) cha sheria ya ununuzi na uondoshaji wa mali za umma nambari 11 ya mwaka 2016 Wizara imeshindwa kutekeleza matakwa ya vifungu hivyo jambo ambalo limepelekea kufanya manunuzi kinyume na utaratibu uliowekwa na Serikali.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 32 cha Sheria ya usimamizi wa fedha za umma nambari 12 ya mwaka 2016, aidha ni kwenda kinyume na kifungu nambari 42 na 43 cha Sheria ya ununuzi na uondoshaji wa mali za umma nambari 11 ya mwaka 2016. Malipo yenyewe ni kama yafuatayo:-

Kufanya matumizi ambayo hayakuwemo katika mpango mkuu wa manunuzi ni kwenda kinyume na Sheria ya manunuzi na uondoshaji wa mali ya umma namba 11 ya mwaka 2016.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wizara kuhakikisha unafanya matumizi kwa mujibu wa mpango wa manunuzi ili kuepuka kufanya matumizi ambayo hayakuidhinishwa na Serikali na hatimae kutokufikiwa kwa malengo yaliyokusudiwa. Hata hivyo pindipo panapotokea matumizi ya dharura na yaliyo katika maelekezo ya Viongozi Wakuu wa Serikali ni vyema kuzingatia kanuni na Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016.

### 6.6.1.13 Ukiukwaji wa taratibu za uhaulishaji shilingi 160,000,000

Ukaguzi umebaini Ofisi ya Rais Kazi Uchumi na Uwekezaji imefanya uhalishaji wa shilingi 160,000,000 kutoka Hesabu ya Maendeleo kwenda Hesabu ya Amana, uhaulishaji huo ulifanywa kwa mujibu wa hati ya malipo nambari 1/2 ya tarehe 03/02/2021 kwa ajili ya ukarabati wa nyumba ya kulelea watoto Mazizini. Dosari ya ukaguzi iliyobainika ni kutokufuatwa kwa taratibu za uhaulishaji jambo ambalo huenda likapelekea kutokujua thamani halisi ya fedha iliyotumiwa kwa mujibu wa kifungu husika.

Ukaguzi unashauri uongozi kuhakikisha unafuata taratibu za uhaulishaji wa fedha pamoja na kuweka vielelezo vyote vinavyohusika kwa mujibu wa utaratibu na miongozo ya Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016.

### 6.6.1.14 Kutokuwepo kwa bajeti ya matumizi ya shilingi 678,160,160

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika jumla ya shilingi 678,160,160 zimetumika kwa ukarabati wa nyumba ya kulelea watoto Mazizini katika kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021 ambapo fedha hizo zilitengwa kwa ajili ya ukarabati wa majengo ya Sebleni na uzio kwa kituo cha Welezo kwa Wazee .

Dosari iliyobainika katika ukaguzi ni kutumika kwa jumla ya shilingi 678,160,160 ambazo hazikuidhinishwa matumizi yake katika bajeti husika na kupelekea kushindwa kupatiwa vielelezo pamoja na taarifa zilizopelekea kufanyika kwa matumizi hayo jambo ambalo limetia shaka juu ya uhalali wa matumizi hayo pamoja na kutokujulikana kwa bajeti halisi ya ukarabati wa nyumba hiyo.

Kufanya matumizi nje ya bajeti kunapelekea kuathiri utekelezaji wa malengo ya taasisi na kushindwa kufanya tathmini ya utekelezaji wa malengo kwa mujibu wa matumizi ya fedha yaliyoidhinishwa.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wizara kuhakikisha matumizi ya fedha hutumika kwa mujibu wa bajeti husika ili kuepusha kujirejea kwa maombi ya utekelezaji wa bajeti kwa jambo ambalo limeshatekelezwa.

### 6.6.1.15 Dosari katika ukarabati wa nyumba ya kulelea watoto Mazizini

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika Ofisi ya Rais Kazi Uchumi na Uwekezaji imefanya ukarabati mkubwa katika nyumba ya kulelea watoto Mazizini kwa kuondoa baadhi ya vifaa na kuweka vifaa vipya ikiwemo mabati , madirisha, milango, pamoja na vifaa vyenginevyo, dosari iliyobainika na ukaguzi ni kutokujulikana kwa thamani halisi ya fedha kwa vifaa vilivyotolewa pamoja na kutokujulikana matumizi ya vifaa vilivyotolewa vilipopelekwa jambo ambalo limetia shaka juu ya uhalali wa matumizi ya vifaa vilivyotolewa.

Kutokujulikana kwa thamani ya matumizi ya vifaa vilivyotolewa na kutokujulikana kwa taarifa ya vifaa hivyo vilipopelekwa kunatia dosari ya usimamizi wa mali za umma na ukiukwaji wa taratibu za uuzwaji wa mali chakavu.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Ofisi ya Rais Kazi Uchumi na Uwezeshaji kuhakikisha unasimamia utaratibu wa uondoshwaji wa mali chakavu kwa lengo la kuipatia Serikali mapato.

**WIZARA YA NCHI (OR) KAZI, UCHUMI NA UWEKEZAJI - PEMBA**

### 6.6.1.16 Dosari katika Utoaji wa Mafuta shilingi 44,956,119

Ukaguzi umebaini kwamba Wizara ya Nchi (OR) Kazi, Uchumi na Uwekezaji - Pemba imenunua mafuta ya aina mbali mbali kwa ajili ya matumizi ya ofisi, dosari zifuatazo zimebaika katika utoaji wa mafuta hayo kwa wafanyakazi na idara mbali mbali kwa shughuli za Ofisi:-

**a) Utoaji wa Mafuta bila ya kuwepo kwa mtiririko wa nambari za vyombo husika katika Daftari la Ghalani na bila ya kurikodiwa katika logbook.**

Ukaguzi umebaini kukosekana kwa mtiririko wa utowaji wa mafuta kwa vyombo vya moto katika daftari la ghalani aidha mafuta hayo hayakuonekana kurikodiwa katika logbook ili kuonesha mwenendo wa utoaji wa mafuta kulingana na safari iliyoendwa.

**b) Utoaji wa Mafuta bila ya kuwepo kibali cha utoleaji (koponi) na uthibitisho wa upokeaji**

Ukaguzi umebaini kukosekana kwa kibali cha utoaji wa mafuta kwa wafanyakazi mbali mbali kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za Ofisi. Hali hii inapelekea ukaguzi kushindwa kuthibitisha idadi ya lita za mafuta yaliyotolewa kwa wafanyakazi wanaohusika.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016. Mchanganuo wa mafuta hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 130 : Utoaji wa mafuta bila ya kuwepo kibali cha utoleaji**

| Hati Namba | Hundi Namba | Kiasi cha fedha kilicholipwa (Tshs.) | Aliyelipwa | Idadi ya lita za Petrol | Idadi ya lita za Diesel | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 10/07 10/07/2020 | 016033 | 1,582,000 | Wete Petrol Station | 990 | - | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa Petrol |
| 10/08 10/08/2020 | 016448 | 1,733,490 | Wete Petrol Station | 990 | - | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa Petrol |
| 36/08 18/08/2020 | 017202 | 5,134,394 | Bakar Petrol Station | 1307.8 | 1388 | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa Petrol na diesel |
| 11/09 7/09/2020 | 016694 | 1,905,750 | Wete Petrol Station | 990 | - | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa Petrol |
| 2/10 2/10/2020 | 017110 | 2,637,310 | Bakar Petrol Station | 1028.5 | 350 | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa Petrol na diesel |
| 3/10 2/10/2020 | 017111 | 3,900,700 | Bakar Petrol Station | 1200.8 | 834.1 | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa Petrol na diesel |
| 33/11 30/11/2020 | 018405 | 226,614 | Bakar Petrol Station | - | 121.4 | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa diesel |
| 52/12 31/12/2020 | 018804 | 1,758,000 | Bakar Petrol Station | 657.9 | 274.7 | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa Petrol na diesel |

| Hati Namba | Hundi Namba | Kiasi cha fedha kilicholipwa (Tshs.) | Aliyelipwa | Idadi ya lita za Petrol | Idadi ya lita za Diesel | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 53/12 31/12/2020 | 018801 | 3,030,000 | Bakar Petrol Station | 1052.5 | 559.1 | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa Petrol na diesel |
| 5/02 04/2/2021 | 019290 | 210,971 | Bakar Petroleum Limited | - | 132.83 | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa diesel |
| 40/3 9/3/2021 | 019869 | 9,308,500 | Zanzibar Petrol Limited | 2373.4 | 2204.8 | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa Petrol na diesel |
| 46/3 9/3/2021 | 019874 | 2,691,250 | Zanzibar Petrol Limited | 856.9 | 2204.8 | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa Petrol na diesel |
| 22/5 10/5/2021 | 021022 | 3,447,695 | Zanzibar Petrol Limited | 1115.1 | 486.5 | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa Petrol na diesel |
| 36/5 19/05/2021 | 021110 | 4,145,000 | Zanzibar Petrol Limited | 912.2 | 1147 | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa Petrol na diesel |
| 1/6 2/6/2021 | 021501 | 2,544,445 | Zanzibar Petrol Limited | 976.7 | 186.5 | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa Petrol na diesel |
| 26/6 11/02/2021 | 021559 | 700,000 | Zanzibar Petrol Limited | - | 320 | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa diesel |
| **Jumla** | | **44,956,119** | | **14,451.8** | **10,209.73** | |

**c) Kutokurikodiwa kwa vibali vya Matumizi ya Mafuta katika daftari la ghalani Shilingi 22,836,890**

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika jumla ya vibali vyenye thamani ya shilingi 22,836,890 vimetolewa kwa ajili ya matumizi ya mafuta kwa vyombo mbali mbali vinavyomilikiwa na Wizara ya Nchi (OR) Kazi Uchumi na Uwekezaji – Pemba.

Dosari iliyobainika katika ukaguzi ni kukosekana kwa kumbukumbu za vibali hivyo vilivyotumika katika daftari la utoaji na uingiziwaji wa ununuzi wa mafuta jambo ambalo limepelekea kushindwa kujiridhisha juu ya uhalali wa matumizi ya mafuta hayo kwa kukosekana taarifa ya chombo kilichoingizwa mafuta hayo.

Ukaguzi unashauri kwa uongozi wa Wizara ya Nchi (OR) Kazi Uchumi na Uwekezaji – Pemba kuweka taratibu za kurikodi matumizi ya mafuta ni vyema kufatwa ili kuweka uwazi na udhibiti mzuri wa matumizi ya mafuta hayo. Mchanganuo wa matumizi ya mafuta hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 131 : Kutokurikodiwa kwa vibali vya Matumizi ya Mafuta**

| Hati Namba | Hundi Namba | Kiasi cha fedha kilicholipwa (Tshs.) | Aliyelipwa | Idadi ya lita za Petrol | Idadi ya lita za Diesel | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 40/3 9/3/2021 | 019869 | 9,308,500 | Zanzibar Petrol Limited | 2373.4 | 2204.8 | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa Petrol na diesel |
| 46/3 9/3/2021 | 019874 | 2,691,250 | | 856.9 | 2204.8 | |
| 22/5 10/5/2021 | 021022 | 3,447,695 | | 1115.1 | 486.5 | |
| 36/5 19/05/2021 | 021110 | 4,145,000 | | 912.2 | 1147 | |
| 1/6 2/6/2021 | 021501 | 2,544,445 | | 976.7 | 186.5 | |
| 26/6 11/02/2021 | 021559 | 700,000 | | - | 320 | |
| **Jumla** | | **22,836,890** | | | | |

### 6.6.1.17 Mikopo ambayo haijarejeshwa shilingi 107,624,000

Ofisi ya Rais Kazi, Uchumi na Uwekezaji hutowa Mikopo midogo midogo kwa wajasiriamali mbali mbali kwa lengo la kuwawezesha kujiajiri wenyewe na kupunguza umasikini kupitia mfuko wa uwezeshaji wananchi kiuchumi.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwa jumla ya shilingi 107,624,000 zimekopeshwa kwa wajasiriamali mbali mbali kisiwani Pemba lakini mikopo hiyo haijarejeshwa licha ya kwamba muda wa kurejesha mikopo hiyo umeshapita. **Kiambatisho Nambari 6 Kinahusika.**

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na muongozo wa mfuko wa uwezeshaji wananchi kiuchumi pamoja na makubaliano katika mkataba wa mkopo.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Ofisi ya Rais Kazi, Uchumi na Uwekezaji – Pemba kuhakikisha unafanya ufuatiliaji wa haraka wa urejeshwaji wa mikopo hiyo kwa lengo la kuweza kuwapatia wajasiriamali wengine kwa mujibu wa utaratibu uliopo kwa lengo la kuwapunguzia ugumu wa kasi ya maisha.

## 6.7 WIZARA YA AFYA USTAWI WA JAMII WAZEE JINSIA NA WATOTO

### 6.7.1 FUNGU H 01 - WIZARA YA AFYA USTAWI WA JAMII WAZEE JINSIA NA WATOTO

Ukaguzi wa hesabu za Wizara ya Afya Ustawi wa Jamii Wazee Jinsia na Watoto kwa mwaka wa fedha 2020/2021 umefanywa kwa mujibu wa Sheria, kanuni, taratibu pamoja na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Taarifa ya Mapato**

Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ilikadiriwa kukusanya jumla ya shilingi 243,831,283,100. Kati ya fedha hizo shilingi 157,090,678,520 ni kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida, shilingi 86,740,604,580 kwa ajili ya matumizi ya kazi za maendeleo na shilingi 21,650,000,000 kutoka washirika wa maendeleo. Aidha jumla ya shilingi 360,505,000 ilikadiriwa kukusanya kutoka katika vyanzo vyake vya ndani.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto ilipokea jumla ya shilingi 53,729,872,313 kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina sawa na asilimia 22.04 ya makadirio, kati ya fedha hizo shilingi 45,332,549,905 ni kwa ajili ya kazi za kawaida sawa na asilimia 29 ya makadirio, na shilingi 8,397,322,407 kwa ajili ya kazi za maendeleo sawa na asilimia 10 ya makadirio, na shilingi 3,314,264,042 kutoka washirika wa maendeleo sawa na asilimia 15 ya makadirio. Aidha jumla ya shilingi 2,597,694,828 zilikusanywa kutoka katika vyanzo mbali mbali vya mapato sawa na asilimia 721 ya makadirio.

**Taarifa ya Matumizi**

Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ilikadiriwa kupokea na kutumia jumla ya shilingi 243,831,283,100, kati ya fedha hizo shilingi 157,090,678,520 ni kwa ajili ya kazi za kawaida, shilingi 86,740,604,580 kwa ajili ya kazi za maendeleo na shilingi 21,650,000,000 kutoka washirika wa maendeleo.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto ilipokea jumla ya shilingi 53,729,872,313 kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina sawa na asilimia 22.04 ya makadirio, kati ya fedha hizo shilingi 45,332,549,905 ni kwa ajili ya kazi za kawaida sawa na asilimia 29 ya makadirio, shilingi 8,397,322,407 kwa ajili ya kazi za maendeleo sawa na asilimia 10 ya makadirio, na shilingi 3,314,264,042 kutoka washirika wa maendeleo sawa na asilimia 15 ya makadirio.

**MATOKEO NA MAPENDEKEZO YA UKAGUZI**

**6.7.1.1 Kutokupatiwa ithibati ya matumizi pamoja na vielelezo vya miamala ya fedha ya shilingi 1,544,029,150.00**

Katika kutekeleza majukumu ya ukaguzi wa taarifa za matumizi ya Wizara ya Afya Ustawi wa Jamii Wazee Jinsia na Watoto, Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ilipokea majibu ya taarifa za ukaguzi wa awali kutoka Wizara ya Afya ambapo ilibainika kuna baadhi ya miamala ya fedha ilisahauliwa kuwasilishwa katika taarifa ya awali (Management Letter) iliyopelekwa Wizara ya Afya.

Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ilichukuwa jitihada za kuwasilisha taarifa za miamala hiyo kupitia barua yenye kumbukumbu nambari AUD/WA/7/VOL.II/10 ya tarehe 25 Aprili 2022 kwa lengo la kuweza kuwasilishiwa ithibati ya matumizi pamoja na vielelezo vya miamala hiyo kwa lengo la kukamilisha ukaguzi na kuweza kutoa maoni ya ukaguzi yatokanayo na taarifa ya hesabu za mwisho wa mwaka iliyowasilishwa kwa ajli ya ukaguzi.

Hadi tunakamilisha ukaguzi baadhi ya miamala hatukuweza kupatiwa uthibitisho wa matumizi pamoja na uwepo wa vielelezo vilivyotumika kwa ajili ya matumizi ya miamala hiyo jambo ambalo limepelekea hesabu ya mwisho wa mwaka wa fedha 2020/2021 kutokuonesha sura sahihi na halisi ya hesabu za Wizara ya Afya Ustawi wa Jamii Wazee Jinsia na Watoto. Miamala hiyo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 132 : Kutokupatikana kwa ithibati ya matumizi na vielelezo vya miamala ya fedha**

| Namba | Tarehe | Kiasi cha Muamala wa fedha uliofanyika (Tshs) | Maelezo |
|---|---|---|---|
| 1. | 11/07/2020 | 628,000,000.00 | TRANSFER FROM A/C – PAYMENT ORDER TRF WITHIN KTB MKUU WIZARA AFYA ACCONTS FROM MALINDI BRANCH |
| 2. | 13/07/2020 | 163,639,886.00 | PG-TRANSFER B2B PRINCIPAL AMOUNT OF 163639886, DEBITED FROM ACCOUNT NO. 0406446000,REF:005RTG2 00713004. |
| 3. | 22/07/2020 | 33,449,974.00 | TRANSFER FROM A/C TO A/C – PAYMENT ORDER TRF KTB MKUU AFYA TO RASHMOH CONTRACTORS CO LTD FROM MALINDI BRANCH |
| 4. | 23/07/2020 | 11,280,000.00 | CASH WITHDRAWAL 192 ALI JUMA ALI FROM MALINDI BRANCH |
| 5. | 23/07/2020 | 28,509,622.00 | CASH WITHDRAWAL 191 ALI JUMA ALI FROM MALINDI BRANCH |
| 6. | 18/08/2020 | 67,486,500.00 | CASH WITHDRAWAL 195 ALI JUMA ALI FROM MALINDI BRANCH |
| 7. | 19/08/2020 | 92,208,200.00 | PG-TRANSFER B2B PRINCIPAL AMOUNT OF 92208200, DEBITED FROM ACCOUNT NO. 0406446000,REF:005RTG2 00819020. |
| 8. | 24/08/2020 | 9,420,000.00 | CASH WITHDRAWAL 202 ALI JUMA ALI FROM MALINDI BRANCH |
| 9. | 24/08/2020 | 52,582,102.00 | CASH WITHDRAWAL 201 ALI JUMA ALI FROM MALINDI BRANCH |
| 10. | 28/08/2020 | 20,290,000.00 | CASH WITHDRAWAL 198 ALI JUMA ALI ZID NO. 310101646 |
| 11. | 28/08/2020 | 18,489,950.00 | CASH WITHDRAWAL 199 ALI JUMA ALI ZID NO. 310101646 FROM MALINDI BRANCH |
| 12. | 01/09/2020 | 211,473,000.00 | OG-TRANSFER B2B PRINCIPAL |
| 13. | 01/09/2020 | 36,867,916.00 | CASH WITHDRAWAL 203 ALI JUMA ALI FROM MALINDI BRANCH |
| 14. | 04/09/2020 | 50,000,000.00 | CASH WITHDRAWAL 205 ALI JUMA ALI FROM MALINDI BRANCH |
| 15. | 04/09/2020 | 25,332,000.00 | CASH WITHDRAWAL 207 ALI JUMA ALI FROM MALINDI BRANCH |
| 16. | 04/09/2020 | 50,000,000.00 | CASH WITHDRAWAL 206 ALI JUMA ALI FROM MALINDI BRANCH |
| 17. | 04/09/2020 | 45,000,000.00 | TRANSFER FROM A/C TO A/C – PAYMENT ORDER WIZARA YA AFYA UNICEF FROM MALINDI BRANCH |
| **Jumla** | | **1,544,029,150.00** | |

### 6.7.1.2 Wafanyakazi waliolipwa mishahara wakiwa wamemaliza muda wao wa utumishi Serikalini shilingi 10,450,000

Katika ukaguzi uliofanyika kwa mwaka wa fedha 2020/2021 imebainika Wizara ya Afya kuendelea kuwalipa mshahara kwa baadhi ya watumishi ambao waliomaliza muda wao wa utumishi na kutakiwa kustaafu kwa mujibu wa Sheria kwa kutimiza muda wao wa utumishi Serikalini kuendelea kulipwa mshahara yenye thamani ya shilingi 10,450,000 jambo ambalo ni kinyume na Sheria Nambari 2 ya Utumishi wa Umma ya mwaka 2011.

Kulipa mishahara wakati mtumishi ameshamaliza muda wake wa utumishi kunapelekea kuitia hasara Serikali na kujitokeza kwa upotevu wa fedha za umma.

Ukaguzi unaushauri Uongozi wa Wizara ya Afya kuhakikisha inachukua jitihada za makusudi kuweka zuio la mshahara kwa watumishi hao ikiwemo pamoja na kutoa taarifa kwa mamlaka husika kukatwa fedha walizo zichukua kwa kulipwa kimakosa, ili ziweze kukatwa kupitia malipo yao ya uzeeni kabla ya Serikali kuwalipa malipo hayo. Malipo hayo ni kama yanavyoonekana katika Jaduali hapo chini:-

**Jadweli Nambari 133 : Wafanyakazi waliolipwa mishahara wakiwa wamemaliza muda wao wa utumishi**

| Namba | Jina | Mwaka wa Ajira | Mwaka wa kustaafu | Mwezi aliopokea Mshahara | Kiwango cha mshahara | Miezi ya ziada | Thamani halisi ya fedha |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Asia Abdalla Suleiman | 1961 | 1/7/2021 | Oktoba 2021 | 781,000 | 4 | 3,124,000 |
| 2. | Zulekha Khalfan Said | 25/12/1959 | 25/12/2019 | Januari 2020 | 715,000 | 1 | 715,000 |
| 3. | Rukia Suleiman Saleh | 17/11/1959 | 30/11/2019 | Februari 2020 | 659,000 | 3 | 1,977,000 |
| 4. | Makame Khamis Juma | 23/11/1959 | - | Feb 2020 | 462,000 | 3 | 1,386,000 |
| 5. | Ghanime Idarus Mohd | 22/9/1960 | - | Nov 2020 | 410,000 | 2 | 820,000 |
| 6. | Abeid Khamis Ame | 1/1/1960 | - | May 2020 | 400,000 | 5 | 2,000,000 |
| 7. | Fakih Hamad Fakih | 1961 | - | July 2021 | 434,000 | 1 | 434,000 |
| **Jumla Kuu** | | | | | | | **10,450,000** |

### 6.7.1.3 Kukosekana kwa stakabadhi za makusanyo ya mapato shilingi 29,927,000

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021 ukaguzi umebaini kwamba Wizara ya Afya kupitia Kitengo cha Afya ya Bandarini kimekusanya mapato yenye thamani ya shilingi 29,927,000 yanayotokana na huduma mbali mbali ambazo zinatolewa Bandarini zikiwemo chanjo ya homa ya ini, homa ya manjano na kubadilisha kadi. Dosari iliyobainika katika ukaguzi ni Kukosekana kwa stakabadhi za kukusanyia mapato hayo ili kuweza kupima tathmini ya fedha halisi iliyokusanywa kupitia huduma iliyotolewa, jambo ambalo limetia shaka juu ya uhalali wa makusanyo hayo kwa kukosekana kwa uthibitisho unaotoa uhalisia wa fedha iliyo kusanywa na kuwasilishwa kama ni mapato halali yanayotokana na vyanzo hivyo vya mapato.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wizara kuhakikisha kwamba mapato yanayokusanywa yanafuata misingi ya sheria na kanuni kwa mujibu wa miongozo ya ukusanyaji wa fedha za umma ili kuepuka kujitokeza kwa viashiria vya upotevu wa fedha za umma.

Uchambuzi wa mapato hayo yaliyokusanywa bila ya kutolewa kwa stakabadhi ni kama yanavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 134 : Stakabadhi za makusanyo ya mapato zilizokosekana kwa ukaguzi**

| Mwezi | Kiwango cha fedha kilichokusanywa | | | (Tshs) |
|---|---|---|---|---|
| | Homa ya manjano | Homa ya Ini | Kubadili kadi | Jumla ya makusanyo |
| Julai 2020 | 350,000 | 275,000 | 110,000 | 735,000 |
| Agosti 2020 | 890,000 | 75,000 | 270,000 | 1,235,000 |
| Septemba 2020 | 1,210,000 | 150,000 | 180,000 | 1,540,000 |
| Oktoba 2020 | 1,382,000 | 75,000 | 210,000 | 1,667,000 |
| Novemba 2020 | 1,340,000 | 300,000 | 260,000 | 1,900,000 |
| Disemba 2020 | 5,280,000 | 125,000 | 730,000 | 6,135,000 |
| Januari 2021 | 3,170,000 | 100,000 | 400,000 | 3,670,000 |
| Februari 2021 | 2,480,000 | 125,000 | 490,000 | 3,095,000 |
| Machi 2021 | 2,440,000 | 50,000 | 490,000 | 2,980,000 |
| Aprili 2021 | 2,005,000 | 50,000 | 230,000 | 2,285,000 |
| Mei 2021 | 1,720,000 | 25,000 | 250,000 | 1,995,000 |
| Juni 2021 | 2,120,000 | 0 | 470,000 | 2,590,000 |
| **Jumla** | **24,387,000** | **1,350,000** | **4,190,000** | **29,927,000** |

### 6.7.1.4 Kukosekana kwa vitabu 15 vya ukusanyaji wa Mapato

Katika mwaka wa fedha 2020/2021 imebainika Wizara ya Afya imetekeleza jukumu lake la kukusanya mapato kupitia vyanzo vyake mbali mbali vya makusanyo. Dosari iliyobainika na ukaguzi ni kukosekana kwa vitabu vya stakabadhi za kukusanyia mapato jambo ambalo limepelekea kushindwa kufahamu mapato halisi yaliyokusanywa yanayotokana na vitabu vya makusanyo hivyo.

Kutokupatikanwa kwa vitabu vya stakabadhi vilivyotumika kwa ukusanyi wa mapato kunatia shaka juu ya mapato hayo kama wamewasilishwa Benki kwa mujibu wa utaratibu jamabo ambalo huenda ikajitokeza upotevu wa fedha za umma.

Ukaguzi unaushauri Uongozi wa Wizara ya Afya kuhakikisha vitabu vyote vilivyokosekana vinapatika kwa ukaguzi ili kuweza kujiridhisha juu ya uhalali wa makusanyo hayo.

Uchambuzi wa vitabu vilivyokosekana kwa ukaguzi ni kama inavyoonekana katika jadweli lifuatalo:-

**Jadweli Nambari 135 : Vitabu 15 vya ukusanyaji wa Mapato vilivyokosekana kwa ukaguzi**

| Namba | Mtiririko wa nambari za Stakabadhi | Jumla ya vitabu |
|---|---|---|
| 1. | 58901-589550 | 1 |
| 2. | 589555-589600 | 1 |
| 3. | 589 60-589 650 | 1 |
| 4. | 589401-589450 | 1 |
| 5. | 595101-595150 | 1 |
| 6. | 595251-595300 | 1 |
| 7. | 69 6951-697000 | 1 |
| 8. | 732151-732200 | 1 |
| 9. | 738401-738450 | 1 |
| 10. | 012401-012450 | 1 |
| 11. | 012251-012300 | 1 |
| 12. | 012901-012950 | 1 |
| 13. | 012951-013000 | 1 |
| 14. | 030 601-030650 | 1 |
| 15 | 030901-030950 | 1 |
| **Jumla** | | **15** |

### 6.7.1.5 Matumizi yaliyozidi makisio ya manunuzi shilingi 59,425,841

Katika ukaguzi uliofanyika katika kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021,Wizara ya Afya iliandaa makisio ya matumizi kwa ajili ya ununuzi na utekelezaji wa kazi za kila siku za Wizara.

Ukaguzi umebaini kwamba kiwango kilichotumika katika manunuzi hayo kimezidi uhalisia wa manunuzi yenyewe. Kukosekana kwa mpango mzuri wa uandaaji wa makisio ya matumizi ya ununuzi wa vifaa kunapelekea kutokupatikana usahihi wa makisio na kusababisha ongezeko kubwa la matumizi yasiokuwa na bajeti.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wizara kuhakikisha kwamba makisio ya ununuzi wa vifaa yanaandaliwa kwa ustadi na umakini mkubwa ili kupunguza matumizi ya ziada ya manunuzi husika jambo ambalo linaweza kupelekea kuathiri mpango wa bajeti ya manunuzi ya Wizara. Makisio yaliyozidi matumizi ni kama yanavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 136 : Matumizi yaliyozidi makisio ya manunuzi**

| Namba | Aina ya Matumizi yaliyofanyika | Nambari ya Zabuni | Bajeti ya Manunuzi iliyoidhinishwa kwa mwaka 2020/2021 (Tshs.) | Kiwango cha Fedha halisi kilichotumika 2020/2021 (Tshs.) | Kiasi cha Fedha kilichoongezeka Excess Amount (Tshs.) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Renovation Of Public Health Emergency Operation Center(Pheoc) Lumumba | SMZ/HOI/W/ NCB/2020/2021/68 | 100,364,684 | 136,040,525 | 35,675,841 |
| 2 | Provision For Consultancy Service For Development Of Negleted Trpical Disease (Ntds) Master Stretegic Plan For Zanzibar | SMZ/HO1/C/ OQ/2020/2021/78 | 9,280,000 | 33,030,000 | 23,750,000 |
| **Jumla** | | | | | **59,425,841** |

### 6.7.1.6 Kuharibika kwa ukuta wa uzio na sakafu ya jengo la Bohari kuu ya dawa Vitongoji Pemba

Wizara ya Afya imefanya mchakato wa zabuni kwa njia ya Domestic Resticted Competitive Bidding na kuingia mkataba na mkandarasi ZEECON Company LTD kwa zabuni nambari SMZ/H01/W/R/RNCB/2020/21/31 ya tarehe 17/11/2020 kwa jumla ya shilingi 597,635,771 pamoja na VAT kwa ajili ya ujenzi wa uzio pamoja na sakafu (Landscaping) ya jengo la Bohari Kuu ya Madawa Vitongoji Pemba. Kupitia barua nambari AB.3/39/02 ya tarehe 03/02/2021, Wizara ya Afya ilimuandikia Wakala wa Majengo kwa ajili ya ombi la kumtaka kusimamia (mshauri elekezi) kazi za ujenzi wa Bohari ya madawa Vitongoji Pemba.

Ukaguzi umebaini kwamba maeneo mengi ya ukuta huo uliojengwa yameharibika kwa kuwa na mipasuko mbali mbali na baadhi ya maeneo ya sakafu yamekatika. Aidha ukaguzi haujapata barua ya mkandarasi ZEECON Company LTD na mshauri elekezi wa mradi huo ambaye ni Wakala wa Majengo Zanzibar ya kukabidhi mradi kwa Wizara.

Kwa mujibu wa barua yenye kumbu kumbu namba K/NO/191/CMS/02/2022/009 ya tarehe 04/02/202 kutoka kwa Meneja wa Bohari ya Madawa Pemba kwenda kwa Mkurugenzi wa Bohari Unguja inayoelezea hali halisi ya kuharibika kwa ukuta huo jambo ambalo limetia shaka juu ya kuharibika kwa ukuta huo kwa muda mfupi tangu kujengwa kwake. Aidha ukaguzi kutokupatiwa kumbukumbu za kikao cha Bodi ya Zabuni kinachoelezea sababu zilizopelekea kutumia njia ya Domestic Resticted Competitive Bidding badala ya zabuni ya wazi.

Pamoja na Kukosekana kwa muhtasari wa kikao cha bodi ya zabuni juu ya kufanyika kwa maamuzi hayo ukaguzi haukupatiwa barua za taarifa za kushindwa kwa wazabuni walioshindwa inayoelezea sababu za kushindwa kwa wazabuni hao kwa mujibu wa sheria Nambari 11 ya ununuzi na uondoshwaji wa mali za umma ya mwaka 2016.

Kuharibika kwa ukuta wa uzio na sakafu ya jengo la Bohari kuu ya dawa Vitongoji Pemba kwa kipindi kifupi kunapelekea kujitokeza kwa changamoto ya kutathmini uwezo wa kampuni ya ZECCON iliyopewa kazi hiyo kama ilifanya kwa ufanisi au haikuwa na uwezo wa kufanya kazi hiyo jambo ambalo linaweza kujitokeza kwa hasara kubwa kwa Serikali kwa kujengewa majengo chini ya Kiwango.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wizara kuhakikisha inapotowa zabuni inatoa kwa kampuni yenye uwezo wa kutosha kwa kuzingatia uzoefu wa kazi zilizofanywa na kampuni hiyo pamoja na kuzingatia thamani ya fedha kwa kazi hiyo ili kuepusha kujitokeza kwa maharibiko yanayojitokeza kwa muda mfupi na kupelekea kujitokeza kwa hasara.

#### 6.7.1.7 Dosari katika matumizi ya ujenzi wa Barabara kwenye jengo la Bohari ya Dawa Vitongoji Pemba

Kwa mujibu wa hati ya malipo nambari 02/09 ya tarehe 09/09/2020 yenye thamani ya shilingi 77,097,000 aliyolipwa Wakala wa Barabara Pemba ikiwa ni gharama za malipo kwa ajili ya ujenzi wa Barabara kwenye jengo la Bohari ya Dawa Vitongoji Pemba.

Dosari zilizobainika na ukaguzi ni kama zifuatazo:-

- Kukosekana kwa mkataba wa ujenzi wa Barabara ili kuweza kujua kiwango cha jumla cha ujenzi huo pamoja na makubaliano ya pande mbili baina ya mjenzi na Wizara.
- Malipo ya fedha hizo kutolewa kwa njia ya fedha taslimu kwa kupitia hesabu ya Katibu Mkuu badala ya kuingiziwa mjenzi moja kwa moja kwa njia ya uhamisho wa kutoka hesabu moja kwenda hesabu nyengine.
- Kutokukatwa kwa kodi ya mapato pamoja na kodi la ongezeko la thamni na kulipwa kwenye Mamlaka husika ikiwemo TRA na ZRB.
- Kukosekana kwa stakabadhi ya malipo husika, ili kuweza kuthibitisha uhalali wa malipo yaliyolipwa na thamani ya kazi inayo fanyika.

Kujitokeza kwa dosari hizo kunatia shaka juu ya uhalali wa matumizi ya fedha hizo, ukaguzi unaushauri Uongozi wa Wizara kuhakikisha unasimamia kikamilifu matumizi ya fedha za umma ili kuweza kuondoa dosari za matumizi ya fedha za umma.

### 6.7.1.8 Kutokutumika nyumba iliyojengwa kwa ajili ya makazi ya Madaktari Taasini Mkoani Pemba

Katika ukaguzi uliofanyika kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021 ukaguzi umebaini jumla ya shilingi 98,000,000 zimetumika na kulipwa mkandarasi ndugu Mohamed Abdalla Rashid kwa ajili ya ujenzi wa nyumba ya makaazi ya madaktari iliyopo Tasini Mkoani – Pemba.

Ukaguzi ulifanya ziara tarehe 28/02/2022 kwenda kuiona nyumba hiyo na kubaini kwamba nyumba imekamilika na imeshakabidhiwa Wizara ya Afya dosari iliyobainika ni kwamba hadi ukaguzi unakamilika nyumba hiyo haijaanza kutumika na kupelekea kutokupatikana kwa tija iliyokusudiwa jambo ambalo linapelekea nyumba hiyo kuharibika.

Ukaguzi unaishauri uongozi wa Wizara kuhakikisha inachukuwa hatua za makusudi kumpatia daktari wa kuishi katika nyumba hiyo ili kuhakikisha malengo yaliyo kusudiwa yanafikiwa.

### 6.7.1.9 Malipo yaliyolipwa kwa fedha taslim (Cash) shilingi 213,195,811

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021 Wizara ya Afya imefanya malipo mbali mbali kwa ajili ya huduma zilizotolewa katika Wizara hiyo.

Ukaguzi umebaini kwamba Wizara ya Afya imefanya malipo kwa njia ya fedha taslim kutoka kwenye hesabu ya Katibu Mkuu badala ya kufanya malipo kwa njia ya kieletroniki kutoka hesabu moja kwenda kwenye hesabu nyengine kwa ajili ya kulipia huduma hiyo moja kwa moja.

Kufanya malipo kwa njia ya fedha taslimu kunaweza kupelekea kujitokeza kwa upotevu wa fedha za umma kunakotokana na kushindwa kuzuia tozo za kodi mbali mbali na kuisababishia Serikali hasara ya fedha za umma. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama yanavyoonekana kwenye jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 137 : Malipo yaliyolipwa kwa fedha taslim (Cash)**

| Namba | Hati ya Malipo nambari | Kiasi cha fedha (Tshs). | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 1 | C02/9 ya 9/9 | 106,697,211 | Katibu Mkuu | Malipo kwa ajili ya Ujenzi wa Barabara jengo la Bohari ya Dawa Vitongoji Pemba |
| 2 | C01/02 ya 2/2 | 57,500,000 | Katibu Mkuu | Malipo ya fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo |
| 3 | C01 -2/10 ya 2/10 | 30,000,000 | Katibu Mkuu | - |
| 4 | 6/2 ya 2/2 | 2,300,000 | Katibu Mkuu | Marejesho ya fedha kwa ununuzi wa vifaa vya mashine |
| 5 | 66/3 ya 2/12 | 1,995,000 | Katibu Mkuu | Ununuzi wa vifaa vya usafi |
| 6 | 66/3 ya 4/11 | 1,000,000 | Katibu Mkuu | Malipo ya fedha kwa ajili ya Ununuzi wa zawadi |
| 7 | 50/3 ya 10/2 | 1,294,500 | Katibu Mkuu | Malipo ya fedha kwa ajili ya Ununuzi wa umeme |
| 8 | 69/1 ya 7/9 | 3,059,100 | Katibu Mkuu | Malipo ya fedha kwa ajili ya Ununuzi wa vifaa vya ofisi |
| 10 | 16/4 | 9,350,000 | Katibu Mkuu | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya kazi za muda wa ziada |
| **Jumla** | | **213,195,811** | | |

### 6.7.1.10 Malipo yasiyokuwa na vielelezo shilingi 233,147,395.1

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika jumla ya shilingi 233,147,395.1 zimetumika kwa ajili ya Ununuzi na upatikanaji wa huduma mbali mbali. Dosari iliyobainika katika ukaguzi ni Kukosekana kwa vielelezo halisi vinavyothibitisha uhalali wa malipo hayo.

Kutokuambatanishwa kwa vielelezo kwenye hati ya malipo kunapelekea kushindwa kuthibitisha juu ya uhalali wa kufanyika kwa malipo hayo jambo ambalo linaweza kujitokeza kwa viashiria kwa upotevu wa fedha za umma, kwa kulipia malipo yasio kua halali kwa mujibu wa mpango wa manunuzi.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa mali za umma ya mwaka 2016. Uchambuzi wa malipo hayo ni kama yanavyoonekana kwenye jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 138 : Malipo yasiyokuwa na vielelezo**

| Namba | Hati ya Malipo | Hundi | Kiasi (Tshs) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | 02/9 ya 9/9 | TT | 77,097,000 | Wakala wa Barabara Pemba | Ujenzi wa Barabara Bohari ya Dawa -Pemba |
| 2 | 02/9 ya 9/9 | TT | 29,600,211.10 | ZECO | Uwekaji wa Transformer kwenye jengo la Bohari ya Dawa - Pemba |
| 3 | 66/1 ya 15/10 | TT | 780,000 | Katibu Mkuu | Malipo ya safari ya kikazi |
| 4 | 54/1 ya 6/7 | TT | 6,559,140 | Lab equip | Ununuzi wa mashine ya x-ray |
| 5 | 17/2 ya 28/9 | TT | 540,000 | K/Mkuu | Malipo kwa ajili ya kulipa vibali kwa madaktari wapya18 |
| 6 | 25/5/2021 | TT | 2,218,000 | K/Mkuu | Malipo kwa ajili ya mkutano wa robo mwaka. |
| 7 | 25/5/2021 | TT | 2,795,000 | K/Mkuu | |
| 8 | 25/5/2021 | TT | 685,000 | K/Mkuu | Malipo ya posho la wajumbe wa kamati ya maadili. |
| 9 | 27/3 ya 2/3 | TT | 3,000,000 | K/Mkuu | Malipo kwa ajili ya kazi mbali mbali za Idara ya tiba |
| 10 | 27/3 ya 3/3 | TT | 3,000,000 | K/Mkuu | Malipo ya Ununuzi wa chakula cha wagonjwa. |
| 11 | 27/3 ya 3/3 | TT | 1,550,900 | K/Mkuu | Malipo ya ukaguzi vituo vya afya na hospitali binafsi |
| 12 | 27/3 ya 2/3 | TT | 900,000 | K/Mkuu | Malipo kwa ajili ya matumizi madogo madogo kwa madaktari wa Cuba |
| 13 | 28/3 ya 1/3 | TT | 1,764,000 | K/Mkuu | Fedha kwa ajili ya afya sports club |
| 14 | 65/3 ya 8/3 | TT | 3,074,260 | K/Mkuu | Ununuzi wa mapazia, zulia na dormet ofisi ya Mhe Waziri |
| 15 | 25/11/2020 | TT | 3,260,000 | K/Mkuu | Malipo kwa ajili ya mkutano wa robo mwaka. |
| 16 | | TT | 930,000 | K/Mkuu | Malipo kwa ajili ya posho la wajumbe wa kamati ya zabuni. |
| 17 | 2/3/2021 | TT | 1,768,000 | K/Mkuu | Malipo kwa ajili ya posho la mkutano. |
| 18 | 16/2/2021 | TT | 6,705,000 | K/Mkuu | Malipo ya fedha kwa ajili ya kuhudhuria mafunzo maalum. |
| 19 | 14/12/2020 | TT | 1,320,000 | K/Mkuu | Malipo kwa ajili ya ukaguzi wa wa maafisa wa afya. |
| 20 | 26/4/2021 | TT | 781,000 | K/Mkuu | Malipo kwa ajili ya fedha zilizotumika kwa wizara |
| 21 | 15/3/2021 | TT | 1,740,000 | K/Mkuu | Malipo kwa ajili ya safari ya Dar es salam |
| 22 | 4/3/2021 | TT | 543,900 | Saleh Decoration | Ununuzi wa zulia ofisi ya Mhe. Waziri |

| Namba | Hati ya Malipo | Hundi | Kiasi (Tshs) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| 23 | 76/3 ya 17/3 | TT | 1,000,000 | K/Mkuu | Fedha kwa ajili ya matengenezo ya majengo ya taasisi ya utafiti. |
| 24 | 76/3 ya 17/3 | TT | 2,160,000 | K/Mkuu | Fedha kwa ajili ya kikao cha kujadili miundo ya taasisi. |
| 25 | 76/3 ya 3/3 | TT | 1,845,000 | K/Mkuu | Fedha kwa ajili ya ukaguzi wa vyuo vya uuguzi na ukunga. |
| 26 | 76/3 ya 16/3 | TT | 3,380,000 | K/Mkuu | Fedha kwa ajili ya ukaguzi wa hospitali na vituo vya afya. |
| 27 | 76/3 ya 15/3 | TT | 1,000,000 | K/Mkuu | Fedha kwa ajili ya matumizi madogo madogo. |
| 28 | 28/9/2020 | TT | 540,000 | K/Mkuu | Malipo ya usajili wa vibali kwa madaktari wapya wa kichina18 |
| 29 | 1/3/2021 | TT | 7,375,000 | K/Mkuu | Malipo ya kazi za kitengo cha ukaguzi wa ndani |
| 30 | 17/3/2021 | TT | 786,000 | K/Mkuu | Malipo ya kikao cha bodi ya zabuni |
| 31 | 2/3/2021 | TT | 2,058,000 | Shirika la Magazeti | Fedha kwa ajili ya tangazo la pongezi |
| 32 | 7/4 | 325 | 3,000,000 | K/ Mkuu | Malipo kwa ajili ya posho na tiketi za safari ya kikazi pemba |
| 33 | 23/4 | 336 | 4,480,000 | K/Mkuu | Malipo ya fedha kwa ajili ya posho la safari kikazi kwenda Dar -saalam |
| 34 | 23/4 | 336 | 6,330,000 | K /Mkuu | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya safari ya pemba |
| 35 | 8/5 ya | TT | 890,820 | Magogoni General Tyre | Malipo ya fedha kwa ajili ya matengenezo ya gari. |
| 36 | 10/5 | TT | 3,645,551 | Double Two General Supply | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa mbali mbali. |
| 37 | 13/5 | TT | 2,107,500 | New Home Furniture | malipo ya ununuzi wa vifaa vya ofisi. |
| 38 | 13/5 | TT | 5,978,000 | New Home Furniture | Ikiwa ni malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa mbali mbali vya ofisi. |
| 39 | 18/5 | 350 | 2,015,000 | K/Mkuu | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya safari kuhudhuria Dar er-salaam |
| 40 | 18/5 | 350 | 2,700,000 | K /Mkuu | Malipo kwa ajili ya matumizi madogo madogo. |
| 41 | 19/5 | 347 | 419,930 | Quseiy Hardware & Electric | Malipo kwa ajili ya fedha kwa ununuzi wa vifaa vya umeme |
| 42 | 23/5 | 353 | 730,000 | K /Mkuu | Malipo kwa ajili ya safari ya dar-es -saalaam |
| 43 | 28/5 | 358 | 2,550,000 | K/Mkuu | Malipo kwa ya gharama ya tiket. |
| 44 | 45/5 | 365 | 4,277,700 | Amo Computer Service | Malipo kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya kuandikia. |
| 45 | 08/5 | | 2,542,610 | Quseiy Hardware & Electric | Malipo kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya matengenezo ya hospitali ya Makunduchi |
| 46 | 1/6 | 370 | 1,844,873 | Karibu Phamacy | Malipo ya ununuzi wa dawa kitengo cha utabibu wa macho |
| 47 | V 15/6 | 377 | 2,340,000 | K/Mkuu | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya safari nchini israil kupeleka wagonjwa. |
| 48 | V 15/6 | 377 | 2,070,000 | K/Mkuu | malipo kwa ajili ya safari ya Dar-es-salaam |

| Namba | Hati ya Malipo | Hundi | Kiasi (Tshs) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| 49 | V 15/6 | 377 | 2,470,000 | K/Mkuu | malipo ya safari ya dodoma kupeleka mgonjwa. |
| 50 | 16/6 | 378 | 1,330,000 | K/ Mkuu | Malipo kwa ajili ya safari ya kikazi Arusha Mhe. Waziri wa afya |
| 51 | 43/6 | 382 | 660,000 | K/Mkuu | Malipo kwa ajili ya utayarishaji wa bajeti |
| 52 | 70/6 | TT | 2,990,000 | K/Mkuu | Malipo ya bakaa la posho kwa muuguzaji hospitali ya Mnazi Mmoja |
| 53 | 38/4 | TT | 7,020,000 | K/Mkuu | Malipo ya posho la Muuguzi Nd. Hassanat Muhidin |
| **Jumla** | | | **233,147,395.1** | | |

### 6.7.1.11 Vifaa ambavyo havikuingizwa katika daftari la kurikodia vifaa vya Ghalani shilingi 19,559,649

Katika ukaguzi uliofanyika umebaini kwamba jumla ya shilingi 19,559,649 zimetumika kwa ajili ya huduma mbali mbali lakini vifaa hivyo havikuingizwa kwenye daftari la kutunza vifaa vya ghalani ili kuweza kuthibitisha uhalali wa mapokezi pamoja na matumizi ya vifaa hivyo.

Kutoingizwa vifaa hivyo katika daftari la kutunza vifaa vya ghalani kunapelekea kushindwa kujiridhisha juu ya uhalali wa malipo ya fedha hizo zilivyotumika jambo ambalo ni kwenda kinyume na Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na uondoshwaji wa mali za Umma ya mwaka 2016. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jaduali hapo chini:-

**Jadweli Nambari 139 : Vifaa ambavyo havikuingizwa katika daftari la kurikodia vifaa vya Ghalani**

| Hati Namba | Hundi Nambari | Ankara / Risiti | Kiasi cha fedha (Tshs) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| 19/4 | TT | 1108 | 4,000,000 | Costal Fuel Service Ltd | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya ununuzi wa mafuta |
| 36/4 | TT | 020 | 2,405,985 | Kyrenaia engineering co | Ikiwa malipo kwa ajili ya ukarabati wa choo |
| 13/5 | TT | 041 | 1,176,000 | New home furniture | Ikiwa ni malipo ya ununuzi wa vifaa vya ofisi ya Mhe waziri |
| 13/5 | TT | | 2,107,500 | New home furniture | Malipo ya ununuzi wa vifaa vya ofisi |
| 16/5 | TT | 03/21/06 | 3,216,850 | Skas building company ltd (sbc) | Ikiwa ni malipo ya fedha kwa ajili ya kununuwa vifaa vya kusafirishia |
| 07/5 | | 1206 | 3,663,107 | Awami general store | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya ulipaji wa famigation wizarani |
| 21/5 | 346 | 0098 | 3,663,107 | Al-Hilal Suppliers | Ikiwa ni malipo ya fedha kwa ajili ya vifaa vya ofisi ya K/Mkuu |
| **Jumla** | | | **19,559,649** | | |

### 6.7.1.12 Malipo yenye vielelezo pungufu shilingi 11,824,404.98

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021 Wizara ya Afya imefanya malipo mbali mbali kutokana na huduma alizopatiwa kupitia taasisi za Serikali na taasisi binafsi.

Ukaguzi umebaini vielelezo kamili vya malipo hayo havikuambatanishwa na hati za malipo ili kuweza kuthibitisha uhalali wa malipo hayo.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na sheria ya usimamizi wa fedha za umma nambari 12 ya mwaka 2016. Malipo yenye vielelezo pungufu ni kama yanavyoonekana kwenye jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 140 : Malipo yenye vielelezo pungufu**

| Hati Namba | Hundi Namba | Kiasi (Tshs) | Kiasi kilicho ambatishwa | Fedha ambazo vielelezo pungufu | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 7/4 | 325 | 3,000,000 | 1,440,000 | 1,080,000 | Katibu Mkuu | Malipo kwa ajili ya posho na tiketi za safari ya kikazi pemba |
| 15/4 | 328 | 15,265,000 | 2,740,000 | 1,080,000 | Katibu Mkuu Wizara ya Afya | Malipo ya kazi za utekelezaji za idara ya kinga |
| 15/4 | 328 | 1,768,000 | 1,620,000 | 148,000 | Katibu Mkuu Wizara ya Afya | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya matumizi ya mkutano. |
| 15/5 | TT | 10,663,196.34 | 9,979,993.86 | 683,202.48 | Zanzibar insurance corperation | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya ulipaji wa bima |
| 18/5 | 350 | 500,000.00 | | 125,122.50 | Katibu Mkuu Wizara ya Afya | Malipo kwa ajili ya usafirishaji wa dawa za chanjo |
| **Jumla** | | | | **2,036,324.98** | | |

### 6.7.1.13 Hati za malipo ambazo hazikupatikana kwa ukaguzi (Missing voucher) shilingi 2,033,334,667.57

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021 Wizara ya Afya imefanya malipo mbali mbali kwa taasisi za Serikali pamoja na taasisi binafsi yenye thamani ya shilingi 2,033,334,667.57 lakini hati za malipo hayo hazikupatikana kwa ukaguzi ili kuweza kuthibitisha uhalali wa malipo hayo.

Kukosekana kwa hati za malipo kwa ukaguzi inapelekea kutokuthibitika kwa matumizi hayo na kusababisha upotevu wa fedha za Serikali.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wizara kuhakikisha kwamba hati za malipo zilizokosekana wakati wa ukaguzi zinapatikana kwa ukaguzi ili kuweza kuthibitisha uhalali wa matumizi hayo. Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na sheria Nambari 12 ya usimamizi wa fedha za umma ya mwaka 2016. Mchanganuo wa hati za malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 141 : Hati za malipo ambazo hazikupatikana kwa ukaguzi**

| Nambari ya hati | Hundi nambari | Aliyelipwa | Kiasi (Tshs) |
|---|---|---|---|
| **Matumizi ya fedha za kawaida (A/C Recurrent)** | | | |
| 36/1 | 000240 | Katibu Mkuu | 210,000 |
| 59/1 | TT | Katibu Mkuu | 4,000,000 |
| 66/1 | 000241 | Katibu Mkuu | 780,000 |
| **Jumla Ndogo (A)** | | | **4,990,000** |
| **Matumizi ya Maendeleo (A/C Capital :Cash Book Namba. 1)** | | | |
| 3/12 | - | Katibu Mkuu | 7,272,750 |
| 4/12 | - | TRA | 3,749,127.60 |
| **Jumla Ndogo (B)** | | | **11,021,877.6** |
| **Matumizi ya Maendeleo (A/C Capital :Cash Book Namba. 2)** | | | |
| 5/10 | | Katibu Mkuu | 2,000,000,000 |
| **Jumla Ndogo (C)** | | | **2,000,000,000** |
| 40/4 | | Katibu Mkuu | 2,340,000 |
| 33/4 | | | 820,000 |
| 32/4 | | Asha Mohd Ali | 3,000,000 |
| 34/4 | | - | 820,000 |
| 20/4 | | - | 985,999.97 |
| 16/4 | | Katibu Mkuu | 9,350,000 |
| 33/5 | | - | 6,790 |
| **Jumla Ndogo (D)** | | | **17,322,789.97** |
| **Jumla Kuu (A+B+C+D)** | | | **2,033,334,667.57** |

### 6.7.1.14 Kukosekana kwa vielelezo vya malipo yenye thamani ya shilingi 746,350,048.75

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021 Wizara a Afya ilifanya malipo yenye thamani ya shilingi 746,350,048.75 ambapo fedha hizo zilitumika kwa ajili ya kuwalipia wanafunzi wanaosomeshwa na Wizara ya Afya ndani na nje ya nchi pamoja na malipo ya ujenzi. Ukaguzi umeshindwa kupatiwa vielelezo vya malipo hayo ili kuweza kuthibitisha uhalali wa malipo husika.

Kukosekana kwa vielelezo vya malipo kunapelekea uhalali wa malipo hayo kutothibitishwa jambo ambalo huenda likasababisha upotevu wa fedha za umma.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wizara kuhakikisha kwamba vielelezo husika vinaambatanishwa na hati za malipo ili kuweza kuthibitisha uhalali wa malipo hayo

Uchambuzi wa malipo hayo ni kama unavyoonekana kwenye jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 142 : Vielelezo vya malipo vilivyokosekana kwa ukaguzi**

| Namba | Hati ya malipo | Nambari ya Hundi | Fedha iliyolipwa kwa mujibu wa Cash book | Thamani ya vielelezo iliyopatikana kwa ukaguzi | Tofauti ya vielelezo ambavyo havikupatikana |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | 17/2 | 000246 | 583,684,000 | 249,795,698 | 333,888,302 |
| 2 | 12/2 | 000246 | 1,125,050,000 | 843,422,439 | 281,627,561 |
| 3 | 2/2 | TT | 352,936,964.94 | 222,102,779.19 | 130,834,185.75 |
| | **Jumla** | | | | **746,350,048.75** |

### 6.7.1.15 Hundi ambazo hazikutengezewa vocha wala hazikurikodiwa katika Daftari la fedha taslim (Cash Book) shilingi 6,334,000

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021 Wizara ya Afya imefanya malipo mbali mbali kwa ajili ya kupatiwa huduma. Ukaguzi umebaini malipo hayo yamefanyika kwa hundi namba 338 aliyolipwa Katibu Mkuu yenye thamani ya shilingi 6,334,000 dosari iliyobainika na ukaguzi fedha hizo zimetumika bila ya kutengenezewa kwa hati za ukaguzi na wala kurikodiwa katika daftari la fedha taslim jambo ambalo limepelekea kutokujuulikana matumizi halisi yaliyofanyika kwa kukosekana kwa vielelezo husika vya matumizi hayo.

Kukosekana kwa hati za malipo pamoja na kutokujuulikana kwa matumizi ya hundi hizo kunatia shaka juu ya uhalali wa matumizi hayo. Ukaguzi unashauri uongozi wa Wizara ya Afya kuhakikisha kwamba malipo yote yanalipwa kwa mujibu wa taratibu, kanuni na sheria za fedha husika.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na sheria nambari 12 ya usimamizi wa fedha za umma ya mwaka 2016.

### 6.7.1.16 Malipo ya ziada yaliyolipwa kinyume na makubaliano ya mkataba shilingi 49,815,134

Katika mwaka wa fedha 2020/2021 imebainika Wizara ya Afya imefunga mkataba na kampuni ya Kim Investment wenye nambari ya kumbukumbu IFB NO.SMZ/HO1/W/NCB/2018/2019/15 kwa thamani ya shilingi 197,408,850 kwa ajili ya ujenzi wa jengo la Utafiti wa Afya Binguni.

Ukaguzi umebaini kwamba Kampuni ya Kin Investment imelipwa jumla ya shilingi 347,223,984 na kupelekea kujitokeza kwa tofauti ya shilingi 49,815,134 ikiwa ni malipo ya ziada yaliyolipwa kinyume na makubaliano ya mkataba huo jambo ambalo haikupatikanwa kwa sababu za uhalali wa uwepo wake.

Aidha, pamoja na ziada ya malipo hayo yaliyobainika ukaguzi haukuweza kupatiwa utaratibu uliotumika wa kuweza kumpata mkandarasi huyo kwa kukosekana mukhtasari wa kikao cha bodi ya zabuni kilicho mpitisha mzabuni huyo, kukosekana kwa mchakato wa wazabuni walioingia katika maombi hayo pamoja na kukosekana kwa ufafanuzi wa malipo ya ziada yaliyobainika.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016. Uchambuzi wa malipo hayo ni kama yanavyoonekana kwenye jedwali hapo chini:-

**Jadweli Nambari 143 : Malipo ya ziada yaliyolipwa kinyume na makubaliano ya mkataba**

| Hati ya malipo | Nambari ya hundi | Thamani ya fedha (Tshs) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 8/4 ya 01/4 | TT | 38,319,438 | Kin Investment Company Limited | Malipo ya umaliziaji wa ujenzi wa jengo la utawala |
| 11/4 ya 12/4 | TT | 145,880,000 | | malipo kwa ajili ya ujenzi wa jengo la uchunguzi |
| 24/6 ya 26/3 | TT | 102,784,096 | | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya umaliziaji wa ujenzi wa jengo la utawala. |
| 75/6 ya 26/6 | TT | 60,240,450 | | Ikiwa ni malipo ikwa ajili ya kumalizia ujenzi jengo la utafiti |
| **Jumla** | | **347,223,984** | | |

### 6.7.1.17 Kuchelewa kuingizwa Fedha za maendeleo za michango ya Serikali kwa program za Malaria na ukimwi, homa ya ini, kifua kikuu na ukoma shilingi 358,348,600

Programu ya Malaria, Ukimwi, Homa ya Ini, Kifua Kikuu na Ukoma ni miradi ya maendeleo iliyo chini ya program maalum ya ufadhili wa Serikali na washirika wa maendeleo kupitia Wizara ya Afya.

Ukaguzi umebaini kwamba fedha za utekelezaji wa miradi hiyo kwa upande wa Serikali kwa mwaka wa fedha 2020/2021 zimechelewa kuingizwa kwenye program hizo ambapo katika kitengo cha malaria kiasi cha shilingi 40,000,000 zimeingizwa tarehe 31/10/2020 na shilingi 118,348,600 zimeingizwa tarehe 15/3/2021 na kwa upande wa program ya Ukimwi, Homa ya Ini, Kifua Kikuu na Ukoma kiasi cha shilingi 200,000,000 zimeingizwa tarehe 10/6/2020.

Kuchelewa kuingizwa kwa fedha kwa wakati kwenye program hizo kunapelekea kutokutekelezeka kwa mipango iliyokusudiwa kutotekelezwa kwa wakati jambo ambalo linaweza kupelekea kutokutekelezeka kwa malengo waliojipangia kwa wakati na hatimae kutokufikia kwa lengo lililokusudiwa au kutokukamilika kwa miradi iliyokusudiwa kwa wakati na hatimae kukosekana kwa tija iliyo kusudiwa kwa jamii.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wizara kuhakikisha kwamba fedha za miradi kutoka Serikali kuu zinapatikana kwa wakati uliopangwa ili kuweza kutekeleza miradi hiyo kwa wakati husika. Uchambuzi wa fedha hizo ni kama inavyoonekana kwenye jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 144 : Kuchelewa kuingizwa Fedha za maendeleo za michango ya Serikali kwa program mbali mbali**

| Hati ya malipo | Hundi namba | Kiasi (Tshs) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 18/6 ya 10/6 | TT | 200,000,000 | Program ya HIV, homa ya ini, kifua kikuu na ukoma | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya kutekeleza program |
| 2/8 ya 31/10 | TT | 40,000,000 | Zanzibar Malaria Control Program | Ikiwa ni uhaulishaji wa fedha kwa kazi za kitengo cha kupambana na malaria |
| 1/3 ya 15/3 | TT | 118,348,600 | Zanzibar Malaria Control Program | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya ununuzi wa dawa na vitendanishi |
| **Jumla** | | **358,348,600** | | |

### 6.7.1.18 Kutopatikana mchakato wa ukarabati wa ujenzi wa Chumba Cha CT-Scan Mnazi Mmoja Hospital (Mapinduzi Kogwe) Shilingi 219,414,891

Katika kutekeleza miradi ya maendeleo ya Wizara ya Afya Ustawi wa Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Wizara ilifanya ukarabati wa ujenzi wa chumba cha CT- SCAN katika Hospitali ya Mnazi Mmoja ambapo ujenzi huo ulitumia jumla ya shilingi 219,414,891 kwa ajili ya utengezaji wa chumba hicho.

Dosari liyobainika katika ukaguzi ni kukosekana kwa uthibitisho wa kufanyika kwa kazi hiyo jambo ambalo limepelekea kutokujuulikana kwa njia za kumpata mkandarasi huyo zilivyotumika kutokana na kutopatiwa utaratibu na mchakato wa kumpata mkandarasi wa ujenzi huo.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria ya ununuzi na uondoshaji wa mali za umma nambari 11 ya mwaka 2016. Malipo ya ujenzi huo ni kama unavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 145 : Kutopatikana mchakato wa ukarabati wa ujenzi wa Chumba Cha CT-Scan Mnazi Mmoja**

| Hati ya malipo | Hundi nambari | Kiasi cha Fedha (Tshs) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 45/5 | TT | 50,126,854 | Skars Building Company | Ikiwa ni malipo ukarabati wa ujenzi Mapinduzi Kongwe |
| | TT | 75,190,282 | | |
| - | TT | 58,950,460 | | Ikiwa ni malipo ya ujenzi wa chumba cha CT-SCAN |
| - | TT | 35,147,295 | | |
| **Jumla** | | **219,414,891** | | |

### 6.7.1.19 Kukosekana vielelezo vya malipo ya Dummy shilingi 2,912,241,610

Ukaguzi umebaini kwamba Wizara ya Afya imetumia jumla ya shilingi 2,912,241,610 kwa matumizi mbalimbali kwa njia ya dummy katika kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021.

Dosari iliyobainika katika ukaguzi ni kukosekana kwa vielelezo vilivyotumika kwa ajili ya malipo hayo jambo ambalo limetia shaka juu ya fedha halisi iliyotumika kwa kukosekana kwa uhalali wa malipo hayo. Hadi ukaguzi unakamilika haukuweza kupatiwa vielelezo vya malipo hayo ili kuweza kuthibitisha uhalisia wa malipo hayo.

Ukaguzi unaushauri Uongozi wa Wizara ya Afya kuhakikisha vielelezo husika vinaambatanishwa na hati za malipo kwa lengo la kuweza kuthibitisha juu ya uhalali wa kufanyika kwa malipo hayo. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama unavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 146 : Malipo ya Dummy yaliyokosa vielelezo**

| Tarehe | Hati namba | Kiasi (Tshs) | Maelezo |
|---|---|---|---|
| 30/10/2020 | 105/10 | 924,544,125 | Dummy |
| 30/10/2020 | - | 28,638,691 | |
| - | - | 177,651,914 | |
| 25/5/2020 | 116/3 | 91,622,851 | |
| 25/3/2020 | 117/3 | 577,880,000 | |
| **Jumla** | | **2,912,241,610** | |

**WIZARA YA AFYA USTAWI WA JAMII WAZEE JINSIA NA WATOTO – PEMBA**

### 6.7.1.20 Kutokufuatwa kwa utaratibu wa ajira za Watumishi wa Umma

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii Jinsia na Watoto Pemba ilifanya uwajiri wa watumishi 19 lakini majina yao hayakuonekana katika vibali vya ajira.

Kufanya hivyo kunapelekea kushindwa kuthibitisha uhalali wa ajira za watumishi hao, aidha ni kwenda kinyume na kifungu nambari 57 cha Sheria Nambari 2 ya Utumishi wa Umma ya mwaka 2011. Mchanganuo wa watumishi hao ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 147 : Kutokufuatwa kwa utaratibu wa ajira za Watumishi wa Umma**

| Namba | Jina la Mtumishi | Jinsia | Tarehe ya Ajira | Mahala pa Kazi |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Ainat Said Ali | F | 1/7/2020 | Vitongoji Cott. Hospital |
| 2. | Ali Hamad Khamis | M | 1/7/2020 | Wete Hospital |
| 3. | Hafidha Yussuf Said | F | 1/7/2020 | Chake Hospital |
| 4. | Nahya Said Hamad | F | 1/7/2020 | Wete Hospital |
| 5. | Maryam Ali Mohd | F | 1/12/2020 | Afisa Tabibu |
| 6. | Ali Rashid Salim | M | 1/12/2020 | Wete Hospital |
| 7. | Aisha Sharif Salim | F | 1/12/2020 | K/A/ Gombani |
| 8. | Aisha Khamis Salim | F | 1/12/2020 | M'weni Cott. Hospital |
| 9. | Asma Khamis Juma | F | 1/12/2020 | Chake Hospital |
| 10. | Yassir Shaaban Seif | M | 1/12/2020 | Wete Hospital |
| 11. | Mulhat Ali Salim | F | 1/9/2020 | Wete Hospital |
| 12. | Shufaa Khamis Salim | F | 1/9/2020 | Wete Hospital |
| 13. | Ahmed Mbarouk Ali | M | 1/9/2020 | Bandarini Wesha |
| 14. | Fihim Abdalla Mohd | M | 1/9/2020 | Kitengo cha Chanjo |
| 15. | Khamis Makame Khamis | M | 1/9/2020 | Uwanja wa Ndege |
| 16. | Hafsa Saleh Abdalla | M | 1/9/2020 | Wete Hospital |
| 17. | Hassan Ali Mbarouk | M | 1/9/2020 | Vitongoji Cott.Hospital |
| 18. | Sabra Juma Azan | F | 1/9/2020 | Vitongoji Cott. Hospital |
| 19. | Hassan Ali Hassan | M | 1/9/2020 | Occupational Health. |

### 6.7.1.21 Malimbikizo ya madeni ya muda mrefu shilingi 24,241,949

Katika Ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Wizara ya Afya Ustawi wa Jamii Jinsia na Watoto Pemba inadaiwa madeni ya muda mrefu na wafanyakazi kutoka Taasisi za Serikali yenye jumla ya shilingi 24,241,949 kwa ajili ya fidia za ajali kazini.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 29(3) cha Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016. Mchanganuo wa madeni hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 148 : Malimbikizo ya madeni ya muda mrefu**

| Kesi Namba | Jina la Mfanyakazi | Taasisi anayotoka | Deni halisi (Tshs.) |
|---|---|---|---|
| P/9/2020 | Maryam Said Massoud | Elimu/M/Amali | 503,732 |
| P/13/2018 | Hamad Shamte Hamad | B/Mji Wete | 955,866 |
| P/3/2019 | Asha Hemed Khamis | B/Mji Wete | 567,100 |
| P/4/2019 | Omar Suleiman Omar | WKUWWW | 13,572,000 |
| P/5/2019 | Said Faki Juma | Kilimo Mali Asili | 442,650 |
| P/6/2019 | Dhulfa Faki Juma | Kilimo Mali Asili | 315,650 |
| P/7/2019 | Raya Hamad Nassor | B/Mji Wete | 584,766 |
| P/8/2019 | Nassor Abdalla Hamad | Ofisi Ya Raisi MBLM | 537,833 |
| P/10/2019 | Sabiha Khamis Juma | Afisi ya Mtakwimu Mkuu | 295,317 |
| P/22/2019 | Mohd Bakari Hamad | Elimu/M/Amali | 765,833 |
| P/17/2019 | Abeid Zubeir Khamis | Afya | 1,406,695 |
| P/19/2019 | Suleimani Abushiri Said | Tawala Za Mikoa | 290,000 |
| P/20/2019 | Salum Hamad Abdalla | A/Mkuu wa Mkoa Kaskazini | 1,204,047 |
| P/23/2019 | Said Ali Abdalla | B/Mji Wete | 1,156,133 |
| P/24/2019 | Maisara Abushir Bilal | Ujenzi Na Mawasiliano | 582,833 |
| P/25/2019 | Salama Suleiman Hamad | Elimu/M/Amali | 592,163 |
| P/26/2019 | Juma Kombo Juma | Elimu/M/Amali | 469,331 |
| **Jumla** | | | **24,241,949** |

### 6.7.1.22 Hati za malipo zenye vielelezo pungufu shilingi 32,734,811

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba jumla ya shilingi 32,734,811 zimelipwa kwa matumizi mbali mbali ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii Jinsia na Watoto Pemba lakini baadhi ya vielelezo vya matumizi hayo havikuambatanishwa katika hati za malipo ili kuweza kuthibitisha uhalali wa malipo hayo.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu 34(1) cha Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016. Mchanganuo wa hati za malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 149 : Hati za malipo zenye vielelezo pungufu**

| Hati Namba | Hundi Namba | Kiasi cha fedha kilicholipwa (Tshs.) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 24/07 20/07/2020 | 016173 | 1,125,000 | Juma Said Juma | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya ujenzi. |
| 28/09 21/09/2020 | 016980 | 1,125,000 | | |
| 37/11 23/11/2020 | 0018324 | 1,145,000 | | |
| 30/09 21/09/2020 | T.O | 316,666 | Platinum Credit Limited | Malipo ya fedha kwa ajili ya Mkato wa Platinum. |
| 38/11 23/11/2020 | T.O | 316,666 | | |
| 12/01 18/01/2021 | - | 5,000,000 | Wizara ya Afya Pemba | Malipo ya fedha kwa ajili ya ujenzi |
| 1/02 03/02/2021 | - | 20,267,798.4 | Wizara ya Fedha na Mipango | Malipo ya fedha kwa ajili ya matumizi mbali mbali. |
| 38/05 19/05/2021 | 021101 | 1,998,684 | Mtambile Petrol Station | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa mafuta ya petrol |
| 52/3 17/3/21 | 019963 | 420,000 | Wizara ya Afya | Malipo ya fedha kwa ajili ya safari ki-kazi |
| 31/4 21/4/21 | T.O | 283,332 | Platinum Credit Limited | Malipo ya fedha kwa ajili ya Mkato wa Platinum. |
| 42/08 27/08/2020 | 017480 | 1,016,294 | Misufini Stationary Centre | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya usafi. |
| 38/08 27/08/2020 | 017477 | 1,046,913 | Suleiman Seif Rashid | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya usafi. |
| 81/05 26/05/2021 | 021430 | 951,458 | Issa Ali Abdalla | Malipo ya fedha kwa ajili ya matengenezo ya Gari. |
| **Jumla** | | **32,734,811** | | |

#### 6.7.1.23 Dosari katika Udhibiti na Utunzaji wa vifaa Tiba

Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii Jinsia na Watoto Pemba inamiliki vifaa tiba mbali mbali kwa ajili ya utoaji wa huduma za matibabu.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba utunzaji na udhibiti wa vifaa tiba hauridhishi kutokana na kutokufanya kazi kwa muda mrefu bila kufanyiwa matengenezo au kuuzwa hali ambayo inaweza kupelekea kuendelea kuharibika na kupungua kwa thamani, **Kiambatisho Nambari 7 Kinahusika.**

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016.

#### 6.7.1.24 Kukosekana kwa vielelezo vya ukusanyaji wa mapato shilingi 5,200,000

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba jumla ya shilingi 5,200,000 zimekusanywa na Wizara ya Afya Ustawi wa Jamii Wazee Jinsia na Watoto Pemba kutokana na ada ya usajili na leseni kwa vituo binafsi vya afya lakini baadhi ya vielelezo vya ukusanyaji wa mapato hayo vimekosekana kwa ukaguzi.

Kukosekana kwa ukaguzi wa vielelezo vya ukusanyaji wa mapato kunatia shaka juu ya uwepo wa upatikanaji wa mapato yaliyokusanywa.

Kufanya hivyo kunapelekea kuikosesha Serikali mapato ambapo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 34 (1) cha Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016. Mchanganuo wa mapato hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 150 : Kukosekana kwa vielelezo vya ukusanyaji wa mapato**

| Jina la Kituo | Jina la Mmiliki | Sehemu ilipo | Tarehe ya Kuanzishwa | Kiasi cha fedha kilicholipwa (Tshs.) |
|---|---|---|---|---|
| Avicenna Dispensary | Said Hamad Hamad | Gombani Chake | July 2019 | 500,000 |
| Bahja | Muhamed Salim Muhamed | Kichungwani Chake | Aprili 2002 | 200,000 |
| Citizen Dispensary | Mselem Hamad Fadhil | Mtemani Wete | 30 Jan 2015 | 500,000 |
| Dira | Othman Said Ali | Machomanne Chake | 2001 | 500,000 |
| Ihsaan Medical Clinic | Omar Hamad Kombo | Madungu Chake | Jan 2020 | 200,000 |
| Konde Clinic | Salma Abeid Daftari | Konde Micheweni | 1992 | 200,000 |
| Muzdalifa | Hamad Said Hamad | Kiungoni Wete | 2017 | 200,000 |
| Mwanamashungi | Thuwaiba Khamis Talib | Madungu Chake | 15 May 2007 | 500,000 |
| SDA | SDA | Wawi Chake | 1990 | 500,000 |
| Selem Dispensary | Khalfan Muhamed Khalfan | Selem Wete | Jan 1994 | 200,000 |
| Shaam | Ameir Abdalla Ali | Konde Micheweni | Febr 2017 | 200,000 |
| Sururu | Salim Sururu Nabahani | Sizini Micheweni | May 2007 | 500,000 |
| Maqboul Medical and D. Centre | | Misufini Chake | | 500,000 |
| Islah Dispensary | | Konde kwa Mchina | | 500,000 |
| **Jumla** | | | | **5,200,000** |

### 6.7.2 FUNGU H 02 - HOSPITALI YA MNAZI MMOJA

Ukaguzi wa hesabu za mwaka wa fedha 2020/2021 kwa Hospitali ya Mnazi Mmoja umefanywa kwa mujibu wa Sheria, kanuni, taratibu pamoja na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Taarifa ya Mapato**

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021 Hospitali ya Mnazi Mmoja ilikadiriwa kupokea jumla ya shilingi 18,806,696,907 kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina. Aidha Hospitali ya Mnazi Mmoja ilikadiriwa kukusanya jumla ya shilingi 675,000,000 kutoka vyanzo vyake vya ndani.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 Hospitali ya Mnazi Mmoja ilipokea na kutumia jumla ya shilingi 16,933,548,803 kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina sawa na asilimia 90 ya makadirio, kukiwa na upungufu wa shilingi 1,873,148,104 sawa na asilimia 10 ya makadirio.

Aidha Hospitali ya Mnazi Mmoja ilikusanya jumla ya shilingi 798,195,849.72 kutoka vyanzo vyake vya ndani sawa na asilimia 118 ya makadirio kukiwa na ongezeko la shilingi 123,195,849.72 sawa na asilimia 18 ya makadirio.

**Taarifa ya Matumizi**

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021 Hospitali ya Mnazi Mmoja ilikadiriwa kutumia jumla ya shilingi 18,806,696,907, kati ya fedha hizo shilingi 13,707,496,907 ni kwa ajili ya mishahara na shilingi 5,099,200,000 kwa ajili ya matumizi mengineyo ya kazi za kuendesha Hospitali.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 Hospitali ya Mnazi Mmoja ilipokea na kutumia jumla ya shilingi 16,933,548,803 sawa na asilimia 90 ya makadirio, kukiwa na upungufu wa shilingi 1,873,148,104 sawa na asilimia 10 ya makadirio.

**MATOKEO NA MAPENDEKEZO YA UKAGUZI**

### 6.7.2.1 Matumizi mabaya ya Stakabadhi za kukusanyia mapato

Ukaguzi umebaini uwepo wa matumizi mabaya ya stakabadhi za kurikodia mapato yatokanayo na malipo ya kitengo cha huduma ya haraka (fast track) ambapo imebainika stakabadhi hizo huharibiwa (cancelled) kwa kuchorwa pasi na stakabadhi hizo kutumika jambo ambalo hupelekea viashiria vya upotevu wa fedha za umma unaojitokeza kwa kuacha baadhi ya stakabadhi kuzitumia kwa lengo la kutegemea kujitokeza kwa mtaka huduma na kuzitumia kinyume na maadili.

Kuwepo kwa matumizi mabaya ya stakabadhi za kukusanyia mapato kunapelekea Hospitali ya Mnazi Mmoja kutumia fedha kinyume na malengo husika kwa kununua vitabu vya stakabadhi kutoka Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais Fedha na Mipango na hatimae stakabadhi hizo kutokutumika kwa lengo lililokusudiwa jambo ambalo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 31(1) cha Kanuni ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2021.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Hospitali ya Mnazi Mmoja kuhakisha kwamba stakabadhi zinatumika kama sheria, kanuni na taratibu za fedha zinavyoelekeza ili kuepuka kujitokeza kwa vitendo vya upotevu wa stakabadhi unaopelekea kusababisha upotevu wa mapato ya Serikali. Uchambuzi wa stakabadhi hizo ni kama zinavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 151 : Orodha ya Stakabadhi zilizoharibiwa**

| Namba | Nambari ya Stakabadhi iliyoharibiwa (Cancelled Receipt) | Namba | Nambari ya Stakabadhi iliyoharibiwa (Cancelled Receipt) |
|---|---|---|---|
| 1. | 693791 | 20. | 431241 |
| 2. | 647834 | 21. | 442741 |
| 3. | 575496 | 22. | 431358 |
| 4. | 575371 | 23. | 431369 |
| 5. | 575385 | 24. | 431371 |
| 6. | 575388 | 25. | 431412 |
| 7. | 458745 | 26. | 431426 |
| 8. | 459746 | 27. | 431442 |
| 9. | 458747 | 28. | 431443 |
| 10. | 458748 | 29. | 431283 |
| 11. | 458749 | 30. | 442609 |
| 12. | 458750 | 31. | 442618 |
| 13. | 431323 | 32. | 442771 |
| 14. | 431332 | 33. | 431463 |
| 15. | 546472 | 34. | 431467 |
| 16. | 546494 | 35. | 431485 |
| 17. | 546035 | 36. | 431491 |
| 18. | 431203 | 37. | 431496 |
| 19. | 431218 | 38. | 546299 |

### 6.7.2.2 Kutokurejeshwa kwa fedha za malipo ya ada ya wanafunzi wa kigeni USD 3,100

Hospitali ya Mnazi Mmoja ina kawaida ya kupokea wanafunzi wa kigeni kutoka nchi mbali mbali wanaokuja kwa ajili ya masomo ya njia ya vitendo (elective study) kwa gharama ya kuchangia **USD 400** kwa kila mwanafunzi.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika jumla ya USD 3,100 zimepokelewa kupitia hesabu ya mapato yenye nambari 0406449000 ya Hospitali ya Mnazi Mmoja, kutokana na uwepo wa janga la maradhi ya UVIKO-19 kulipelekea jumla ya wanafunzi nane (8) kushindwa kuhudhuria mafunzo hayo kutokana na masharti yaliyowekwa na nchi zao (lock down) na kuitaka Hospitali ya Mnazi Mmoja iwarudishie gharama za fedha walizokwisha kuzilipia katika mafunzo hayo.

Dosari ya ukaguzi iliyobainika ni pamoja na uwepo wa majibizano ya barua pepe hadi ukaguzi unakamilika fedha hizo bado hazijarejeshwa kwa wanafunzi hao jambo ambalo ukaguzi haukuweza kujiridhisha juu ya uhalali wa uwepo wa fedha hizo.

Aidha, uwepo wa mapokezi ya fedha hizo umetia shaka kutokana na kushindwa kuwasilishwa katika taarifa za hesabu za mwisho wa mwaka za Hospitali kama ni fedha ya mapato iliyopokewa kwa ajili ya mafunzo jambo ambalo hutoa kiashiria cha upotevu wa fedha hizo ambao utatokana na kuhujumiwa kwa vile kumekosekana kwa taarifa za fedha hizo. Mchanganuo wa malipo ya fedha hizo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 152 : Fedha za malipo ya ada ya mafunzo ambazo hazijarejeshwa kwa wanafunzi wa kigeni**

| Namba | Jina la mwanafunzi | Kada | Nchi anayotoka | Tarehe ya kuanza mafunzo | Tarehe ya kumaliza mafunzo | Kiwango alicholipa (USD) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Chanmi Park | MD | Korea | 25-May-20 | 12-Jun-20 | 300 |
| 2. | Melissa Cryan | MD | Ireland | 20-Jun-20 | 17-Jul-20 | 400 |
| 3. | Sarah Lyne | MD | Ireland | 22-Jun-20 | 17-Jul-20 | 400 |
| 4. | Adam Bowden | MD | Ireland | 22-Jun-20 | 20-Jul-20 | 400 |
| 5. | Ameisbichler Elisa | Midwife | Austria | 14-Jul-20 | 09-Aug-20 | 400 |
| 6. | Kinzer Isabella | Midwife | Austria | 14-Jul-20 | 09-Aug-20 | 400 |
| 7. | Sunk Anna | Midwife | Austria | 14-Jul-20 | 09-Aug-20 | 400 |
| 8. | Kornfeld Magdalena | Midwife | Austria | 14-Jul-20 | 09-Aug-20 | 400 |
| **Jumla** | | | | | | **3,100** |

Hata hivyo ukaguzi umebaini uwepo wa wanafunzi watatu (3) wa kigeni ambao hufika hospitali ya Mnazi Mmoja kwa vipindi tofauti kwa ajili ya mafunzo ya vitendo ambao hulipa malipo ya USD 300 kinyume na muongozo wa kuwataka kulipa dola 400. Kutokana na uwepo wa dosari hiyo ukaguzi haukupatiwa majibu ya kutosheleza sababu za msingi zilizopelekea kukusanya mapato ya USD 300 kinyume na utaratibu jambo ambalo limetia shaka juu ya upotevu wa USD 100 kwa kila mwanafunzi aliyepata mafunzo ya vitendo na kupelekea upotevu wa USD 300 ambazo hazikupatikana kwa ukaguzi. Mchanganuo wa fedha hizo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 153 : Malipo ya ada za wanafunzi wa kigeni yaliyolipwa pungufu**

| Namba | Jina la Mwanafunzi | Nchi anayotoka | Tarehe ya kuanza Mafunzo | Tarehe ya kumaliza Mafunzo | Kiwango alichopaswa kulipwa (USD) | Kiwango kilicholipwa (USD) | Tofauti (USD) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Kristin Emma Fritzenschaft | Austria | 14-Sep-20 | 14-Oct-20 | 400 | 300 | 100 |
| 2. | Magdalena Wiesinger | Austria | 14-Sep-20 | 14-Oct-20 | 400 | 300 | 100 |
| 3. | Lisa Fasching | Austria | 14-Sep-20 | 14-Oct-20 | 400 | 300 | 100 |
| **Jumla** | | | | | **1200** | **900** | **300** |

Kutokurejeshewa fedha hizo kwa wanafunzi wa kigeni kunaweza kukapelekea kuitia dosari Nchi kwa kuonekana kuwa kumekosekana kwa uaminifu kwa watendaji wa Hospitali ya Mnazi Mmoja. Aidha, kujitokeza kwa mapokezi ya mapato pungufu bila ya kuwepo kwa sera ya msamaha wa mapato ilioandaliwa na Hospitali ya Mnazi Mmoja ukaguzi umeshindwa kujiridhisha uhalali wa uwepo wa mapokezi hayo.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 121(2)(f) cha Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma Nambari 12 ya mwaka 2016

Ukaguzi unashauri uongozi wa Hospitali ya Mnazi Mmoja kuhakikisha kwamba fedha zinalipwa kwa mujibu wa makubaliano, sheria na miongozo husika ili kuondoa shaka ya uwepo wa upotevu wa mapato ya Serikali.

### 6.7.2.3 Malipo kwa njia ya fedha taslimu (cash payment) shilingi 36,800,000

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika Hospitali ya Mnazi Mmoja imefanya malipo yenye thamani ya shilingi 36,800,000 kwa ajili ya malipo ya posho za Wakurugenzi nane (8) pamoja na Msemaji Mkuu wa Hospitali ya Mnazi Mmoja. Dosari ya ukaguzi iliyobainika ni uwepo wa malipo ya posho kwa njia ya fedha taslim, posho ambalo lilipaswa kuingizwa katika mshahara wa mtumishi kwa mujibu wa muundo wa utumishi wa taasisi za umma.

Uwepo wa malipo ya posho la nafasi ya ukurugenzi kwa mujibu wa muundo wa utumishi wa umma kulipwa kwa njia ya fedha taslim ni kwenda kinyume na kanuni ya utumishi wa umma ya mwaka 2014.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na toleo la Miongozo ya Utumishi wa Umma katika Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya mwaka 2021.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Hospitali ya Mnazi Mmoja kuchukuwa jitihada za makusudi kuhakikisha malipo yatokanayo na posho za Wakurugeni yalipwe kwa mujibu wa Miongozo ya Utumishi wa Umma ili kuepuka kujitokeza kwa viashiria vya upotevu wa fedha au kulipa malipo ya posho ambayo hayakuidhinishwa kwa mujibu wa muundo  Utumishi wa Umma. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama unavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 154 :  Malipo yaliyofanyika kwa njia ya fedha taslimu (cash payment)**

| Namba | Hati ya malipo Nambari | Nambari ya hundi | Thamani ya fedha (Tshs.) | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 1. | 08/08 | 000102 | 4,200,000 | Malipo kwa ajili ya posho la wakurugenzi kuanzia mwezi wa Julai 2020 hadi Aprili 2021 |
| 2. | 69/08 | - | 4,200,000 | |
| 3. | 07/10 | 000108 | 4,200,000 | |
| 4. | 03/11 | 000115 | 4,200,000 | |
| 5. | 02/12 | 000119 | 4,200,000 | |
| 6. | 10/02 | 000126 | 4,200,000 | |
| 7. | 38/02 | 000127 | 4,200,000 | |
| 8. | 16/05 | 000138 | 3,700,000 | |
| 9. | 30/06 | 000142 | 3,700,000 | |
| **Jumla** | | | **36,800,000** | |

### 6.7.2.4 Dosari katika ajira za Mkataba

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika Hospitali ya Mnazi Mmoja imeingia mkataba kwa kipindi cha kila baada ya miezi sita na **Ndugu Bilali Mohammed Khatib** mwenye nambari ya utambulisho wa mzanzibari mkaazi 620251150 na **Ndugu Salum Said Ali** mwenye nambari ya utambulisho wa mzanzibari mkaazi nambari 90198258 kwa ajili ya kufanya kazi ya kujaza 'oxygen' katika mitungi, kusambaza mitungi ya oxygen ndani ya Hospitali ya Mnazi Mmoja kwa muda uliokubaliwa, pamoja na majukumu mengine watakayopangiwa kwa gharama ya shilingi 300,000 kwa mwezi kwa kila mmoja.

Kwa mujibu wa kifungu nambari 60(1)(b) cha Sheria Nambari 2 ya Utumishi wa Umma ya mwaka 2011 kinaeleza kwamba " Mkataba wa muda mfupi au muda maalum wa utumishi ambao utakuwa kwa kipindi cha kurejewa rejewa baina ya miezi sita na miaka mitatu utafungwa baada ya kupata kibali cha Katibu Mkuu Kiongozi na idhini ya Tume ya Utumishi inayohusika……….". Dosari iliyobainika katika ukaguzi ni kukiukwa matakwa ya kifungu kilichonakiliwa hapo juu.

Aidha, ukaguzi umebaini uwepo wa watumishi hao kuendelea kufanya kazi kwa muda wa mwaka mmoja zaidi bila ya uwepo wa mikataba baada ya kumalizika kwa mikataba yao ya awali tarehe 30/04/2021. Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 60(1)(b) cha Sheria Nambari 2 ya Utumishi wa Umma ya mwaka 2011.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Hospitali ya Mnazi Mmoja kuhakikisha unafuata taratibu, kanuni na sheria za utumishi wa umma katika kuwapatia ajira watumishi wa mkataba ili kuweza kuepusha kuwakosesha waajiriwa hao stahiki zao za msingi kupitia Serikali kuu pamoja na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii.

### 6.7.2.5 Uwepo wa mali chakavu kwa muda mrefu

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika Hospitali ya Mnazi Mmoja inamiliki vyombo vya moto aina ya AMBULANCE CITRON yenye nambari ya usajili SMZ 6395 na AMBULANCE yenye nambari ya usajili DFPA 1379 . Dosari ya ukaguzi iliyobainika ni kutokufanyiwa matengenezo kwa muda mrefu na kupelekea uwepo wa mali za kudumu zilizochakaa, ukaguzi umefanya mazungumzo na fundi mkuu kutaka kujuwa khatma ya uwepo wa mali chakavu hizo na kusema "Magari hayo hayawezi kufanya kazi tena kwa kuwa gharama za utengenezaji ni kubwa sana kulinganisha na thamani ya magari husika".

Ukaguzi unashauri uongozi wa Hospitali ya Mnazi Mmoja kuchukuwa jitihada za makusudi ili kuweza kuuzwa kwa mali hizo kwani kadri magari yanavyozidi kukaa yanazidi kuharibika na hayataweza kuuzika (Mali Chakavu) na kupelekea thamani yake kuzidi kushuka jambo ambalo litaisababishia Serikali hasara kubwa.

### 6.7.2.6 Ukiukwaji wa taratibu za Manunuzi shilingi 139,734,188

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika Hospitali ya Mnazi Mmoja imetangaza zabuni kwa njia ya Ushindani yenye kumbu kumbu nambari SMZ/HO110/NBC/G/2020/2021/07 ya tarehe 13/08/2020 yenye thamani ya shilingi 139,734,188 kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya dahalia ya Hospitali pamoja na kuvifunga (Supply of Hospital Hostel and Installation).

Kwa mujibu wa maamuzi ya kikao cha Bodi ya Zabuni kilimchagua Mzabuni Lab Equip Limited na kupewa hati ya makubaliano (mkataba) iliyosainiwa tarehe 29/04/2021.

Kwa mujibu wa Ripoti ya Kamati ya Tathmini mzabuni Gareeb Nawaaz alitolewa katika ushindani kwa kuwa maombi yake hayakukidhi idadi (quantity) ya vifaa vilivyoainishwa kwenye hati ya zabuni (bid document). Ukaguzi umebaini kwamba idadi ya vifaa vilivowasilishwa na mzabuni Gareeb Nawaaz kwenye taarifa yake ya maombi ya zabuni haikutofautiana na ipo sawa sawa na idadi ya vifaa vilivyomo kwenye hati ya zabuni (bid document) ya Hospitali ya Mnazi Mmoja.

Kitendo cha Bodi ya Zabuni kushindwa kujiridhisha na ripoti ya tathmini na kupelekea kutoa maamuzi ya kumbariki zabuni Lab Equip Limited kwa visingizio vya kutokukidhi vigezo kunatoa kiashiria ukiukwaji wa maadili ya manunuzi ya umma ambayo yatapelekea kujitokeza kwa vitendo vya uhujumu wa uchumi.

Aidha, ukaguzi umebaini gharama alizowasilisha Gareeb Nawaaz kwenye zabuni hiyo ni shilingi 130,029,000 na kufanya ziada ya shilingi 9,705,188 ukilinganisha na mzabuni aliyeteuliwa na Bodi ya Zabuni ambae ni Lab Equip Limited jambo ambalo limeonesha dosari ya kuwa makini kwa kitengo cha Bodi ya Zabuni na kupelekea kuitia hasara Serikali kwa kufanya maamuzi yasiyozingatia haki.

Uwepo wa utoaji wa maamuzi yasiyozingatia haki na mipaka ya kisheria ya ununuzi wa umma yanavyoelekeza kwamba "Taratibu zote za kuchagua wazabuni watakaoalikwa kushiriki zitaruhusu ushindani ulio sawa na wa haki na kuhakikisha unashirikisha ushindani wa hali ya juu." Jambo ambalo halikutendeka na kupelekea ukiukwaji wa kifungu nambari 49 cha Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshwaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Hospitali ya Mnazi Mmoja kusimamia maadili ya maamuzi yatokanayo na Sheria ya Ununuzi na Uondoshwaji wa Mali za Umma kwa lengo la kuepusha kuingia kwenye migogoro na wazabuni kwa jambo la kutoa haki kwa asiehusika jambo ambalo huwenda likapelekea upotevu wa fedha za umma kwa mzabuni kuweza kuishitaki Serikali na kuingia gharama za kumlipa ambazo zingeliweza kuepukika ikiwa mipaka ya kisheria imesimamiwa na kutekelezwa ipaswavyo, vile vile uongozi unashuriwa kuzidisha umakini katika kufanya maamuzi ya zabuni mbali mbali wanazozitoa ili kuepuka kumpa mzabuni ambae gharama zake ni kubwa kulinganisha na wazabuni wengine na kupelekea kusababisha matumizi mabaya ya fedha za serikali.

### 6.7.2.7 Ukiukwaji wa maamuzi ya kikao cha Kamati ya Tathmini.

Ukaguzi umebaini kwamba Hospitali ya Mnazi Mmoja ilitangaza zabuni yenye kumbukumbu nambari SMZ/HO110/NCS/NCB/2020-2021/16 (LOT 1) kwa thamani ya shilingi 231,380,064 kwa ajili ya kufanya usafi kwa Hospitali ya Mnazi Mmoja, (LOT 2) kwa thamani ya shilingi 115,690,032 kwa ajili ya Hospitali ya wagonjwa wa Akili Mentali pamoja na (LOT 3) kwa shilingi 38,563,344 kwa ajili ya Hospitali ya Mwembeladu.

Ukaguzi umebaini kwamba Kamati ya Tathmini ilimchagua Astonish Company Limited kuwa ndiye mzabuni aliyeshinda zabuni kwa LOT zote tatu.

Aidha Ukaguzi umebaini kwamba Bodi ya Zabuni ya Hospitali ya Mnazi Mmoja katika kikao chake cha tarehe 13/08/2020 ilifuta maamuzi ya kamati ya tathmini kwa LOT 2 ya usafi wa Hospitali ya Wagonjwa wa Akili (Mentali) kwa kampuni ya Astonish yenye gharama ya shilingi 115,690,032 na kuipa kampuni ya Pangani Ascending Ltd kwa gharama ya shilingi 132,004,800 na kupelekea ongezeko la ziada ya shilingi 16,314,768. Ukaguzi haukupatiwa sababu na vielelezo vilivyopelekea kubadilishwa kwa maamuzi ya kamati ya tathmini.

Hata hivyo, kutokana na mabadiliko ya maamuzi hayo mzabuni alieshinda zabuni hiyo (Astonish) hakuweza kujuulishwa sababu za kushindwa kwa zabuni ya ufanyaji wa usafi wa hospitali ya wagonjwa wa Akili (Lot 2) kama Sheria ya ununuzi na uondoshwaji wa mali za umma inavyoelekeza.

Kitendo cha ukiukwaji wa maamuzi ya Kamati ya Tathmini kinaweza kusababisha migogoro isiyo ya lazima na hatimae kupelekea Serikali kushtakiwa na kulipa gharama kubwa za fedha pasipokuwa na tija.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Hospitali ya Mnazi Mmoja kusimamia maadili ya maamuzi yatokanayo na Sheria ya Ununuzi na Uondoshwaji wa Mali za Umma kwa lengo la kuepusha kuingia kwenye migogoro na wazabuni kwa jambo la kutoa haki kwa asiehusika jambo ambalo huwenda likapelekea upotevu wa fedha za umma kwa mzabuni kuweza kuishitaki Serikali na kuingia gharama za kumlipa ambazo zingeliweza kuepukika ikiwa mipaka ya kisheria imesimamiwa na kutekelezwa ipaswavyo, vile vile uongozi unashuriwa kuzidisha umakini katika kufanya maamuzi ya zabuni mbali mbali wanazozitoa ili kuepuka kumpa mzabuni ambae gharama zake ni kubwa kulinganisha na wazabuni wengine na kupelekea kusababisha matumizi mabaya ya fedha za Serikali.

### 6.7.2.8 Kutokuwekwa wazi sababu za wazabuni walioshindwa zabuni

Kanuni ya Ununuzi na Uondoshwaji wa Mali za Umma kifungu nambari 8 kinaeleza juu ya uwepo wa uwazi na usawa kwenye michakato ya ununuzi katika taasisi za Serikali.

Ukaguzi umebaini kwamba baadhi ya wazabuni walioomba zabuni mbalimbali wamepewa barua za kushindwa kwa zabuni bila ya kutajiwa sababu zilizopelekea kushindwa kwa zabuni hizo.

Uchamuzi wa wazabuni hao na zabuni walizoomba ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 155 : Kutokuwekwa wazi sababu za wazabuni walioshindwa zabuni**

| Namba | Jina la Zabuni | Lot | Nambari ya Mkataba | Jina la Mkandarasi/ Msambazaji | Tarehe ya Mkataba | Kiwango cha Fedha cha Mkataba (Tshs.) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Procurement of Engineering equipments for Mnazi Mmoja, Mental Hosp and mwembeladu Hosp | LOT 1 - Engineering and Carpentry | SMZ/H0110/ NBC/G/2020/2021/21 | Juma Issa Omar | 30/03/21 | 838,972,150 |
| 2. | | LOT 2 - Air Condition and Refrigeration Tools | SMZ/HO110/ NBC/G/2020/2021/2 | Electrothermal Supplier and Services Ltd | 15/03/21 | 62, 616,350 |
| 3. | | LOT 3 - Automotives Equipments | SMZ/HO110/ NBC/2020/2021/21 | Visiwani Gern-eral Traders | 30/03/21 | 93, 679,000 |
| 4. | Supply of Hospital Hostel and Installation | - | SMZ/HO110/ NBC/G/2020/2021/07 | Lab Equip LTD | 29/04/21 | 139,734,188 |
| 5. | Supply of Stationery for Mnazi Mmoja, Mental and Mwembeladu Hospital | - | SMZ/HO110/NC-B/G/2020/2021/13 | SBK Secretary Services | 15/03/21 | 104,107,200 |
| 6. | Supply and Installation of Laboratory Equipments | - | SMZ/HO110/ NBC/G/2020/2021/01 | LAB Equip Limited | 29/04/21 | 183,975,290 |
| 7. | Supply of Cleaning equipment | | SMZ/H001/NC-B/G/2019/2020/13 | Bakari Yussuf Bakari | 09/01/20 | 139,870,000 |

Kukosekana kwa uwazi na usawa katika utoaji wa taarifa za wazabuni walioshindwa kunaweza kukapelekea migogoro na wazabuni na hatimae kuishtaki Serikali na kuisababishia hasara kubwa ya fedha za umma.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 8 cha Kanuni ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2021.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Hospitali ya Mnazi Mmoja kusimamia maadili ya maamuzi yatokanayo na Sheria ya Ununuzi na Uondoshwaji wa Mali za Umma kwa lengo la kuepusha kuingia kwenye migogoro na wazabuni kwa jambo la kutoa haki kwa asiehusika jambo ambalo huwenda likapelekea upotevu wa fedha za umma kwa mzabuni kuweza kuishitaki Serikali na kuingia gharama za kumlipa ambazo zingeliweza kuepukika ikiwa mipaka ya kisheria imesimamiwa na kutekelezwa ipaswavyo, vile vile uongozi unashuriwa kuzidisha umakini katika kufanya maamuzi ya zabuni mbali mbali wanazozitoa ili kuepuka kumpa mzabuni ambae gharama zake ni kubwa kulinganisha na wazabuni wengine na kupelekea kusababisha matumizi mabaya ya fedha za Serikali.

### 6.7.2.9 Kutokuwepo daftari la kurikodia, kuhifadhia na kutolea Mafuta

Sheria ya Ununuzi na Uondoshwaji wa Mali za Umma inelekeza vifaa vyote vinavyonunuliwa kurikodiwa katika daftari la ghalani na kuwekea utaratibu mzuri wa kutolewa kwa vifaa hivyo kila vinapohitajika kwa matumizi mbali mbali ya kiofisi.

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021, ukaguzi umebaini mafuta yenye thamani ya shilingi 56,888,000 sawa na Lita 11,279.3 za petrol na 19,077.90 za dizeli hayakuingizwa katika daftari la kurikodia, kuhifadhia na kutolea mafuta la ghalani.

Aidha ukaguzi umeshindwa kujuwa nambari za magari ambayo yalitumika kwa ajili ya kuingizia mafuta hayo katika kipindi chote hicho cha utumiaji wa mafuta hayo..

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria ya ununuzi na uondoshwaji wa mali za umma nambari 11 ya mwaka 2016. Mchanganuo wa matumizi hayo yanayoonesha thamani ya fedha iliyotumika na idadi ya lita za mafuta zilizotumika ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 156 : Matumizi ya mafuta yaliyokuwa hayakurikodiwa kwenye daftari la kutunzia kumbu kumbu za mafuta.**

| Hati ya malipo Nambari | Tarehe | Kiwango cha fedha (Tshs.) | Nambari ya Ankara | Lita za mafuta ya Petrol | Lita za mafuta ya Diesel |
|---|---|---|---|---|---|
| 75/8 | 12/8/2020 | 8,000,000 | 911 ya 11/8/20 | 1061.0 | 3116.9 |
| 40/10 | 6/10/2020 | 8,000,000 | 1121 ya 23/9/20 | 1048.8 | 3107.2 |
| 26/12 | 14/12/2020 | 16,000,000 | 1390 ya 2/12/20 | 1026.7 | 3215.4 |
| 25/2 | 17/2/2021 | 8,000,000 | 49 ya 7/1/21 | 1046.0 | 3296.7 |
| 44/3 | 16/3/2021 | 8,000,000 | 115 ya 2/2/21 | 1062.7 | 3280.5 |
| 16/4 | 16/4/2021 | 8,888,000 | 236 ya 3/3/21 | 1034.1 | 3061.2 |
| **Jumla** | | **56,888,000** | | **11,279.3** | **19,077.90** |

Kutokuwepo daftari la kurikodia na kutolea mafuta katika Hospitali ya Mnazi Mmoja kunapelekea utaratibu wa kurikodi na utokaji wa mafuta kutokuwa sahihi na kusababisha upotevu wa mafuta hayo.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Hospitali ya Mnazi Mmoja kuhakikisha kwamba inaweka daftari la kupokelea, kuhifadhia na kutolea mafuta ili kuweza kuondosha uwezekano wa upotevu wa raslimali hiyo ya mafuta.

### 6.7.2.10 Kuwepo matumizi ya mara kwa mara ya ununuzi wa gesi ya Oxygen pamoja na posho la safari kwa mfanyakazi wa Hospitali shilingi 86,756,000

Hospitali ya Mnazi Mmoja ina chanzo kimoja cha kuzalishia gesi ya oxygen ambao ni mtambo unaozalisha mitungi 30 yenye ujazo wa lita 50 kwa siku.

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021 ukaguzi umebaini kwamba Hospitali ya Mnazi Mmoja inamsafirisha mfanyakazi wake mara kwa mara kwenda Dar-es-Salaam kwa ajili ya kununua mitungi ya gesi inayotumika hospitali kwa shughuli zinazohusiana na gesi. Kutokana na hali hiyo ukaguzi umebaini Hospitali inatumia gharama kubwa kwa ajili ya safari hizo na kumlipa mfanyakazi posho la safari kila anapokwenda Dar es Salaam, kama Hospitali itanunua mitungi zaidi basi gharama hizo zingepungua sana.

Aidha, kwa mujibu wa barua ya tarehe 12/08/2021 kutoka kwa Mkurugenzi Huduma za Ufundi kwenda kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali ya Mnazi Mmoja ya kuomba Hospitali kununuliwa mtambo mpya wa kuzalishia gesi ya Oxygen ambao utakuwa na uwezo wa kuzalisha mitungi 120 kwa siku kwa lengo la kupunguza matumizi makubwa ya fedha za posho zinazolipwa kwa ajili ya mtumishi kwenda kununua gesi hizo Dar es Salaam.

Uchambuzi wa fedha za posho zinazotumika kwa ajili ya kwenda Dar es Salaam kununua oxygen ni kama zinavyoonekana kwenye jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 157**: **Gharama za matumizi ya posho kwa ajili ya ununuzi wa gesi kwa matumizi ya Hospitali**

| Hati ya malipo Nambari | Tarehe | Gharama ya Gesi (Tshs.) | Posho (Tshs.) | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 113/8 | | 2,972,000 | 540,000 | Malipo kwa ajili ya safari ya Dar-es-salaam kwa ununuzi wa medicai oxygen |
| 8/10 | 1/10/2020 | 2,972,000 | 540,000 | |
| 7/12 | 8/12/2020 | 2,972,000 | 540,000 | |
| 96/12 | 21/12/2020 | 2,892,000 | 540,000 | |
| 24/1 | 5/1/2021 | 2,932,000 | 540,000 | |
| 4/2 | 8/2/2021 | 2,932,000 | 540,000 | |
| 5/2 | 8/2/2021 | 2,932,000 | 540,000 | |
| 7/2 | 8/2/2021 | 2,932,000 | 540,000 | |
| 8/2 | 8/2/2021 | 2,932,000 | 540,000 | |
| 35/2 | 18/2/2021 | 5,012,000 | 540,000 | |
| 36/2 | 18/2/2021 | 2,882,000 | 540,000 | |
| 12/3 | 26/2/2021 | 2,922,000 | 540,000 | |
| 29/3 | 16/3/2021 | 2,842,000 | 490,000 | |
| 40/3 | 16/3/2021 | 1,800,000 | 490,000 | |
| 42/3 | 16/3/2021 | 2,922,000 | 490,000 | |
| 4/4 | 8/4/2021 | 5,014,000 | 490,000 | |
| 10/4 | 15/4/2021 | 2,922,000 | 490,000 | |
| 57/4 | 29/4/2021 | 2,400,000 | 490,000 | |
| 58/4 | 29/4/2021 | 4,802,000 | 490,000 | |
| 18/5 | 5/5/2021 | 2,922,000 | 490,000 | |
| 3/6 | 9/6/2021 | 2,802,000 | 490,000 | |
| 4/6 | 9/6/2021 | 2,842,000 | 490,000 | |
| 5/6 | 9/6/2021 | 2,922,000 | 490,000 | |
| 6/6 | 9/6/2021 | 2,922,000 | 490,000 | |
| **Jumla** | | **74,396000** | **12,360,000** | |

Kuwepo kwa matumizi ya mara kwa mara ya ununuzi wa gesi ya Oxygen pamoja na posho la safari kwa wafanyakazi kunapelekea kujitokeza kwa matumizi yasiyo ya lazima kwa Hospitali.

Kutokana na umuhimu wa matumizi ya gesi kwa Hospitali ya Mnazi Mmoja, Ukaguzi unashauri uongozi wa Hospitali ya Mnazi Mmoja kupitia Serikali Kuu kuchukua jitihada za makusudi kuhakikisha kunanunuliwa mtambo mpya wa kuzalisha Oxygen ili kuweza kupunguza gharama za matumizi ya fedha za umma.

#### 6.7.2.11 Ukiukwaji wa makubaliano ya mkataba wa ununuzi wa vifaa vya kuandikia

Hospitali ya Mnazi Mmoja ilifunga mkakata wa ununuaji wa vifaa vya kuandikia na msambazaji **Skotch General Supplies Co. Ltd** tarehe 9/01/2020 kwa kipindi cha miaka mitatu.

Ukaguzi umebaini kwamba Hospitali ya Mnazi Mmoja imekiuka makubaliano ya kimkataba ambapo walikubaliana na mzabuni kusambaziwa vifaa vya kuandikia kwa muda wa miaka mitatu, kinyume chake hospitali ilifanya manunuzi ya vifaa hivyo kutoka kwa mzabuni **Khamis Hamad Stationary** kupitia hati ya malipo yenye nambari 16/12 ya tarehe 10/12/2020 na Ankara nambari 557 ya tarehe 21/9/2020 kwa shilingi 17,106,539 bila ya kuwepo kwa taarifa yoyote ya kuvunjwa kwa mkataba wa awali.

Kusitisha makubaliano ya mkataba wa awali bila ya uwepo wa taarifa wa mzabuni wa awali kunaweza kukapelekea kuingizia Serikali hasara pindipo mzabuni atakapoamua kuishitaki Serikali na kudai fidia kutokana na kuvunja makubaliano pasi na sababu za msingi. Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria ya ununuzi na uondoshwaji wa mali za umma namba 11 ya mwaka 2016.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Hospitali ya Mnazi Mmoja kufuata matakwa ya Sheria ya manunuzi uondoshaji wa mali za umma nambari 11 ya mwaka 2016.

### 6.7.3 MAABARA YA AFYA YA JAMII (PHL) PEMBA

Ukaguzi wa hesabu za Maabara ya Afya ya Jamii (PHL) kwa mwaka wa fedha 2020/2021 umefanywa kwa mujibu wa Sheria, kanuni, taratibu pamoja na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**MATOKEO NA MAPENDEKEZO YA UKAGUZI**

#### 6.7.3.1 Malipo ambayo hayakukatwa kodi ya zuio shilingi 12,838,937

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba jumla ya shilingi 12,838,937 zimetumika kwa ajili ya matumizi mbali mbali ya Maabara ya Afya ya Jamii Pemba kwa watoa huduma mbali mbali bila ya kukatwa kodi ya zuio.

Kutokukata kodi ya zuio ni kuikosesha Serikali mapato ambapo ni kwenda kinyume na kifungu namba 50(2) cha Sheria nambari 7 ya Usimamizi wa Kodi ya Bodi ya Mapato ya mwaka 2009 pamoja na marekebisho yake. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 158 : Malipo ambayo hayakukatwa kodi ya zuio**

| Hati Namba | Hundi Namba | Aliyelipwa | Kiasi cha fedha kilicholipwa (Tshs.) | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 8/03 4/8/2020 | 005478 | Suleiman Seif Rashid | 300,000 | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya maabara |
| 8/025 5/8/2020 | 005483 | Mbarouk Juma Ali | 320,000 | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa sabuni |
| 8/026 5/8/2020 | 005472 | Mabrouk Saadum Songoro | 350,000 | Malipo ya fedha kwa ajili ya matengenezo ya gari |
| 8/027 5/8/2020 | 005482 | Mbarouk Juma Ali | 242,000 | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa |
| 8/031 7/8/2020 | 005489 | Capital Technology Centre | 365,000 | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya kuandikia |
| 8/032 7/8/2020 | 005488 | Mohammed Aboud Ali | 353,000 | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa bidhaa |
| 8/033 7/8/2020 | 005487 | | 480,000 | |
| 8/067 21/8/2020 | 005512 | Tahfif Auto Works | 281,750 | Malipo ya fedha kwa ajili ya matengenezo ya gari |
| 8/068 21/8/2020 | 005512 | Tahfif Auto Works | 241,500 | Malipo ya fedha kwa ajili ya matengenezo ya gari |
| 8/069 21/8/2020 | 005512 | | 293,250 | Malipo ya fedha kwa ajili ya matengenezo ya gari |
| 1/024 8/01/2021 | T.T | Hosp Lab surgical Distributtors | 5,242,559 | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya maabara |
| 1/044 15/01/2021 | 005709 | Quik-Win Computer Repair | 228,144 | Malipo ya fedha kwa ajili ya matengenezo ya photocopy |
| 1/045 15/01/2021 | 005710 | Mohammed Aboud Ali | 413,987 | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa sabuni |
| 1/046 15/01/2021 | 005711 | | 212,935 | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa viburudishaji |
| 1/053 19/01/2021 | 005713 | Moza Mohammed Ali | 595,000 | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa viburudishaji |
| 8/070 21/08/2020 | 005512 | Tahfif Auto Work | 264,500 | Malipo ya fedha kwa ajili ya matengenezo ya gari |
| 11/030 13/11/2020 | 005606 | Suleiman Seif Rashid | 298,775 | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya ujenzi. |
| 1/018 7/01/2021 | 005693 | Pandu Book Shop | 531,385 | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya kuandikia |
| 01/088 29/1/2021 | 005728 | Rashid Mohammed Soud | 1,468,677 | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya gari |
| 02/065 9/02/2021 | T.T | Hosp Lab surgical Distributtors | 356,475 | Malipo ya fedha kwa ajili ya vifaa vya mradi |
| **Jumla** | | | **12,838,937** | |

### 6.7.3.2 Malipo kwa watoa huduma ambao hawakusajiliwa na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma shilingi 5,510,515

Kwa mujibu wa kifungu cha 23(1) cha Sheria ya Manunuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma kinaeleza kulingana na masharti ya sheria hii mtu, kampuni au taasisi haitawasilisha zabuni au vyenginevyo kushiriki katika manunuzi ya Umma isipokua chombo kiwe kimesajiliwa na Mamlaka ya Manunuzi.

Kwa mujibu wa kifungu cha 23(2), zabuni kutoka kwa mtu, kampuni au chombo ambacho hakijasajiliwa haifai na hakitazingatiwa na taasisi ya ununuzi.

Ukaguzi umebaini kwamba Maabara ya Afya ya Jamii Pemba imefanya manunuzi na watoa huduma mbali mbali ambao hawakusajiliwa na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya Zanzibar.

Kufanya hivyo kunapelekea kuikosesha Serikali mapato ambapo ni kwenda kinyume na Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 159 : Watoa huduma ambao hawakusajiliwa na Mamlaka ya ununuzi na uondoshaji wa Mali za Umma**

| Hati Namba | Hundi Namba | Aliyelipwa | Kiasi cha fedha kilicholipwa (Tshs.) | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 8/025 5/8/2020 | 005483 | Mbarouk Juma Ali | 320,000 | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa sabuni |
| 8/026 5/8/2020 | 005472 | Mabrouk Saadum Songoro | 350,000 | Malipo ya fedha kwa ajili ya kodi ya Gari |
| 8/027 5/8/2020 | 005482 | Mbarouk Juma Ali | 242,000 | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya kazi za vitendo |
| 8/079 27/8/2020 | 005515 | Sultan Said Amiri | 250,000 | Malipo ya fedha kwa ajili ya matengenezo ya rafu |
| 11/023 12/11/2020 | 005600 | Aras Company Ltd | 760,000 | Malipo ya fedha kwa ajili ya uwekaji wa mfumo wa ulinzi |
| 11/024 12/11/2020 | 005601 | Mbarouk Juma Ali | 243,354 | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa sabuni |
| 11/027 12/11/2020 | 005603 | Aras Company Ltd | 346,969 | Malipo ya fedha kwa ajili ya utengenezaji wa vitambulisho |
| 1/018 7/1/2021 | 005693 | Pandu Book Shop | 531,385 | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya kuandikia |
| 1/080 27/1/2021 | 005725 | | 998,130 | |
| 1/088 29/1/2021 | 005728 | Rashid Mohammed Soud | 1,468,677 | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya gari |
| **Jumla** | | | **5,510,515** | |

### 6.7.3.3 Hati za malipo zenye vielelezo pungufu shilingi 163,304,535

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba jumla ya shilingi 163,304,535 zimelipwa na Maabara ya Afya ya Jamii kwa matumizi mbali mbali lakini baadhi ya vielelezo husika havikupatikana kwa ukaguzi ili kuweza kuthibitisha uhalali wa matumizi hayo.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 34(1) cha Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016. Mchanganuo wa hati za malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 160 : Hati za malipo zenye vielelezo pungufu**

| Hati Namba | Hundi Namba | Kiasi cha fedha kilicholipwa (Tshs.) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 8/019 5/08/2020 | 005473 | 1,000,000 | Abdalla Shaib Kheri | Malipo ya fedha kwa ajili ya washiriki wa kikao |
| 8/020 5/8/2020 | 005474 | 2,500,000 | Milfat Nassor Khalfan | |
| 11/028 12/11/2020 | 005604 | 2,321,200 | Sharif Petrol Station | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa mafuta |
| 11/053 20/11/2020 | 005622 | 500,000 | | |
| 11/066 23/11/2020 | 005626 | 373,200 | | |
| 1/005 6/01/2021 | 005695 | 1,912,000 | | |
| 1/009 7/01/2021 | 005692 | 420,000 | Mabrouk saadun Songoro | Malipo ya fedha kwa ajili ya nauli za mama wajawazito |
| 1/014 7/01/2021 | 005692 | 900,000 | Abdalla sahib Kheir | |
| 1/016 7/01/2021 | 005693 | 1,200,000 | Milfat Nassor Khalfan | |
| 1/024 8/01/2021 | T.T | 5,242,559 | Hosp Lab Surgical Distrbutors | Malipo ya fedha kwa ajili ununuzi wa vifaa vya maabara. |
| 1/053 19/01/2021 | 005713 | 595,000 | Moza mohammed Ali | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa viburudishaji |
| 1/068 26/01/2021 | TT | 3,864,189 | Hosp Lab Surgical Distributors | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya maabara |
| 1/069 26/1/2021 | TT | 2,851,800 | | |
| 1/080 27/1/2021 | 005725 | 998,130 | Pandu Book Shop | |
| 01/088 29/1/2021 | 005728 | 1,468,677 | Rashid Mohammed Soud | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya magari |
| 8/034 7/8/2020 | 005486 | 2,307,800 | Sharif Petrol Station | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa mafuta |
| 2/4 1/4/2021 | 005865 | 1,000,000 | Halima Mkubwa Juma | Malipo ya fedha kwa ajili ya Mkopo kwa mfanyakazi. |
| 4/4 1/4/2021 | 005866 005866 | 9,600,000 | Hookwom staff | |
| 33/4 12/4/21 | 005879 | 3,247,500 | Sharif Petrol Station | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa mafuta |

| Hati Namba | Hundi Namba | Kiasi cha fedha kilicholipwa (Tshs.) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 74/4 27/4/21 | 005902 na 005903 | 7,026,000 | PHL- Idc Staff | Malipo ya fedha kwa ajili ya posho kwa mfanyakazi |
| 81/4 27/4/21 | 005902 na 005903 | 9,015,000 | Moxi staff | |
| 87/4 28/4/21 | 005902 na 005903 | 1,236,000 | Zest Staff | |
| 22/4 8/4/2021 | 005873 | 975,000 | CPHK Staff | |
| 73/4 27/4/2021 | 005902 005903 | 1,800,000 | Schistobreak staff | |
| 74/4 27/4/21 | 005902 na 005903 | 7,026,000 | PHL- Idc Staff | |
| 81/4 27/4/21 | 005902 na 005903 | 9,015,000 | Moxi staff | |
| 87/4 28/4/21 | 005902 na 005903 | 1,236,000 | Zest Staff | |
| 91/4 30/4/21 | 005901 | 3,400,000 | Hookworm expulsion staff | |
| 30/7 16/7/2020 | 005453 | 73,847,480 | Saleh Juma Mohd | Malipo ya fedha kwa ajili ya mafunzo. |
| 58/7 | - | 1,800,000 | Ulfat A.Mohd Suleiman A. Suleiman Said M.Said | Malipo ya fedha kwa ajili ya posho kwa wafanyakazi |
| 59/7 | | 1,000,000 | Khamis R.Suleiman Ahmed H. Said Mohd N. Ali | |
| 20a/10 | 005559 | 1,813,000 | Petty Cash | Malipo ya fedha kwa ajili ya matumzi madogo madogo |
| 20b/10 | 005559 | 1,813,000 | | |
| | **Jumla** | **163,304,535** | | |

### 6.7.4 WAKALA WA MAABARA YA MKEMIA MKUU WA SERIKALI

Ukaguzi wa hesabu za Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali kwa mwaka wa fedha 2020/2021 umefanywa kwa mujibu wa Sheria, kanuni, taratibu pamoja na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Taarifa ya Mapato**

Wakala wa Maabara ya Mkemia wa Serikali ilikadiriwa kukusanya jumla ya shilingi 1,806,950,622 kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 jumla ya shilingi 1,308,295,259.7 zilikusanywa sawa na asilimia 72 ya makadirio.

**Taarifa ya Matumizi**

Wakala wa Maabara ya Mkemia wa Serikali kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ilikadiriwa kutumia jumla ya shilingi 1,806,950,622 kwa matumizi ya kazi za kawaida. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 jumla ya shilingi 1,263,438,297 ziliingizwa na kutumika kwa kazi za kawaida sawa na asilimia 59.2 ya makadirio.

**MATOKEO NA MAPENDEKEZO YA UKAGUZI**

### 6.7.4.1 Kukosekana kwa mchanganuo wa makusanyo ya mapato ya Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu yenye jumla ya shilingi 253,813,904

Katika kupitia taarifa mbalimbali za fedha Ukaguzi umeshindwa kutofautisha makusanyo halisi ya huduma mbalimbali zinazotolewa na Wakala kwa mujibu wa Sheria ya Wakala kutokana na kushindwa kuweka kumbukumbu za ukusanyaji wa mapato kwa Bandarini na Ofisi kuu kwenye mfumo ambao utaainisha tofauti ya huduma hizo (mchanganuo). kwa kawaida uchunguzi huo unakusanya mapato yanayotokana na uchunguzi wa DNA, Asali, Dawa Asili, Mafuta, Pombe, Maji, Mkojo, Kemikali, vile vile wanatoa huduma ya utoaji Vibali (chemical na chemical product).

Kushindwa kuweka mchanganuo wa makusanyo ya mapato katika mfumo mzuri ambao utapelekea ufungaji mzuri wa Hesabu za mwaka kutapelekea kushindwa kujua mapato halisi yaliyotokana na vyanzo hivyo, aidha kutojua gharama zinazotumika kwa kufanya huduma ya vifaa vya uchunguzi pamoja na ununuzi wa bidhaa zitakazoleta tija kwa Taasisi.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wakala wa Maabara ya Mkemia wa Serikali kuchukuwa jitihada za kuhakikisha kuwa mapato yote yanayotokana na utoaji wa huduma za Maabara yanarikodiwa kwa utaratibu uliowekwa wa kutofautisha huduma hizo.

### 6.7.4.2 Kukosekana kwa kibali cha ruhusa za matumizi ya fedha za mapato shilingi 315,000,000

Ukaguzi umebaini kuwa Taasisi ya Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu inafanya matumizi yake kwa kutumia fedha za makusanyo ya ndani kwenye hesabu nambari 0403978000 jumla ya shilingi 315,000,000 zimebainika kutumika kwa matumizi mbali mbali dosari iliyobainika katika ukaguzi ni kukosekana kwa muongozo au ruhusa kutoka kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali inayowataka wakala kutumia fedha za mapato kwa ajili ya uendeshaji wa huduma zinazotolewa na taasisi hiyo.

Kutumia fedha za mapato kwa matumizi mbali mbali bila ya kuwepo kwa ruhusa kutoka kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali ni kwenda kinyume na Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wakala wa Maabara ya Mkemia wa Serikali kuhakikisha unafanya matumizi ya fedha zilizoidhinishwa ili kuepuka kufanya matumizi yasiyo na tija.

**Jadweli Nambari 161 : Matumizi ya fedha za mapato zisizoidhinishwa**

| Hati Namba | Hundi namba | Aliyelipwa | Thamani (Tshs.) |
|---|---|---|---|
| R/4/5 ya 20/5/2021 | T.T kutoka A/C 0403978000 ya mapato kwenda 0404060000 PBZ ya matumizi | Wakala wa Maabara ya Mkemia | 35,000,000 |
| R/19/3 ya 24/3/2021 | T.T | | 30,000,000 |
| R/2/2/2021 ya 12/2/2021 | | | 50,000,000 |
| R/15/01 ya 15/1/2021 | | | 25,000,000 |
| R/17/11 ya 25/11/2020 | | | 20,000,000 |
| R/11/7 ya 27/7/2020 | | | 20,000,000 |
| R/11/6 ya 17/6/2021 | | | 30,000,000 |
| R/28/9 ya 11/9/2020 | | | 30,000,000 |
| R/38/10 ya 21/10/2020 | | | 25,000,000 |
| R/17/11 ya 25/11/2020 | | | 20,000,000 |
| R/11/6 ya 17/6/2021 | | | 30,000,000 |
| **Jumla** | | | **315,000,000** |

Taasisi kufanya matumizi ya fedha za makusanyo ya ndani bila ya kuwa na kibali kutoka kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali kutapelekea kufanya matumizi yaliyo nje ya bajeti ambayo hayatakuwa na ulazima na kupelekea kujitokeza kwa viashiria vya ukiukwaji wa matumizi ya fedha za umma.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wakala wa Maabara ya Mkemia wa Serikali kuchukuwa jitihada za kuhakikisha Wakala inapata ruhusa ya kutumia fedha za makusanyo kutoka katika taasisi husika.

### 6.7.4.3 Kukosekana kwa ulinzi dhamana katika Taasisi ya Wakala wa Mkemia

Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu inajukumu la kutoa huduma za uchunguzi wa madawa ya kulevya, sumu, uchunguzi wa vinasaba pamoja na kuweka kumbukumbu za vinasaba, kudhibiti usajili kemikali na bidhaa zinazotokana na kemikali za majumbani na viwandani, kufanya uchunguzi wa sampuli za chakula pamoja na vinywaji. Ukaguzi umebaini kuwa Taasisi hiyo ina vifaa nyeti (Mashine za kufanyia uchunguzi mbalimbali) kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu yao bila ya uwepo wa Ulinzi dhamana kwa lengo la kulinda usalama wa vitendea kazi hivyo.

Kutokuwa na usalama wa kutosha katika Taasisi ya wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu kuna uwezekano mkubwa wa kuhujumiwa kwa mashine ambazo Serikali imetumia fedha nyingi kwa kufanya manunuzi hayo.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wakala wa Maabara ya Mkemia wa Serikali kuchukuwa jitihada za haraka kuhakikisha kwamba Taasisi hiyo inakuwa na ulinzi dhamana kwa ajili ya usalama wa vitendea kazi

### 6.7.4.4 Kukosekana kwa utaratibu wa utoaji mikopo ya ndani kwa wafanyakazi wa Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Zanzibar

Katika kupitia taarifa za fedha pamoja na taarifa za benki, Ukaguzi umebaini kuwepo kwa shilingi 13,576,364.35 katika hesabu ya Wakala yenye namba 0406584000 ambazo zinatumika kwa ajili ya Mfuko wa mikopo ya ndani kwa wafanyakazi wa Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu Zanzibar, Mfuko huo ulianzishwa kipindi cha mwaka fedha 2017/2018 kupitia makusanyo ya ndani "Capital" wa jumla ya shilingi 50,000,000.

Aidha, Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu wameanzisha mfuko huo bila ya kuwa na sera zinazotoa muelekeo wa namna ya kukopa pamoja na kurejesha fedha zilizokopeshwa, jambo ambalo linapelekea kukosekana kwa muongozo na masharti ya kukopa na kulipa mikopo inayotolewa na taasisi hiyo kwa muda muafaka kwa kuzingatia vigezo na masharti ili tija ipatikane kwa watumishi pamoja na taasisi kwa ujumla.

Kukosekana kwa sera ya mikopo kwa mfuko wa mikopo katika Taasisi kutapelekea Taasisi kukosa vigezo vya kumchukulia hatua mtendaji ambae atashindwa kulipa mkopo pindipo atakwenda kinyume na vigezo na masharti yake. Vile vile inapelekea upendeleo wa kupata mikopo.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wakala wa Maabara ya Mkemia wa Serikali jitihada za kukaa na watendaji wanaohusika na suala zima la mfuko wa mkopo kwa lengo la kuandaa sheria ya mikopo pamoja na sera za mikopo (Credit Policy)

### 6.7.4.5 Kutokuwepo kwa Msimamizi wa Kitengo cha TEHAMA

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika Wakala wa Maabara ya Mkemia wa Serikali inatekeleza makujumu yake ya kazi mbali mbali ikiwemo majukumu ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano, katika ukaguzi uliofanyika timu ya wakaguzi ilifanya mahojiano mbali mbali kwa lengo la kutathmini mwenendo wa kazi za kitengo cha TEHAMA na kubaini kitengo hicho hakina msimamizi dhamana ambae atakuwa na jukumu la kusimamia sera za TEHAMA pamoja na kusamiamia miundombinu na vifaa vyote vya TEHAMA vinayotumika katika taasisi hiyo ikiwemo "hardware, software" pamoja na watumiaji wa miundombinu na vifaa hivyo vya TEHAMA.

Kukosekana kwa msimamizi wa kitengo cha TEHAMA kutapelekea kukosekana kwa udhibiti wa vifaa pamoja na miundombinu ya mifumo ya TEHAMA ya taasisi.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wakala wa Maabara ya Mkemia wa Serikali kuhakikisha unachukuwa jitihada za makusudi ili kumtafuta mtumishi mwenye uwezo na uweledi wa kusimamia masuala ya TEHAMA pamoja na kuwajengea uwezo watumishi waliokuwepo ili kuweza kusaidia changamoto za matumizi ya TEHAMA zinazoweza kujitokeza katika taasisi hiyo.

### 6.7.4.6 Kukosekana kwa ushahidi wa majaribio ya taarifa za nakala (Restoration test)

Katika kupitia taarifa zinazofungamana na mifumo ya mawasiliano, ukaguzi umebaini umebaini kwamba Wakala wa Maabara ya Mkemia wa Serikali huhifadhi taarifa zake muhimu katika vifaa mbali mbali vya tehama, dosari iliyobainika na ukaguzi ni kwamba taarifa hizo hazifanyiwi majaribio (Restoration test ) ili kuweza kutambua na kuhakikisha kwamba ziko katika hali ya uzima na usalama wa kuweza kufanya kazi kwa ufanisi endapo zikihitajika kufanyiwa kazi.

Kutokuzifanyia majaribio ya utendaji kazi kila mara kwa taarifa zilizokuwa zimehifadhiwa kunaweza kukapelekea athari ya kutozipata taarifa hizo kutokana na kuharibika au kuathirika kwa namna yoyote bila ya kujulikana na hatimae kupelekea kutokezea kwa janga

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wakala wa Maabara ya Mkemia wa Serikali uongozi wa Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu kuanzisha sera za kuhifadhi nakala za taarifa kutoka katika mifumo yote ya taasisi na kuzifanyia majaribio ya mara kwa mara ili kuweza kuona kama ni sahihi na zinaweza kufanya kazi vzuri na kuzitegemea endapo janga lolote likitokea katika miundombinu ya mikuu ya mawasiliano ya Wakala.

#### 6.7.4.7 Kutozingatiwa vizuri kwa utengenezaji wa akanti za watumiaji wa mfumo wa Data Pack

Ukaguzi umebaini kuwa, kumetengenezwa akaunti nyingi zisizokuwa na ulazima katika mfumo wa (Data Pack) na kubainika akaunti ambazo hazina majina halisi ya watumiaji na nyengine hazitumiwi kabisa na wahusika.

Kutengenezwa kwa akaunti zisizokuwa na majina halisi ya watumiaji au kutengeneza akaunti za matumizi ya mfumo zisizokuwa na ulazima katika mfumo kunaweza kupelekea kutumiwa akaunti hizo kwa kufanya uharibifu bila ya kutambuliwa aliefanya uharibifu huo.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wakala wa Maabara ya Mkemia wa Serikali kuzipitia akaunti zote za mfumo wa data pack na kuhakikisha kuwa kila akaunti inatumika kwa mtumiaji husika wa mfumo na vile vile akaunti hizo ziwekewe ukomo wa matumizi katika mfumo huo (priveledges user access).

#### 6.7.4.8 Kutokufanya kazi vizuri kwa Mfumo wa (Data pack)

Katika kupitia nyaraka mbalimbali zikiwemo hesabu za mwaka, ilibanika kwamba Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu iliununua mfumo wa **Data Pack** kwa lengo la kurahisisha kazi za taarifa za sampuli na utekelezaji wa kazi ya wachambuzi (Analysts). Ukaguzi umebaini kwamba mfumo wa Data pack ulionunuliwa unahitilafu za muda mrefu ambazo zimepelekea kushindwa kutumika vizuri na kuleta tija na ufanisi kwa ofisi hadi sasa.

Kushindwa kufanyakazi kwa mfumo huo kunapelekea kupunguza ufanisi wa kazi zote zilizokuwa zikifanywa ndani ya mfumo huo.

Ukaguzi unashauri kwamba, ofisi ya Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu kuchukuwa jitihada za kuimarisha mfumo huo ikiwemo kufanya mazungumzo na walioutengeneza (System Vendor) ili kurudisha ufanisi wa utendaji kazi wa mfumo kulingana na thamani ya fedha iliyotumika kwa kununulia mfumo huo.

#### 6.7.4.9 Kutokuwepo kwa Mkataba wa mfumo wa (Data Pack)

Katika kuhakiki taarifa mbali mbali zikiwemo taarifa za Hesabu ya mwaka za Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu ukaguzi umebaini kuwa, Wakala imenunua mfumo wa Data Pack kutoka kwa muuzaji na kuutumia kwa ajili ya kuhifadhi taarifa za vielelezo vya sampuli (Data pack), dosari iliyobainika na ukaguzi ni kwamba Wakala imenunua mfumo huo na kuutumia bila ya kuingia Mkataba wa aina yoyote na muuzaji wa mfumo kwa lengo la kuweza kupata msaada pamoja na huduma za kiufundi kutoka kwa muuzaji ikiwa mfumo utaleta changamoto au ikibainika dosari yoyote ya kiutendaji katika mfumo huo.

Kutofungwa mkataba wowote baina ya Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu na wauzaji wa mfumo huo kunaweza kupelekea kushindwa kupata huduma kamili za utendaji kazi katika mfumo ikiwemo kupata msaada wa kiufundi, kuimairishwa kwa mfumo (updates) pamoja na leseni za matumizi ya mfumo huo na kuweza kuwawajibisha wauzaji hao kutokana na dosari na hitilafu kubwa za kiutendaji zitakapotokezea katika mfumo bila ya maelewano yoyote.

Ukaguzi unashauri kwamba, ni vyema kufungwa mikataba madhubuti ya manunuzi baina ya Taasisi ya Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu na Taasisi yoyote itakayonunua mifumo kwao kwani mikataba hiyo itaweza kuilinda taasisi ili kuweza kupata haki ya kulipwa kwa mujibu wa makubaliano ya mkataba.

### 6.7.4.10 Mapungufu yaliyojitokeza katika kufanya service Machine ya DNA yenye thamani ya USD 21,315.60. (Tshs. 49,857,188.40)

Ukaguzi umebaini kuwa Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu wameingia mkataba na Company ya M/S. AFRICA BIOSYSTEMS TANZANIA LTD uliofungwa tarehe 15/7/2021 wenye thamani ya USD 21,315.60 sawa na shilingi 49,857,188.40 zilizolipwa kwa hati namba R/33/6 ya tarehe 14/6/2021 kwa ajili ya kutoa huduma ya kuifanyia Service Mashine ya Uchunguzi wa Vinasaba (DNA Machine) kwa lengo la kuhakikisha mashine hiyo inadumu kwa muda mrefu.

Dosari ya ukaguzi iliyobainika ni kukosekana kwa taratibu za kumpata mtoa huduma huyo jambo ambalo linaweza likapelekea kutumia gharama kubwa ya fedha kwa kukosekana ushindani wa bei.

Kutokana kukiukwa kwa taratibu za kumpata mtoa huduma kumepelekea kujitokeza kwa changamoto mbali mbali ikiwemo kutokuainishwa kwa aina ya kazi na muda ambao utatumika kufanya kazi hiyo, kukosekana kwa mapato ya Serikali yatokanayo na kutokukatwa kodi kwa mtoa huduma huyo na kuiwasilisha kwa mamlaka husika.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wakala wa Mkemia Mkuu wa Serikali kuhakikisha unafuata na kuzingatia matakwa ya kanuni na sheria ya Ununuzi na Uondoshwaji wa Mali za Umma ili kuweza kupatikana kwa mapato yanayokusudiwa.

### 6.7.4.11 Mapungufu yaliyojitokeza katika ununuzi wa DNA Consumables yenye thamani ya USD 60,585.92 (Tshs. 141,710,466.90)

Ukaguzi umebaini kuwa Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu wameingia mkataba na Company ya M/S. AFRICA BIOSYSTEMS TANZANIA LTD uliofungwa tarehe 15/7/2021 wenye thamani ya USD 60,585.92 sawa na shilingi 141,710,466.90 zilizolipwa kwa hati namba R/38/6 ya tarehe 30/6/2021 kwa ajili ya ununuzi wa (DNA Machine) kwa lengo la kuhakikisha mashine hiyo inadumu kwa muda mrefu.

Dosari ya ukaguzi iliyobainika ni kukosekana kwa taratibu za kumpata mtoa huduma huyo jambo ambalo linaweza likapelekea kutumia gharama kubwa ya fedha kwa kukosekana ushindani wa bei.

Kutokana kukiukwa kwa taratibu za kumpata mtoa huduma kumepelekea kujitokeza kwa changamoto mbali mbali ikiwemo kutokuainishwa kwa aina ya kazi na muda ambao utatumika kufanya kazi hiyo, kukosekana kwa mapato ya Serikali yatokanayo na kutokukatwa kodi kwa mtoa huduma huyo na kuiwasilisha kwa mamlaka husika.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wakala wa Mkemia Mkuu wa Serikali kuhakikisha unafuata na kuzingatia matakwa ya kanuni na sheria ya Ununuzi na Uondoshwaji wa Mali za Umma ili kuweza kupatikana kwa mapato yanayokusudiwa.

### 6.7.4.12 Uwepo wa deni litokanalo na utanuzi wa Maabara ya Mkemia shilingi 335,301,404

Ukaguzi umebaini kuwa Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu wameingia mkataba na M/S SHAMJO COMPANY LTD na CHIEF GOVERNMENT CHEMIST LABOURATORY AGENCY uliofungwa tarehe 31/5/2019 wenye thamani ya USD 767,540,558 zilizolipwa kwa ajili ya utanuzi wa ghorofa moja ambayo imeongezewa katika jengo la zamani na kuongezewa kwa kipande cha nyuma ubavuni mwa jengo hilo.

Dosari ya ukaguzi iliyobainika ni kutokufuatwa kwa taratibu za manunuzi ikiwemo kutangaza zabuni ya wazi kwa lengo la kumpata msambazaji atakaetoa huduma kwa bei nafuu na kiwango bora cha ujenzi huo, jambo ambalo limekosekana na kupelekea kujitokeza kwa ongezeko la thamani la shilingi 335,301,404 ukilinganisha na bei ya awali.

Kufanya hivyo kwenda kinyume na kifungu nambari cha 49(4)(5) Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshwaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016 kinachoeleza kwamba "Iwapo malipo ya mkataba yatazidi asilimia 15 yatalazimika kuwasilishwa kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali kwa lengo la kupata idhini ya matumizi." Jambo ambalo hadi ukaguzi unakamilika hatukuweza kupatiwa idhini ya matumizi iliyopelekea Wakala kulipa malipo ya ziada.

Ukaguzi unashauri  uongozi wa Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali unashauriwa kuipitia kwa kina mikataba yote wakati wa uandaaji wake, ili kuhakikisha dosari kama hizo zinaepukika.

### 6.7.4.13 Uwepo wa matumizi mabaya ya fedha shilingi 18,000,000 (VFM)

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika uwepo wa matumizi mabaya ya fedha za umma yenye thamani ya shilingi 18,000,000 yanayotokana na mshauri elekezi kutokuzingatia matakwa na vigezo vinavyohitajika katika ujenzi wa maabara. Kwa mujibu wa ujenzi wa maabara uliofanyika kwa mwaka wa fedha 2018/2019 na kukabidhiwa 2019/2020 umebainika ya kwamba mshauri elekezi aliwasilisha wazo la kuweka Tiles bila ya kuzingatia unyevu unyevu utakaojitokeza pindipo pakimwagika vimiminika na kusababisha utelezi au kuanguka kwa watumiaji wa eneo hilo.

Dosari iliyobainika katika ukaguzi ni kutokuzingatiwa kwa thamani ya fedha na aina ya ujenzi uliotumika jambo ambalo baada ya muda mfupi ililazimika kuvunjwa na kuondoshwa kwa taizi zote na kuamuliwa kuwekwa tarazo ambazo zitahimili unyevu unyevu na utelezi jambo ambalo limepelekea upotevu wa fedha za umma kwa kutokuzingatia taaluma na uzoefu wa mshauri elekezi katika ushauri alioutoa.

Pamoja na uwepo wa dosari hizo ukaguzi umeshindwa kujiridhisha uhalali wa matumizi ya fedha hizo kutokana na kukosekana kwa mchanganuo wa matumizi kwa mujibu wa thamani ya vifaa vinavyohitajika kununuliwa na kutumika (BOQ), Quotation document ili kupima ufanisi na tija itakayofikiwa mara baada ya kukamilika kwa ujenzi huo.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali kuhakikisha kwamba anafuata na kuzingatia matakwa ya kisheria ili kunusuru matumizi mabaya ya fedha za umma yanayopelekea kuisababishia Serikali hasara.Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 162 : Malipo yaliyofanyika kwa ajili ya uwekaji wa tarazo**

| Hati namba | Aliyelipwa | Kiasi (Tshs.) | Maelezo |
|---|---|---|---|
| R/3/3 ya 5/3/2021 | Iddi Moh'd Nindi a/c **0740631001** | 4,500,000 | Malipo ya awamu ya pili ya uwekaji tarazo katika jengo la Maabara |
| R/12/3 ya 18/3/2021 | | 4,500,000 | Uwekaji wa Tarazo katika vyumba saba vya Maabara ya Mkemia jumla ya Fedha 5,940,000 |
| R/34/2/2021 Ya 23/2/2021 | | 9,000,000 | Malipo ya awamu ya kwanza ya uwekaji wa Tarazo katika Maabara ya Mkemia |
| **Jumla** | | **18,000,000** | |

**WAKALA WA MAABARA YA MKEMIA MKUU WA SERIKALI - PEMBA**

### 6.7.4.14 Malipo kwa Watoa huduma ambao Hawakujasajiliwa na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma shilingi 10,345,300

Kwa mujibu wa kifungu cha 23(1) cha Sheria ya Manunuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma kinaeleza kulingana na masharti ya sheria hii mtu, kampuni au taasisi haitawasilisha zabuni au vyenginevyo kushiriki katika manunuzi ya Umma isipokua chombo kiwe kimesajiliwa na Mamlaka ya Manunuzi.

Kwa mujibu wa kifungu cha 23(2), zabuni kutoka kwa mtu, kampuni au chombo ambacho hakijasajiliwa haifai na hakitazingatiwa na taasisi ya ununuzi.

Ukaguzi umebaini kwamba Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali Pemba imefanya manunuzi na watoa huduma mbali mbali ambapo watoa huduma hao hawakusajiliwa na Mamlaka ya Manunuzi kwa mujibu wa sheria ambapo kumepelekea kushindwa kujiridhisha uhalali wa malipo hayo.

Kuwatumia wafanya biashara ambao hawajasajiliwa kwa mujibu wa Sheria kunapelekea kuikosesha Serikali mapato yanayotokana na kodi aidha ni kwenda kinyume na Sheria nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Afisi ya Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali- Pemba kufanya manunuzi kwa kuzingatia kanuni,sheria pamoja na miongozo mbali mbali iliyopo. Mchanganuo wa watoa huduma ni kama inavyoonekana katika jadweli lifuatalo:-

**Jadweli Nambari 163 : Malipo kwa watoa huduma ambao hawakusajiliwa na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma.**

| Hati Namba. | Hundi Namba. | Kiasi cha Fedha kilicholipwa (Tshs) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 03/01<br>25/01/2021 | 001261 | 1,500,000 | Trust Construction Company Ltd | Malipo ya fedha kwa ajili ya kazi za ujenzi |
| 01/01<br>30/12/2021 | T.T | 3,500,000 | Ushirika wa Umawa Cooperative Society | Malipo ya fedha kwa ajili ya huduma ya ulinzi |
| 12/02<br>17/02/2021 | 001267 | 1,639,500 | Trust Construction Company Ltd | Malipo ya fedha kwa ajili ya kazi za ujenzi |
| 13/02<br>17/02/2021 | 001268 | 1,000,000 | Asam Electrical Limited | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa Air condition |
| 02/05<br>30/04/2021 | T.T | 205,800 | One 2 One Ltd | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa Antivirus |
| 10/05<br>07/05/2021 | T.T | 2,500,000 | Umoja wa Askari Wastaafu (UMAWA) | Malipo ya fedha kwa ajili ya huduma ya ulinzi |
| **Jumla** | | **10,345,300** | | |

#### 6.7.4.15 Hati ya malipo iliyokosenekana kwa ukaguzi (missing voucher) shilingi 2,533,502

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwa Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali Pemba imefanya malipo yenye jumla ya shilingi 2,533,502 kwa hati ya malipo namba 05/11 ya tarehe 30/11/2020 lakini hati ya malipo hayo haikupatikana kwa ajili ya ukaguzi.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 34(1) cha Sheria nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016.

#### 6.7.4.16 Kukosekana kwa mapato yatokanayo na uchunguzi wa sampuli na DNA shilingi 20,730,000

Katika Ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba ofisi ya Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali Pemba inadai Taasisi mbali mbali za Serikali jumla ya shilingi 20,730,000 kwa ajili ya utoaji wa huduma ya uchunguzi sampuli pamoja na utoaji wa huduma katika uchunguzi wa vinasaba.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Ofisi ya Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali Pemba kuchukuwa juhudi za makusudi ili kuhakikisha kwamba mapato yote kutoka katika vianzio mbali mbali yanakusanywa na kuingizwa katika hesabu husika ya taasisi. Mchanganuo wa mapato yaliokosekana ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 164 : Mapato yatokanayo na uchunguzi wa sampuli na DNA.**

| Namba | Jina la Taasisi | Kiasi cha Fedha kinachodaiwa (Tshs) |
|---|---|---|
| 1. | Ofisi ya Jeshi la Polisi Mkoa wa Kusini Pemba | 12,150,000 |
| 2. | Ofisi ya Jeshi la Polisi Mkoa wa Kaskazini Pemba | 8,580,000 |
| **Jumla** | | **20,730,000** |

### 6.7.5 WAKALA WA CHAKULA, DAWA NA VIPODOZI ZANZIBAR

Ukaguzi wa hesabu za Wakala wa Chakula,Dawa na Vipodozi Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2020/2021 umefanywa kwa mujibu wa Sheria, kanuni, taratibu pamoja na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Taarifa ya Mapato**

Wakala wa Chakula, Dawa na Vipodozi Zanzibar ilikadiriwa kukusanya jumla ya Shilingi 7,027,072,460 kwa mwaka wa fedha 2020/2021. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 Wakala ilikusanya jumla ya shilingi 2,760,838,955.27 sawa na asilimia 39.3 ya makadirio.

**Taarifa ya Matumizi**

Wakala wa Chakula, Dawa na Vipodozi Zanzibar ilikadiriwa kutumia jumla ya shilingi 4,423,863,761 kwa matumizi ya kazi za kawaida. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 jumla ya shilingi 2,659,071,233.7 zimetumika kwa kazi za kawaida sawa na asilimia 60.1 ya makadirio.

## MATOKEO YA UKAGUZI NA MAPENDEKEZO

### 6.7.5.1 Kutokuainishwa kwa Mapato yatokanayo Ofisi ya Pemba katika taarifa za fedha za mwisho wa mwaka ya shilingi 129,635,679

Ukaguzi umepitia taarifa za fedha za mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2021 pamoja na taarifa za benki zinazoonesha mapokezi ya mapato yote ya Wakala wa Dawa na Vipodozi Zanzibar kwa upande wa Unguja na Pemba na kubaini kutokuainishwa kwa mapato ya Ofisi ya Pemba katika taarifa ya fedha ya mwisho wa mwaka iliyowasilishwa kwa Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali Zanzibar.

Kufanya hivyo kunapelekea taarifa za fedha za mwisho wa mwaka kutotoa sura halisi ya mapato yaliyokusanywa na Wakala kwa mwaka husika.

Ukaguzi unashauri uongozi Wakala wa Chakula, Dawa na Vipodozi Zanzibar kujumuisha mapato yote yanayokusanywa na Wakala katika taarifa za fedha za mwisho wa mwaka

### 6.7.5.2 Kuwepo kwa tofauti ya taarifa za Mapato zilizoainishwa katika taarifa za fedha ya shilingi 74,056,000

Ukaguzi umepitia taarifa za fedha za mwisho wa mwaka kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2021 iliyowasilishwa kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Zanzibar na kubaini kuwepo kwa tofauti ya fedha zilizoripotiwa katika taarifa ya mapato na matumizi (Statement of Receipts and Payments) na taarifa ya Mapato (Statement of Revenue). Kutokukubaliana kwa taarifa hizo hakutoi sura sahihi na halisi juu ya mapato yaliyokusanywa kwa mwaka husika. Mchanganuo wa mapato hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 165 : Taarifa za ukusanyaji wa Mapato zilizoainishwa katika taarifa za fedha za mwisho wa mwaka**

| Vifungu (Mapato ya Ndani) | Mwaka wa fedha 2020/2021 | |
|---|---|---|
| | Makadirio (shs) | Kilichokusanywa (shs) |
| Impotation Of Drug/Medical Devices 1422039 (2%) | 199,609,000 | 212,528,750 |
| Importation Of Cosmetics 1422039 (1%) | 30,850,000 | 11,650,000 |
| Importation Of Food 1422039 (0.5%) | 897,513,129 | 624,410,025.27 |
| Registration Of Food (1422025 (Food) | 435,815,500 | 315,825,470 |
| Registration Of Drug/Cosmetics 1422025 (Drug/Cosmetics) | 184,949,000 | 160,973,500 |
| 1422025 GMP | 200,550,000 | 30,290,000 |
| **Jumla Ndogo** | | **1,355,677,745** |
| Sub Office – Pemba | 174,991,500 | 102,287,779 |
| **Jumla Kuu (Statement of Revenue) iliyopo katika Taarifa ya hesabu** | **2,124,278,129** | **1,457,965,524** |
| **Non Tax Revenue**<br><br>**(Mapato yaliyoainishwa katika taarifa ya fedha ya mwisho wa mwaka (Statement of Receipts and Payments)** | **2,124,278,129** | **1,383,906,524.27** |
| **Tofauti** | | **74,059,000** |

Kuwepo kwa tofauti hiyo kumepelekea taarifa ya fedha kutokuwa na usahihi na kutoleta sura halisi ya mapato yaliyoripotiwa.

Ukaguzi unashauri uongozi Wakala wa Chakula, Dawa na Vipodozi Zanzibar juu ya kuweka umakini wakati wa uandaaji wa taarifa za fedha za mwisho wa mwaka ili kutoa taarifa sahihi na zenye kuleta uhalisia wa mapato yaliyokusanywa.

### 6.7.5.3 Kukosekana kwa taarifa za "Ledger" za kila kifungu cha Hesabu

Kitengo cha Uhasibu kina jukumu la kuandaa na kuweka kumbukumbu za taarifa zote za fedha zinahusiana na mapato na matumizi kwa usahihi ili kuweza kuandaa taarifa za fedha za mwisho wa mwaka zinazoendana na taratibu na miongozo inayotolewa na Taasisi za ndani na zile za kimataifa (International Accounting Standard) juu ya usahihi wa uandaaji wa taarifa za fedha za mwisho wa mwaka.

Katika kupitia taarifa mbali mbali za fedha ukaguzi umebaini kuwa kitengo cha uhasibu hakikuandaa taarifa za kila kifungu "Ledger" ili kurahisisha kuandaliwa kwa taarifa za fedha za mwisho wa mwaka zilizoendana na taratibu na miongozo inayotolewa na taasisi za ndani na za kimataifa. Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na taratibu na miongozo ya uandaaji wa taarifa za fedha za mwisho wa mwaka inayotolewa na Taasisi za ndani na zile Kimataifa (International Accounting Standard).

Kutoandaa General Ledger kutapelekea kushindwa kulinganisha taarifa za kibenki na matumizi halisi yaliyotumika.

Ukaguzi unashauri uongozi Wakala wa Chakula, Dawa na Vipodozi Zanzibar kuchukua juhudi ya kuandaa taarifa zote za kifedha kwa mujibu wa Sheria.

### 6.7.5.4 Dosari katika ukusanyaji wa Mapato

Ukaguzi umebaini kuwepo kwa dosari katika ukusanyaji wa mapato pamoja na uwekaji wa kumbukumbu za taarifa ya mapato yaliyokusanywa, dosari hizo ni kutokuwepo kwa uwiano kati ya fedha zilizokusanywa kupitia stakabadhi za mapato na fedha zilizorikodiwa katika daftari la kuweka kumbukumbu za mapato. Mchanganuo wa dosari hizo ni kama inavyoonekana katika jadweli lifuatayo:-

**Jadweli Nambari 166 : Tofauti ya taarifa za stakabadhi na daftari la kuhifadhi kumbu kumbu za mapato**

| Tarehe | Stakabadhi Namba | Mlipaji | Fedha zilizorikodiwa kwenye Stakabadhi (Tshs.) | Fedha zilizorikodiwa kwenye Daftari la kumbukumbu za mapato (Tshs.) | Tofauti (Tshs.) |
|---|---|---|---:|---:|---:|
| 14/10/2020 | 12353 | Kigongo | 18,000 | 13,000 | (5,000) |
| 17/10/2020 | 12355 | Rashid Dosa | 44,000 | 40,000 | (4,000) |
| 17/10/2020 | 12356 | Senga | 20,000 | 24,0000 | (4,000) |
| 25/10/2020 | 12363 | Rashid Dosa | 34,000 | 30,000 | (4,000) |
| 26/10/2020 | 12364 | Makame Kasa | 8,000 | 4,000 | (4,000) |
| 16/10/2020 | 12365 | Nahoda Makame | 18,000 | 13,000 | (5,000) |
| 07/12/2020 | 12372 | Makame Kasa | 18,000 | 13,000 | (5,000) |
| 09/11/2020 | 12374 | Denge | 34,000 | 30,000 | (4,000) |
| 10/11/2020 | 12375 | Rashid Dosa | 28,000 | 25,000 | (3,000) |
| 10/11/2020 | 12376 | Hamad Khalfani | 28,000 | 25,000 | (3,000) |
| 27/12/2020 | 13724 | Abuubakar Ali | 18,000 | 14,000 | (4,000) |
| 14/12/2020 | 12430 | Suleiman Nassor | 10,000 | 16,000 | 6,000 |

| Tarehe | Stakabadhi Namba | Mlipaji | Fedha zilizorikodiwa kwenye Stakabadhi (Tshs.) | Fedha zilizorikodiwa kwenye Daftari la kumbukumbu za mapato (Tshs.) | Tofauti (Tshs.) |
|---|---|---|---|---|---|
| 31/05/2021 | 16581 | Mohammed Said | 26,000 | 25,000 | (1,000) |
| 15/12/2020 | 13601 | Mahmoud Juma | 2,000 | 7,000 | 5,000 |
| 13/07/2020 | 08867 | Royal Cosmetics | 400,000 | 44,000 | (356,000) |
| 13/07/2020 | 08868 | Kauthar Sea Food Limited | 558,900 | 585,000 | (26,100) |
| 16/07/2020 | 08892 | BF Suma Limited | 95,000 | 75,000 | (20,000) |
| 4/8/2020 | 10184 | C.tren | 95,000 | 5,000 | (90,000) |
| 20/8/2020 | 10459 | Jabu Ali Suleiman | 75,000 | 95,000 | 20,000 |
| 26/8/2020 | 10493 | The medi life co.ltd | 95,000 | 15,000 | (80,000) |
| 14/9/2020 | 10427 | Scotch store | 431,517 | 44,343 | (387,174) |
| 19/9/2020 | 10659 | Mahmoud Juma | 4,000 | 8,000 | 4,000 |
| **Jumla** | | | | | **(970,274)** |

Kufanya hivyo kunapelekea upotevu wa Mapato ya Serikali pamoja na kutojua usahihi wa mapato yaliyopokelewa jambo ambalo ni kwenda kinyume na kifungu namba 23(4) cha Kanuni ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2021.

Ukaguzi unashauri uongozi Wakala wa Chakula, Dawa na Vipodozi Zanzibar kuchukuwa jitihada za udhibiti wa mapato katika maeneo ya machinjio kwa kutumia risiti ya kimtandao (EFD) ili kurahisishwa udhibiti wa mapato hayo kwani ukusanyaji wake ni wa muda wa usiku.

### 6.7.5.5 Ucheleweshaji wa upelekaji wa Mapato benki shilingi 18,085,000

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba kuna ucheleweshaji mkubwa wa uwasilishwaji wa mapato yanayokusanywa na Wakala katika Maeneo ya Machinjio ambapo mapato hayo yanakusanywa na **Afisa Afya** kutoka Wakala na kuwasilisha kwa Muhasibu kwa ajili ya kupelekwa benki.

Aidha, Ukaguzi umeshindwa kujiridhisha juu ya muda na usahihi wa mapato yanayopokelewa na kupelekwa benki kama yanavyokusanywa kutoka vituoni, hii ni kutokana na kutokuwepo kwa taarifa sahihi za upokeaji na upelekaji wa mapato hayo Benki.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016. Mapato yenyewe ni kama yanavyoonekana katika jadweli lifuatalo:-

**Jadweli Nambari 167 : Baadhi ya Mapato ambayo yamecheleweshwa kupelekwa benki**

| Tarehe ya Makusanyo | Risiti Namba | Thamani (Shs) |
|---|---|---|
| 05/08/2020 – 17/08/2020 | 10301 – 10321 | 238,000 |
| 18/08/2020 – 31/08/2020 | 10322 – 10341 | 338,000 |
| 01/09/2020 – 13/09/2020 | 10342 – 10350 | 392,000 |
| 15/12/2020 – 31/12/2020 | 13601 – 13614 | 22,000 |
| 31/12/2020 | 13615 | 12,000 |
| 8/1/2021 – 15/1/2021 | 13616 - 13625 | 20,000 |
| 25/1/2021 - 31/1/2020 | 13626 – 13631 | 12,000 |
| 31/1/2021 -31/1/2021 | 13632 - 13637 | 26,000 |
| 9/2/2021 - 14/2/2021 | 13638 - 13646 | 30,000 |
| 19/2/2021 - 28/2/2021 | 13647 - 13650 | 24,0000 |
| 7/2/2021 - 28/2/2021 | 15701 - 15722 | 338,000 |
| 1/3/2021 - 8/3/2021 | 15723 - 15730 | 150,000 |
| 9/3/2021 - 28/3/2021 | 15731 -15750 | 322,000 |
| 13/6/2021 - 24/3/2021 | 16651 -16671 | 403,000 |

| Tarehe ya Makusanyo | Risiti Namba | Thamani (Shs) |
|---|---|---|
| 25/6/2021 - 6/7/2021 | 16672 - 16693 | 434,000 |
| 16/12021 - 29/1/2021 | 15601 - 15618 | 537,000 |
| 30/1/2021 - 12/2/2021 | 15619 - 15642 | 550,000 |
| 13/2/2021 - 19/2/2021 | 15643 15650 | 324,000 |
| 17/12/2020 - 30/12/2020 | 13651 - 13663 | 278,000 |
| 2/1/2021 - 8/1/2021 | 13664 - 13671 | 186,000 |
| 9/1/2021 - 24/1/2021 | 13672 -13687 | 306,000 |
| 28/1/2021 - 31/1/2021 | 13688 - 13694 | 136,000 |
| 31/1/2021 - 6/2 /2021 | 13695 - 13700 | 118,000 |
| 18/8/2020 - 18/8/2020 | 09051 - 09061 | 204,000 |
| 25/8/2020 - 25/8/2020 | 09062 - 09069 | 252,000 |
| 31/8/2020 - 31/8/2020 | 09070 - 09077 | 220,000 |
| 3/9/2020 - 7/9/2020 | 09078 - 09087 | 304,000 |
| 14/9/2020 - 14/9/2020 | 09088 - 09096 | 260,000 |
| 16/9/2020 - 16/9/2020 | 09097 - 09099 | 38,000 |
| 6/1/2021 | 15501 | 70,000 |
| 7/1/2021 - 11/1/2021 | 15502 - 15505 | 140,000 |
| 13/1/2021 - 15/1/2021 | 15506 - 15509 | 120,000 |
| 16/1/2021 - 21/1/2021 | 15510 - 15515 | 195,000 |
| 21/1/2021 - 29/1/2021 | 15516 - 15521 | 224,0000 |
| 30/1/2021 - 31/1/2021 | 15522 - 15523 | 104,000 |
| 2/2/2021 - 3/2/2021 | 15524 – 15525 | 136,000 |
| 4/2/2021 - 10/2/2021 | 15526 -15531 | 242,000 |
| 11/2/2021 - 19/2/2021 | 15532 - 15540 | 356,000 |
| 20/2/2021 - 23/2/2021 | 15541 - 15544 | 98,000 |
| 24/2/2021 - 25/2/2021 | 15545 - 15549 | 228,000 |
| 1/3/2021 | 15550 | 50,000 |
| 21/10/2020 - 31/10 /2020 | 12451 - 12457 | 264,000 |
| 2/11/2020 - 3/11/2020 | 12458 - 12461 | 210,000 |
| 13/11/2020 - 13/11/2020 | 12462 -12466 | 156,000 |
| 23/11/2020 - 23/11/2020 | 12467 - 12470 | 256,000 |
| 28/11/2020 - 23/11/2020 | 12471 - 12473 | 264,000 |
| 29/11/2020 - 2/12/2020 | 12474 - 12477 | 110,000 |
| 3/12/2020 - 6/12/2020 | 12478 - 12481 | 222,000 |
| 12/12/ 2020 - 14/12/2020 | 12482 -12485 | 258,000 |
| 16/12/2020 - 24/12/2020 | 12486 - 12490 | 308,000 |
| 23/12/2020 - 29/12/2020 | 12491 - 12495 | 292,000 |
| 30/12/2020 - 5/1/2021 | 12496 - 12500 | 212,000 |
| 24/4/2021 - 29/1/2021 | 16501 - 1604 | 238,000 |
| 30/4/2021 - 10/5/2021 | 1605 - 16515 | 656,000 |
| 11/5/2021 - 12/5/2021 | 16116 - 16517 | 360,000 |
| 13/5/2021 – 17/5/2021 | 16518 - 16522 | 398,000 |
| 18/5/2021 - 23/5/2021 | 16523 - 16529 | 130,000 |
| 24/5/2021 - 1/6/2021 | 16539 - 15638 | 431,000 |
| 2/6/2021 - 8/6/2021 | 16538 - 16544 | 410,000 |
| 9/6/2021 - 10/6/2021 | 16545 - 16546 | 80,000 |
| 11/6/2021 - 14/6/2021 | 16547 - 16550 | 240,000 |
| 15/6/2021 - 18/6/2021 | 16751 - 16755 | 218,000 |
| 12/6/2021 – 28/6/2021 | 16756 - 16766 | 406,000 |
| 29/6/2021 - 30/6/2021 | 16767 - 16768 | 94,000 |
| 3/11/2020 - 16/11/2020 | 12051 - 12520 | 372,000 |
| 17/11/2020 - 3/12/2020 | 12521 - 12537 | 446,000 |
| 4/12/2020 - 17/12/2020 | 12538 - 12550 | 385,000 |
| **Jumla** | | **18,085,000** |

Ucheleweshwaji wa mapato kupelekwa benki kwa wakati kunapelekea kujitokeza viashiria vya upotevu wa mapato ambapo mapato hayo yanaweza kutumika kinyume na utaratibu na kupelekea kuitia hasara Serikali.

Ukaguzi unashauri uongozi ni vyema kwa Idara husika kuhakikisha kwa mapato yote yanakusanywa na kwa wakati na kuwasilishwa benki katika muda muafaka ili kuepusha upotevu wa rasilimali hiyo.

### 6.7.5.6 Kukosekana kwa ripoti za mapato za kila mwezi

Kitengo cha Uhasibu kina jukumu la kuandaa ripoti za kila mwezi za makusanyo ya mapato ili kuweza kulinganisha taarifa za hesabu hizo na makusanyo yanayopelekwa benki kwa lengo la kuweka kumbukumbu za fedha na kuziwasilisha Hazina ya Serikali kama zitakavyohitajika. Kutofanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu namba 34(2) cha Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016.

Kutoandaa taarifa za mapato ya kila mwezi kunapelekea kushindwa kulinganisha taarifa za usuluhisho wa kibenki na mapato yaliyorikodiwa kwa kipindi cha mwaka wa fedha husika.

Ukaguzi unashauri uongozi Wakala wa Chakula, Dawa na Vipodozi Zanzibar kuchukuwa juhudi za kuandaa ripoti za makusanyo ya kila mwezi kwa lengo la kuweka kumbukumbu za mapato ili kupata ufanisi na uwajibikaji mzuri.

### 6.7.5.7 Kuwepo kwa mapato yaliyopokelewa nje ya Mfumo wa kieletroniki (Control Number) wa Ukusanyaji wa Mapato ya shilingi 110,961,814.27

Ukaguzi umepitia taarifa za ukusanyaji wa Mapato kwa mwaka 2020/2021 kupitia Mfumo wa kieletroniki wa upokeaji wa mapato (Control Number) unaotumiwa na Wakala wa Dawa na Vipodozi Zanzibar na kubaini kuwepo kwa jumla ya mapato ya shilingi 1,272,944,710 yaliyokusanywa kupitia mfumo huo.

Aidha ,ukaguzi umepitia taarifa za fedha za mwisho wa mwaka na kubaini kuwepo kwa mapato yatokanayo na vyanzo vya ndani yenye jumla ya shilingi 1,383,906,524.27 ambapo zinafanya kuwepo na tofauti ya shilingi 110,961,814.27 ukilinganisha na kiasi kilichopokelewa kupitia mfumo wa kieletroniki.Hata hivyo ukaguzi umebaini mapato ya shilingi 1,272,944,710 yalipaswa kurikodiwa kwenye vitabu vya kumbukumbu kwa lengo la kurahisisha usuluhisho wa kibenki jambo ambalo hadi ukaguzi unakamilika jambo hilo halikufanyika.

Ukaguzi umeshindwa kujiridhisha juu ya usahihi wa mapato hayo kutokana na kutokuwepo kwa usuluhishi (Reconciliation) baina ya mfumo wa kieletroniki na mfumo wa kawaida ambapo bado unaendelea kutumika licha ya kuwepo kwa mfumo wa kieletroniki.

Kufanya hivyo kunaweza kupelekea upotevu wa mapato kwani Mfumo wa kieletroniki bado haufanyi kazi kama inavyotakiwa.

Ukaguzi unashauri uongozi Wakala wa Chakula, Dawa na Vipodozi Zanzibar kuchukuwa jitihada za kutoa elimu kwa wafanyabishara na wajasiriamali kufanya malipo kwa kutumia mfumo wa elektroniki (Control Number) ili kuepuka kufanya malipo nje ya mfumo jambo ambalo linapelekea kutokujuulikana kima halisi cha fedha kilichopokewa na kinachoripotiwa katika hesabu za mwisho wa mwaka.

#### 6.7.5.8 Kukosekana kwa utunzaji mzuri wa taarifa za Fedha

Katika kupitia taarifa mbali mbali za Fedha za Wakala wa Chakula, Dawa na Vipodozi ukaguzi umebaini kuwepo na utunzaji usioridhisha wa kumbukumbu ya taarifa za fedha (Bank Slip) ambazo zimekuwa zikiwekwa bila ya utaratibu unaofaa kwa ajili ya utumiaji wa siku za mbele.

Kutokutunza vizuri kumbukumbu za malipo ya fedha kunapelekea kujitokeza kwa upotevu wa taarifa za fedha na hatimae kuwasilisha taarifa za mapato na matumizi ambazo haziendani na uhalisia wa ukusanyaji wa mapato hayo.

Ukaguzi unashauri uongozi Wakala wa Chakula, Dawa na Vipodozi Zanzibar kuchukuwa jitihada za kutosha katika kutunza vizuri taarifa za fedha ili kurahisisha upatikanaji wa taarifa hizo pale zinapohitajika.

#### 6.7.5.9 Kukosekana kwa mchanganuo wa vyanzo vya makusanyo ya mapato shilingi 1,383,906,524.27

Katika ukaguzi uliofanyika Wakala wa Chakula, Dawa na Vipodozi Zanzibar imewasilisha mapato yenye thamani ya shilingi 1,383,906,524.27 ambayo yamekusanywa kutoka katika vyanzo mbali mbali vya mapato, dosari iliyobainika katika ukaguzi ni kutokuoneshwa mchanganuo wa mapato kwa kila chanzo kilichokusanya mapato hayo jambo ambalo limepelekea ugumu kuweza kujua na kutathmini fedha halisi iliyokusanywa kwa kila chanzo kwamba kilifikia lengo lililokusudiwa kwa mujibu wa makadirio ya ukusanyaji wa fedha katika chanzo husika.

Kushindwa kubainisha mchanganuo wa makusanyo ya fedha kwa chanzo husika kunaweza kukapelekea kushindwa kufikia malengo ya ukusanyaji wa mapato ya taasisi kwa mujibu wa chanzo husika na hatimae kuwasilisha makadirio ya makusanyo ambayo hayaendani na uhalisia.

Ukaguzi unashauri uongozi Wakala wa Chakula, Dawa na Vipodozi Zanzibar kuchukuwa jitihada za kuhakikisha kuwa mapato yote yanayotokana na utoaji wa huduma mbali mbali zinazotolewa na Wakala yanarikodiwa kwa utaratibu uliowekwa wa kutofautisha huduma hizo na bei halisi.

#### 6.7.5.10 Kukosekana kwa Mkataba wa ununuzi wa mafuta (Framework Contract) wenye jumla ya shilingi 65,070,896.

Katika kupitia hati za malipo pamoja na taarifa mbali mbali za utendaji wa Wakala, Ukaguzi umebaini ya kwamba Wakala wa Chakula, Dawa na Vipodozi Zanzibar wananunua mafuta kutoka kwa UNITED GROUP LIMITED kwa ajili ya kuendesha shughuli zao za kila siku za Ofisi bila ya kuwa na makubaliano ya kisheria (Mkataba), kufanya manunuzi katika taasisi za serikali bila ya kuwa na makubaliano ya kisheria ni kwenda kinyume na kifungu nambari 29(m) na kifungu nambari 42(2)(b) cha Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama yanavyoonekena katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 168**: **Malipo kwa ajili ya Ununuzi wa Mafuta**

| Hati Namba | Thamani (Tshs.) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|
| 02/07 ya 14/07/2020 | 3,607,000 | United Group Limited | Ni malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa mafuta ya Afisi |
| 28/07 ya 04/07/2020 | 3,607,000 | | |
| 20/08 ya 11/08/2020 | 3,810,000 | | |
| 11/10 ya 09/10/2020 | 1,000,000 | | |
| 40/09 ya 28/09/2020 | 2,686,600 | | |
| 32/09 ya 08/09/2020 | 3,810,000 | | |
| 36/11 ya 12/11/2020 | 2,289,700 | | |
| 60/12 ya 11/12/2020 | 3,424,400 | | |
| 64/12 ya 17/12/2020 | 1,998,596 | | |
| 72/12 ya 07/01/2020 | 3,349,600 | | |
| 45/01 ya 19/01/2021 | 3,334,600 | | |
| 28/02 ya 20/05/2021 | 3,507,200 | | |
| 23/02 ya 11/02/2021 | 3,120,400 | | |
| 47/03 ya 12/03/2021 | 4,071,500 | | |
| 65/03 ya 31/03/2021 | 4,071,500 | | |
| 54/04 ya 23/04/2021 | 4,280,800 | | |
| 50/05 ya 18/05/2021 | 4,343,000 | | |
| 39/06 ya 02/06/2021 | 4,323,000 | | |
| 53/06 ya 22/06/2021 | 4,436,000 | | |
| **Jumla** | **65,070,896** | | |

Kukosekana kwa mkataba wa ununuzi wa mafuta kunaweza kuapelekea kuathiri shughuli za Wakala endapo kutatokezea kutofautiana baina ya Wakala wa Chakula, Dawa na Vipodozi Zanzibar na watoa huduma hizo muhimu.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wakala wa Chakula, Dawa na Vipodozi Zanzibar kuandaa mkataba kwa ajili ya kuepuka migogoro endapo ikijitokeza ili kuweka usawa pande zote mbili kati yao.

### 6.7.5.11 Kugawanywa kwa manunuzi ya vifaa vya Maabara yenye jumla ya shilingi 54,576,240

Kifungu nambari 42(2)(c) cha Sheria ya Manunuzi na Uondoshaji wa mali za Umma kinakataza kugawanywa kwa Manunuzi kwa lengo la kutotumia utaratibu wa ununuzi na uondoshaji wa mali za umma.

Ukaguzi umepitia hati mbali mbali za malipo yaliyofanywa na Wakala wa Chakula, Dawa na Vipodozi Zanzibar na kubaini kuwepo kwa ununuzi wa vifaa vya maabara ambapo ununuzi wa vifaa hivyo haukutumia utaratibu wa ununuzi uliowekwa kisheria

Ukaguzi umebaini kuwa Wakala wa Chakula, Dawa na Vipodozi amekuwa akifanya manunuzi mbali mbali yaliyokiuka kifungu namba 57(1) cha Kanuni ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2021 inayokataza kugawanywa kwa manunuzi. Mchanganuo wa matumizi hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 169: Ununuzi wa Vifaa vya Maabara**

| Hati Namba | Thamani (Tshs) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|
| 16/10 ya 09/10/2020 | 5,129,050 | Lab Equip Ltd | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya maabara na vitendanishi |
| 14/09 ya 15/09/2020 | 1,050,000 | | |
| 26/11 ya 25/11/2020 | 2,442,450 | | |
| 65/12 ya 17/12/2020 | 5,000,000 | | |
| 26/02 ya 16/02/2021 | 2,151,490 | | |
| 27/02 ya 16/02/2021 | 2,280,000 | | |
| 51/04 ya 12/04/2021 | 5,600,000 | | |
| 61/05 ya 27/05/2021 | 5,923,250 | | |
| 41/03 ya 02/03/2021 | 20,000,000 | Indepth Scientific Company Limited | |
| 48/06 ya 28/06/2021 | 5,000,000 | | |
| **Jumla** | **54,576,240** | | |

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 57(1) cha Kanuni ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2021.

Ukaguzi unashauri uongozi Wakala wa Chakula, Dawa na Vipodozi Zanzibar kufuata na kutekeleza kikamilifu sheria ya Manunuzi na Uondoshaji wa mali za umma pamoja na kanuni zake.

### 6.7.5.12 Kukosekana kwa Muongozo wa ulipaji wa Posho kwa wanafunzi wanaofanya kazi kwa vitendo shilingi 55,540,000

Ukaguzi umepitia ripoti na taarifa za utekelezaji, hati za malipo na kubaini jumla ya shilingi 350,000 hutumika kulipa malipo ya posho kwa mwezi kwa kila mwanafunzi anayefanya kazi kwa vitendo (Internship) katika Taasisi ya Wakala wa Chakula, Dawa na Vipodozi bila ya kuwepo kwa muongozo unaoruhusu ulipaji wa posho hilo.

Ulipwaji wa posho bila ya kuwepo kwa muongozo wa malipo hayo kunaweza kukapelekea matumizi mabaya ya fedha za umma kwa kujitokeza udanganyifu wa malipo hayo kwa kisingizio cha malipo ya wanafunzi wanaofanya kazi za vitendo (Intenship).

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria Nambari 2 ya Utumishi wa Umma ya mwaka 2011.

**Jadweli Nambari 170 : Hati za malipo zilizolipwa posho kwa wanafunzi wanaofanya kazi kwa vitendo**

| Hati Namba | Hundi Namba | Thamani (Tshs.) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 30/09 ya 30/09/2020 | 0054 | 9,100,000 | Zanzibar Food And Drugs Agency | Malipo ya fedha kwa ajili ya posho kwa wanafunzi wa intenship. |
| 16/11 ya 18/11/2020 | 0085 | 7,350,000 | | |
| 01/12 ya 02/12/2020 | 0098 | 8,050,000 | | |
| 49/12 ya 30/12/2020 | 0138 | 8,400,000 | | |
| 11/2 ya 11/2/2021 | 0183 | 4,200,000 | | |
| 01/03 ya 01/03/2021 | 0189 | 8,550,000 | | |
| 15/04 ya 12/04/2021 | 0230 | 4,900,000 | | |
| 37/05 ya 31/05/2021 | 0271 | 4,900,000 | | |
| **Jumla** | | **55,450,000** | | |

Kutokuwepo kwa muongozo huo kunapelekea kufanyika kwa matumizi ambayo siyo sahihi.

Ukaguzi unashauri uongozi Wakala wa Chakula, Dawa na Vipodozi Zanzibar kufuata Sheria, Kanuni,Miongozo na taratibu zilizopo katika kutekeleza majukumu yake ili kuleta ufanisi wa utendaji wa kazi.

**WAKALA WA CHAKULA, DAWA NA VIPODOZI – PEMBA**

### 6.7.5.13 Kutokuwepo kwa ghala la kuhifadhia bidhaa zilizokamatwa.

Wakala wa Chakula, Dawa na Vipodozi Pemba ina jukumu la kufanya ukaguzi wa Chakula, dawa na vipodozi na kukamata bidhaa ambazo zimepitiwa na muda, zimeharibika au zilizokua hazifai kwa matumizi ya binaadamu pamoja na bidhaa ambazo hazijasajiliwa.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kutokuwepo kwa ghala la kuhifadhia bidhaa hizo. Hali hii inapelekea baadhi ya bidhaa za vyakula, vipodozi na dawa zilizokamatwa kuhifadhiwa sehemu ambazo sio sahihi.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 61(5)(b)(f) cha Sheria ya uanzishwaji wa Wakala wa Chakula, Dawa na Vipodozi.

### 6.7.5.14 Kukosekana kwa kumbukumbu za mapato yatokanayo na usajili wa machinjio.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Wakala wa Chakula, Dawa na Vipodozi Pemba haina kumbukumbu sahihi zinazotokana na usajili wa machinjio ambapo imepelekea kushindwa kujua idadi ya machinjio pamoja na kiwango sahihi cha mapato kilichokusanywa,hali ambayo inaweza kujenga taswira ya kutokufahamu uhalisia wa mapato mbali mbali yatokanayo na usajili wa machinjio. Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu cha 40(1),(2) cha sheria nambari 2 ya Wakala wa Chakula, Dawa na Vipodozi ya mwaka 2006,

Aidha ni kwenda kinyume na kifungu cha 34(1) cha Sheria nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016.

### 6.7.5.15 Hati za malipo zenye vielelezo pungufu shilingi 5,782,900

Ukaguzi umebaini kwamba jumla ya shilingi 5,782,900 zimetumika kwa malipo mbali mbali ya Wakala wa Chakula, Dawa na Vipodozi Pemba lakini vielelezo husika havikuambatanishwa na hati za malipo ili kuweza kuthibitisha uhalali wa malipo hayo.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu cha 34(1) cha Sheria nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wakala wa Chakula, Dawa na Vipodozi Pemba kuhakikisha kwamba malipo yote yanayofanyika yanatakiwa kufuata utaratibu ikiwemo kuweka rikodi katika vitabu vya kumbukumbu pamoja na uwekaji wa vielelezo sahihi kulingana na malipo yaliyofanyika. Mchanganuo wa malipo yenye vielelezo pungufu ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 171 : Hati za malipo zenye vielelezo pungufu**

| Hati namba | Hundi namba | Kiasi cha fedha kilicholipwa (Tshs) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 2/07 13/07/2020 | 000195 | 120,000 | Wakala wa Chakula Dawa na Vipodozi-Pemba. | Malipo ya Fedha kwa ajili ya malipo baada ya saa za kazi. |
| 07/09 09/09/2020 | 000210 | 250,000 | | Malipo ya fedha kwa ajili ya gharama za upimaji. |
| 08/09 19/09/2020 | 000210 | 630,000 | | Malipo ya fedha kwa ajili ya uangamizaji wa mchele. |
| 08/01 25/01/2021 | 000242 | 180,000 | | Malipo ya fedha kwa ajili ya kazi maalum |
| 16/01 28/01/2021 | 000250 | 2,092,900 | | Malipo ya fedha kwa ajili ya zoezi la utekelezaji wa bidha ya mchele usiofaa kwa binadamu. |
| 02/02 04/02/2021 | 000253 | 600,000 | | Malipo ya fedha kwa ajili ya matumizi madogomadogo ya Ofisi ya ZFDA-Pemba. |
| 09/04 28/04/2021 | 000293 | 250,000 | | Malipo ya fedha kwa ajili ya Mafunzo. |
| 15/04 30/04/2021 | 000299 | 1,660,000 | | Malipo ya fedha kwa ajili ya uangamizaji wa mchele. |
| **Jumla** | | **5,782,900** | | |

### 6.7.5.16 Ucheleweshwaji wa Upelekaji Mapato Benki shilingi 39,339,540

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba jumla ya shilingi 39,339,540 zimakusanywa na Wakala wa Chakula, Dawa na Vipodozi kwa kupitia vianzio vyake mbali mbali lakini mapato hayo yamecheleweshwa kupelekwa benki hali ambayo inaweza kupelekea upotevu wa fedha zilizokusanywa na kushindwa kutoa huduma bora zilizokusudiwa kwa wananchi na hivyo kupelekea ukosekanaji wa tija iliyokusudiwa na Serikali **Kiambatisho Nambari 8 Kinahusika.**

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 56(2) cha Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa fedha za Umma ya mwaka 2016.

## 6.8 WIZARA YA UTALII NA MAMBO YA KALE

### 6.8.1 FUNGU J01 - WIZARA YA UTALII NA MAMBO YA KALE

Ukaguzi wa hesabu za Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale kwa mwaka wa fedha 2020/2021 umefanywa kwa mujibu wa Sheria, kanuni, taratibu pamoja na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Taarifa ya Mapato**

Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale imefanikiwa kukusanya jumla ya shilingi 40,091,222 kwa kipindi cha kuanzia Januari 2021 hadi kufikia Juni 2021 ambapo ndio kipindi kilichoanza kufanya kazi kutokana na mabadiliko yaliyotokezea ya muundo wa Wizara.

**Taarifa ya Matumizi**

Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale katika kipindi cha kuanzia mwezi wa Januari 2021 hadi Juni 2021 ilikadiriwa kutumia jumla ya shilingi 4,645,374,986 ambapo shilingi 1,127,690,320 kwa ajili ya mishahara, shilingi 1,228,056,423 kwa ajili ya matumizi mengineyo, shilingi 1,695,003,094 kwa ajili ya kazi za maendeleo na shilingi 594,625,149 ikiwa ni ruzuku.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 jumla ya shilingi 1,759,867,480 zimeingizwa na kutumika sawa na asilimia 38 ya makadirio. Kati ya fedha hizo jumla ya shilingi 983,186,585 zimeingizwa na kutumika kwa mishahara sawa na asilimia 87.2 ya makadirio, shilingi 352,852,000 zimetumika kwa matumizi mengineyo sawa na silimia 29 ya makadirio, shilingi 165,000,000 zimeingizwa na kutumika kwa kazi za maendeleo sawa na asilimia 10 ya makadirio pamoja na shilingi 258,828,895 zimeingizwa na kutumika ikiwa ni ruzuku kwa taasisi zilizopo chini ya Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale ambapo ni sawa na asilimia 44 ya makadirio.

**WIZARA YA UTALII NA MAMBO YA KALE – PEMBA**

**MATOKEO NA MAPENDEKEZO YA UKAGUZI**

### 6.8.1.1 Kutokuthibitishwa kazini kwa watumishi waliomaliza muda wa majaribio

Kwa mujibu wa kanuni ya Utumishi wa Umma kifungu nambari 9(1) Bila ya kuathiri kifungu cha 60 cha Sheria ya Ajira, Namba 11 ya 2005, mtumishi yeyote ambae ameajiriwa kwa mara ya kwanza atalazimika kuwemo katika majaribio ya utumishi kwa muda wa miezi kumi na mbili kuanzia tarehe ya kuajiriwa. Aidha Kanuni ya Utumishi wa Umma ya mwaka 2014 kifungu nambari 9(2) kinamtaka Mtumishi wa Umma aliyemaliza muda wa majaribio kuthibitishwa kazini.

Ukaguzi umebaini kwamba pamoja na matakwa ya Kanuni ya Utumishi wa Umma ya Zanzibar ya mwaka 2011, Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale Pemba imeshindwa kuwathibitisha watumishi ambao wamemaliza muda wa majaribio jambo ambalo linapelekea kuwakosesha haki zao za msingi ikiwemo kupata nafasi za mikopo, kupata nafasi za masomo pamoja na kupandishwa madaraja. Mchanganuo wa watumishi hao ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 172 : Watumishi waliomaliza muda wa majaribio ambao hawajathibitishwa kazini**

| Namba | Jina la Mtumishi | Tarehe ya kuajiriwa |
|---|---|---|
| 1. | Khamis Khatib Faki | 02/03/2019 |
| 2. | Mussa Said Khamis | 02/03/2019 |
| 3. | Thureya Ghalib Moh'd | 02/09/2019 |
| 4. | Juma Seif Haji | 02/09/2019 |
| 5. | Amour Seif Amour | 02/09/2019 |
| 6. | Asma Khamis Ali | 02/09/2019 |
| 7. | Omar Daud Omar | 02/09/2019 |
| 8. | Khamis Mzee Ali | 02/05/2019 |
| 9. | Khalid Kombo Khamis | 02/03/2019 |
| 10. | Khairiya Moh'd Abdul-kadir | 02/03/2019 |
| 11. | Rabia Shaali Mwadini | 02/03/2019 |
| 12. | Saleh Juma Omar | 02/03/2019 |

### 6.8.2 FUNGU J 02 - KAMISHENI YA UTALII

Ukaguzi wa hesabu za Kamisheni ya Utalii Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2020/2021 umefanywa kwa mujibu wa Sheria, kanuni, taratibu pamoja na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Taarifa ya Mapato**

Kamisheni ya Utalii Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ilikadiriwa kukusanya jumla ya shilingi 5,492,029,000. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2020 Kamisheni ya Utalii ilikusanya jumla ya shilingi 3,581,898,480 sawa na asilimia 69.21 ya makadirio.

**Taarifa ya Matumizi**

Kamisheni ya Utalii Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ilikadiriwa kutumia jumla ya shilingi 4,115,300,000. Kati ya fedha hizo jumla ya shilingi 791,127,650 kwa ajili ya mishahara, shilingi 1,324,172,350 kwa ajili ya kazi za kawaida na shilingi 2,000,000,000 kwa ajili ya kazi za maendeleo.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 jumla ya shilingi 1,504,485,851 ziliingizwa na kutumika sawa na asilimia 37 ya makadirio. Kati ya hizo shilingi 720,412,705 ni kwa ajili ya Mishahara sawa na asilimia 91 ya makadirio, shilingi 422,000,575 ziliingizwa na kutumika kwa matumizi ya kazi za kawaida sawa na aslilimia 32 ya makadirio na jumla ya shilingi 362,072,571 ziliingizwa nakutumika kwa kazi za maendeleo sawa na asilimia 18 ya makadirio.

**MATOKEO NA MAPENDEKEZO YA UKAGUZI**

#### 6.8.2.1 Dosari iliyobainika katika majengo ya kamisheni ya utalii yaliopo Bungi yaliyojengwa kwa thamani ya shilingi 1,219,146,244.36

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Kamisheni ya Utalii imeingia mkataba wa makubaliano wa mradi wa Utalii kwa wote (Bikhole Intergrated Recreation Center) katika mwezi wa Aprili 2019, kwa kipindi cha miezi sita (6) kwa awamu ya kwanza ambapo mradi huu ulikuwa wa awamu tatu.

Awamu ya kwanza (Phase 1) ilikuwa ni ujenzi wa eneo la maegesho ya magari, bustani, vyoo, maduka ya kutoa huduma za vyakula na umeme ambapo jumla ya shilingi 1,219,146,244.36 zilitumika. Ufadhili wa ujenzi huu Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa asilimia 100 kutoka katika bajeti ya mwaka wa fedha 2018/2019 na 2019/2020.

Katika ufuatiliaji imebaika kuwa jumla ya shilingi 996,304,625.36 zimelipwa kwa mkandarasi pamoja na VAT, jumla ya shilingi 31,875,000 Wakala wa Barabara kwa ajili ya ujenzi wa barabara pamoja na shilingi 46,134,029 zimelipwa Shirika la Umeme. Dosari iliyobainika na ukaguzi ni kutotumika kwa majengo hayo (kutelekezwa) kwa muda mrefu, aidha kwa fedha iliyotumika kwa ajili ya ujenzi wa barabara haiendani na hali halisi ya ujenzi uliofanyika (hauridhishi).

Kufanya hivyo kunapelekea uwepo wa viashiria vya matumizi mabaya ya fedha za Serikali ambapo ni kwenda kinyume na Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Kamisheni ya Utalii kuhakikisha kwamba unasimamia na kutekeleza mipango yote iliyokusudiwa kwa ufanisi mkubwa na kuendeleza shughuli iliyopangwa kwa maslahi ya wananchi na Taifa kwa ujumla ambapo Sheria, Kanuni na miongozo mbali mbali iliyopo zinatumika ipaswavyo ili kuepusha uwezekano wa kutokezea viashiria vya ubadhirifu wa fedha na mali za Umma.

### 6.8.2.2 Vifaa ambavyo havikurikodiwa katika daftari la kutunzia vifaa vya ghalani shilingi 35,802,911

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwa jumla ya shilingi 35,802,911 zimetumika kwa ajili ya ununuzi wa vifaa mbali mbali lakini dosari iliyobainika ni kutokurikodiwa kwa vifaa hivyo katika daftari la kutunzia vifaa ghalani ili kuweza kuthibitisha uhalali wa mapokezi na matumizi ya vifaa hivyo.

Kufanya hivyo kunaweza kupelekea kutokujulikana kwa matumizi ya vifaa husika pamoja na kupelekea upotevu wa vifaa vilivyonunuliwa ambapo ni kwenda kinyume na Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016. Mchanganuo wa vifaa hivyo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 173 : Vifaa ambavyo havikurikodiwa katika daftari la kutunzia vifaa vya ghalani**

| Hati namba | Ankara | Aliyelipwa | Maelezo | Kiasi cha fedha kilicholipwa (Tshs) |
|---|---|---|---|---|
| 2/9 ya 1/9/2020 | Tax/Invoice 028 ya 1/7/2020<br>Rpts 519 ya 10/07/2020 | Seven Enterprises | Ikiwa ni malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa Camera na vifaa vyake | 8,175,160.00 |
| 1/9 ya 1/9/2020 | ZCQAR09A ya 21/07/2020. | Zanzibar Connection Co. Ltd., | Ikiwa ni malipo ya gharama za ununuzi wa vifaa vya huduma ya Internet. | 1,586,250.00 |
| 2/10 ya 1/10/2020 | P/Invoice ……<br>Rpts 316 ya 02/10/2020. | Aritech Security Ltd | Malipo kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya vitambulisho vya Wafanyakazi wa ZCT | 2,746,578.00 |
| 03/10 ya 1/10/2020. | P/Invoice 218 na 219 ya 20/6/2020 Rpts Nill | Mwananchi Supply Store | Malipo kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya matengenezo ya umeme. | 1.159,732.00 |
| 4/10 ya 8/10/2020 | T/invoice 4052 ya 9/6/2020. P/Invoice 4433. Rpts 9/10/2020. | Miembeni Lubricants Center | Malipo kwa ajili ya ya kufanya services gari ya Kamisheni ya Utalii. | 1,437,307.00 |
| 354/2 ya 15/2/2021. | P/invoice 082 ya 8/1/2021. Rpts 265 ya 15/02/2021. | Melisha Media Production | Ikiwa ni fedha kwa ajili ya malipo ya ununuzi wa wino wa kuchapia Leseni. | 6,615,000.00 |
| 5/2 ya 15/02/2021. | P/Invoce 464 ya 28/1/2021. Rpts 285 ya 15/2/2021. T/invoice 286 ya 27/8/2020. | Zan Printing | Malip kwa ajili ya ununuzi wa stationary | 880,000.00<br>3,697,834.00 |
| 9/3 ya 10/03/2021 | T/Invoice 2086 ya 10/3/2021. Rpts 007 ya 25/3/2021. | Mashal Printing Solution. | Malipo kwa ajili ya gharama za ununuzi wa wino na cards za kurikodia wageni | 9,505,050.00 |
| **Jumla** | | | | **35,802,911.00** |

## 6.9 WIZARA YA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI, NA MICHEZO

### 6.9.1 FUNGU NAMBA J 03 - WIZARA YA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO

Ukaguzi wa hesabu za Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kwa mwaka wa fedha 2020/2021 umefanywa kwa kuzingatia misingi, taratibu na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Taarifa ya Matumizi**

Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ilikadiriwa kutumia jumla ya shilingi 2,552,682,312 kwa ajili ya matumizi ya Mishahara, jumla ya shilingi 5,287,795,997 kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida na jumla ya shilingi 9,369,687,170 kwa ajili ya kazi za maendeleo.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 jumla ya shillingi 1,6,00,049,170 ziliingizwa kwa ajili ya matumizi ya Mishara sawa na asilimia 63 ya makadirio, jumla ya shilingi 360,816,000 ziliingizwa kwa ajili ya matumizi ya kazi ya kawaida sawa na asilimia 7 ya makadirio na jumla ya shilingi 193,187,909 ziliingizwa kwa ajili ya kazi za maendeleo sawa na asilimia 2 ya makadirio.

**MATOKEO NA MAPENDEKEZO YA UKAGUZI**

#### 6.9.1.1 Kukosekana kwa daftari la usaili wa mikataba (Contract registrar)

Ukaguzi umepitia hati mbali mbali na kubaini kwamba Wizara ya Vijana, Utamaduni na michezo imefunga mikataba jumla ya shilingi 1,582,259,511 kwa mwaka 2020/2021 kupitia shughuli zake za miradi ya Maendeleo lakini mikataba hiyo haijarekodiwa katika daftari maalum la mikataba.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016.

Kutorikodiwa Kwa mikataba katika daftari maalum kunapelekea Mkaguzi kushindwa kujirizisha juu ya mikataba yote iliofungwa na wizara.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wizara uhakikishe mikataba yote inayofungwa na Wizara kurikodiwa na kuwekewa kumbukumbu zake katika Daftari Maalum.

#### 6.9.1.2 Dosari zilizobainika katika ununuzi wa Taa za Uwanja wa Amani shilingi 270,280,000

Ukaguzi umepitia mikataba na hati mbali mbali na kubani kua Wizara ya Vijana, Utamaduni na michezo imetumia jumla ya Dola za Kimarekani USD 119,000 ambazo ni sawa na shilingi 270,280,000 katika ununuzi wa taa kutoka kampuni ya HONG KONG LIGHT TECHNOLOGY kwa ajili ya kiwanja cha Amani.

Dosari iliyobainika katika ukaguzi ni kutotangazwa kwa zabuni ya wazi kwa ajili ya kumpata Mkandarasi. Aidha ukaguzi haukuweza kupatiwa muhtasari wa kikao cha Bodi ya Zabuni kilichompendekeza Mzabuni huyo jambo ambalo limepelekea kushindwa kujiridhisha juu ya uhalali wa malipo hayo ambapo ni kwenda kinyume kifungu 68(1) cha Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo uhakikishe unafuata kikamilifu sheria ya Manunuzi na uondoshaji wa mali za umma nambari 11 ya mwaka 2016 wakati wa kufanya manunuzi.

#### 6.9.1.3 Dosari katika ununuzi wa PA System shilingi 84,908,050

Ukaguzi umebaini kwamba Wizara ya Vijana, Utamadunina michezo imetumia jumla ya Tsh 84,908,050 katika ununuzi wa PA System za kiwanja cha Amani kutoka kwa Kampuni ya RAKAM GENERAL SUPLY LTD.

Dosari iliyobainika katika ukaguzi ni kutotangazwa kwa zabuni ya wazi kwa ajili ya kumpata Mkandarasi. Aidha ukaguzi haukuweza kupatiwa muhtasari wa kikao cha Bodi ya Zabuni kilichompendekeza Mzabuni huyo jambo ambalo limepelekea kushindwa kujiridhisha juu ya uhalali wa malipo hayo ambapo ni kwenda kinyume kifungu 68(1) cha Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo uhakikishe unafuata kikamilifu sheria ya Manunuzi na uondoshaji wa mali za umma nambari 11 ya mwaka 2016 wakati wa kufanya manunuzi.

#### 6.9.1.4 Mapungufu katika Ufungwaji wa mkataba wa ujenzi wa Uwanja wa Mkokotoni shilingi 205,750,000

Ukaguzi umetembelea miradi ya uimarishaji wa viwanja na kutambua kua mnamo mwaka 2020 Wizara iliingia makubaliano ya kimkataba baina ya Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi akiwa ni mkandarasi na Wakala wa Majengo (ZBA) akiwa ni mshauri elekezi wa ujenzi wa kiwanja cha Michezo cha mpira wa miguu na (Multiplay ground) ikijumuisha kiwanja cha, Net ball, Volley ball na Hand ball na Basket ball wenye thamani ya shilingi 205,750,000. Dosari iliyobainika katika ukaguzi ni kutokukamilika kwa mradi wa ujenzi huo kunakotokana na kukosekana kwa tathmini nzuri ya upembuzi yakinifu juu ya utekelezaji wa mradi huo jambo ambalo limepelekea kukosekana kwa tija ya mradi huo.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wizara kuongeza umakini katika kusimamia miradi ya maendeleo ikiwa ni pamoja na kufanyika kwa upembuzi yakinifu kabla ya utekelezaji wa mradi ili kuepusha athari inayoweza kujitokeza.

#### 6.9.1.5 Dosari iliyobainika katika utekelezaji wa maamuzi ya ugawaji wa vifaa shilingi 388,987,000

Ukaguzi umetembelea miradi ya maendeleo ya ajira kwa vijana na kubaini kuwa Wizara ilinunua vifaa vya uchongaji na uchomaji tarehe 27/5/2020 kwa thamani ya shilingi 388,987,000 kwa ajili ya vijana wa Wilaya zote za Unguja na Pemba kwa lengo la kujiajiri na kujikwamua na ugumu wa maisha. Dosari iliyobainika katika ukaguzi ni kutokugaiwa kwa vifaa ivyo katika Wilaya ya Mjini na kupelekea kuendelea kuhifadhiwa katika ghala la Wilaya ya Mjini jambo ambalo linapelekea kukosekana kwa malengo ya kuondoshea ugumu wa maisha vijana hao.

Aidha, ukaguzi umebaini kwa upande wa Wilaya zote za Unguja na Pemba baadhi ya vifaa hivyo tayari vimeshakabidhiwa kwa walengwa na kuwanufanisha kwa malengo yaliyokusudiwa.

Kutokugawiwa kwa vifaa hivyo kwa Wilaya ya Mjini bila ya kuwepo kwa maelekezo mengine ya Kiserikali yaliyotolewa kunaweza kukapelekea vifaa hivyo kuharibika au kupotea kwa kukaa kwa muda mrefu bila ya matumizi na kuisababishia hasara Serikali.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wizara kwa kushikamana na uongozi wa Wilaya ya Mjini kuhakikisha unachukuwa maamuzi ya haraka kuvigawa vifaa hivyo kwa mujibu wa malengo ya Serikali.

**BARAZA LA KISWAHILI ZANZIBAR (BAKIZA)**

### 6.9.1.6 Uwepo wa Vitabu vya mda mrefu shilingi 260, 094,000

Ukaguzi umebaini kwamba BAKIZA imechapisha Vitabu vya aina mbali mbali kwa muda mrefu bila ya uwepo wa matumizi ya vitabu hivyo ambavyo vimehifadhiwa katika chumba kilichopo Uwanja wa Amani sehemu inayotumiwa kama ofisi ya wasafishaji wa kiwanja hicho. Dosari iliyobainika katika ukaguzi ni kuhifadhiwa kwa vitabu vyenye thamani kubwa ya fedha katika sehemu ambayo haina usalama kwa uwekaji na utunzaji wa vitabu hivyo jambo ambalo linaweza kupelekea kujitokeza kwa viashiria vya upotevu wa vitabu hivyo na kupelekea kukosekana kwa malengo ya uchapishwaji wa vitabu hivyo ambavyo vimehifadhiwa kwa muda mrefu.

Kujitokeza kwa dosari hiyo kunaweza kupelekea kuisababishia hasara ya fedha za umma na hatimae kukosekana kwa malengo yaliyokusudiwa.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wizara kuhakikisha unasimamia kikamilifu matumizi ya fedha za umma pamoja na rasilimali zinazonunuliwa kwa lengo la kuhakikisha kunakuwa na matumizi mazuri ya rasilimali hizo. Mchanganuo wa vitabu pamoja na gharama zilizotumika kuchapisha vitabu hivyo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 174: Mchanganuo wa vitabu pamoja na gharama zilizotumika kuchapisha**

| Nam. | Wakati wa Ukaguzi | | | Bei ya kitabu | Kiasi cha fedha (Tshs) |
|---|---|---|---|---|---|
| | Vitabu vilivyoonekana | Mwaka vilivyochapishwa | Idadi ya vitabu viliyopo | | |
| 1. | Kamusi la Kiswahili Fasaha | 2010 | 12045 | 17,000 | 192,984,000 |
| 2. | Kamusi la Lahaja za Kitumbatu | 2012 | 273 | 10,000 | 3,760,000 |
| 3. | Kamus la Lahaja za Kimakunduchi | 2012 | 382 | 10,000 | 3,830,000 |
| 4. | Kamusi la Lahaja za Kipemba | 2012 | 4080 | 12,000 | 24,084,000 |
| 5. | Mawasiliano ya Msingi Kiswahili kwa Wageni | 2013 | 907 | 12,000 | 10,884,000 |
| 6 | Dr shein na Maendeleo | 2020 | 409 | 7000 | 2,996,000 |
| 7 | Jahazi no 1 | 2016 | 538 | 9,000 | 4,842,000 |
| 8 | Jahazi no 2 | 2017 | 771 | 9,000 | 6,939,000 |
| 9 | Jahazi no 3 | 2019 | 387 | 25,000 | 9,775,000 |
| | **Jumla** | | | | **295,478,000** |

**AFISI YA MSAJILI WA HAKIMILIKI (COSOZA)**

### 6.9.1.7 Kutokukusanywa kwa mapato yatokanayo na mirahaba ya hakimiliki shilingi 117,019,000 na USD 51,100

Ukaguzi umebaini kwamba Afisi ya Msajili wa hakimiliki (COSOZA) katika kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021 haikuweza kukusanya mapato yatokanayo na mirahaba ya hakimiliki yenye jumla ya shilingi 117,019,000 na USD 51,100 kutokana na watumiaji mbali mbali wa kazi za hakimiliki.

Kutokukusanywa kwa mirahaba hiyo kunapelekea kuwakosesha mapato wasanii wanaotumia nguvu na vipaji vyao katika kuhakikisha tasnia ya sanaa inakuwa na kupiga hatua kwa ajili kujiongezea vipato kutokana na kazi ya sanaa jambo amabalo linaweza kupelekea kudumaza kwa vipaji vya wasanii hao na kuwakatisha tamaa kimaisha na hatimae silka na utamaduni kwa Mzanzibari kupotea.

Ukaguzi unashauri jitihada mbali mbali ziendelee kuchukuliwa na COSOZA ili kuhakikisha mapato hayo yanakusanywa na kuwasilishwa kwa wahusika kwa lengo la kuwakwamua kimaisha.

**Jadweli Nambari 175: linaonesha Orodha ya madeni ya wadaiwa wa Mirabaha ni kama inavyoonekana**

| Hoteli zilizopelekewa ankara ambazo hazijafanya Malipo kwa mwaka 2020/2021 | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Nam.** | **Jina La Hoteli** | **Eneo** | **Wilaya** | **Ankara namba** | **Mwaka** | **Malipo kwa mwaka (USD)** |
| 1 | Konokono Beach Resort | Michamvi | Kusini | 400 | 2020-2021 | 1200 |
| 2 | Matlai | Michamvi | Kusini | 443 | 2020-2021 | 1200 |
| 3 | Baladin | Michamvi | Kusini | 444 | 2020-2021 | 1200 |
| 4 | Dongwe Club (Vacanze) | Michamvi | Kusini | 447 | 2020-2021 | 1200 |
| 5 | Baraza Resort And Spa Zanzibar | Michamvi | Kusini | 449 | 2020-2021 | 1200 |
| 6 | The Palm Zanzibar | Michamvi | Kusini | 450 | 2020-2021 | 1200 |
| 7 | Zawadi Hotel Zanzibar | Michamvi | Kusini | 451 | 2020-2021 | 1200 |
| 8 | Breezes Beach Club And Spa Zanzibar | Michamvi | Kusini | 448 | 2020-2021 | 1200 |
| 9 | Michamvi Sunset Bay Zanzibar | Michamvi | Kusini | 399 | 2020-2021 | 1200 |
| 10 | Fruits And Spice Wellness Resort | Mchangamule | Kusini | 417 | 2020-2021 | 1200 |
| 11 | Villa Kiva | Nungwi | Kaskazini | 390 | 2020-2021 | 1200 |
| 12 | Zanzibar Magic Hotel | Nungwi | Kaskazini A | 391 | 2020-2021 | 1200 |
| 13 | Waridi Beach Resort | Pwani Mchangani | Kaskazini A | 392 | 2020-2021 | 1200 |
| 14 | Tatu Restaurent | Forodhani | Mjini | 404 | 2020-2021 | 350 |
| 15 | Dhow Palace Hotel | Shangani | Mjini | 406 | 2020-2021 | 1200 |
| 16 | Spice And Antonio | Shangani | Mjini | 409 | 2020-2021 | 1200 |
| 17 | African House Hotel | Shangani | Mjini | 407 | 2020-2021 | 1200 |
| 18 | Tausi | Shangani | Mjini | 408 | 2020-2021 | 1200 |
| 19 | Amani Kendwa Hotel | Kiwegwa | Kaskazini B | 355 | 2020-2021 | 1200 |
| 20 | Gold Zanzibar | Kiwegwa | Kaskazini B | 356 | 2020-2021 | 1200 |
| 21 | Kendwa Rock Hotel | Kiwegwa | Kaskazini B | 357 | 2020-2021 | 1200 |

| Hoteli zilizopelekewa ankara ambazo hazijafanya Malipo kwa mwaka 2020/2021 | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Nam.** | **Jina La Hoteli** | **Eneo** | **Wilaya** | **Ankara namba** | **Mwaka** | **Malipo kwa mwaka (USD)** |
| 22 | Zuri Hotel | Nungwi | Kaskazini A | 363 | 2020-2021 | 1200 |
| 23 | The Royal Zanzibar | Nungwi | Kaskazini A | 366 | 2020-2021 | 1200 |
| 24 | New My Blue Hotel | Nungwi | Kaskazini A | 367 | 2020-2021 | 1200 |
| 25 | Vera Club Sunset Beach | Nungwi | Kaskazin A | 368 | 2020-2021 | 1200 |
| 26 | Away Hotel Zanzibar | Nungwi | Kaskazin A | 369 | 2020-2021 | 1200 |
| 27 | Double Tree By Hilton | Nungwi | Kaskazin A | 370 | 2020-2021 | 1200 |
| 28 | Essque Zalu | Nungwi | Kaskazini A | 372 | 2020-2021 | 1200 |
| 29 | Mnarani Beach Resort | Nungwi | Kaskazini A | 380 | 2020-2021 | 1200 |
| 30 | Bravo(Voi) Hotels | Kiwengwa | Kaskazini A | 381 | 2020-2021 | 1200 |
| 31 | Vera Club | Kiwengwa | Kaskazini B | 382 | 2020-2021 | 1200 |
| 32 | Zan View | Kiwengwa | Kaskazini B | 385 | 2020-2021 | 1200 |
| 33 | Sea Cresi | Kiwengwa | Kaskazini B | 386 | 2020-2021 | 1200 |
| 34 | Coral Reef | Pwani Mchangani | Kaskazini A | 388 | 2020-2021 | 1200 |
| 35 | Plan Hotel | Pwani Mchangani | Kaskazini A | 389 | 2020-2021 | 1200 |
| 36 | Villa Serenity | Jambiani | Kusini | 427 | 2020-2021 | 350 |
| 37 | Blue Oyster Hotel | Jambiani | Kusini | 429 | 2020-2021 | 1200 |
| 38 | Kisiwa On The Beach | Jambiani | Kusini | 415 | 2020-2021 | 1200 |
| 39 | The White Front | Paje | Kusini | 412 | 2020-2021 | 1200 |
| 40 | Nur Beach Hotel | Jambiani | Kusini | 434 | 2020-2021 | 1200 |
| 41 | New Teddy On The Beach | Jambiani | Kusini | 435 | 2020-2021 | 1200 |
| 42 | Jambiani White Sands Ban-galoo | Jambiani | Kusini | 436 | 2020-2021 | 1200 |
| 43 | Upendo Hotel | Michamvi | Kusini | 445 | 2020-2021 | 1200 |
| 44 | Lemersenne Beach Resort (Jumeirah Holding Ltd) | Michamvi | Kusini | 446 | 2020-2021 | 1200 |
| **Jumla** | | | | | | **$51,100** |

**IDARA YA MICHEZO: UWANJA WA AMANI/MAO-AKAUNTI NAM. 0404256000**

### 6.9.1.8 Madeni ya kodi ambayo hayajalipwa shilingi 16,350,000

Kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ukaguzi umebaini Uwanja wa Amani umekodisha vyumba kwa taasisi za Serikali na binafsi kwa thamani ya shilingi 16,350,000. Dosari iliyobainika katika ukaguzi ni kukosekana kwa mapato hayo kutokana na kutokuwa na usimamizi imara wa kuweza kufanya ufuatiliaji wa madeni yanayodaiwa kwa taasisi hizo.

Kukosekana kwa sera imara za ufuatiliaji wa madeni ikiwemo kutoza tozo ya ziada kwa taasisi zitakazobainika zimeshindwa kulipa deni lake kwa wakati kunaweza kupelekea kukwamisha mipango ya shughuli za Uwanja wa Amani kutekelezeka kama ilivyokusudiwa na hatimae kukosekana kwa tija inayotokana na ukodishwaji wa vyumba hivyo.

Ukaguzi unashauri jitihada mbali mbali ziendelee kuchukuliwa na uongozi wa Uwanja wa Amaan ili kuhakikisha mapato yanayotokana na ukodishwaji wa vyumba yanakusanywa na kuwasilishwa katika hesabu husika kwa lengo la kuweza kupangiwa matumizi yatokanayona na kuendeleza huduma za viwanja.

**Jadweli Nambari 176 : Orodha ya madeni yanayodaiwa kwa taasisi za Serikali na Binafsi**

| Namba | Jina la Mdaiwa | Maelezo ya Deni | Kiasi cha Deni (Tshs) |
|---|---|---|---|
| 1. | ZABESA | Ikiwa ni deni la Kodi ya Ofisi Uwanja wa Amaan. | 600,000 |
| 2. | IKULU | | 900,000 |
| 3. | RIADHA | | 450,000 |
| 4. | ZFF | | 14,400,000 |
| **Jumla** | | | **16,350,000** |

### 6.9.1.9 Limbikizo la deni la Umeme katika Uwanja wa Amani shilingi 49,440,975

Kwa mujibu wa barua ya yenye kumbukumbu namba ZECO/CONF.2/8/VOL3/667 ya tarehe 04 Juni 2021 inayobainisha uwepo wa deni la umeme lenye thamani ya shilingi 49,440,975 linalodaiwa na Shirika la Umeme la Zanzibar (ZECO) kwa ajili ya huduma za matumizi ya umeme katika Uwanja wa Amaan.

Dosari iliyobainika katika ukaguzi ni kujitokeza kwa matumizi ya ziada ya umeme yanayoendelea kutumiwa bila ya uwepo wa jitihada zinazochukuiwa kupunguza madeni ya awali jambo ambalo linaweza kupelekea deni hilo kuendelea kuongezeka mara dufu na hatimae kutokuweza kulipika na kusababisha kusitishwa kwa huduma hiyo.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Uwanja wa Amani kuchukua jitihada za makusudi katika kuweka mkakati wa ulipaji wa deni hilo ili kujipunguzia mzigo wa deni ambalo halitaweza kulipika kwa haraka.

### 6.9.1.10 Udhaifu katika ukusanyaji wa mapato shilingi 28,075,220

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika jumla ya shilingi 28,075,220 zimekusanywa ikiwa ni mapato yatokanayo na ada ya uwanja wa Amaan. Dosari iliyobainika katika ukaguzi ni kukosekana kwa muongozo ambao ungeweza kutumika katika kuongea ufanisi wa ukusanyaji wa mapato yatokanayo na ada ya uwanja pamoja na kusaidia mbinu za uibuaji wa vyanzo vipya vya mapato vitokanavyo na uwepo wa matumizi ya uwanja huo.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Idara ya Usimamizi wa Uwanja wa Amaan kuweka mipango imara na mikakati itakayosaidia kujiongezea mapato yatokanayo na matumizi ya uwanja ikiwemo kubuni michezo ya aina mbali mbali kwa wanafunzi, vijana, wasanii, ngoma za utamaduni, halaiki, mabonanza ya michezo, vikundi vya mazoezi ambavyo watatumia eneo la uwanja wa amani kwa malipo ya gharama nafuu kwa lengo la kuingiza mapato ambayo yatasaidia kuudumisha na kuuhudumia uwanja pasi na kutegemea ruzuku ya uwendeshaji kutoka Serikalini.

### 6.9.1.11 Kutokuwepo kwa ufanisi wa ukusanyaji wa mapato

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika Baraza la Michezo limeweka Ada ya mwaka kwa timu zote (Vilabu) ambapo vinalazimika kulipa shilingi 10,000 kwa kila mwaka. Dosari iliyobainika ni kukosekana kwa ubunifu wa ukusanyaji wa mapato yanayoweza kupatikana kutokana na michezo mbali mbali ya utamaduni ambayo yataruhusika kuutumia uwanja kwa ajili ya kufanya maonyesho au ushindani wa michezo yao kwa kulipia gharama nafuu ili kuweza kuongeza mapato ambayo yatasaidia kusimamia shughuli zinazoendeshwa katika kutunza matumizi ya uwanja huo na kuacha kutegemea mapato pekee yatokanayo na ada za vilabu vya michezo ya mpira wa miguu pekee.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Baraza la Michezo kuhakikisha unakuwa na ubunifu wa matumizi ya viwanja vya mipira kwa lengo la kujipatia kipato ambacho kitaudumia huduma mbali mbali zinazohitajika katika viwanja hivyo ili kufikia tija ya uwepo wa viwanja hivyo.

**WIZARA YA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO - PEMBA**

### 6.9.1.12 Hati za malipo zenye vielelezo Pungufu shilingi 6,055,790

Ukaguzi umebaini kwamba jumla ya shilingi 6,055,790 zimetumika kwa malipo mbali mbali ya Wizara ya Habari Vijana Utamaduni na Michezo Pemba lakini vielelezo husika havikuambatanishwa na hati za malipo ili kuweza kuthibitisha uhalali wa malipo hayo.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na sheria za usimamizi wa fedha za umma kifungu nambari 34(1) cha Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya Zanzibar ya mwaka 2016. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 177 : Hati za Malipo zenye vielelezo Pungufu**

| Hati Namba | Hundi Namba | Kiasi cha fedha kilicholipwa (Tshs.) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 24/07<br>23/07/2020 | 016307 | 47,573 | Misufini stationery | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya kuandikia. |
| 25/07<br>23/07/2020 | 016308 | 2,167,475 | | |
| 2/8<br>3/8/2020 | 016321 | 428,157 | Moharash Restaurant | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa vinywaji |
| 35/8<br>24/8/2020 | 017405 | 152,233 | | |
| 33/8<br>24/8/2020 | 017403 | 256,894 | Vista Auto Parts | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya gari. |
| 4/9<br>31/8/2020 | 017513 | 285,437 | Misufini Stationery | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa ya vifaa vya kuandikia |
| 14/1<br>04/01/2021 | 018857 | 686,952 | | |
| 17/1<br>05/01/2021 | 018898 | 380,583 | | |
| 19/3<br>22/2/2021 | 019801 | 300,000 | WHVUM Pemba | Malipo ya fedha kwa ajili ya wa ubani kwa mfanyakazi. |
| 22/03<br>03/03/2021 | 019886 | 428,155 | Welfit Auto Spare Parts | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vifaa vya gari |
| 23/03<br>03/03/2021 | 019885 | 922,331 | Chake chake Youth Company | Malipo ya fedha kwa ajili ya huduma ya usafi |
| **Jumla** | | **6,055,790** | | |

#### 6.9.1.13 Malimbikizo ya madeni ya muda mrefu shilingi 19,600,450

Katika Ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Wizara ya Habari Vijana Utamaduni na Michezo Pemba inadaiwa madeni ya muda mrefu na Taasisi za Serikali, Wafanyabiasha pamoja na Wafanyakazi wa Wizara yenye jumla ya shilingi 19,600,450 kwa ajili ya huduma mbali mbali

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016. Mchanganuo wa madeni hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 178 : Malimbikizo ya madeni ya muda mrefu**

| Namba | Jina la Taasisi | Kiasi cha fedha kinachodaiwa (Tshs) |
|---|---|---|
| 1. | Wafanyakazi wa Ofisi | 8,615,000 |
| 2. | Wafanyabiashara | 10,417,450 |
| 3. | Taasisi za Serikali | 568,000 |
| **Jumla** | | **19,600,450** |

#### 6.9.1.14 Makadirio ya ukusanyaji wa mapato kinyume na uhalisia shilingi 24,000,000

Jumla ya shilingi 24,000,000 zilikadiriwa kukusanywa na Wizara ya Habari Vijana Utamaduni na Michezo Pemba kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

Ukaguzi umebaini kwamba makadirio hayo ni madogo ukilinganisha na makusanyo halisi kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ambapo hadi kufikia 30 Juni 2021, jumla ya shilingi 30,646,900 zilikusanywa sawa na asilimia 127.7 ya makadirio.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya Zanzibar nambari 12 ya mwaka 2016 kifungu nambari 32(1) (2).

#### 6.9.1.15 Kukosekana kwa mapato yatokanayo na huduma za sanaa shilingi 44,300,000

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Wizara ya Habari Vijana Utamaduni na Michezo Pemba inawadai wateja wake jumla ya shilingi 44,300,000 zinazotokana na utoaji wa huduma za sanaa.

Hali hii inapelekea kukosekana kwa mapato yatokanayo na fedha za utoaji wa huduma za sanaa. Aidha ni kwenda kinyume na Sheria Nambari 7 ya Baraza la Sanaa, Sensa, Filamu na Utamaduni Zanzibar ya mwaka 2015. Mchanganuo wa mapato hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 179 : Mapato yaliyokosekana yanayotokana na huduma za sanaa**

| Jina la Hoteli | Muda wa Deni | Kiasi cha fedha kinachodaiwa (Tshs.) | Kiasi cha fedha kilicholipwa (Tshs.) | Deni halisi (Tshs) |
|---|---|---|---|---|
| Manter Resourt Hotel - Makangale | 2017 – 2021 | 6,500,000 | - | 6,500,000 |
| Pemba Paradise Hotel - Makangale | 2017 – 2021 | 6,500,000 | - | 6,500,000 |
| Ayyana Hotel – Makangale | 2017 – 2021 | 6,500,000 | - | 6,500,000 |
| Pemba Lodge Hotel – Shamiani Mwambe | 2017 – 2021 | 6,500,000 | - | 6,500,000 |
| Planet Sankara Hotel – Shamiani Mwambe | 2017 - 2021 | 6,500,000 | - | 6,500,000 |
| Fundu Lagon Hotel – Wambaa | 2017 - 2021 | 4,000,000 | 2,500,000 | 1,500,000 |
| Ocean view Hotel – Wesha | 2017 - 2021 | 4,500,000 | 2,000,000 | 2,500,000 |
| ZSSF Hotel – Tibirinzi | 2018 - 2021 | 5,200,000 | - | 5,200,000 |
| Ukumbi wa makonyo – Wawi | 2020 – 2021 | 2,600,000 | - | 2600,000 |
| **Jumla** | | **48,800,000** | **4,500,000** | **44,300,000** |

## 6.10 WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA AMALI

### 6.10.1 FUNGU K 01 – WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA AMALI

Ukaguzi wa hesabu za Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa mwaka wa fedha 2020/2021 umefanywa kwa mujibu wa Sheria, kanuni, taratibu pamoja na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Taarifa ya Mapato**

Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ilikadiriwa kukusanya jumla ya shilingi 215,700,000. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 Wizara ilikusanya jumla ya shilingi 141,108,343 sawa na asilimia 65 ya makadirio.

**Taarifa ya Matumizi**

Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ilikadiriwa kutumia jumla ya shilingi 140,080,860,441. Kati ya fedha hizo shilingi 19,267,400,000 zilikadiriwa kutumika kwa matumizi ya kawaida, shilingi 59,666,476,441 kwa ajili ya mshahara, shilingi 46,180,400,000 kwa ajili ya matumizi ya ruzuku kwa taasisi zilizo chini ya Wizara ya Elimu na mafunzo ya Amali, shilingi 19,116,840,400 zilikadiriwa kutumika katika Taasisi zilizo chini wa Wizara kutokana na vyanzo vyao vya mapato ya ndani. Aidha Jumla ya shilingi 4,500,000,000 zilikadiriwa kutumika kwa kazi za maendeleo ikiwa ni mchango wa Serikali na jumla ya shilingi 14,962,084,000 zilikadiriwa kutumika kwa kazi za maendeleo ikiwa ni mchango wa washirika wa maendeleo.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 jumla ya shilingi 129,891,236,818 zilitumika ikiwa sawa na asilimia 82.60 ya makadirio, kati ya fedha hizo shilingi 4,526,990,407 zilitumika kwa matumizi ya kawaida sawa na asilimia 23.50 ya makadirio, shilingi 58,469,446,248 zilitumika kwa ajili ya mshahara sawa na asilimia 109.83 ya makadirio, shilingi 30,847,082,611 zilitumika ikiwa ni Ruzuku kwa Taasisi zilizo ndani ya Wizara ya Elimu ikiwa sawa na asilimia 66.80 ya makadirio, shilingi 19,186,564,553 zilitumika katika Taasisi zilizo chini wa Wizara kutokana na vyanzo vyao vya mapato ya ndani ikiwa sawa na asilimia 100.36 ya makadirio. Aidha, shilingi 3,509,000,000 zilitumika kwa kazi za maendeleo ikiwa ni mchango wa Serikali sawa na asilimia 77.98 ya makadirio na shilingi 13,352,152,999 zilitumika kwa kazi za maendeleo ikiwa ni mchango wa washirika wa maendeleo sawa na asilimia 89.24 ya makadirio.

**MATOKEO NA MAPENDEKEZO YA UKAGUZI**

#### 6.10.1.1 Kutokukamilika kwa ujenzi wa Skuli ya Sekondari Kibuteni kwa wakati

Katika ukaguzi uliofanyika kwa mwaka wa fedha 2020/2021 imebainika Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ilifunga mkataba wa makubaliano wenye kumbukumbu namba CW/1/SMZ/B/01/210/LOT1 wa tarehe 3 Septemba, 2012 na mzabuni United Distributers Ltd kwa ajili ya ujenzi wa skuli ya Sekondari Kibuteni, ambapo mkataba huo ulitarajiwa kumalizika tarehe 12 Oktoba, 2013 sawa na wiki 58 wenye thamani ya shilingi 3,945,259,264 ambapo ujenzi huo ulikuwa unafadhiliwa na BADEA I.

Dosari iliobainika katika ukaguzi ni kutokukamilika ujenzi kwa wakati na kupelekea shughuli zifuatazo kutokutekelezwa:-

- Ujenzi wa jengo la utawala na madarasa
- Ujenzi wa jengo la chakula
- Ujenzi wa jengo la bweni la wanafunzi
- Ujenzi wa jengo la waalimu

Kutokana na dosari zilizobainika hapo juu Wizara ilifanya maamuzi ya kusitisha mkataba na mzabuni huyo baada ya kujiridhisha kuwa hana uwezo wa kuendelea na kazi hiyo na kumtaka ailipe Serikali hasara ya shilingi 675,277,138.4

Dosari ziliobainika katika ukaguzi kutokana na kadhia hiyo ni kama zifuatazo:-

- Serikali kupata hasara ya kutokutumia majengo kwa wakati.
- Hasara inayotokana na uchelewaji wa ununuzi wa baadhi ya vifaa vya kutoa huduma skuli kutokana na kuongezeka kwa thamani halisi ya bei za bidhaa.
- Hasara ya kuchelewa kwa mradi kukamilika kwa wakati na kupelekea Serikali kubeba gharama za kuumalizia mradi huo kutokana na muda wa mradi kumalizika bila ya mafanikio yaliokusudiwa.
- kushindwa kujiridhisha na kufanya maamuzi sahihi kwa kamati ya tathmini ya kumtafuta mzabuni mwenye uwezo jambo ambalo limepelekea kuitia Serikali hasara.
- Mzabuni kutokuwa na uwezo wa kifedha jambo ambalo limetia shaka bodi ya zabuni kumteuwa.
- Kukosekana kwa taarifa za mzabuni mahala alipotekeleza mradi wa aina kama hiyo jambo ambalo limeonesha kutokuwa na uzoefu wa utekelezaji wa miradi mikubwa kwa kipindi kifupi.
- Kutokutekelezwa kwa maagizo ya mkataba yanayoitaka Wizara kuchukuwa hatua ndani ya siku 28 pale inapobainika mkandarasi amesimamisha shughuli za utekelezaji wa mradi bila sababu yoyote jambo ambalo Wizara ilichukuwa miaka 8 ndio kuanza kufanya ufuatiliaji.

Pamoja na uwepo wa dosari hizo ukaguzi umebaini Wizara ilishafanya malipo ya shilingi 2,058,486,497 kutoka katika mkataba wake wenye shilingi 3,945,259,264 na kuwepo kwa bakaa ya shilingi 1,886,772,767 ambazo alikuwa hajalipwa.

Aidha, pamoja na uwepo wa bakaa hiyo ya fedha ukaguzi umebaini Wizara kuchelewa kufanya maamuzi kumepelekea mkandarasi kuhamisha vifaa vyake katika eneo la ujenzi bila ya taarifa jambo ambalo kwa mujibu wa makubaliano ya mkataba kama mkandarasi atashindwa kuendelea na hatua ya ujenzi atalazimika vifaa vyote kuviwacha katika eneo la ujenzi.

Katika kuendelea na ujenzi kutokana na hatua iliyofikia Wizara ilifanya mkataba wa nyongeza na kampuni ya Rans Company Ltd kwa thamani ya shilingi 2,054,020,400 kwa ajili ya kazi ya ukamilishaji wa jengo aliloliwacha mkandarasi wa awali ambapo ujenzi wa dakhalia ya wanaume imegharimu shilingi 1,129,593,900 pamoja na PC SUM shilingi 747,000,000 kwa kazi ya ziada ambazo hazimo katika mkataba wa mwanzo na jumla ya gharama yote 3,930,614,300 ambapo Wizara imeshafanya malipo ya shilingi 2,361,092,402.

Kutokana na kuendelea kwa ujenzi na kampuni ya Rans ukaguzi umebaini dosari zifuatazo:-

- Kwa mujibu wa mkataba wa awali ulieleza iwapo mzabuni atashindwa kuendelea na ujenzi atapewa mkandarasi mpya kwa gharama iliyobakia jambo ambalo halikuwezekana kutekelezeka kutokana na kupanda kwa gharama za ujenzi kulikosababishwa na uzembe wa Wizara kuchelewa kuchukuwa maamuzi ya mapema baada ya kubaini mkandarasi wa mwanzo hana uwezo wa kifedha kuendelea na ujenzi.
- Hadi ujenzi utakapo kamilika utagharimu jumla ya shilingi 5,989,100,797 ambapo ni sawa na asilimia 66 ya ziada ya gharama ya awali jambo ambalo ilipaswa Wizara kufanya maamuzi ya kufunga mkataba mpya kwa mujibu wa taratibu na sheria za ununuzi na uondoshaji wa mali za Umma.
- Ukiukwaji wa kifungu nambari 49(4)(5) cha Kanuni ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2021 kinaeleza kwamba iwapo malipo yatazidi bei ya mkataba zaidi ya asilimia 15 yawasilishwe kwa mlipaji Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kupata uthibitisho (Approval).

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wizara ya Elimu kuhakikisha unaongeza umakini katika kufanya tathmini katika kumteuwa mzabuni ambaye atakuwa na uwezo wa kifedha, pamoja na uzoefu kwa mujibu wa kazi anayotaka kupewa ili kuepusha Serikali kupata hasara zinazotokana na urasimu wa kutokuchukuwa maamuzi haraka.

#### 6.10.1.2 Dosari katika usimamizi wa Dahalia

Katika ukaguzi uliofanyika kwa mwaka wa fedha 2020/2021 umeweza kutembelea maeneo mbalimbali ikiwemo utekelezaji wa miradi ya maendelezo inayotekelezwa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, kutembelea baadhi ya Skuli za ufundi zinazojishughulisha na uzalishaji mali, pamoja na dakhalia mbalimbali kwa lengo la kuweza kubaini baadhi ya changamoto zinazoweza kupelekea kutofaulu vizuri kwa wanafunzi au kutokufikiwa kwa malengo ya uzalishaji mali unaotokana na uwepo wa changamoto mbalimbali zinazojitokeza katika skuli hizo kama zifuatavyo:-

- Uchache wa upatikanaji wa fedha za chakula kwa mujibu wa bajeti za maskuli ambazo zinazoenda sambamba na wingi wa wanafunzi waliopo na wanaolala katika dakhalia.
- Uchache wa mabweni ya kulala wanafunzi kutokna na idadi kubwa ya wanafunzi wanaolala kutokana na maeneo wanayoishi au skuli wanazotoka.
- Kutokuwepo gari maalum katika dakhalia kwa ajili ya kutoa huduma kwa wanafunzi pale dharura inapojitokeza.
- Kutokuwepo kwa kituo cha huduma ya Afya kwa ajili ya huduma ndogo ndogo za afya.
- Kukosekana kwa viwanja vya kuchezea watoto ambavyo vitapelekea akili za watoto kukuwa na kuibua vipaji vipya kupitia michezo.
- Kukosekana kwa vifaa vya kisasa vya kufundishia masomo ya vitendo na nadharia ikiwemo "electronic drawing cards, computer drawing rooms, grinding machines" jambo ambalo linapelekea kuwepo kwa vyumba vya kufanyia mafunzo ya vitendo ambavyo haviendani na uhalisia wa mitaala ya mafunzo ya ufundi stadi.
- Baadhi ya skuli za ufundi kushindwa kufanya uzalishaji mali kutokana na kukosekana kwa ruzuku ya fedha inayopelekea wanafunzi kushindwa kufanya mafunzo ya vitendo na hatimaye Skuli za ufundi kufundisha zaidi kwa nadharia kuliko vitendo.

Kutokana na changamoto zilizobainika ukaguzi unaishauri Serikali kupitia Wizara ya Elimu kuhakikisha inaandaa mazingira bora ya kuboresha skuli za ufundi pamoja na dakhalia mbalimbali ili ziweze kuendana na wakati wa uzalishaji wanafunzi ambao wataweza kujitegemea pindi wanapomaliza mafunzo yao na kuacha kutegemea ajira kutoka Serikalini ambapo lengo la Serikali kuanzisha skuli za ufundi ni kuhakikisha kuwa mwanafunzi anakua mjasiriamali au kuzalisha wahandisi ambao wataendana na dhana ya kuitoa Serikali katika uchumi wa Kati na kuipeleka katika uchumi wa viwanda na kujitegemea. Aidha, ni vyema Wizara ya Elimu kuhakikisha inaondokana na matumizi ya kutumia umeme mkali katika uzalishaji wa usanifu wa vyuma katika maskuli ya ufundi na kuanza kutumia umeme mwepesi wa usanifu wa aluminium ambapo leo ndipo dunia ilipofikia.

**Hesabu ya Madawati namba 0404019000**

### 6.10.1.3 Dosari katika Ununuzi wa madawati shilingi 2,882,981,080

katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Wizara ya Elimu na mafunzo ya amali imeingia mkataba wa nyongeza (Addendum) uliosainiwa tarehe 15 Novemba, 2019 wenye thamani ya dola za kimarekani USD 1,254,529.20 kwa ajili ya ununuzi wa madawati 35,610 na kupelekea uwepo wa mkataba halisi uliosainiwa tarehe 21 Septemba 2020 kufikia thamani ya dola za kimarekani USD 2,641,528.70.

Aidha, ukaguzi umebaini kujitokeza kwa dosari za kuitendaji katika utekelezaji wa mkataba wa nyongeza ambapo imebainika uwepo wa ziada ya matumizi ya dola za kimarekani 1,386,999.5 sawa na asilimia 111 ya ongezeko la gharama za awali.

Kutokana na kuwepo kwa ongezeko hilo kumejitokeza ukiukwaji wa sheria ya Ununuzi ambapo kifungu nambari 49(4-5) cha kanuni ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2021 kinaeleza kwamba " iwapo malipo yatazidi bei ya mkataba zaidi ya asilimia 15 yawasilishwe kwa mlipaji Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kupata uthibitisho au Baraza la Wawakilishi (Approval)." Jambo ambalo ukaguzi haukupatiwa uthibitisho huo.

Kukosekana kwa muhtasari wa maamuzi ya kikao cha bodi ya zabuni kilichoamua kumpitisha mzabuni huyo na kuendelea na harakati za zabuni yake kwa mujibu wa kifungu cha 6(1)(c) cha Sheria Nambari 11 ya Manunuzi na Uondoshaji wa Mali za ya mwaka 2016, pindipo inapotokezea nyongeza ya mkataba wa awali kupewa mzabuni wa mwanzo kuendela na kazi hio haitatakiwa kuongezeka kwa asilimia 25 ya thamani ya zabuni ya awali jambo ambalo halikuzingatiwa katika utowaji wa zabuni hio.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara kwa mujibu wa dosari zilizobainika hapo juu Wizara ilipaswa kutangaza zabuni mpya ili kuweza kujitokeza wazabuni ambao watakuwa na ushindani wa bei kwa lengo la kuleta tija iliokusudiwa vyenginevyo ni kuitia hasara Serikali na kupelekea upotevu wa fedha za Umma.

Vile vile kwa mujibu wa sheria kama Wizara ilikuwa haina budi kuendelea na mzabuni huyo ilipaswa kufanya malipo ya aslimia 25 na sio malipo yalofanyika ya aslimia 110 jambo ambalo limepelekea kuisababishia hasara Serikali kwa malipo ya asilimia 85 ya ziada ya malipo ya awali. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

### Jadweli Nambari 180 : Fedha zilizotumika kwa ajili ya ununuzi wa madawati

| Hati namba | Kiasi cha Fedha (Tshs) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|
| 1/10/2020 | Tshs. 960,818,930 **(USD 416,102.85)** | JIANGMEN KEYI METAL MANUFACTURE CO. LTD | Malipo ya fedha kwa Kampuni ya JIANGMEN KMM COY. LTD kwa ajili ya ununuzi wa madawati. |
| 1/1/2021 | Tshs. 961,081,075 **(USD 416,102.85)** | | |
| 2/6/2021 | Tshs. 961,081,075 **(USD 416,102.85)** | | |
| **Jumla** | **Tshs. 2,882,981,080** | | |

## 6.10.2 BODI YA MIKOPO YA ELIMU YA JUU

Ukaguzi wa hesabu za mwaka wa fedha 2020/2021 kwa Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu umefanywa kwa mujibu wa Sheria, kanuni, taratibu pamoja na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Taarifa ya Mapato**

Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ilikadiriwa kukusanya jumla ya shilingi 3,515,475,000. Hadi kufikia tarehe 30, Juni 2021 Bodi ilifanikiwa kukusanya jumla ya shilingi 10,352,345,318 sawa na asilimia 294 ya makadirio.

**Taarifa ya Matumizi**

Bodi ya mikopo ya Elimu ya Juu Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2020/2021 iliidhinishiwa kutumia jumla ya shilingi 16,651,350,000. Kati ya fedha hizo shilingi 389,400,000 kwa ajili ya mshahara na shilingi 16,261,950,000 kwa ajili ya matumizi mengineyo.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 jumla ya shillingi 15,147,623,168 zilitumika ambazo ni sawa na asilimia 91 ya makadirio. Kati ya fedha hizo shilingi 386,148,100 zilitumika kwa ajili ya mishahara sawa na asilimia 99 ya makadirio na shilingi 14,761,475,068 kwa ajili matumizi mengineyo sawa na asilimia 97 ya makadirio.

**MATOKEO NA MAPENDEKEZO YA UKAGUZI**

### 6.10.2.1 Madeni ya wanafunzi shilingi 1,921,043,698.69

Ukaguzi umebaini kuwepo kwa deni kubwa la wanufaika wa mikopo ya Elimu wa fani mbalimbali kwa vipindi tofauti kuanzia mwaka 2006 hadi 2011, lakini hadi sasa mikopo hiyo bado haijarejeshwa pamoja na kufikia muda wa kuanza kufanya marejesho. Wanufaika 206 ambao wamepata mkopo wa jumla ya shilingi **1,921,043,698.69** wanaonekana kuwa ni wadaiwa sugu wa Bodi ya Mikopo.

Kutofanya marejesho ya mkopo kwa wakati kunapelekea kuzirejesha nyuma juhudi za Serikali za kuwapatia fursa wananchi na kuweza kujiendeleza katika elimu ya juu jambo ambalo litakwaza utekelezaji wa shughuli za bodi ya mikopo walivyojipangia ikiwa mikopo hiyo haitarejeshwa kwa wakati, **Kiambatisho Nambari 9 Kinahusika.**

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Bodi ya Elimu ya Juu kuhakikisha juhudi za makusudi zinachukuliwa kuwatafuta wadaiwa wote popote walipo na taratibu za kuwakata madeni ya mikopo yao kutokana na mishahara wanayoipata katika taasisi wanazozifanyia kazi.

Aidha, uongozi uchukue juhudi za kusambaza majina ya wadaiwa kwa taasisi zote za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar pamoja na Muungano ili kuwataka Wakuu wa taasisi watoe ushirikiano wa taarifa za mtumishi yoyote ambae jina lake litakuwa limebainika katika taarifa za deni zilizosambazwa ili hatua stahiki ziweze kuchukuliwa juu yake ikiwemo urejeshwaji wa mikopo hiyo.

### 6.10.2.2 Kukosekana kwa mfumo wa uhakiki wa wanafunzi waliopo vyuoni

Ukaguzi umebaini kwamba hakuna mfumo maalum uliotayarishwa kwa mashirikiano baina ya Bodi ya Mkopo wa Elimu ya juu Zanzibar na vyuo husika ili kuthibitisha uwepo wa wanafunzi wanaoendelea na masomo yao katika vyuo husika kuanzia muhula wa pili na kuendelea kwa mnasaba wa kuendelea kupatiwa mkopo. Mfumo huo ambao ungekuwa ni uthibitisho wa wanafunzi wanaoendelea na masomo na wangepaswa kuendelea kupatiwa mkopo ili kuondoa utata wa kuwalipia wanafunzi ambao hawapo vyuoni kuendelea na masomo kutokana na sababu zozote zile zilizowakabili, ama kujitokeza kwa wanafunzi waliokosa sifa za kupata mkopo kwa Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu Zanzibar.

Kukosekana kwa mfumo wa uhakiki wa wanafunzi kumepelekea Serikali kupoteza fedha nyingi kuendelea kuwalipa wanafunzi ambao kwa njia moja ama nyengine wamepoteza sifa ya kuwa wanafunzi wa elimu ya juu kutoka katika vyuo mbalimbali ima kwa sababu ya utoro au kushindwa kuendelea na masomo kutokana na sababu mbalimbali jambo litapelelekea ugumu wa kuwatambua walipo na hatimae kutokupatikana kwa marejesho ya fedha iliyokusudiwa kutumika kuwasomeshea wanafunzi wengine.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Bodi ya Mikopo ya Elimu ya juu kuhakikisha unafanya kazi karibu na Bodi ya mikopo ya elimu ya juu Tanzania Bara kwa lengo la kusaidiana utelekezaji wa majukumu yao ambapo utaibua kuwabaini wanafunzi wanaochukua mikopo na kushindwa kuirejesha kwa wakati.

**BODI YA MIKOPO YA ELIMU YA JUU - PEMBA**

### 6.10.2.3 Malipo kwa Watoa huduma ambao hawakusajiliwa na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma shilingi 3,187,830

Kwa mujibu wa kifungu cha 23(1) cha Sheria ya Manunuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma kinaeleza kulingana na masharti ya sheria hii mtu, kampuni au taasisi haitawasilisha zabuni au vyenginevyo kushiriki katika manunuzi ya Umma isipokua chombo kiwe kimesajiliwa na Mamlaka ya Manunuzi.

Kwa mujibu wa kifungu cha 23(2), zabuni kutoka kwa mtu, kampuni au chombo ambacho hakijasajiliwa haifai na hakitazingatiwa na taasisi ya ununuzi.

Ukaguzi umebaini kwamba Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu Pemba imefanya manunuzi na watoa huduma mbali mbali ambao hawakusajiliwa na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya Zanzibar.

Kufanya hivyo kunapelekea kuikosesha Serikali mapato ambapo ni kwenda kinyume na Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 181: Malipo kwa Watoa huduma ambao Hawakusajiliwa na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma**

| Hati Namba | Hundi Namba | Kiasi cha fedha kilicholipwa (Tshs.) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 3/7 24/7/2020 | 000061 | 300,000 | Pandu Bookshop | Malipo ya fedha kwa ajili ya matumizi madogo madogo ya ofisi. |
| 1/8 3/8/2020 | 000063 | 400,000 | Ali Miraj Abdallah | Malipo ya fedha kwa ajili ya posho na huduma nyengine . |
| 5/9 9/9/2020 | 000068 | 100,000 | Pandu Bookshop | Malipo ya fedha kwa ajili ya matumizi madogo madogo ya ofisi. |
| 6/9 1/9/2020 | 000066 | 120,000 | | |
| 3/10 26/10/2020 | 000071 | 300,000 | Pandu Bookshop, Khamis Omar Moh'd na Masoud Khamis Moh'd | Malipo ya fedha kwa ajili ya matumizi madogo madogo ya ofisi. |
| 6/11 10/11/2020 | 000077 | 300,000 | Pandu Bookshop na Abuu Ahmed Omar. | |
| 2/1 6/1/2021 | 000080 | 300,000 | Michenzani Store na Ali Suleiman Ali. | |
| 6/1 15/1/2021 | 000083 | 300,000 | Pandu Book Shop na African Café | |
| 12/1 20/1/2021 | 000097 | 85,000 | Juma Abdalla Kheir | Malipo ya fedha kwa ajili ya utengezaji wa Printer ya ofisi. |
| ½ 1/2/2021 | 000090 | 300,000 | Nassor Kassim Issa na Sharif Restaurant. | Malipo ya fedha kwa ajili ya matumizi madogo madogo ya ofisi. |
| 1/3 9/3/2021 | 000096 | 300,000 | Nassor Kassim Issa na Ali Kheri Rashid. | |
| 5/6 2/6/2021 | TT | 285,180 | Ali Kheri Rashid | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa mbali mbali |
| 7/6 2/6/2021 | 000101 | 300,000 | African Café | Malipo ya fedha kwa ajili ya matumizi madogo madogo ya ofisi |
| 8/6 2/6/2021 | 000101 | 520,000 | Sharif Restaurant. | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa chakula |
| 10/6 11/6/2021 | TT | 237,650 | Ali Kheir Rashid | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa |
| **Jumla** | | **3,187,830** | | |

### 6.10.2.4 Bidhaa ambazo hazikurikodiwa katika daftari la ghalani shilingi 3,425,180

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwa jumla ya shilingi 3,425,180 zimetumika kwa ajili ya ununuzi wa bidhaa mbali mbali kwa matumizi ya Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu Pemba lakini bidhaa hizo hazikurikodiwa katika madaftari ya ghalani ili kuweza kuthibitisha uhalali wa mapokezi pamoja na matumizi ya bidhaa hizo.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016. Mchanganuo wa bidhaa hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 182 : Bidhaa ambazo hazikurikodiwa katika daftari la ghalani**

| Hati Namba | Hundi Namba | Kiasi cha fedha kilicholipwa (Tshs.) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 3/7 24/7/2020 | 000061 | 300,000 | ZHELB – Pemba | Ununuzi wa vifaa vya kuandikia. |
| 6/9 1/9/2020 | 000066 | 120,000 | | |
| 5/9 9/9/2020 | 000068 | 100,000 | | Ununuzi wa maji ya kunywa. |
| 3/10 26/10/2020 | 000071 | 300,000 | | Ununuzi wa vifaa vya kuandikia |
| 6/11 10/11/2020 | 000077 | 300,000 | | |
| 2/1 6/1/2021 | 000080 | 300,000 | | Ununuzi wa bidhaa mbali mbali |
| 6/1 15/1/2021 | 000083 | 300,000 | | Ununuzi wa viburudishaji |
| 1 /2 1/2/2021 | 000090 | 300,000 | | Ununuzi wa vifaa vya kuandikia |
| 1/3 9/3/2021 | 000096 | 300,000 | | Ununuzi wa viburudishaji. |
| 5/6 2/6/2021 | TT | 285,180 | Ali Kheri Rashid | Ununuzi wa bidhaa mbali mbali |
| 7/6 2/6/2021 | 000101 | 300,000 | ZHELB – Pemba | Ununuzi wa viburudishaji |
| 8/6 2/6/2021 | 000101 | 520,000 | | |
| **Jumla** | | **3,425,180** | | |

### 6.10.2.5 Makadirio ya ukusanyaji wa mapato kinyume na uhalisia shilingi 300,000,000

Jumla ya shilingi 300,000,000 zilikadiriwa kukusanywa na Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu Pemba kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

Ukaguzi umebaini kwamba makadirio hayo ni madogo ukilinganisha na makusanyo halisi kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ambapo hadi kufikia 30 Juni 2021, jumla ya shilingi 459,901,000 zilikusanywa sawa na asilimia 153.3 ya makadirio.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya Zanzibar nambari 12 ya mwaka 2016 kifungu nambari 32(1)(2).

### 6.10.3 OFISI YA MKAGUZI MKUU WA ELIMU

Ukaguzi wa hesabu za Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Elimu kwa mwaka wa fedha 2020/2021 kwa umefanywa mujibu wa Sheria, kanuni, taratibu pamoja na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Taarifa ya Mapato**

Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Elimu kwa mwaka wa fedha 2020/2021 iliidhinishiwa kutumia jumla ya shilingi 1,109,500,000. Kati ya fedha hizo shilingi 756,900,000 kwa ajili ya mshahara na shilingi 352,600,000 kwa ajili ya matumizi mengineyo.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 jumla ya shilingi 1,015,144,043 ziliingizwa na kutumika ambazo ni sawa na asilimia 91 ya makadirio. Kati ya fedha hizo shilingi 892,270,193 zilitumika kwa ajili ya mshahara sawa na asilimia 118 ya makadirio na shilingi 122,873,850 zilitumika kwa ajili ya matumizi mengineyo sawa na asilimia 35 ya makadirio.

### 6.10.4 OFISI YA MRAJIS WA BARAZA LA ELIMU ZANZIBAR

Ukaguzi wa hesabu za Ofisi ya Mrajis wa Baraza la Elimu Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2020/2021 umefanywa kwa mujibu wa Sheria, kanuni, taratibu pamoja na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Taarifa ya Mapato**

Ofisi ya Mrajis wa Baraza la Elimu Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ilikadiriwa kukusanya jumla ya shilingi 215,700,000. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 Ofisi ya Mrajis wa Elimu Zanzibar ilikusanya jumla ya shilingi 141,018,343 sawa na asilimia 65.37 ya makadirio.

**Taarifa ya Matumizi**

Ofisi ya Mrajis wa Baraza la Elimu Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2020/2021 iliidhinishiwa kutumia jumla ya shilingi 264,200,000. Kati ya fedha hizo shilingi 154,000,000 kwa ajili ya mishahara, na shilingi 110,200,000 kwa ajili ya matumizi mengineyo.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 jumla ya shilingi 197,526,722 ziliingizwa na kutumika ambazo ni sawa na asilimia 75 ya makadirio. Kati ya fedha hizo shilingi 145,176,831 zilitumika kwa ajili ya mishahara sawa na asilimia 94 ya makadirio, na shilingi 52,349,891 zilitumika kwa ajili ya matumizi mengineyo sawa na asilimia 47 ya makadirio.

**MATOKEO NA MAPENDEKEZO YA UKAGUZI**

#### 6.10.4.1 Kutofikia lengo la ukusanyaji wa mapato shilingi 74,681,657

Ofisi ya Mrajis wa Baraza la Elimu ilipanga kukusanya jumla ya shilingi 215,700,000 kupitia vyanzo vyake mbalimbali vya mapato. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 ilikusanya jumla ya shilingi 141,018,343 ambazo ni sawa na asilimia 65 ya makadirio na kuwa na upungufu wa shilingi 74,681,657 sawa na asilimia 35 ya upungufu.

Aidha,ukaguzi umebaini kutokufikiwa kwa malengo yaliokusudiwa kunatokana na uwepo wa dosari zifuatazo:-

- Kukosekana kwa ufuatiliaji wa madeni ya wanafunzi.
- Kutokusimamia vyema ukusanyaji kwa mapato kutoka kwenye vyanzo mbalimbali vya mapato vinavyozalisha au kukodishwa kwa ajili ya kutoa huduma nyenginezo za Mrajis wa Baraza la Elimu.

Kutokufikiwa kwa lengo la ukusanyaji wa mapato kunaweza kupelekea kushindwa kutekelezeka kwa baadhi ya malengo waliojipangia kwa wakati na muda husika.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Ofisi ya Mrajis wa Baraza la Elimu kuhakikisha unaweka mfumo imara ambao utapelekea kuongezeka kwa makusanyo ya mapato yaliyokusudiwa iwapo watasimamia vyema vyanzo vya mapato. Mchanganuo wa makadirio na makusanyo halisi ya vyanzo vya mapato ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 183 : Mapato yaliyokusanywa ambayo hayakufikia lengo**

| Chanzo cha makusanyo | Makisio | Kilichokusanywa | Tofauti (%) |
|---|---|---|---|
| Usajili wa leseni za skuli binafsi | 115,700,000 | 91,608,840 | 79 |
| Leseni za walimu | 100,000,000 | 49,409,503 | 49 |
| **Jumla** | **215,700,000** | **141,018,343** | **65** |

## 6.10.5 BARAZA LA MITIHANI ZANZIBAR

Ukaguzi wa hesabu za Baraza la Mitihani Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2020/2021 umefanywa kwa mujibu wa Sheria, kanuni, taratibu pamoja na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Taarifa ya Mapato**

Baraza la Mitihani Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2020/2021 lilikadiriwa kukusanya jumla ya shilingi 183,095,000. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 jumla ya shilingi 288,124,016 zilikusanywa sawa na asilimia 157 ya makadirio.

**Taarifa ya Matumizi**

Baraza la Mitihani Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2020/2021 lilipanga kutumia jumla ya shilingi 5,672,231,000. Kati ya fedha hizo shilingi 419,400,000 kwa ajili ya mishahara na shilingi 5,252,831,000 kwa ajili ya matumizi mengineyo.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 jumla ya shilingi 4,093,485,826 zilitumika ambazo ni sawa na asilimia 72 ya makadirio. Kati fedha hizo shilingi 456,585,940 zilitumika kwa ajili ya mishahara sawa na asilimia 108 ya makadirio na shilingi 3,636,899,886 zilitumika kwa ajili matumizi mengineyo sawa na asilimia 89 ya makadirio.

**MATOKEO NA MAPENDEKEZO YA UKAGUZI**

### 6.10.5.1 Mapungufu yaliyojitokeza katika ufungaji wa hesabu

Katika ukaguzi uliofanyika kwa mwaka wa fedha 2020/2021 imebainika Baraza la Mitihani halikuweza kuzingatia matakwa ya ufungaji wa hesabu kwa mujibu wa vigezo vilivyowekwa kitaifa na kimataifa na kupelekea hesabu za Baraza la Mitihani kutokuonesha sura sahihi na halisi kwa mujibu wa vigezo vilivyowekwa.

Aidha, ukaguzi ulifanya mawasiliano ya mara kwa mara ikiwemo kuwataka wahusika wafanye marekebisho juu ya dosari zilizobainika ili kuepuka kujitokeza kwa wingi wa hoja za ukaguzi ambazo zitapelekea utolewaji wa hati isiyoridhisha jambo ambalo hawakuweza kutekeleza hadi ukaguzi unakamilika taarifa za hesabu za Baraza la Mitihani zilikuwa na dosari zifuatazo:-

**a) Taarifa ambazo hazikuambatanishwa na hesabu za mwisho wa mwaka**

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika taarifa za mali za kudumu hazikuwasilishwa kwa ajili ya ukaguzi na kupelekea kubainika kwa kasoro mbalimbali zinazotokana na kutokujulikana sehemu mali zilipo, thamani halisi ya mali hiyo pamoja na kukosekana kwa hati miliki inayothibitisha umiliki halali wa mali hizo pamoja na kutokujulikana thamani na sera za uchakavu wa mali hizo ili kuweza kuishauri Serikali juu ya namna bora ya kuzitambua mali zake pamoja na kuziwekea kumbukumbu maalum ya utambulisho wa mali hizo ili zisiweze kuvamiwa ,kuuzwa, pamoja na kukutumika vibaya kinyume na utaratibu uliowekwa na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

Aidha, kutokuziainisha mali za Serikali na kuziingiza katika daftari maalum kunaweza kukapelekea mali hizo kutokujulikana na hatimae kuibiwa au kupotea na kuipelekea hasara Serikali.

Ukaguzi unaushauri uongozi kuhakikisha mali zote zinaainishwa katika buku maalum la kuwekea kumbukumbu pamoja na kuziwekea hesabu yake mwisho wa mwaka ili kuweza kuonesha mtaji wa mali unaomilikiwa na taasisi za Serikali.

**Jadweli Nambari 184 : Taarifa ambazo hazikuambatanishwa na hesabu za mwisho wa mwaka**

| Namba | Aina ya Mali |
|---|---|
| 1 | Kiwanja kinachomilikiwa na Baraza la Mitihani kilichopo Pemba |
| 2 | Kiwanja kinachomilikiwa na Baraza la Mitihani kilichopo Tunguu |

#### 6.10.5.2 Matumizi mabaya ya fedha za Umma shilingi 3,003,808,085

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kupitia hesabu za mwisho wa mwaka Baraza la Mitihani Zanzibar liliwasilisha matumizi yanayohusiana na usimamizi na usahihishaji mitihani ya taifa ya elimu ya Msingi na Sekondari ya awali yenye thamani ya shilingi 3,003,808,085 kwa mwaka wa fedha 2020/2021. Dosari iliyobainika katika ukaguzi ni kama ifuatavyo:-

- Kukosekana kwa vielelezo vinavyothibitisha uhalali wa matumizi ya shilingi 3,003,808,085 zilizotumika kwa ajili ya usimamizi na usahihishaji wa mitihani.
- Kukosekana kwa mchanganuo wa matumizi ya fedha hizo jambo ambalo limepelekea kushindwa kushibitisha kilichonunuliwa pamoja na thamani halisi ya kilicholipwa.
- Kukosekana kwa taarifa za kumbukumbu za matumizi hayo.
- Kukosekana kwa muongozo wa ulipwaji wa wasimamizi wa mitihani, watungaji wa mitihani, wasafirishaji, wasahihishaji na washughulikiaji wa mitihani jambo ambalo linapelekea Baraza kulipa thamani ndogo ya fedha ambayo haiendani na ugumu wa kazi yenyewe.
- Walimu kutokuwa na hamasa ya kushughulia zoezi zima la mitihani kuanzia kutunga kusimamia kusainisha na hata kutoka matokeo kutokana na malipo dhaifu wanayolipwa na Baraza la Mitihani kutokana na kukosekana kwa muongozo wa malipo.

Kutokana na dosari zilizoainishwa hapo juu ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara ya Elimu kuchukua jitihada za makusudi kuhakikisha wanatoa kipaumbele kwa walimu na washughulikiaji wa mitihani kuwapatia malipo stahiki kutokana na ugumu wa kazi wanayoifanya vyenginevyo inaweza ikajitokeza thamani ya elimu kushuka kutokana na walimu kupoteza ari ya kazi yao.

### 6.10.6 TAASISI YA ELIMU ZANZIBAR

Ukaguzi wa hesabu za Taasisi ya Elimu Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2020/2021 umefanywa kwa mujibu wa Sheria, kanuni, taratibu pamoja na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Taarifa ya Matumizi**

Taasisi ya Elimu Zanzibar iliidhinishiwa kutumia jumla ya shilingi 5,925,000,000 kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kati ya fedha hizo shilingi 343,200,00 kwa ajili ya mshahara na shilingi 331,800 kwa ajili ya matumizi mengineyo. Aidha shilingi 3,250,000,000 ikiwa ni fedha za mradi kutoka kwa washirika wa maendeleo, na shilingi 2,000,000,000 ikiwa ni mchango wa Serikali kwa shughuli za maendeleo.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 jumla ya shilingi 743,951,087 ziliingizwa na kutumika ambazo ni sawa na asilimia 13 ya makadirio. Kati ya fedha hizo shilingi 408,759,557 zilitumika kwa ajili ya mshahara sawa na asilimia 119 ya makadirio na shilingi 94,140,530 zilitumika kwa ajili ya matumizi mengineyo sawa na asilimia 28 ya makadirio.

**MATOKEO NA MAPENDEKEZO YA UKAGUZI**

### 6.10.6.1 Kufanya Malipo bila ya kuwepo kwa Bajeti shilingi 8,780,800

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika Taasisi ya Elimu Zanzibar imefanya matumizi kwa ajili ya ununuzi wa vitu mbalimbali vyenye thamani ya shilingi 8,780,800 kwa ajili ya shughuli za uwendeshaji wa taasisi.

Dosari iliyobainika katika ukaguzi ni kufanya malipo bila ya kuwepo kwa bajeti iliyoidhinishwa kwa ajili ya ununuzi wa samani na vifaa vyenginevyo. Kwa mjibu wa utaratibu Taasisi inaweza kufanya manunuzi yaliyo nje ya bajeti ikiwa itazingatia taratibu za uhaulishwaji wa fungu la bajeti kutoka sehemu moja na kutumika sehemu nyengine baada ya kupata idhini ya Mlipaji Mkuu wa Serikali. Hadi ukaguzi unakamilika hatukuweza kupatiwa idhini ya matumizi hayo kwa kukosekana taratibu za uhaulishwaji kufuatwa. Ukaguzi unaushauri uongozi wa Taasisi ya Elimu kuhakikisha unafanya uhaulishaji wa fedha kwa mujibu wa miongozo na taratibu za fedha zinavyoelekeza ili kuepusha kujitokeza kwa mianya ya upotevu wa fedha za Umma. Mchanganuo wa matumizi hayo ni kama inavyoonekana hapo chini:-

**Jadweli Nambari 185 : Malipo yaliyofanyika bila ya kuwepo kwa bajeti**

| Namba ya hati ya malipo | Namba ya hundi | Kiasi cha fedha kilicholipwa (shs) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 21/8 ya 19/8/2020 | TT | 4,547,200 | New Home Furniture | Ununuzi wa samani za ofisi |
| 7/9 ya 9/9/2020 | TT | 4,233,600 | | |
| **Jumla** | | **8,780,800** | | |

## 6.11 WIZARA YA KILIMO, UMWAGILIAJI, MALIASILI NA MIFUGO

### 6.11.1 FUNGU L 01 - WIZARA YA KILIMO,UMWAGILIAJI, MALIASILI NA MIFUGO

Ukaguzi wa hesabu za Wizara ya Kilimo,Umwagiliaji,Maliasili na Mifugo kwa mwaka wa fedha 2020/2021 umefanywa kwa mujibu wa Sheria, kanuni, taratibu pamoja na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Taarifa ya Mapato**

Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ilikadiriwa kupokea jumla ya shilingi 113,035,689,777. Kati ya fedha hizo shilingi 42,707,249,777 kutoka Serikali Kuu, shilingi 59,860,176,000 kutoka kwa Washirika wa Mendeleo na shilingi 10,468,264,000 zikiwa ni Makusanyo kutoka Vyanzo vya Ndani.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo ilipokea shilingi 37,476,202,629 kutoka Serikali kuu ambapo ni sawa na asilimia 88 ya makadirio, na ilipokea shilingi 20,945,742,820 kutoka kwa Washirika wa Mendeleo ikiwa ni sawa na asilimia 34 ya makadirio ya fedha zilizotarajiwa kupokelewa kutoka kwa Washirika wa Mendeleo.

Aidha, Wizara ilikusanya jumla ya shilingi 5,080,418,228 kutoka vyanzo vyake vya ndani sawa na asilimia 49 ya makadirio.

**Taarifa ya Matumizi**

Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ilikadiriwa kutumia jumla ya shilingi 102,567,425,777. Kati ya fedha hizo shilingi 10,365,921,974 kwa ajili ya mishahara, shilingi 4,900,048,531 kwa matumizi mengineyo , shilingi 21,000,000,000 na shilingi 59,860,176,000 kwa ajili ya kazi za maendeleo na shilingi 6,441,279,272 ikiwa ni ruzuku kutoka Serikalini.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 jumla ya shilingi 37,476,202,629 ziliingizwa na kutumika sawa asilimia 37 ya makadirio. Kati ya fedha hizo shilingi 10,236,935,592 zimeingizwa na kutumika kwa mishahara sawa na asilimia 99 ya makadirio, shilingi 1,595,238,583 zimeingizwa kwa ajili ya matumizi mengineyo sawa na silimia 33 ya makadirio, shillingi 4,698,285,634 zimeingizwa ikiwa ni ruzuku kwa Kutoka Serikalini kwa taasisi zinazopewa ruzuku zilizopo chini ya Wizara sawa na asilimia 73 ya makadirio.

Aidha; Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ilipokea shilingi 498,000,000 ikiwa ni mchango wa Serikali katika matumizi ya maendeleo sawa na asilimia 2 ya makadirio na shilingi 20,447,742,820 ikiwa ni mchango wa Washirika wa Maendeleo katika matumizi ya maendeleo sawa na asilimia 34 ya makadirio.

**MATOKEO NA MAPENDEKEZO YA UKAGUZI**

**6.11.1.1 Dosari zilizobainika katika Taarifa ya Hesabu za Mwisho wa Mwaka 2020/2021.**

Kwa mujibu wa muongozo wa uandaaji wa Taarifa za Hesabu za uliotolewa na Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kitengo cha Mhasibu Mkuu uliwataka wahasibu wa Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo kuainisha taarifa kuhusu mambo mbalimbali pamoja na yale yaliyozoeleka katika kipengele cha Maelezo ya Taarifa za Hesabu (Notes of Financial Statement) kama yalivyotajwa hapo chini.

a) Maelezo kuhusu Madeni (Debtors and Creditors)

b) Maelezo kuhusu Bakaa za Mali (Stock)

c) Maelezo kuhusu Mali Zisizohamishika (Asset List)

d) Maelezo kuhusu Ruzuku zinazoingizwa Wizarani kwa ajili ya Taasisi Tanzu za Wizara na Muhtasari wa Matumizi yake (Subvension Allocation with Expenses).

Ukaguzi umepitia hesabu za Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo za mwaka ulimalizika tarehe 30 Juni, 2021 na kubaini kutokuepo kwa maelezo ya hayo katika kipengele cha Maeelezo ya Taarifa za Hesabu (Notes of Financial Statement).

Kukosekana kwa maelezo hayo katika kipengele cha Maelezo ya Taarifa za Hesabu (Notes of Financial Statement) hizo ni kuenda kinyume toleo la Mhasibu Mkuu kuhusu uandaaji wa Taarifa za Hesabu kwa mwaka wa fedha 2020/2021. Aidha kufanya hivyo ni kuenda kinyume na viwango vya kiuhasibu vya kimataifa (IPSAS).

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wizara kufuata miangozo na taratibu za uandaaji wa Taarifa za Hesabu zinazotolewa na Ofisi ya Raisi, Fedha na Mipango, kadhalika kuenda sambamba na viwango vya uhasibu vya kimataifa (IPSAS).

### 6.11.1.2 Kuchelewa kuwasilishwa kwa Taarifa za Hesabu za Mwaka 2020 /2021.

Kwa mujibu wa kifungu nambari 119 (1) cha Sheria nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016, Taasisi za Umma zinatakiwa kuwasilisha Taarifa za Hesabu za Mwaka kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu Zanzibar miezi mitatu baada ya mwisho wa mwaka wa fedha.

Ukaguzi umebani kwamba Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo iliwasilisha taarifa zake hesabu za mwaka wa fedha 2020/2021 kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu Zanzibar mnamo tarehe 12/10/2021, hivyo Wizara ilichelewa kuwasilisha taarifa hizo kwa muda wa siku kumi na mbili.

Kuchelewa kuwasilisha Taarifa za Hesabu kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu Zanzibar ni kuenda kinyume na kinyume na vifungu namabri 119 (1) cha Sheria nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wizara kuwailisha Taarifa za Hesabu kwa mujibu wa sheria.

### 6.11.1.3 Kutokuanisha kwa Makusanyo ya Mapato yaliyopokelewa kwenye Nambari za Benki za Idara ya Misitu yenye Thamani ya Shilingi 1,483,400,503.47

Ukaguzi umebaini kwamba Idara ya Misitu inamiliki nambari za Benki mbali mbali ambazo inakusanyia mapato kutoka kwenye vyanzo vyake vya ndani. Mapato hayo hukusanywa kutoka katika hifadhi za Misitu, mauzo ya mazao ya misitu, fedha kutoka kwa wahisani na adhabu zinatozwa kwa mujibu wa Sheria na Kanuni za usimamizi wa rasilimali za Misitu.

Aidha, Ukaguzi umepitia Taarifa za Hesabu za Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo na kubaini kwamba jumla shilingi 1,483,400,503.47 ambazo zimekusanywa na Idara ya Misitu kutoka vyazo vyake vya ndani hazikuainishwa katika taarifa hiyo. Taarifa za mapato hayo ni kama zinavyonekana katika jadweli nambari 3 hapo chini:-

**Jadweli Nambari 186: Makusanyo ya Mapato ambayo hayakuainishwa katika Taarifa za Hesabu za mwaka 2020 -2021**

| Nambari ya Benki | Jina la Nambari ya Benki | Jina la Benki na Tawi | Mapato yaliokusanywa kwa 2020 -2021 (Tshs) | Jumla (Tshs) |
|---|---|---|---|---|
| 404206000 | Mfuko wa Maendeleo ya Misitu | PBZ - Forodhani Branch TZS | 215,206,846.13 | 215,206,846.13 |
| 406009000 | Kiwengwa - Pongwe Forest Reserve | PBZ - Forodhani Branch TZS | 4,464,500.00 | 4,464,500.00 |
| 730065001 | Jozani Chwaka Bay Conservation | PBZ - Forodhani Branch TZS | 876,796,159.36 | 876,796,159.36 |
| 0404288000 | Maendeleo na Huduma za Kilimo | PBZ - Forodhani Branch TZS | 384,552,997.98 | 384,552,997.98 |
| 0404288000 | Maendeleo ya Huduma ya Kilimo | PBZ - Forodhani Branch TZS | 2,380,000.00 | 2,380,000.00 |
| **Jumla** | | | | **1,483,400,503.47** |

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Viwango vya Uhasibu vya Kimataifa vya IPSAS na pia ni kwenda kinyume na vifungu nambari 27, 30 (2) na 34 vya Sheria nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wizara kuandaa Taarifa za Hesabu kwa mujibu wa sheria na viwango vinavyoeleweka ili kutoa taarifa sahihi katika hesabu za mwaka.

### 6.11.1.4 Kutokuanisha kwa bakaa lenye thamani ya shilingi 981,065,601.36 katika Taarifa za Hesabu za Mwaka 2020/ 2021

Ukaguzi ulipitia taarifa za nambari za Benki za Idara ya Misitu pamoja na Taarifa ya Hesabu ya Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo na kubaini kwamba jumla ya shilingi 981,065,601.36 ambazo zilibakia katika nambari za Benki hizo hazikuanishwa katika Taarifa ya Hesabu ya Wizara ya mwaka 2020 /2021.

Jadweli nambari hapo chini linaonesha taarifa za bakaa la fedha katika nambari za Benki za Idara ya Misitu hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021.

**Jadweli Nambari 187 : Makusanyo ya Mapato Ambayo hayakuanishwa katika Taarifa za Hesabu za mwaka 2020 -2021**

| Nambari ya Benki | Jina la Nambari ya Benki | Jina la Benki na Tawi | Bakaa ya fedha kwa 2020/2021 (Tshs) | Jumla ya fedha (Tshs) |
|---|---|---|---|---|
| 404206000 | Mfuko wa Maendeleo ya Misitu | PBZ - Forodhani Branch TZS | 69,901,172.82 | 69,901,172.82 |
| 406009000 | Kiwengwa - Pongwe Forest Reserve | PBZ - Forodhani Branch TZS | 15,998,066.45 | 15,998,066.45 |
| 730065001 | Jozani Chwaja Bay Conservation | PBZ - Forodhani Branch TZS | 792,251,439.08 | 792,251,439.08 |
| 775026001 | Jozani Chwaja Bay Conservation | PBZ - Forodhani Branch USD | USD 6,362.00 | 14,632,600.00 |
| 0404288000 | Maendeleo na Huduma za Kilimo | PBZ - Forodhani Branch TZS | 88,282,323.01 | 88,282,323.01 |
| **Jumla** | | | | **981,065,601.36** |

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na viwango vya Uhasibu vya kimataifa vya IPSAS (Cash Basis) vile vile ni kwenda kinyume na vifungu nambari 56 na 122 (2) vya Sheria nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wizara kuandaa Taarifa za Hesabu kwa mujibu wa sheria na viwango vilivyoekwa ili kutoa taarifa sahihi pamoja na kufanya marekebisho kwa hesabu zilizowasilishwa.

#### 6.11.1.5 Kutokuwepo kwa Taarifa za Usuluhishi (Revenue Reconciliation) wa Makusanyo ya Mapato Baina ya Wizara na Idara zinazokusanya Mapato.

Ukaguzi umepitia taarifa za mapato za Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo zilizoanishwa katika taarifa za hesabu za mwaka wa fedha 2020-2021 na baadae kulinganisha taarifa zilizopo kwenye Idara zinazohusika na ukusanyaji wa mapato hayo na kubaini kuwepo kwa tofauti baina yake.

Jadweli hapo chini linaanisha utofauti wa taarifa hizo baina ya zile zilizopo katika hesabu za mwisho za Wizara na zile zilizopatika na ukaguzi kutoka Idara husika.

Kutokuwepo kwa taarifa za usuluhishi wa ukusanyaji mapato unaweza kupelekea kutopata taarifa sahihi za makusanyo ya fedha hizo ni kwenda kinyume na kifungu namabri 27 (1), (2)(a)  na kifungu nambari 30 (1) na ( 2) vya Sheria namba 12 ya usimamizi wa fedha za umma mwaka 2016.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wizara kuwa na mpangilio mzuri wa kufanya usuluhishi wa taarifa za mapato baina yake na Idara zinazokusanya kila mwezi ili kuweza kufahamu kama kuna kasoro ambazo zinaweza kujitokeza.

**Jadweli Nambari 188:Tofauti ya Taarifa za Makusanyo ya Mapato Baina ya Idara na Taarifa za Hesabu za Wizara 2020-2021**

| | Taarifa za Mapato kwa Mujibu wa Idara - Taarifa za Ukaguzi | | | | | | | Taariza za Hesabu za mwaka 2020-2021 | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **CHANZO CHA MAPATO** | **PEMBA** | **IDARA YA MISITU NA MALIASILI ZISIZORE-JESHEKA** | **IDARA YA KILIMO** | **TAASISI YA UTAFITI WA KILIMO** | **IDARA YA UVU-VI** | **IDARA YA MIFUGO** | **JUMLA – A** | **JULAI -FEB** | **MAR - JUNI** | **JUMLA - B** | **TOFAUTI (B-A)** |
| ADA YA MAZAO YA MISITU | 31,907,700 | 362,243,100 | | | | | **394,150,800** | 199,229,800 | 131,628,000 | **330,857,800** | (63,293,000) |
| ADA YA UUZAJI WA MAWE NA MICHANGA NA KOKOTO | | 11,866,000 | | | | | | | | | |
| | 344,471,610 | 1,741,476,892 | | | | | **2,097,814,502** | 2,567,314,610 | 3,061,200 | **2,570,375,810** | 472,561,308 |
| MAUZO YA UZALISHAJI WA MICHE | 575,800 | 3,179,500 | | | | | **3,755,300** | 230,000 | 2,035,800 | **2,265,800** | (1,489,500) |
| ADA UKAGUZI WA MAZAO | 107,484,800 | 114,766,800 | | | | | **222,251,600** | 116,862,350 | 206,265,400 | **323,127,750** | 100,876,150 |
| UTIBABU WA WANYAMA | 1,280,400 | | | | | 1,539,523,508 | **1,540,803,908** | 474,932,924 | 1,066,350,984 | **1,541,283,908** | 480,000 |
| MAPATO YA MIFUGO | 12,017,400 | | | | | 692,500 | **12,709,900** | 6,927,600 | 5,781,800 | **12,709,400** | (500) |
| ADA YA UINGI-ZAJI WAGENI | | 1,111,155,305 | | 3,432,000 | | | **1,114,587,305** | 2,411,000 | 1,021,000 | **3,432,000** | (1,111,155,305) |
| | | | 101,239,150 | | | | **101,239,150** | | | - | (101,239,150) |

#### 6.11.1.6 Kuwepo kwa watumishi ambao hawajalipwa stahiki zao za Likizo

Kwa mujibu wa kifungu nambari 58 (1)(a) cha Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2014 Mtumishi wa Umma anastahiki posho la likizo kila baada ya miaka mitatu.

Ukaguzi umebaini kwamba Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo haikuwa na utaratibu mzuri wa kulipa stahiki za watumishi ndani ya muda sahihi.

Orodha ya watumishi hao kutoka maeneo wanayofanya kazi zilipatikana kwa ajili ya ukaguzi na kubainika kwamba jumla ya shilingi 86,000,000 za stahiki za likizo zilikuwa bado hazijalipwa hadi kumalizika kwa ukaguzi huu. Jadweli hapo chini linaonesha jumla ya watumishi hao na fedha wanazodai.

**Jadweli Nambari 189:Taarifa za Watumishi Wanaodai Stahiki za Likizo**

| Idara | Jumla ya Watumishi Wanaodai | Kima cha Posho la Likizo (Tshs) | Jumla (Tshs) |
|---|---|---|---|
| Idara ya Uendeshaji na Utumishi | 17 | 100,000 | 1,700,000 |
| Idara ya Mipango, Sera na Utafiti | 2 | 100,000 | 200,000 |
| Idara ya Maendeleo ya Mifugo | 131 | 100,000 | 13,100,000 |
| Idara ya Mistu na Maliasili Zisizirejesheka | 333 | 100,000 | 33,300,000 |
| Idara ya Umwagiliaji Maji | 63 | 100,000 | 6,300,000 |
| Idara ya Kilimo | 126 | 100,000 | 12,600,000 |
| Idara ya Uhakika wa Chakula na Lishe | 17 | 100,000 | 1,700,000 |
| Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Zanzibar | 171 | 100,000 | 17,100,000 |
| **Jumla** | | | **86,000,000** |

Kufanya hivyo ni kuenda kinyume kifungu nambari 58 (1)(a) cha Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2014. Vile vile kutokuwalipa stahiki zao watumishi hao ndani ya muda kunaweza kukapelekea kushuka kwa ufanisi katika utendaji kazi.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wizara kuhakikisha unalipa stahiki za watumishi kwa wakati ili kuepuka malimbikizo ya muda mrefu.

#### 6.11.1.7 Kuwepo kwa Watumishi 165 ambao Washamaliza Muda wa Majaribo ila Bado Hawajathibitishwa.

Kifungu nambari 9 (2) cha Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2014 zimeweka ukomo wa muda wa majaribio usiozidi mwaka mmoja na nusu na baada ya hapo mtumishi wa umma anahitajika kuthibitishwa, na endapo bado mtumishi huyo hajatimiza masharti ya kuthibishwa Taasisi ya Umma inatakiwa kuchukua hatua za kumuachisha kazi.

Ukaguzi umebaini kuwepo kwa jumla watumishi 165 katika Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo ambao wameshapindukia muda wa majario na bado hawajathibitishwa. Jadweli nambari lifuatalo linaonesha idadi ya watumishi hao.

**Jadweli Nambari 190 : Orodha ya Watumishi ambao Hawajathibitishwa**

| Nambari | Jina Kamili | Tarehe ya Ajira | Tarehe ya Ukaguzi | Siku alizochelewa kuthibitishwa |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Asma Kombo Haji | 11/05/2019 | 30/06/2021 | 234 |
| 2 | Abdulrahim Bakar Mataka | 11/05/2019 | 30/06/2021 | 234 |
| 3 | Husna Saleh Juma | 01/11/2019 | 30/06/2021 | 60 |
| 4 | Raudha Abdalla Mohammed | 01/11/2019 | 30/06/2021 | 60 |
| 5 | Riziki Abdalla Sheria | 05/06/2019 | 30/06/2021 | 209 |
| 6 | Rukia Mashaka Issa | 05/06/2019 | 30/06/2021 | 209 |
| 7 | Marya Afani Othman | 05/06/2019 | 30/06/2021 | 209 |
| 8 | Abubakar Masoud Ibrahim | 06/05/2019 | 30/06/2021 | 239 |
| 9 | Sadik Maulid Khamis | 01/11/2019 | 30/06/2021 | 60 |
| 10 | Hassan Shaaban Idd | 06/11/2019 | 30/06/2021 | 55 |
| 11 | Yussuf Bakar Salum | 01/11/2019 | 30/06/2021 | 60 |
| 12 | Masoud Juma Ali | 01/11/2019 | 30/06/2021 | 60 |
| 13 | Khamis Juma Makame | 01/11/2019 | 30/06/2021 | 60 |
| 14 | Gora Haji Gora | 01/11/2019 | 30/06/2021 | 60 |
| 15 | Abdul-Wahid Yusuf Mohd | 01/11/2019 | 30/06/2021 | 60 |
| 16 | Ashura Abdalla Haji | 01/11/2019 | 30/06/2021 | 60 |
| 17 | Khamis Haji Khamis | 01/11/2019 | 30/06/2021 | 60 |
| 18 | Moh'd Ali Mohd | 01/11/2019 | 30/06/2021 | 60 |
| 19 | Yassir Hamad Ali | 01/11/2019 | 30/06/2021 | 60 |
| 20 | Talib Juma Khamis | 11/01/2019 | 30/06/2021 | 354 |
| 21 | Abdul-Latif Ramadhan Abdalla | 11/01/2019 | 30/06/2021 | 354 |
| 22 | Wanu Makame Makbul | 11/01/2019 | 30/06/2021 | 354 |
| 23 | Wahid Juma Khamis | 01/11/2019 | 30/06/2021 | 60 |
| 24 | Zuhura Makame Ali | 11/01/2019 | 30/06/2021 | 354 |
| 25 | Wanu Khamis Nyange | 11/01/2019 | 30/06/2021 | 354 |
| 26 | Salim Athumani Guzo | 11/01/2019 | 30/06/2021 | 354 |
| 27 | Mahamudu Faki Mohammed | 06/05/2019 | 30/06/2021 | 239 |
| 28 | Maryam Hussen Ame | 11/01/2019 | 30/06/2021 | 354 |
| 29 | Mkasi Maulid Simai | 11/01/2019 | 30/06/2021 | 354 |
| 30 | Mohammed Mwinyiwesa Muhija | 06/05/2019 | 30/06/2021 | 239 |
| 31 | Khadija Abdalla Habib | 11/01/2019 | 30/06/2021 | 354 |
| 32 | Lila Makata Mwintum | 11/01/2019 | 30/06/2021 | 354 |
| 33 | Fathia Abdalla Juma | 11/01/2019 | 30/06/2021 | 354 |
| 34 | Haitham Bakar Khatib | 11/01/2019 | 30/06/2021 | 354 |
| 35 | Fatma Mmaka Hamad | 11/01/2019 | 30/06/2021 | 354 |
| 36 | Fatma Khamis Hamad | 05/06/2019 | 30/06/2021 | 209 |
| 37 | Habiba Mkombe Pandu | 11/01/2019 | 30/06/2021 | 354 |
| 38 | Juma Moh'd Haji | 11/01/2019 | 30/06/2021 | 354 |
| 39 | Hamad Yussuf Ameir | 11/01/2019 | 30/06/2021 | 354 |
| 40 | Hassan Mussa Ali | 11/01/2019 | 30/06/2021 | 354 |
| 41 | Salama Khalid Suleiman | 11/01/2019 | 30/06/2021 | 354 |
| 42 | Abdulwahid Mwadin Hassan | 11/01/2019 | 30/06/2021 | 354 |
| 43 | Ali Zahran Moh'd | 01/12/2015 | 30/06/2021 | 1,491 |

| Nambari | Jina Kamili | Tarehe ya Ajira | Tarehe ya Ukaguzi | Siku alizochelewa kuthibitishwa |
|---|---|---|---|---|
| 44 | Khadija Sharif Juma | 05/06/2019 | 30/06/2021 | 209 |
| 45 | Idrissa Hamdan Idrissa | 05/06/2019 | 30/06/2021 | 209 |
| 46 | Zubeida Issa Mohamed | 07/01/2014 | 30/06/2021 | 2,184 |
| 47 | Zainab Omar Mmanga | 14/09/2017 | 30/06/2021 | 838 |
| 48 | Yaeni Khamis Kombo | 11/01/2019 | 30/06/2021 | 354 |
| 49 | Wanu Khmais Juma | 06/05/2019 | 30/06/2021 | 239 |
| 50 | Ummulkulthum Khamis Haji | 11/01/2019 | 30/06/2021 | 354 |
| 51 | Thumeya Rashid Ngushi | 11/01/2019 | 30/06/2021 | 354 |
| 52 | Stara Makame Ameir | 11/01/2019 | 30/06/2021 | 354 |
| 53 | Sleyum Said Khamis | 14/09/2017 | 30/06/2021 | 838 |
| 54 | Silima Haji Ussi | 11/01/2019 | 30/06/2021 | 354 |
| 55 | Seleman Mwiga Silima | 05/06/2019 | 30/06/2021 | 209 |
| 56 | Seif Uweza Foum | 11/01/2019 | 30/06/2021 | 354 |
| 57 | Salum Suleiman Mkasi | 11/01/2019 | 30/06/2021 | 354 |
| 58 | Salum Bakar Saad | 01/02/2018 | 30/06/2021 | 698 |
| 59 | Salha Mkuwi Hamza | 11/01/2019 | 30/06/2021 | 354 |
| 60 | Sadik Ameir Makame | 05/06/2019 | 30/06/2021 | 209 |
| 61 | Sadam Hussein Khamis | 11/01/2019 | 30/06/2021 | 354 |
| 62 | Rose Hillary Mbuya | 09/01/2019 | 30/06/2021 | 356 |
| 63 | Rahma Mohamed Said | 05/06/2019 | 30/06/2021 | 209 |
| 64 | Rafii Hassan Juma | 07/01/2015 | 30/06/2021 | 1,819 |
| 65 | Nassor Omar Saleh | 11/01/2019 | 30/06/2021 | 354 |
| 66 | Nassir Salum Ali | 07/01/2015 | 30/06/2021 | 1,819 |
| 67 | Mzee Khamis Moh'd | 07/01/2015 | 30/06/2021 | 1,819 |
| 68 | Mzee Ali Mzee | 11/01/2019 | 30/06/2021 | 354 |
| 69 | Mussa Makame Kassim | 07/01/2019 | 30/06/2021 | 358 |
| 70 | Mpaji Juma Haji | 11/01/2019 | 30/06/2021 | 354 |
| 71 | Mohamed Abass Abdulla | 11/01/2019 | 30/06/2021 | 354 |
| 72 | Mkasi Mtumwa Saleh | 11/01/2019 | 30/06/2021 | 354 |
| 73 | Makame Juma Ame | 11/01/2019 | 30/06/2021 | 354 |
| 74 | Maryam Shaaban Mabundu | 11/01/2019 | 30/06/2021 | 354 |
| 75 | Madina Juma Zubeir | 11/01/2019 | 30/06/2021 | 354 |
| 76 | Khamis Omar Makame | 11/01/2019 | 30/06/2021 | 354 |
| 77 | Kassim Mohamed Omar | 11/01/2019 | 30/06/2021 | 354 |
| 78 | Juma Omar Mohamed | 11/01/2019 | 30/06/2021 | 354 |
| 79 | Izhaka Mselem Issa | 07/01/2015 | 30/06/2021 | 1,819 |
| 80 | Hassan Maulid Makame | 11/01/2019 | 30/06/2021 | 354 |
| 81 | Haji Shukuru Makame | 11/01/2019 | 30/06/2021 | 354 |
| 82 | Haji Khamis Omar | 11/01/2019 | 30/06/2021 | 354 |
| 83 | Haidar Juma Khamis | 05/01/2019 | 30/06/2021 | 360 |
| 84 | Hafidh Khamis Kalamu | 06/05/2019 | 30/06/2021 | 239 |
| 85 | Hadia Abass Mrisho | 07/06/2014 | 30/06/2021 | 2,033 |
| 86 | Fatma Mbarouk Nassor | 11/01/2019 | 30/06/2021 | 354 |
| 87 | Farida Masoud Ame | 11/01/2019 | 30/06/2021 | 354 |
| 88 | Biubwa Haji Ussi | 11/01/2019 | 30/06/2021 | 354 |

| Nambari | Jina Kamili | Tarehe ya Ajira | Tarehe ya Ukaguzi | Siku alizochelewa kuthibitishwa |
|---|---|---|---|---|
| 89 | Bahati Abdalla Kassim | 11/01/2019 | 30/06/2021 | 354 |
| 90 | Amour Khamis Juma | 11/01/2019 | 30/06/2021 | 354 |
| 91 | Amour Haji Ibrahim | 07/01/2015 | 30/06/2021 | 1,819 |
| 92 | Aisha Mohamed Naim | 11/01/2019 | 30/06/2021 | 354 |
| 93 | Ahmed Khatib Abdalla | 11/01/2019 | 30/06/2021 | 354 |
| 94 | Ahmed Haji Haji | 07/01/2015 | 30/06/2021 | 1,819 |
| 95 | Adam Moh'd Salum | 05/06/2019 | 30/06/2021 | 209 |
| 96 | Adam Juma Mpwani | 11/01/2019 | 30/06/2021 | 354 |
| 97 | Abdulshakur Bakar Shaaban | 11/01/2019 | 30/06/2021 | 354 |
| 98 | Abdulkarim Ali Mussa | 11/01/2019 | 30/06/2021 | 354 |
| 99 | Abdulaaziz Zahran Mohamed | 14/09/2017 | 30/06/2021 | 838 |
| 100 | Abdullatif Ibrahim Salmin | 11/01/2019 | 30/06/2021 | 354 |
| 101 | Abdi Mohamed Mwinyi | 19/06/2015 | 30/06/2021 | 1,656 |
| 102 | Abdalla Ali Sharif | 11/01/2019 | 30/06/2021 | 354 |
| 103 | Pili Kitwana Mustafa | 01/11/2019 | 30/06/2021 | 60 |
| 104 | Mwanaidi Amour Ibrahim | 01/11/2019 | 30/06/2021 | 60 |
| 105 | Zubeid Ali Haji | 01/11/2019 | 30/06/2021 | 60 |
| 106 | Sumaiya Ali Makame | 11/01/2019 | 30/06/2021 | 354 |
| 107 | Ali Mohamed Ali | 11/01/2019 | 30/06/2021 | 354 |
| 108 | Suleiman Zamani Mshenga | 11/01/2019 | 30/06/2021 | 354 |
| 109 | Haji Ali Ameir | 11/01/2019 | 30/06/2021 | 354 |
| 110 | Chum Salum Chum | 11/01/2019 | 30/06/2021 | 354 |
| 111 | Asha Ali Yussuf | 06/03/2015 | 30/06/2021 | 1,761 |
| 112 | Hassan Silima Ali | 06/03/2015 | 30/06/2021 | 1,761 |
| 113 | Khadija Abdalla Khamis | 11/08/2019 | 30/06/2021 | 142 |
| 114 | Asha Haji Masoud | 05/08/2019 | 30/06/2021 | 148 |
| 115 | Tatu Juma Ussi | 11/05/2019 | 30/06/2021 | 234 |
| 116 | Mtumwa Mohd Tahir | 05/06/2019 | 30/06/2021 | 209 |
| 117 | Fauzia Ibrahim Iddi | 05/06/2019 | 30/06/2021 | 209 |
| 118 | Mwajuma Banzi Mgongo | 05/06/2019 | 30/06/2021 | 209 |
| 119 | Mpaji Hakimu Suleiman | 05/03/2019 | 30/06/2021 | 301 |
| 120 | Mpaji Shadhil Ali | 05/03/2019 | 30/06/2021 | 301 |
| 121 | Amina Rajab Salum | 05/03/2019 | 30/06/2021 | 301 |
| 122 | Abass Hafuru Abdulrhman | 05/03/2019 | 30/06/2021 | 301 |
| 123 | Khamis Machano Ali | 05/03/2019 | 30/06/2021 | 301 |
| 124 | Ibrahim Yahya Yussuf | 05/03/2019 | 30/06/2021 | 301 |
| 125 | Laila Haroub Hassan | 11/01/2019 | 30/06/2021 | 354 |
| 126 | Ruzuna Othman Ameir | 11/01/2019 | 30/06/2021 | 354 |
| 127 | Neema Abdi Basha | 11/01/2019 | 30/06/2021 | 354 |
| 128 | Teresia Victo Fabian | 11/01/2019 | 30/06/2021 | 354 |
| 129 | Terezia Lazaro Yakoub | 11/01/2019 | 30/06/2021 | 354 |
| 130 | Warda Ali Vuaa | 11/01/2019 | 30/06/2021 | 354 |
| 131 | Lucy Michael Shija | 11/01/2019 | 30/06/2021 | 354 |
| 132 | Maryam Borafya Hamza | 11/01/2019 | 30/06/2021 | 354 |
| 133 | Maryam Jecha Salum | 11/01/2019 | 30/06/2021 | 354 |

| Nambari | Jina Kamili | Tarehe ya Ajira | Tarehe ya Ukaguzi | Siku alizochelewa kuthibitishwa |
|---|---|---|---|---|
| 134 | Khamis Amour Khamis | 11/01/2019 | 30/06/2021 | 354 |
| 135 | Pandu Mbata Pandu | 11/01/2019 | 30/06/2021 | 354 |
| 136 | Salma Bakil Abdalla | 11/01/2019 | 30/06/2021 | 354 |
| 137 | Selina Gerphas Bundala | 11/01/2019 | 30/06/2021 | 354 |
| 138 | Rehema Abdalla Sanga | 11/01/2019 | 30/06/2021 | 354 |
| 139 | Chiku Juma Ali | 11/01/2019 | 30/06/2021 | 354 |
| 140 | Patima Makame Ali | 11/01/2019 | 30/06/2021 | 354 |
| 141 | Issa Shija Magulu | 11/01/2019 | 30/06/2021 | 354 |
| 142 | Ali Seif Salum | 11/01/2019 | 30/06/2021 | 354 |
| 143 | Hidaya Silima Juma | 11/01/2019 | 30/06/2021 | 354 |
| 144 | Eliza Joseph Edward | 11/01/2019 | 30/06/2021 | 354 |
| 145 | Othman Juma Othman | 05/08/2018 | 30/06/2021 | 513 |
| 146 | Machano Bakari Haji | 05/01/2019 | 30/06/2021 | 360 |
| 147 | Raya Khamis Abdalla | 11/01/2019 | 30/06/2021 | 354 |
| 148 | Abdallah Athuman Ramadhan | 11/01/2019 | 30/06/2021 | 354 |
| 149 | Khadija Mzee Nadhardeen | 11/01/2019 | 30/06/2021 | 354 |
| 150 | Oliva Tomas Ramadhan | 11/01/2019 | 30/06/2021 | 354 |
| 151 | Mosi Abdalla Haji | 11/01/2019 | 30/06/2021 | 354 |
| 152 | Hamad Suleiman Ali | 05/06/2019 | 30/06/2021 | 209 |
| 153 | Mtumwa Mohamed Kassim | 05/06/2019 | 30/06/2021 | 209 |
| 154 | Fatma Juma Mussa | 05/06/2019 | 30/06/2021 | 209 |
| 155 | Zuwena Issa Mgongo | 01/05/2016 | 30/06/2021 | 1,339 |
| 156 | Vuai Mkoko Hassan | 07/01/2014 | 30/06/2021 | 2,184 |
| 157 | Idrissa Ibrahim Jaji | 05/06/2019 | 30/06/2021 | 209 |
| 158 | Asma Othman Khamis | 17/04/2015 | 30/06/2021 | 1,719 |
| 159 | Ame Juma Ali | 19/06/2015 | 30/06/2021 | 1,656 |
| 160 | Miraji Ajae Seremala | 07/01/2015 | 30/06/2021 | 1,819 |
| 161 | Riziki Ikrabu Daud | 11/01/2019 | 30/06/2021 | 354 |
| 162 | Khamis Juma Makame | 11/01/2019 | 30/06/2021 | 354 |
| 163 | Ruzuna Othman Mussa | 01/11/2019 | 30/06/2021 | 60 |
| 164 | Salma Bakil Abdalla | 01/11/2019 | 30/06/2021 | 60 |
| 165 | Neema Abdi Basha | 01/11/2019 | 30/06/2021 | 60 |

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 9 (2) cha Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2014.Vile vile kutokuwathibitisha watumishi hao kunaweza kuwakosesha stahiki na haki zao za kazi.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wizara kuchukua hatua za kuwathibitisha watumishi hao ili kuendana na sheria na kanuni za umtumishi wa umma.

### 6.11.1.8 Mapungufu katika Ujazaji wa Kalamazoo za Watumishi

Ukaguzi umebaini kitengo cha utumishi chenye dhamana ya kutunza kumbukumbu za watumishi ikiwa pamoja na kujaza Kalamazoo hawajazi Kalamazoo hizo kwa ukamilifu wa taarifa zote za mtumishi hadi kufikia mwezi husika, Kalamazoo nyingi zilizojazwa taarifa zake zimeishia mwaka 2020.

Kutokujaza kwa ukamilifu kunaweza kupelekea usumbufu katika kutambua kwa uhakika taarifa za mtumishi aidha inaweza kupelekea kukosekana taarifa kamili pale wanapojiandaa kumtengenezea haki za kiinua mgongo na pensheni pindi mfanyakazi anapostaafu.

Kusita kujaza taarifa za mtumishi kunaweza kupelekea kuharibu mtiririko mzuri wa taarifa za stahiki na mikato ya mtumishi.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wizara kuhakikisha unaandaa usimamizi mzuri ili kuweza kuhakikisha taarifa za wafanyakazi zinajazwa kikamilifu.

### 6.11.1.9 Kutokununua Vifaa vya Kuandika kutoka kwa Wakala wa Mchapaji wa Serikali na Bohari Kuu.

Kifungu nambari 35 cha Sheria ya Wakala wa Serikali wa Uchapaji Zanzibar ya mwaka 2018 kimezitaka Taasisi zote za Serikali kupeleka kazi zake zote za uchapaji na mahitaji ya vifaa vya ofisi na vya kuandikia kwa Wakala wa Uchapaji wa Serikali Zanzibar.

Ukaguzi umebaini Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo iliafanya manunuzi ya vifaa vya kuandikia kutoka kwa wasamabazaji wengine na jumla shilingi 58,274,141 zilitumika kwa ajili manunuzi ya vifaa hivyo kutoka kwa wasambazaji ambao hawakuruhusiwa kisheria, Jadweli namabri 10 linaanisha:-

**Jadweli Nambari 191**:**Manunuzi ya Uchapaji na Vifaa vya Kuandikia**

| Code | Maelezo | Kima |
|---|---|---|
| 6112208 | Manunuzi ya Kompyuta | 17,513,088 |
| 6112209 | Manunuzi ya Mashine ya Kuchapishia (Printer) | 1,700,500 |
| 2206001 | Manunuzi ya Vifaa vya Kuandikia | 34,447,749 |
| 2206002 | Gharama za Uchapaji | 14,610,443 |
| 2206005 | Vifaa vya Kompyuta | 2,689,833 |
| **Jumla** | | **70,961,613** |

Kutokufuata utaratibu ambao umewekwa na serikali katika ununuzi wa vifaa vya ofisi ni kwenda kinyume na sheria ya 35(1) ya kifungu cha Wakala wa Serikali wa Uchapaji Zanzibar cha mwaka 2018.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wizara kufuata sheria na kuanza kununua vifaa hivyo kama ilivyoelekezwa na sheria.

### 6.11.1.10 Kuwepo kwa Vyombo vya Moto vilivyolala kwa Muda Mrefu

Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo inamiliki vyombo vya aina tofauti vya usafiri, Ukaguzi umebaini baadhi ya vyombo hivyo vimelala kwa sababu ya ubovu kwa muda mrefu sasa. Kuwacha vyombo vya moto vikiwa vimelala kwa muda mrefu kunaweza kupelekea kuitia hasara kubwa Wizara kwa kuongezeka kwa gharama za matengenezo au kupelekea kutotengenezeka kabisa. Baadhi ya magari yaliyolala ni kama ifuatavyo katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 192 : Orodha ya Magari yaliyolala kwa Muda Mrefu.**

| Namba | Namba za Gari | Idara Inayotoka |
|---|---|---|
| 1. | SMZ 316 A Nissan<br>SMZ 166 B Nissan | Idara ya umwagiliaji maji. |
| 2. | SMZ 522 Toyota | Idara ya misitu |
| 3. | SMZ 478 A | Idara ya mifugo |
| 4. | SMZ 203 A Nissan | Idara ya mipango. |
| 5. | SMZ 136 A<br>SMZ 174 A | Taasisi ya utafiti |
| 6. | SMZ 603 A | Idara ya kilimo. |
| 7 | SMZ 166 A | Taasisi ya utafiti wa kilimo kizimbani |

Kuviacha vyombo hivyo vikiwa vimelala kwa ajili ya ubovu kunaweza kupelekea kuharibika kabisa na kutoweza kutumika tena.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wizara kuvitengeneza vyombo hivyo ili kupata tija katika shughuli za kiutendaji.

### 6.11.1.11 Kutokukata Bima kwa Ajili ya Vyombo vya Moto vya Wizara

Ukaguzi umebaini Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo haikuchukua hatua za tahadhari kwa kuvikatia bima vyombo vyake ili kuiepusha Wizara na hasara za matengenezo endapo kutatokea ajali. Orodha ya gari ambazo hazijakatiwa bima zinaonekana katika jadweli hapo chini.

**Jadweli Nambari 193:Orodha ya Gari Zisizokuwa na Bima**

| Namba | Namba ya Gari | Tarehe iliyokatiwa Bima | Tarehe iliyokwisha Bima |
|---|---|---|---|
| 1. | SMZ 382 B | 05/04/2019 | 04/04/2020 |
| 2. | SMZ 653 A | 05/04/2019 | 04/04/2020 |
| 3. | SMZ 785 A | 05/04/2019 | 04/04/2020 |
| 4. | SMZ 383 B | 05/04/2019 | 04/04/2020 |

Kutovikinga vyombo kwa kuvikatia bima inaonesha udhaifu wa Wizara katika kujilinda na majanga yanayoweza kuleta hasara kwa Mali zinazomilikiwa na Wizara.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wizara kuvitengeneza vyombo hivyo ili kupata tija katika shughuli za kiutendaji.

## IDARA YA MAENDELEO YA MIFUGO ZANZIBAR

### 6.11.1.12 Dosari katika Ukusanyaji wa Tozo za Leseni ya Mbwa

Ukaguzi ulizungumza na maofisa wa Idara ya Maendeleo ya Mifungo pamoja kupitia Sheria namabri 11 ya Usimamaizi wa Rasilimali za Wanyama ya mwaka 1999 na taarifa za mapato za Idara ya Maendeleo ya Mifugo ili kujua vyanzo vya mapato vya Idara hiyo.

Kwa mujibu wa kifungu nambari 58, 59 na 60 vya Sheria namabri 11 ya Usimamaizi wa Rasilimali za Wanyama ya mwaka 1999 vinaonesha chanzo cha mapato cha Leseni za Mbwa ambao wana umri wa zaidi ya miezi mitatu na utaratibu wa udhibiti wake.

Ukaguzi ulipitia Jadweli la Saba (Malipo ya Tozo na Ada kwa Huduma za Mifugo) la Sheria namabri 11 ya Usimamaizi wa Rasilimali za Wanyama ya mwaka 1999 pamoja na taarifa za mapato za Idara ya Maendeleo ya Mifugo na kubaini kwamba chanzo hicho cha mapato hakikutumika katika ukusanyaji wa mapato ya mwaka wa fedha 2020-2021.

Kutokutumika kwa chanzo hicho cha mapato kunaweza kusababisha upungufu wa ukusanyaji wa mapato ya Idara na kufanya hivyo ni kwenda kinyume ya vifungu nambari 58, 59 na 60 vya Sheria namabri 11 ya Usimamaizi wa Rasilimali za Wanyama ya mwaka 1999.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wizara kutumia vyanzo vyake vya mapato kikamilifu ili kuongeza kima cha mapato ya Serikali.

**IDARA YA MISITU ZANZIBAR**

### 6.11.1.13 Kutokuandaa Taarifa za Hesabu za Mfuko wa Maendeleo ya Misitu za mwaka wa fedha 2020-2021

Ukaguzi umebaini kwamba Idara ya Misitu inamiliki Mfuko wa Maendeleo ya Misitu ambao unafanya shuhuli za maendeleo ya misitu kwa kupokea mapato na kufanya matumizi kupitia hesabu ya Benki kama inavyoainishwa katika jadweli hapo chini.

**Jadweli Nambari 194: Muhtasari wa Nambari ya Benki ya Mfuko wa Maendeleo ya Misitu kwa Mwaka wa Fedha 2020 - 2021**

| Maelezo | 2020 - 2021 |
|---|---|
| Nambari ya Benki | 404206000 |
| Jina la Nambari ya Benki | MFUKO WA MAENDELEO YA MISITU |
| Benki na Tawi | PBZ - Forodhani Branch |
| Bakaa ya Mwanzo wa Mwaka | 12,367,920.02 |
| Mapato 2020 – 2021 | 215,206,846.13 |
| Matumizi 2020 -2021 | 157,286,676.50 |
| Fedha Zilizorejeshwa | |
| Gharama za Benki | 386,916.83 |
| Bakaa ya Mwisho wa Mwaka | 69,901,172.82 |

Aidha; kwa mujibu wa kifungu nambari 82 (3) cha Sheria nambari 10 ya Usimamizi na Uhifadhi wa Rasilimali za Misitu ya mwaka 1996, kinamtaka Msimamizi wa Misitu (Forest Administrartor) kuandaa Taarifa za Kifedha za kila mwaka ambazo zitakaguliwa na kujumuishwa katika Taarifa ya Mfuko wa Maendeleo na kuwasilishwa kwa Waziri mwenye dhamana.

Kufanya hivyo ni kuenda kinyume na kifungu nambari 82 (3) cha Sheria nambari 10 ya Usimamizi na Uhifadhi wa Rasilimali za Misitu ya mwaka 1996. Vile vile ni kuenda kinyume na kifungu nambari 120(1) na kifungu nambari 119(1) vya Sheria nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wizara kuhakikisha hesabu za mfuko wa maendeleo ya misitu zinafungwa kwa wakati na kuwasilishwa sehemu zote husika kama matakwa ya sheria ya Mfuko yalivyoamrisha.

### 6.11.1.14 Kukosekana kwa Taarifa za Kielektroniki za Mapato ya Mchanga yanayokusanywa kwa Makampuni

Ukaguzi ulifanya mahojiano na watumishi wenye dhamana ya mapato ya Mchanga na kubaini kwamba Idara ya Misitu ilikuwa inatumia Mfumo wa Kielectroniki (Mail Merge) kwa ajili ya kutunzia kumbu kumbu za Vibali vya Mchanga. Taarifa hizo zilitayarishwa na kutunzwa katika makundi matatu amabayo ni:-

a) Taarifa za Vibali vya Mchanga kwa Makampuni na Miradi.

b) Taarifa za Vibali vya Mchanga kwa Viwanda vya Matofali.

c) Taarifa za Vibali vya Mchanga kwa Wananchi wa Kawaida.

Ukaguzi ulihitaji kupatiwa Taarifa hizo na kuzikosa Taarifa za Vibali vya Mchanga kwa Makampuni na Miradi. Aidha, Ukaguzi ulihitaji maelezo ya kukosekana kwa Taarifa na kupata maelezo ya kwamba Kompyuta iliyokuwa ikitumika kuhifadhia Taarifa hizo liharibika na Idara ya Misitu haikuwa na nakala yake.

Hadi kumalizika kwa Ukaguzi wa mwaka wa fedha 2020/2021, Taarifa za Vibali vya Mchanga kwa Makampuni na Miradi hazikupatikana kwa ajili ya Ukaguzi.

Kufanya hivyo ni kuenda kinyume na vifungu namabri 27 (2)(a), 32 (2) na 34 (1) vya Sheria nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wizara kuhakikisha unalisimamia suala la upatikana wa taarifa za kieletroniki za mapato ya mchanga na kuziwasilishwa kwa ajili ya kukamilisha ukaguzi.

### 6.11.1.15 Kutopatikana kwa baadhi ya vitabu vya mapato kwa Ukaguzi katika Idara ya Misitu

Ukaguzi uliomba taarifa za mapato ya Idara pamoja na kumbukumbu za ukusanyaji wa mapato hayo kwa ajili ya kazi za ukaguzi wa mapato. Aidha, baadhi ya vitabu vya risiti vilivyotakiwa kuwasilishwa kwa ukaguzi havikupatikana hadi kumalizika kwa Ukaguzi na hali hiyo kupelekea ukaguzi kushindwa kujiridhisha usahihi wa taarifa za mapato ya Idara. Jadweli hapo chini linaonesha orodha ya vitabu hivyo.

**Jadweli Nambari 195: Orodha ya Vitabu vya Stakabadhi Ambavyo Havikupatikana kwa Ukaguzi.**

| Namba | Tarehe | Nambari ya Mwanzo ya Stakabadhi | Nambari ya Mwisho ya Stakabadhi | Idadi ya Vitabu vya Stakabadhi Vilivyokosekana kwa Ukaguzi |
|---|---|---|---|---|
| 1. | 1.8.2020 | 604901 | 604950 | 1 |
| 2. | 3.8.2020 | 604951 | 605000 | 1 |
| 3. | | 605051 | 605100 | 1 |
| 4. | 4.8.2020 | 605001 | 605050 | 1 |
| 5. | | 605101 | 605150 | 1 |
| 6. | 5.8.2020 | 605151 | 605300 | 3 |
| 7. | 6.8.2020 | 605301 | 605400 | 2 |

| Namba | Tarehe | Nambari ya Mwanzo ya Stakabadhi | Nambari ya Mwisho ya Stakabadhi | Idadi ya Vitabu vya Stakabadhi Vilivyokosekana kwa Ukaguzi |
|---|---|---|---|---|
| 8. | 7.8.2020 | 605401 | 605450 | 1 |
| 9. | | 681601 | 681650 | 1 |
| 10. | 10.8.2020 | 681651 | 681800 | 3 |
| 11. | 11.8.2020 | 681801 | 681900 | 2 |
| 12. | 12.8.2020 | 681901 | 682000 | 2 |
| 13. | 13.8.2020 | 676501 | 676600 | 2 |
| | 14.8.2020 | 626001 | 626100 | 2 |
| 14. | 15.8.2020 | 622101 | 622200 | 2 |
| 15. | 17.9.2020 | 723751 | 723800 | 1 |
| 16. | 2.10.2020 | 670851 | 670900 | 1 |
| 17. | 9.1.2021 | 7001 | 7200 | 4 |
| 18. | 13.1.2021 | 7201 | 7300 | 2 |
| 19. | | 10751 | 10800 | 1 |
| 20. | 14.1.2021 | 10801 | 10950 | 3 |
| 21. | 15.1.2021 | 10951 | 11050 | 2 |
| 22. | 16.1.2021 | 11051 | 11150 | 2 |
| 23. | 18.1.2021 | 11151 | 11250 | 2 |
| 24. | 19.1.2021 | 32201 | 32250 | 1 |
| 25. | | 32101 | 32150 | 1 |
| 26. | 20.1.2021 | 32151 | 32200 | 1 |
| 27. | | 32251 | 32400 | 3 |
| 28. | 21.1.2021 | 32401 | 32550 | 3 |
| 29. | 23.1.2021 | 32651 | 32750 | 2 |
| 30. | 22.1.2021 | 32551 | 32600 | 1 |
| 31. | 25.1.2021 | 32601 | 32650 | 1 |
| 32. | | 67001 | 67100 | 2 |
| 33. | 26.1.2021 | 32751 | 32850 | 1 |
| 34. | | 67101 | 67150 | 2 |
| 35. | 27.1.2021 | 67151 | 67300 | 3 |
| 36. | 28.1.2021 | 67301 | 67400 | 2 |
| 37. | 29.1.2021 | 67401 | 67500 | 2 |
| 38. | 30.1.2021 | 66701 | 66800 | 2 |
| **Jumla** | | | | **70** |

Kufanya hivyo kunapelekea kutokukamilika kwa taarifa zinazohitajika kwa ajili ya ukaguzi hivyo kushindwa kutoa maoni ya ukaguzi kuhusu taarifa za fedha za Wizara.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wizara kuhakikisha unawasilishwa vitabu hivyo ili kuweza kukamilisha ukaguzi.

### 6.11.1.16 Malipo ya Posho yaliyolipwa Bila ya Toleo Maalum

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba kuna maposho ambayo yamelipwa bila ya kuwepo kwa ruhusa maalum ambayo inaidhinisha kulipwa kwa maposho hayo. Aidha ukaguzi umeshindwa kupata orodha maalum ya wanaostahiki kulipwa maposho hayo.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016. Malipo yenyewe ni kama yafuatayo:-

**Jadweli Nambari 196 : Malipo ya Posho yaliyolipwa Bila ya Toleo Maalum**

| Hati Namba | Hundi Namba | Thamani (Tshs) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 06/10 | 001264 | 4,420,000 | Mfuko wa maendeleo ya misitu | Ikiwa ni malipo ya posho maalum kwa mwezi wa Agosti 2020 kwa watendaji wa mchanga |

Kufanya malipo ya posho za watumishi bila ya kuwepo kwa toleo ni kuenda kinyume na sheria za utumishi wa umma.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa idara kuwasilisha dokezo lililoruhusu malipo ya posho ili kufanyiwa ukaguzi wa mara ya pili.

### 6.11.1.17 Uhamishaji wa Vitabu 109 vya Stakabadhi bila ya kuwepo kwa maandishi kutoka Idara ya Misitu kwenda Wizara ya Ardhi

Awali, Taasisi za Umma huchukua Vitabu vya stakabadhi kutoka Ofisi ya Rais Fedha na Mipango, kwa jukumu la kuvitunza na kuvitumia kwa dhumuni la kukusanya mapato ili kupata uhalali wa mapato hayo.

Ukaguzi umebaini kwamba Idara ya Misitu ilitoa jumla ya vitabu vya stakabadhi 109 na kuvipeleka Wizara ya Ardhi bila ya kuwepo kwa barua ya makabidhiano hali ambayo inaweza kupelekea kutokea kwa upotevu au udanganyifu.

Orodha ya vitabu vya stakabadhi vilivyopelekwa Wizara ya Ardhi vinaonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 197**:**Orodha ya vitabu vilivyopelekwa Wizara ya Ardhi Bila ya Idhini ya Kimaandishi**

| Namba | Jina la Mtumishi Aliechukua Vitabu | Nambari ya Mwanzo ya Stakabadhi | Nambari ya Mwisho ya Stakabadhi | Idadi ya Vitabu vya Stakabadhi Vilivyochukuliwa |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Juma Khamis Ame | 749501 | 749600 | 2 |
| | - | 001751 | 001850 | 2 |
| | - | 034401 | 035100 | 3 |
| | - | 001851 | 002000 | 3 |
| 2. | Time Shaame | 709651 | 709700 | 1 |
| | | 004851 | 005000 | 3 |
| 3. | Haji Ali Haji | 747001 | 747050 | 1 |
| | | 006251 | 006450 | 3 |
| 4. | Tausi Shaaban | 032101 | 032850 | 15 |
| | | 007001 | 007300 | 6 |
| 5. | Abdalla Abeid Yakut | 011251 | 011400 | 3 |
| 6. | Fatma Salum | 010751 | 011250 | 10 |
| 7. | Moh'd Tahir Moh'd | 004451 | 004550 | 2 |

| Namba | Jina la Mtumishi Aliechukua Vitabu | Nambari ya Mwanzo ya Stakabadhi | Nambari ya Mwisho ya Stakabadhi | Idadi ya Vitabu vya Stakabadhi Vilivyochukuliwa |
|---|---|---|---|---|
| | | 003601 | 004450 | 16 |
| 8. | Rukia Mustafa | 000501 | 001000 | 10 |
| 9. | Fatma Amar | 007551 | 008000 | 9 |
| 10. | Haji Khamis | 032851 | 033350 | 10 |
| 11. | Haruna Abdallah | 033851 | 034350 | 10 |
| **Jumla** | | | | **109** |

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 27 cha Sheria nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wizara kufuata taratibu za Makabidhiano kwa kuweka kumbukumbu za kimaandishi.

### 6.11.1.18 Kukosekana kwa Daftari la Vifungu la Idara ya Misitu

Barua rasmi ya Katibu Mkuu wa Ofisi ya Rais Fedha na Mipango ya tarehe 9 Juni 2021 yenye kumbu kumbu nambari AD.5/184/01/01/80 kuenda kwa Taasisi za Umma ilielekeza kwamba " Matumizi yote yaliyofanywa mwaka 2020/2021 yaingizwe katika "Vote Book" kwa mujibu wa Kasma husika. Aidha "Vote Book" zifungwe kwa ajili ya kukaguliwa."

Ukaguzi umebaini kwamba Idara ya Misitu ilifanya matumizi ya shilingi 798,466,751.94 kupitia Nambari za Benki kama jadweli nambari 18 linavyoanisha hapo chini.

Aidha; Ukaguzi umebaini Idara ya Misitu haikuwa na Daftari la vifungu hali ambayo inasababisha ugumu katika kazi za Ukaguzi.

**Jadweli Nambari 198**:**Matumizi ya Idara ya Misitu kupitia Misitu kwa Mwaka wa Fedha 2020 - 2021**

| Nambari ya Benki | Jina la Nambari ya Benki | Jina la Benki na Tawi | Matumizi kwa mwaka 2020 -2021 (Tshs) | Jumla (Tshs) |
|---|---|---|---|---|
| 404206000 | Mfuko wa Maendeleo ya Misitu | PBZ - Forodhani Branch TZS | 157,286,676.50 | 157,286,676.50 |
| 730065001 | Jozani Chwaja Bay Conservation | PBZ - Forodhani Branch TZS | 641,180,075.44 | 641,180,075.44 |
| **Jumla** | | | | **798,466,751.94** |

Kutotumia Daftari la vifungu kunasababisha mambo yafuatayo:-

- Kumsababishia mkaguzi mzunguko mrefu wa kujua uwiano wa hesabu katika kila kasma (Component) na uhalisia wa matumizi.
- Kufanya uhaulishaji wa vifungu bila kuzingatia sheria na kujificha kwa taarifa endapo mkaguzi hatokuwa na upeo mkubwa katika kazi zake.

Kusababisha kutoelewana kwa mkaguzi na mkaguliwa na kuleta uhusiano mbaya endapo mkaguzi atakapotaka kuchambuliwa taarifa hizo ili kujiridhisha kama ilivyo katika lengo mojawapo la ukaguzi n.k.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wizara kuanzisha matumizi ya Daftari la Vifungu kwa ajili ya utunzaji mzuri wa hesabu.

**6.11.1.19 Kufanya Matumizi ya shilingi 798,466,751.94 Bila ya Mpango wa Manunuzi wa Idara ya Misitu**

Kifungu nambari 29 (e) na kifungu nambari 42 (2) vya Sheria namabri 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016 vinaitaka Taasisi ya Umma kuandaa na kutangaza mpango wa manunuzi na uondoshaji wa mali za Umma.

Vile vile kifungu nambari 42 (7) kimeeleza kwamba ununuzi hautofanyika kinyume na mpango wa ununuzi na uondoshaji wa mali za umma isipokuwa kwa hali ya haraka na dharura.

Ukaguzi umebaini Idara ya Misitu ilifanya manunuzi yenye thamani ya shilingi 798,466,751.94 kupitia Hesabu za Benki namabri 404206000 na 730065001 kama inavyoanishwa katika jadweli nambari 18 hapo juu. Aidha, Ukaguzi umebaini manunuzi hayo yalifanywa katika hali ya kawaida bila ya kuwepo kwa mpango huo wa manunuzi.

Kufanya hivyo ni kuenda kifungu nambari 42 (7) cha Sheria namabri 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wizara kuhakikisha wanandaa mpango wa manunuzi wa mwaka (Annual Procurement Plan) ili kuepukana na manunuzi holela.

**6.11.1.20 Kutopatikana kwa ripoti ya tathmini ya malipo ya Fidia Shilingi 32,248,400**

Idara ya misitu na mali zisizorejesheka imefanya malipo kwa ajili ya fidia kwa wakulima wa Kiombamvua waliothirika na shughuli za uchimbaji wa mchanga, hadi tunamaliza ukaguzi ripoti ya tathmini haikupatikana kwa ajili ya ukaguzi ili kuthibitisha uhalali wa viwango walivyolipwa kwa Waathirika. Malipo hayo yamefanyika kupitia hati namba 04/07 kupiti hesabu ya Mfuko wa Maendeleo ya Misitu.

Kufanya malipo bila ya kuambatanisha nyaraka kwa ukamilifu nikuenda kinyume na kanuni 95(4) ya kanuni za sheria ya fedha za umma.

Ukaguzi unawashauri viongozi wa idara kuwasilisha ripoti ya tathmini kwa ajili ya kufanyiwa ukaguzi.

**6.11.1.21 Dosari katika Hifadhi ya Taifa ya Jozani**

Ukaguzi ulifanya mazungumzo na watumishi wa Hifadhi ya Taifa Jozani kwa lengo la kujua hali halisi ya uendeshaji wa hifadhi hiyo. Ukaguzi ulibani mbali mbali katika hifadhi hiyo kama zinavyoanishwa hapo chini:-

**a) Kukosekana kwa Mihutasari ya Vikao vya Kamati ya Kiintelijensia ya Hifadhi ya Taifa ya Jozani**

Vifungu namabari 10 na 11 vya Kanuni ya Hifadh ya Ukanda Jozani Chakwa ya mwaka 2018 iliyotolewa katika Gazeti Rasmi la Serikali nambari 62 vimetambulisha na kutaja kazi za Kamati ya Kiintekigenisia.

Ukaguzi ulitaka kuona mihutasari ya vikao vya kamati hiyo ili kujiridhisha utekelezaji wa majukumu yake ya kiusalama na uimarishaji wa mahusiano mazuri na wadau wanaoizunguka Hifadhi ya Taifa ya Jizani.

Hadi kumalizika kwa Ukaguzi mihutasari ya vikao vya kamati hiyo haikupatikana kwa ajili ya Ukaguzi.

**b) Kutokuwepo kwa Bodi ya Ushauri ya Hifadhi ya Taifa ya Jozani**

Kwa mujibu wa kifungu nambari 12 cha Kanuni ya Hifadh ya Ukanda Jozani Chwaka ya mwaka 2018 kinaitaka Hifadhi ya Taifa ya Jozani kuwa na Bodi ya Ushauri ambayo utendaji wake umetajwa katika kifungu nambari 13 hadi 16 vya Kanununi hiyo.

Ukaguzi umebaini kwamba Hifadhi ya Taifa ya Jozani haikuwa na Bodi ya Ushauri kwa mwaka wa fedha uliomalizika tarehe 30 Juni, 2021.

**c) Mapato ya Mgahawa kutumika kwa kulipa Posho la muda wa ziada kwa Wafanyakazi wa Hifadhi ya Taifa Jozani bila ya Idhini ya Kiimandishi.**

Ukaguzi ulifanya mazungumzo na uongozi wa Hifadhi ya Taifa ya Jozani na kubaini kuwepo kwa Mgahawa katika hifadhi hiyo ambao mapato yanayopatikana katika mgahawa huwo hutumika kwa kulipa posho la muda wa ziada kwa wafanyakazi wa hifadhi hiyo.

Ukaguzi ulihoji na kuomba kupatiwa ruhusa ya kiimandishi iliyodhinisha kufanyika hivyo.

Hadi kumalizika kwa ukaguzi ruhusa ya kufanya hivyo haikupatikana kwa ajili ya Ukaguzi.

**d) Kukosekana kwa Mikataba ya Makampuni yanayotembeza Wageni kwa Mkopo katika Hifadhi ya Msitu wa Jozani**

Ukaguzi umebaini Hifadhi ya Msitu wa Jozani hupokea wageni kutoka Makampuni yanayotembeza wageni hao kwa njia ya mkopo. Makampuni hayo huandaliwa Ankara za thamani ya fedha ya ada za wageni waliokwenda katika Hifadhi hiyo kwa muda wa mwezi kutoka Idara ya Misitu na baadae hulipa kupitia hesabu ya Benki ya Hifadhi ya Taifa ya Jozani.

Ukaguzi ulihitaji kupatiwa nakala za mikatba inayotoa ruhusa kwa makampuni hayo kutolipa fedha taslim wakati wakitembeza wageni katika hifadhi, hadi kumalizika kwa Ukaguzi mikataba hiyo haikupatikana.

Orodha ya Makampuni hayo yanatembeza wageni ni kama inavyonekana hapo chini:-

- Zan Tours
- Gallery
- Africa Spirit
- Madeira

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 42 (7) cha Sheria nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016.

Kufanya hivyo kunaweza kupelekea kuongezeka kwa changamoto za kiutendaji na kudhoofisha uendelezaji wa Hifadhi ya Taifa ya Jozani.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wizara kuhakikisha wanafuta taratibu na sheria kwa ajili ya uendeshaji mzuri wa Hifadhi ya Taifa ya Jozani.

#### 6.11.1.22 Dosari katika Hifadhi ya Msitu wa Asili wa Masingini

Ukaguzi ulifanya mazungumzo na watumishi wa Msitu wa Asili wa Masingini kwa lengo la kujua hali halisi ya uendeshaji wa hifadhi hiyo. Ukaguzi ulibani mbali mbali katika hifadhi hiyo kama zinavyoanishwa hapo chini:-

**a) Kutokuwepo kwa Bodi ya Ushauri ya Hifadhi ya Msitu ya Asili wa Masingini**

Kwa mujibu wa kifungu nambari 10 cha Kanuni ya Hifadhi ya Misitu ya Asili ya mwaka 2018 kinaitaka Hifadhi ya Msitu ya Asili wa Masingini kuwa na Bodi ya Ushauri ambayo utendaji wake umetajwa katika kifungu nambari 11 cha Kanununi hiyo.

Ukaguzi umebaini kwamba Hifadhi ya Msitu ya Asili wa Masingini haikuwa na Bodi ya Ushari kwa mwaka wa fedha uliomalizika tarehe 30 Juni, 2021.

**b) Uchakavu wa Miundombinu na Kukosekana kwa baadhi ya Huduma katika Hifadhi ya Msitu wa Asili wa Masingini**

Ukaguzi ulitembelea Hifadhi ya Msitu wa Asili wa Masingini tarehe 17.12.2021 kwa madhumuni ya kuona hali halisi ya hifadhi na uendeshaji wake, ukaguzi ulibaini dosari mbalimbali katika miundombinu ya hifadhi hiyo kama zifuatazo:-

- Njia ya kuingilia kwenye hifadhi ilikuwa na mabonde na hivyo hupelekea kutokufika kwa wepesi na haraka katika hifadhi ya Masingini.
- Mnara unaotumika kuangalia mji wa Zanzibar uliojengwa kwa kutumia magogo ya miti na boriti ulionekana na athari za kuoza na paa la makuti likiwa lishaharibika, pamoja na kuwa mnara huo ni chanzo kizuri cha kuingiza mapato lakini hakuna kilichoingia kwa muda mrefu.
- Vibaraza vya maeneo ya kumpumzikia wageni na Vyoo havijaendelezwa toka mwaka 2018 vilipojengwa.
- Paa la banda la mkahawa lilijengwa kwa makuti lilioneka kuwa lishaharibika hivyo kuhatarisha kuoza kwa miti na magogo yaliyojengewa mkahawa huo.

**c) Kutokuendelezwa kwa mradi wa kujenga vyoo kwa muda mrefu**

Hifadhi ya masingini ilianzisha mradi wa kujenga vyoo ndani ya hifadhi hiyo ili kuepusha usumbufu kwa wageni wanaotembelea hifadhi kadhalika wafanyakazi, ukaguzi umebaini ujenzi huo haukuendelezwa tangu uliposimama 2018 hivyo kushindwa kutatua changamoto hiyo na kupelekea kupotea kwa rasilimali fedha zilizowekezwa kwenye mradi huo na kushusha mapato ya hifadhi hiyo kwa kuondosha mvuto kunakosababishwa na kukosekana na huduma muhimu za vyoo.

**d) Idadi Isiyokidhi ya Wafanyakazi Ndani ya Hifadhi ya Masingini**

Ukaguzi umebaini Wizara ya Kilimo Umwagiliaji Maliasili na Mifugo haijaandaa mpango mzuri wa wafanyakazi kwa ajili ya kutunza hifadhi, kulinda, kutembeza wageni na kuendeleza eneo la uhifadhi, kumekuwa hakuna mbadala wa wafanyakazi wanaofariki, wanaostaafu kwa mujibu wa sheria na wanaohamishwa kikawaida hali iliyopelekea kuwepo na idadi ya chini ya wafanyakazi wanaoelekea kushindwa kutoa huduma kamilifu ndani ya hifadhi.

**e) Upungufu wa ziara za Viongozi wa Wizara na Idara Kukagua Changamoto za Hifadhi ya Masingini**

Ziara za mara kwa mara za viongozi husaidia uongozi kutambua kwa kina mafanikio na changamoto zinazoikabili sehemu husika, ukaguzi umebaini viongozi wa Wizara na idara hawana utaratibu wa kufanya ziara ndani ya hifadhi ilikutambua vikwazo wanavyokabiliana navyo watendaji. Kufanya hivyo kunadumaza jitihada za watendaji na kuongezeka kwa changamoto zitazopelekea kudumaa na huenda kutoweka kwa hifadhi hiyo.

Kuwepo kwa dosari hizo kunaweza kupelekea kuongezeka kwa changamoto za kiutendaji na kudhofisha uendelezaji wa Hifadhi ya Msitu wa Asili wa Masingini.

Uongozi wa Wizara unapaswa kuhakikisha miradi yote iliyoanzishwa inatekelezwa na kukamilika ili kuepusha kupotea kwa rasilimali fedha iliyowekezwa ikiwa ni pamoja na kutilia mkazo kukakamilika kwa ujenzi wa vyoo ili kurejesha haiba njema ya hifadhi ya masingini.

Aidha, uongozi wa Wizara inaweza kuimarisha hifadhi kwa kuweka utaratibu na idadi yakutosha ya watumishi katika Hifadhi pamoja na kuandaa utaratibu wa usafiri kwa wafanyakazi ili waweze kutimiza majukumu yao kwa ufanisi, vile vile kuwaandalia malipo ya utumishi baada ya saa za kazi kwa watendaji wa hifadhi.

**IDARA YA KILIMO**

**6.11.1.23 Malipo yasiyokuwa na stakabadhi shilingi 56,840,000**

Ukaguzi umebaini kwamba kuna malipo yamefanyika lakini stakabadhi za malipo husika hazikuambatanishwa na hati za malipo ili kuweza kuthibitisha uhalali wa malipo hayo.

Kutoambatanisha stakabadhi za malipo ni kwenda kinyume na sheria za fedha za Zanzibar za mwaka 2016. Malipo hayo yanaonekana katika mchanganuo wa jadweli nambari 21 hapo chini:-

**Jadweli Nambari 199**: **Orodha ya Malipo yasiyokuwa na Stakabadhi**

| Namba | Hati Namba | Hundi Namba | Thamani (shs) | Alielipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | M4/06 | | 56,840,000 | Mafada kilimo limited | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya ununuzi wa pembejeo |

Kutoambatanishwa kwa stakabadhi za malipo hayo kutapelekea kukosekana kwa uhalali wa malipo hayo.

Ukaguzi unapendekeza kwamba ni vyema kwa Wizara ikahakikisha kwamba stakabadhi zote zinaambatanishwa na hati za malipo husika.

**HESABU YA MAENDELEO NA HUDUMA ZA KILIMO - NAMBARI 0404288000**

**6.11.1.24 Kukosekana kwa Toleo Maalum Linaloruhusu Utumiaji wa Fedha za Mapato**

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba akaunti hii ya Maendeleo na huduma za Kilimo ni Akaunti inayokusanya mapato kupitia vyanzo vifuatavyo:-

- Mabanda ya maonyesho

- Matangazo ya Tenda mbalimbali
- Pesa za Pembejeo
- Bajeti kutoka Hazina.

Kwa mujibu wa Kanuni za fedha za mwaka 2021, namba 29 (1-4) ambayo inaitaka Taasisi kuwasilisha mapato yote katika mfuko mkuu wa Hazina au kuwe na toleo maalum linaloidhinisha kutumika kwa mapato hayo.

Hadi tunamaliza ukaguzi tulishindwa kupata toleo hilo ambalo linaidhinisha kufanyika kwa matumizi kwa fedha hizo.

Kufanya matumizi bila kupata idhini ya kutumiwa kunaweza kupelekea kutumika vibaya kwa rasilimali za Serikali.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa wizara kuhakikisha wanafata taratibu za matumizi ya fedha za umma.

### 6.11.1.25 Kutokugonga Muhuri wa Paid Katika Hati na Nyaraka za Malipo

Ukaguzi umebaini Wizara ya Kilimo Umwagiliaji Maliasili na Mifugo hukugonga muhuri wa "PAID" kwenye hati na nyaraka za malipo, kufanya hivyo ni kuenda na kinyume na kifungu cha 95(1) cha kanuni za sheria za fedha za umma.

Kutokukugonga muhuri wa paid kwenye hati na nyaraka za malipo kunaweza kupelekea kufanya malipo mara mbili kwa nyaraka zilizokuwa tayari zimelipwa.

Uongozi wa wizara unawajibu kuhakikisha hati na nyaraka za malipo zinagongwa muhuri wa paid mara tu baada ya kukamilika malipo.

### 6.11.1.26 Kutofuatwa kwa sheria Nambari 11 ya Mwaka 2016, Sheria ya Manunuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma

Kwa mujibu wa kifungu nambari 29 (a) cha Sheria Nambari 11 ya mwaka 2016 ya Manunuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma kinazitaka taasisi zote za umma kufanya manunuzi yote kwa kufuata sheria hiyo ambayo imezilazimisha taasisi zote zitakazofanya manunuzi ni lazima yapitie kitengo cha manunuzi cha wizara (PMU).

Ukaguzi umebaini manunuzi yote yaliyofanyika kupitia hesabu za maendeleo ya huduma za kilimo hayakuanzia katika kitengo cha manunuzi. ya umma kufanya hivyo nikuenda kinyume kifungu namba 29 (a).

Kufanya manunuzi ya umma bila kupitia kitengo cha manunuzi nikuenda kinyume na sheria ya manunuzi na uondoshaji wa mali za umma.

Ukaguzi unashauri uongozi wa wizara kuhakikisha unatumia kitengo cha manunuzi ya umma kufanya manunuzi yote ya wizara.

### 6.11.1.27 Malipo yasiyokamilisha vielelezo shilingi 103,257,694

Ukaguzi umebaini kwamba kuna malipo yamefanyika lakini viambatinisho muhimu havikuweza kuambatanishwa na hati za malipo ili kuweza kuthibitisha uhalali wa malipo hayo.

Kutoambatanisha nyaraka za malipo ni kwenda kinyume na sheria ya fedha za umma namba 12 ya mwaka 2016. Malipo yenyewe ni kama yanavyoanishwa katika jadwweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 200: Orodha ya Malipo Yasiyokuwa na Viambatisho Kamili**

| Namba | Hati Namba | Aliyelipwa | Maelezo | Thamani (Tshs) |
|---|---|---|---|---|
| 1. | 02/07 | Katibu Mkuu Wkmm U | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya matayarisho ya maonyesho nane nane | 3,000,000 |
| 2. | 03/07 | | | 3,000,000 |
| 3 | 05/07 | Thiney Ali Juma | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya ukodishwaji wa mashamiana. | 16,970,873 |
| 3 | 06/07 | | | 21,628,641 |
| 4 | 04/07 | Katibu Mkuu WKMMU | Ikiwa ni sehemu ya malipo kwa ajili ya ufungaji wa gazebo kwa ndg. Beatus Haule | 2,662,500 |
| 5 | 10/07 | Katibu Mkuu WKMMU | Malipo kwa ajili ya maandalizi ya kamati ya uenezi katika maonyesho ya kilimo nane nane 2020. | 3.480,000 |
| 6 | 13/07 | Katibu Mkuu WKMMU | Ikiwa ni malipo ya safari ya kikazi Pemba | 530,000 |
| 7 | 05/08 | Katibu Mkuu WKMMU | Ikiwa ni sehemu ya malipo kwa ajili ya ufungaji wa gazebo pemba | 4,050,000 |
| 8 | 15/08 | Thney Ali Juma | Ikiwa ni bakaa ya malipo kwa ajili ya kukodisha mashamiana yaliyotumika | 21,628,641 |
| 9 | 16/08 | Thney Ali Juma | Ikiwa ni malipo ya asilimia 50 kwa ajili ya kukodishia mashamiana. | 16,924,757 |
| 10 | 01/10 | Thney Ali Juma | Ikiwa nai malipo kwa ajili kukodishwa mashamiana ya ziada | 10,007,282 |
| 11 | 09/11 | Katibu Mkuu WKMMU | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya ufuatiliaji wa mrejesho wa mkutano mkuu wa upovu | 1,280,000 |
| 12 | 09/12 | Katibu Mkuu WKMMU | Ikiwa ni malipo kwa ajili ya kuhudumia kikao cha madeni ya jamuhuri ya muungano wa tanzania | 1,575,000 |
| **Jumla** | | | | **103,257,694** |

Kukosekana kwa viambatisho vya malipo kutapelekea kukosekana kwa uhalali wa malipo hayo.

Ukaguzi unapendekeza kwamba ni vyema kwa Wizara ikahakikisha kwamba viambatisho vyote vinambatanishwa na ha

## 6.11.2 TAASISI YA UTAFITI WA MIFUGO ZANZIBAR (ZALIRI)

Ukaguzi wa hesabu za Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2020/2021 umefanywa kwa mujibu wa Sheria, kanuni, taratibu pamoja na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

### Taarifa ya Matumizi

Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Zanzibar (ZALIRI) kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ilikadiriwa kutumia jumla ya shilingi 1,310,971,925 kwa ajili ya kazi za kawaida. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 jumla ya shilingi 850,343,925 ziliingizwa na kutumika kwa kazi za kawaida sawa na asilimia 65 ya makadirio.

**MATOKEO NA MAPENDEKEZO YA UKAGUZI**

### 6.11.2.1 Kukosekana kwa Sera za Utafiti wa Mifugo

Kwa mujibu wa kifungu nambari 8 (1) (c) cha Sheria Nambari 7 ya Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Zanzibar ya mwaka 2020 kimeanisha kwamba Bodi ya Wakurugenzi ya Taasisi hiyo ina jukumu la kutoa miongozo kuhusu utayarishaji na utekelezaji wa sera za utafiti wa mifugo.

Ukaguzi uliomba kupatiwa sera za utafiti wa mifugo kwa dhumuni la kuzipitia na kujiridhisha utekelezaji wake. Hadi kumalizika kwa ukaguzi sera za utafiti wa mifugo hazikuwasilishwa kwa ajili ya ukaguzi.

Kukosekana kwa sera hizo katika ukaguzi kumepelekea kujitokeza kukwamisha jitihada za wakaguzi za kuweza kushauri namna bora ya utayarishaji na utekelezaji wa sera za utafiti wa mifumo.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Zanzibar kuhakikisha unaandaa sera madhubuti na kuziwasilisha wa wakaguzi kwa lengo la kuzipitia na kutoa ushauri wao juu ya maboresho ya sera hizo kwa lengo la kuisaidia Serikali kufikia malengo ya kuanzishwa kwa Taasisi hiyo.

### 6.11.2.2 Kukosekana kwa Daftari la Usajili wa Utafiti na Maendeleo ya Mifugo

Kwa mujibu wa kifungu 5(2)(j) cha Sheria nambari 7 ya Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Zanzibar kimeanisha kwamba ZALIRI itakuwa na jukumu la kusajili watoa huduma muhimu wa tafiti za mifugo katika sekta ya umma na sekta binafsi, na itaendeleza daftari kuu la usajili wa utafiti na maendeleo ya mifugo.

Ukaguzi umebaini kwamba Taasisi ya Utafiti wa Mifugo haikuandaa daftari la usajili wa utafiti na maendeleo ya mifugo kama ilivyopaswa kisheria.

Kutokuanzishwa kwa daftari hilo kunapelekea kushindwa kuwatambua na kuwasajili watoa huduma muhimu wa tafiti za mifugo katika sekta ya umma na sekta binafsi jambo ambalo linaweza kupelekea kukwamisha jitihada za Serikali za kuwawezesha na kuwajengea uwezo watoa huduma hao.

Ukaguzi unashauri uongozi wa ZALIRI kuhakikisha unatekeleza matakwa ya kifungu 5(2)(j) cha Sheria nambari 7 ya Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Zanzibar ili kuweza kufikia malengo ya Serikali ya kuwafikia na kuwawezesha watoa huduma wadogo wadogo ili waweze kufikia malengo waliyojipangia.

### 6.11.3 TAASISI YA UTAFITI WA KILIMO ZANZIBAR (ZARI)

Ukaguzi wa hesabu za Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2020/2021 umefanywa kwa mujibu wa Sheria, kanuni, taratibu pamoja na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Taarifa ya Mapato**

Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ilikadiriwa kukusanya jumla ya shilingi 95,000,000. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Zanzibar iliweza kukusanya jumla ya shilingi 19,078,500 sawa na asilimia 20 ya makadirio.

**Taarifa ya Matumizi**

Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ilikadiriwa kutumia jumla ya shilingi 3,052,200,000 kwa ajili ya kazi za kawaida. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 jumla ya shilingi 2,542,982,092 ziliingizwa na kutumika kwa kazi za kawaida sawa na asilimia 83 ya makadirio.

Kwa upande wa matumizi ya kazi za maendeleo Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2020/2021 haikupanga kufanya matumizi kwa ajili ya kazi za maendeleo. Hata hivyo hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 Taasisi ilipokea msaada wa shilingi 90,257,672 kutoka kwa washirika wa maendeleo kwa ajili ya kazi za maendeleo.

### 6.11.4 WAKALA WA SERIKALI WA HUDUMA ZA MATREKTA NA ZANA ZA KILIMO

Ukaguzi wa hesabu za Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo kwa mwaka wa fedha 2020/2021 umefanywa kwa mujibu wa Sheria, kanuni, taratibu pamoja na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Taarifa ya Mapato**

Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ilikadiriwa kupokea jumla ya shilingi 2,211,833,672 kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina. Kati ya fedha hizo shilingi 1,374,900,000 ni kwa ajili ya kazi za kawaida na shilingi 836,933,672 kwa ajili ya Mishahara.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni 2021 Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo ilipokea jumla ya shilingi 1,559,210,786 kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina sawa na asilimia 70.49 ya makadirio. Kati ya fedha hizo shilingi 613,246,711 kwa ajili ya kazi za kawaida sawa na asilimia 44.6 ya makadirio na shilingi 830,929,504 kwa ajili ya mshahara sawa na asilimia 99.28 ya makadirio.

Aidha Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo ilikusanya jumla ya shilingi 115,034,571.00 kutoka vyanzo vyake vya ndani kwa mwaka huo ambapo Wakala haikuwa na makadiro ya makusanyo.

**Taarifa ya Matumizi**

Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ilikadiriwa kutumia jumla ya shilingi 2,211,833,672. Kati ya fedha hizo shilingi 836,933,672 kwa ajili ya mishahara na shilingi 1,374,900,000 kwa ajili ya kazi za kawaida.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo iliingiziwa na kutumia jumla ya shilingi 1,444176,215 sawa na asilimia ya makadirio. Kati ya fedha hizo shilingi 830,929,504 kwa ajili ya mishahara sawa na asilimia ya makadirio na shilingi 613,246,711 kwa ajili ya kazi za kawaida sawa na asilimia ya makadirio.

**MATOKEO NA MAPENDEKEZO YA UKAGUZI**

#### 6.11.4.1 Kutokuwepo kwa hesabu (Account) ya mapato Unguja na Pemba

Wakala wa serikali wa huduma za Matrekta na zana za kilimo kwa upande wa Unguja na Pemba hakuna hesabu ya mapato ambayo itahusika na uingizwaji wa fedha zinazohusiana na mapato pekeyake. Hali iliyopelekea mapato yote yanayokusanywa huchanganywa na fedha za matuimizi ya kawaida (OC) na kufanya uwepo wa hesabu za matumizi pasi na kuwepo hesabu ya mapato.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu namba 28(5) cha sheria namba 2 ya ya uanzishwaji wa Wakala wa Serikali wa huduma za Matrekta na zana za kilimo ya mwaka 2019

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekata na Zana za Kilimo kufungua hesabu kwa ajili ya uwekaji taarifa za mapato yanayokusanywa kutoka katika vyanzo vyake vya ndani.

#### 6.11.4.2 Kutokuonyeshwa kwa Makadirio ya mapato ya shilingi 115,034,571

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021 ukaguzi umebaini kwamba Wakala wa serikali wa huduma za Matrekta na zana za kilimo Zanzibar imekusanya jumla ya Tsh 115,034,571 ikiwa ni mapato ya ndani yanatokana na vyanzo mabali mbali vya mapato ya wakala, lakini makadirio ya mapato hayo hayakuweza kubainishwa ambapo ni kwenda kinyume na Sheria Nambari 12 ya Usimamaizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016 .

Ukaguzi unashauri kuwepo makadirio ya mapato ili kuweza kupima ufanisi utokanao na makusanyo kutoka katika vyanzio mbali mbali vya mapato sambamaba na upatikanajai wa ufanisi wa shughuli za Wakala.

#### 6.11.4.3 Kutokuidhinishwa kwa chanzo kipya cha Kodi

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba jumla ya shilingi 1,650,000 zimepokelewa na Wakala wa seikali wa wa huduma za Matrekta na zana za kilimo kupitia mkataba wa 1/4/ 2021 wa makubaliano ya ukodishwaji wa Trecta kwa Sinohdro Coparation Ltd kwa ajili ya utayarishaji wa mashamba kupitia makubaliano hayo imebainika kuwa mkodishwaji atapaswa kufanya malipo ya muda wa saa moja la ufanyaji kazi wa trekta na fedhaa hizo ziingizwe kwenye muamala wa Wakala baada ya kutoa Ankara (invoce) ya kudai malipo kwa mpokea huduma.

Ukaguzi umebaini kuwa mapato yanayotokana na chanzo hicho hayakuidhinishwa na na Bodi ambao ndio wasimamizi wakuu wa wakala wa serikali wa huduma za Matrekta na zana za kilimo kinachohusika na mipango ya kibiashara.

Ukaguzi unashauri kuwa katika kila hatua ya utekelezaji wa Shughuli za Wakala ni vyemakufanya ushirikishwaji wa bodi katika masuala yote ya maamuzi ili kuepusha ataharai ya kufanyika kwa shughuli ambazo hazijaridhiwa na bodi.

#### 6.11.4.4 Kuwepo kwa fedha zisizostahiki katika hesabu (Account) ya Wakala shilingi 5,795,072.98

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwa katika hesabu ya wakala kuna ongezeko la fedha kiasi cha shilingi 5,795,072.98 katika kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021 bila ya kupatikana kwa maelezo yanayohusiana na fedha hiyo hali mabyo inaweza kupelekea kutokupatikana kwa usahihi wa hesabu za wakala ambapo ni kwenda kinyume na viwano vya ufungaji wa Hesabu za mwishoo wa mwaka vya Kitaifa na Kimataifa

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wakala kuwa makini katika kuandaa Taarifa za Hesabu kwa usahihi na kwa mujibu wa sheria na viwango vilivyoekwa ili kuepuka kuingiza kiasi cha fedha zisizostahiki katika hesabu za wakala.

### WAKALA WA SERIKALI WA HUDUMA ZA MATREKTA NA ZANA ZA KILIMO - PEMBA

#### 6.11.4.5 Kutokuwepo kwa kitengo cha uhasibu

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kutokuwepo kwa kitengo cha uhasibu katika ofisi ya Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta na zana za Kilimo Pemba ili kuweza kudhibiti mfumo wa fedha wa mapato na matumizi pamoja na usimamia wa rasilimali za Umma.

Hali hii imepelekea kutokuwepo kwa udhibiti wa mapato na matumizi yanayohusu ofisi hiyo kwa upande wa Pemba ambapo ni kwenda kinyume na Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Ofisi ya Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta na zana za Kilimo Pemba kuhakikisha kwamba kitengo cha uhasibu kinakuwepo na kinafanya kazi ya utowaji wa huduma zinazokusudiwa kwa kufanya mawasiliano ya karibu na Ofisi ya Rais Fedha na Mipango Pemba ili kuharakisha upatikanaji wa watendaji kwa ajili ya kuhudumia kitengo hicho.

#### 6.11.4.6 Dosari zilizobainika katika mapokezi ya vitabu vya mapato

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika uwepo wa dosari za mapokezi ya vitabu vya mapato kwa Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo Pemba ambapo dosari hizo ni kama zifuatazo:-

- Kutokujulikana idadi kamili ya vitabu vilivyopokelewa.
- Kukosekana kwa uthibitisho wa mapokezi (Delivery Order).

Kukosekana kwa taarifa kamili ya vitabu vilivyowasilishwa kutoka makao makuu ya Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo Zanzibar na kujulikana idadi halisi ya vitabu vilivyopokelewa kunatia shaka juu ya ukusanyaji wa mapato kuwa umeendana na vitabu halisi vilivyopokewa jambo ambalo linaweza kupelekea upotevu wa mapato kwa kutumia vitabu ambavyo havikupokelewa na kuorodheshwa katika daftari maalum la kuwekea kumbukumbu za vitabu vya ukusanyaji wa mapato (counter foil register).

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 34(1) cha Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma nambari 12 ya mwaka 2016.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo Pemba kuhakikisha kwamba mapokezi yote yanayofanyika yanatakiwa kufuata utaratibu ikiwemo kuweka rikodi katika vitabu vya uthibitisho wa mapokezi na kuwasilisha hati ya mapokezi (delivery Order).

#### 6.11.4.7 Kutokuonekana kwa mapato katika taarifa za benki shilingi 3,257,500

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba jumla ya shilingi 3,257,500 ni mapato ya Wakala kutokana na utoaji wa huduma mbali mbali lakini mapato hayo hayakuonekana katika taarifa za benki hali ambayo inatia shaka katika ufuatiliaji wa taarifa za mapato yatokanayo na huduma mbali mbali zinazotolewa, hivyo kushindwa kujiridhisha juu ya ufanisi wa mapokezi na matumizi halisi ya mapato hayo.

Kufanya hivyo nikwenda kinyume na Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016. Mchanganuo wa mapato yaliokosekana ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 201 : Mapato yaliyokosekana katika taarifa za benki**

| Nambari ya stakatabadhi | Nambari ya slip ya benki | Tarehe iliyolipwa | Aliyelipa | Kiasi cha fedha kilichopokelewa (Tshs) | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| 00604 | Haina | 30/4/2021 | Wakala wa Matrekta na zana za Kilimo | 110,000 | Fedha Kwa ajili ya uchongaji na Ukodishaji matrekta |
| 00512 | 0665813 | 21/9/2020 | Khamis Mgau Kombo | 20,000 | Fedha kwa ajili ya kuchoma na kuchonga |
| 00590 | 0358035, 0637900, 0358273, 0665812 | 30/9/2020 | Wakala wa Matrekta na zana za Kilimo | 3,127,500 | Fedha kwa ajili ya huduma ya kulimia. |
| **Jumla** | | | | **3,257,500** | |

## 6.12 WIZARA YA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAAZI

### 6.12.1 FUNGU N 01 – WIZARA YA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAAZI

Ukaguzi wa hesabu za Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi kwa mwaka wa fedha 2020/2021 umefanywa kwa mujibu wa Sheria, kanuni, taratibu pamoja na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Taarifa ya Mapato**

Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ilikadiriwa kukusanya jumla ya shilingi 3,405,399,000 kutoka na vyanzo mbalimbali vya mapato vya ndani , shilingi 22,040,513,485 kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina na shilingi 70,406,975,000 kutokana na Misaada na mikopo kutoka kwa washirika wa maendeleo.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi Zanzibar ilifanikiwa kukusanya mapato ya shilingi 769,306,362.64 kutoka vyanzo vya ndani sawa na asilimia 23 ya makadirio, shilingi 9,047,373,671 kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina sawa na asilimia 41 ya makadirio na shilingi 525,393,241 kutokana na Misaada na mikopo kutoka kwa washirika wa maendeleo sawa na asilimia 1 ya makadirio.

**Taarifa ya Matumizi**

Katika kipindi cha mwaka 2020/2021 Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi ilikadiriwa kutumia jumla ya shilingi 92,447,488,485. Kati ya fedha hizo shilingi 47,119,896,485 zilipangwa kwa kazi za matumizi ya kawaida na shilingi 45,327,592,000 kwa kazi za maendeleo.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi imeingiziwa na kutumia jumla ya shilingi 9,553,708,844 sawa na asilimia 10.33 , kati ya fedha hizo shilingi 8,552,161,249 kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida sawa na asilimia 18 ya makadirio na shilingi 1,001,547,595 kwa ajili ya kazi za maendeleo sawa na asilimia 2 ya makadirio.

**MATOKEO NA MAPENDEKEZO YA UKAGUZI**

### 6.12.1.1 Migogoro ya ardhi ambayo haijapatiwa usuluhisho kwa muda mrefu.

Katika ukaguzi uliofanyika umebaini kwamba kuna malalamiko mengi ya migogoro ya ardhi ambayo yamewasilishwa katika Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi kabla ya kwenda Mahkamani kwa kupitia Kamati ya Migogoro ya Ardhi iliyoanzishwa na Mheshimiwa Waziri ili kupunguza wimbi la mrundikano wa kesi katika Mahkama ya Ardhi. Dosari iliyobainika na ukaguzi ni kwamba kamati hiyo inakabiliwa na changamoto nyingi kutokana na kesi nyingi kuwa ni za muda mrefu, hata hivyo ukaguzi umebaini kamati hiyo imefanyia kazi migogoro mingi pamoja na kuyatolea ushauri na maamuzi lakni kilichobainika ni kwamba baadhi ya walalamikaji bado hawajakubaliana na maamuzi yaliyotolewa na kamati hiyo na kupelekea kuendelea kuwepo kwa mrundikano wa migogoro ya ardhi, **Kiambatisho Nambari 10 Kinahusika.**

Baadhi ya changamoto hizo ni kama zifuatazo:-

- Kuwepo kwa migogoro ya muda mrefu kuanzia miaka mitano na kuendelea.
- Kufariki kwa wenye kesi ambapo kunapelekea kujitokeza kwa ugumu wa utatuzi wa migogoro hiyo.
- Kujitokeza kwa walalamikaji wengi wanaomiliki eneo moja la ardhi na kupelekea kuchelewa kwa suluhu za kesi hizo.
- Ucheleweshwaji wa maamuzi katika Idara husika unaopelekea kukuwa kwa tatizo na kulifanya zoezi la suluhu kuwa gumu.
- Kujitokeza kwa changamoto ya mgogoro kurithiwa kwa migogoro kutokana na asili ya wenye migogoro kufariki dunia.

Kutokana na kuendelea kujitokeza kwa migogoro ya ardhi ambayo inakaa muda mrefu bila ya kupatiwa usuluhisho, ukaguzi unashauri uongozi wa Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi kuchukuwa jitihada za makusudi kuhakikisha inazuia uuzwaji wa maeneo kiholela bila ya kufuata sheria, ushirikishwaji wa viongozi wa Serikali za Mitaa katika hatua za uuzwaji wa maeneo pamoja na kuhakikisha maeneo yote yanafanyiwa uhaulishaji na Bodi ya Uhaulishaji wa Ardhi kwa lengo la kujulikana mmiliki halali kisheria wa eneo husika.

Aidha, uongozi wa Wizara ya Ardhi ya Maendeleo ya Makaazi uhakikishe kwamba unasimamia Taasisi na Idara zake kuharakisha utekelezaji wa utatuzi wa migogoro ili kuepuka changamoto ya wadai wengi kusubiri kwa muda mrefu kupatiwa haki zao na hatimae kufariki dunia kabla ya kupatiwa haki hizo na kupelekea migogoro hiyo ya ardhi kuendelea kurithiwa kizazi na kizazi na hatimae haki kutokupatikana na kudhoofisha juhudi za Serikali katika utatuzi wa migogoro ya ardhi.

**WIZARA YA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAAZI – PEMBA**

### 6.12.1.2 Malipo kwa watoa huduma ambao hawakusajiliwa na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma shilingi 3,450,000

Kwa mujibu wa kifungu cha 23(1) cha Sheria ya Manunuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma kinaeleza kulingana na masharti ya sheria hii mtu, kampuni au taasisi haitawasilisha zabuni au vyenginevyo kushiriki katika manunuzi ya Umma isipokua chombo kiwe kimesajiliwa na Mamlaka ya Manunuzi.

Kwa mujibu wa kifungu cha 23(2), zabuni kutoka kwa mtu, kampuni au chombo ambacho hakijasajiliwa haifai na hakitazingatiwa na taasisi ya ununuzi.

Ukaguzi umebaini kwamba Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi Pemba imefanya manunuzi kwa watoa huduma mbali mbali ambao hawakusajiliwa na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya Zanzibar.

Kufanya hivyo kunapelekea kuikosesha Serikali mapato, aidha ni kwenda kinyume na Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 202 : Malipo kwa watoa huduma ambao hawakusajiliwa na mamlaka ya ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma**

| Hati namba | Hundi namba | Kiasi cha fedha kilicholipwa (Tshs.) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 13/8<br>15/8/2020 | 0017231 | 290,000 | Aziza Ali Rashid | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa viburudishaji. |
| 17/8<br>15/8/2020 | 0017231 | 200,000 | Amour Hamad Mussa | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa viburudishaji |
| 34/9<br>24/9/2020 | 0017000 | 2,000,000 | Ali Kheri Rashid | Malipo ya fedha kwa ajili ya Uniform za wafanyakazi |
| 6/3<br>24/12/2020 | 019771 | 290,000 | Aziza Ali Rashid | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa viburudishaji |
| 12/3<br>5/3/2021 | 19834 | 220,000 | Mohammed Hamoud Seif | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa viburudishaji |
| 29/5<br>10/5/2021 | 21001 | 450,000 | Mau Food and Snacks | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa chakula. |
| **Jumla** | | **3,450,000** | | |

### 6.12.1.3 Utumiaji wa Ofisi moja ya Masjala kwa ajili ya Wizara mbili tofauti.

Katika Ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi pamoja na Wizara ya Maji Nishati na Madini Pemba zinatumia Ofisi moja ya Masjala.

Hali hii inaweza kupelekea kuvuja kwa taarifa za siri za Serikali pamoja na kupelekea kuwepo kwa mchanganyiko wa majalada ya nyaraka yatokanayo na Wizara hizo jambo ambalo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 52(1) cha Kanuni ya Utumishi wa Umma ya Zanzibar ya mwaka 2014.

### 6.12.2 BODI YA KONDOMINIO ZANZIBAR

Ukaguzi wa hesabu za mwaka wa fedha 2020/2021 kwa Bodi ya Kondominio Zanzibar umefanywa kwa mujibu wa Sheria, kanuni, taratibu pamoja na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Taarifa ya Matumizi**

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021 Bodi ya Kondominio ilikadiriwa kutumia jumla ya shilingi 200,000,000 kutoka Mfuko Makuu wa Hazina , kati ya fedha hizo shilingi 180,000,000 kwa ajili ya kazi za kawaida na 20,000,000 kwa ajili ya kazi za maendeleo.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 Bodi ya Kondominio ilitumia jumla ya shilingi 57,800,166 sawa na asilimia 28.90 ya makadirio. Kati ya fedha hizo shilingi 52,250,166 zilitumika kwa kazi za kawaida sawa na asilimia 29 ya makadirio na shilingi 3,550,000 zilitumika kwa kazi za maendeleo sawa na asilimia 18 ya makadirio.

### 6.12.3 BODI YA UHAULISHAJI ARDHI

Ukaguzi wa hesabu za mwaka wa fedha 2020/2021 kwa Bodi ya Uhaulishaji Ardhi umefanywa kwa mujibu wa Sheria, kanuni, taratibu pamoja na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Taarifa ya Mapato**

Bodi ya Uhaulishaji wa Ardhi Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ilikadiriwa kukusanya jumla ya shilingi 2,289,890,000 kupitia vianzio vyake vya ndani, na shilingi 1,717,000,000 kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 Bodi ya Uhaulishaji wa Ardhi ilikusanya jumla ya shilingi 2,462,636,564.34 kupitia vyanzo vyake vya ndani sawa na asilimia 108 ya makadirio na shilingi 220,702,364 kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina sawa na asilimia 13 ya makadirio. Aidha mapato ya shilingi 269,654,121 kutoka vitengo vyengine vya Serikali ambazo hazikuwa na makadirio.

**Taarifa ya Matumizi**

Bodi ya Uhaulishaji wa Ardhi Zanzibar ilikadiriwa kutumia jumla ya shilingi 1,717,000,000 kwa mwaka wa fedha 2020/2021, kati ya fedha hizo shilingi 1,670,750,000 zilitumika kwa kazi za kawaida na shilingi 46,250,000 zilitumika kwa kazi za maendeleo.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 jumla ya shilingi 464,136,073.50 zimeingizwa na kutumika, kati ya fedha hizo shilingi 438,229,498 zimetumika kwa kazi za kawaida sawa na asilimia 26 ya makadirio na shilingi 25,906,575 zimetumika kwa kazi za maendeleo sawa na asilimia 56 ya makadirio.

**MATOKEO YA UKAGUZI NA MAPENDEKEZO**

#### 6.12.3.1 Fedha ambazo hazikutumika katika mwaka wa fedha husika shilingi 8,213,164.89

Kwa mujibu wa kifungu nambari 52(2) cha Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma nambari 12 ya mwaka 2016, kinaeleza kwamba "bakaa ya matumizi ambayo hayakutumika hadi mwisho wa mwaka wa fedha husika fedha zake zitalipwa na kuingizwa katika Mfuko Mkuu wa Serikali".

ukaguzi umebaini jumla ya shilingi 8,213,164.80 hazikurejeshwa katika Mfuko Mkuu wa Hazina na kubainika kuendelea kutumika kwa mwaka wa fedha 2020/2021 kinyume na matakwa ya kifungu nambari 52(2) cha Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016.

Kujitokeza kwa matumizi ambayo hayakuwa katika bajeti ya mwaka husika na hayakuwekewa malengo "commitment" kunaweza kukapelekea kufanya matumizi kinyume na makadirio ya bajeti au kujitokeza kwa upotevu wa fedha unaotokana na matumizi mabaya ya fedha.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Bodi ya Uhaulishaji Ardhi kuhakikisha kwamba fedha ambazo hazikutumika katika mwisho wa mwaka husika zinawasilishwa katika Mfuko Mkuu wa Serikali mwa mujibu wa sheria.

### 6.12.4 BODI YA UDHIBITI KODI ZA NYUMBA

Ukaguzi wa hesabu za mwaka wa fedha 2020/2021 kwa Bodi ya Udhibiti wa Kodi za Nyumba umefanywa kwa mujibu wa Sheria, kanuni, taratibu pamoja na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Taarifa ya Matumizi**

Bodi ya Kudhibiti Kodi za Nyumba Zanzibar ilikadiriwa kutumia jumla ya shilingi 200,000,000 kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina kwa mwaka wa fedha 2020/2021. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 Bodi ya Kudhibiti Kodi za Nyumba ilipokea na kutumia jumla shilingi 48,535,850 sawa na asilimia 24.26 ya makadirio, kukiwa na upungufu wa shilingi 151,464,150 sawa na asilimia 76 ya makadirio.

### 6.12.5 KAMATI YA UDHIBITI WA UJENZI IDARA YA MIPANGO MIJI NA VIJIJI (DCU)

Ukaguzi wa hesabu za Kamati ya Udhibiti wa Ujenzi Idara ya Mipango Miji na Vijiji kwa mwaka wa fedha 2020/2021 umefanywa kwa mujibu wa Sheria, kanuni, taratibu pamoja na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Taarifa ya Mapato**

Kamati ya Udhibiti Ujenzi Idara ya Mipango Miji na Vijiji kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ilikadiriwa kukusanya jumla ya shilingi 1,240,800,000 kutoka vyanzo vyake vya ndani na shilingi 1,039,600,000 kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 Kamati ilikusanya jumla ya shilingi 818,000,378 kutoka vyanzo vya ndani sawa na asilimia 66 ya makadirio, na shilingi 675,333,529 sawa na asilimia 65 ya makadirio.

**Taarifa ya Matumizi**

Kamati ya Udhibiti Ujenzi Idara ya Mipango Miji na Vijiji kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021 ilikadiriwa kutumia jumla ya shilingi 1,039,600,000 kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina katika kipindi cha mwaka 2020/2021.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni 2021, Kamati ilipokea na kutumia shilingi 675,333,529 kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina sawa na asilimia 65 ya makadirio.

**MATOKEO NA MAPENDEKEZO YA UKAGUZI**

**AKAUNTI NAMBARI 0404116000**

### 6.12.5.1 Kukosekana ufafanuzi na uchambuzi juu ya kifungu (Note) cha mapato shilingi 818,000,378.60

Baada ya kupitia taarifa za hesabu za mwisho wa mwaka 2020/2021, ukaguzi umebaini kuwepo na dosari ya kutokutolewa ufafanuzi na uchambuzi wa kifungu cha mapato chenye thamani ya shilingi 818,000,378.60 ambapo mapato hayo yaliainishwa katika taarifa za hesabu za mwisho wa mwaka husika jambo ambalo ukaguzi umeshindwa kupata ufafanuzi na uchambuzi wa kina juu ya mapato hayo ili kuweza kuthibitisha vyanzo halisi vilivyochangia mapato ili kupima uwezo wa kila chanzo kilicho changia pamoja na kujiridhisha iwapo chanzo hiko kimefikia malengo au kuweza kuishauri taasisi husika juu ya namna bora ya ukusanyaji wa mapato au uibuaji wa vyanzo vipya vya mapato.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma nambari 12 ya mwaka 2016.

### 6.12.5.2 Malipo yasiyokuwa na vielelezo shilingi 16,940,000

Ukaguzi umebaini kwamba Kamati ya Udhibiti Ujenzi idara ya Mipango Miji na Vijiji imefanya malipo yenye thamani ya shilingi 16,940,000. Dosari iliyobainika katika ukaguzi ni Kukosekana kuambatishwa kwa vielelezo husika vilivyofanya malipo hatika hati ya malipo ili kuweza kujiridhisha juu ya uhalali wa malipo.

Kufanya malipo bila ya kuambatanishwa katika hati za malipo kunaweza kupelekea kujitokeza kwa upotevu wa fedha za umma kwa kulipia bidhaa zisizo na ubora au kulipia bidhaa zisizo na uhalisia (bidhaa hewa).

**Jadweli Nambari 203 : Malipo yasiyokuwa na vielelezo**

| Hati ya malipo nambari | Hundi nambari | Thamani ya fedha -shilingi | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 13/8 ya 24/8/20 | 000470 | 5,000,000 | Ndg. Halima Omar Ali | Malipo ya matumizi ya Idara ya Mipango Miji na Vijiji Unguja. |
| 7/9 ya 1/9/20 | 000478 | 11,940,000 | DCU | Malipo ya nauli na posho kwa watendaji wa Manispaa na Halmashauri za Zanzibar kwa ziara ya Dodoma.. |
| **Jumla** | | **16,940,000** | | |

### 6.12.5..3 Utekelezaji wa miradi ya maendeleo shilingi 120,000,000

Katika ukaguzi uliofanyika imebaini kwamba jumla ya shilingi 120,000,000 zimetolewa na DCU–Zanzibar kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo mbali mbali kupitia Mabaraza ya Manispaa na Halmashauri katika kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021.

Baada ya kufanya ziara za kikazi katika Mabaraza ya Manispaa na Halmashauri ukaguzi umebaini kwamba baadhi ya Mabaraza ya Manispaa na Halmashauri zilizopelekewa fedha hizo hazikutumika katika miradi ya maendeleo kama ilivyoelekezwa jambo ambalo linakwamisha malengo ya DCU walivyojiwekea.

Ukaguzi unashauri uongozi wa DCU kuhakikisha kwa fedha za miradi zinazotolewa zinatumika kwa miradi iliyokusudiwa ili walengwa kuweza kufaidika kwa makusudio ya fedha hizo na kupelekea upatikanaji wa tija iliyo kusudiwa. Fedha na utekelezaji wake ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 204 : Fedha zilizotumika katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo**

| Hati ya malipo | Hundi namba | Thamani ya fedha – shilingi | Aliyelipwa | Maelezo | Hatua za uterkelezaji wa miradi ya maendeleo |
|---|---|---|---|---|---|
| 8/11 ya 9/11/2021 | T T | 30,000,000 | Halmashauri ya Wilaya ya Kaskazini 'A' | Ujenzi wa skuli ya maaandalizi Chaani Masingini | Fedha hazikutumika katika mradi husika na badala yake zimetumika kwa kazi za Ofisi. |
| 2/11 ya 22/10/2021 | T T | 30,000,000 | Halmashauri ya Wilaya ya Kaskazini 'B' | Ujenzi wa paki ya magari Kiwengwa. | Ukaguzi umebaini fedha hizi hazikutumika kulingana mradi husika, badala yake zimetumika ujenzi wa vyoo vya umma |
| 6/9 ya 1/9/2021 | T T | 30,000,000 | Halmashauri ya Wilaya ya Kati | Ikiwa ni fedha kwa ajili ya uimarishaji wa taa za barabarani | Ukaguzi umebaini fedha hizo hazikutumika |
| | TT | 30,000,000 | Baraza la Manispaa -Wete | Ikiwa ni fedha kwa ajili ya ujenzi wa Bustani | Ukaguzi umebaini fedha hizo hazikutumika kwa ujenzi huo. |
| | TT | 30,000,000 | Halmashauri ya Micheweni | Ikiwa ni fedha kwa ajili ya mradi wa ujenzi wa Kituo cha Magari | Matumizi ya fedha hizo hayakuwa na tija Kutokana na Kukosekana kwa uhalisia wa matumizi. |
| | TT | 30,000,000 | Baraza la Manispaa – Chake chake | Ikiwa ni malipo ya fedha za mradi wa ujenzi wa skuli ya maandalizi Machomanne | Ukaguzi umebaini ujenzi wa mradi huu upo katika hatua ya kuridhisha. |
| **Jumla** | | **120,000,000** | | | |

### 6.12.6 BODI YA USAJILI WA WAKANDARASI

Ukaguzi wa hesabu za mwaka wa fedha 2020/2021 kwa Bodi ya Usajili wa Wakandarasi umefanywa kwa mujibu wa Sheria, kanuni, taratibu pamoja na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Taarifa ya Mapato**

Bodi ya Usajili wa Wakandarasi kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ilikadiriwa kukusanya jumla ya shilingi 1,345,415,750. Kati ya fedha hizo jumla ya shilingi 768,809,000 ikiwa ni makusanyo kutoka vyanzo vya ndani na shilingi 576,606,750 ikiwa ni makusanyo kutoka kwa washirika wa maendeleo.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 Bodi ya Usajili ya Wakandarasi imekusanya jumla ya shilingi 592,254,747 sawa na asilimia 44.02 ya makadirio. Kati ya fedha hizo shilingi 471,464,661 zimekusanywa kutoka vyanzo vya ndani sawa na asilimia 61.32 ya makadirio na shilingi 120,790,086 zimekusanywa kutoka washirika wa maendeleo sawa na asilimia 20 ya makadirio.

**Taarifa ya Matumizi**

Bodi ya Usajili wa Wakandarasi kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021 ikadiriwa kutumia jumla ya shilingi 1,161,766,000 kwa matumizi ya kazi za kawaida, na shilingi 576,606,750 kwa matumizi ya kazi za maendeleo.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 jumla ya shilingi 228,930,716.27 ziliingizwa na kutumika kwa kazi za kawaida sawa na asilimia 19.71 ya makadirio na jumla ya shilingi 120,790,086 zimeingizwa na kutumika kwa kazi za maendeleo sawa na asilimia 21 ya makadirio.

**MATOKEO NA MAPENDEKEZO YA UKAGUZI**

### 6.12.6.1 Malipo yaliyolipwa kwa washiriki ambao hawakushiriki katika vikao shilingi 12,070,000

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021 Bodi ya Usajili wa Wakandarasi imefanya malipo yenye thamani ya shilingi 12,070,000 kwa ajili ya vikao vya utekelezaji kazi za kila siku.

Dosari iliyobainika na ukaguzi ni kujitokeza kwa malipo ya posho walizolipwa washiriki ambao hawakuhudhuria katika vikao hivyo kutokana na kukosekana kwa uthibitisho wa kujisajili kushiriki katika vikao hivyo.

Kufanya malipo kwa washiriki ambao kumekosekana ushiriki wao katika vikao kunaweza kukapelekea kujitokeza kwa viashiria vya upotevu wa fedha za umma pamoja na kutokupata uhalali wa matumizi hayo.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Bodi ya Usajili wa Wakandarasi kuhakikisha kwamba vielelezo husika vya mahudhurio ya washiriki vinapatikana kwa ukaguzi ili kuweza kuthibitisha uhalali wa malipo hayo.Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 205 : Malipo yaliyolipwa kwa washiriki ambao hawakushiriki katika vikao**

| Hati ya malipo Namba | Fedha Zilizolipwa shilingi | Malipo ya Walioshiriki wa Kikao shilingi | Malipo ya Wasioshiriki kikao shilingi | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| 19/9 ya 28/9/20 | 3,640,000 | 2,500,000 | 1,140,000 | Bodi ya usajili wa Wakandarasi | Ikiwa ni malipo ya posho la kusikiliza kesi mbalimbali za ujenzi |
| 2/10 ya 01/10/2020 | 3,475,000 | 2,825,000 | 650,000 | Bodi ya usajili wa Wakandarasi | Ikiwa ni malipo ya posho la kikao cha tano cha Bodi ya nne ya usajili wa Wakandarasi |
| 17/10 ya 22/10/2020 | 3,000,000 | 1,940,000 | 1,060,000 | Bodi ya usajili wa Wakandarasi | Ikiwa ni malipo ya posho la kusikiliza kesi mbalimbali za ujenzi Unguja. |
| 3/3 ya 2/3/2021 | 3,440,000 | 2,400,000 | 1,040,000 | Bodi ya usajili wa Wakandarasi | |
| 2/5 ya 12/5/2021 | 3,930,000 | 3,480,000 | 450,000 | Bodi ya usajili wa Wakandarasi | |

| Hati ya malipo Namba | Fedha Zilizolipwa shilingi | Malipo ya Walioshiriki wa Kikao shilingi | Malipo ya Wasioshiriki kikao shilingi | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| 12/8 ya 24/8/2020 | 3,980,000 | 2,500,000 | 1,480,000 | Bodi ya usajili wa Wakan-darasi | Ikiwa ni malipo ya posho la kikao kwa wanaohalifu sheria ya ujenzi. |
| 1/2 ya 3/2/2021 | 3,775,000 | 3,100,000 | 675,000 | Bodi ya usajil wa Wakan-darasi | Ikiwa ni malipo ya posho kwa wajumbe na watendaji walioshiriki kikao cha sita cha kawaida cha Bodi ya nne ya usajili wa wakandarasi. |
| 5/4 ya 27/4/2021 | 3,675,000 | 3,225,000 | 450,000 | Bodi ya usajili wa wakan-darasi | Ikiwa ni malipo ya posho kwa wajumbe na watendaji walioshiriki kikao cha sita cha dharura cha Bodi. |
| 1/5 ya 8/5/2021 | 3,775,000 | 2,625,000 | 1,150,000 | Bodi ya usajili wa wakan-darasi | |
| 2/5 ya 12/5/2021 | 3,930,000 | 2,810,000 | 1,120,000 | Bodi ya usajili wa wakan-darasi | Ikiwa ni malipo ya posho kwa kusikiliza kesi mbalimbali za ujenzi Unguja kwa mwezi wa Disemba |
| 9/9 ya 18/9/2020 | 11,500,000 | 8,645,000 | 2,855,000 | Bodi ya usajili wa Wakan-darasi | Ikiwa ni malipo ya posho na nauli kwa safafi ya Pemba kwa ukaguzi wa miradi mikubwa |
| **Jumla** | **48,120,000** | **36,050,000** | **12,070,000** | | |

### 6.12.6.2 Kuwepo kwa madeni wanayodaiwa Wakandarasi kwa muda mrefu shilingi 355,786,500

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Bodi ya Usajili ya Wakandarasi inadai jumla ya shilingi 355,786,500 kutoka kwa Wakandarasi mbali mbali ambao hawajalipa madeni yao kwa kipindi kirefu kutokana na makosa mbali mbali waliyotozwa yakiwemo utozwaji wa adhabu (Penalty) kwa makosa yanayotokana na ujenzi uliofanywa bila ya kutokuwekwa kwa bango katika eneo la ujenzi husika, kutosajili kwa miradi, kuwepo kwa wakandarasi ambao hawajasajiliwa na Bodi katika miradi wanayayaoshughulikia.

Uwepo wa madeni hayo kwa muda mrefu unapelekea kutokupatikana kwa ufanisi na malengo yaliyopangwa jambo ambalo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 4 cha Sheria nambari 6 ya Uanzishwaji wa Bodi ya Usajili Wakandarasi ya mwaka 2008.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Bodi ya Usajili wa Wakandarasi kuhakikisha unachukuwa jitihada za makusudi za ufuatiliaji wa madeni ikiwemo kuweka kifungu cha adhabu kwa atakaeshindwa au kuchelewesha ulipwaji wa madeni hayo kwa wakati, **Kiambatisho Nambari 11 Kinahusika.**

### 6.12.6.3 Kukosekana kwa Mfumo wa Usajili wa Wakandarasi

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika Bodi ya Usajili wa Wakandarasi haina Mfumo wa kielektroniki utakaotumika kwa lengo la kuweka rikodi na kumbu kumbu za kuwatambua Wakandarasi wanaopewa kazi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na wale Wakandarasi binafsi wanaotakiwa kujisajili kwa mujibu wa sheria.

Kutokuwepo kwa mufumo wa usajili wa wakandarasi kunapelekea kujitokeza kwa changamoto mbali mbali ikiwemo malimbikizo ya madeni ya Wakandarasi ambao wameshamaliza kazi zao na kuondoka, kutokutambua sehemu aliyokuwepo mkandarasi, kutokutambua uwezo alionao Mkandarasi na aina ya kazi anazozifanya.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi kuhakikisha unaanzisha mfumo maalum utakaoweza kuwasajili na kuwatambua Wakandarasi wote ili kuweza kupata taarifa zao kikamilifu ikiwemo uwezo wa kiufundi, kifedha pamoja na uzoefu wa kazi anazozifanya na alizowahi kusimamia na kuzifanya kwa lengo la kuepuka kujitokeza kwa ujenzi uliokuwa chini ya viwango.

### 6.12.7 KAMISHENI YA ARDHI

Ukaguzi wa hesabu za mwaka wa fedha 2020/2021 kwa Kamisheni ya Ardhi umefanywa kwa mujibu wa Sheria, kanuni, taratibu pamoja na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Taarifa ya Mapato**

Kamisheni ya Ardhi kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ilikadiriwa kukusanya jumla ya shilingi 3,321,000,000. Kati ya fedha hizo shilingi 2,651,000,000 kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali, shilingi 45,000,000 kutoka vitengo vyengine vya Serikali na shilingi 535,000,000 kutoka katika vyanzo vya ndani.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 Kamisheni ya Ardhi ilikusanya jumla ya shilingi 2,805,266,000.97 sawa na asilimia 84.47 za makadirio. Kati ya fedha hizo, shilingi 2,073,441,000.38 kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali sawa na asilimia 78 ya makadirio, shilingi 667,534,000.23 kutoka kwa vyanzo vya ndani sawa na asilimia 125 ya makadirio, shilingi 45,740,000 kutoka vitengo vyengine vya Serikali sawa na asilimia 102 ya makadirio na shilingi 18,551,000.35 kutoka misaada ya maendeleo ambapo fedha hizi hazikutengewa bajeti.

**Taarifa ya Matumizi**

Kamisheni ya Ardhi ilikadiriwa kutumia jumla ya shilingi 2,716,000,000, kati ya fedha hizo shilingi 2,507,900,000 kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida na shilingi 208,100,000 kwa kazi za maendeleo.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 Kamisheni Ardhi ilitumia 2,716,000,000 sawa na asilimia 100 ya makadirio , kati ya fedha hizo, shilingi 2,007,450,000.34 kwa kazi za kawaida sawa na asilimia 80 ya makadirio na shilingi 127,884,000.02 kwa kazi za maendeleo sawa na asilimia 61 ya makadirio.

**KAMISHENI YA ARDHI-PEMBA**

#### 6.12.7.1 Malipo kwa Watoa huduma ambao hawajasajiliwa na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma Shilingi 8,629,448

Kwa mujibu wa kifungu cha 23(1) cha Sheria ya Manunuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma kinaeleza kulingana na masharti ya sheria hii mtu, kampuni au taasisi haitawasilisha zabuni au vyenginevyo kushiriki katika manunuzi ya Umma isipokua chombo kiwe kimesajiliwa na Mamlaka ya Manunuzi.

Kwa mujibu wa kifungu cha 23(2), zabuni kutoka kwa mtu, kampuni au chombo ambacho hakijasajiliwa haifai na hakitazingatiwa na taasisi ya ununuzi.

Ukaguzi umebaini kwamba Kamisheni ya Ardhi Pemba imefanya manunuzi na watoa huduma mbali mbali ambao hawakusajiliwa na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya Zanzibar.

Kufanya hivyo kunapelekea kuikosesha Serikali mapato ambapo ni kwenda kinyume na Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016.

Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 206 : Malipo kwa watoa huduma ambao hawakusajiliwa na mamlaka ya ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma**

| Hati Namba | Hundi Namba | Kiasi cha fedha kilicholipwa (Tshs.) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 26/9<br>3/9/2020 | T.O | 3,507,238 | Salim Hamdan Maalim | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya ujenzi |
| 27/9<br>24/9/2020 | T.O | 218,638 | | |
| 6/4<br>14/4/2021 | T.O | 483,380 | | |
| 26/10 | T.O | 304,192 | Hassan Ali Mohammed | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa viatu vya rainboot |
| 40/6<br>28/6/2021 | T.T | 4,116,000 | Techno Trade Investment Ltd | Malipo ya fedha kwa ajili ya matengenezo ya vifaa vya upimaji |
| **Jumla** | | **8,629,448** | | |

### 6.12.7.2 Kukosekana kwa mapato yatokanayo na upimaji wa ardhi na utoaji wa ramani shilingi 4,538,000

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Kamisheni ya Ardhi Pemba kupitia idara ya upimaji na ramani inawadai wateja wake jumla ya shilingi 4,538,000 zinazotokana na upimaji wa ardhi pamoja na uandaaji wa ramani.

Hali hii inapelekea kukosekana kwa mapato yatokanayo na fedha za upimaji wa ardhi na utoaji wa ramani. Mchanganuo wa madeni hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 207 : Mapato yatokanayo na upimaji wa ardhi na utoaji wa ramani**

| Namba | Jina la Mdaiwa | Muda wa deni | Fedha zinazodaiwa (Tshs.) |
|---|---|---|---|
| 1. | Mkuu wa Wilaya ya Micheweni | 29/05/2017 | 500,000 |
| 2. | Mkuu wa Wilaya ya Micheweni | 21/02/2019 | 500,000 |
| 3. | KMKM (%Barefoot Resort) | 02/06/2019 | 900,000 |
| 4. | Polisi (%Bare Foot Resort) | 02/06/2019 | 300,000 |
| 5. | Wizara ya Biashara (Saltind) | 23/09/2019 | 403,000 |
| 6. | Wiazara ya Biashara (Seaweed Ind) | 23/09/2019 | 585,000 |
| 7. | OMPR | 23/09/2019 | 400,000 |
| 8. | Afisa Mdhamini MBM | 17/02/2017 | 400,000 |
| 9. | Afidha Mdhamini Kilimo | 21/06/2017 | 300,000 |
| 10. | Mkuu wa Wilaya ya Micheweni | 9/11/2016 | 250,000 |
| **Jumla** | | | **4,538,000** |

#### 6.12.7.3 Kushindwa kufikia lengo la kukusanya Mapato shilingi 215,000,000

Jumla ya shilingi 215,000,000 zilikadiriwa kukusanywa na Kamisheni ya Ardhi-Pemba kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

Ukaguzi umebaini kwamba makadirio haya ni makubwa ukilinganisha na makusanyo halisi kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ambapo hadi kufikia 30 Juni 2021, jumla ya shilling 106,317,084 zilikusanywa sawa na asilimia 49.45 ya makadirio. Hali hii inaonyesha kuwepo kwa upungufu wa fedha za makusanyo zenye jumla ya shilingi 108,682,916 sawa na asilimia 50.55

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016 kifungu nambari 32(1) (2).

## 6.13 WIZARA YA UJENZI, MAWASILIANO NA UCHUKUZI

### 6.13.1 FUNGU P 01 - WIZARA YA UJENZI, MAWASILIANO NA UCHUKUZI

Ukaguzi wa hesabu za Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi kwa mwaka wa fedha wa fedha 2020/2021 umefanywa kwa mujibu wa Sheria, kanuni, taratibu pamoja na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Taarifa ya Mapato**

Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ilikadiriwa kukusanya jumla ya shilingi 3,387,008,000. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 Wizara ilikusanya jumla ya shilingi 2,509,124,000 sawa na asilimia 74 ya makadirio.

**Taarifa ya Matumizi**

Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ilikadiriwa kutumia jumla ya shilingi 190,975,973,000. Kati ya fedha hizo, shilingi 6,214,000,000 kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida, shilingi 7,351,600,000 kwa ajili ya matumizi ya ruzuku kwa taasisi zilizo chini ya Wizara na shilingi 177,410,373,000 kwa ajili ya matumizi ya kazi za maendeleo.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 jumla shilingi 35,560,738,579 zimeingizwa na kutumika ambapo ni sawa na asilimia 18.62 ya makadirio. Kati ya fedha hizo shilingi 2,543,884,348 zilitumika kwa kazi za kawaida sawa na asilimia 40.94 ya makadirio, shilingi 6,219,037,740 zilitumika ikiwa ni ruzuku kwa taasisi zilizochini ya Wizara sawa na asilimia 84.6 ya makadirio, na shilingi 26,797,816,491 zilitumika kwa kazi za maendeleo sawa na asilimia 15.10 ya makadirio.

**MATOKEO NA MAPENDEKEZO YA UKAGUZI**

#### 6.13.1.1 Dosari katika udhibiti wa matumizi ya mafuta shilingi 17,407,515

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika uwepo wa dosari wa matumizi ya mafuta yanayonunuliwa kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za Ofisi ambapo imebainika kwa mwaka wa fedha 2020/2021 Wizara ya Ujenzi Mawasiliano na Uchukuzi imetumia jumla ya lita 8,895 zenye thamani ya shilingi 17,407,515 ambapo imebainika mafuta hayo hayakutumika kwa shughuli za kiofisi badala yake yalitumika kwa shughuli binafsi za Mkurugenzi Utumishi pamoja na Mkurugenzi wa Mawasiliano hali ya kuwa viongozi hao hulipwa stahiki maalum kwa ajili ya matumizi ya mafuta ili kuhakikisha wanatekeleza majukumu yao kwa ufanisi bila ya kikwazo chochote.

Aidha, ukaguzi umebaini kati ya lita 8,895 zilizonunuliwa kwa ajili ya matumizi ya ofisi jumla ya lita 3,735 zenye thamani ya shilingi 7,309,395 zilitumiwa na Mkurugenzi Utumishi pamoja na lita 5,160 zenye thamani ya shilingi 10,098,120 zilitumiwa na Mkurugenzi wa Mawasiliano jambo ambalo ni ukiukwaji wa taratibu za matumizi ya ofisi pamoja na kutokuzingatia miongozo ya utumishi wa umma inayoelekeza namna bora ya kupunguza kutumia matumizi yasio ya lazima na kuelekeza matumizi ya fedha katika maeneo yalikuwa na kipaumbele cha Serikali. Hata hivyo pamoja na uwepo wa dosari hio ukaguzi umebaini udhaifu uliojitokeza katika udhibiti wa mafuta kwa kukosekana mtumishi mwenye sifa na uadilifu wa  kufanya kazi hio badala yake kazi hio imefanywa na mtu wa asie na uadilifu.

Kutumia mafuta yaliopangiwa shughuli za uwendeshaji wa ofisi kunapelekea kuzorotesha malengo ya uwendeshaji wa shughuli za ofisi kwa mujibu yalivyopangwa na hatimae kupelekea kutokufikiwa kwa malengo yaliyokusudiwa.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara ya Ujenzi na Mawasiliano na Uchukuzi kuhakikisha wanatekeleza majukumu ya kazi yao kwa mujibu wa makadirio ya matumizi ya fedha waliopangiwa ili kuepusha upotevu wa fedha za umma kwa matumizi binafsi ambayo hayana tija na taasisi ya umma. Mchanganuo wa matumizi ya mafuta hayo ni kama inavyoonekana katika **Kiambatisho Nambari 12.**

### 6.13.1.2 Uwepo wa matumizi mabaya ya fedha yatokanayo na ujenzi wa barabara shilingi 353,000,000

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika Wizara ya Ujenzi Mawasiliano na Uchukuzi imefanya uhaulishaji wa fedha zenye thamani ya shilingi 353,000,000 zilizopelekwa Wakala wa Barabara kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya Charawe/Ukongoroni na Kizimbani/Kiboje Mkoa wa Kusini Unguja.

Timu ya ukaguzi ilifanya matembezi ya kutaka kujionea hali halisi pamoja na kupima thamani ya fedha iliotumika na uhalisia wa ujenzi wa barabara ulivyo na kubaini uwepo wa ujenzi usioridhisha kutokana na thamani halisi ya fedha iliotumika kutoendana na hali ya ujenzi uliojengwa kwa hatua ya kifusi jambo ambalo limepelekea kujitokeza kwa mashimo makubwa kwa baadhi ya maeneo na maeneo kuto kupitika kabisa. Katika ufuatiliaji wa matumizi ya fedha ya shilingi 353,000,000 kupitia hati za malipo na vielelezo vyengine kumejitokeza kutokufahamika mchanganuo wa matumizi halisi ya fedha ziliotumika na aina ya vifaa vilivyonunuliwa na kutumika badala yake imebainika fedha nyingi kutumika kwa shuhuli za uwendeshaji ikiwa ni pamoja na masaa ya ziada (over time) pamoja na matengenezo ya vifaa  vya magari vilivyogharimu jumla ya shilingi 191,000,000 bila ya kujulikana kazi iliofanyika ambayo imegharimu malipo ya saa za ziada.

kutokuwepo kwa mchanganuo wa fedha zinazopelekwa Wakala wa Barabara kwa ajili ya ujenzi wa Barabara mbali mbali kunapelekea ugumu wa ufuatiliaji wa matumizi hayo jambo ambalo linaweza kupelekea kujitokeza kwa matumizi yasio tarajiwa.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara ya Ujenzi na Mawasiliano na Uchukuzi kuhakikisha matumizi yote yanayoombewa kufanyiwa matumizi ya barabara ni vyema fedha hizo kuwekewa mchanganuo wake kwa kila hatua yautekelezaji wa ujenzi wa barabara kabla ya fedha hizo kuwasilishwa sehemu husika ili kuweka urahisi wa ufuatiliaji wa vielelezo vya matumizi ya fedha hizo ili kuepuka matumizi yasio ya lazima. Mchanganuo wa matumizi hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli:-

**Jadweli Nambari 208 : Fedha zilizotumika kwa ajili ya ujenzi wa barabara**

| Hati Namba | Kiasi cha fedha zilizolipwa (Tshs) | Maelezo |
|---|---|---|
| 05/01 | 7,469,794 | Malipo baada ya saa za kazi kwa ujenzi wa barabara ya Charawe Ukongoroni. |
| 12/01 | 11,037,577 | |
| 13/01 | 3,801,102 | |
| 49/01 | 262,656 | |
| 04/12 | 2,180,000 | |
| 03/12 | 3,559,874 | |
| 22/12 | 1,406,300 | Ununuzi wa vipuri vya Grader (spare parts) |
| 14/11 | 3,000,000 | Matumizi madogo madogo kwa Wakala wa Barabara |
| 11/10 | 12,583,157 | Malipo ya baada ya saa za ziada kwa ujenzi wa barabara ya Charawe Ukongoroni |
| 14/10 | 2,002,815 | Ununuzi wa chakula cha wafanyakazi |
| 12/4 | 14,565,376 | Malipo ya baada ya saa za kazi kwa barabara ya Ukongoroni Charawe |
| 12/14 | 2,473,941 | Ununuzi wa vifaa vya Bull dozer |
| 12/14 | 1,694,243 | Ununuzi wa vifaa vya magari |
| 12/14 | 1,129,894 | |
| 12/12 | 25,314,874 | Malipo baada ya saa za kazi kwa wafanya kazi walioshiriki kazi ya uwekaji wa lami barabara ya Charawe/ Ukongoroni |
| 12/28 | 11,368,000 | Ununuzi wa vipuri vya magari. |
| 12/29 | 7,679,563 | |
| 10/22 | 12,583,157 | Malipo baada ya saa za kazi kwa barabara ya Charawe Ukongoroni. |
| 10/22 | 2,188,090 | |
| 16/10 | 2,117,814 | |
| 12/1 | 11,037,577 | |
| 13/01 | 3,801,102 | |
| 49/01 | 262,656.00 | |
| 5/1 | 7,469,794 | |
| 27/10 | 1,053,500 | Malipo ya uchukuaji wa picha ya Juu kwa (Model) daraja la Kibonde mzungu |
| 20/10 | 687,960 | Ikiwa ni malipo ya ununuzi wa vifaa kwa matumizi ya Mtambo mpya wa Lami Kibele |
| 19/10 | 4,590,320 | Malipo ya ununuzi wa vifaa kwa matumizi ya mtambo mpya wa lami Kibele. |
| 18/10 | 7,158,900 | Malipo ya ununuzi wa mchanga kwa matumizi ya RAMP ya mtambo mpya wa Lami |
| 23/10 | 3,920,000 | Malipo ya ununuzi wa saruji kwa matumizi ya Ramp ya Mtambo mpya wa Lami |
| 28/10 | 4,110,709 | Malipo ya ununuzi wa vipuri vya Hino Dump Truck TATA Prim SMZ 512B ya Wakala wa Barabara. |
| 24/10 | 1,166,200 | Malipo ya ununuzi wa wa Rain Coat kwa matumizi ya wafanyakazi wa Wakala wa Barabara. |
| 14/10 | 2,002,815 | Malipo ya utoaji wa huduma ya chakula kwa Wafanyakazi wa Wakala wa Barabara walioshiriki kazi ya matengenezo ya barabara ya Jozani-Charawe -Ukongoroni. |
| 20/01 | 4,802,000 | Malipo ya ununuzi wa vifaa vya Gari SMZ 207B IVEGO ya Wakala wa Barabara |
| 26/02 | 1,840,000 | Ununuzi wa vifaa vya Clutch Plate moja kwa ajili ya SMZ 277B ya Wakala wa Barabara. |
| 13/11 | 2,395,400 | Ununuzi wa Injector pump |
| 26/2 | 1,840,000 | Malipo ya vifaa vya Clutch |
| 16/11 | 5,369,000 | Ununuzi wa vifaa kwa ajli ya gari SMZ 273B |
| **Jumla** | **191,926,160** | |

### 6.13.1.3 Dosari zilizojitokeza katika mkataba wa nyongeza (Addendum) wa Mshauri elekezi wa barabara ya Uzi Ng'ambwa wa shilingi 546,107,500

Ukaguzi umepitia mkataba wa nyongeza uliosainiwa tarehe 15 Agosti 2019, baina ya Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi na Kampuni ya MS DAR AL HANDASH CONSULTANTS wenye thamani ya shilingi 546,107,500 kwa kazi ya upembuzi yakinifu na kuandaa Michoro na Kabrasha la zabuni kwa Barabara ya Uzi Ng'ambwa yenye urefu wa kilomita 3.5 kama ilivyoelezwa katika Mkataba.

Dosari iliyobainika katika ukaguzi ni kama ifuatavyo:-

- Ukaguzi umeshindwa kupata muhtasari wa kikao cha Bodi ya zabuni kilichoidhinisha nyongeza hiyo ya mkataba.
- Kukosekana kwa ushindani wa wazi juu ya mkandarasi atakaepewa zabuni ya ujenzi wa Barabara hiyo jambo ambalo limetia shaka juu ya gharama halisi iliowasilishwa.
- Mkataba wa awali Mkandarasi alifanya kazi hiyo kwa barabara mbali mbali za Unguja na Pemba zenye urefu kwa kilo mita 103.5km kwa thamani ya shilingi za kitanzania 4,000,000,000 ikiwa ni sawa na shilingi 38,647,342 kwa kilomita moja, ukaguzi umebaini kilomita 3.5 za nyongeza ya Barabara ya Uzi Ng'ambwa ilifanywa kwa shilingi za Kitanzania 546,107,500 sawa na shilingi 156,030,714 kwa kila kilomita moja, kwa tofauti ya shilingi 351,429,444.
- Kwa vile kazi ya ushauri elekezi wa barabara ya uzi ng'ambwa ya kilomita 3.5 ni tofauti na barabara za awali zenye urefu wa kilomita 103.5 haikupaswa kufanyika kwa (addendum) mkataba wa nyongeza badala yake kulitakiwa kufanyike zabuni mpya ya wazi ili kuwepo na ushindani wa bei.
- Kutokubadilika kwa vigezo na masharti za utekelezaji wa ujenzi wa barabara ya kilomita 3.5 ambayo ni barabara ya mnyanyuko badala yake kutumika kwa vigezo vya barabara ya chini jambo ambalo linaweza kupelekea kukosekana kwa ubunifu wa utekelezaji wa agizo la pili.

Kutokana na kujitokeza kwa athari zilizobainika hapo juu Wizara ina uwezekano mkubwa wa kutumia gharama kubwa za kufanya ushauri elekezi unaotokana na mlinganisho wa matumizi ya fedha yanayotokana na ushauri elekezi wa barabra za chini jambo ambalo linaweza likapelekea upotevu wa fedha za Umma

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara ya ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi kuhakikisha unatekeleza na kuzingatia Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016.

### 6.13.1.4 Kujitokeza kwa viashiria vya upotevu wa fedha za Umma shilingi 1,335,730,533

Katika ukaguzi uliofanyika kwa mwaka wa fedha 2020/2021 imebainika kupitia mfumo wa malipo wa IFMS Wizara ya Ujenzi Mawasiliano na Uchukuzi imefanya malipo mbalimbali kwa ajili ya kuwalipa watoa huduma mbalimbali, dosari iliyobainika katika ukaguzi ni kukosekana kwa hati za malipo, vielelezo vilivyofanyiwa malipo, kurikodiwa kwenye daftari la kumbukumbu za miamala ya fedha (cash book) na kukosekana kwa taarifa za kazi iliyofanyika yenye thamani inayolingana na fedha iliyotumika.

Kutokana na uwepo wa dosari hizo ukaguzi ulifanya mawasiliano na Mhasibu Mkuu wa Hesabu za Serikali na kumtaka atupatie taarifa ya uthibitisho wa matumizi ya fedha ya shilingi 1,335,730,533 pamoja na kutupatia mambo yafuatayo:-

- Hati za malipo kutoka katika mfumo wa IFMS katika ripoti za Central Payment Capital Exp TISS zenye akaunti nambari 9928190704
- Kupatiwa taarifa za kibenki za walipwaji (Vendor Bank Details).
- Kupatiwa vivuli vya "summary voucher list" zilizowasilishwa na Wizara ya Ujenzi katika kitengo cha CPO kwa ajili ya kuombewa malipo.

Kutokana na maombi ya taarifa hizo tuliozoomba kwa Mhasibu Mkuu wa Serikali, ukaguzi umethibitisha kwamba Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi iliingiziwa fedha hizo zenye jumla ya shilingi **1,335,730,533** na kufanya miamala tofauti kwa watoa huduma mbali mbali ikiwemo mtoa huduma SH Trader and Furmigation mwenye nambari ya akaunti nambari 021104003510 katika tawi la benki ya PBZ ambapo imebainika ameingiziwa jumla ya shilingi 216,930,666 kwa nyakati tofauti na miamala yote hiyo imefanyika kwa njia ya uhaulishaji kutoka hesabu ya Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi kwenda kwa mtoa huduma huyo.

Aidha, imebainika mtoa huduma mwengine anaejulikana kwa jina la SAS Construction Ltd mwenye account namba 0451700000 katika tawi la benki ya PBZ ameingiziwa jumla ya shilingi 900,730,060 kwa nyakati tofauti ambapo miamala yote hiyo imefanyika kwa njia ya uhaulishaji kutoka hesabu ya Wizara ya Ujenzi kwenda kwa mtoa huduma huyo.

Pia imebainika mtoa huduma anaejulikana kwa jina la SKIFARU Investment and Engineering Ltd mwenye akaunti namba 0718591001 katika tawi la benki ya PBZ ameingiziwa jumla ya shilingi 218,069,807 kwa nyakati tofauti ambapo miamala yote hiyo imefanyika kwa njia ya uhaulishaji kutoka hesabu ya Wizara ya Ujenzi kwenda kwa mtoa huduma huyo.

Vile vile ukaguzi umefanya mawasiliano na benki Kuu ya Tanzania (BOT) kwa ajili ya kutaka kupatiwa taarifa za uhaulishwaji wa miamala hiyo kutoka Wizara ya Ujenzi kwenda kwa watoa huduma hao, BOT ilitoa taarifa za kibenki (bank statement) kwa njia ya 'soft copy' na 'hard copy' inayothibitisha kufanyika kwa miamala hiyo, hata hivyo ukaguzi uliwasiliana na Benki ya PBZ nayo imethibitisha kufanyika kwa miamala hiyo. **Kiambatisho Nambari 13 Kinahusika.**

Pamoja na uwepo wa ushahidi huo ukaguzi umethibitisha kupokewa kwa fedha hizo na kutumika kinyume na utaratibu jambo ambalo limepelekea kujitokeza kwa vashiria vya upotevu wa fedha kutokana na taarifa za fedha zilizoandaliwa na kuasiniwa na Katibu Mkuu wa Wizara ya Ujenzi Mawasilano na Uchukuzi na kuviwasilisha Ofisi ya Mdhibiti kwa ajili ya kufanyiwa ukaguzi ambapo Ofisi inasikitika kupokea majibu ya Katibu Mkuu yaliyokosa ukweli hasa pale aliposema "hakuna malipo yaliofanywa kwa makampuni hayo katika Wizara ya Ujenzi Mawasiliano na Uchukuzi na ndio maana hakuna vielelezo vyovyote vya malipo hayo labda inawezekana kulikuwa na kasoro katika mtandao iliyojitokeza ikapelekea matatizo hayo".

Kauli hiyo inapingana na kauli ya Mhasibu Mkuu wa Wizara ya Ujenzi Mawasiliano na Uchukuzi inayosema "ni kweli wakati kunafanyika ukaguzi kwenye Wizara malipo hayo yalikosekana vielelezo vya malipo kama taratibu zinavyotaka, hivyo tumechukua hatua kwa kuchukuwa ushauri wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali kulifanyia kazi ya kurekebisha suala hili ili kuondoa kasoro hiyo."

Malipo hayo yalifanyika kupitia mfumo wa malipo IFMIS na yanaonekana katika ripoti ya "Central Payment Capital Exp TISS yenye namba 9928190704 kwa tarehe tofauti kama yanavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 209 : Malipo yaliyofanyika kwa watoa huduma mbali mbali**

| Tarehe ya Muamala | Jina la Mtoa Huduma aliyelipwa | Nambari ya Hesabu | Jina la Benki | Nambari ya Utambulisho wa Benki | Nambari ya Hundi | Kiasi cha Fedha Kilicholipwa (Tshs.) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 19/4/2021 | Sas Construction Ltd | 0451700000 | PBZ | PBZATZTZ | 50002339 | 190,000,000 |
| 19/4/2021 | Sh Trader And Fumigation | 021104003510 | PBZ | PBZATZTZ | 50002340 | 73,786,407 |
| 07/5/2021 | Sh Trader And Fumigation | 021104003510 | PBZ | PBZATZTZ | 50002374 | 63,333,333 |
| 07/5/2021 | Skifaru Investment And Engineering Ltd | 0718591001 | PBZ | PBZATZTZ | 50002375 | 218,069,807 |
| 27/5/2021 | Sas Construction Ltd | 0451700000 | PBZ | PBZATZTZ | 50002429 | 294,086,956.54 |
| 29/6/2021 | Sh Trader And Fumigation | 021104003510 | PBZ | PBZATZTZ | 50002511 | 79,810,926 |
| 29/6/2021 | Sas Construction Ltd | 54120100003482 | PBZ | PBZATZTZ | 50002510 | 416,645,104.36 |
| **Jumla** | | | | | | **1,335,730,533** |

**WIZARA YA UJENZI, MAWASILIANO NA UCHUKUZI – PEMBA**

### 6.13.1.5 Malipo yaliokosa ruhusa ya Mkuu wa Taasisi shilingi 13,756,988

Kifungu nambari 57(2) cha kanuni ya Utumishi wa Umma ya mwaka 2014 kinaeleza kwamba Kazi itakayolazimika kufanywa katika muda wa saa za ziada na ikapelekea kulipwa posho la kufanya kazi hiyo lazima ipatikane idhini ya Katibu Mkuu au Mkuu wa Taasisi kabla ya kazi hiyo kufanyika.

Katika Ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba jumla ya shilingi 13,756,988 zimelipwa kwa watendaji mbali mbali wa Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi Pemba kwa ajili ya malipo ya muda baada ya saa za kazi bila ya kupata idhini ya Mkuu wa Taasisi.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 57(2) cha Kanuni ya Utumishi wa Umma ya mwaka 2014. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 210 : Malipo yaliokosa ruhusa ya Mkuu wa Taasisi**

| Hati namba | Hundi namba | Kiasi cha fedha kilicholipwa (Tshs.) | Maelezo |
|---|---|---|---|
| 1/8 ya 13/08/2020 | - | 807,790 | Malipo baada ya saa za kazi kwa walinzi. |
| 1/8 ya 13/08/2021 | | 2,213,666 | |
| 3/8 ya 19/08/2020 | | 909,378 | |
| 1/1 ya 31/12/2020 | - | 1,555,317 | |
| 2/2 ya 12/02/2021 | 19411 | 2,122,102 | |
| 4/3 ya 11/03/2021 | 19899 | 1,994,214 | |
| 7/3 ya 15/03/2021 | | 655,572 | |
| 7/4 ya 15/04/2021 | 20412 | 2,270,344 | |
| 18/5 ya 25/05/2021 | 21263 | 350,000 | |
| 2/5 ya 06/05/2021 | | 226,679 | |
| 4/6 ya 10/06/2021 | | 651,926 | |
| **Jumla** | | **13,756,988** | |

### 6.13.1.6 Malipo ya huduma ya ulinzi yasiyokua na mkataba shilingi 6,000,000

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Wizara ya Uchukuzi na Mawasiliano Pemba imefanya malipo ya shilingi 6,000,000 kwa ajili ya huduma ya ulinzi kwa Jeshi la Kujenga Uchumi Pemba lakini mkataba wa huduma hiyo umekosekana kwa ukaguzi.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu 139(2) cha Kanuni Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 211 : Malipo ya huduma ya ulinzi yasiyokua na mkataba**

| Hati Namba | Hundi Namba | Kiasi cha fedha kilicholipwa (Tshs.) | Maelezo |
|---|---|---|---|
| 21/10 ya 20/10/2020 | 017758 | 1,200,000 | Malipo ya fedha kwa ajili ya huduma ya ulinzi |
| 3/1 ya 31/12/2020 | 018828 | 2,400,000 | |
| 2/8 ya 13/08/2020 | 016466 | 2,400,000 | |
| **Jumla** | | **6,000,000** | |

### 6.13.1.7 Malipo ambayo hayakukatwa kodi ya zuio shilingi 10,400,000

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba jumla ya shilingi 10,400,000 zimelipwa kwa ajili ya huduma ya ulinzi lakini malipo hayo hayakukatwa kodi ya zuio.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya Zanzibar ya mwaka 2016. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 212 : Malipo ambayo hayakukatwa kodi ya zuio**

| Hati Namba | Hundi Namba | Aliyelipwa | Kiasi cha fedha kilicholipwa (Tshs.) | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 21/10 ya 20/10/2020 | 17758 | Wizara ya UMU | 1,200,000 | Malipo ya fedha kwa ajili ya huduma ya ulinzi |
| 3/1 ya 31/12/2020 | 018828 | Miradi ya JKU Pemba | 2,400,000 | |
| 2/8 ya 13/08/2020 | 016466 | | 2,400,000 | |
| 3/5 ya 07/05/2021 | 20973 | Miradi wa Kujiendeleza KVZ | 4,400,000 | |
| **Jumla** | | | **10,400,000** | |

### 6.13.1.8 Malimbikizo ya madeni ya muda mrefu shilingi 31,977,600

Katika Ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Wizara ya Ujenzi Mawasiliano na Uchukuzi inadaiwa madeni ya muda mrefu na Taasisi za Serikali yenye jumla ya shilingi 31,977,600 kwa ajili ya huduma za Ulinzi na Ujenzi.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya Zanzibar ya mwaka 2016. Mchanganuo wa madeni hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 213 : Malimbikizo ya madeni ya muda mrefu**

| Namba | Jina la Taasisi | Kiasi cha fedha kinachodaiwa (Tshs.) |
|---|---|---|
| 1. | Jeshi la Kujenga Uchumi (JKU) | 22,800,000 |
| 2. | Kikosi cha Valantia (KVZ) | 4,400,000 |
| 3. | Wakala wa Majengo Zanzibar (ZBA) | 4,777,600 |
| **Jumla** | | **31,977,600** |

### 6.13.1.9 Kutokuthibitishwa kazini kwa watumishi waliomaliza muda wa majaribio

Kwa mujibu wa kanuni ya Utumishi wa Umma kifungu nambari 9(1) Bila ya kuathiri kifungu cha 60 cha Sheria ya Ajira, Namba 11 ya 2005, mtumishi yeyote ambae ameajiriwa kwa mara ya kwanza atalazimika kuwemo katika majaribio ya utumishi kwa muda wa miezi kumi na mbili kuanzia tarehe ya kuajiriwa. Aidha Kanuni ya Utumishi wa Umma ya mwaka 2014 kifungu nambari 9(2) kinamtaka Mtumishi wa Umma aliyemaliza muda wa majaribio kuthibitishwa kazini.

Ukaguzi umebaini kwamba pamoja na matakwa ya Kanuni ya Utumishi wa Umma ya Zanzibar ya mwaka 2011, Wizara ya Ujenzi Mawasiliano na Uchukuzi Pemba imeshindwa kuwathibitisha watumishi ambao wamemaliza muda wa majaribio. Orodha ya watumishi hao ni kama ifuatavyo:-

**Jadweli Nambari 214 : Watumishi waliomaliza muda wa majaribio ambao hawajathibitishwa kazini**

| Namba | Jina la Mtumishi | Tarehe ya kuajiriwa |
|---|---|---|
| 1. | Time Abdalla Seif | 1/8/2018 |
| 2. | Issa Shaib Moh'd | 1/10/2019 |
| 3. | Abdul Latif Khalid Abdalla | 1/10/2019 |

### 6.13.1.10 Fedha ambazo hazikuhaulishwa Benki Kuu kipindi cha mwisho wa mwaka shilingi 81,747,539.

Toleo nambari AD./184/01/07/80 la tarehe 9/6/2021 kipengele D kinaeleza kwamba Bakaa ya fedha za Wizara/Idara/Mikoa na Taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (Central Government) zilizokua na Commitment zote ziingizwe katika hesabu Kuu ya Serikali ilioko Benki Kuu nambari 9928161804 (c. Miscellaneous deposit account) na bakaa ambazo hazina Commitment zirejeshwe Mfuko Mkuu wa Hazina (mfuko mkuu wa hazina account nambari 0404381000).

Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 ukaguzi umebaini kwamba baada ya kusitishwa kwa mradi wa ujenzi wa barabara maeneo ya viwanda Chamanangwe jumla ya fedha 81,747,539 zilibaki bila ya kuhaulishwa Benki Kuu hesabu nambari 9928161804 kama sheria inavyotaka na pia zinaendelea kutumika kwa matumizi kinyume na matakwa ya mkataba.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na toleo nambari AD./184/01/07/80 kutoka Ofisi ya Rais Fedha na Mipango.

### 6.13.1.11 Kutumika kwa Fedha za mradi wa ujenzi wa barabara ya Chamanangwe nje ya makubaliano ya mkataba shilingi 7,820,000

Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi Pemba iliingia Mkataba na Wizara ya Baishara na Viwanda Pemba kwa lengo la kujenga barabara za ndani ya eneo la Viwanda kwa muda wa miezi mitatu baada ya kusainiwa kwa mkataba huo kuanzia tarehe 6/8/2020 kwa shilingi milioni mia tatu (300,000,000). Wakati wa kutekeleza mradi huo kulitokea Mgogoro mkubwa kati ya jamii ya maeneo hayo na Serikali na kupelekea Mradi huo kusitishwa. Wakati Mradi unasitishwa jumla ya shilingi **81,747,539** ilikuwa ni bakaa ya fedha iliyobainika katika mradi huo.

Ukaguzi umebaini kwamba jumla ya shilingi **7,820,000** kati ya shilingi **81,747,539** ziliendelea kutumika kwa matumizi mbali mbali ya Ofisi jambo ambalo ni kinyume na makubalino ya mkataba.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume ya makubaliano ya mkataba pamoja na Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 215 : Fedha za mradi wa ujenzi wa barabara ya Chamanangwe**

| Hati Namba | Hundi Namba | Kiasi cha fedha kilicholipwa (Tshs) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 1/7<br>12/7/2021 | 457 | 3,820,000 | W/M/U/P | Malipo kwa ajili ya kwenda na kurudi Dar es salaam kupeleka Barner za mtambo wa lami na kumlipa fundi. |
| 2/7<br>16/7/2021 | 459 | 2,500,000 | W/M/U/P | Malipo kwa ajili ya matengenezo ya Bana |
| 1/8<br>9/8/2021 | - | 1,500,000 | W/M/U/P | Imprest kwa ajili ya malipo ya bana. |
| **Jumla** | | **7,820,000** | | |

### 6.13.2 WAKALA WA KARAKANA KUU YA MAGARI ZANZIBAR

Ukaguzi wa hesabu za mwaka wa fedha 2020/2021 kwa Wakala wa Karakana Kuu ya Magari Zanzibar umefanywa kwa mujibu wa Sheria, kanuni, taratibu pamoja na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Taarifa ya Mapato**

Wakala wa karakana Kuu ya Magari Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ilikadiriwa kukusanya jumla ya shilingi 842,700,000 kutoka katika vyanzo vyake vya mapato. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 Wakala ilikusanya mapato yenye jumla ya shilingi 419,219,509 sawa na asilimia 49.7 ya makadirio.

**Taarifa ya Matumizi**

Wakala wa Karakana Kuu ya Magari Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2020/2021 iliidhinishiwa kutumia jumla ya shilingi 842,700,000 kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 kiasi cha shilingi 398,120,031 kimeingizwa na kutumika kwa kazi za kawaida sawa na asilimia 47 ya makadirio.

**MATOKEO NA MAPENDEKEZO YA UKAGUZI**

### 6.13.2.1 Kukosekana kwa mapato yatokanayo na Mnara na Maduka katika maeneo ya Wakala wa Karakana.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika eneo la Ofisi ya Karakana Kuu ya Magari lina vitega uchumi vya maduka pamoja na uwepo wa mnara wa mawasiliano ambapo maeneo hayo hufanya biashara mbali mbali, dosari iliyobainika katika ukaguzi ni kutokujulikana kwa wamiliki wa vitega uchumi hivyo, wakodishaji walioingia makubaliano na wamiliki wa maeneo hayo, thamani halisi ya fedha iliyokodishwa maeneo hayo pamoja na fedha inayopatikana kutokana na kukosekana mikataba ya ukodishwaji wa maeneo hayo.

Uwepo wa vitega uchumi katika maeneo ya Ofisi ya Karakana Kuu ya Magari ambayo hayajuulikani uingiaji wa mapato yake Serikalini kunatia shaka juu ya uhalali wa vitega uchumi vilivyopo sehemu hizo jambo ambalo linapelekea kuikosesha Serikali mapato yatokanayo na vitega uchumi vilivyopo ndani ya eneo la Karakana.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wizara ya Mawasiliano kupitia Karakana Kuu ya Magari Zanzibar kuchukuwa jitihada za makusudi kuhakikisha vitega uchumi vilivyomo ndani ya eneo la Karakana Kuu ya Magari Zanzibar vinatambulika na kujulikana waliokodishwa pamoja na mapato halisi yanayopatikana kutokana na vitega uchumi hivyo ili kuweza kunufanisha malengo ya uwepo wa vitega uchumi hivyo kwa karakana kuu.

### 6.13.3 BODI YA USAJILI WASANIFU, WAHANDISI, NA WAKADIRIAJI MAJENGO

Ukaguzi wa hesabu za mwaka wa fedha 2020/2021 kwa Bodi ya Usajili Wasanifu, Wahandisi na Wakadiriaji Majengo umefanywa kwa mujibu wa Sheria, kanuni, taratibu pamoja na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Taarifa ya Mapato**

Bodi ya Wasanifu, Wahandisi na Wakadiriaji majengo kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ilikadiriwa kukusanya jumla ya shilingi 412,802,000 kupitia vyanzo vya ndani na shilingi 793,280,000 kupitia misaada na ruzuku kutoka Serikalini.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 Bodi ilikusanya jumla ya shilingi 364,079,970 kupitia vyanzo vya ndani sawa na asilimia 88 ya makadirio na shilingi 136,383,786 kutoka serikalini sawa na asilimia 17 ya makadirio.

**Taarifa ya Matumizi**

Bodi ya Wasanifu, Wahandisi na Wakadiriaji majengo ilikadiriwa kutumia jumla ya shilingi 588,199,000 kwa matumizi ya shughuli mbali mbali za Bodi. Hadi kufikia tarehe 30 Juni ,2021 Bodi ilipokea na kutumia jumla ya shilingi 136,383,786 sawa na asilimia 17 ya matumizi kukiwa na upungufu wa shilingi 656,896,214 sawa na asilimia 83 ya makadirio.

### 6.13.4 WAKALA WA MAJENGO ZANZIBAR

Ukaguzi wa hesabu za mwaka wa fedha 2020/2021 kwa Wakala wa Majengo Zanzibar umefanywa kwa mujibu wa Sheria, kanuni, taratibu pamoja na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Taarifa ya Mapato**

Wakala wa Majengo Zanzibar ilikadiriwa kukusanya jumla ya shilingi 410,000,000 kwa mwaka wa fedha 2020/2021. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 mapato halisi ya Wakala wa Majengo yalikuwa ni shilingi 242,783,000 sawa na asilimia 59.2 ya makadirio.

**Taarifa ya Matumizi**

Wakala wa Majengo ilikadiriwa kutumia jumla ya shilingi 365,000,000 kwa matumizi ya kazi za kawaida kwa mwaka wa fedha 2020/2021, hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 jumla ya shilingi 207,498 000 ziliingizwa na kutumika sawa na asilimia 56.8 ya makadirio.

**MATOKEO NA MAPENDEKEZO YA UKAGUZI**

### 6.13.4.1 Kukosekana kwa Mkataba wa Ununuzi wa Mafuta (Sub Contract) wenye jumla ya shilingi 32,795,700

Katika kupitia hati za malipo pamoja na vielelezo vyake, Ukaguzi umebaini kwamba, Wakala wa Majengo Zanzibar wanapata huduma ya mafuta kutoka kwenye kampuni ya KISAUNI FILLING STATION bila ya kuwa na makubaliano ya kisheria, kufanya manunuzi katika taasisi za Serikali bila ya kuwa na makubaliano ya kisheria ni kwenda kinyume na kifungu nambari 29(m) cha Sheria Nambari 11 ya Ununuzi, Undoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 216 : Ununuzi wa Mafuta bila ya mkataba**

| Hati Namba | Hundi Namba | Thamani (Tshs) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 5\8\2020 | 000223 | 2,091,500 | Kisauni filling station | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa mafuta ya Diesel lita 450 na Petrol 650 kwa matumizi vyombo vya Wakala. |
| 10\8\2020 | 000227 | 2,091,500 | | |
| 4\10\2020 | 000232 | 2,108,500 | | |
| 2\2\2021 | 000257 | 2,046,350 | | |
| 1\3\2021 | 000262 | 2,139,100 | | |
| 8\3B\2021 | 000266 | 2,139,100 | | |
| 2\6\2021 | 000296 | 4,786,700 | | |
| 19\7\2020 | 000353 | 1,973,350 | | |
| 5\11\2020 | 000399 | 2,102,150 | | |
| 24\11\2020 | 000411 | 2,105,900 | | |
| 29\12\2020 | 000438 | 2,061,800 | | |
| 9\1\2021 | 000447 | 2,61,800 | | |
| 4\4\2021 | 000464 | 2,363,050 | | |
| 7\5\2021 | 000471 | 4,786,700 | | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa mafuta ya Diesel lita 900 na Petrol lita 1300 kwa matumizi ya vyombo vya Wakala. |
| **Jumla** | | **32,795,700** | | |

Kukosekana kwa mkataba wa ununuzi wa mafuta kunaweza kuapelekea kuathiri shughuli za Wakala endapo kutatokezea kutofautiana baina ya Wakala wa Majengo na watoa huduma hizo muhimu.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wakala wa Majengo Zanzibar kuandaa mkataba kwa ajili ya kuepuka migogoro endapo itakapojitokeza ili kuweka usawa pande zote mbili kati yao.

### 6.13.4.2 Matumizi ya fedha yaliyofanywa bila ya kuingizwa katika mpango wa manunuzi wa mwaka

Katika kuptia taarifa mbalimbali za hesabu za Wakala wa Majengo, ukaguzi umebaini kuwepo kwa makadirio ya matumizi ya fedha kutoka katika vyanzo vya mapato ya ndani bila ya kuingizwa katika mpango wa manunuzi wa mwaka (Annual Procurement Plan). Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu namba 42(1) cha Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016. Mchanganuo wa matumizi hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

### 6.13.4.3 Matumizi ya fedha yaliyofanywa bila ya kuingizwa katika mpango wa manunuzi wa mwaka

| Namba | Kazi iliyopangwa kutekelezwa | Jumla ya Makadirio (Tshs) | Makadirio ya Fedha kutoka Serikalini (OC) (Tshs) | Matumizi ya fedha kutoka Vyanzo vya ndani ya Taasisi (Tshs) |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Ununzi wa vifaa vya Matengenezo ya Ofisi | 101,172,920 | 84,000,000 | 17,172,920 |
| 2. | Ununzi wa Mafuta | 55,863,250 | 36,300,000 | 19,563,250 |
| 3. | Huduma za Bima | 7,510,353 | 4,700,000 | 2,810353 |
| 4. | Ununuzi wa viburudishaji | 9,540,000 | 8,800,000 | 740,000 |
| 5. | Matengenezo ya vyombo vya Usafiri | 15,129,475 | 12,000,000 | 3,129475 |
| 6. | Ununuzi wa Stationeries | 43,214,225 | 9,542,500 | 33,671,725 |
| 7. | Ununzi wa vifaa vya ICT | 85,558,900 | 14,200,000 | 71,358,900 |
| 8. | Ununzi wa Fanicha | 12,247,500 | 0 | 12,247,500 |
| **Jumla** | | **330,236,623** | **169,542,500** | **160,694,123** |

Kufanya matumizi ambayo yapo nje ya makadirio au Mpango wa manunuzi kunapelekea kujitokeza kwa manunuzi yasiyo ya lazima na hatimae kutokufikiwa kwa lengo lililokusudiwa.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wakala wa Majengo Zanzibar kuhakikisha kuwa kitengo cha manunuzi kinafuata sheria na miongozo iliyowekwa kwa lengo la kufanikisha malengo yaliyokusudiwa na Taasisi kwa mwaka husika.

### 6.13.4.4 Tofauti ya fedha zilizoripotiwa katika hesabu ya mwisho wa mwaka na matumizi halisi shilingi 137,635,517

Katika kupitia taarifa mbali mbali zikiwemo taarifa za Hesabu ya mwaka, daftari la kurikodia kumbukumbu za fedha pamoja na hati za malipo, Ukaguzi umebaini kwamba baadhi ya vifungu vilivyoripotiwa katika taarifa ya Hesabu ya mwisho wa Mwaka vinatofautiana na taarifa za hati za malipo halisi. Mchanganuo wa fedha hizo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 217 : Tofauti baina ya taarifa ya fedha na matumizi halisi**

| Vifungu | Makadirio | Kilichoainishwa katika hesabu (Tshs) | Matumizi halisi kupitia hati za malipo (Tshs) | Tofauti (Tshs) |
|---|---|---|---|---|
| Leave Travel | 9,320,000 | 8,880,000 | 3,775,000 | 5,105,000 |
| Over Time | 23,920,000 | 19,450,000 | 18,788,829 | 661,171 |
| Sitting Allowances | 20,350,000 | 19,200,000 | 4,025,000 | 15,175,000 |
| Food and Refreshments | 7,500,000 | 6,840,000 | 5,830,500 | 1,009,500 |
| Sundry | 8,000,000 | 7,350,000 | 4,991,065 | 2,358,935 |
| Domestic Travel | 57,820,000 | 38,820,000 | 3,100,000 | 35,720,000 |
| Petrol | 16,260,000 | 16,260,000 | 10,281,050 | 5,978,950 |
| Diesel | 16,900,000 | 15,050,000 | 7,121,700 | 7,928,300 |
| Electrisity | 7,800,000 | 6,600,000 | 2,550,000 | 4,050,000 |
| Stationery Supply | 15,457,000 | 15,000,000 | 3,287,362 | 11,712,638 |
| Local Training | 8,400,000 | 6,750,000 | 6,370,000 | 380,000 |
| Maintainace of Motorvehicle | 8,000,000 | 7,700,000 | 3,183,764 | 4,516,236 |
| Leave Travel | 9,320,000 | 8,880,000 | 3,775,000 | 5,105,000 |
| Over Time | 23,920,000 | 19,450,000 | 18,788,829 | 661,171 |
| Purchase of Computer | 4,200,000 | 4,200,000 | 36,330,000 | 32,130,000 |
| Purchase of Furniture | 6,000,000 | 5,196,984 | 10,340,600 | 5,143,616 |
| **Jumla** | **243,167,000** | **205,626,984** | **142,538,699** | **137,635,517** |

Kuwepo kwa tofauti hizo kunapelekea taarifa ya fedha kutotoa sura halisi na sahihi ndani ya hesabu husika ya mwisho wa mwaka ya Wakala wa Majengo.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wakala wa Majengo Zanzibar kuhakikisha kwamba taarifa zote zinazoingizwa katika hesabu ya mwisho wa mwaka zimekamilika na sahihi.

### 6.13.4.5 Kukosekana kwa bei elekezi (fees) kwa ajili ya malipo kwa wateja wa Wakala wa Majengo

Wakala wa majengo imekuwa ikitoa huduma mbali mbali ikiwemo ushauri elekezi, ukodishaji wa nyumba na milango ya maduka, kazi za Seremala, ukodishaji wa mashine ya kokoto na ujenzi wa ofisi na nyumba za Serikali. Dosari iliyobainika katika ukaguzi ni kuwa Wakala wa Majengo wanatoa huduma hizo bila ya kuwepo kwa bei elekezi zilizothibitishwa na Bodi.

Kutokuwa na bei elekezi kunapelekea kufanya malipo kwa bei tofauti (bei ambayo hazijaainishwa) hivyo inapelekea kuikosesha Serikali mapato yake kupitia Wakala.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wakala wa Majengo Zanzibar kuchukuwa jitihada za kuhakikisha kwamba huduma zote zinazotolewa na Wakala wa Majengo zithibitishwe kwa maandishi zikiwemo bei halisi za huduma hizo.

### 6.13.4.6 Ukiukwaji wa makubaliano ya mkataba shilingi 31,000,000

Katika kupitia hati za malipo na mikataba mbalimbali ya kazi za kuendesha Miradi inayosimamiwa na Wakala wa Majengo, Ukaguzi umebaini kuwa katika makubaliano ya mikataba hiyo kupitia kipengele cha malipo, Muajiriwa (ambae ni mtaalam aliekabidhiwa kazi husika) atalipwa malipo yake ya kufanya kazi hiyo kwa awamu mbili tofauti, dosari iliyobainika ni kwamba Wakala wa Majengo wanafanya malipo hayo kwa awamu moja tu. Kufanya hivyo ni kukiuka makubaliano ya mkataba.

Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 218 : Malipo yaliyolipwa kinyume na makubaliano ya Mkataba**

| Hati Namba | Hundi Namba | Thamani (Tshs) | Anaelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 8\7\2020 | 000345 | 4,500,000 | Wakala wa Majengo | Malipo ya fedha kwa ajili ya kazi ya usanifu wa kiuhandisi. |
| 9\7\2020 | 000345 | 4,500,000 | | Malipo ya fedha kwa ajili ya kazi ya kufanya usanifu wa miundombinu kwa mradi wa ZECO. |
| 10\7\2020 | 000345 | 4,500,000 | | Malipo ya fedha kwa ajili ya kazi ya kufanya usanifu wa miundombinu kwa ofisi ya Bodi ya Mikopo Elimu ya Juu. |
| 11\7\2020 | 000345 | 4,500,000 | | Malipo ya fedha kwa ajili ya kazi ya kufanya usanifu wa miundombinu kwa mradi wa ZECO. |
| 4\10\2020 | 000386 | 3,500,000 | | Malipo ya fedha kwa ajili ya kazi ya usanifu wa Ramani za miundombinu kwa mradi wa jengo la Hospitali ya Polisi. |
| 5\10\2020 | 000386 | 2,500,000 | | Malipo ya fedha kwa ajili ya kuandaa makisio ya (BOQ) na Nyaraka za Zabuni kwa mradi wa jengo la Hospitali ya Polisi. |
| 6\10\2020 | 000386 | 3,500,000 | | Malipo ya fedha kwa ajili ya kazi ya usanifu wa ramani miundombinu ya umeme na mawasiliano (ICT) kwa mradi wa jengo la Hospitali ya Polisi. |
| 7\10\2020 | 000386 | 3,500,000 | | Malipo ya fedha kwa ajili ya kazi ya usanifu wa kihandisi (Structural Design) kwa mradi wa jengo la Hospitali ya Polisi. |
| **Jumla** | | **31,000,000** | | |

Kufanya malipo ambayo yanakwenda kinyume na makubaliano ya mkataba na kutofuatwa kwa vipengele muhimu katika mikataba kunapelekea kusababisha Wakala kulipa fedha kinyume na makubaliano jambo ambalo litapelekea kujitokeza kwa matumizi yasiyokubalika na kuingizia hasara Taasisi kwa kulipa gharama zinazoweza kuepukika.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wakala wa Majengo Zanzibar kuhakikisha kuwa vipengele vyote vilivyokuwemo katika mikataba midogo ya kazi vinafuatwa na kutekelezwa kikamilifu ili kuleta ufanisi katika kazi zake na kuiepusha taasisi kuingia hasara.

### 6.13.4.7 Dosari zilizojitokeza katika utekelezaji wa Mikataba ya makubaliano ya ukodishaji wa milango na nyumba mbalimbali zinazosimamiwa na Wakala wa Majengo

Katika kupitia mikataba mbali mbali ya ukodishaji wa milango ya maduka pamoja na nyumba za Viongozi, Ukaguzi umebaini kwamba, katika mikataba hiyo ya makubaliano ya kodi kuna dosari mbali mbali za kiutekelezaji. Baadhi ya dosari hizo ni kama inavyoonekana katika Jadweli lifuatalo:-

### Jadweli Nambari 219 : Dosari zinazotokana na mikataba ya ukodishwaji

| Jina la mteja | Tarehe ya mkataba | Eneo husika | Gharama ya kodi kwa mwezi (Tshs) | Gharama ya kodi kwa miaka miwili | Gharama ya kodi iliyolipwa (shs) | Tofauti (shs) | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Yussuf Haji Khamis | 20/12/2019 hadi 20/12/2020 | Mazizini Sh/ks/50m Nyumba ya kuishi | 60,000 | 720,000 | 120,000 | 600,000 | Mkataba Umemaliza mda na malipo ya kodi hayajakamilika |
| Hassan Khamis Burhan | 01/02/2018 hadi 31/01/2020 | Saateni Mlango wa duka | 150,000 | 3,600,000 | 1,300,000 | 2,300,000 | |
| Makame Mshimba Mbarouk | 03/10/2019 hadi 3/10/2021 | Makunduchi kiwanda cha kokoto | 200,000 | 4,800,000 | 200,000 | 4,600,000 | |
| Ramla Talib Omar | 1/1/2020 hadi 31/12/20 | Mazizini Ks/mz/33 | 60,000 | 720,000 | 180,000 | 540,000 | mkataba mpya na wa zamani kuna miezi kumi (10) haina mkataba na Malipo ya kodi kwa mkataba wa zamani hayajakamilika |
| | 5/11/2021 hadi 4/11/2022 | Nyumba ya kuishi | 100,000 | 1,200,000 | 100,000 | 1,100,000 | |
| Lulu Abdallah Shaaban | 05/11/2021 hadi 04/11/2022 | Vuga 2266 Nyumba ya kuishi | 100,000 | 1,200,000 | 600,000 | 600,000 | Mkataba wa mwaka wa Nyuma haukupatikana |
| Thuwayba E Kissasi | 02/11/2021 hadi 01/11/2022 | Mazizini Sh/ks/53m | 100,00 | 1,200,000 | 300,000 | 900,000 | Mkataba wa mwaka wa Nyuma haukupatikana |
| Juma Hassan Reli | 19/2/2020 hadi 19/2/2021 | Mazizini Sh/ks/60m | 60,000 | 720,000 | 180,000 | 540,000 | Mkataba mpya na wa zamani kuna miezi tisa (9) haina mkataba na Malipo ya kodi kwa mkataba wa zamani hayajakamilika |
| | 02/11/2021 hadi 01/11/2022 | Nyumba ya kuishi | 100,000 | 1,200,000 | 120,000 | 1,080,000 | |
| Jumuiya ya Chan-gamoto | 02/07/2018 hadi 02/07/2020 | Saateni Afisi ya jumuiya | 75,000 | 1,800,000 | 1,800,000 | 0 | Mkataba mpya na wa zamani kuna mwaka mmoja na miezi mine (8) haina mkataba |
| | 02/11/2021 hadi 01/11/2022 | | 150,000 | 1,800,000 | 1,200,000 | 600,000 | |
| Masoud Kamal Basha | 20/12/2019 hadi 20/12/2020 | Mazizini Sh/ks/54m | 60,000 | 720,000 | 360,000 | 360,000 | Mkataba mpya na wa zamani kuna miezi kumi (10) haina mkataba na Malipo ya kodi kwa mkataba wa zamani hayajakamilika |
| | 02/11/2021 hadi 01/11/2022 | Nyumba ya kuishi | 100,000 | 1,200,000 | 300,000 | 900,000 | |
| **Jumla** | | | **1,375,000** | **23,520,000** | **10,360,000** | **15,080,000** | |

Kuwepo kwa mapungufu katika mikataba hiyo kunaweza kuisababishia Wakala wa Majengo kukosa mapato yake ambayo yangesaidia Wakala katika kutekeleza maajukumu waliyojipangia.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wakala kuwa makini katika utekelezaji wa mikataba hiyo na kuhakikisha wateja wao wanafuata na kutii makubaliano yao ili kuhakikisha kwamba mapato yanakusanywa kama ilivyopangwa.

### 6.13.4.8 Kukosekana kwa Mikataba ya makubaliano ya kusimamia Miradi mbalimbali ya kazi za ujenzi wa Nyumba na Majengo ya Ofisi za Serikali

Katika kupitia taarifa mbalimbali za malipo pamoja na mikataba, ukaguzi umebaini kwamba Wakala wa Majengo umekuwa ukisimamia na kutoa ushauri elekezi kwa miradi mbalimbali ya Ujenzi wa Nyumba na Majengo ya Ofisi za Serikali pamoja na kufanya kazi za ujenzi kwa miradi hiyo inapohitajika. Dosari iliyobainika katika ukaguzi ni kwamba baadhi ya Taasisi wanapewa huduma za ushauri elekezi au ujenzi wa miradi yao bila ya kuwa na makubaliano ya kisheria kwa kazi hizo.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 29(m) cha Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016. Taasisi hizo ni kama zinavyoonekana katika Jadweli lifuatalo:-

**Jadweli Nambari 220 : Orodha ya kazi zinazosimamiwa na wakala wa majengo**

| Namba | Taasisi/ Client | Aina ya Kazi | Majukumu ya ZBA | Maendeleo ya Utekelezaji | Mahala pa Kazi |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Wakala wa Majengo | Matayarisho ya Nyaraka za Ujenzi kwa kazi ya Ujenzi wa Nyumba za Mawaziri na Makatibu Wakuu wa SMZ | Kutayarisha Ramani za Ujenzi na BOQ | Utayarishaji wa Ramani na BOQ upo kwenye hatua za mwisho za kukamilika kwake | Fumba, Unguja. |
| 2. | Ofisi ya Rais na BLM Zanzibar | Ujenzi wa jengo jipya la Ofisi ya Raisi wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi – Jengo la ghorofa moja | Hii ni kazi ya kusanifu na kujenga (Design and Build) ambapo ZBA ilitakiwa kutayarisha nyaraka za ujenzi na kujenga. | Kazi imekamilika | Tibirinzi Chakechake Pemba |
| 3. | Tume ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC) | Matayarisho ya nyaraka kwa kazi ya ujenzi wa Afisi ya Tume ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC) | Pre-Contract (Kutayarisha ramani,BOQ na nyaraka za zabuni) | Kazi inaendelea | Maisara, Unguja. |
| 4. | ZEMA | Matayarisho ya nyaraka kwa kazi ya ujenzi wa Afisi ya ZEMA | | | Maruhubi, Unguja. |
| 5. | Wizara ya Afya Zanzibar | Matayarisho ya nyaraka za ujenzi kwa kazi ya ujenzi wa Maabara ya Taifa BSL3 | | Ujenzi umesimama | Binguni,Unguja. |

| Namba | Taasisi/ Client | Aina ya Kazi | Majukumu ya ZBA | Maendeleo ya Utekelezaji | Mahala pa Kazi |
|---|---|---|---|---|---|
| 6. | Wizara ya Kazi,Uchumi na Uwekezaji | Matayarisho ya nyaraka za ujenzi kwa kazi ya ujenzi wa Afisi ya Wizara ya Kazi, Uchumi na Uwekezaji. | Pre-Contract (Kutayarisha ramani,BOQ na nyaraka za zabuni) | Utayarishaji wa Ramani na nyaraka za zabuni unaendelea | M/kwerekwe, Unguja. |
| 7. | Utumishi wa Umma | Matayarisho ya nyaraka za ujenzi kwa kazi ya ukarabati wa jengo la Ofisi ya Mufti Mazizini | | Utayarishaji wa Ramani na nyaraka za zabuni unaendelea kwa kazi ya kukusanya taarifa ya jengo lililopo sasa. | Mazizini,Unguja |
| 8. | Wizara ya Afya | Matayarisho ya michoro kwa ajili ya ukarabati wa kituo cha afya Mbuzini | | Kazi inaendelea | Mbuzini,Unguja |
| 9. | ZFDA | Matayarisho ya nyaraka za ujenzi kwa kazi ya ujenzi wa Afisi na Maabara ya Dawa na Chakula | | | Chamanangwe |
| 10. | Bodi ya Uhaulishaji | Matayarisho ya nyaraka za ujenzi kwa kazi ya ujenzi wa Afisi ya Bodi ya Uhaulishaji | | Mkataba haujasainiwa na malipo hayajafanyika lakini utayarisaji wa ramani na nyaraka za zabuni unaendelea | Gombani, Pemba |
| 11. | Uhamiaji | Matayarisho ya nyaraka za upanuzi wa jengo la Uhamiaji | | Mkataba haujasainiwa na malipo hayajafanyika lakini utayarisaji wa ramani na nyaraka za zabuni unaendelea | Chakechake, Pemba. |
| 12. | Uhamiaji | Matayarisho ya nyaraka za ujenzi wa jengo la Idara ya Uhamiaji | | Mkataba haujasainiwa na malipo hayajafanyika lakini utayarisaji wa ramani na nyaraka za zabuni unaendelea | Mkoani,Pemba. |
| 13. | Uhamiaji | Matayarisho ya nyaraka za ukarabati wa jengo la kupumzikia (Rest House) Idara ya Uhamiaji | | Mkataba haujasainiwa na malipo hayajafanyika lakini utayarisaji wa ramani na nyaraka za zabuni unaendelea. | Chakechake na Mkoani, Pemba. |
| 14. | Uhamiaji | Matayarisho ya nyaraka za ujenzi wa uzio wa nyumba ya Idara ya Uhamiaji (VIP Main House) | | Mkataba haujasainiwa na malipo hayajafanyika lakini utayarisaji wa ramani na nyaraka za zabuni unaendelea. | Chakechake, Pemba. |
| 15. | Uhamiaji | Matayarisho ya nyaraka za Ujenzi wa Afisi ya Idara ya Uhamiaji Mkoa wa Kaskazini Pemba. | | Mkataba haujasainiwa na malipo hayajafanyika lakini utayarisaji wa ramani na nyaraka za zabuni unaendelea. | Wete na Micheweni, Pemba. |

| Namba | Taasisi/ Client | Aina ya Kazi | Majukumu ya ZBA | Maendeleo ya Utekelezaji | Mahala pa Kazi |
|---|---|---|---|---|---|
| 16. | Uhamiaji | Marayarisho ya nyaraka za ujenzi wa Mkahawa wa Idara ya Uhamiaji Mkoa wa Kaskazini Pemba | Pre-Contract (Kutayarisha ramani,BOQ na nyaraka za zabuni) | Mkataba haujasainiwa na malipo hayajafanyika lakini utayarisaji wa ramani na nyaraka za zabuni unaendelea. | Wete,Pemba |
| 17. | Uhamiaji | Matayarisho ya nyaraka za ukarabati wa nyumba za wafanyakazi wa Idara ya Uhamiaji | | Kazi inaendelea. | Micheweni, Pemba |
| 18. | Uhamiaji | Matayarisho ya nyaraka za ukarabati wa uzio wa Ofisi ya Idara ya Uhamiaji | | Mkataba haujasainiwa na malipo hayajafanyika lakini utayarisaji wa ramani na nyaraka za zabuni unaendelea. | Micheweni, Pemba. |
| 19. | ZACPA | Matayarisho ya nyaraka za ukarabati wa jengo la Mpiga Chapa wa Serikali | | Kazi inaendelea | Chakechake, Pemba |
| 20. | Wizara ya Vijana | Usimamizi wa ujenzi wa viwanja vya michezo vya Wilaya ya Mkokotoni | | Ujenzi unaendelea | Mkokotoni ,Unguja |
| 21. | Mkemia Mkuu wa Serikali Zanzibar | Ujenzi wa Afisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali Zanzibar | | Ujenzi umekamilika | Maruhubi, Unguja |
| 22. | Mamlaka ya Udhibiti wa Madawa ya Kulevya Zanzibar | Ukarabati wa jengo la Mamlaka ya Udhibiti wa Madawa ya Kulevya | | Utayarishaji wa ramani, BOQ na nyaraka za ujenzi umekamilika | Migombani, Unguja |
| 23. | Wizara ya Kilimo Zanzibar | Ujenzi wa Soko la Samaki Malindi | | Ujenzi unaendelea | Malindi, Unguja |
| 24. | Wizara ya Kilimo Zanzibar | Ukarabati wa Soko la Samaki Tumbe (Mradi wa SWOFISH) | | Kazi imekamilika | Tumbe, Pemba |
| 25. | Uhamiaji | Ujenzi wa vibanda vya kukagulia wageni wanaoingia katika Uwanja wa Ndege wa AAKIA | | | Uwanja wa ndege wa AAKIA |
| 26. | ZSSF | Ujenzi wa Kisonge Mall | Karani wa Ujenzi (Clerk of Works) | Ujenzi umekamilika | Michenzani, Unguja |
| 27. | Wizara ya Fedha Zanzibar | Ujenzi wa nyumba za maendeleo Kwahani | | | Kwahani, Unguja |
| 28. | MahakamaKuu Zanzibar | Ujenzi wa Mahakama Kuu | | | Tunguu, Unguja |
| 29. | Bodi ya Mapato Zanzibar | Ujenzi wa jengo la Ofisi ya ZRB | | | Gombani, Pemba |
| 30. | Wakala wa Majengo Zanzibar | Ukarabati wa nyumba ya Serikali Mazizini | Usanifu na ujenzi (Design and Build) | Usanifu na ujenzi unaendelea | Mazizini, Unguja |

Kukosekana kwa mkataba kunaweza kuathiri shughuli za Wakala wa Majengo endapo kutatokezea kutofautiana baina ya Wakala na wanaopewa huduma hizo.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wakala wa Majengo Zanzibar kuandaa mikataba ya makubaliano kwa kila Taasisi itakayopewa huduma za ushauri elekezi kwa ajili ya kuepuka migongano itakayojitokeza ili kuweka usawa pande zote mbili.

### 6.13.4.9 Utunzaji wa nyumba za Serikali usioridhisha kwa makaazi ya Viongozi wa Serikali na Watumishi wa Umma

Katika kutembelea na kujionea kazi mbalimbali za maendeleo zinazosimamiwa na Wakala wa Majengo (ZBA) ukaguzi umebaini kwamba Nyumba za Serikali kwa ajili ya Viongozi na Watumishi wa Umma zipo katika hali zisizoridhisha (zimeota mwitu, kuta zimefanya nyufa, mabati yamechoka,mifumo ya makaro hayaridhishi n.k).

Kutozifanyia matengenezo nyumba zinazosimamiwa na Wakala wa Majengo na kutozingatia Utunzaji mzuri wa nyumba hizo kutapelekea nyumba hizo kuharibika zaidi na kusababisha hasara kubwa kwa Serikali.

Uongozi wa Wakala wa Majengo unatakiwa kuchukua juhudi kwa kufanya ukarabati na matengenezo kwa kila jengo linalostahili kukarabatiwa ili kuhakikisha makaazi bora na salama kwa ajili ya Viongozi na Watumishi wa Umma.

### 6.13.4.10 Kutotekelezeka kwa baadhi ya kazi za Maendeleo zinazosimamiwa na Wakala wa Majengo

Ukaguzi umefanya ziara na kutembelea baadhi ya nyumba za viongozi zinazosimamiwa na Wakala wa Majengo na kubaini kuwa Wakala wanafanya ukarabati na kuzijenga vizuri nyumba hizo za Serikali kwa ajili ya viongozi na watumishi wa umma, lakini ujenzi huo umesimama na matengenezo ya nyumba hizo hayafanyiki kwa sasa.

Kusimama kwa kazi za ukarabati wa nyumba za Serikali kutapelekea kuongezeka kwa gharama zaidi za matengenezo hayo na kuchelewa kufikia kwa malengo yaliyopangwa na Serikali.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wakala wa Majengo Zanzibar kuchukua jitihada za makusudi kusimamia harakati zote za ujenzi na ukarabati wa Nyumba ya Serikali ili kuhakikisha unakamilisha kazi zake kwa wakati uliopangwa.

### 6.13.4.11 Kukosekana kwa taarifa muhimu katika uwasilishaji wa taarifa ya hesabu ya mwisho wa mwaka 2020/2021

Katika kupitia taarifa mbali mbali zikiwemo taarifa za Hesabu ya mwisho mwaka 2020/2021 ukaguzi umebaini kwamba Taarifa kamili za kifedha zinazoandaliwa kwa mujibu wa viwango vya Kitaifa na Kimataifa vya uhasibu wa sekta ya Umma kwa misingi ya fedha tasilim (IPSAS Cash Basis) haikukamilika. Taarifa hiyo inajumuisha mapungufu ya taarifa zifuatazo:-

- Kukosekana kwa Taarifa ya Mtiririko wa uingiaji na utokaji wa fedha.
- Ukusanyaji wa mapato yasiyofungamana na vyanzo vya mapato.
- Kukosekana kwa kumbukumbu za makadirio ya fedha ya mapato yanayofungamana na vyanzo vyake.
- Fedha za mapato halisi hazikurikodiwa katika taarifa ya hesabu ya mwisho wa mwaka.

Kukosekana kwa taarifa hizo katika taarifa ya mwisho ya mwaka kunapelekea kwa taarifa ya Fedha ya Wakala wa Majengo kutofikia viwango vya Kitaifa na Kimataifa vya uhasibu (IPSAS) na ukaguzi kushindwa kuthibitisha usahihi wa taarifa zilizomo ndani ya hesabu ya mwaka.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wakala wa Majengo kuhakikisha kwamba utayarishaji wa taarifa ya fedha ya Mwaka unazingatiwa na kufuata taratibu na Misingi yote ya uhasibu iliyowekwa pia Uongozi uhakikishe taarifa zote zinazowekwa katika hesabu ya mwisho zipo sahihi.

### 6.13.4.12 Kutokuwepo kwa makadirio (budget) ya mapato na matumizi ya fedha za Miradi ya Wakala

Ukaguzi umepitia daftari la fedha taslim (cash book) la Wakala wa Majengo la hesabu ya benki nambari 0406703000 na kubaini kwamba jumla ya shilingi 425,679,780.50 zimeripotiwa kukusanywa kupitia vyanzo vyake vya ndani na jumla ya shilingi 591,671,917.70 zimeripotiwa kutumika kupitia makusanyo hayo kwa mwaka wa fedha 2020/2021, hata hivyo Ukaguzi umeshindwa kupata bajeti ya mapato na matumizi ya fedha hizo za ndani kwa Miradi ya Wakala.

Kutokuwepo kwa bajeti ya mapato na matumizi kwa miradi hiyo kunapelekea kufanyika kwa matumizi yasiyo ya lazima na yasiyoidhinishwa.

Uongozi wa wakala unashauriwa kuandaa bajeti ya mapato yatokanayo na vyanzo vya ndani pamoja na bajeti ya matumizi yatokanayo na fedha hizo.

### 6.13.4.13 Kutoainishwa kwa baadhi ya Mapato na Matumizi katika hesabu ya mwisho wa mwaka

Ukaguzi umepitia taarifa ya fedha ya mwaka 2020/2021 pamoja na daftari la pesa taslim (cash books) la hesabu nambari 0406703000 ya Wakala wa Majengo.

Kumbukumbu zilizorikodiwa katika daftari la pesa taslim zinaonesha kwamba jumla ya shilingi 591,671,917.70 zimeshatumika kwa ajili ya uendeshaji na usimamizi wa miradi mbali mbali, aidha jumla ya shilingi 425,679,780.50 zimepatikana kutokana na kazi za ushauri elekezi kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

Ukaguzi umebaini kwamba taarifa hizo za makusanyo (mapato) na matumizi hazikuanishwa katika taarifa ya fedha ya mwaka inayoishia Juni 2021.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na taratibu za uandaaji wa taarifa za fedha pamoja na viwango vya uhasibu.

Kukosekana kwa taarifa hizo katika taarifa ya mwisho wa mwaka kunapelekea kwa taarifa ya Fedha ya Wakala wa Majengo kutofikia viwango vya Kitaifa na Kimataifa vya uhasibu (IPSAS) na ukaguzi kushindwa kuthibitisha usahihi wa taarifa zilizomo ndani ya hesabu ya mwaka.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wakala wa Majengo Zanzibar kuhakikisha kwamba Utayarishaji wa taarifa ya fedha ya Mwaka unazingatia na kufuata taratibu na misingi yote ya uhasibu iliyowekwa pia Uongozi uhakikishe taarifa zote zinazowekwa katika hesabu ya mwisho wa mwaka zipo sahihi.

**WAKALA WA MAJENGO - PEMBA**

### 6.13.4.14 Malipo ambayo hayakukatwa kodi ya zuio shilingi 12,838,937

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba jumla ya shilingi 12,838,937 zimetumika kwa ajili ya matumizi ya Wakala wa Majengo Pemba kwa watoa huduma mbali mbali bila ya kukatwa kodi ya zuio (withholding Tax)

Kutokukata kodi ya zuio kunapelekea kuikosesha Serikali mapato yatokanayo na malipo hayo pia ni kwenda kinyume na kifungu namba 50(2) cha Sheria nambari 7 ya Usimamizi wa Kodi ya Bodi ya Mapato ya mwaka 2009 pamoja na marekebisho yake. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 221 : Malipo ambayo hayakukatwa kodi ya zuio**

| Hati Namba | Hundi Namba | Kiasi cha Fedha kilicholipwa (Tshs) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 08/07 ya 22/07/2020 | 000097 | 1,600,000 | Said Khamis Salum | Malipo kwa ajili ya marekebisho ya Slab Overhang. |
| 11/07 ya 22/07/2020 | 000100 | 500,000 | Mohammed Mbarouk Haji | Malipo kwa ajili ya kazi ya matengenezo ya mashine ya kubanjia kokoto. |
| 09/07 ya 22/07/2020 | 000098 | 7,204,400 | Massoud Othman Lauma | Malipo kwa ajili ya matengenezo ya ofisi. |
| 14/07 ya 27/07/2020 | 000102 | 1,000,000 | Said Khamis Salim | |
| 13/08 ya 24/08/2020 | 000178 | 2,400,000 | Iddi Rajabu Sudi | |
| 14/08 ya 24/08/2020 | 000119 | 800,000 | Abdalla Ali Suleiman | Malipo kwa ajili ya kazi ya ufundi. |
| 02/10 ya 01/10/2020 | 000135 | 2,700,000 | Said Khamis Salim | |
| 15/10 ya 22/10/2020 | 000147 | 3,000,000 | Abdalla Ali Rashid | Malipo kwa ajili ya matengenezo ya ofisi |
| 18/10 ya 26/10/2020 | 000150 | 1,000,000 | | |
| 01/03 ya 29/03/2021 | 000166 | 800,000 | Said Khamis Salim | |
| **Jumla** | | **21,004,400** | | |

### 6.13.4.15 Kukosekana kwa mapato yatokanayo na kodi shilingi 47,195,000

Katika Ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Wakala wa Majengo Pemba inadai Taasisi za Serikali pamoja na watu binafsi jumla ya shilingi 47,195,000 zitokanazo na ukodishaji wa nyumba zinazomilikiwa na Wakala katika Wilaya mbali mbali zilizopo kisiwani Pemba bila ya kufanyiwa ufuatiliaji wa ukusanyaji wa mapato hayo hali ambayo inaweza kupelekea kuikosesha Serikali mapato yatokanayo na ukodishwaji wa nyumba na kupelekea kushindwa kutoa huduma bora zilizokusudiwa kwa jamii ikiwa ni pamoja na gharama za matengenezo ya majengo hayo.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016. Mchanganuo wa malipo yatokanayo na ukodishwaji wa majengo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 222 : Mapato yatokanayo na kodi.**

| Wilaya | Wapangaji | Mahali ilipo | Nambari ya nyumba | Kodi ya mwezi (Tshs.) | Mapato yaliyokosekana (Tshs.) |
|---|---|---|---|---|---|
| WETE | Idrissa Moh'd Abdalla | Ikulu | SMZ-2A | 50,000 | 1,700,000 |
| | Yahya Ali Juma | Ikulu | SMZ-2B | 50,000 | 1,700,000 |
| | Abdalla Khalfan Ali | Ikulu | SMZ-3A | 50,000 | 1,700,000 |
| | Wizara ya Afya | Ikulu | SMZ-3B | 50,000 | 1,700,000 |
| | Mrajis wa mahkama | Uzunguni | SMZ-6 | 60,000 | 2,040,000 |
| | Mkuu wa wilaya wete | Uzunguni | SMZ-5 | 60,000 | 2,040,000 |
| | Raya Mkoko Hassan | Uzunguni | SMZ-8A | 25,000 | 175,000 |
| | Sharifa Humoud | Uzunguni | SMZ-8A | 25,000 | 50,000 |
| | Zainab Ali Abdalla | Uzunguni | SMZ-8B | 25,000 | 45,000 |
| | Asha Ali Juma | Uzunguni | SMZ-9A | 50,000 | 700,000 |
| | Wizara ya Afya | Uzunguni | SMZ-9B | 50,000 | 1,700,000 |
| | Mrajis wa Mahkama | Uzunguni | SMZ-9C | 50,000 | 1,700,000 |
| | Wizara ya Afya | Uzunguni | SMZ-9D | 60,000 | 2,040,000 |
| | Wizara ya Afya | Vuga | SMZ-10A | 60,000 | 2,040,000 |
| | Wizara ya Afya | Vuga | SMZ 10B | 60,000 | 2,040,000 |
| | Suleiman Bakar Suleiman | Vuga | SMZ-10C | 60,000 | 1,965,000 |
| | Wizara ya Afya | Vuga | SMZ-10D | 60,000 | 2,040,000 |
| | Wizara ya Afya | Vuga | SMZ-10E | 60,000 | 2,040,000 |
| | Wizara ya Afya | Vuga | SMZ-10F | 60,000 | 2,040,000 |
| | Mrajis wa Mahkama | Police line | SMZ-16 | 50,000 | 1,315,000 |
| | Wizara ya Afya | Bomani | SMZ-36A | 50,000 | 1,700,000 |
| | Wizara ya Afya | Bomani | SMZ-36B | 50,000 | 1,700,000 |
| | Wizara ya Afya | Bomani | SMZ-37 | 50,000 | 1,700,000 |
| **Jumla ya deni Wilaya ya Wete** | | | | | **35,870,000** |
| CHAKE | Wizara ya Afya | Tenis Court | SMZ-5 | 60,000 | 2,040,000 |
| CHAKE | Maryam Ali Moh'd | Tenis Court | SMZ-6 | 60,000 | 1,965,000 |
| | Wizara ya Afya | Madungu | SMZ-9 | 60,000 | 1,200,000 |
| | Wizara ya Afya | Madungu | SMZ-11 | 60,000 | 2,040,000 |
| | Wizara ya Afya | Madungu | SMZ-12 | 60,000 | 2,040,000 |
| | Wizara ya Afya | Tenis court | SMZ -7 | 60,000 | 2,040,000 |
| | Seif Salim Seif | Madungu | SMZ-15 | 50,000 | 275,000 |
| | Moh'd Khatib Faki | Mdungu | SMZ-16 | 50,000 | 800,000 |
| | Jongo Juma Jongo | Madungu | SMZ-17 | 50,000 | 725,000 |
| | Tabia Issa Moh'd | Madungu | SMZ-9 | 60,000 | 355,000 |
| | Sharif Hamad Khatib | Mdungu | SMZ-10 | 60,000 | 1,940,000 |
| **Jumla ya deni Wilaya ya Chake** | | | | | **15,420,000** |
| **Jumla kuu** | | | | | **47,195,000** |

### 6.13.4.16 Kukosekana kwa muongozo wa huduma ya ushauri elekezi

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Wakala wa Majengo Pemba inatoa huduma ya ushauri elekezi pale inapohitajika na Taasisi za Serikali pamoja na Taasisi binafsi lakini Wakala imekosa muongozo rasmi ambao unaonesha utaratibu wa utowaji wa huduma ya ushauri elekezi pamoja na kiwango stahiki cha tozo kinachotokana na utowaji wa huduma hiyo hali ambayo inaweza kupelekea kutokuwepo kwa usawa wa gharama ya ushauri elekezi inayotolewa baina ya Taasisi moja na nyengine pamoja na kwamba kazi zinazofanyika zinaweza kulingana.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria Namba 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa mali za Umma ya mwaka 2016.

### 6.13.4.17 Kukosekana kwa zabuni ya ujenzi wa lifti shilingi 138,850,241.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba jumla ya shilingi 138,850,241 zimetumika kwa ajili ya ujenzi wa lifti katika jengo la Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi lililopo Tibirinzi Chake Chake Pemba lakini zabuni za kumpata msambazaji wa vifaa hazikufanyika hivyo kukosekana kwa ushindani miongoni mwa wasambazaji wa bidhaa pamoja na uwezekano wa kukosekana kwa tija,ubora wa bidhaa na kutokufikiwa kwa malengo yaliyokusudiwa.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 68 cha Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016. Mchanganuo wa malipo ya ujenzi wa lift ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 223 : Malipo ya ujenzi wa lift.**

| Nambari ya Hati | Nambari ya Hundi | Kiasi cha Fedha kilicholipwa (Tshs) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 4/12<br>7/12/2020 | T.T | 57,351,186 | Derm Elevators Ltd | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi na uingizaji wa lift katika Ofisi ya Rais BLM. |
| 02/05<br>05/05/2021 | TT | 34,410,711 | | |
| **Jumla** | | **138,850,241** | | |

### 6.13.4.18 Malipo kwa watoa huduma ambao hawakusajiliwa na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma shilingi 72,487,358

Kwa mujibu wa kifungu cha 23(1) cha Sheria ya Manunuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma kinaeleza kulingana na masharti ya sheria hii mtu, kampuni au taasisi haitawasilisha zabuni au vyenginevyo kushiriki katika manunuzi ya Umma isipokua chombo kiwe kimesajiliwa na Mamlaka ya Manunuzi.

Kwa mujibu wa kifungu cha 23(2), zabuni kutoka kwa mtu, kampuni au chombo ambacho hakijasajiliwa haifai na hakitazingatiwa na taasisi ya ununuzi.

Ukaguzi umebaini kwamba Wakala wa Majengo Pemba imefanya manunuzi na watoa huduma mbali mbali ambao hawakusajiliwa na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya Zanzibar.

Kufanya hivyo kunapelekea kuikosesha Serikali mapato ambapo ni kwenda kinyume na Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 224 : Watoa huduma ambao Hawakusajiliwa na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma.**

| Hati Namba | Hundi namba | Kiasi cha Fedha kilicholipwa (Tshs) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 05/07 10/07/2020 | 000094 | 7,800,000 | Mohammed S.Massoud | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa saruji na mchanga kwa matumizi ya ujenzi |
| 06/07 16/07/2020 | 000095 | 15,589,840 | | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa shata za milango |
| 15/07 30/07/2020 | 000103 | 4,139,863 | | Malipo kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya ujenzi. |
| 16/07 27/07/2020 | 000105 | 10,377,514 | Al-Hilal General Trading Co. LTD | |
| 05/08 10/08/2020 | 000111 | 3,245,245 | Kansai Plascon znz LTD | |
| 06/08 10/08/2020 | 000112 | 4,243,996 | Kansai Plascon ZNZ ltd | Malipo kwa ajili ya ununuzi wa rangi. |
| 14/08 24/08/2020 | 000119 | 800,000 | Abdalla Ali Suleiman | Malipo kwa ajili ya ufundi wa ufungaji bomba za maji. |
| 13/08 24/08/2020 | 000178 | 2,400,000 | Iddi Rajabu Sudi | Malipo ya fedha kwa ajili ya kazi ya matengenezo ya ofisi. |
| 15/08 25/08/2020 | 000120 | 2,175,000 | Salim Rashid Salim | Malipo ya fedha kwa ajili ya kazi ya ufundi. |
| 05/10 05/10/2020 | 000138 | 7,000,000 | Ali Omar Juma | Malipo kwa ajili ya kazi ya ufungaji wa mfumo wa ulinzi (CCTV). |
| 11/10 22/10/2020 | 000144 | 4,802,000 | Hamad Said Bakar | Malipo kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya ujenzi |
| 12/10 ya 22/10/2020 | 000144 | 6,913,900 | | |
| 15/10 22/10/2020 | 000147 | 3,000,000 | Abdalla Ali Rashid | Malipo kwa ajili ya matengenezo ya ofisi. |
| **Jumla** | | **72,487,358** | | |

## 6.14 WIZARA YA UCHUMI WA BULUU NA UVUVI

### 6.14.1 FUNGU L02 – WIZARA YA UCHUMI WA BULUU NA UVUVI

Ukaguzi wa hesabu za Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi kwa mwaka wa fedha 2020/2021 umefanywa kwa mujibu wa Sheria, kanuni, taratibu pamoja na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Taarifa ya Mapato**

Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ilikadiriwa kukusanya jumla ya shilingi 1,078,623,680. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 Wizara iliweza kukusanya jumla ya shilingi 638,838,001 sawa na asilimia 59.2 ya makadirio.

**Taarifa ya Matumizi**

Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ilikadiriwa kutumia jumla ya shilingi 2,959,801,632 kwa ajili kazi za kawaida na shilingi 25,680,960,000 kwa kazi za maendeleo. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 jumla ya shilingi 1,368,443,527 ziliingizwa na kutumika kwa kazi za kawaida sawa na asilimia 46.2 ya makadirio na shilingi 6,415,992,796 ziliingizwa na kutumika kwa kazi za maendeleo ni sawa na asilimia 25 ya makadirio.

**WIZARA YA UCHUMI WA BULUU NA UVUVI – PEMBA**

### 6.14.1.1 Malipo kwa Watoa huduma ambao Hawakusajiliwa na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma Shilingi 7,506,000.

Kwa mujibu wa kifungu cha 23(1) cha Sheria ya Manunuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma kinaeleza kulingana na masharti ya sheria hii mtu, kampuni au taasisi haitawasilisha zabuni au vyenginevyo kushiriki katika manunuzi ya Umma isipokua chombo kiwe kimesajiliwa na Mamlaka ya Manunuzi.

Kwa mujibu wa kifungu cha 23(2), zabuni kutoka kwa mtu, kampuni au chombo ambacho hakijasajiliwa haifai na hakitazingatiwa na taasisi ya ununuzi.

Ukaguzi umebaini kwamba Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi Pemba imefanya manunuzi na watoa huduma mbali mbali ambao hawakusajiliwa na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya Zanzibar.

Kufanya hivyo kunapelekea kuikosesha Serikali mapato, aidha ni kwenda kinyume na Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 225 : Malipo kwa Watoa huduma ambao Hawakusajiliwa na mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma**

| Hati Namba | Hundi Namba | Kiasi cha fedha kilicholipwa (Tshs.) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 16/3 29/3/2021 | 020293 | 3,039,000 | Zanzibar Petroleum LTD | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa mafuta ya petrol |
| 12/5 19/5/2021 | 021125 | 2,195,000 | | |
| 10/6 16/6/2021 | 022232 | 2,272,000 | | |
| **Jumla** | | **7,506,000** | | |

### 6.14.1.2 Malimbikizo ya madeni ya muda mrefu bila ya kulipwa shilingi 58,766,000

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi Pemba inadaiwa madeni ya muda mrefu na wananchi wa kijiji cha Tumbe yenye jumla ya shilingi 58,766,000 kwa ajili ya fidia ya vipando vilivyokatwa kupitisha umeme.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 29(3) cha Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya Zanzibar ya mwaka 2016.

## 6.15 WIZARA YA BIASHARA NA MAENDELEO YA VIWANDA

### 6.15.1 FUNGU R 01 - WIZARA YA BIASHARA NA MAENDELEO YA VIWANDA

Ukaguzi wa hesabu za Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda kwa mwaka wa fedha 2020/2021 umefanywa kwa kuzingatia Sheria,kanuni, taratibu na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Taarifa ya Mapato**

Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ilikadiriwa kukusanya jumla ya shilingi 2,367,797,000 kupitia vyanzo vyake vya mapato. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 Wizara ilifanikiwa kukusanya jumla ya shilingi 1,449,951,785.72 sawa na asilimia 61 ya makadirio.

**Taarifa ya Matumizi**

Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda kwa mwaka wa fedha 2020/2021, ilikadiria kutumia jumla ya shilingi 23,569,700,000. Kati ya fedha hizo jumla ya shilingi 8,769,700,000 ni kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida na shilingi 14,800,000,000 kwa matumizi ya kazi za maendeleo.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 Wizara ilifanikiwa kupokea na kutumia jumla ya shilingi 7,828,994,723 sawa na asilmia 33.22 ya makadirio. Kati ya fedha hizo shilingi 5,228,443,968 zilitumika kwa ajili ya kazi za kawaida na na shilingi 2,600,550,755 zimeingizwa na kutumika kwa ajili ya kazi za maendeleo.

**MATOKEO NA MAPENDEKEZO YA UKAGUZI**

#### 6.15.1.1 Kutowepo kwa mfumo wa kusajili na kuweka kumbu kumbu za taarifa za walipa kodi

Wakala wa Mizani na Vipimo imeanzishwa kwa Sheria Nambari 6 ya mwaka 2020 ambapo miongoni mwa vipaumbele vyake baada ya kuanzishwa ni kuandaa kanuni ya uwendeshaji muundo na mpango mkakati. Katika mwaka wa fedha 2021 imebainika kukusanya taarifa za mapato ambayo yamehifadhiwa katika mfumo wa kawaida. Dosari iliobainika katika ukaguzi ni kutokuwepo kwa mfumo wa kuwekea taarifa za kumbukumbu za walipa kodi pamoja na kuwepo kwa mapato ya vipimo vya mezania ambayo yanatokana na ukaguzi wa mizani za wafanya biashara bila ya kuwepo kwa idadi maalum inayoonyesha uhalisia wa orodha ya walipaji (authentic list of payees) kulingana na makisio ya makusanyo pamoja na mapato halisi ya Wizara.

Kukosekana kwa mfumo imara wa usajili wa walipa kodi ambao utabainisha idaidi ya walipa kodi waliosajiliwa, waliokuwa hawakusajiliwa na fedha halisi inayopaswa kulipwa kwa kila mlipa kodi kunaweza kupelekea kukosekana kwa udhibiti mzuri wa taarifa za walipa kodi jambo ambalo litapelekea kuikosesha Wizara mapato yaliyokadiriwa na hatimae kutokufikiwa kwa malengo yalikusudiwa.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara uhakikishe unatengeneza mfumo wa kusajili walipa Kodi na kuweka kumbu kumbu za mapato kutoka kwa walipa kodi ili kuweza kupatikana udhibiti na ufanisi katika makusanyo ya kodi jambo ambalo litapelekea kuongeza mapato katika Serikali.

#### 6.15.1.2 Ucheleweshwaji wa fedha kupelekwa benki shilingi 8,824,500

Baada ya kupitia kumbukumbu za mapato kwa Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda ukaguzi umebaini uwepo wa ucheleweshwaji wa mapato kupelekwa benki. Kwa mujibu wa utaratibu wa sheria ya usimamizi wa fedha za umma inawataka Wakuu wa taasisi kuhakikisha fedha zinazokusanywa zinawasilishwa benki kwa wakati ili kuweza kunusuru kujitokeza kwa vitendo vya ukiukwaji wa maadili na kupelekea kuitia hasara Serikali kutokana na upotevu wa fedha utakaoweza kujitokeza. Aidha, kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha ya mwaka 2016.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda kuhakikisha unawasilisha fedha zote kwa wakati uliopangwa kisheria ili kunusuru mizozo itakayoweza kujitokeza kutokana na hatua kali zitakazochukuliwa kwa wale watakaobainika wametenda matendo ya uhujumu wa uchumi.

Mchanganuo wa baadhi ya makusanyo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli la hapo chini:-

**Jadweli Nambari 226 : Fedha zilizocheleweshwa kupelekwa benki**

| Namba ya Stakabadhi | Tarehe ya Makusanyo | Kiasi cha fedha (TShs) | Aliyelipa | Slip Namba | Tarehe ya kupelekwa Benki |
|---|---|---|---|---|---|
| 540508 | 18/2/2021 | 2,250,000 | Feisal Ali Sultan | 0044681 | 28/6/2021 |
| 540507 | 14/1/2021 | 1,440,000 | Khalfan Omar Hilal | 0044680 | 28/6/2021 |
| 082951-082953 | 0/3/2021 | 300,000 | - | 0290149 | 24/6/2021 |
| 540332 | 4/3/2020 | 400,000 | Nhunga Oil | 0041492 | 24/6/2021 |
| 1214786 | 22/7/2020 | 400,000 | Kijangwani Petrol Station | 0041492 | 24/6/2021 |
| 1214784 | 20/7/2020 | 250,000 | Coastal Petrol Station | 0041492 | 24/6/2021 |
| 540501 | 9/9/2020 | 1,200,000 | Shaban Mwinyi Kombo | 0048861 | 18/2/2021 |
| 607252 | 24/12/2020 | 250,000 | Nungwi Kilindi Petro Station | 0023090 | 12/02/2021 |
| 597507-597568 | 18/11/- 19/11/2020 | 441,000 | - | 0203402 | 28/12/2020 |
| 597629-597666 | 31/11 – 1/12/2020 | 272,500 | - | 202414 | 30/12/2020 |
| 540911-540944 | 10/11/2020 | 228,500 | - | 0552833 | 30/12/2020 |
| 540865-540909 | 21/10/ - 9/11/2020 | 288,000 | - | 0588684 | 26/11/2020 |
| 540781 – 540856 | 12/10 -13/10/2020 | 308,000 | - | 0792861 | 18/11/2020 |
| 540484 -540683 | 21/9/ - 30/9/2020 | 796,500 | - | 0831060 | 9/10/2020 |
| **Jumla** | | **8,824,500** | | | |

#### 6.15.1.3 Dosari zilizobainika katika daftari la upokeaji na utoaji wa vitabu vya risiti (Counter Foil Register)

Ukaguzi uliofanyika katika Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda ulipitia daftari la kupokelea na kutolea vitabu vya makusanyo kutoka Wizara ya Fedha (counter foil register) na kubaini dosari zifuatazo:-

- Hakuna mpangilio maalum wa utoaji wa vitabu vya risiti jambo ambalo linaweza kujitokeza utopevu wa vitabu vya risiti.

- Kukosekana kwa majina ya makarani wa mapato wanaokabidhiwa vitabu vya stakabadhi kwa ajili ya ukusanyaji wa mapato.
- Kukosekana kwa taarifa ya fedha wanayoiwasilisha kwa karani mkuu wa ukusanyaji wa mapato ili iweze kujumuisha katika ripoti kuu ya makusanyo ya mapato inayotakiwa kutolewa kila baada ya mwezi au miezi mitatu kwa lengo la kujuwa thamani halisi ya fedha iliyokusanywa kwa mujibu wa makadirio ya kila chanzo cha mapato.
- Kukosekana kwa taarifa za marejesho ya vitabu vilivyotumika na kujaa ambavyo vitaonesha tarehe ya uchukuwaji pamoja na tarehe ya urejeshaji katika buku la kumbukumbu la kurekodia taarifa za stakbadhi hizo.

Kutokana na dosari zilizobainika hapo juu ukaguzi unaushauri uongozi wa wizara kuhakikisha unazifanyia kazi dosari zote zilizobainishwa ikiwemo kuandaa utaratibu maalum wa uanzishwaji wa mfumo wa utunzaji wa taarifa za mapato ili kuhakikisha mapato ya Serikali hayavuji na kutumika kwa maslahi binafsi.

### 6.15.1.4 Kukosekana kwa hati miliki kwa baadhi ya mali zinazomilikiwa na Wizara

Katika ukaguzi uliofanyika wa mwaka unaoishia tarehe 30 Juni, 2021 umebaini kuwa Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda inamiliki maeneo, majengo na milango ya duka na kuikodisha bila la kuwa na hati miliki ya vitu hivyo. Kukosekana kwa hati ya utambulisho wa eneo linalomilikiwa kihalali na wizara linaweza likapelekea kujitokeza kwa migogoro ya ardhi kutokana na kuvamiwa kwa eneo hilo na kuporwa, au kuchukuliwa kinyume na sheria pasi na wizara au Serikali kuweza kutambua jambo ambalo litapelekea kuikosesha Serikali mapato kupitia vyanzo vyake vya mapato.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa wizara kuhakikisha unachukuwa hatua za haraka za kuwasiliana na viongozi wakuu kuhakikisha maeneo hayo yanapimwa kisheria, yanaekewa utambulisho wa kujulikana pamoja na upatikanaji wa hati miliki ya eneo husika. Mchanganuo wa baadhi ya maeneo hayo ni kama ifuatavyo:-

**Jadweli Nambari 227 : Mali zilizokosa hati miliki ambazo zinamilikiwa na Wizara**

| Namba | Aina ya Mali | Mahali Ilipo |
|---|---|---|
| 1. | Nyumba (TIC) | Darajani |
| 2. | Jengo. No.III | Saateni |
| 3. | Mlango wa duka | Darajani |
| 4. | Ghala la Matunda Mnadani | Darajani |
| 5. | Ghala (Usumba) la bidhaa | Mwembe Makumbi |
| 7. | Ghala | Saateni (kwa Abass Hussein) |
| 8. | Kiwanda cha soda Mkunazini Kibokoni | Mkunazini |
| 9. | Kiwanda cha Usumba Meli Nne Unguja | Meli nne |
| 10. | Eneo la kikangoni | Bububu Kikaangoni |
| 11. | Eneo la Kiwanda-Gofu, Mpapa-Bambi | Bambi Mpapa |
| 12. | Kiwanda cha mafuta ya Nazi na Sabuni | Mwanakwerekwe |
| 13. | Duka la vioo kubwa No.1233B | Darajani |
| 14. | Duka la Vioo Vodacom | Lipo katika hatua za Kimahakama na K/Al ghubra |
| 15. | Eneo la viwanda Dunga | Dunga |
| 16. | Eneo la kiwanja Nyamanzi | Dimani |

### 6.15.1.5 Kufanya Malipo bila ya kuwepo kwa Bajeti 13,437,000

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda imefanya matumizi kwa ajili ya ununuzi wa vitu mbalimbali vyenye thamani ya shilingi 13,437,000 kwa ajili ya shughuli za uwendeshaji wa taasisi.

Dosari ilobainika katika ukaguzi ni kufanya malipo bila ya kuwepo kwa bajeti iliyoidhinishwa kwa ajili ya ununuzi wa bidhaa mbalimbali . Kwa mjibu wa utaratibu Wizara inaweza kufanya manunuzi yalio nje ya bajeti ikiwa itazingatia taratibu za uhaulishwaji wa fungu la bajeti kutoka sehemu moja na kutumika sehemu nyengine baada ya kupata idhini ya Mlipaji Mkuu wa Serikali. Hadi ukaguzi unakamilika hatukuweza kupatiwa idhini ya matumizi hayo kutokana na kukosekana taratibu za uhaulishwaji.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara kuhakikisha unafanya uhaulishaji wa fedha kwa mujibu wa miongozo na taratibu za fedha zinavyoelekeza ili kuepusha kujitokeza kwa mianya ya upotevu wa fedha za Umma. Mchanganuo wa matumizi ya fedha hizo ni kama ifuatavyo:-

**Jadweli Nambari 228 : Malipo yaliyofanyika bila ya kuwepo kwa Bajeti**

| Hati namba | Hundi | Kiasi cha fedha (Tshs) | Aliyelipwa | Maelezo | |
|---|---|---|---|---|---|
| 49/1/2021 (11/1/21) | -- | 5,237,000 | Katibu Mkuu | Malipo kwa ajili ya wakulima ambao wameharibikiwa na mazao yao kwa dawa za kiwanda cha sukari mahonda | Ni malipo ya deni la mwaka uliopita. |
| 1/2/21 (29/1/21) | -- | 5,000,000 | Smart Future Co. Ltd | Malipo ya mwisho ya huduma za cctv katika viwanja vya maisara katika maonyesho ya tamasha la biashara januari 2021 | Ni malipo yaliyotakiwa yalipwe kupitia mfuko wa tamasha. |
| 29/5/21 (29/4/21) | 289 of 10/5/21 | 800,000 | Katibu Mkuu WBV | Malipo ya fedha za bakaa la deni marehemu Hemed Bakar Kondo kwa kazi ya matengenezo ya jengo la wizara liliopo malindi Zanzibar | |
| 43/10 (30/9/20) | -- | 2,400,000 | Multi Refrigeration | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa AC 4 zilizotumika katika banda la VIP na banda la siku maalum ya ubunifu kwa wajasiriamali | Matumizi yalipaswa kutoka katika mfuko wa tamasha |
| **Jumla** | | **13,437,000** | | | |

### 6.15.1.6 Mapungufu yaliyojitokeza katika ufungaji wa hesabu

Katika ukaguzi uliofanyika kwa mwaka wa fedha 2020/2021 imebainika Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda haikuweza kuzingatia matakwa ya ufungaji wa hesabu kwa mujibu wa vigezo vilivyowekwa kitaifa na Kimataifa na kupelekea hesabu za Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda kutokuonesha sura sahihi na halisi kwa mujibu wa vigezo vilivyowekwa.

Aidha, ukaguzi ulifanya mawasiliano ya mara kwa mara ikiwemo kuwataka wahusika wafanye marekebisho juu ya dosari zilizobainika ili kuepuka kujitokeza kwa wingi wa hoja za ukaguzi ambazo zitapelekea utolewaji wa hati isiyoridhisha jambo ambalo hawakuweza kulitekeleza hadi ukaguzi unakamilika taarifa za hesabu za Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda zilikuwa na dosari ifuatayo:-

- **Kutofautiana kwa taarifa za Hesabu (Financial Statements) na Daftari la hesabu (Cash Book) kwa miamala iliyowasilishwa.**

Ukaguzi umebaini kuwepo kwa tofauti ya taarifa za hesabu za mwaka (Financial Statement) na malipo halisi yaliyolipwa kupitia hati za malipo mbali mbali ambazo zinaonesha kwa baadhi ya malipo kuwa na miamala mikubwa ya fedha ukilinganisha na uhalisia wa kilichokusanywa jambo ambalo linabainisha makoseo katika taarifa ya makadirio halisi, hesabu za mwisho wa mwaka, na uhalisia wa kilichokusanywa na kupelekea kubainika kwa tofauti. Mchanganuo wa kasoro hizo ni kama inavyoonekana katika jadweli la hapo chini:-

**Jadweli Nambari 229 : Tofauti iliyobainika katika taarifa za hesabu za mwisho wa mwaka**

| Namba | Maelezo | Makadirio (Tshs) | Kilichowasilishwa katika Hesabu za mwisho wa mwaka (Tshs) | Matumizi halisi (Tshs) |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Huduma za Usafi | 63,500,000 | 22,540,790 | 25,410,925 |
| 2. | Manunuzi ya Viyoyozi | 1,800,000 | -- | 2,400,000 |
| 3. | Malipo ya Umeme | 36,000,000 | 15,920,000 | 18,400,000 |
| 4. | Vifaa vya Kuandikia | 84,642,000 | 45,538,761 | 31,198,230 |
| 5. | Posho la safari (Travel allowance) | 116,335,000 | 24,535,400 | 75,309,726 |
| **Jumla** | | **302,277,000** | **85,994,161** | **152,718,881** |

### 6.15.1.7 Kukosekana kwa vielelezo vya matumizi ya shilingi 25,879,358

Katika kazi ya ukaguzi uliofanywa kwa kupitia taarifa za matumizi ulibaini kuwa Mradi ulitumia kiasi cha shilingi 25,879,358 kwa malipo mbali mbali yanayohusu wataalamu kutoka nchini Indonesia kwa ajili ya kutoa ushauri na kusimamia muendelezo wa ujenzi wa Kiwanda cha Mwani.

Dosari iliyobainika katika ukaguzi ni kukosekana kwa vielelezo vinavyothibitisha uhalali wa malipo ya matumizi yaliyofanyika jambo ambalo limepelekea kutia shaka juu ya uhalali wa matumizi hayo.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara kuhakikisha matumizi yote yanaambatanishwa na vielelezo ili kuepuka kujitokeza kwa viashiria vya upotevu wa fedha za umma. Mchanganuo wa matumizi yaliyokosekana vielelezo ni kama inavyoonekana katika jadweli la hapo chini:-

**Jadweli Nambari 230 : Malipo yaliyofanyika ambayo yamekosekana vielelezo**

| Hati namba | Kiasi cha fedha (Tshs) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|
| 1/3/2021 (9/3/2020) | 1,165,580 | Katibu Mkuu WBMV/ kiwanda cha Mwani | Makaazi ya Hotel |
| 2/3/2021 (1/3/2021) | 9,468,272 | | Nauli kwa wataalam kutoa nchini Indonesia. |
| 3/3/2021 (1/3/2021) | 8,771,250 | | Posho kwa wataalamu wawili kutoka Indonesia |
| 4/3/2021 (1/3/2021) | 257,290 | | Nauli ya kurudi Surabaya Jakarta kwa mtaalamu Nd. Hamza |
| 5/3/2021 (1/3/2021) | 102,916 | | Upimaji wa covid 19 kwa wataalam wawili |
| 6/3/2021 (8/3/2021) | 1,120,000 | | Nauli kwa wataalam kutoka nchini Indonesia kwenda Pemba kikazi |
| 7/3/2021 (1/3/2021) | 467,800 | | Fedha kwa ajili ya visa kwa wataalam wawili kutoka Indonesia |
| 10/3/2021 (19/3/2021) | 2,138,500 | | Gharama za malazi na chakula kwa wadau wa ujenzi wa kiwanda cha mwani Chamanagwe |
| 11/3/2021 (25/3/2021) | 1,420,000 | | Ununuzi wa tiketi kwa wataalamu na wahandishi wa ZBA na wadau wa ujenzi wa Kiwanda cha Mwani Chamanangwe |
| 12/3/2021 (25/3/2021) | 967,750 | | Gharama za malazi na chakula kwa mdau wa ujenzi wa Kiwanda cha Mwani |
| | **25,879,358** | | |

**WIZARA YA BIASHARA NA MAENDELEO YA VIWANDA – PEMBA**

### 6.15.1.8 Malipo kwa Watoa huduma ambao hawakusajiliwa na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma shilingi 2,040,500

Kwa mujibu wa kifungu cha 23(1) cha Sheria Nambari 11 ya Manunuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016 kinaeleza kulingana na masharti ya sheria hii mtu, kampuni au taasisi haitawasilisha zabuni au vyenginevyo kushiriki katika manunuzi ya Umma isipokua chombo kiwe kimesajiliwa na Mamlaka ya Manunuzi.

Kwa mujibu wa kifungu cha 23(2), zabuni kutoka kwa mtu, kampuni au chombo ambacho hakijasajiliwa haifai na hakitazingatiwa na taasisi ya ununuzi.

Ukaguzi umebaini kwamba Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda Pemba imefanya manunuzi na watoa huduma mbali mbali ambao hawakusajiliwa na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya Zanzibar.

Kufanya hivyo kunapelekea kuikosesha Serikali mapato, aidha ni kwenda kinyume na Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 231 : Malipo kwa Watoa huduma ambao hawakusajiliwa na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma.**

| Hati namba | Hundi namba | Kiasi cha fedha kilicholipwa (Tshs.) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 10/10 15/10/2019 | 009709 | 168,000 | Mohd Juma Mohd | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa rangi |
| 35/8 24/08/2020 | 017427 | 787,500 | Ali Mohamed Suleiman | Malipo ya fedha kwa ajili ya posho la mazingira hatarishi |
| 20/10 13/10/2020 | 017682 | 980,000 | | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa Risasi za mizani. |
| 10/05 11/05/2021 | 21039 | 105,000 | Pemba Aluminium and Glass work | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa picha |
| **Jumla** | | **2,040,500** | | |

### 6.15.1.9 Malimbikizo ya madeni ya muda mrefu shilingi 28,765,725

Katika Ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda Pemba inadaiwa madeni ya muda mrefu na Taasisi za Serikali, watoa huduma pamoja na wafanyakazi wa Wizara yenye jumla ya shilingi 28,765,725 kwa ajili ya huduma mbali mbali.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 29(3) Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya Zanzibar ya mwaka 2016. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 232 : Malimbikizo ya madeni ya muda mrefu**

| Jina la mdai | Mwaka | Kiasi cha fedha kinachodaiwa (Tshs) | Kiasi cha fedha kilicholipwa (Tshs.) | Deni halisi (Tshs.) |
|---|---|---|---|---|
| Shirika la Magazeti | 2017/2020 | 2,198,500 | 400,000 | 1,798,500 |
| Tahfif Auto Works | 2018/2019 | 5,397,225 | 1,000,000 | 4,397,225 |
| (OR) Fedha na Mipango | 2018/2020 | 1,260,000 | 600,000 | 660,000 |
| Wafanyakazi | 2020/2021 | 21,910,000 | 0 | 21,910,000 |
| **Jumla** | | | | **28,765,725** |

### 6.15.10 Kushindwa kufikia lengo la kukusanya mapato shilingi 50,985,000

Jumla ya shilingi 50,985,000 zilikadiriwa kukusanywa na Wizara Biashara na Maendeleo ya Viwanda Pemba kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

Ukaguzi umebaini kwamba makadirio haya ni makubwa ukilinganisha na makusanyo halisi kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ambapo hadi kufikia 30 Juni 2021, jumla ya shilingi 30,907,750 zilikusanywa sawa na asilimia 60.62 ya makadirio. Hali hii inaonyesha kuwepo kwa upungufu wa fedha za makusanyo zenye jumla ya shilingi 20,077,250 sawa na asilimia 39.38

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya Zanzibar nambari 12 ya mwaka 2016 kifungu nambari 32(1) (2).

### 6.15.2 WAKALA WA MAENDELEO YA VIWANDA VIDOGO VIDOGO, VIDOGO NA VYA KATI (SMIDA)

Ukaguzi wa hesabu za Wakala wa Maendeleo ya Viwanda Vidogo Vidogo, Vidogo na vya Kati kwa mwaka wa fedha 2020/2021 umefanywa kwa mujibu wa Sheria, kanuni, taratibu pamoja na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Taarifa ya Mapato**

Wakala wa Maendeleo ya Viwanda Vidogo Vidogo, Vidogo na vya Kati kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ilifanikiwa kukusanya jumla ya shilingi 303,792,286 kutokana na uuzaji wa vitakasa mikono. Mapato hayo hayakukadiriwa kwa sababu chanzo cha mapato hayo yamepatikana kutokana na mripuko wa maradhi ya korona.

**Taarifa ya Matumizi**

Wakala wa Maendeleo ya Viwanda Vidogo Vidogo, Vidogo na vya Kati kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ilikadiriwa kutumia jumla ya shilingi 2,076,000,000. Kati ya fedha hizo shilingi 1,076,000,000 kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida na shilingi 1,000,000,000 kwa matumizi ya kazi za maendeleo.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni 2021 Wakala imeingiziwa jumla ya shilingi 300,960,192.26 sawa na asilimia 14.50 ya makadirio. Kati ya fedha hizo jumla ya shilingi 289,252,537.26 kwa kazi za kawaida sawa na asilimia 27 ya makadirio na shilingi 11,707,655.00 kwa kazi za maendeleo ambazo ni sawa na asilimia 1.17 ya makadirio.

**MATOKEO NA MAPENDEKEZO YA UKAGUZI**

#### 6.15.2.1 Kutokurejeshwa kwa fedha za mikopo ya Wajasiriamali shilingi 212,719,000

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwa Jumla ya shilingi 284,791,000 zimetolewa kwa ajili ya kuwakopesha wajasiriamali mbali mbali lakini baada ya kupitia kumbukumbu za mikopo iliyotolewa zinaonyesha kuwa ni jumla ya shilingi 72,072,000 ndizo ambazo zimeweza kurejeshwa hivyo kupelekea kuwepo kwa Jumla ya shilingi 212,719,000 ambazo hazikuweza kurejeshwa.

Kufanya hivyo kunapelekea kutopatikana kwa fedha amabazo zingeweza kutumika kwa ajili ya kuwakopesha wajasiriamali wengine. Hali halisi ya mikopo iliyotolewa pamoja na urejeshwaji wa mikopo hiyo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

Ukaguzi unashauri Uongozi wa Wakala uhakikishe kwamba wahusika wote waliopatiwa mikopo wanafuatiliwa kikamilifu ili kuweza kufanya urejeshwaji wa mikopo iliyotolewa kwa wakati ili kuweza kupata fedha amabzo zingeweza kutumika kwa ajili ya kuwakopesha wajasiriamali wengine.

**Jadweli Nambari 233 : Mikopo ambayo haikuweza kurejeshwa na wajasiriamali**

| Hati namba | Mkopaji | Kiasi cha fedha za mkopo uliotolewa (Tshs) | Kiasi cha fedha kili-chopangwa kurejeshwa (Tshs) | Tarehe ya mwisho kulipa | Muda wa mkopo (miezi) | Kiasi cha fedha kilichorejeshwa (Tshs) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 19/26 | Suleiman Rashid | 5,000,000 | 5,000,000 | 25/1/2020 | 3 | 5,000,000 |
| 19/27 | Ahmada Abdalla | 5,000,000 | 5,000,000 | 25/1/2020 | 3 | 5,000,000 |
| 19/7 | Anfal | 5,000,000 | 5,500,000 | 10/3/2020 | 12 | 200,000 |
| 19/4 | ZANOP | 10,000,000 | 11,000,000 | 11/1/2020 | 12 | 9,200,000 |
| 19/6 | Handloom | 10,000,000 | 11,000,000 | 11/1/2020 | 12 | 5,200,000 |
| 20/1 | Abham | 20,000,000 | 22,000,000 | 31/12/2020 | 12 | 2,700,000 |
| 20/23 | Rehema Said | 500,000 | 500,000 | 30/1/2020 | 1 | 160,000 |
| 20/24 | Wasila Said | 500,000 | 500,000 | 30/1/2020 | 1 | 120,000 |
| 20/25 | Masika Said | 500,000 | 500,000 | 30/1/2020 | 1 | 80,000 |
| 20/16 | Wema Cooperative | 5,000,000 | 5,500,000 | 4/1/2021 | 12 | 800,000 |
| 20/20 | Mshimba Food | 16,000,000 | 17,600,000 | 6/7/2020 | 6 | 200,000 |
| 20/3 | Fauz | 15,000,000 | 16,500,000 | 30/12/2020 | 12 | 2,550,000 |
| 20/8 | Faki Rice | 5,000,000 | 5,500,000 | 30/3/2020 | 3 | 3,000,000 |
| 20/11 | Kusudio Sio Hilo | 4,000,000 | 4,400,000 | 1/3/2021 | 12 | 1,400,000 |
| 20/14 | Shina Association | 6,650,000 | 7,315,000 | 30/4/2021 | 12 | 1,100,000 |
| 20/12 | Mohd's tin works | 2,000,000 | 2,200,000 | 30/9/2020 | 6 | - |
| 20/15 | Jam's tin works | 2,000,000 | 2,200,000 | 30/9/2020 | 6 | - |
| 20/22 | Idrissa Jecha | 2,641,000 | 2,641,000 | 30/6/2020 | 2 | 2,642,000 |
| 20/5 | Rajab | 10,000,000 | 11,000,000 | 30/9/2020 | 18 | 2,400,000 |
| 20/2 | ZSH | 15,000,000 | 16,500,000 | 30/12/2020 | 18 | 1,870,000 |
| 20/17 | Alpha Quqlity Chalk | 20,000,000 | 22,000,000 | 30/6/2022 | 24 | 1,400,000 |
| 20/13 | Huasa Zan Trading | 19,000,000 | 20,900,000 | 30/6/2022 | 24 | 8,000,000 |
| 20/19 | Salah & Sons | 20,000,000 | 22,000,000 | 30/6/2022 | 24 | 5,000,000 |
| 20/10 | Bin Pandu Enterp | 16,000,000 | 17,600,000 | 30/1/2022 | 18 | 500,000 |
| 20/21 | Kangaroo | 30,000,000 | 33,000,000 | 30/1/2022 | 18 | 6,500,000 |
| 20/9 | Amani Salt | 5,000,000 | 5,500,000 | 1/9/2021 | 12 | 300,000 |
| 20/18 | Lipi Cooperative | 35,000,000 | 38,500,000 | 3/3/2023 | 30 | 6,750,000 |
| **Jumla** | | | | | | **72,072,000** |

**WAKALA WA MAENDELEO YA VIWANDA VIDOGO VIDOGO NA VYAKATI (SMIDA) - PEMBA**

### 6.15.2.2 Hati za malipo zenye vielelezo pungufu shilingi 3,400,000

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba jumla ya shilingi 3,400,000 zimelipwa kwa matumizi mbali mbali ya Wakala (SMIDA) Pemba lakini baadhi ya vielelezo vya matumizi hayo havikuambatanishwa katika hati za malipo ili kuweza kuthibitisha uhalali wa malipo hayo.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu 34(1) cha Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 234 : Hati za malipo zenye vielelezo pungufu**

| Hati Namba | Hundi namba | Kiasi cha fedha kilicholipwa (Tshs.) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 3/9 10/9/2020 | 000043 | 400,000 | Zanzibar Petroleum Ltd. | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa mafuta ya petrol. |
| 1/11 7/11/2020 | 000047 | 3,000,000 | Khalfan Salim Ali | Malipo ya fedha kwa ajili ya msaada kwa kiwanda cha mafuta ya alizeti. |
| **Jumla** | | **3,400,000** | | |

### 6.15.3 TAASISI YA VIWANGO ZANZIBAR (ZBS)

Ukaguzi wa hesabu za Taasisi ya Viwango Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2020/2021 umefanywa kwa mujibu wa Sheria, kanuni, taratibu pamoja na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Taarifa ya Mapato**

Taasisi ya Viwango Zanzibar (ZBS) kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ilikadiriwa kupata jumla ya shilingi 9,125,320,000. Kati ya fedha hizo shilingi 625,700,000 ni ruzuku ya mshahara, shilingi 277,800,000 kwa ajili ya kazi nyenginezo, na shilingi 3,000,000,000 kwa ajili ya kazi za maendeleo. Ambazo ni sawa na shilingi 3,903,500,000 ni makadirio mapato ya ruzuku kutoka Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda.

Na shilingi 5,221,820,000 ni makadiriyo ya mapato ya makusanyo kutoka katika vyanzo vyake mbali mbali vya ndani ya Taasisi.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 Taasisi ilipokea jumla ya shilingi 4,047,937,004.51 .Kati ya fedha hizo shilingi 901,224,765 ni kutoka Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda (Ruzuku), ambazo fedha hizo shilingi 818,773,515 ni ruzuku ya mishahara sawa na asilimia 130 ya makadirio,na shilingi 82,451,250 ni ruzuku ya mapato kwa kazi nyenginezo(OC) sawa na 30% ya makadirio, kukiwa na ongezeko la asilimia 30 kwa upande wa mapato ya mishahara na upungufu wa asilimia 70 katika mapato ya kazi nyenginezo (OC).

Aidha Taasisi ya Viwango Zanzibar ilikusanya jumla ya shilingi 3,146,712,239.51/- kutoka vyanzo vyake vya ndani sawa na asilimia 60 ya makadirio kukiwa na upungufu wa 2,075,107,760.49 sawa na asilimia 40. Mchanganuo wa makadirio na mapato halisi ya Taasisi ya Viwango Zanzibra (ZBS) ni kama unavyoonekana katika jaduweli hapo chini:-

**Taarifa ya Matumizi**

Taasisi ya Viwango Zanzibar (ZBS) kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ilikadiriwa kutumia jumla ya shilingi 9,117,128,000, kati ya fedha hizo shilingi 1,949,372,593.00 ni makadirio ya kwa matumizi ya mishahara na maposho na shilingi 7,167,755,407.00 ni makadirio ya matumizi mengineyo ya kazi za kawaida.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 Taasisi ilifanikiwa kutumia jumla ya shilingi 3,821,261,704.77 sawa na asilimia 42 ya makadirio. Kati ya fedha hizo shilingi 2,061,077,562.00 ni matumizi ya mishahara na maposho, na shilingi 1,760,544,142.77 ni kwa matumizi mengineyo ya kawaida.

**MATOKEO NA MAPENDEKEZO YA UKAGUZI**

### 6.15.3.1 Kukosekana kwa ufanisi katika ukusanyaji wa mapato shilingi 5,077,432,973.75

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Taasisi ya Viwango Zanzibar ilikadiria kukusanya mapato kupitia vyanzo mbali mbali kwa mwaka wa fedha 2020/2021 lakini ufanisi katika ukusanyaji wa mapato hayo haukupatikana na kutokuwepo ukadiriaji mdogo kwa baadhi ya vianzio, baadhi ya vyanzo kutokukusanywa mapato kama ilivyopangwa.

Kufanya hivyo kunaweza kupelekea kuwepo kwa upotevu wa mapato, aidha ni kwenda kinyume na kifungu nambari 32(1)(2) cha Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016. Mchanganuo wa mapato hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 235 : Kukosekana kwa ufanisi katika ukusanyaji wa mapato**

| Chanzo cha Mapato | Makadirio yaliyopangwa (Tshs) | Mapato Halisi Yaliyokusanywa (Tshs) | Tofauti ya mapato iliyojitokeza (Tshs) | Asilimia (%) |
|---|---|---|---|---|
| Ruzuku kutoka Serikalini | 3,903,500,000 | 901,224,765 | 3,002,275,235 | 23.8 |
| FOB | 584,380,000 | 96,575,080.35 | 487,804,919.65 | 16.5 |
| Mapato ya Ukaguzi | 3,116,840,000 | 2,246,209,929.27 | 870,630,070.73 | 72 |
| Ada ya Majaribio | 1,161,600,000 | 498,399,134.78 | 663,200.865.22 | 42.9 |
| Ada ya uthibitisho | 18,000,000 | 19,776,954 | (1,776,954) | 109.9 |
| Ada ya mafunzo | 10,000,000 | 0 | 10,000,000 | - |
| Faini | 66,000,000 | 300,000 | 65,700,000 | 0.45 |
| Batch | 201,600,000 | 237,534,629.50 | (35,934,629.50) | 117.82 |
| Fomu za maombi | 56,200,000 | 45,261,533.35 | 10,938,466.65 | 80.5 |
| Mauzo ya Bidhaa | 7,200,000 | 2,605,000 | 4,595,000 | 36 |

### 6.15.3.2 Malipo kwa wazabuni wasiosajiliwa na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma shilingi 14,276,945

Kwa mujibu wa kifungu cha 23(1) cha Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016 kinaeleza kulingana na masharti ya sheria hii mtu, kampuni au taasisi haitawasilisha zabuni au vyenginevyo kushiriki katika manunuzi ya Umma isipokua chombo kiwe kimesajiliwa na Mamlaka ya Manunuzi.

Kwa mujibu wa kifungu cha 23(2), zabuni kutoka kwa mtu, kampuni au chombo ambacho hakijasajiliwa haifai na hakitazingatiwa na taasisi ya ununuzi.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Taasisi ya Viwango Zanzibar imetoa zabuni kwa watoa huduma mbali mbali ambao hawakusajiliwa na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya Zanzibar.

Kufanya hivyo kunapelekea kuikosesha Serikali mapato, ambapo ni kwenda kinyume na Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 236 : Malipo kwa wazabuni wasiosajiliwa na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma**

| Hati Namba | Hundi Namba | Kiasi cha fedha kilicholipwa (Tshs) | Aliyelipwa | Maelezo | |
|---|---|---|---|---|---|
| 15/8 | 1011 | 4,562,880.00 | Nalasa Perfect Company | Malipo kwa ajili ya ununuzi wa viburudishaji matumizi ya ofisi. | Mzabuni amesajiliwa kutoa huduma ya ulinzi na usafi. |
| 2/8 | 1006 | 2,245,065.00 | Juma Foum Mcha | | Mzabuni amesajiliwa kuuza vifaa vya ujenzi. |
| 26/9 | 1031 | 7,469,000.00 | Double two General Supply | Malipo kwa ajili ya ununuzi wa AC | Mzabuni amesajiliwa kuuza vifaa vya kuandikia. |
| **Jumla** | | **14,276,945** | | | |

## 6.15.4 WAKALA WA USAJILI WA BIASHARA NA MALI ZANZIBAR (BPRA)

Ukaguzi wa hesabu za mwaka wa fedha 2020/2021 kwa Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali Zanzibar (BPRA) umefanywa kwa mujibu wa Sheria, kanuni, taratibu pamoja na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Taarifa ya Mapato**

Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali Zanzibar ilikadiriwa kukusanya jumla ya shilingi 1,666,068,313 kwa mwaka wa fedha 2020/2021. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 Wakala ilikusanya jumla ya shilingi 1,589,295,005 sawa na asilimia 95.4 ya makadirio.

**Taarifa ya Matumizi**

Wakala wa usajili wa Biashara na Mali Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ilikadiriwa kutumia jumla ya shilingi 1,666,068,313 kwa matumizi ya kazi za kawaida. Hadi kufikia tarehe 30 Juni , 2021 Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali Zanzibar iliingiziwa na kutumia jumla ya shilingi 1,586,295,005 kwa kazi za kawaida sawa na asilimia 99.2 ya makadirio.

**MATOKEO NA MAPENDEKEZO YA UKAGUZI**

### 6.15.4.1 Upungufu wa Watendaji katika Taasisi ya Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali.

Ukaguzi umebaini kwamba Taasisi ya Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali ina upungufu wa watendaji katika vitengo vyake mbalimbali katika kutekeleza majukumu yake ya kila siku, ili kufikia ufanisi katika uwajibikaji inapaswa uwepo wa watendaji zaidi ili kufikia malengo yaliyopangwa kwa kukabiliana na majukumu yao.

Kuwepo kwa upungufu wa wafanyakazi utapelekea taasisi kushindwa kufikia malengo waliyojipangia na hatimae kujitokeza kwa mrundikano wa majukumu ya kazi ambayo yatapelekea taasisi kutumia fedha nyingi kulipa wafanyakazi muda wa ziada (overtime).

Ukaguzi unashauri jitihada za makusudi zichukuliwe kuondoa tatizo hilo ikiwemo kuliripoti Serikalini ili waweze kupatiwa wafanyakazi wa kuazimwa kwa muda mfupi kwa mujibu wa kifungu nambari 12(2)(3) cha Kanuni za Utumishi wa Umma ya mwaka 2014. Mchanganuo wa watendaji waliopo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 237 : Upungufu wa watumishi katika vitengo mbali mbali**

| Namba | Idara | Watendaji wanaohitajika | Watendaji walioopo sasa | Upungufu |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Sehemu ya Hesabu | 5 | 4 | 1 |
| 2. | Mkaguzi wa ndani | 2 | 0 | 2 |
| 3. | Kitengo cha sheria | 2 | 0 | 2 |
| 4. | Manunuzi | 3 | 1 | 2 |
| 5. | Mipango | 2 | 1 | 1 |
| **Jumla** | | **14** | **6** | **8** |

### 6.15.4.2 Malipo yenye vielelezo pungufu yenye thamani ya shilingi 21,636,873.6

Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali wamefanya matumizi mbalimbali katika kufanikisha majukumu yao waliyojipangia yenye thamani ya shilingi 21,636,873.6. Dosari iliyobainika katika ukaguzi ni kuambatanisha vielelezo pungufu katika hati za malipo jambo ambalo limepelekea kushindwa kuthibitisha uhalali wa matumizi hayo. Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 238 : Malipo yenye vielelezo pungufu**

| Hati namba | Hundi namba | Aliyelipwa | Thamani (Tshs) | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 6/8/2020 | T.T | Zantel | 4,829,645.60 | Malipo ya huduma za mtandao. |
| 2/10/2020 | 000818 | Wakala wa usajili wa biashara na mali | 800,000 | Malipo ya fedha kwa ajlii ya posho. |
| 3/10/2020 | T.T | Mohammed Salim Hamdoun | 1,710,000 | Sadaka ya Idd kwa wafanyakazi wa BPRA. |
| 7/10/2020 | T.T | Babesh catering cleaning | 1,900,000 | Huduma za usafi |
| 16/1/2021 | 000837 | Wakala wa usajili biashara na mali. | 1,313,004 | Mzee Batromeo Kassin (mrithi ni Hilda) |
| 6/1/2021 | 000828 | | 1,750,000 | Malipo ya fedha kwa ajili ya Posho. |
| 9/1/2021 | 000827 | Babesh catering cleaning | 1,900,000 | Malipo ya hudma za usafi. |
| 18/1/2021 | 000858 | GBS Company limited cleaner | 828,000 | |
| 23/1/2021 | 000832 | Rashid Said Ali | 448,400 | Ununuzi wa meza. |
| 5/2/2021 | 0008467 | Mao General Supplies Computer | 1,147,252 | Utengenezaji wa gril za madirisha ya ofisi. |
| 13/5/2012 | 000880 | | 1,090,572 | Utengenezaji wa gril. |
| 7/2/2021 | 000850 | Wakala wa usajili wa Biashara na Mali | 3,420,000 | Malipo kwa ajili ya safari ya kikazi Dodoma. |
| 19/2/2021 | 000860 | | 500,000 | Malipo kwa ajili ya safari ya kikazi Dar es Salaam. |
| **Jumla** | | | **21,636,873.6** | |

Kukosekana kwa vielelezo hivyo katika hati za malipo kwa ukaguzi kunapelekea kupatikana kwa hati ambazo hasijakamilika na kupelekea ukaguzi kushindwa kujiridhisha juu ya uhalali wa malipo hayo.

Uongozi wa wakala unashauriwa kuhakikisha kwamba vielelezo vyote vinavyohusiana na hati husika vinaambatanishwa pamoja kwa ajili ya ukaguzi kwa wakati

### 6.15.4.3 Ucheleweshaji wa Kuwasilisha Malipo ya ZSSF shilingi

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali (BPRA) hutekeleza wajibu wa kuwakata watumishi wa umma fedha za mchango wa Mfuko wa Hiari kwa asilimia saba (7%) kutokana na mishahara yao pamoja na kuchangia asilimia kumi na tatu (13%) ya mchango wa Serikali kwa lengo la kuwasilisha michango hiyo katika Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (ZSSF) kwa mujibu wa sheria ya Mfuko wa hifadhi ya Jamii nambari 2 ya mwaka 2005 pamoja na marekebisho yake ya mwaka 2010.

Kwa mujibu wa Sheria ya Uanzishwaji wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii inazitaka taasisi za umma kuwasilisha michango ya watumishi wao ndani ya kipindi cha siku 15 bila ya kuchelewa ili kuepukana na malipo ya tozo ya adhabu. Dosari iliyobainika katika ukaguzi ni ucheleweshwaji wa mikato hiyo kuwasilishwa ZSSF jambo ambalo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 17(3) cha Sheria ya Uanzishwaji wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii nambari 2 ya mwaka 2005 pamoja na marekebisho yake ya mwaka 2010.

Ucheleweshwaji wa mikato ya wafanyakazi kuwasilishwa kwa wakati kunaweza kukapelekea upotevu wa fedha za umma na matumizi mabaya ya fedha za Serikali na hatimae kujitokeza kulipa fedha za ziada zinazotokana na tozo ya adhabu ya ucheleweshwaji wa fedha kupelekwa kwa wakati.

Ukaguzi unashauri uongozi wa ZBPRA kuhakikisha unawasilisha mikato ya wafanyakazi wake kwa wakati ili kuepuka adhabu ya tozo ya ziada pamoja na kukiuka Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016. Mchanganuo wa mikato hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 239 : Ucheleweshwaji wa michango ya ZZSF kuwasilishwa kwa wakati.**

| Hati Namba | Kiasi cha fedha (Tshs) | Idadi ya Siku zilizoche leweshwa | Maelezo |
|---|---|---|---|
| PV 6/7 | 4,620,600 | 94 days | Malipo ya Makato ya ZSSF kwa mwezi wa Julai 2020 |
| PV 10/8 | 4,620,600 | 64 days | Malipo ya Makato ya ZSSF kwa mwezi wa Agosti 2020 |
| PV 11/9 | 4,620,600 | 34 days | Malipo ya Makato ya ZSSF kwa mwezi wa Septemba 2020 |
| PV 7/12 | 4,524,800 | 37 days | Malipo ya Makato ya ZSSF kwa mwezi wa Oktoba 2020 |
| PV 2/3 | 4,588,400 | 15 days | Malipo ya Makato ya ZSSF kwa mwezi wa Februari 2021 |

**WAKALA WA USAJILI WA BIASHARA NA MALI (BPRA) - PEMBA**

### 6.15.4.4 Matumizi yaliyofanywa nje ya vifungu husika shilingi 5,455,890.

Katika ukaguzi uliofanywa imebainika kwamba jumla ya shilingi 5,455,890 zimelipwa na Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali kwa matumizi mbalimbali lakini matumizi hayo yamefanywa nje ya vifungu husika.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 50(3)(a) cha sheria nambari 12 ya Fedha za Umma ya mwaka 2016. Mchanganuo wa malipo yaliofanywa nje ya vingufu ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 240 : Matumizi yaliyofanywa nje ya vifungu husika**

| Tarehe | Hati namba | Hundi namba | Kiasi cha fedha kilicholipwa (Tshs) | Aliyelipwa | Kifungu kilichotumika | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 2/08/2020 | 2/08 | 000215 | 126,000 | Wete Petrol Station | Internet | Malipo ya fedha kwa ajili ya Ununuzi wa petrol |
| 13/10/2020 | 02/10 | 000221 | 800,000 | Malinge Enter-prises-Pemba | Cleaning, Umeme na Overtime | Malipo ya fedha kwa ajili ya Ununuzi wa vya kuandikia |
| 01/01/2021 | 01/01 | 000227 | 800,000 | Wakala wa Usajili Biashara na Mali-Pemba | Cleaning Services na Transport | Malipo ya fedha kwa ajili ya matumizi madogo madogo |
| 01/01/2021 | 1/01 | 000227 | 240,000 | Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali-Pemba | Tuition Fee na Internet | Malipo ya fedha kwa ajili ya posho la likizo |
| 02/01/2021 | 02/01 | 000228 | 550,000 | Wete Petrol Station | Umeme, Transport na Internet. | Malipo ya fedha kwa ajili ya Ununuzi wa wa mafuta. |
| 04/01/2021 | 04/01 | 000230 | 309,000 | Nd. Abass Salim Khatib | Tuition Fee | Malipo ya fedha kwa ajili ya Ununuzi wa likizo la Nd. Abass Salim Khamis. |
| 01/02/2021 | 01/02 | 000234 | 530,000 | Wete Petrol Station | Internet | Malipo ya fedha kwa ajili ya Ununuzi wa mafuta ya petrol. |
| 02/02/2021 | 02/02 | 000235 | 500,000 | Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali –Pemba | Umeme na Internet. | Malipo ya fedha kwa ajili ya matumizi madogo madogo. |
| 02/04/2021 | 02/04 | 000238 | 500,000 | Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali-Pemba | Petrol | |
| 03/04/2021 | 03/04 | 000239 | 100,000 | Mamlaka ya Maji Pemba (ZAWA) | Umeme | Malipo ya fedha kwa ajili ya Ununuzi wa maji. |
| 06/04/2021 | 06/04 | 000242 | 617,890 | Malinge Enterprises Pemba | Internet | Malipo ya fedha kwa ajili ya Ununuzi wa ununuzi vifaa vya kuandikia. |
| 18/05/2021 | 02/04 | 000247 | 400,000 | Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali-Pemba | Petrol | Malipo ya fedha kwa ajili ya matumizi madogo madogo. |
| 29/06/2021 | - | - | 83,000 | Wete Petrol Station | Umeme | Malipo ya fedha kwa ajili ya Ununuzi wa Petrol |
| **Jumla** | | | **5,455,890** | | | |

### 6.15.4.5 Kuwepo kwa madeni ya muda mrefu bila ya kulipwa shilingi 21,148,000

Katika Ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Ofisi ya Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali inadaiwa deni na Taasisi za Serikali jumla ya shilingi 21,148,000 kwa ajili ya ujenzi wa ukuta wa ofisi ambapo imebainika kwamba deni hilo ni la muda mrefu bila ya kufanyika kwa juhudi maalum za kuhakikisha kwamba deni hilo linalipwa ili kuepusha usumbufu unaoweza kujitokeza kutokana na kutolipwa kwa deni hilo.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 29(3) (b) cha Sheria nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016.

### 6.15.5 BARAZA LA USIMAMIZI WA MFUMO WA UTOAJI LESENI

Ukaguzi wa hesabu za Baraza la Usimamizi wa Mfumo wa Utoaji Leseni kwa mwaka wa fedha 2020/2021 umefanywa kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu pamoja na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Taarifa ya Mapato**

Baraza la Usimamizi wa Mfumo wa Utoaji wa Leseni kwa mwaka wa fedha 2020/2021 lilikadiriwa kupokea jumla ya shilingi 745,900,000 kutoka katika mfuko wa Serikali. Kati ya fedha hizo shilingi 345,900,000 kwa ajili ya kazi za kawaida na shilingi 400,000,000 ni kwa ajili ya kazi za maendeleo.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 Baraza la Usimamizi wa Mfumo wa Utoaji wa Leseni limepokea shilingi 419,940,000 kutoka katika mfuko wa Serikali sawa na asilimia 56.3 ya makadirio. Kati ya fedha hizo shilingi 149,940,000 zimeingizwa kwa ajili ya kazi za kawaida sawa na asilimia 43.35 ya makadirio na shilingi 270,000,000 kwa kazi za maendeleo sawa na asilimia 67.5 ya makadirio.

**Taarifa ya Matumizi**

Baraza la Usimamizi wa Mfumo wa Utoaji wa Leseni kwa mwaka wa fedha 2020/2021 lilikadiriwa kutumia jumla ya shilingi 745,900,000. Kati ya fedha hizo shilingi 345,900,000 kwa ajili ya kazi za kawaida na shilingi 400,000,000 kwa ajili ya kazi za Maendeleo.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 Baraza la Usimamizi wa Mfumo wa Utoaji wa Leseni limeingiziwa na kutumia jumla ya shilingi 419,940,000 sawa na asilimia 43.3 ya makadirio. Kati ya fedha hizo shilingi 149,940,000 ni kwa ajili ya kazi za kawaida sawa na asilimia 43 na shilingi 270,000,000 kwa ajili ya kazi za maendeleo sawa na asilimia 67.5 ya makadirio.

### 6.15.6 TUME YA USHINDANI HALALI WA BIASHARA

Ukaguzi wa hesabu za mwaka wa fedha 2020/2021 kwa Tume ya Ushindani Halali wa Biashara umefanywa kwa mujibu wa Sheria, kanuni, taratibu pamoja na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Taarifa ya Mapato**

Tume ya Ushindani halali wa Biashara kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ilikadiriwa kukusanya jumla ya shilingi 1,383,800,000 . Hadi kufikia tarehe 30 Juni 2021 jumla ya shilingi 447,030,548 zilikusanywa sawa na asilimia 32.3 ya makadirio.

**Taarifa ya Matumizi**

Tume ya Ushindani Halali wa Biashara kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ilikadiria kutumia jumla ya shilingi 1,539,600,000. Hadi kufikia 30 Juni, 2021 jumla ya shilingi 429,335,187.86 zimetumika sawa na asilimia 27.89 za makadirio.

**MATOKEO NA MAPENDEKEZO YA UKAGUZI**

### 6.15.6.1 Kutokuwepo kwa Hesabu ya Tume Pemba

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Tume ya Ushindani Halali wa Kibiashara Pemba haina hesabu (akaunti) kwa ajili ya mapato na matumizi ambapo mapato yanayokusnywa huingizwa katika Hesabu ya Tume Zanzibar na vielelezo vya makusnyo hayo hutumwa kwa njia ya simu, aidha fedha za matumizi kwa upande wa Pemba hufanywa kupitia Hesabu binafsi ya anayefanyiwa malipo hayo.

Kufanya hivyo kunaweza kupelekea kuwepo kwa upotevu wa fedha za Serikali ambapo pia ni kwenda kinyume na Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Tume kuhakikisha unafuata Sheria, Kanuni na Miongozo mbali mbali ikiwemo ufunguaji wa Hesabu (akaunti) katika Ofisi ya Pemba. Mchanganuo wa matumizi hayo umefanyika kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 241 : Kutokuwepo kwa Hesabu ya Tume Pemba**

| Hati Namba | Hundi Namba | Kiasi cha fedha kilicholipwa (Tshs.) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| Pv7/6/2021 | 211 | 560,000 | Said Saleh Moh'd | Malipo kwa ajili ya safari kikazi. |
| Pv17/6/2021 | TT | 681,600 | Chake Chake petrol Station | Malipo kwa ajili ya ununuzi wa mafuta |
| pv10/7/2020 | TT | 742,400 | Wete Petrol Station | |
| pv15/8/2020 | TT | 770,000 | Wete Petrol Station | |
| pv28/1/2021 | TT | 800,000 | Chake Petrol Station | |
| | **Jumla** | **3,554,000** | | |

## 6.16 WIZARA YA MAJI NISHATI NA MADINI

### 6.16.1 FUNGU N 03 - WIZARA YA MAJI, NISHATI NA MADINI

Ukaguzi wa hesabu za mwaka wa fedha 2020/2021 kwa Wizara ya Maji,Nishati na Madini umefanywa kwa mujibu wa Sheria, kanuni, taratibu pamoja na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Taarifa ya Mapato**

Wizara ya Maji, Nishati na Madini kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ilikadiriwa kupokea jumla ya shilingi 9,104,641,343 kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina kwa ajili ya kazi za kawaida , na shilingi 78,959,316,000 kutoka Washirika wa Maendeleo, kwa ajili ya kazi za maendeleo.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2021 Wizara ya Maji, Nishati na Madini ilipokea na kutumia jumla ya shilingi 2,661,097,220 kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina sawa na asilimia 29 ya makadirio, kukiwa na upungufu wa shilingi 6,443,544,123 sawa na asilimia 71 katika kazi za kawaida, na shilingi 1,183,767,216 sawa na asilimia 01 ya makadirio, kukiwa na upungufu wa shilingi 77,775,548,784 sawa na asilimia 99 ya makadirio. Aidha Wizara ya Maji, Nishati na Madini ilikusanya jumla ya shilingi 3,872,292,013 kutoka vyanzo vyake vya ndani.

**Taarifa ya Matumizi**

Wizara ya Maji, Nishati na Madini katika mwaka wa fedha 2020/2021 ilikadiriwa kutumia jumla ya shilingi 83,532,737,343, kati ya fedha hizo shilingi 83,219,978,315 kwa matumizi ya kazi za kawaida na shilingi 312,759,028 kwa kazi za maendeleo, na jumla ya shilingi 78,959,316,000.00 kutoka kwa washirika wa maendeleo.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni 2021, jumla ya shilingi 7,717,156,449 zimeingizwa na kutumika, kati ya fedha hizo shilingi 3,840,916,116 zilitumika kwa kazi za kawaida sawa na asilimia 5 ya makadirio na shilingi 3,948,320 kwa kazi za maendeleo sawa na asilimia 1 ya makadirio. Aidha Wizara ilipokea shilingi 1,183,767,216 kutoka washirika wa maendeleo sawa na asilimia 01 ya makadirio.

**MATOKEO NA MAPENDEKEZO YA UKAGUZI**

### 6.16.1.1 Upotevu wa mapato utokanao na kutofuatwa sheria ya utozaji faini ya mali asili zisizorejesheka shilingi 9,100,000

Kwa mujibu wa kifungu nambari 19(3) cha Kanuni ya Usimamizi wa Mazingira kwa Maendeleo Endelevu ya mwaka 1996 kinaeleza kwamba "Mtu yeyote anayekiuka masharti yoyote ya kanuni hii atakuwa ametenda kosa na akitiwa hatiani atawajibika kulipa faini ya shilingi 150,000 kwa usafirishaji wa maliasili zisizorejesheka bila ya kuwa na leseni au kibali kwa kila tani au kifungo kisichopungua miezi sita au vyote kwa pamoja".

Ukaguzi umebaini Wizara ya Maji, Nishati na Madini kwa mwaka wa fedha 2020/2021 imetoza tozo mbali mbali za adhabu ambazo haziendani na matakwa ya kanuni ya Usimamizi wa Mazingira ya Maendeleo Endelevu ya mwaka 1996 kwa mujibu wa kifungu kilichonakiliwa hapo juu jambo ambalo linapelekea kujitokeza kwa vitendo vya upotevu wa mapato ya Serikali yenye thamani ya shilingi 9,100,000.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wizara kuhakikisha kwamba tozo za faini zinatolewa kwa mujibu wa sheria husika ili kuepuka kujitokeza kwa upotevu wa fedha za umma.

Mchanganuo wa tozo zilizotolewa ambazo haziendani na matakwa ya kanuni ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 242 : Upotevu wa mapato utokanao na faini za mali asili zisizorejesheka**

| Namba | Jina la Mhusika | Namba ya Gari na Tani | Kosa | Faini kwa tani moja (Tshs.) | Faini aliyotozwa (Tshs.) | Faini kwa mujibu wa utaratibu wa faini zilizowekwa na Wizara (Tshs.) | Tofauti (Tshs.) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Abrahman Abdallah Simai | Z-187 KW ya tani 6 | Mchanga Bila Kibali | 150,000 | 200,000 | 900,000 | 700,000 |
| 2. | Moh'd Masoud Moh'd | Z – 965 LA ya tani 4 | | 150,000 | 300,000 | 600,000 | 300,000 |
| 3. | Ali Khalid Moh'd | Z- 923 LN ya tani 10 | | 150,000 | 500,000 | 1,500,000 | 1,000,000 |
| 4. | Rashid Hassan Khalifa | Z- 719 KX ya tani 4 | | 150,000 | 150,000 | 600,000 | 450,000 |
| 5. | Omar Mbwana Saleh | Z-436 CU ya tani 10 | | 150,000 | 100,000 | 1,500,000 | 1,400,000 |
| 6. | Kassim Soud Haji | Z- 112 KS ya tani 10 | | 150,000 | 500,000 | 1,500,000 | 1,000,000 |
| 7. | Jadi Moh'd Ali | Z-508 JJ ya tani 10 | | 150,000 | 500,000 | 1,500,000 | 1,000,000 |
| 8. | Muhamadi Abdallah Khamis | Z-653 HF ya tani 10 | | 150,000 | 250,000 | 1,500,000 | 1,250,000 |
| 9. | Abuubakar Mwinyi Rashid | Z-736 LP ya tani 10 | | 150,000 | 500,000 | 1,500,000 | 1,000,000 |
| 10. | Issa Amour Haji | Z-329 KQ ya tani 10 | | 150,000 | 500,000 | 1,500,000 | 1,000,000 |
| **Jumla** | | | | | | | **9,100,000** |

**WIZARA YA MAJI, NISHATI NA MADINI – PEMBA**

### 6.16.1.2 Kukosekana kwa Ofisi za Ukusanyaji wa Mapato

Wizara ya Maji Nishati na Madini inamiliki vituo sita "6" vya ukusanyaji wa mapato kwa ajili ya mali zisizorejesheka lakini vituo hivyo vimebainika kutokuwa na ofisi maalum kwa ajili ya utowaji wa huduma pamoja na ukusanyaji wa mapato. Ukaguzi umebaini watendaji wa Wizara ya Maji, Nishati na Madini ambao wamepewa jukumu la ukusanyaji wa mapato kwa ajili ya mali zisizorejesheka hutekeleza wajibu huo katika mazingira magumu kwani imebainika hukaa chini ya Miembe au miti mikubwa kwa kutegemea vivuli vya miti hiyo au kutengeneza vibanda vidogo vidogo kwa ajili ya ukusanyaji wa mapato hayo jambo ambalo haliendani na uhalisia wa mapato wanayoyakusanya na mazingira magumu na hatarishi ya utekelezaji wa majukumu yao.

Kwa wastani mapato yanayokusanywa ni zaidi ya shilingi 421,758,900 zilikusanywa sawa na asilimia 674.82 ya makadirio kwa mwaka wa fedha 2020/2021. Kutokuwepo kwa ofisi katika vituo hivyo kunapunguza ufanisi katika ukusanyaji wa mapato ambapo kunaweza kupelekea upotevu wa mapato pamoja na nyaraka muhimu.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu namba 61(5) (a) (b) (f) na kifungu namba 77(1) vya Sheria nambari 2 ya Utumishi wa Umma ya mwaka 2011.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wizara ya Maji Nishati na Madini kuharakisha utaratibu wa upatikanaji wa miundombinu wezeshi kwa lengo la upatikanaji wa tija na ufikiwaji wa malengo ya ukusanyaji wa mapato.

#### 6.16.1.3 Makadirio ya ukusanyaji wa mapato kinyume na uhalisia shilingi 62,500,000

Jumla ya shilingi 62,500,000 zilikadiriwa kukusanywa na Wizara ya Maji Nishati na Madini -Pemba kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

Ukaguzi umebaini kwamba makadirio hayo ni madogo ukilinganisha na makusanyo halisi kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ambapo hadi kufikia 30 Juni 2021, jumla ya shilingi 421,758,900 zilikusanywa sawa na asilimia 674.82 ya makadirio.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 32(1)(2) cha Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016.

## VIAMBATISHO

### Kiambatisho Nambari 1 :

### Kukosekana kwa Tozo la adhabu kwa wawekezaji wanaopatiwa huduma za kimazingira

| Namba | Jina la Mradi | Tarehe ya Kibali | Tarehe ya Kumaliza Kibali | Eneo la Mradi | Nambari ya Kibali |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Construction of Jetty For Fruit And Spice Hotel | 27/01/2014 | 27/01/2019 | Mchangamle Muyuni | IM/EIA/44/2014. |
| 2. | Construction of 9 Holes Golf Course | 17/02/2014 | 17/02/2019 | Kama | IM/EIA/45/2014 |
| 3. | Zenj Petrogas Deport For Zenj Petrogas Company Ltd | 6/6/2014 | 06/06/2019 | Mtoni | IM/EIA/45/2014 |
| 4. | The Liqufied Petroleum Gas Filling Station | 6/6/2014 | 6/6/2019 | Welezo-Makufuli | IM/EIA/50 |
